

Juzuu 6  
(Toleo la Pili)

Historia ya kushushwa Qur-an 96:1 - 5, inatukumbusha na kutufunza kuwa Mtume(s.a.w) alianza kushushiwa wahy kwa kupewa amri ya kusoma. Hivyo, hapana shaka kabisa kuwa Elimu ndiyo Faradhi ya kwanza inayopaswa kutekelezwa na kila Muislamu tangu zama za Mtume (s.a.w) hadi sasa.

Kusoma au kutafuta elimu kumefanywa kuwa Faradhi ya kwanza ili kumuwezesha mja kumjua Mola wake na kumpatia ujuzi wa kutosha juu ya kanuni na sheria alizoiweka Allah(s.w) zikifuatwa katika kila kipengele cha maisha ya kila siku, hupatikana uadilifu na amani ya kweli katika jamii.

Hii ni juzuu ya sita ya maarifa ya Uislamu katika mfululizo wa juzuu 7 za masomo kwa Darasa la Watu Wazima unaokusudia kumuwezesha mja na jamii kufikia kilele hicho.

Mfululizo huu wa masomo katika juzuu 7 ni:

1. Lengo la Maisha ya Mwanadamu
2. Nguzo za Uislamu
3. Qur-an na Sunnah
4. Familia ya Kiislamu
5. Jamii ya Kiislamu
6. Historia ya Kuhuisha Uislamu
7. Kuhuisha Uislamu katika Jamii

Historia ya Kuhuisha Uislamu

# HISTORIA YA KUHUISHA UISLAMU



**Maarifa ya Uislamu**

**Darasa la Watu Wazima**

**Juzuu 6**

**(Toleo la Pili)**

**HISTORIA YA KUHUISHA  
UISLAMU**

**Islamic Propagation Centre**

Maarifa ya Uislamu  
(Darasa la Watu Wazima)  
Juzuu ya 6 (Toleo la pili)  
Historia ya Kuhuisha Uislamu

© Islamic Propagation Centre (IPC)

Toleo la Pili limetoka Novemba, 2009/Dhulqaada, 1430.

Juzuu hii imeandikwa na kusambazwa na:  
Islamic Propagation Centre (IPC)  
S.L.P 55105, Dar es Salaam, Tanzania.  
Simu: 022-2450069 Fax: 022-2450822  
website: [www.ipctz.org](http://www.ipctz.org)  
Nakala 1000

Imechapwa na:  
Afroplus Industries(Ltd)  
P.O.Box 32427, Tel:No:022-2773751  
**DAR ES SALAAM.**

# بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

## NENO LA AWALI

Shukurani zote anastahiki Allah(s.w), Bwana mlezi wa viumbe vyote. Rehema na amani ziwaendee Mitume wake wote na wale wote waliofuata na wanaofuata mwenendo wao katika kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii.

Tunamshukuru Allah(s.w) kwa kutuwezesha kutoa toleo la pili la Juzuuu ya Sita ya Maarifa ya Uislamu kwa "Darasa la watu wazima". Toleo hili la pili limeboreshwa zaidi na limewasilishwa katika sura nane badala ya zile sita za toleo la kwanza. Sura zilizoongezeka ni "Dhana juu ya Historia" na "Kuhuisha Uislamu wakati wa Tabii Tabiina". Pamoja na nyongeza ya hizi sura mbili kuna mengi yaliyongezwa katika toleo hili la pili.

Lengo la juzuu hii, ni kuwawezesha waumini kutekeleza dhima kuu waliyonayo ya **kuuhuisha na kuusimamisha** Uislamu katika jamii kwa kuiga juhudi na mwenendo wa Mitume wa Allah(s.w) na watu wema waliowaamini na kufuata nyayo zao. Tunamuomba Allah(s.w) awawezeshe wasomaji wa juzuu hii wafikie lengo tarajiwa - Inshaa Allah.

Kama kawaida tunawakumbusha wasomaji wetu kuwa kazi ya binaadamu haiwezi kuepukana na mapungufu. Hivyo tunawa omba mtusamehe kwa mapungufu yatakayojitokeza na mtusaidie kuyapunguza kwa kutoa maoni yenu na masahihisho yanayostahili.

---

..... رَبَّنَا آتِنَا مِن لَّدُنكَ رَحْمَةً وَهَيِّئْ لَنَا مِنْ أَمْرِنَا رَشَدًا ﴿١٠﴾

".....Mola wetu! Tupe rehema zinazotoka kwako na tutengenezee uongofu katika kila jambo letu" (18:10)

---

## YALIYOMO

<b>Neno la awali</b> .....	(iii)
<b>Utangulizi</b> .....	(xv)

<b>Sura ya kwanza:</b> .....	1
<b>Dhana Juu ya Historia</b> .....	1

Mtizamo wa Kikafiri Juu ya Historia na Udhaifu Wake .....	1
Mtizamo wa Makafiri Juu ya Chanzo cha Dunia, Mwanaadamu na Lengo la Uhai Wake .....	2
Chimbuko la Mtizamo wa Makafiri Juu ya Chanzo cha Dunia na Mwanadamu .....	5
Chimbuko la Fikra za Karl Marx .....	5
Nadharia za Kikafiri na Sayansi .....	9
Ukafiri si Zao la Sayansi .....	10
Nadharia ya Sayansi Juu ya Chanzo cha Ulimwengu .....	13
Mtizamo wa Sayansi juu ya Chanzo cha Ulimwengu na Uhai .....	15
Sayansi Yasemaje Kuhusu Dhana Kuwa Mwanadamu Katokana na Kizazi cha Manyani .....	17
Mtizamo wa Uislamu Juu ya Historia .....	18
Lengo la Maumbile Yote Yaliyomzunguka Mwanaadamu ..	19
Lengo la Maisha ya Mwanaadamu Hapa Ulimwenguni ...	20
Kwa Nini ni Muhimu Kujifunza Historia .....	23
Zoezi la 1 .....	32

<b>Sura ya Pili:</b> .....	33
<b>Historia ya Uislamu Kabla ya Muhammad(s.a.w)</b> .....	33

<b>Adam(a.s)</b> .....	34
Kuumbwa kwa Adam(a.s) .....	34
Hadhi ya Adam(a.s) na Kizazi Chake .....	35
Kibri cha Iblis na Uadui Wake Dhidi ya Binadamu .....	38

Adam(a.s) na Mkewe Katika Pepo . . . . .	41
Adam na Hawah Kushushwa Ardhini . . . . .	45
Mwongozo wa Allah kwa Wanaadamu . . . . .	46
Historia ya Watoto Wawili wa Nabii Adam . . . . .	47
Mafunzo Yatokana na Historia ya Adam(a.s) . . . . .	51
<b>Idris(a.s)</b> . . . . .	54
<b>Nuhu(a.s)</b> . . . . .	55
Mazingira ya Jamii Aliyoikuta Nabii Nuhu (a.s) . . . . .	55
Wito wa Nabii Nuhu(a.s) kwa Watu Wake . . . . .	56
Mbinu za Da'wah Alizotumia Nuhu(a.s) . . . . .	56
Waliomuamini Nabii Nuhu(a.s) . . . . .	59
Wapinzani wa Ujumbe wa Nabii Nuhu(a.s) na Vitimbi Vyao . . . . .	60
Msimamo wa Nabii Nuhu(a.s) Dhidi ya Makafiri . . . . .	62
Ushindi wa Nabii Nuhu(a.s) na Wale Walioamini Pamoja Naye . . . . .	63
Kuangamia kwa Mtoto na Mke wa Nuhu(a.s) . . . . .	65
Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Nuhu(a.s): . . . . .	68
<b>Hud(a.s)</b> . . . . .	70
Mbinu za Hud(a.s) katika Kufikisha Ujumbe . . . . .	71
Wapinzani wa Ujumbe wa Hud(a.s) . . . . .	73
Msimamo wa Nabii Hud(a.s) Dhidi ya Makafiri wa Kaumu Yake: . . . . .	75
Ushindi wa Nabii Hud(a.s) Juu ya Makafiri . . . . .	76
Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Hud(a.s) . . . . .	79
<b>Salih(a.s)</b> . . . . .	79
Ujumbe wa Nabii Salih(a.s) kwa Watu Wake . . . . .	80
Mbinu za Mtume Salih(a.s) Katika Kulingania Uislamu . . . . .	80
Wapinzani wa Ujumbe wa Nabii Salih(a.s) . . . . .	82
Vitimbi vya Makafiri Dhidi ya Nabii Salih(a.s) na Waumini . . . . .	84
Kuangamizwa Makafiri na Kususuriwa Waumini . . . . .	85

Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Salih(a.s) . . . . .	86
<b>Ibrahiim(a.s)</b> . . . . .	87
Kuandaliwa kwa Nabii Ibrahiim(a.s) . . . . .	87
Nabii Ibrahiim(a.s) Kumlingania Uislamu Baba yake . . . . .	89
Nabii Ibrahiim(a.s) Kuulingania Uislamu kwa Jamii Yake . . . . .	90
Ujumbe wa Nabii Ibrahiim(a.s) kwa Mfalme Namrudh . . . . .	93
Ibrahim(a.s) Avunja Masanamu Kuwatanabahisha Washirikina . . . . .	94
Allah(s.w) Amnusuru Ibrahim (a.s) na Hila za Makafiri . . . . .	98
Nabii Ibrahiim(a.s) Kuhama Iraq . . . . .	98
Ibrahiim(a.s) Aomba Kupata Kizazi Chema . . . . .	100
Kutahiniwa Nabii Ibrahiim(a.s) . . . . .	102
Nabii Ibrahiim(a.s) Afanywa Kiongozi wa Harakati za Uislamu Ulimwenguni . . . . .	104
Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Ibrahiim(a.s) . . . . .	106
<b>Lut(a.s)</b> . . . . .	108
Tabia ya Watu wa Miji ya Sodoma na Gomora . . . . .	108
Nasaha za Lut(a.s) kwa Watu Wake . . . . .	110
Jawabu la Makafiri Dhidi ya Nasaha za Nabii Lut(a.s) . . . . .	111
Kuangamizwa kwa Watu wa Lut(a.s) . . . . .	112
Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Lut (a.s) . . . . .	113
<b>Ismail(a.s)</b> . . . . .	113
Kuinua Kuta za Ka'bah . . . . .	115
Ismail(a.s) na Taifa la Waarabu . . . . .	116
Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Ismail(a.s) . . . . .	117
<b>Is-Haq(a.s) na Ya'aquub(a.s)</b> . . . . .	118
Shukurani za Nabii Ibrahiim(a.s) kwa Allah(s.w) . . . . .	119
Mafunzo Yatokanayo na Historia Nabii Is-haqa na Ya'aquub(a.s) . . . . .	120

<b>Yusufu(a.s.)</b> .....	121
Ndoto ya Nabii Yusufu(a.s) .....	121
Njama za Kumuuu Nabii Yusufu(a.s) .....	122
Kutumbukizwa Yusufu(a.s) Kisimani .....	123
Yusufu Aokotwa na Kuuzwa nchini Misri .....	124
Yusufu(a.s) apewa Utume na Kukumbana na Mtihani ...	124
Yusufu(a.s) Atupwa Gerezani .....	129
Maisha ya Yusufu(a.s.) Gerezani .....	129
Yusufu Afikisha Ujumbe wa Uislamu kwa Wafungwa ....	130
Kufunguliwa Yusufu(a.s) kutoka Gerezani .....	131
Yusufu(a.s.) Akutana na Ndugu Zake .....	134
Ndoto ya Nabii Yusufu(a.s) Yatimia .....	137
Shukurani za Nabii Yusufu(a.s) kwa Allah(s.w) .....	138
Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Yusufu(a.s) ...	138
 <b>Ayyuub(a.s)</b> .....	 141
Mitihani iliyomfika Ayyuub(a.s) .....	141
Dua ya Ayyuub(a.s) .....	142
Nabii Ayyuub(a.s) Kutekeleza Kiapo Chake .....	144
Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Ayyuub(a.s) ..	144
 <b>Shu'ayb(a.s)</b> .....	 146
Tabia ya Watu wa Madian .....	147
Ujumbe wa Nabii Shu'ayb kwa Watu Wake .....	147
Mbinu Alizozitumia Nabii Shu'ayb(a.s)	
Katika Kufikisha Ujumbe Wake .....	148
Vitimbi vya Wapinzani Dhidi ya Ujumbe wa Nabii Shu'ayb(a.s) .....	150
Kuangamizwa Waovu na Kuokolewa Waumini .....	152
Mafunzo Yatokanayo na Kisa cha Nabii Shu'ayb(a.s) ...	153
 <b>Musa(a.s) na Harun(a.s)</b> .....	 153
Kuzaliwa kwa Musa(a.s) .....	154
Allah(s.w) Ajaalia Musa(a.s) Kunyonyeshwa na Mama Yake	
Mzazi .....	155



Allah(s.w) Amruzuku Musa(a.s) Elimu . . . . .	156
Musa(a.s) Ahamia Madiani . . . . .	156
Musa(a.s)Kupewa Utume Rasmi . . . . .	158
Miujiza kama Ushahidi wa Utume wa Nabii Musa(a.s) . . .	159
Harun(a.s), Achaguliwa Kuwa Msaidizi wa Musa(a.s) . . .	160
Musa na Harun(a.s) Kumkabili Firaun . . . . .	161
Kusilimu kwa Wachawi wa Firaun . . . . .	163
Kuangamizwa Firauni na Majeshi Yake . . . . .	165
Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Musa(a.s) na Harun(a.s) . . . . .	166
<b>Historia ya Bani Israil . . . . .</b>	<b>169</b>
Musa(a.s) Kupewa Taurati . . . . .	169
Bani Israil Kuabudu Ndama . . . . .	171
Musa(a.s) Kuwaongoza Bani Israil Hadi Palestina . . . . .	172
Amri ya Kuchinja ng'ombe . . . . .	174
Neema za Allah(s.w) Juu ya Bani Israil. . . . .	176
Kulaaniwa Bani Israil . . . . .	179
Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Bani Israil . . . . .	183
<b>Al-Yas'a(a.s) . . . . .</b>	<b>185</b>
<b>Dhul-Kifl(a.s) . . . . .</b>	<b>186</b>
<b>Daud (a.s) . . . . .</b>	<b>186</b>
Kupewa Daudi(a.s) Utume na Ufalme . . . . .	187
Neema Alizotunukiwa Nabii Daudi(a.s) . . . . .	193
Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Daud(a.s) . . . .	199
<b>Suleiman(a.s) . . . . .</b>	<b>200</b>
Uchambuzi wa Neema Alizopewa Nabii Sulaiman(a.s) . . .	202
Kisa cha Malkia wa Sabaa . . . . .	206
Kusingiziwa Nabii Sulaiman Uchawi . . . . .	208
Kifo cha Nabii Sulaiman . . . . .	210
Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Sulaiman(a.s) . . . . .	210

<b>Ilyasa(a.s)</b> .....	213
<b>Yunus(a.s)</b> .....	214
Yunus(a.s) Kulingania Uislamu kwa Watu Wake .....	215
Nabii Yunus(a.s) Amuomba Allah(s.w) Msamaha .....	217
Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Yunus(a.s) ...	218
<b>Zakaria(a.s) na Yahya(a.s)</b> .....	219
Nabii Zakaria(a.s) Kumlea Maryam na Kuomba Mtoto Mwema .....	219
Yahya(a.s) Jibu la Dua ya Mzee Zakaria(a.s) .....	221
Yahya(a.s) Kupewa Utume .....	221
Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Zakaria(a.s) na Yahya(a.s) .....	222
<b>Isa(a.s)</b> .....	223
Nasaba na Kuzaliwa Nabii Isa(a.s) .....	223
Kuzaliwa Maryam, Mama wa Nabii Isa(a.s) .....	223
Zakaria(a.s) Akabidhiwa Ulezi wa Maryam .....	224
Maryam Apewa Habari ya Kumzaa Isa(a.s) .....	225
Kuzaliwa Nabii Isa(a.s) .....	226
Nabii Isa(a.s) Azungumza Akiwa Mtoto Michanga .....	227
Je, Nabii Isa(a.s) ni Mtoto wa Mungu? .....	228
Nabii Isa(a.s) Alitumwa kwa Wana wa Israil. ....	229
Ujumbe wa Nabii Isa(a.s) kwa Wana wa Israil .....	230
Miujiza Aliyoonesha Nabii Isa(a.s) .....	232
Wito wa Nabii Isa(a.s) kwa Wanafunzi Wake .....	233
Njama za Mayahudi Kutaka Kumuuua Nabii Isa(a.s) .....	235
Ahadi ya Allah(s.w) Kumuokoa Nabii Isa(a.s) .....	236
Si Yesu Aliyesulubiwa .....	238
Kuokolewa Nabii Isa(a.s) .....	238
Kupotoshwa Mafundisho ya Nabii Isa(a.s) .....	242
Nabii Isa(a.s) Siku ya Kiyama .....	246
Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Isa(a.s) .....	247

<b>Watu Wema Waliotajwa Ndani ya Qur'an</b> .....	249
Vijana wa Pangoni .....	250
Al-Khidhri .....	255
Dhulqarnain .....	261
Luqman .....	265
<b>Watu Waovu Waliotajwa Katika Qur'an</b> .....	268
Watu Waliovunja Amri ya Kuheshimu Siku ya Jumamosi .	268
Firaun, Qarun na Hamana .....	273
Watu wa Mahandaki ya Moto .....	275
Watu wa Mji Waliomuua Muislamu kwa kuwa Amewasadikisha Wajumbe wa Allah(s.w) .....	277
Zoezi la 2 .....	284
<b>Sura ya Tatu :</b> .....	288
<b>Historia ya Uislamu Wakati wa Muhammad(s.a.w)</b> .....	288
Zama za Jahiliyyah .....	289
Kuandaliwa Mtume(s.a.w) .....	291
Maandalizi ya Ki-il-hamu .....	291
Mafunzo Yatokanayo na Maandalizi ya ki-il-hamu .....	299
Maandalizi ya Kimafunzo .....	300
Mafunzo Yatokanayo na Maandalizi ya Kimafunzo .....	304
Mtume(s.a.w) Kulingania Uislamu Makka .....	311
Kuanza Kulingania kwa Siri .....	311
Kulingania Uislamu kwa Jamii Nzima .....	314
Upinzani Dhidi ya Ujumbe wa Mtume(s.a.w) .....	317
Mtume(s.a.w) Mwenyewe .....	321
Mtume(s.a.w) Kulingania Uislamu katika Mji wa Taif .....	328
Mafunzo Yatokanayo na Kufariki Bibi Khadija, Abu Twalib na Tukio la Taif .....	331
Safari ya Mi'raj .....	331
Mtume(s.a.w) Kulingania Uislamu Siku za Hija .....	338
Mikataba ya 'Aqabah .....	340
Mafunzo Yatokana na Mikataba ya 'Aqabah .....	343

Kuhajiri Waislamu wa Makka Kwenda Madinah . . . . .	344
Hijra ya Mtume(s.a.w) kwenda Madinah . . . . .	345
Njama za Kumuuwa Mtume(s.a.w) . . . . .	345
Mafunzo Yatokanayo na Hijira ya Mtume(s.a.w) na Maswahaba Zake . . . . .	351
Mtume(s.a.w) Kusimamisha Dola ya Kiislamu Madinah . . . . .	353
Kujengwa Msikiti wa Quba . . . . .	353
Yathrib inakuwa Al-Madinah al-Munawwarah . . . . .	354
Mambo ya Msingi Aliyofanya Mtume(s.a.w) Katika Kuanzisha Dola ya Kiislamu Madinah . . . . .	358
Mafunzo Yatokanayo na Mambo Aliyofanya Mtume (s.a.w) Katika Kuanzisha Dola ya Kiislamu . . . . .	365
Mapambano Dhidi ya Maadui wa Dola ya Kiislamu . . . . .	367
Makafiri wa Kabila la Qiquraish . . . . .	367
Wanafiq . . . . .	372
Mayahudi . . . . .	377
Makabila Mengine ya Kiarabu . . . . .	383
Warumi (Wakatoliki) . . . . .	385
Mafunzo Yatokanayo na Vita vya Muttah . . . . .	387
Msafara wa Tabuk Dhidi ya Warumi . . . . .	388
Mafunzo Yatokanayo na Mapambano Dhidi ya Maadui wa Dola ya Kiislamu. . . . .	390
Mkataba wa Hudaybiyah . . . . .	390
Kusibu kwa Bishara ya Ushindi . . . . .	394
Mafunzo Yatokanayo na Mkataba wa Hudaybiyah . . . . .	399
Hija ya Kuaga . . . . .	400
Hutuba ya Mtume(s.a.w) Katika Uwanja wa 'Arafa, 9 Dhul-Hijjah 10 A.H. . . . .	401
Ugonjwa wa Mtume(s.a.w) na Kufariki kwake . . . . .	404
Zoezi la 3 . . . . .	407
<b>Sura ya Nne . . . . .</b>	<b>410</b>
<b>Uongozi wa Dola ya Kiislamu wakati wa Makhalifa wa Mtume(s.a.w) . . . . .</b>	<b>410</b>

Uchaguzi wa Abubakar Kuwa Khalifa . . . . .	410
Uchaguzi wa 'Umar bin Khattab kuwa Khalifa wa Pili . . . .	416
Uchaguzi wa Uthman bin Affan kuwa Khalifa wa Tatu . . .	418
Uchaguzi wa Ali bin Abu Twalib kuwa Khalifa wa Nne . . .	419
Kuzuka Imani ya Kishia . . . . .	421
Uendeshaji wa Dola ya Kiislamu Wakati wa Makhaliifa . . .	423
Kazi na Wajibu wa Khalifa . . . . .	423
Haki za Wasiokuwa Waislamu Chini ya	
Uongozi wa Khalifa . . . . .	430
Kuanzishwa kwa Polisi. . . . .	431
Kuanzishwa kwa Magezea . . . . .	431
Pato la Serikali . . . . .	433
Ulinzi na Usalama . . . . .	436
Usalama wa Taifa . . . . .	437
Upinzani Dhidi ya Dola ya Kiislamu Wakati wa Makhaliifa	437
Uasi wa Dola (Riddah) . . . . .	438
Sababu Zilizopelekea Uasi . . . . .	439
Kukomeshwa kwa Riddah na Chokocho Nyingine . . . .	440
Kuporomoka kwa Dola ya Kiislamu	
Aliyoiacha Mtume(s.a.w) . . . . .	443
Upinzani Kutoka Miongoni mwa Waislamu . . . . .	444
Madai Dhidi ya Khalifa 'Uthman . . . . .	444
Fitna za Abdullah bin Sabaa . . . . .	450
Hatua ya Serikali Dhidi ya Waanzilishi wa	
Fitna na Farka . . . . .	452
Kuwasilisha Malalamiko KwenyeKikao cha Magavana . . .	453
Khalifa Uthman Kufa Shahidi . . . . .	454
Vita vya Wenyewe kwa Wenyewe . . . . .	456
Vita kati ya Bibi Aisha na Khalifa Ali . . . . .	458
Vita kati ya Khalifa Ali na Gavana Muawiya . . . . .	460
Yaliyopelekea Kuzuka kwa Vita vya Siffin . . . . .	360
Kuibuka kwa Khawarij (waliojitenga) . . . . .	464
Tamko la Wapatanishi . . . . .	465
Muawiyah ateka jimbo la Misri . . . . .	466
Ghasia Sehemu Mbali Mbali za Dola ya Kiislamu . . . . .	467

Kutekwa kwa Makka, Madina na Yemen . . . . .	468
Kuuwawa kwa Ali . . . . .	468
Kuanzishwa Ufalme. . . . .	469
Zoezi la 4 . . . . .	470
<b>Sura ya Tano . . . . .</b>	<b>472</b>
<b>Kuhuisha Uislamu Wakati wa Tabiina . . . . .</b>	<b>472</b>
Khalifa 'Umar bin Abdul Aziz . . . . .	472
Maimamu Wanne wa Fiq-hi . . . . .	476
Imam Abu Hanifah . . . . .	478
Imam Malik bin Anas . . . . .	479
Imam Muhammad Idris al-Shafii . . . . .	480
Imam Ahmad bin Muhammad bin Hambal . . . . .	482
Zoezi la 5 . . . . .	484
<b>Sura ya Sita . . . . .</b>	<b>485</b>
<b>Kuhuisha Uislamu wakati wa Tabii Tabiina . . . . .</b>	<b>485</b>
Sahih al-Bukhari . . . . .	486
Sahih Muslim . . . . .	487
Sunnan Abu Daud . . . . .	487
Jami'u at-Tirmidh . . . . .	488
Sunnan Ibn Majah . . . . .	489
Sunan ya an-Nasai . . . . .	489
Zoezi la 6 . . . . .	490
<b>Sura ya Saba . . . . .</b>	<b>491</b>
<b>Kuhuisha Uislamu Katika Karne ya 20. A.D . . . . .</b>	<b>491</b>
Baadaee – U-Zaman Said Nursi . . . . .	491
Ikhwani Muslimiin wa Misr. . . . .	499
Ikhwani Muslimiin wa Sudan. . . . .	504
Jama'atil Islamy ya Pakistan . . . . .	506
Zoezi la 7 . . . . .	513

<b>Sura ya Nane</b> .....	514
<b>Historia ya Kuhuisha Uislamu Tanzania</b> .....	514
Historia ya Kuingia Uislamu Afrika ya Mashariki .....	514
Upinzani Dhidi ya Uislamu Afrika ya Mashariki. ....	516
Mbinu za Kuwaghibu na Kuwaritadisha Waislamu Afrika Mashariki .....	518
Kupigwa Vita Uislamu Tanganyika .....	520
Mchango wa Waislamu katika Kuleta Uhuru Tanganyika .	524
Mkutano wa Kwanza wa Waislamu, 1962. ....	528
Pingamizi katika Kuleta Mabadiliko ya Kunufaisha Waislamu, 1963. ....	529
Mkutano wa Pili wa Waislamu, 1963 .....	532
Juhudi za Kuanzisha Chuo Kikuu cha Kiislamu Chini ya EAMWS, 1964 .....	537
Mgogoro wa EAMWS 1968 .....	540
Mvutano wa Nyerere, Tewa na Bibi Titi kuhusu EAMWS, 1968. ....	549
Kuasisiwa BAKWATA, 1968 .....	555
Athari ya BAKWATA kwa Waislamu na Uislamu .....	565
Kuibuka kwa Vikundi mbali mbali badala ya BAKWATA .	568
Sheikh Malik na Warsha .....	570
Juhudi za Kuirekebisha BAKWATA 1979 .....	572
Kuanzishwa kwa Seminari ya Masjid Qubah, 1983 .....	575
Kuibuka kwa Seminari Nyingi za Kiislamu .....	577
Kuanzishwa Vyuo vya Ualimu na Chuo Kikuu .....	577
Kuanzishwa BARAZA KUU ,1992 .....	578
Kadhia ya Mabucha ya Nguruwe, 1993 .....	583
Mauaji ya Waislamu Mwembechai, 1998 .....	589
Kuanzishwa kwa Kamati za Kuendeleza Uislamu, 2003 .	595
Hitimisho .....	597
Zoezi la 8 .....	597
 <b>Rejea zilizotumiwa</b> .....	 599

## UTANGULIZI

Lengo la kuumbwa watu na kuletwa hapa ulimwenguni ni kumuabudu Mola wao, Allah (s.w), kama inavyobainishwa katika Qur-an:

﴿٥١﴾ وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ

*"Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu". (51:56)*

Kumuabudu Allah (s.w) kama lengo la maisha ni kumtii Allah (s.w) kwa unyenyekevu katika kila kipengele na kila nukta ya maisha ya mtu akiwa binafsi na akiwa katika jamii.

Sijambo linalowezekana kwa watu kufikia lengo hili la kumuabudu Mola wao katika kila nukta ya maisha yao ya kibinafsi na kijamii bila ya kuwa na mfumo wa maisha ya jamii unaofuata mwongozo wa Allah(s.w) katika kila kipengele. Ilivyo ni kwamba watu wameumbwa katika hali ya kutofautiana vipaji, uwezo, na kadhalika, hali ambayo inawalazimisha kuishi maisha ya kijamii. Hapana mtu yeyote anayeweza kujitosheleza kwa kila kitu bila ya kuwategemea wenzake. Hivyo, kama mfumo wa maisha ya jamii haukuwekwa katika hali ya kumtii Allah (s.w) katika kila kipengele cha maisha ya jamii kama vile siasa, uchumi, elimu na utamaduni na kadhalika. Mtu binafsi hawezi kufikia lengo la kuumbwa kwake.

Hivyo, ili watu waweze kumuabudu Mola wao katika kila kipengele na kila nukta ya maisha yao, hawanabudi kwanza, kuwa waumini wa kweli wa Allah (s.w) na kisha kufanya juhudi za makusudi za kuwa **makhalifa** wa Allah katika jamii. **Makhalifa** wa Allah ni wale wanaoiongoza jamii kwa kufuata mwongozo wa Allah (s.w) kupitia kwa Mitume yake na vitabu vyake. Waumini wakifanya jitihada za kusimamisha **ukhalifa** katika jamii, Allah (s.w) ata wawezesha kufikia lengo la kuumbwa kwao kama anavyoahidi:



وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي  
 الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي  
 ارْتَضَى لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي  
 شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٥٥﴾

*"Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, kuwa atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya makhalifa wale waliokuwako kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia Dini yao Aliyowapendelea, na atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu, hawanishirikishi na chochote. Na watakaokufuru baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri zetu." (24:55)*

Aya hii inatuweka wazi kuwa tutaweza tu kumuabudu Allah (s.w) katika kila kipengele cha maisha ya kibinafsi na kijamii pale tu Dola ya Kiislamu itakapo simama katika jamii. Ni kwa msingi huu Allah (s.w) ameleta Mitume mbali mbali kuanzia Mtume wa kwanza, Adam (a.s) mpaka Mtume wa mwisho, Muhammad (s.a.w) kwa lengo la kusimamisha uadilifu katika jamii ili kuyafanya maisha ya binaadamu yawe ya furaha na amani.

Kuhusu lengo la kuletwa mitume wote kwa ujumla Allah(s.w) anatumfahamisha:

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ  
 لِيَتَّقُوا اللَّهَ بِالْقِسْطِ وَأَنزَلْنَا الْحَدِيدَ فِيهِ بَأْسٌ شَدِيدٌ وَمَنفَعٌ لِلنَّاسِ  
 وَلِيَعْلَمَ اللَّهُ مَن يَنصُرُهُ وَرُسُلَهُ بِالْغَيْبِ إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٢٥﴾

*"Kwa hakika tuliwapeleka Mitume wetu kwa dalili wazi wazi na kuteremsha vitabu na uadilifu pamoja nao, ili watu wasimamie uadilifu(haki). Natukateremsha chuma chenye nguvu nyingi na manufaa kwa watu; na ili Mwenyezi Mungu ajulishe anayemnusuru na mitume yake, na hali ya kuwa hawamuoni Mwenyezi Mungu. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu,mwenye kushinda." (57:25)*

Kwa mujibu wa aya hii suala la kusimamisha uadilifu(haki) katika jamii ni suala la lazima kiasi kwamba Allah(s.w) ameumba chuma (madini) kwa ajili ya kutengeneza silaha zitakazo wawezesha mitume na waumini kusimamisha uadilifu(haki) katika jamii.

Lengo la kuletwa Mtume wa mwisho, Muhammad(s.a.w),nalo linabainishwa katika aya ifuatayo:

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظَاهِرَهُ  
عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٢٢﴾

*"Yeye(Allah) ndiye aliyemtuma Mtume wake(Muhammad) kwa uongofu na kwa dini ya haki ili kuifanya iwe juu ya dini zote (itawale katika jamii) iwapokuwa washirikina watachukia." (9:33,61:9)*

Kwa mujibu wa aya hii washirikina ni wale wote wanaofuata mifumo ya maisha mbali na Uislamu. Mtume(s.a.w), katika mchakato wa kuutawalisha Uislamu katika jamii, washirikina walichukia na kupambana naye kwenye vita mbalimbali, yeye mwenyewe aliongoza vita 27 na hatimaye Uislamu ulishinda na kuwa juu ya mifumo yote ya masisha na ulimwengu ukashuhudia hivyo kama Qur'an inavyobainisha:

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ ۗ

وَكَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا ﴿٢٨﴾

*Yeye ndiye aliyemtuma, (aliyemleta) Mtume wake kwa uwongofu na dini iliyo ya haki, ili ishinde juu ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Shahidi. (48:28)*

Kwa kuwa hapana Mtume mwingine atakayekuja baada ya Muhammad(s.a.w),Qur'an(33:40), waumini wa ummah huu, kwa kumfuata Mtume(s.a.w) na mitume wote waliotngulia, wanadhima ya kusimamisha uadilifu (haki) katika jamii kwa kuutawalisha Uislamu juu mifumo yote ya maisha iliyopo ili waweze kumuambdu mola wao katika kila kipengele cha maisha yao.

Juzuu hii ya sita imekusudiwa kuwaonesha waumini, kwa kurejea historia, uwezekanao wa kutekeleza dhima hii kuu ya kuutawalisha Uislamu katika jamii. Ili kuwafikisha wasomaji kwenye lengo tarajiwa, juzuu hii ya "Historia ya kuhuisha Uislamu katika Jamii," kuanzia Mtume Adam(a.s)mpaka hivi leo, imewasilisha maudhui yake kwa anuani ya mada kuu zifuatazo:

1. Dhana juu ya Historia.
2. Historia ya Uislamu kabla ya Muhammad(s.a.w).
3. Historia ya Uislamu wakati wa Muhammad(s.a.w).
4. Ungozi wa Dola ya Kiislamu wakati wa Makhalifa wa Mtume(s.a.w).
5. Kuhuisha Uislamu wakati wa Tabiin.
6. Kuhuisha Uislamu wakati wa Tabiin Tabiin.
7. Kuhuisha Uislamu katika karne ya 20 A.D.
8. Historia ya kuhuisha Uislamu Tanzania.

Kutokana na mafunzo haya ya kihistoria na msisitizo wa Qur'an na Sunnah juu ya umuhimu wa kuhuisha na kusimamisha

Uislamu katika jamii, ni tumaini letu waislamu wa kweli wataliendea kwa usahihi na kwa juhudi kubwa suala zima la kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii.



# *Sura ya Kwanza*

## **DHANA JUU YA HISTORIA**

Historia kama somo ina sehemu kubwa sana ya kuchangia katika maendeleo ya mwanadamu. Ni kutokana na historia binaadamu wa leo hufahamu vipi watu waliotangulia walifanikiwa au walifeli katika maisha yao. Na hivyo kujifunza juu ya namna ya kuyakabili mazingira yake.

Hata hivyo fundisho lolote lipatikanalo kutokana na historia, linategemeana sana na mtizamo wa muhusika juu ya historia. Ipo mtizamo mkuu miwili: **Mtizamo wa Kiislamu** na **Mtizamo wa Kikafiri**. Kabla hatujaendelea na lengo letu la kuangalia historia katika Uislamu, ni vyema tuone makafiri wanasema nini juu ya historia

### **Mtizamo wa Kikafiri Juu ya Historia na Udhaifu Wake**

Historia kwa waandishi wengi wa kileo hufasiriwa kama ni kumbukumbu ya matendo ya mwanadamu. Matendo hayo yawe ni yenye kumwezesha mwanadamu kupata mahitaji yake muhimu kutoka kwenye maumbile ya asili (nature). Kwa makafiri mahitaji muhimu ya wanadamu ni **chakula**, **nguo** na **makazi**. Kwa hiyo matendo yote ya mwanadamu yana lengo moja tu; la kumpatia mahitaji muhimu ya maisha ambayo ni **chakula**, **nguo** na **makazi**.

Kwa mtizamo wao huo makafiri wameyahusisha matendo yote ya mwanadamu na uzalishaji vitu au uzalishaji mali (Material Production). Kwa hiyo basi wakawa wanaiangalia historia katika ngazi mbili. Katika ngazi ya kwanza huiangalia historia kama somo lenye kuelezea mapambano ya mwanadamu dhidi ya mazingira yake. Mapambano ambayo ni ya lazima ili mwanadamu aweze kupiga hatua katika maendeleo.

Katika ngazi ya pili, makafiri huitazama historia kama somo lenye kuonyesha vipi harakati za uzalishaji mali zinavyoathiri uhusiano baina ya mtu na mtu.

Hii ni kutokana na imani yao kuwa mwanadamu ni mnyama kama wanyama wengine. Na badiliko lolote litakalotokea kwa binadamu aonekane tofauti na wanyama wengine, basi litakuwa ni zao la harakati zake dhidi ya maumbile (Nature). Kwa hiyo kwa makafiri kusoma historia ni muhimu kwa sababu huwasaidia kuelewa mabadiliko ya mahusiano kati ya mtu na mazingira yake na kati ya mtu na mtu. Na kwa njia hiyo wanaweza kufahamu hali ya mwanadamu iliyopita na ya sasa na hivyo kuweza kujiandaa ili kuukabili vyema wakati ujao.

Mtizamo huu wa makafiri katika kuiainisha historia una udhaifu mkubwa sana. Wao wamemtazama mwanaadamu na mazingira yake au kwa maneno mengine viumbe na mazingira yao na kumwachilia mbali Muumbaji wa vyote hivyo viwili.

## **Mtizamo wa Makafiri Juu ya Chanzo cha Dunia, Mwanaadamu na Lengo la Uhai Wake.**

Baada ya kuona mtizamo wa kikafiri juu ya historia, itakuwa ni vyema tuone wanasema nini juu ya chanzo cha dunia, mwanaadamu na lengo la uhai wake. Katika kukiendea kipengele hiki tutaangalia hoja za wanafalsafa wa kisoshalist au wakomunist. Kisha tutaangalia wanasayansi wanavyosema. Hii itatusaidia kufahamu endapo ukafiri (ukanaji kuwepo kwa Mola Muumba) ni zao la maendeleo ya sayansi au la.

Kutokana na maelezo ya makafiri, chanzo cha Ulimwengu, mwanaadamu na vitu vyote kwa jumla ni maada (matter) ambayo haina mwanzo wake wala mwisho wake. Uhai ulitokea kwa bahati nasibu na hakuna mwanzilishi wala mwenye kuuongoza uhai.

Makafiri hudai vile vile kuwa binadamu ni zao la kiumbe dhalili chenye chembe hai moja tu (Unicellular creature) ambacho kilibadilika kutoka katika hali hiyo ya uduni kupitia hatua ya kuwa pweza, chura, mjusi, nyani hadi kuwa mtu kamili. Kwa hivyo kwa makafiri binaadamu ni zao la mabadiliko ya kidogo kidogo (evolutionary changes) na kwamba hakuumbwa na Allah(s.w). Kwani tangu hapo kwa Mtazamo wao Allah(s.w) hayupo (wana'uudhubillah).

Jitihada kubwa sana zimefanyika kuzieneza fikra hizi na zimepewa umuhimu mkubwa katika somo la Historia mashuleni. Tukiangalia kitabu cha historia cha shule za sekondari kidato cha kwanza, kilichotolewa na Taasisi ya Elimu – Tanzania ukurasa wa 11 kuna maelezo yafuatayo juu ya chanzo cha mwanadamu:

### **Origin of Man:**

*“Man came into existence together with other animals more than thirty million years ago. In the beginning, man belonged to the family of primates which include apes, monkeys, and gorillas. These primates lived in troops in trees. As well as walking on all fours, these primates had developed different uses for their limbs.*

*The fore-limbs were used for catching and gripping. Hind-limbs were used for standing on branches or on the ground. As the forests became smaller some of these primates had to live in open grasslands.*

*The new environment and experience forced this primate to adopt to life in the grasslands. Over time his hind-limbs became specialized for walking and standing. For example, he had to stand up, watch out for enemies and run away from them. This freed the fore-limbs which could now be used for tool using. He used sticks to dig-up roots or turn-over stones in the search for insects.*

*Using tools and bi-pedalism were accompanied by the development of the brain. These three were very crucial changes*

*in the evolution of man, who began to appear different from other animals. However man is distinguished from the other primates by his ability to design tools for specific purposes.*

*At first the body of man's ancestors was closer to that of chimpanzee in appearance. It was huge and covered with plenty of hair. Gradually as he developed by improving his methods of obtaining food, shelter, and clothing his shape became that of a modern man. By about 50,000 years ago true man had appeared. This process is known as evolution."*

Kwa muhtasari mwandishi anasema kuwa:

- Mwanadamu na wanyama wengine wametokea zaidi ya miaka milioni thelathini iliyopita.
- Awali binadamu alikuwa ni katika kizazi cha manyani, akiishi mitini na kutembea kwa miguu minne.
- Kadri zilivyopita siku misitu ilipungua, hivyo ikabidi manyani waishi nyikani. Mazingira haya ya wazi yalimlazimisha nyani kusimama kwa miguu miwili ili aweze kuona maadui toka mbali. Hali hii ikamkomboa nyani-mtu kutokana na kutembelea miguu minne.
- Wakati huo huo akawa anatumia miguu ya mbele kuchimba mizizi na kuchuma matunda. Aidha akili yake ikakua na kupea zaidi. Hatimae miaka 50,000 iliyopita alitokea mtu tunayemwona leo.
- Mchakato huu wa kutokea binaadamu na viumbe vingine unajulikana kama "evolution".

Huo ndio mtizamo wa makafiri juu ya chanzo cha mwanadamu. Mtizamo ambao kila kukicha hupandikizwa kwenye vichwa vya kizazi kichanga katika somo la Historia mashuleni.



## **Chimbuko la Mtizamo wa Makafiri Juu ya Chanzo cha Dunia na Mwanadamu.**

Labda itakuwa vyema kabla ya kuchambua mtizamo huu wa makafiri huu wa kumkana muumba juu ya chanzo cha dunia na mwanadamu, tuangalie kwanza chimbuko la mtizamo wenyewe.

Karl Marx, mwanzilishi wa itikadi ya kijamaa hutambulika katika karne ya ishirini kuwa ndiye chimbuko la ukafiri huu wa kumkana muumba(atheism). Hatumaanishi hapa kuwa kabla ya Karl Marx hawakuwepo makafiri, la. Bali tunamtaja yeye kwa vile ndiye aliyechukua jitihada kubwa kuusomesha na kueneza ukafiri huu katika zama zetu hizi. Ukafiri ulioshadidi katika nchi zilizokuwa zikijiita za kikomunisti ni zao la kazi ya Karl Marx.

Kwa fikra zake Marx, na wafuasi wake, ulimwengu huu hauna muumba na kwamba ulimwengu huu huongozwa na kanuni za kibaiolojia, kikemia na kifizikia. Na hivyo basi sayansi ndio jawabu la kila kitu. Kutokana na dhana hii Karl Marx na wafuasi wake hukana kuwepo kwa Allah(s.w) kwa hoja kwamba imani juu ya Allah(s.w) ni imani ya kibubusa na kwamba kumkana Allah(s.w) ni suala la kisayansi.

## **Chimbuko la Fikra za Karl Marx**

Kwa vile Juzuu yetu hii inaangalia suala zima la historia, itakuwa vyema tuonyeshe kwa muhtasari chimbuko la fikra za Marx. Kuibuka kwa fikra za Marx na makafiri wengine juu ya chanzo cha dunia na suala la kuwepo Mungu Muumba kwa ujumla, kumechochewa na hali ya kutisha iliyoondoa mahusiano yote kati ya Dini na maisha huko Ulaya, hatimaye kutenganisha itikadi ya Dini na utaratibu wa maisha ya kijamii. Hali hiyo ilitokeaje?

**Kwanza**, Kanisa lilihodhi peke yake haki ya kuelewa na kuifafanua Biblia kwa kumkataza mtu yeyote nje ya makada wao kujaribu kuelewa na kuifahamu Biblia. Halafu kukafuatia kuingiza

katika mafundisho ya Dini hiyo imani za kibubusa (dogmas) ambazo zilikuwa hazieleweki, hazikubaliki na wala haziaminiki. Kanisa likazifanya imani hizo zisizoeleweka “mafumbo ya Mungu” au “ibada”. Mfano dhahiri ni imani ya kibubusa juu ya Ekaristi (Chakula cha jioni cha Bwana) imani ambayo ilipingwa na Martin Luther, John Calvin na Ulrich Swingli na kuanzisha madhehebu ya Waprotestanti.

Suala la Ekaristi ni uzushi usio na msingi wowote katika kitabu kitakatifu, katika historia ya Wakristo wa mwanzo na hata katika mabaraza ya Kanisa.

Kilichotokea ni kwamba kwa mila zao Wakristo walikuwa wakila mkate na kunywa mvinyo wakati wa pasaka na wakakiita chakula cha jioni cha Bwana. Hatimaye Kanisa likadai kuwa mkate na mvinyo vilibadilika kuwa mwili na damu ya Yesu. Yeyote atakayekula mkate na mvinyo wakati wa kuingia katika Dini hiyo atapata Rehema kwa kupitia mwili na damu ya Yesu. Kanisa likashinikiza dai hili kwa wafuasi wake na likakataza mijadala ya hoja kwa tishio la kutengwa.

Zaidi ya imani hizi potofu zilizoingizwa katika Dini hiyo zilizoandamana na kuwakatiza watu kuzithibitisha katika Biblia (ambayo walizuiwa kuifafanua), Kanisa likajiingiza katika kutoa nadharia juu ya uhai na ulimwengu. Likaziunga mkono nadharia fulani fulani za kijiografia, kihistoria na kifizikia zilizokuwa maarufu wakati huo, nadharia ambazo zilijaa makosa na udhanifu wa ajabu na Kanisa likadai kuwa nadharia hizo hazihojiki, hazisahihishiki, hazipingiki na hazibadilishiki.

Hili lilikuwa pigo la mwisho kwani imani hizo zisizokuwa za kisayansi zilikuwa zimejengwa juu ya uwongo, na hivyo rahisi kutenguliwa kwa majaribio mepesi tu. Zaidi ya hayo kutafuta na kuthibitisha elimu ni jambo ambalo Mwenyezi Mungu ameusia akili ya binaadamu kudadisi kwa makini upeo wa uwezo wake bila Mwenyezi Mungu kutanguliza tafsiri maalum.

Juu ya hilo, A. Nadwi anaelezea kwa ufasaha kama ifuatavyo juu ya matokeo ya msiba huu mkuu katika kitabu chake mashuhuri, **“What the World Lost by Muslim Decadence”**.

*“Moja ya makosa makubwa yaliyotendwa na mapadri wa Kizungu, na pengine laweza kuwa kosa kubwa kabisa lililofanywa dhidi ya Dini ni kwamba waliingiza katika vitabu vyao vitakatifu baadhi ya elimu za kibinaadamu na habari za zama zao juu ya historia, geografia na sayansi ya maumbile. Habari hizo za sayansi zilizoingizwa wakati huo zilionekana sahihi kabisa na ikadhaniwa kuwa ni kweli zisizo shaka na zisizoweza kutangulika”.*

*“Hata hivyo, kilele cha elimu katika kipindi fulani si kauli ya mwisho na elimu haituami, kwani elimu ya binadaamu daima huongezeka na hukua. Lau Dini itajengwa juu ya elimu ya binadaamu, basi jengo hilo limesimama katika mchanga unaodidimia. Yawezekana kuwa mapadri walipandikiza katika vitabu vyao habari hizo kwa nia njema kabisa. Lakini wamejidhuru wenyewe na Dini yao, kwani mapandikizi hayo yalianzisha mapambano yasiyofaa kati ya sayansi, hoja na ‘Dini’, na hatimaye ‘Dini’ ilishindwa vibaya sana. Ilikuwa ni Dini ambayo kweli na urongo na haki na batili vimechanganywa na hivyo watetezi wake wasingeweza kupata chochote isipokuwa kushindwa ambako hawakuweza tena kurudisha hadhi yao. Kibaya zaidi ni matokeo yake; kwani Ulaya yote ilipuuza au karibu kuikana kabisa Dini”.*

*“Zaidi ya hayo, mapadri waliyainua tena yote yaliyoelezwa na yalikuwa yakijulikana na kila mtu pamoja na sehemu ya ufafanuzi wa Agano la Kale na JIpya kuhusu jiografia na sayansi ya maumbile. Wakazipa habari hizi **“utukufu wa kidini”** na wakazifanya kuwa ni sehemu ya Dini na hivyo kila mtu lazima aamini na akikatae kilicho kinyume na habari hizo. Wakaandika vitabu juu yake na wakauita*

udhanifu huo wa jiografia '**Jiografia ya Kikristo**' na wakaishikilia kwa jino na ukucha na kila asiyeamini udhanifu huo akaitwa mpagani”.

“Yote hayo yalitokea katika kipindi ambacho hoja ilikuwa ikiibuka huko Ulaya na wanasayansi walikuwa wakianza kuvivunja vizingiti vya ‘Dini’, na kuikosoa jiografia ya Kikristo waziwazi pamoja na vitabu vyake vingine wakatangaza kutoamini kwao fikra hizo kuwa ni takatifu na wakaonesha ugunduzi wao kupitia majaribio yao. Hili likaamsha ghadhabu ya Kanisa na viongozi wao huko Ulaya wakawahesabu wanasayansi hao kuwa ni wapotofu na makafiri. Hivyo wakaimwaga damu yao na wakawanyang’anya mali zao kwa madai kuwa wanautetea Ukristo, na zikaanzishwa Mahakama za Uchunguzi ili kuwaadhibu wale ambao kwa maneno ya papa ‘wale makafiri na waasi waliotawanyika katika miji, nyumba, misitu, mapango na mashamba’.

Mahakama za Uchunguzi hazikupoteza muda na zikafanya kazi kwa mori na zikajitahidi zilivyoweza kumteketeza kila adui katika ulimwengu wa Kikristo. Wakaanzisha taasisi za wapelelezi katika nchi zote, wakichunguza kila mtu kwa msisitizo ambao ulimfanya mwanatheolojia mmoja wa Kikristo aseme, “hakuna mtu awezaye kuwa Mkristo na kufa katika hali ya kawaida”.

“Inahisiwa kuwa walioangamizwa na mahakama hizi walifika elfu mia tatu, na kati ya hao elfu thelathini na mbili walichomwa moto wakiwa hai. Miongoni mwao alikuwepo mwanafizikia mashuhuri Bruno ambaye fikra zake juu ya uwingi wa ulimwengu zilighadhibisha kanisa kiasi ambacho walimwua bila kumwaga tone la damu. Hii ilikuwa na maana ya kumchoma moto akiwa hai! Alikuwepo pia mwanasayansi maarufu **Galileo** aliyeamini kuwa dunia inalizunguka jua na imani yake ilimgharimu uhai wake”.

*“Mambo yalipofikia hatu hii, wasomi na wagunduzi walishindwa kuvumilia na wakatangaza uasi wao dhidi ya Kanisa, mapadri na dhidi ya wote wanaoshikilia ukale. Wakakipinga kila kilichohusiana nao iwe imani au elimu, sayansi au maadili. Wakajenga uadui kwanza na dini ya Kikristo, halafu na dini zote bila kubagua; na mapambano kati ya wanasayansi na hoja dhidi ya viongozi wa Dini ya Kikristo yakawa ni mapambano kati ya sayansi na dini kwa ujumla. Wanamapinduzi wakahitimisha kuwa sayansi na Dini havipikiki chungu kimoja. Mtu ilimpasa achague moja na asuse jingine. Dini kwao ilileta kumbukizi za damu za mashahidi waliopoteza maisha yao kwa ajili ya sayansi na utafiti na kumbukizi za watu wasio na hatia waliouliwa kwa sababu ya ukatili wa mapadri na kwa sababu ya kutoamini kwao. Katika akili zao Dini ilileta taswira ya nyuso zilizosawajika, zenye ukali na mapaji ya uso yenye makunyazi, ghadhabu isiyo na subira na ujinga usio kiasi. Walichukizwa katika nyoyo zao na wakaamua kuchukia na kupigana dhidi ya Kanisa na kila walilowakilisha au walilohubiri. Vizazi vilivyofuata vilirithi hisia na kumbukizi hizi chungu”.*<sup>1</sup>

Marx alikuwa miongoni mwa wanafalsafa walioathiriwa na hali hiyo. Lakini kosa walilofanya ni kule kushindwa kutofautisha Dini na wale waliohodhi uongozi wa Dini. Kwa vile Ukristo (dini) huo kule Ulaya ndio ulikuwa ukiongoza mafundisho juu ya kuwepo kwa Mungu Muumba na kwa vile chuki ilishamea dhidi ya dini, Marx na wenzake walijitoa kwenye dini na hivyo kujitoa kwenye imani juu ya kuwepo kwa Mungu Muumba.

## **Nadharia za Kikafiri na Sayansi**

Karl Marx pamoja na makafiri wote kwa ujumla, katika kuzielezea nadharia zao juu ya ulimwengu na uhai, huzihusisha sana na sayansi. Kwa hakika hudai hasa kuwa nadharia zao ni zao

la magunduzi ya kisayansi. Marx mwenyewe na rafiki yake Engels waliitathmini na kuitumia nadharia ya Darwin ya “Evolution”.

Marx na Engels waliiangalia dhana ya chanzo cha mwanaadamu aliyobuni Darwin kama ni upembuzi wa kiyakinifu (Dialectical-materialist) katika chanzo chake. Hata hivyo wanasisitiza kusema kuwa Darwin mwenyewe hakuwa na habari na dhana hiyo (kuwa yeye ni Mpembuzi - dialectician). Hivyo basi Marx na Lenin katika mafundisho yao hawakuegemeza tu katika mafanikio ya elimu ya jamii na mafunzo ya kihistoria bali pia waliegemeza katika uvumbuzi wa elimu ya kimaumbile ya wakati wao. Uvumbuzi huu ndio uliokuja kuzaa falsafa ya kisayansi ijulikanayo kama “dialectical and historical materialism” (uyakinifu wa kihistoria na kipembuzi).

Bila shaka maelezo haya yatakuwa yametupa picha ni vipi falsafa ya Marx ya kukana kuwepo Mungu Muumba aliyoiita upembuzi na historia ya kiyakinifu, ilihusishwa na sayansi. Lakini je, wagunduzi wa zama hizo kama Darwin walikuwa wanasayansi kweli? Sayansi ya leo inasemaje juu ya ugunduzi wao?

## **Ukafiri si Zao la Sayansi**

Yawezekana kabisa kina Darwin walikuwa wanasayansi wakubwa katika zama zao. Lakini jambo la hakika ni kuwa kina Darwin hawakufahamu kabisa juu ya uhai na hivyo hawakutumia nadharia za kisayansi katika kuelezea chanzo cha uhai. Bali walitumia njia iitwayo “Naturalistic point of view”.(Nadharia ya kimaumbile)

Darwin na wenzake katika moja ya vikao vyao wanakiri kutofahamu uhakika wa uhai katika maeneo yafuatayo:

*“The Scientist’s approach to the origin of life is not in need of an exhaustive definition of what life is. We must attack from the naturalistic point of view, namely, that principles*

*unknown or unknowable to science can not be used to solve the problem. In other words, we proceed under the assumption that life is a process that escapes at present our complete understanding only for reasons of its complexity”.*<sup>2</sup>

Tafsiri:

*“Mtazamo wa kisayansi juu ya chanzo cha uhai hauhitaji kujiuliza uhai (maisha) ni nini. Hatuna budi kuangalia nadharia za kimaumbile. Misingi yote isiyotambulika kisayansi haiwezi kujibu suala hili. Hivyo ni laizma tufahamu kuwa tunaonokea na dhana kuwa uhai (maisha) uko mbali na ufahamu wa binaadamu katika maisha ya leo.”*

Maelezo haya ya Darwin na wenzake yapo wazi – kwamba nadharia zao wamezijiunga juu ya dhana tu na kwamba hawaelewi hakika ya uhai kwa sababu ya utata wake. Bila shaka mwenye akili timamu hawezi kuikubali nadharia iliyojengwa juu ya dhana na si hivyo tu, bali dhana ya mtu asiyelewa hakika ya kitu anachokitolea nadharia.

Jambo la kushangaza zaidi ni kule kuona jinsi makafiri wanavyoing’ang’ania dhana ya Darwin na kuiita ya Kisayansi, wakati Darwin mwenyewe anakiri kuwa nadharia yake ya ‘evolution’ ni imani tu ambayo hata yeye mwenyewe hawezi kuithibitisha. Kwa maneno yake Darwin anasema:

*“Lakini naamini mabadiliko ya kimaumbile, sio kwamba naweza kuthibitisha angalau jamii moja kwamba imebadilika kutoka hali moja hadi nyingine, ila kwa sababu yanagawanya na kueleza vizuri (kama nionavyo mimi) ukweli wa mambo juu ya mgawanyo wa aina mbali mbali, taaluma ya ufanyikaji na ukuaji wa mtoto tumboni (embryology), ufanyikaji na mgawanyiko wa miti na wanyama, viungo chipukizi, mabadiliko ya udongo na mgawanyiko wake.”*<sup>3</sup>

Bila shaka maelezo haya ya Darwin mwenyewe yathibitisha wazi jinsi nadharia ya 'evolution' isivyokuwa ya kisayansi. Kwa hivyo basi mtizamo wa makafiri juu ya chanzo cha uhai na mwanaadamu kwamba hakuna muumba, bali ni zao la "evolution" ni imani potofu isiyo na misingi ya kisayansi.

Labda ingekuwa vyema pia kuonyesha hapa kuwa, hata hao wanasayansi walioiendeleza dhana ya Darwin ya 'evolution' wamekiri kuwa inaudhaifu mkubwa kwa sababu inashindwa kujibu maswali mengi ya msingi. Bwana Harlay Shapley katika makala yake "On the Evidences of inorganic evolution", ana haya ya kusema:-

*"Sababu yetu nzito ni kusema kuwa dunia nzima iliibuka kama ilivyo, lakini namna ilivyoibuka, kutoka wapi na wapi inapoelekea, ni miongoni mwa masuala tusiyoyajua".*

Nadharia ambayo inashindwa kujibu maswali hayo ya msingi ni dhahiri kuwa haiwezi kutupa jibu sahihi juu ya chanzo cha uhai, mwanadamu na lengo la kuumbwa kwake.

Swali la kujiuliza hapa ni kuwa inakuwaje makafiri kuichukua dhana ambayo udhaifu wake umeshadhihirishwa si tu na waasisi wake bali hata na dhana yenyewe?

Tumeona kwenye kurasa za nyuma kuwa Karl Marx alikuwa miongoni mwa wanafalsafa wa karne ya 19 waliokuwa na chuki kali dhidi ya Ukristo (dini). Kwa hiyo alikuwa tayari kutumia silaha yoyote kutokomezee mbali dini.

Kwa upande mwingine tunaona kuwa dhana ya Darwin ya 'evolution' inapinga kuwepo kwa Muumba (Materialistic doctrine). Hivyo kwa vile Marx na wenzake walihusisha suala la kuamini kuwepo kwa Mungu Muumba na dini, waliona dhana hii ni silaha nzuri sana ya kuipiga vita dini.




Maelezo yote haya yaliyotangulia yanaweka wazi kwamba: Ukafiri si zao la sayansi, na pili ni kuwa nadharia ya ‘evolution’ ya Darwin inayoendelea kupaliliwa na kutumiwa na makafiri, sio kwa sababu ni sahihi au ni ya kisayansi bali ni kwa sababu za kiitikadi tu. Ni nadharia ya kikafiri hivyo silaha (nzuri kwa makafiri) ya kupambana na waumini wa Mungu Muumba.

## **Nadharia ya Sayansi Juu ya Chanzo cha Ulimwengu**

Kabla ya kuangalia sayansi inasemaje juu ya kuumbwa kwa Ulimwengu ni bora kwanza tuone sayansi inautazama vipi ulimwengu.(Universe).

### **(i) Jua na Sayari zilizotuzunguka (Solar System)**

Kwa mujibu wa taaluma ya sayansi, Dunia (earth) na sayari nyingine zinazozunguka jua, hufanya ulimwengu (universe) ambao kwa vipimo vyetu vya kibinaadamu ni mkubwa mno. Dunia (earth) yetu hii ipo umbali wa kiasi cha maili 93 Milioni kutoka kwenye jua. Umbali huu ni mkubwa sana kwa mwanaadamu, lakini ni mdogo sana ukilinganishwa na umbali unaolitenganisha jua na sayari iliyo mbali kuliko zote katika “Solar System” yetu hii, Pluto. Umbali baina ya jua na Pluto ni mara 40 zaidi ya umbali kati ya jua na dunia. Yaani kiasi cha maili 3720 Milioni. Pamoja na kuwa mwanga wa jua husafiri kwa mwendo wa kasi sana – mwendo wa maili 186,000 kwa sekunde, lakini huchukua takriban saa 6 kwa mwanga huo kufikia Pluto.



Picha ya Solar System

## (ii) Kundi la nyota (Galaxy)

Jua ambalo dunia yetu na sayari nyingine hulizunguka, lenyewe ni sehemu ndogo sana kati ya mabilioni ya nyota ambazo kwa pamoja hufanya kundi la nyota "Galaxy". Wakati wa usiku tunaona nyota ndogo nyingi sana pamoja, ambazo hufanya kitu kama wingu jeupe angani usiku (The Milky Way). Kundi hili la nyota "The Milky Way", ni kubwa mno kiasi kwamba mwanga husafiri kutoka upande mmoja wa "Solar System" hadi upande mwingine (Cross the Solar System) kwa muda wa saa moja; basi utahitajia kiasi cha miaka 90,000 kusafiri kutoka upande mmoja hadi mwingine wa kundi lililofungamana zaidi (Most Compact) la nyota zinazofanya galaxy yetu. Pamoja na kuwa kundi la nyota "Galaxy" ambamo imo "Solar System" yetu, huonekana kuwa kubwa mno kupita kiasi, ni sehemu ndogo sana ya anga. Kuna mkusanyiko mkubwa sana wa nyota sawa na "Milky Way" ambazo zipo nje ya "galaxy" yetu. Mkusanyiko wa nyota hizo "Galaxies" nje ya "galaxy" yetu uligunduliwa baada ya ugunduzi wa vifaa vya kuonea mbali vya kileo (Modern Sophisticated Optical Instrument).

Hivi ndivyo sayansi ya leo inavyoutazama ulimwengu. Ulimwengu ambao ni mkubwa ajabu, kiasi kwamba akili ya binaadamu haiwezi kudhibiti uhakika wa ukubwa na mipaka yake.

## **Mtizamo wa Sayansi Juu ya Chanzo cha Ulimwengu na Uhai.**

Sayansi ya leo hutufunza kuwa dunia, nyota na sayari zote zina umri maalum na kwamba zimetokea katika kipindi Fulani cha wakati. Hata hivyo ni vigumu mno kwa sayansi kutoa kipindi hakika (tarehe/siku) ulimwengu ulipoanza kutokea. Baadhi ya wanasayansi hukisia kuwa ulimwengu huu umetokea kiasi cha miaka kati ya 15 hadi 20 bilioni iliyopita.

Wanasayansi hutuambia kuwa ulimwengu mwanzoni kabisa umetokana (au umetengenezwa) na hewa au moshi (a gaseous mass) ambayo inakisiwa hasa kuwa ni hydrogen. Hatimaye bongwe hilo la hydrogen lilitenganishwa na kufanya vipande vidogo vidogo ambavyo vilifanya galaxies. Galaxy yetu yakisiwa kutokea miaka kama bilioni kumi iliyopita. Vipande vipande vilivyofanya galaxy ndivyo hivyo vilivyounda Solay System kwa kuchangukana zaidi (fragmentation). Bongwe la mwanzo la hewa (gaseous mass) laweza kuwa limetokea kwa njia ya mshindilio '(condensation)'. Kwa njia hii hydrogen ilitoa helium, kisha Carbon na Oxygen kwa hivyo kukatoka madini ya kila namna.

Kuhusu chanzo cha uhai sayansi hutufahamisha kuwa uhai umeanzia majini na kwamba maji hufanya sehemu kubwa ya chembe hai zote. Viumbe wa mwanzo walikuwa ni wenye chembe hai moja – “Unicellular Organisms” na hivyo walikuwa ni wadogo mno kiasi cha kutokuweza kuonekana na macho ya kawaida (mpaka darubini yenye nguvu sana). Hata hivyo sayansi yatuonyesha kuwa chembe moja (Cell) hiyo ya viumbe hao ilikuwa ina kila kitu ambacho kilihitajika kwa uhai. Palikuwa na “Cytoplasm”, “Nucleus”. “Chromosomes” zenye “genes” na kila chenye kuufanya uhai uwepo. Viumbe hawa wenye chembe hai moja kama “amoeba” wapo hadi hii leo. Na kama tulivyotangulia kutaja wanasayansi hudhani hivi ndivyo viumbe vya mwanzo kutokea.

Maelezo haya ya wanasayansi hutupa picha ni wapi uhai ulianzia na viumbe gani wa mwanzo kutokea. Lakini hayatupi maelezo ni vipi uhai huu wenye utata (complex) kiasi hicho ulitokea. Akishangaa kuhusu utata wa uhai na chanzo chake, Dr. Maurice Bucaille ana haya ya kusema:

*As far as I am concerned, however, the brilliant analysis of the way this system works (for each and every cell is a kind of computer comprised of innumerable interrelations) is just as amazing as the general conclusions cited above concerning the supposed resolution of unexplained facts on the origins of life. One very important question of these investigations: How could a system as complex as this have been formed? Was it the work of chance, following a host of trials and errors? That seems most unlikely. What other logical theories are there? It is common knowledge that a computer will only function if it has been programmed, a fact that implies the existence of a programming intellect, that provides the information required to operate the system. That is the problem facing all thinking people who refuse to accept mere words or groundless theories, people who will only acknowledge conclusions based on facts. Given the present state of knowledge, however, science has not provided any answer to this precise point.*

Tafsiri:

*Kwa namna ninavyoona mimi, kwa jinsi mfumo huu (wa maisha) unavyofanya kazi (kila chembe hai ni kama namna ya kompyuta iliyofanyika kwa ushirikiano na maingiliano ya vitu chungu nzima) ni jambo la kustaajabisha unapoangalia ukweli wa chanzo cha uhai. Suala moja ambalo linafungamana na uchunguzi huu ni kwamba, ni vipi mfumo huu (system) ulio tata (complex) umeweza kuundwa? Je! Ilitokezea kwa bahati nasibu baada ya majaribio? Hii haingii akilini. Kuna ufafanuzi wowote ule? Inabainika wazi kuwa kompyuta haiwezi kufanya kazi bila ya kupangiliwa vyema (programmed), ukweli unaobainisha kuwepo kwa mpangaji mweledi anayetoa habari zinazohitajika*

*katika kuuendesha mfumo huo. Hilo ndilo tatizo linalowakumba watu wenye kutumia akili zao ambao hutaka kujua ufafanuzi wa masuala, watu wanaokataa kukubali maneno matupu yasio na ithibati au nadharia zisizo na utegemezi wowote, watu watakaokubaliana na maelezo yaliyofungamana na kweli tupu. Hata hivyo hadi hivi sasa, sayansi haijatoa jibu lolote lile lililo sahihi.*

Maelezo haya ya mwanasayansi Dr. Bucaille yanatosha kututhibitishia kuwa sayansi haina jibu kamili na sahihi juu ya chanzo cha uhai.

## **Sayansi Yasemaje Kuhusu Dhana Kuwa Mwanadamu Katokana na Kizazi cha Manyani.**

Wanahistoria wa Kikafiri hudai kuwa mwanaadamu ametokana na kizazi cha manyani kama tulivyoona kaitka kurasa za nyuma. Wao huinasibisha dhana yao hiyo na sayansi. Madai hayo ni uwongo; kwani sayansi haikubaliani kabisa na dhana hiyo. Hapa tunapenda tumnukuu tena mwanasayansi mashuhuri Dr. Maurice Bucaille (Surgeon) akitoa maelezo juu ya chanzo cha mwanadamu:

*There is absolutely no scientific proof to suggest that man was born of the evolved forms of present-day apes. On the contrary, everything argues against this outmoded theory. What science has shown is that, at a certain point in time, a human species appeared which gradually transformed itself into today's man. From a scientific point of view, the crux of problem is that we do not know what man evolved from: Was it from an autonomous lineage or from one that could be connected with another animal lineage? Science does not supply indisputable indication as to the actual moment that the transformation took place; nor on the initial matter employed in the process: Many of the ways in which the change occurred remain a mystery to us.*

## Tafsiri:

*Hakuna ushahidi wowote wa kisayansi unaosema kuwa binaadamu alitokana na nyani hawa wa siku hizi. Kinyume chake ni kuwa nadharia hii ya kale inapingwa. Sayansi imeonyesha kuwa katika wakati fulani, binaadamu alianza kukua kidogo kidogo (hatua kwa hatua) mpaka kufikia hii hatua aliyo leo. Katika mtazamo wa kisayansi, ugumu wa tatizo uko kwenye suala la binaadamu alitokana na nini? Je, ilikuwa kutokana na uzao usiojulikana au uzao ambao unaweza kuhusishwa na wanyama. Sayansi haitoi dalili zisizopingika (zisizo na mushkeli) zinazoeleza ni lini chanzo cha binaadamu kilianza, wala dalili zinazoonyesha kitu cha mwanzo kinachohusika na chanzo hicho. Ni kusema kuwa njia nyingi zinazoonyesha namna mabadiliko yalivyotokea, hatuwezi kuzielezea.*

Hatuhitaji kutoa maelezo zaidi kuweka wazi kuwa mwanaadamu hatokani na nyani, kwani maelezo haya ya Dr. Bucaille yapo wazi kabisa. Neno la kusisitiza hapa tu ni kuwa, maelezo mengi yaliyo kwenye vitabu vya historia kuwa binaadamu katokana na kizazi cha manyani si maelezo ya kisayansi. Bali makafiri huingizilia sayansi ili wapate kuustawisha ukafiri wao.

## **Mtizamo wa Uislamu Juu ya Historia**

Imeshabainishwa kuwa Historia, kwa ujumla, ni kumbukumbu za matendo na matukio yanayohusu maisha yote ya mwanaadamu katika jamii yake kwa muda wote uliopita.

Uislamu unaitizamaje Historia ya mwanaadamu? Mtizamo wa Uislamu juu ya historia kwa ujumla anatofautiana sana na ule wa makafiri. Ambapo makafiri wanadai kuwa hapana Muumba wa Ulimwengu na vyote vilivyomo kwa ujumla, Uislamu unauhusisha Ulimwengu (Universe) na vyote vilivyomo akiwemo mwanaadamu, na Muumba mmoja tu Mwenye Hekima na Ujuzi usio na kikomo, ambaye ameumba kila kitu kwa lengo maalumu.

## Lengo la Maumbile Yote Yaliyomzunguka Mwanaadamu.

Mwenyewe Muumba Allah(s.w), anabainisha lengo la kumbwa mbingu na ardhi na vyote vilivyomo katika aya zifuatazo:

هُوَ الَّذِي خَلَقَ لَكُمْ مَّا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا ثُمَّ أَسْتَوَىٰ إِلَى السَّمَاءِ

فَسَوَّاهُنَّ سَبْعَ سَمَوَاتٍ وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٢٩﴾

*“Yeye (Allah) ndiye aliyekuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi, tena akakusudia kuumba mbingu; na akazifanya mbingu saba. Naye ndiye ajuaye kila kitu” (2:29).*

وَلَقَدْ مَكَّنَّاكُمْ فِي الْأَرْضِ وَجَعَلْنَا لَكُمْ فِيهَا مَعِيشًا قَلِيلًا مَّا تَشْكُرُونَ ﴿١٠﴾

*“Na hakika tumekumakinisheni (tumekukalisheni) katika ardhi na tumekuwekeeni humo (vitu vyote) vinavyohitajia maisha yenu. Ni shukurani chache tu mnayoshukuru” (7:10).*

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa maumbile yote ya ardhini na mbinguni(angani) yaliyomzunguka mwanaadamu, anayoyaona na asiyoyaona, yote yako pale kwa ajili ya kumtumikia na kuboresha maisha yake. Ili kufikia lengo hili, Allah(s.w) amevitiisha vitu hivi kwa mwanaadamu kwa kuviwekea sheria madhubuti za kimaumbile (natural laws):

وَسَخَّرَ لَكُمْ مَّا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا مِنْهُ

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿١٣﴾

*“Na amekutiisheni vilivyomo mbinguni na ardhini, vyote vimetoka kwake.”Bila shaka katika haya zimo alama kwa watu wanaofikiri (45:13).*

Kisha, mwanaadamu akatunukiwa akili na vipawa vya fahamu na elimu ya kumuwezesha kuyatumikisha maumbile kwa ajili ya

kuboresha maisha yake. Sayansi na teknolojia ni katika jitihada za harakati za mwanaadamu za kuyatumikisha maumbile na nguvu asili kwa ajili ya kuboresha maisha yake.

## Lengo la Maisha ya Mwanaadamu Hapa Ulimwenguni

Kama vitu vyote vimeumbwa kwa lengo la kumtumikia mwanaadamu, je, mwanaadamu ameumbwa kumtumikia nani? Je, lengo la maisha ni kujipatia tu mahitaji muhimu ya maisha – chakula, nguo na makazi? Mbona wanyama nao wanajitosheleza kwa mahitaji hayo hayo pamoja na kuwa hawakutunukiwa kipawa cha elimu (kujiilemisha) kama mwanaadamu? Je, ni busara kukubaliana na makafiri kuwa lengo la maisha ya mwanadamu ni lile la kutosheleza tu matashi yake ya kinyama? Hii ni dhana tu ya makafiri kama Allah(s.w) anavyotutanabahisha:

وَمَا خَلَقْنَا السَّمَاءَ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا بَطْلًا ذَٰلِكَ ظَنُّ

الَّذِينَ كَفَرُوا فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ كَفَرُوا مِنَ النَّارِ ﴿٢٧﴾

*“Na hatukuumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake bure. Hii ni dhana ya wale waliokufuru. Basi adhabu kali ya moto itawathubutikia wale waliokufuru” (38:27).*

Bila shaka kwa wale wenye akili na busara wanayakini kuwa mwanaadamu hakuumbwa tu bure na kuletwa hapa duniani bila ya lengo lolote analotarajiwa na muumba wake alifikie. Bila shaka mwanaadamu atakuwa na lengo la juu zaidi kuliko viumbe wengine, hasa kutokana na vipawa vya akili na elimu alivyotunukiwa kuliko viumbe wengine. Lengo la kuumbwa mwanaadamu amelibainisha Muumba mwenyewe:

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥١﴾

*“Sikuwaumba majini na watu ila tu wapate kuniabudu” (51:56).*



Maana ya Ibada ni kumtumikia Allah(s.w) katika maisha yetu yote. Kumtumikia Allah(s.w) ni kumfanya Allah(s.w) kuwa ndiye Bwana (Rabb) wetu pekee ambaye ndiye pekee tunayepaswa kumtii kwa unyenyekevu kwa kufuata barabara mwongozo wa maisha aliyotuwekea. Utiifu na unyenyekevu wetu kwa Allah(s.w) utadhihiri pale tutakapopenia kwa moyo mkunjufu kutenda yale yote aliyotuamrisha na anayoyaridhia na kujiepusha mbali kutenda yale yote aliyotukataza na yanayomchukiza katika kuendea harakati za maisha yetu yote ya kila siku. Ibada kwa mtizamo huu inamuhusu kila mtu binafsi na jamii kwa ujumla. Ili kila mtu amuabudu Allah(s.w) inavyostahiki, jamii inawajibika kuweka mazingira ya kumuabudu Allah(s.w) katika kila kipengele cha maisha kwa muda wote kwa kuunda dola yenye mamlaka kamili ya kuamrisha mema yanayoleta furaha na amani katika jamii na kukataza na kuyatokomeza maovu yanayoleta huzuni na vurugu katika jamii.

Pamoja na lengo hili mwanaadamu ametunukiwa akili na vipawa vya fahamu vya kumuwezesha kulifahamu lengo na kuweza kuishi kwalo. Kisha akaletewa Mitume na vitabu vya kumuongoza kutoka kwa Allah(s.w). Lakini wakati huo huo akapewa uhuru kamili wa kuamua kulifuata lengo hilo au kutolifuata. Hapa ndipo mtihani wake ulipo:

إِنَّا خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ مِنْ نُّطْفَةٍ أَمْشَاجٍ نَّبْتَلِيهِ فَجَعَلْنَاهُ سَمِيعًا بَصِيرًا ﴿٢﴾

*“Kwa hakika tumemuumba mtu kutokana na mbegu ya uhai iliyochanganyika (ya mwanamume na mwanamke) ili tumfanyie mtuhani (kwa amri zetu na makatazo yetu) kwa hiyo tukamfanya ni Mwenye kusikia na Mwenye kuona” (76:2).*

أَلَمْ نَجْعَلْ لَهُ عَيْنَيْنِ ﴿٨﴾ وَلِسَانًا وَشَفَتَيْنِ ﴿٩﴾ وَهَدَيْنَاهُ النَّجْدَيْنِ ﴿١٠﴾

*“Je, hatukumpa mtu macho mawili? Na ulimi na midomo miwili? Na tukambainishia zote njia mbili (iliyo nzuri na iliyo mbaya)” (90:8-10).*

Kutokana na mtihani huu historia ya mwanaadamu haiwezi kuishia katika maisha haya ya ulimwengu huu, bali hayana budi kuendelea kwenye maisha mengine baada ya haya, maisha ya akhera, ili avune kulingana na alichokipanda hapa ulimwenguni. Atalazimika mtu kutoa hisabu yake mbele ya Bwana wake ni vipi na ni kiasi gani aliishi kulingana na lengo la maisha yake? Je, aliishi maisha ya kumtii na kumyenyekea Allah(s.w) katika kuendea kila kipengele cha maisha yake au aliishi kwa kumkanusha Allah(s.w) na kumuasi? Kila mtu atalipwa kwa uadilifu kulingana na utendaji wake hapa ulimwenguni. Tunakumbushwa katika Qur'an:

وَيَوْمَ نُسَيِّرُ الْجِبَالَ وَتَرَى الْأَرْضَ بَارِزَةً وَحَشَرْنَاهُمْ فَلَمْ  
تُعَادِرْ مِنْهُمْ أَحَدًا ﴿٤٧﴾ وَعَرِضُوا عَلَىٰ رَبِّكَ صَفًّا لَقَدْ  
جِئْتُمُونَا كَمَا خَلَقْنَاكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ بَلْ زَعَمْتُمْ أَلَّن نَجْعَلَ لَكُم مَّوْعِدًا  
﴿٤٨﴾ وَوَضِعَ الْكِتَابَ فَتَرَى الْمُجْرِمِينَ مَشْفِقِينَ مِمَّا فِيهِ  
وَيَقُولُونَ يَا وَيْلَتَنَا مَا لِهَذَا الْكِتَابِ لَا يُغَادِرُ صَغِيرَةً وَلَا كَبِيرَةً  
إِلَّا أَحْصَاهَا وَوَجَدُوا مَا عَمِلُوا حَاضِرًا ۗ وَلَا يَظْلِمُ رَبُّكَ أَحَدًا ﴿٤٩﴾

*“Nasi siku hiyo tutawafufua (viumbe wote) wala hatutamwacha hata mmoja katika wao. Na watahudhurishwa mbele ya Mola wako safu safu (wataambiwa): Bila shaka mumetujia kama tulivyokuumbeni mara ya kwanza. Bali mlidhani yakuwa hatutakuwekeeni miadi hii. Na madaftari yatawekwa (mbele yao) utaona wabaya wanavyoogopa kwa sababu ya yale yaliyomo (madaftarini), na watasema: “Ole wetu! Namna gani madaftari haya! Hayaachi dogo wala kubwa ila yamelidhibiti”. Na watakuta yote yale waliyoyafanya yamehudhurishwa hapo; na Mola wako hamdhulumu yoyote’ (18:47-49).*

Pia Historia ya mwanaadamu haishii tu katika kutizama matendo ya maisha ya mtu binafsi, bali pia huyaangalia matendo

ya maisha ya jamii ambayo ni mkusanyiko wa matendo ya maisha ya watu binafsi na mahusiano baina yao. Jamii imepewa jukumu la kusimamisha uadilifu katika ardhi kwa kuamrisha mema na kukataza maovu. Hatima ya jamii kama mtu binafsi itategemeana na namna itakavyolitekeleza jukumu hili. Lakini kuna tofauti kubwa kati ya hatima ya mtu binafsi na hatima ya jamii. Ni kuwa hukumu ya jamii hupitishwa hapa hapa duniani. Kwa maana kuwa jamii itakapoacha kutekeleza jukumu lake, watu katika jamii hiyo watateseka kwa kukosekana utulivu na amani ya kweli kwa kila mwanajamii. Hutokea pia jamii inapokithiri katika uasi, Allah(s.w) akaiangamiza kabisa kama iliyokuwa kwa watu wa Nabii Nuhu(a.s) na Lut(a.s). Kinyume chake mtu binafsi anaweza kuwa dhalimu na faasiq (Asi mkubwa) lakini bado akaonekana mwenye kunawiri na kustawi katika maisha haya ya dunia kama walivyo matajiri na wafalme wengi ulimwenguni.

## Kwa Nini ni Muhimu Kujifunza Historia

Kutokana na maelezo yaliyotangulia tunaweza kusema kuwa waislamu tunalazimika kujifunza ili kwa kuzingatia matendo ya watu binafsi na jamii zilizopita tuweze kubakia katika lengo la maisha yetu ya kibinafsi na kijamii na kufuata njia iliyonyooka (njia ya Allah) kwa kuigiza mwenendo wa watu wema waliofaulu katika maisha ya hapa ulimwenguni na kubashiriwa pepo na kujiepusha na mwenendo wa watu waovu waliofeli katika maisha ya hapa ulimwenguni na wengine wakaangamiziwa mbali na katika akhera wameahidiwa adhabu kali ya motoni.

Ni kumbukumbu za Historia pekee zitakazo tuwezesha kuishi kulingana na mazingira ya dua tunayoiomba katika kila rakaa ya swala zetu katika kusoma Suratul-Faatiha:

أَهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ ﴿١﴾ صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ غَيْرِ  
 الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّينَ ﴿٥﴾

*“Tuongoze njia iliyonyooka, Njia ya wale uliowaneemesha; Sio ya wale waliokasirikiwa wala ya wale waliopotea” (1:6-7).*

Walioneemeshwa na Allah(s.w) ni wale watu wema walioishi kulingana na lengo la maisha yao. Watu wema wamebainishwa katika Qur’an:

وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَأُولَئِكَ مَعَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنَ النَّبِيِّينَ  
وَالصَّادِقِينَ وَالشُّهَدَاءِ وَالصَّالِحِينَ وَحَسُنَ أُولَئِكَ رَفِيقًا ﴿١٤﴾

*“Na wenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, basi hao watakuwa pamoja na wale aliowaneemesha Mwenyezi Mungu: Manabii, Masidiq, Mashahidi na Maswalihi (watenda wema). Na uzuri ulioje (kwa mtu) watu hao kuwa rafiki (zake)” (4:69).*

Historia inadhihirisha mwenendo wa hawa waliotajwa katika aya hii. Walioghadhikiwa na Allah(s.w) na waliopotea njia kabisa, pia mwenendo wao umebainishwa wazi katika Historia ya mwanaadamu iliyodhihirishwa katika Qur’an.

Pamoja na muhtasari huu, kujifunza Historia kwa Waislamu ni jambo muhimu kwa sababu:

### **(i) Historia hutuonesha asili na Hadhi yetu juu ya viumbe wengine hapa duniani**

Tumeona kwamba hakuna ushahidi wowote wa historia au sayansi unaohitibisha madai ya makafiri kuwa mwanaadamu katokana na jamii ya masokwe (apes). Historia inaonesha na kutufunza kuwa tangu awali mwanaadamu aliumbwa akiwa mtu kamili aliyekuwa na fahamu na elimu kubwa juu ya mazingira ya maisha ya dunia. Mwenyezi Mungu amemtunuki mwanaadamu elimu na uwezo mkubwa wa kujielimisha ili awe Khalifa hapa duniani. Khalifa ni kiongozi anayeutawala Ulimwengu kwa ajili ya Allah(s.w) kwa kutumia mwongozo Wake (s.w). Asili ya

Mwanaadamu na Hadhi yake inabainishwa vyema katika aya zifuatazo:

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلٰٓئِكَةِ اِنِّىْ خَلَقْتُ بَشَرًا مِّنْ صَلٰٓصَلٍ مِّنْ حَمَآءٍ مَّسْنُوٰنٍ  
 ۙ فَاِذَا سَوَّيْتُهُۥ وَنَفَخْتُ فِيْهِ مِنْ رُّوْحِىْ فَقَعُوْا لَهٗۙ سَٰجِدِيْنَ ﴿۲۹﴾  
 فَسَجَدَ الْمَلٰٓئِكَةُ كُلُّهُمْ اٰجْمَعُوْنَ ﴿۳۰﴾

*Na (kumbuka)Mola wako alipowaambia Malaika, “Hakika Mimi nitamuumba mtu kwa udongo mkavu unaotoa sauti, wenye kutokana na matope meusi yaliyovunda“Basi Nitakapomkamilisha na kumpulizia roho inayotokana na Mimi, basi mumuangukie kwa kumtii”. “Basi Malaika wakatii wote pamoja” (15:28-30).*

وَلَقَدْ خَلَقْنَاكُمْ ثُمَّ صَوَّرْنَاكُمْ ثُمَّ قُلْنَا لِلْمَلٰٓئِكَةِ اسْجُدُوْا لِاٰدَمَ فَسَجَدُوْٓا  
 اِلَّاۤ اِبْلِیْسَ لَمْ یَّكُنْ مِنَ السَّٰجِدِيْنَ ﴿۱۱﴾

*Na hakika Tulikuumbeni, kisha Tukakutieni sura, kisha Tukawaambia Malaika: “Msujudieni Adam”. Basi Iblisi hakuwa miongoni mwa waliosujudu. (7:11).*

﴿۷﴾ وَمِنَ الطَّیِّبٰتِ وَفَضَّلْنٰهُمۡ عَلٰی كَثِیْرٍ مِّمَّنْ خَلَقْنَا تَفْضِیْلًا

*“Na bila shaka tumemtukuza mwanaadamu, na tumempa vipande vya barani na baharini, na tumewaruzuku vitu vizuri vizuri na tumewatukuza kuliko wengi katika wale tuliowaumba kwa utukufu ulio mkubwa” (17:70).*

**(ii) Hutukumbusha lengo la kuumbwa kwetu na namna ya kulifikia**

Historia pia hutukumbusha lengo la kuumbwa kwetu na namna ya kulifikia lengo hilo. Tunafahamishwa katika Qur’an kuwa

kabla hatujayaanza maisha ya duniani, Mwenyezi Mungu kwa uweza wake alituwezesha kumtambua na kisha tukachukua ahadi kuwa hatutamwabudu kiumbe yeyote wala kufuata mwongozo wa asiyekuwa Mwenyezi Mungu katika kuendesha maisha yetu yote hapa duniani. Tukio hilo limeelezwa katika aya ifuatayo:

وَإِذْ أَخَذَ رَبُّكَ مِنْ بَنِي آدَمَ مِنْ ظُهُورِهِمْ ذُرِّيَّتَهُمْ وَأَشْهَدَهُمْ  
عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ أَلَسْتُ بِرَبِّكُمْ قَالُوا بَلَىٰ شَهِدْنَا أَنْ تَقُولُوا يَوْمَ الْقِيَامَةِ  
إِنَّا كُنَّا عَنْ هَذَا غَافِلِينَ ﴿١٧٢﴾ أَوْ تَقُولُوا إِنَّمَا أَشْرَكَ آبَاؤُنَا مِنْ قَبْلُ  
وَكُنَّا ذُرِّيَّةً مِنْ بَعْدِهِمْ أَفَتُهْلِكُنَا بِمَا فَعَلَ الْمُبْطِلُونَ ﴿١٧٣﴾

*Na Mola wako alipowaleta wanaadamu kutoka miongoni mwa kizazi chao, na akawashuhudisha juu ya nafsi zao; (akawaambia) “Je mimi si Mola wenu?” wakasema: “Ndiyo tunashuhudia”. Allah akasema: “Msije mkasema Siku ya kiyama kuwa sisi tulikuwa tumeghafilika na hayo (hatujui). Au mkasema, “Baba zetu ndio walioshirikisha zamani, nasi tulikuwa kizazi nyuma yao, basi utatuangamiza kwa sababu ya yale waliyoyafanya waovu?” (7:172-173).*

Baada ya Mwanaadamu kumtambua Mola wake, anawajibika kumuabudu Yeye pekee katika kukiendea kila kipengele cha maisha yake. Kufanya hivyo ndio hasa lengo la kuumbwa kwake:

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥١﴾

*“Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu” (51:56).*

Ili mwanaadamu aweze kumuabudu Mola wake katika kila kipengele cha maisha yake hanabudi kufauti mwongozo kutoka kwa Mola wake ulioahidiwa tangu mwanzo wa kuanza maisha yake hapa duniani:

فَلَمَّا أَهْبَطُوا مِنْهَا جَمِيعًا فَأَمَّا يَأْتِيَنَّكُمْ مَيِّسٌ هُدًى فَمَنْ تَبِعَ هُدَايَ فَلَا  
 خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٣٨﴾ وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا  
 أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٣٩﴾

*Tukasema shukeni humo nyote, na kama ukikufikieni uongozi utokao kwangu, basi watakaofuata uongozi wangu huo haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika. Lakini wenye kukufuru na kuyakadhibisha maneno Yetu, hao ndio watakaokuwa watu wa Motoni, humo watakaa milele” (2:38-39).*

### (iii) Hutuonesha namna Mwenyezi Mungu alivyotuneemesha ili tuweze kumwabudu ipasavyo

Kila umma au kaumu katika historia ya mwanaadamu iliruzukiwa neema mbalimbali katika rasilimali, elimu na teknolojia zilizolenga kuwawezesha kufikia lengo la maisha yao kwa urahisi. Katika hili historia inatuonesha ukweli usiopingika kuwa Mwenyezi Mungu ametuneemesha zaidi sisi kuliko kaumu zilizotangulia. Maendeleo ya sayansi na teknolojia tuliyonayo sasa yameifanya dunia kuwa kama kijiji kwa kumuwezesha mwanaadamu kufika au kuwasiliana na watu wa pande zote za dunia kwa muda mfupi. Kwahiyo inakuwa rahisi katika zama hizi kuitikia wito wa Mwenyezi Mungu pale alipotuamrisha kuwa:

قُلْ سِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَانظُرُوا كَيْفَ بَدَأَ الْخَلْقَ ثُمَّ اللَّهُ يُنشِئُ النَّشْأَةَ  
 الْأَخْرَةَ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٠﴾

*Sema: “Tembeeni katika ardhi ili muone namna Mwenyezi Mungu alivyoanzisha maumbile; Kisha atavirudisha kwa mara ya pili. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu” (29:20).*

Hivyo tusipojielimisha na kuuchunguza ulimwengu ili kumjua vema Mwenyezi Mungu na kumuabudu ipasavyo ni kukanusha

neema tulizopewa na Mwenyezi Mungu atatuuliza juu ya neema hizi kama Qur'an inavyosisitiza:

ثُمَّ لَسْأَلَنَّ يَوْمَئِذٍ عَنِ النَّعِيمِ ﴿٨﴾

*“Kisha kwa hakika siku hiyo mtaulizwa juu ya neema (mlizopewa mmezitumiaje)” (102:8).*

#### **(iv)Hutuonesha madhara ya kutofuata mwongozo wa Mwenyezi Mungu**

Historia pia hutuonesha madhara yanazozikumba jamii za wanaadamu zilizokataa kufuata mwongozo wa Mwenyezi Mungu na badala yake zikaishi kwa kufuata sheria na kanuni zilizobuniwa na wanaadamu kwa kufuata matashi ya nafsi. Jamii hizo ziligubikwa na giza nene la dhulma, ukandamizaji, ukatili, ubabe, ufuska, alimuradi kila mtu aliishi kwa wasiwasi pasina amani wala furaha ya kweli. Mfano wa jamii hizi ni ule wa Thamud, Ad, kaumu Lut na watu wa Nabii Shu'aib ambao historia yao tutaiona baadaye katika historia ya Mitume wa Allah(s.w).

#### **(v)Hutuonesha namna Mitume na watu wema walivyosimama imara katika kupambana na dhulma na watawala madhalimu**

Historia pia hutuonesha namna Mitume na watu wema walivyosimama imara katika kupambana na dhulma na watawala madhalimu. Kwa maneno mengine historia inatuonesha na kutufunza umuhimu wa kusimamisha haki na uadilifu katika jamii na kuondoa aina zote za dhulma na ukandamizaji. Allah(s.w) anasisitiza juu ya umuhimu huu katika aya ifuatayo:

وَمَا لَكُمْ لَا تُقِنْتُلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَالْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ الرِّجَالِ وَالنِّسَاءِ

وَالْوَالِدِينَ الَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا أَخْرِجْنَا مِنْ هَذِهِ الْقَرْيَةِ الظَّالِمِ أَهْلُهَا

وَأَجْعَلْ لَنَا مِنْ لَدُنْكَ وَلِيًّا وَاجْعَلْ لَنَا مِنْ لَدُنْكَ نَصِيرًا ﴿٧٥﴾



*“Na mna nini hampigani katika njia ya Mwenyezi Mungu na kuwakomboa watu madhaifu katika wanaume na wanawake na watoto, ambao wanasema kumwambia Mola wao: Mola wetu! Tutoe katika mji huu ambao watu wake ni madhalimu. Na utupe ulinzi kutoka kwako na utupe ushindi kutoka kwako” (4:75).*

**(vi) Hutupatia fursa ya kujifunza toka kwa kaumu zilizopita na kuchukua tahadhari kabla hayajatufika yaliyowasibu**

Historia pia hutupatia fursa ya kujifunza masahibu yaliyowakuta kaumu zilizopita kutokana na makosa waliyofanya. Tunasoma makosa yao, madhara waliyoyapata na maangamizi yaliyowakumba. Kwa mfano, Kaumu ya Lut iliagamizwa kwa sababu ya kufanya kwao ubaradhuli wa kutamaniana na kuendeanana wanaume kwa wanaume. Hakika watu hawa walifanya uchafu na uovu mkubwa kabisa wenye kuchukiza mbele ya Allah(s.w) na mbele ya watu wema. Mwishowe wakaangamizwa!

فَتَجِيْتُهُ وَأَهْلُهُ أَجْمَعِينَ ﴿١٧٦﴾ إِلَّا عَجُوزًا فِي الْغَدِيرِ ﴿١٧٦﴾ ثُمَّ دَمَرْنَا  
 الْآخِرِينَ ﴿١٧٧﴾ وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهِمْ مَطَرًا فَسَاءَ مَطَرُ الْمُنْذَرِينَ ﴿١٧٧﴾ إِنَّ فِي  
 ذَلِكَ لَآيَةً وَمَا كَانَ أَكْثَرُهُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١٧٨﴾

*“Basi tukamuokoa yeye (Lut) na watu wake wote. Isipokuwa kikongwe aliye khiari kuwa katika wakaao nyuma. Kisha tukawaangamiza wale wengine (aliokwenda mke wa Nabii Luti kuchanganyika nao). Na Tukawanyeshenzea (Tukawamininia) mvua (ya mawe), basi ni mbaya mno (kabisa) mvua ya (hao) walioonywa (wasionyeye). Bila shaka katika haya kuna mazingatio, lakini wengi katika wao hawakuwa wenye kuamini” (26:170-174).*

Kwa kuzingatia hayo tunachukua tahadhari ya kutoyaendea makosa yaliyopelekea maangamizi yao, na kufanya jitihada ili pasiwepo na mtu au kikundi cha watu katika jamii watakaoachiwa kufanya ovu lolote la kuihilikisha jamii nzima.

**(vii) Kujitathmini na kuongeza jitihada za kusimamisha haki na uadilifu kama walivyofanya Mitume na watu wema waliotangulia**

Historia pia hutupatia fursa ya kuona jitihada zilizofanywa na Mitume na watu wema waliotangulia katika kusimamisha haki na uadilifu kwenye jamii zao. Kwa kuzilinganisha jitihada zao na zetu na mafanikio waliyoyapata, tunaweza kuona ni kwa kiwango gani tunazembea kwa kudharau au kubweteka kwa kuridhika na ile sehemu ndogo ya ibada tunazofanya kama vile kuswali, kufunga na kuhiji, hali ya kuwa Mtume(s.a.w) na Waislamu waliokuwa pamoja naye waliyafanya yote hayo na kuweza kuiongoza jamii ya wanaadamu kwa sheria za Mwenyezi Mungu zilizoleta maisha ya furaha na amani ya kweli kwa walimwengu. Ni kutokana na jitihada kubwa walizofanya ndipo Allah(s.w) akawakamilishia ahadi yake anayoitaja katika aya ifuatayo:

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي  
الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي  
أَرْتَضَى لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي  
شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٥٥﴾

*“Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, kuwa Atawafanya Makhaliifa katika ardhi kama alivyowafanya Makhaliifa wale waliokuwa kabla yao, na kwa hakika atawasimamishia Dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu, hawanishirikishi na chochote. Na watakao kufuru baada ya hayo, basi hao ndio mafasiqi (24:55).*

**(viii) Hutuonesha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu na mamlaka yake juu ya mwandaadamu.**

Jambo lingine kubwa ni kwamba, historia hudhihirisha kuwepo Mwenyezi Mungu na mamlaka yake juu ya wanaadamu. Jamii mbalimbali zilizokuwa na nguvu kubwa kuliko zingine zilifutwa na

kusahaulika kabisa na nguvu kubwa iliyokuwa juu ya uwezo wao. Kwa mfano, tunakumbushwa historia ya kaumu ya Ad, Thamud na Firaun ambao walikuwa na nguvu kubwa kijeshi na maendeleo makubwa ya teknolojia, lakini walifutwa na sehemu na nafasi zao za uongozi wakarithishwa waumini waliokuwa wanyonge kiuchumi na kijeshi.

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِعَادٍ ﴿٦﴾ إِرَمَ ذَاتِ الْعِمَادِ ﴿٧﴾ الَّتِي لَمْ يُخْلَقْ  
 مِثْلُهَا فِي الْبِلَادِ ﴿٨﴾ وَثَمُودَ الَّذِينَ جَابُوا الصَّخْرَ بِالْوَادِ ﴿٩﴾ وَفِرْعَوْنَ  
 ذِي الْأَوْتَادِ ﴿١٠﴾ الَّذِينَ طَعَوْا فِي الْبِلَادِ ﴿١١﴾ فَأَكْثَرُوا فِيهَا الْفُسَادَ ﴿١٢﴾  
 فَصَبَّ عَلَيْهِمْ رَبُّكَ سَوْطَ عَذَابٍ ﴿١٣﴾

“Je! Huoni Mola wako alivyowafanya Ad? Iram waliokuwa na majumba marefu marefu; ambao hawakuumbwa mfano wao katika miji. Na Thamud waliochonga majabali wakafanya nyumba katika uwanja wao; Na Firaun mwenye majumba kama vigingi, ambao walifanya maovu katika miji, kisha walizidisha humo maovu, kwahiyo Mola wako aliwapiga mjeledi mmoja tu wa adhabu” (89:6-13).

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِأَصْحَابِ الْفِيلِ ﴿١﴾ أَلَمْ يَجْعَلْ كَيْدَهُمْ فِي  
 تَضْلِيلٍ ﴿٢﴾ وَأَرْسَلَ عَلَيْهِمْ طَيْرًا أَبَابِيلَ ﴿٣﴾ تَرْمِيهِمْ بِحِجَارَةٍ مِّنْ  
 سِجِّيلٍ ﴿٤﴾ فَجَعَلَهُمْ كَعَصْفٍ مَّا كُولٍ ﴿٥﴾

“Je! Huoni jinsi Mola wako Alivyowafanya watu wenye ndovu? Je! Hakujaalia vitimbi vyao kuharibika. Na akawapelekea ndege maundi kwa makundi. Wakawapiga kwa mawe ya udongo wa kuchoma. Akawafanya kama majani yaliyoliwa (yakatapikwa)?” (105:1-5).

## **Zoezi la 1**

1. Tofautisha lengo la maisha la waumini na lile la Makafiri.
2. Dhana ya Makafiri juu ya Historia na tofauti na ile ya waislamu kutokana na kutofautiana kwao katika maeneo yafuatayo:  
(a) \_\_\_\_\_ (b) \_\_\_\_\_ (c) \_\_\_\_\_ (d) \_\_\_\_\_
3. (a) Kwa mtazamo wa makafiri Historia ni \_\_\_\_\_  
(b) Kwa mtazao wa waislamu Historia ni \_\_\_\_\_
4. Tofautisha mtizamo wa waislamu na ule wa makafiri juu ya
  - (a) Chanzo au asili ya mwanaadamu na viumbe vyote vilivyomzunguka
  - (b) Lengo la maisha ya mwanaadamu ni viumbe vyote vilivyomzunguka.
  - (c) Hadhi ya mwanaadamu hapa ulimwenguni
  - (d) Hatima ya maisha ya mwanaadamu na viumbe vyote vilivyomzunguka.
5. Kwa nini ni muhimu kwa muislamu kujifunza Historia? Toa sababu tano za msingi.



## *Sura ya Pili*

# HISTORIA YA UISLAMU KABLA YA MUHAMMAD(S.A.W)

### Utangulizi

Katika Sura hii imeelezwa kwa muhtasari historia ya mitume waliotajwa katika Qur'an waliomtangulia Mtume Muhammad(s.a.w). Mitume waliotajwa katika Qur'an kabla ya Mtume(s.a.w) ni hawa wafuatao:

- |                   |                      |
|-------------------|----------------------|
| (1) Adam(a.s)     | (13)Shu'ayb(a.s)     |
| (2) Idris(a.s)    | (14) Musa(a.s)       |
| (3) Nuhu(a.s)     | (15) Harun(a.s)      |
| (4) Hud(a.s)      | (16) Al-yasaa(a.s)   |
| (5) Salih(a.s)    | (17) Dhul-Kifil(a.s) |
| (6) Ibrahim(a.s)  | (18) Daud(a.s)       |
| (7) Lut(a.s)      | (19) Sulaiman(a.s)   |
| (8) Ismail(a.s)   | (20)Ilyasa(a.s)      |
| (9) Is-haq(a.s)   | (21) Yunus(a.s)      |
| (10)Ya'aquub(a.s) | (22) Zakaria(a.s)    |
| (11) Yusufu(a.s)  | (23) Yahya(a.s)      |
| (12) Ayyuub(a.s)  | (24) Isa(a.s)        |

Lengo la kupitia historia ya mitume hawa ni kuwaandaa wasomaji na kuwapa ari na hamasa itakayo wawezesha kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii kama walivyofanya mitume hao na wafuasi wao. Kuna mafundisho mengi msomaji anayoyapata kutokana na historia ya kila Mtume.

Katika sura hii pia imeelezwa historia ya watu wema na watu waovu waliotajwa katika Qur'an na mafunzo yatokanayo na makundi haya mawili.

Watu wema waliotajwa katika Qur-an ni

- (1) Vijana wa pangoni
- (2) Dhulqarinain
- (3) Al-Khidhri
- (4) Luqman

Watu waovu waliotajwa katika Qur-an ni

- (1) Watu waliovunja amri ya Jumamosi
- (2) Karun na Hamana
- (3) Watengenezaji mahandaki ya Moto
- (4) Watu wa mji waliomuua muislamu kwa kusadikisha Mitume wa Allah(s.w)

Baada ya utangulizi huu, tutaanza kupitia historia ya Mtume baada ya Mtume na mafunzo yatokanayo na kisha tutamalizia kwa kupitia historia ya **makundi ya watu wema** na **watu waovu** na mafunzo yatokanayo.

Ikumbukwe kuwa lengo kuu la kupitia historia hii ni kupata mafunzo yatakayotuwezesha kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii.

## **ADAM(A.S)**

### **Kuumbwa kwa Adam(a.s)**

Adam(a.s) ni mtu na Mtume wa Allah(s.w) wa kwanza. Adam(a.s) ameumbwa kwa udongo uliofinyangwa ukafanywa kuwa sanamu la mtu kisha likapuliziwa roho na kuwa mtu kamili kama tunavyofahamishwa katika Qur-an:

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَائِكَةِ إِنِّي خَالِقٌ بَشَرًا مِّنْ صَلْصَلٍ مِّنْ حَمَإٍ مَّسْنُونٍ

﴿٢٨﴾ فَإِذَا سَوَّيْتُهُۥ وَنَفَخْتُ فِيهِ مِن رُّوحِي فَقَعُوا لَهُۥ سَاجِدِينَ ﴿٢٩﴾

*Na (kumbuka) Mola wako alipowaambia Malaika, “Hakika Mimi nitamuumba mtu kwa udongo mkavu unaotoa sauti, wenye kutokana na matope meusi yaliyovunda.” “Basi nitakapomkamilisha na kumpulizia roho inayotokana na Mimi, basi mumuangukie kwa kumtii.” (15:28-29)*

﴿٧١﴾ إِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَائِكَةِ إِنِّي خَالِقٌ بَشَرًا مِّن طِينٍ

﴿٧٢﴾ فَإِذَا سَوَّيْتُهُۥ وَنَفَخْتُ فِيهِ مِن رُّوحِي فَقَعُوا لَهُۥ سَاجِدِينَ ﴿٧٣﴾

*(Kumbuka) Mola wako alipowaambia Malaika: Hakika mimi nitaumbwa mtu kwa udongo. Na nitakapomkamilisha na kumpulizia roho inayotokana na mimi basi msujudieni (kama ishara ya kumheshimu). (38:71-72).*

## Hadhi ya Adam(a.s) na Kizazi Chake

Kabla ya Adam(a.s) kuumbwa, Allah(s.w) aliwafahamisha Malaika kuwa atamleta Khalifa (kiongozi) katika ardhi atakayesimamisha Ufalme wa Allah(s.w) (Dola ya kiislamu) kwa kufuata mwongozo wake Allah(s.w). Mazungumzo baina ya Allah(s.w) na Malaika wake juu ya ukhalifa wa Adam(a.s) na kizazi chake tunayapata katika aya zifuatazo:

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَائِكَةِ إِنِّي جَاعِلٌ فِي الْأَرْضِ خَلِيفَةً

﴿٣٠﴾ قَالُوا أَتَجْعَلُ فِيهَا مَن يُفْسِدُ فِيهَا وَيَسْفِكُ الدِّمَاءَ وَنَحْنُ نُسَبِّحُ

﴿٣١﴾ بِحَمْدِكَ وَنُقَدِّسُ لَكَ قَالَ إِنِّي أَعْلَمُ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٣٢﴾

*(Wakumbushe watu khabari hii): Wakati Mola wako alipowambia Malaika: “Mimi nitaleta Khalifa katika ardhi.”*

*Wakasema (Malaika): “Utaweka humo watakaofanya uharibifu humo na kumwaga damu, hali sisi tunakutukiza kwa sifa zako na kukutaja kwa utakatifu wako?” Akasema (Mwenyezi Mungu): “Hakika Mimi nayajua msiyoyajua.”(2:30)*

وَعَلَّمَ آدَمَ الْأَسْمَاءَ كُلَّهَا ثُمَّ عَرَضَهُمْ عَلَى الْمَلَائِكَةِ فَقَالَ أَأَدَّبْتُمُونِي بِأَسْمَاءِ  
هَٰؤُلَاءِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٣٠﴾

*Na (Mwenyezi Mungu) akamfundisha Adam majina ya vitu vyote, kisha akaviweka mbele ya Malaika, na akasema (kuwaambia Malaika): “Niambieni majina ya vitu hivi ikiwa mnasema kweli (kuwa nyinyi ndio wajuzi wa mambo).”(2:31)*

قَالُوا سُبْحٰنَكَ لَا عِلْمَ لَنَا إِلَّا مَا عَلَّمْتَنَا إِنَّكَ أَنْتَ الْعَلِيمُ الْحَكِيمُ ﴿٣١﴾

*Wakasema (Malaika): “Utakatifu ni wako! Hatuna ilimu isipokuwa ile uliyotufundisha; bila shaka wewe ndiye Mjuzi na ndiye Mwenye hikima.” (2:32).*

قَالَ يَا آدَمُ أَنْبِئْهُمْ بِأَسْمَائِهِمْ فَلَمَّآ أَنْبَأَهُمْ بِأَسْمَائِهِمْ قَالَ  
أَلَمْ أَقُلْ لَكُمْ إِنِّي أَعْلَمُ غَيْبَ السَّمٰوٰتِ  
وَالْأَرْضِ وَأَعْلَمُ مَا تُبْدُونَ وَمَا كُنْتُمْ تَكْتُمُونَ ﴿٣٢﴾

*Akasema (Mwenyezi Mungu): “Ewe Adam! Waambie majina yake.” Alipowaambia majina yake alisema (Mwenyezi Mungu) “Sikukwambieni kwamba mimi najua siri za mbinguni na za ardhi; tena najua mnayoyadhihirisha na mliyokuwa mnayaficha?”.(2:33)*

وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ أَبَىٰ وَاسْتَكْبَرَ وَكَانَ  
مِنَ الْكَافِرِينَ ﴿٣٣﴾



*Na (wakumbushe watu khabari hii): Tulipowaambia Malaika “Msujudieni Adam”. Wakamsujudia wote isipokuwa Iblis; akakataa na akajivuna; na (tokea hapo) alikuwa katika makafiri(2:34)*

Kutokana na aya hizi tunajifunza yafuatayo:

**Kwanza**, Adam(a.s) na kizazi chake(wanaadamu) wamekusudiwa kuwa **Makhalifa** wa Allah (s.w) katika ardhi, yaani kuwa wasimamishaji wa Ufalme wa Allah(s.w) katika ardhi (Dola ya Kiislamu) kwa niaba yake pamoja na kuwa yeye mwenyewe ni Muweza wa kuusimamisha kwa kusema: “**kuwa**” na “**ukawa**”.

**Pili**, ili kuweza kusimamisha **ukhalifa** katika ardhi watu hawanabudi kuwa na ujuzi wa kutosha juu ya mazingira ya ardhi na namna ya kukabiliana nayo. Nabii Adam(a.s) kufundishwa “**majina ya vitu vyote**” ni kielelezo kuwa alifunzwa fani zote za elimu zinazohitajika katika kuendea kila kipengele cha maisha ya binafsi na ya jamii ya mwanaadamu hapa ardhini. Pamoja na elimu ya vitu mbali mbali (elimu ya mazingira), Adam(a.s) na kizazi chake waliahidiwa kuletewa mwongozo kutoka kwa Allah(s.w) utakaowawezesha kusimamisha ukhalifa na kuvuna matunda yake ambayo ni kuishi kwa furaha na amani na kupata radhi za Allah(s.w) hapa duniani na huko akhera kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

فَلَنَّا أَهْبَطُوا مِنْهَا جَمِيعًا ۖ فَمَا يَأْتِيَنَّكُمْ مِنِّي هُدًى فَمَنْ تَبِعَ هُدَايَ فَلَا

خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٢٨﴾

*“Tukasema: Shukeni humo nyote (kutoka peponi) na kama ukikufikieni uwongozi utokao kwangu, wale watakaoufuata uwongozi wangu huo, haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika.(2:38)*

وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ

فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٣٩﴾

*Lakini wenye kukufuru na kuyakadhibisha maneno yetu, hao ndio watakaokuwa watu wa motoni, humo watakaa milele”. (2:39)*

**Tatu**, kusimamisha **ukhalifa** katika ardhi au kusimamisha Uislamu katika jamii ni jambo linalompandisha mwanaadamu hadhi na daraja mbele ya Allah(s.w) kuliko ile hadhi na daraja ya Malaika mbele ya Allah(s.w). Hili linadhihirika pale Malaika walipoamrisha kumsujudia Adam(a.s). Sijda ni kitendo cha heshima ya hali ya juu kinachomstahiki Allah(s.w) peke yake, lakini kama ishara ya kuonesha hadhi ya Khalifa (Naibu) wa Allah(s.w), hapa ardhini, Allah(s.w) aliwaamrisha Malaika wamsujudie Adam na wakatii. Ubora wa kusimamisha Ukhaliifa (Uislamu) katika jamii pia unadhihirishwa katika aya zifuatazo:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا هَلْ أَذُكُّكُمْ عَلَىٰ تَجَرَّةٍ تَنْجِيكُمْ

مِّنْ عَذَابِ أَلِيمٍ ﴿٦١﴾

*“Enyi mliaoamini! Je! Nikujulisheni biashara itakayokuo keni na adhabu iumizayo?(61:10)*

تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ۖ وَتُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنفُسِكُمْ

ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿١١﴾

*(Biashara yenyewe ni hii);- Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake na piganieni Dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zenu na nafsi zenu, **haya ni bora** kwenu ikiwa mnajua”. (61:-11)*

## **Kibri cha Iblis na Uadui Wake Dhidi ya Binadamu**

Iblis ni katika jamii ya majini aliyekuwa pamoja na Malaika wakati amri ya kumsujudia Adam inatolewa. Iblis alitarajiwa kutii

amri hiyo ya Mola wake pamoja na Malaika, lakini hakufanya hivyo bali alitakabari kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

فَسَجَدَ الْمَلَائِكَةَ كُلَّهُمْ أَجْمَعُونَ ﴿٧٣﴾ إِلَّا إِبْلِيسَ أَسْتَكْبَرَ وَكَانَ مِنَ  
 الْكَافِرِينَ ﴿٧٤﴾ قَالَ يَتَّبِعُ لَيْسَ مَا مَتَّعَكَ أَنْ تَسْجُدَ لِمَا خَلَقْتُ بِيَدَيَّ  
 أَسْتَكْبَرْتَ أَمْ كُنْتَ مِنَ الْعَالِينَ ﴿٧٥﴾

“Basi Malaika wakatii (amri ya kusujudu) wote pamoja isipokuwa Iblis, akajivuna na akawa katika makafiri.” (Allah) akamuuliza: “Ewe Iblis! Kipi kilichokuzuia kumtii yule niliyemuumba kwa mikono yangu?” Je! Umetakabari au umo miongoni mwa wakubwa (kweli)? (38:73-75)

قَالَ أَنَا خَيْرٌ مِنْهُ خَلَقْتَنِي مِنْ نَّارٍ وَخَلَقْتَهُ مِنْ طِينٍ ﴿٧٦﴾ قَالَ  
 فَأَخْرَجَ مِنْهَا فَايَّكَ رَجِيمٌ ﴿٧٧﴾

Akasema (Iblis katika kujibu): “Mimi ni bora kuliko yeye, kwani mimi umeniumba kwa moto na yeye umemuumba kwa udongo” (38:76)

Iblis badala ya kuzingatia amri ya Mola wake na kutii, amepeleka fikra zake kwenye asili ya umbile la Adam(a.s) na kuanza kujifananisha naye na kuona kuwa asili ya umbile lake ni bora kuliko ile asili ya umbile la Adam(a.s). Hatakama ingelikuwa kweli kuwa moto ni bora kuliko udongo, Iblis asingelipaswa kukataa kumsujudia Adam(a.s) kwa sababu si Adamu aliyetaka asujudiwe, bali aliyetoa amri ya kumsujudia Adam ni Allah(s.w) ambaye ni Muumba wa Adam na Iblis.

Baada ya Iblis kuvunja amri ya Mola wake kwa takaburi kiasi hicho, alilaaniwa na kubaidishwa (kufukuzwa) na rehema za Mola wake:

قَالَ فَأَخْرُجْ مِنْهَا فَإِنَّكَ رَجِيمٌ ﴿٧٧﴾ وَإِنَّ عَلَيْكَ لعُنْتِي إِلَى يَوْمِ الدِّينِ ﴿٧٨﴾

(Mwenyezi Mungu) akasema: Basi toka humo kwani umetengwa na rehema. Na hakika laana yangu itakuwa juu yako mpaka siku ya malipo.”(38:77-78)

Badala ya Ibilis kukiri kosa lake na kumuelekea Mola wake kwa toba ya kweli, alielekeza lawama zake kwa Adam(a.s) na kuapa mbele ya Allah (s.w) kuwa atalipiza kisasi kwa Adam(a.s) na kizazi chake kwa kukipoteza na njia ya Allah(s.w):

قَالَ فَبِعِزَّتِكَ لأَعُوْبَتَهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٨٢﴾

“Akasema (Ibilis) Naapa kwa haki ya utukufu wako, bila shaka nitawapoteza wote (hao watoto wa huyu adui yangu – Adam)” (38:82)

قَالَ فَيَمَّا أَعُوْبَتِنِي لأَقْعُدَنَّ لَهُمْ صِرَاطَكَ الْمُسْتَقِيمَ ﴿١١﴾ ثُمَّ لَأَنزِلَنَّهُمْ مِن بَيْنِ أَيْدِيهِمْ وَمِنْ خَلْفِهِمْ وَعَنْ أَيْمَنِهِمْ وَعَنْ شَمَائِلِهِمْ<sup>ط</sup> وَلَا تَجِدُ أَكْثَرَهُمْ

شَاكِرِينَ ﴿١٧﴾

“Akasema: “Kwa kuwa umenihukumia upotofu (upotevu) basi nitawakalia (waja wako). Katika njia yako iliyonyooka (ili niwapoteze) kisha nitawafikia kwa mbele yao na nyuma yao na kuumeni kwao na kushotoni kwao, wengi katika wao hutawakuta ni wenye kushukuru.(7:16-17)

قَالَ أَخْرُجْ مِنْهَا مَذْمُومًا مَّدْحُورًا<sup>ط</sup> لَمَنْ تَبِعَكَ مِنْهُمْ لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنْكُمْ

أَجْمَعِينَ ﴿١٨﴾

Akasema (Mwenyezi Mungu). Toka humo, hali ya kuwa ni mwenye kudharauliwa na mwenye kufukuzwa. Atakayekufuata miongoni mwao (nitamtia motoni) niijaze Jahannamu kwa nyinyi nyote.”(7:18).

Iblis mwenyewe alikiri kuwa hataweza kuwapoteza wale waja wema waliomshika sawa sawa Mola wao kama tunavyojifunza katika Qur'an:

قَالَ رَبِّ بِمَا أَغْوَيْتَنِي لَأُزَيِّنَنَّ لَهُمْ فِي الْأَرْضِ  
 وَلَا أُغْوِيَنَّهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٣٩﴾ إِلَّا عِبَادَكَ مِنْهُمُ الْمُخْلَصِينَ ﴿٤٠﴾ قَالَ هَذَا  
 صِرَاطٌ عَلَيَّ مُسْتَقِيمٌ ﴿٤١﴾ إِنَّ عِبَادِي لَيْسَ لَكَ عَلَيْهِمْ سُلْطَانٌ إِلَّا  
 مَنِ اتَّبَعَكَ مِنَ الْغَاوِينَ ﴿٤٢﴾

*“Akasema Mola wangu! kwa sababu umenihukumu kupotea, basi nitawapambia(upotofu) katika ardhi na nitawapoteza wote. Isipokuwa wale waja wako waliosafika kweli kweli. Mwenyezi Mungu akasema: Hii njia yao ya kuja kwangu imenyooka wanaweza kunijia wakati watakao. Hakika waja wangu wewe hutakuwa na mamlaka juu yao isipokuwa wale wenyue kukufuata kwa khiari zao katika hao wapotofu.(15:39-42).*

### **Adam(a.s) na Mkewe Katika Pepo**

Adam(a.s) aliumbiwa mkewe kutokana na asili ile ile kama tunavyojifunza katika Qur-an:

يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ  
 وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيرًا وَنِسَاءً.....

*Enyi watu! Mcheni Mola wenu ambaye amekuumbeni katika nafsi (asili) moja. Na akamuumba mkewe katika nafsi ile ile. Na akaeneza wanaume wengi na wanawake kutoka wawili hao.....” (4:1).*

Adam(a.s) na mkewe waliwekwa katika Bustani (Pepo) na wakapewa uhuru wa kufurahia wapendavyo ndani ya bustani hiyo na kula matunda yote wapendavyo lakini

wasikurubie matunda ya mti moja tu waliobainishiwa. Iblis (shetani), alimlaghai Adam(a.s) na mkewe wakala matunda ya mti ule waliokatazwa.

وَيَتَّعَادِمُ أَسْكُنُ أَنْتَ وَزَوْجُكَ الْجَنَّةَ فَكُلَا مِنْ حَيْثُ شِئْتُمَا وَلَا تَقْرَبَا

هَذِهِ الشَّجَرَةَ فَتَكُونَا مِنَ الظَّالِمِينَ ﴿١٩﴾

(kisha Allah akasema): “Na wewe Adamu! Kaa Peponi pamoja na mkeo, na kuleni mnapopenda, lakini msiukaribie mti huu msije kuwa miongoni mwa waliodhulumu (nafsi zao).” (7:19)

فَوَسَّوَسَ لَهُمَا الشَّيْطَانُ لِيُبْدِيَ لَهُمَا مَا وُورِيَ عَنْهُمَا مِنْ سَوْءَاتِهِمَا

وَقَالَ مَا نَهَاكُمَا رَبُّكُمَا عَنِ هَذِهِ الشَّجَرَةِ إِلَّا أَنْ تَكُونَا مَلَائِكَةً

أَوْ تَكُونَا مِنَ الْخَالِدِينَ ﴿٢٠﴾

Basi Shetani; (naye ni yule Iblisi), aliwatia wasiwasi ili kuwadhihirishia aibu zao walizofichiwa, na akasema: “Mola wenu hakukukatazeni mti huu ila (kwa sababu hii) msije kuwa Malaika au kuwa miongoni mwa wakao milele (wasife). (7:20)

وَقَالَتْ لَأَبْلُغَنَّ مِنَ الشَّقْوَةِ أَهْدَىٰ لَكُمْ مَنِ الْنَّاصِحِينَ ﴿٢١﴾ فَذَلَّلَهُمَا بِغُرُورٍ

فَلَمَّا ذَاقَا الشَّجَرَةَ بَدَتْ لَهُمَا سَوْءَاتُهُمَا وَطَفِقَا يَخْصِفَانِ عَلَيْهِمَا مِنْ

وَرَقٍ الْجَنَّةِ وَنَادَاهُمَا رَبُّهُمَا أَلَمْ أَنْهَكُمَا عَنْ تِلْكَ الشَّجَرَةِ وَأَقُلُّ لَكُمْ

إِنَّ الشَّيْطَانَ لَكُمْ عَدُوٌّ مُبِينٌ ﴿٢٢﴾

Naye akawaapia (kuwaambia): “kwa yakini mimi ni mmoja wa watowao shauri njema kwenu.” Basi akawateka (wote wawili) kwa khadaa (yake). Na walipouonja mti ule, aibu zao ziliwadhihirikia na wakaingia kujibandika majani ya (miti ya huko) Peponi. Na Mola wao akawaita (akawaambia) “Je, sikukukatazeni mti huu na kukwambieni ya kwamba Shetani ni adui yenu aliye dhahiri?” (7:21-22)

Tofauti na Iblis ambaye baada ya kumuasi Mola wake hakujuta

hata baada ya kukumbushwa, Adam(a.s) na mkewe walijuta sana kwa kumuasi Mola wao kisha wakalalama kwake kuleta toba:

قَالَ رَبَّنَا ظَلَمْنَا أَنفُسَنَا وَإِن لَّمْ تَغْفِرْ لَنَا وَتَرْحَمْنَا لَنَكُونَنَّ مِنَ

الْحٰسِرِينَ ﴿٢٣﴾

*“Mola wetu! Tumedhulumu nafsi zetu; na kama hutatusamehe na kuturehemu, bila shaka tutakuwa miongoni mwa wenye khasara (kubwa kabisa)”. (7:23).*

Kisa cha kulaghaiwa Adam na Hawwah na adui yao Iblis mpaka wakamuasi Mola wao kwa kula matunda waliyokatazwa, kinatufunza kuwa kuna maadui wasiopenda kuona Allah(s.w) anatiwa ipasavyo katika kuendea kila kipengele cha maisha ya kila siku. Na adui mkubwa kwa waumini ni shetani ambaye huingia katika nyoyo za watu na kuwahadaa kwa kuwapambia mambo maovu na kuyafanya mazuri kama Iblis (mkuu wa mashetani) alivyo wahadaa wazazi wetu kwa kuwaambia

..... وَقَالَ مَا نَهَاكُمَا رَبُّكُمَا عَنِ هَذِهِ الشَّجَرَةِ إِلَّا أَن تَكُونَا

مَلَٰكِيْنَ أَوْ تَكُونَا مِنَ الْخٰلِدِيْنَ ﴿٢٠﴾

*“Ewe Adamu, Je! Nikujulishe mti wa umilele na wa Ufalme usiokoma? (20:120), aidha aliwaambia: “Mola wenu hakukukatazeni mti huu ila msije kuwa Malaika au kuwa miongoni mwa wakaao milele (wasife)” (7:20).*

Shetani hakuishia hapo, bali aliwaapia kwa kuwaambia:

..... إِنِّي لَكُمَا لَمِنَ النَّٰصِحِيْنَ ﴿٢١﴾

*“.....Kwa yakini mimi ni mmoja wa watowao shauri njema kwenu.” (7:21).*

Hivyo waumini pamoja na jitihada zao za kuhuisha Uislamu na kuusimamisha katika jamii, hawana budi kuwa makini sana na adui

shetani ambaye daima huwajia watu kwa hadaa, tashwishi na ahadi za uongo. Mashetani ambao ni miongoni mwa majini na watu, huwapotosha watu na njia ya Allah(s.w) kupitia udhaifu wa matashi waliyo nayo; kwa mfano kama mtu anatamani kupata vitu vizuri kwa urahisi bila ya kuvifanyia juhudi stahiki,shetani atampambia aviendee vitu hivyo kwa njia ya kumuasi Mola wake japo anaweza pia asivipate kama si katika makadirio ya Allah(s.w). Tamaa ya kuwa **Malaika** au **kuishi milele** ndiyo iliyowaponza wazazi wetu, Adam na Hawwah. Tujue kuwa shetani hanauwezo wa kumlazimisha mtu kumuasi Mola wake kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

قَالَ رَبِّ بِمَا أَغْوَيْتَنِي لَأُزَيِّنَنَّ لَهُمْ فِي الْأَرْضِ  
وَلَأُغْوِيَنَّهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٣٩﴾

*“Akasema (Iblis): Mola wangu! Kwa Sababu umenihukumu kupotea, basi nitawapambia (wanaadamu upotevu) katika ardhi na nitawapoteza wote. (15:39)*

إِلَّا عِبَادَكَ مِنْهُمُ الْمُخْلَصِينَ ﴿٤٠﴾ قَالَ هَذَا صِرَاطٌ عَلَيَّ مُسْتَقِيمٌ ﴿٤١﴾ إِنَّ  
عِبَادِي لَيْسَ لَكَ عَلَيْهِمْ سُلْطَانٌ إِلَّا مَنِ اتَّبَعَكَ مِنَ الْغَاوِينَ ﴿٤٢﴾

*Isipokuwa waja wako waliosafika kweli kweli. Akasema (Mwenyezi Mungu) Hii njia yao ya (kuja) kwangu imenyooka. Hakika waja wangu, wewe hutakuwa na mamlaka juu yao; isipokuwa wale wenye kukufuata (kwa khiari zao) katika hao wapotofu.” (15:40-42)*

Wanaharakati wa kuhuisha Uislamu katika jamii wataepukana na hadaa za sheitwani kwa kufanya harakati kwa Ikhlas na kufuata vilivyo Qur-an na sunnah pamoja na kuomba msaada wa Allah(s.w) na kujikinga kwake na sheitwani kama Qur-an inavyotuongoza:



قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ ﴿١﴾ مَلِكِ النَّاسِ ﴿٢﴾ إِلَهِ النَّاسِ ﴿٣﴾ مِنْ شَرِّ  
 أَلْوَسَايَ الْخَنَّاسِ ﴿٤﴾ الَّذِي يُوَسْوِسُ فِي صُدُورِ النَّاسِ ﴿٥﴾ مِنَ الْجِنَّةِ  
 وَالنَّاسِ ﴿٦﴾

“Sema: Najikinga na Bwana Mlezi wa watu, Mfalme wa watu, Mola wa watu, na shari ya mwenye kutia wasiwasi, mwenye kurejea nyuma, atiaye wasiwasi nyoyoni mwa watu ambaye ni katika majini na watu.” (114:1-6).

au kuleta dua ifuatayo:

..... رَبِّ أَعُوذُ بِكَ مِنْ هَمَزَاتِ الشَّيْطَانِ ﴿٩٧﴾  
 وَأَعُوذُ بِكَ رَبِّ أَنْ يَحْضُرُونِ ﴿٩٨﴾

“.....Mola wangu! Najikinga kwako uniepushe na wasiwasi wa mashetani. Najikinga kwako Mola wangu, ili wasinihudhuri” (23:97-98)

Pamoja na kujikinga na sheitwani, hatunabudi kujiepusha na tabia za kishetani kama kuwa na kibri, majivuno na chuki binafsi dhidi ya watu pasina sababu ya msingi.

## Adam na Hawah Kushushwa Ardhini

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَائِكَةِ إِنِّي جَاعِلٌ فِي الْأَرْضِ خَلِيفَةً.....

(Wakumbeshe watu khabari hii) wakati Mola wako alipowaambia Malaika: “Mimi niteleta Khalifa kukaa katika ardhi” (2:30).

Hivyo bustani aliyowekwa ilikuwa ni mapito tu. Awamu ya kwanza ya maisha ya mwanaadamu ilikuwa ni peponi, awamu ya pili ni maisha ya hapa ardhini awamu ya tatu maisha ya Barzakh (kaburini) na awamu ya nne baada ya hukumu (Siku ya Kiyama),

maisha ya milele, peponi au motoni. Mwanzo wa mwanaadamu kuishi katika ardhi unabainishwa na aya zifuatazo;

قَالَ أَهْبِطُوا بَعْضُكُمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ وَلَكُمْ فِي الْأَرْضِ مُسْتَقَرٌّ وَمَتَاعٌ إِلَىٰ حِينٍ ﴿٢٤﴾ قَالَ فِيهَا تَحْيَوْنَ وَفِيهَا تَمُوتُونَ وَمِنْهَا تُخْرَجُونَ ﴿٢٥﴾

*Akasema (Mwenyezi Mungu): “Shukeni (katika ardhi), nyinyi kwa nyinyi ni maadui. Na makao yenu yatakuwa katika ardhi, na starehe yenu (pia) mpaka muda (niutakao mimi mwenyewe)”.* Akasema (Mwenyezi Mungu): “Mtaishi humo na mtafia humo, na mtatolewa humo (mtafufuliwa kwenda Akhera kulipwa)” (7:24-25).

## Mwongozo wa Allah kwa Wanaadamu.

Allah(s.w) hakumuacha Khalifa wake aanze maisha gizani. Bali alimpa mwongozo wa namna ya kuutekeleza Ukhalifa wake. Tunasoma katika Qur’an:

قُلْنَا أَهْبِطُوا مِنْهَا جَمِيعًا فَإِمَّا يَأْتِيَنَّكُمْ مِنِّي هُدًى فَمَنْ تَبَعَ هُدَايَ فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٣٨﴾ وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٣٩﴾

*Tukasema: “Shukeni humo nyote, na kama ukikufikieni mwongozo utokao kwangu basi watakaofuata uongozi wangu huo haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika, lakini wenye kukufuru na kuyakadhibisha maneno yetu, hao ndio watakoakuwa watu wa motoni, humo watakaa milele” (2:38-39).*

Utaratibu wa Allah unaobainishwa na aya hizi wa kuleta mwongozo unafanya kazi toka binaadamu wa mwanzo, Adam, hadi wa mwisho wa maisha haya ya duniani. Ni ahadi aliyoichukua Allah(s.w) kuwaletea waja wake mwongozo. Mwongozo ambao unakusudiwa watu waufuata wasibuni mifumo ya maisha kinyume na ule aliouleta Allah(s.w). Na zipo njia mbili tu za kuujua mwongozo wa Allah(s.w). Ama mtu kuletewa Wahyi

(Mitume) au kusoma kutoka kwa walioletewa Wahyi. Ndio maana tunaona Allah(s.w) ameleta Mitume pamoja na vitabu kuubanisha mwongozo huo.

Mwongozo huo umeletwa hatua kwa hatua, hadi kufikia kwa Mtume wa mwisho. Ni mwongozo unaokigusa kila kipengele cha maisha kwa mtu binafsi, taifa, na kimataifa katika ngazi zote, hali zote, mahali popote na wakati wowote. Hapana anachokihitajia mwanaadamu ila kimebainishwa katika mwongozo wa Allah(s.w)

## Historia ya Watoto Wawili wa Nabii Adam .

❖ وَأَنْزَلْنَا عَلَيْهِمْ نَبَأَ ابْنَيْ آدَمَ بِالْحَقِّ إِذْ قَرَّبَا قُرْبَانًا فَتُقُبِّلَ مِنْ أَحَدِهِمَا  
وَلَمْ يُتَقَبَّلْ مِنَ الْآخَرِ قَالَ لَأَقْتُلَنَّكَ قَالَ إِنَّمَا يَتَقَبَّلُ اللَّهُ مِنَ الْمُتَّقِينَ  
﴿٢٧﴾ لَئِن بَسَطتَ إِلَيَّ يَدَكَ لِتَقْتُلَنِي مَا أَنَا بِبَاسِطٍ يَدِيَ إِلَيْكَ لِأَقْتُلَنَّكَ  
إِنِّي أَخَافُ اللَّهَ رَبَّ الْعَالَمِينَ ﴿٢٨﴾ إِنِّي أُرِيدُ أَنْ تَبُوءَ بِإِثْمِي  
وَإِثْمِكَ فَتَكُونَ مِنْ أَصْحَابِ النَّارِ وَذَلِكَ جَزَاءُ الظَّالِمِينَ ﴿٢٩﴾  
فَطَوَّعَتْ لَهُ نَفْسُهُ قَتْلَ أَخِيهِ فَقَتَلَهُ فَأَصْبَحَ مِنَ الخَاسِرِينَ ﴿٣٠﴾  
فَبَعَثَ اللَّهُ غُرَابًا يَبْحَثُ فِي الْأَرْضِ لِيُرِيَهُ كَيْفَ يُورِي سَوْءَةَ أَخِيهِ قَالَ  
يَسْؤِلُنِّي أَعْجَزْتُ أَنْ أَكُونَ مِثْلَ هَذَا الْغُرَابِ فَأُوْرِي سَوْءَةَ أَخِي  
فَأَصْبَحَ مِنَ النَّادِمِينَ ﴿٣١﴾ مِنْ أَجْلِ ذَلِكَ كَتَبْنَا عَلَى بَنِي إِسْرَائِيلَ  
أَنَّهُ مَنْ قَتَلَ نَفْسًا بِغَيْرِ نَفْسٍ أَوْ فَسَادٍ فِي الْأَرْضِ فَكَأَنَّمَا قَتَلَ النَّاسَ  
جَمِيعًا وَمَنْ أَحْيَاهَا فَكَأَنَّمَا أَحْيَا النَّاسَ جَمِيعًا وَلَقَدْ جَاءَتْهُمْ رُسُلُنَا  
بِالْبَيِّنَاتِ ثُمَّ إِنْ كَثِيرًا مِنْهُمْ بَعْدَ ذَلِكَ فِي الْأَرْضِ لَمُسْرِفُونَ ﴿٣٢﴾

*“Na wasomee khabari za watoto wawili wa Adam kwa kweli, walipotoa sadaka, ikakubaliwa ya mmoja wao na ya mwingine haikukubaliwa Akasema (yule asiyekubaliwa sadaka yake):*

*“Nitakuua”. Akasema (yule aliyeahidiwa kuuawa): “Mwenyezi Mungu huwapokea wamchao tu”. “Kama utanyoosha mkono wako kwangu kuniua, mimi sitanyoosha mkono wangu kukuuwa. Hakika mimi ninamuogopa Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu .*

*“Mimi nataka ubebe dhambi zangu na dhambi zako, na kwa hivyo uwe miongoni mwa watu wa motoni. Na haya ndiyo malipo ya madhalimu”. “Basi nafsi yake ikamwezesha kumwua nduguye, na akawa miongoni mwa wenye kukhasirika”. Hapo Mwenyezi Mungu akamleta Kunguru anayefukua katika ardhi ili amwonyeshe jinsi ya kuificha maiti ya ndugu yake. Akasema: (yule ndugu aliyeua) “Ole wangu: Nimeshindwa kuwa sawa na kunguru huyu na kuficha maiti ya ndugu yangu”? Basi akawa miongoni mwa wenye kujuta. Kwa sababu ya hayo tukaawandikia wana wa Israel ya kwamba atakayemuua mtu bila ya yeye kuua mtu, au bila ya kufanya fisadi katika nchi, basi ni kama ameuu watu wote, na mwenye kumwacha mtu hai (kumsaidia kuishi) ni kamaH amewaacha hai watu wote. Bila shaka Mitume waliwafikia na hoja zilizo wazi; kisha wengi katika wao baada ya haya walikuwa waharibifu sana katika nchi” (5:27-32).*

Katika ya hizi majina ya watoto hawa wa Adam hayakutajwa. Bali majina hayo yamechukuliwa kutokana na maandishi mengi ya historia hasa historia ya Mayahudi. Wafasiri wengi wa Qur’an wanataja katika kuzitafsiri aya hizi kuwa, Habil na Kabil ni watoto wa moja kwa moja wa Adam na Hawwa. Na sio imetajwa kwa ishara tu kwa kuzingatia kuwa watu wote wametokana na Adam na Hawwa. Kwa mujibu wa maelezo ya Sheikh A. S. Farsy, hiki ndicho kisa cha awali cha mtu kumuua mwenziwe. Na aliyeuawa ndiye mwanaadamu wa mwanzo kufa. Kwa sababu hiyo basi aliyefanya mauaji hakujua nini la kufanya na yule maiti. Ndipo Allah(s.w) akamleta kunguru kumwonyesha namna ya kuhifadhi maiti ya ndugu yake.

Ili kuyafahamu vyema mafundisho ya kisa hiki cha watoto wa Adam(a.s) ni vyema tuyazingatie mazingira na wakati ziliposhuka aya za kukielezea kisa chenyewe. Tunafahamu kuwa awali Allah(s.w) aliwachagua Mayahudi na kuwapa ujumbe wake ili watekeleze wao wenyewe na kisha waufikishe kwa watu. Kwa hiyo akawatuma Mitume wengi miongoni mwa Mayahudi. Kutokana na neema hii waliyopewa kuletewa mwongozo na kupewa jukumu la kuusimamia, wakawa ni watu wenye hadhi kubwa.

يَدْبِنِي إِسْرَائِيلَ أَذْكَرُوا نِعْمَتِي الَّتِي أَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ وَأَنْتِي فَضَّلْتِكُمْ عَلَيَّ

الْعَلَمِينَ ﴿٤٧﴾

*“Enyi kizazi cha Israil (Mayahudi); Kumbukeni neema zangu nilizokuneemesheni na nikakutukuzeni kuliko viumbe wengine (wa wakati huo)” (2:47).*

Hata hivyo Mayahudi hawakuithamini neema hii ila wachache tu. Zaidi ya wao wenyewe kutokufuata mwongozo waliwaua mitume na kufuata baadhi ya kitabu huku wakiacha sehemu nyingine. Hii iliwapelekea kupata laana ya Allah(s.w).

Aidha Mayahudi waliobashiriwa kuja kwa Mtume(s.a.w) na waliahidi kuwa watamfuata. Bali alipokuja walimkataa.

وَإِذْ قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ يَدْبِنِي إِسْرَائِيلَ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ

إِلَيْكُمْ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيَّ مِنَ التَّوْرَةِ وَمُبَشِّرًا بِرَسُولٍ يَأْتِي مِنْ

بَعْدِي اسْمُهُ أَحْمَدٌ فَلَمَّا جَاءَهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ قَالُوا هَذَا سِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿٦١﴾

*Na(wakumbushe)aliposema (Nabii) Isa bin Maryam(kuwaambia Mayahudi): Enyi wana wa Israil! Mimi ni mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, nisadikishaye yaliyokuwa kabla yangu katika Taurati, na kutoa habari njema ya Mtume atakayekuja nyuma yangu ambaye jina lake litakuwa Ahmad(Muhammad). Lakini alipowajia na hoja zilizo wazi walisema: Huu ni udanganyifu ulio dhahiri. (61:6)*

Mayahudi hawakuishia kumkataa tu Mtume(s.a.w) walidhamiria kumwua pia. Hapakuwa na jingine lililowapelekea kufanya hayo, bali ni husuda na kibri. Ilikuwa wao baada ya kunyan'ganywa neema ya kuwa wafikishaji wa ujumbe wa Allah, watanabahi na kufanya mema ili Allah aweze kuwasamehe. Lakini wao walimwonea husuda Mtume(s.a.w) na wakawa wanafanya njama za kumwua.

Ni katika mazingira haya Allah(s.w) anabainisha kisa hiki cha watoto wa Adam(a.s) ili kuwaonya Mayahudi na sisi sote kuwa: Tusiwe na husuda juu ya Neema na amali njema za watu wengine hata tukaingia kwenye makosa kama ya mtoto wa Adam. Bali nasi tuzitakase nafsi zetu kwa kutenda mema asaa Allah(s.w) nasi akatunua daraja.

Allah hawaongoi na kuwapokelea maombi watu madhalimu. Aidha uongofu haupatikani kwa kumwonea husuda na kijicho mwenye kufanya mema. Bali kwa kujitakasa na kufanya amali njema.

..... قَالَ لَأَقْتُلَنَّكَ قَالَ إِنَّمَا يَتَقَبَّلُ اللَّهُ مِنَ الْمُتَّقِينَ ﴿٢٧﴾

.....*Akasema (yule asiyokubaliwa sadaka yake) nitakuwa” Akasema (yule aliyeaahidiwa kuuawa) “Mwenyezi Mungu huwapokelea wamchao tu.” (5:27)*

Vile vile Uislamu unatutaka tusiwe ni wenye kulipiza ubaya juu ya ubaya tunaotendewa. Mtu anatakiwa ajitete na awatete wengine dhulma inapotaka kufanyika. Lakini asipike uovu dhidi ya wengine. Bali amuogope Allah(s.w) na kushika njia iliyo sawa:

لَيْنٌ بَسَطْتَ إِلَىٰ يَدِكَ لِتَغْتُلَنِي مَا أَنَا بِبَاسِطٍ يَدِي إِلَيْكَ لِأَقْتُلَنَّكَ إِنِّي أَخَافُ

﴿٢٨﴾ رَبِّ الْعَالَمِينَ

“*Kama utanyosha mkono wako kwangu kuniua; mimi sitakuyooshea mkono wangu kukuua, hakika mimi namwongopa Mwenyezi. Mola wa walimwengu pia.” (5:28)*

## Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Adam(a.s)

- (i) Utukufu wa mtu katika Uislamu hautokani na nasaba, rangi, kabila, utajiri ila uwajibikaji kwa Allah(s.w) unaolandana na Elimu sahihi.
- (ii) Tujiepushe na tabia ya kiiblis ya kumtukuza au kumdharau mtu kutokana na nasaba, rangi, sura, hali yake kiuchumi, n.k.
- (iii) Tujiepushe na tabia ya Kiiblis ya kuwa na chuki binafsi dhidi ya watu wasio na hatia yeyote.
- (iv) Tujiepushe na tabia ya Kiiblis ya kibri na majivuno.
- (v) Tuwe na msimamo katika kutekeleza amri za Allah(s.w) na Mtume wake na tusiwe tayari kuyumbishwa na hadaa za shaitwani.
- (vi) Tunapofikwa na tashwishi za kishetani tujikinge kwa Allah(s.w).

وَإِنَّمَا يَنْزَغَنَّكَ مِنَ الشَّيْطَانِ نَزْعٌ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٣٦﴾

*“Na kama shetani akikushawishi kwa tashwishi (zake), wewe jikinge kwa Mwenyezi Mungu (kwa kusema: A'uudhubillah Minash-shaytwanir-Rajjim). Yeye ni mwenye kusikia mwenye kujua.” (41:36)*

Au ujikinge kwa kusema:

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ ﴿١﴾ مَلِكِ النَّاسِ ﴿٢﴾ إِلَهِ النَّاسِ ﴿٣﴾ مِنْ شَرِّ  
الْوَسْوَاسِ الْخَنَّاسِ ﴿٤﴾ الَّذِي يُوَسْوِسُ فِي صُدُورِ النَّاسِ ﴿٥﴾ مِنَ الْجِنَّةِ  
وَالنَّاسِ ﴿٦﴾

*Sema: najikinga kwa Bwana mlezi wa watu. Mfalme wa watu. Muabudiwa wa watu. Na shari ya mwenye kutia wasiwasi mwenye kurejea nyuma. Atiaye wasiwasi nyoyoni mwa watu. Ambaye ni katika majini na watu. (114:1-6)*

Au kuleta Dua ifuatayo:

..... رَبِّ أَعُوذُ بِكَ مِنْ هَمَزَاتِ الشَّيْطَانِ ﴿٩٧﴾ وَأَعُوذُ بِكَ رَبِّ أَنْ

يَحْضُرُونِ ﴿٩٨﴾

“..... Mola wangu! Najikinga kwako uniepushe na wasiwasi wa mashetani. Na najikinga kwako, Mola wangu, ili wasinihudhurie”. (23:97-98)

(vii) Muda wote Waislamu hawana budi kuchukua tahadhari kwani kiasili (tangu mwanzo wake) Uislamu ni dini yenye maadui miongoni mwa mashetani wa kijini na watu.

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا شَيْطَانِ الْإِنْسِ وَالْجِنِّ يُوحِي بَعْضُهُمْ إِلَى بَعْضٍ زُخْرُفَ الْقَوْلِ غُرُورًا.....

“Na namna hii tumemfanyia kila Nabii maadui, (nao ni) mashetani katika watu na majini. Baadhi yao wanawafunulia wenziwao maneno ya kupamba pamba ili kuwadanganya.....” (6:112)

(viii) Mwanaadamu tangu mwanzo wa kuumbwa kwake amekusudiwa kuwa Khalifa katika ardhi na nyenzo kuu ya kumuwezesha kuwa Khalifa ni **elimu ya mazingira na ya mwongozo**.

(ix) Tujiepushe na kuwahusudu watu juu ya meema walizotunukiwa na Allah(s.w) bali tumuelekee Allah(s.w) kwa unyenyekevu na k umuomba atuneemeshe kama wale aliowaneemesha.

وَلَا تَتَمَنَّوْا مَا فَضَّلَ اللَّهُ بِهِ بَعْضَكُمْ عَلَى بَعْضٍ لِّلرَّجَالِ نَصِيبٌ مِّمَّا كُتِبُوا وَلِلنِّسَاءِ نَصِيبٌ مِّمَّا كُتِبْنَ وَسَأَلُوا اللَّهَ مِن

فَضْلِهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمًا ﴿٣٢﴾



*Wala msitamani vile ambavyo Mwenyezi Mungu amewafadhilisha badhi yenu (kwa vitu hivyo) kuliko wengine. wanaume wanayo sehemu (kamili) ya vile walivyovichuma; na wanawake nao wanayo sehemu(kamili) ya vile walivyovichuma na mwombeni Mwenyezi Mungu fadhila zake. Hakika Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa kila kitu.(4:32)*

- (x) Allah(s.w) huwaongoza na kupokea maombi ya wale wajitakasao:

.....إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ التَّوَّابِينَ وَيُحِبُّ الْمُتَطَهِّرِينَ ﴿٢٢٢﴾

“..... Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanaotubu na kuwapenda wanaojitakasa” (2:222)

- (xi) Muislamu muumini anatakiwa ajihidi kuondosha ubaya au alipize ubaya aliofanyiwa kwa wema,yaani kumsamehe aliyemkosea kumpa aliyemnyima na kumchangamkia aliye mkasirikia. Tunahimizwa katika Qur’an:

وَلَا تَسْتَوِي الْحَسَنَةُ وَلَا السَّيِّئَةُ ادْفَعْ بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ فَإِذَا الَّذِي بَيْنَكَ  
وَبَيْنَهُ عَدَاوَةٌ كَأَنَّهُ وَلِيٌّ حَمِيمٌ ﴿٣٤﴾ وَمَا يُلْقِيهَا إِلَّا الَّذِينَ صَبَرُوا وَمَا  
يُلْقِيهَا إِلَّا ذُو حَظٍّ عَظِيمٍ ﴿٣٥﴾

“Mambo mazuri na mabaya hayawi sawa. Ondosha (ubaya uliofanyiwa kwa wema), tahamaki yule ambaye baina yako na baina yake kuna uadui atakuwa kama ni jamaa (yako) mwenye kukufia uchungu. Lakini (jambo hili) hawatapewa ila wale wanaosubiri wala hawatapewa ila wenye hadhi kubwa (mbele ya Mwenyezi Mungu)”(41:34-35)

- (xii) Tunapoteleza na kumkosea Allah(s.w),tumuelekee kwa unyenyekevu kwa kuleta toba ya kweli kama alivyofanya Adam(a.s) na mkewe.

- (xiii) Kumkosea Allah(s.w) kwa kibri kama alivyofanya Iblis ni jambo baya mno la hatari kwani humpelekea mtu kupigwa muhuri moyoni mwake kiasi cha kumfanya asione haja yoyote ya kuleta toba. Tunakumbushwa hili katika Qur'an.

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا سَوَاءٌ عَلَيْهِمْ ءَأَنذَرْتَهُمْ أَمْ لَمْ تُنذِرْهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٦﴾ خَتَمَ اللَّهُ عَلَى قُلُوبِهِمْ وَعَلَى سَمْعِهِمْ وَعَلَى أَبْصَارِهِمْ غِشَاوَةٌ وَلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٧﴾

“Hakika wale waliokufuru (kwa ukaidi tu na inadi) ni sawa kwao ukiwaonya au usiwaonye hawataamini. Kama kwamba Mwenyezi Mungu amepiga muhuri juu ya nyoyo zao na juu ya masikio yao; na juu ya macho yao pana kifuniko; basi watakuwa na adhabu kubwa.”(2:6-7)

## IDRISA(A.S)

Mtume aliyemfuatia Nabii Adam(a.s) katika Mitume 25 waliotajwa katika Qur-an ni Idrisa(a.s).

Nabii Idrisa(a.s) ametajwa kwa ufupi katika Qur-an

وَأَذْكُرُ فِي الْكِتَابِ إِدْرِيْسَ إِنَّهُ كَانَ صِدِّيقًا نَبِيًّا ﴿٥٦﴾ وَرَفَعْنَاهُ مَكَانًا عَلِيًّا ﴿٥٧﴾

“Na mtaje Idrisa katika Kitabu (hiki). Bila shaka yeye alikuwa mkweli sana (na) Nabii. Na tulimuinua daraja ya juu kabisa.” (19:56-57).

وَإِسْمَاعِيلَ وَإِدْرِيْسَ وَذَا الْكِفْلِ كُلٌّ مِّنَ الصَّابِرِينَ ﴿٨٥﴾

Na (mtaje) Ismail, na Idrisa na Dhul-kifli wote walikuwa miongoni mwa wanaosubiri.” (21:85)

Katika aya hizi Nabii Idrisa(a.s) ametajwa kuwa alikuwa Nabii wa Allah(s.w) aliyepoa katika **ukweli** na **subira** na Allah akamnyanyua daraja ya juu kabisa kutokana na sifa zake hizo. Hatuna taarifa zaidi ya harakati za Nabii Idrisa(a.s) katika kuhuisha Uislamu na kuusimamisha katika jamii yake, bali itoshe tu kuwa mwanaharakati anayefanya kazi ya Mitume wa Allah ya kusimamisha Uislamu katika jamii hanabudi kujipamba na tabia ya **ukweli** na **subira**.

## **NUHU(A.S)**

Mtume aliyemfuatia Nabii Idrisa(a.s)katika Mitume waliotajwa katika Qur-an ni Nabii Nuhu(a.s). Nuhu(a.s) ni miongoni mwa Mitume wa mwanzo mwanzo kabisa. Kutokana na mabaki ya kihistoria tunajifunza kuwa Nabii Nuhu na kaumu yake waliishi katika nchi ya Iraq.

### **Mazingira ya Jamii Aliyoikuta Nabii Nuhu (a.s)**

Nabii Nuhu(a.s) aliwakuta watu wa jamii yake wakimshirikisha Allah(s.w) kwa namna mbali mbali nawalikuwa wakiabudia masanamu waliyoyachonga na kuyapa majina ya **Wadda, Suwa’a, Yaghuutha, Ya’uuka** na **Nasraa**. Kama tulivyofahamishwa katika Qur-an kuwa viongozi wa jamii ya kishirikina ambao walikuwa ndio wapinzani wakubwa wa ujumbe wa Nabii Nuhu waliwanasihwa wafuasi wao:

وَقَالُوا لَا تَذَرُنَّ آلِهَتَكُمْ وَلَا تَذَرُنَّ وَدًّا وَلَا سُوَاعًا وَلَا يَغُوثَ وَيَعُوقَ

وَنَسْرًا ﴿٢٢﴾

*“Msiache miungu yenu, wala msiwache Wadda wala Suwa’a wala Yaghuutha na Ya’uka na Nasraa.” (71:23).*

Mtume(s.a.w) anatufahamisha katika Hadith kuwa **Wadda** na wale waliotajwa pamoja naye walikuwa ni watu wacha-Mungu katika jamii yao. Walipofariki,watu wakaanza kuyazungukia

makaburi yao na shetani akakichochea kizazi kilichofuata kuunda sanamu za watu hao. Kwa kufanya hivyo walidhani wangeliveza kuwaiga vitendo vyao vyema kwa kuwa na taswira za watu hao daima katika akili zao. Kizazi cha tatu kilishawishika kirahisi sana kuwa watu hao walikuwa ni miungu wanaostahiki kuabudiwa badala au pamoja na Allah(s.w). Masanamu yote yanayoabudiwa yana historia ya namna hii.

## **Wito wa Nabii Nuhu(a.s) kwa Watu Wake**

Nabii Nuhu(a.s) kama walivyofanya Mitume wote, aliwafundisha watu wake Tawhiid kuwa wamuamini Allah (s.w) kwa kuzingatia ishara mbali mbali zilizowazunguka, na kwamba wamuabudu yeye peke yake na wasimshirikishe na chochote. Aliwaonya juu ya adhabu kali itakayowafika iwapo hawatakoma kumshirikisha Allah(s.w) na miungu wengine. Juu ya wito wa Nuhu(a.s) kwa watu wake Qur-an inatufahamisha:

لَقَدْ أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِهِ فَقَالَ يَنْقُومُ الْعِبَادُ لِلَّهِ مَا لَهُمْ مِنْ إِلَهٍ غَيْرُهُ ۖ إِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿٥٩﴾

*“Tulimpeleka Nuhu kwa watu wake, naye akasema: “Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna Mungu ila yeye. Hakika mimi ninakukhofieni adhabu ya siku (hiyo) iliyo kuu.” (7:59).*

## **Mbinu za Da’wah Alizotumia Nuhu(a.s)**

Katika kufikisha ujumbe huu kwa watu wake Nuhu(a.s), alijitahidi kutumia mbinu mbali mbali ili wapate kumuelewa vizuri na kufuata ipasavyo ujumbe aliowaletea. Miongoni mwa mbinu alizozitumia ni hizi zifuatazo:

**Kwanza** alitoa hoja kwa watu wake za kuonesha haja na umuhimu wa kumuamini Allah(s.w) na kumuabudu ipasavyo. Aliwatanabahisha:

مَا لَكُمْ لَا تَرْجُونَ لِلَّهِ وَقَارًا ﴿١٣﴾ وَقَدْ خَلَقَكُمْ أَطْوَارًا ﴿١٤﴾  
 أَلَمْ تَرَوْا كَيْفَ خَلَقَ اللَّهُ سَبْعَ سَمَاوَاتٍ طِبَاقًا ﴿١٥﴾ وَجَعَلَ الْقَمَرَ  
 فِيهِنَّ نُورًا وَجَعَلَ الشَّمْسُ سِرَاجًا ﴿١٦﴾ وَاللَّهُ أَدْبَتَكُمْ مِنَ الْأَرْضِ  
 نَبَاتًا ﴿١٧﴾ ثُمَّ يُعِيدُكُمْ فِيهَا وَيُخْرِجُكُمْ إِخْرَاجًا ﴿١٨﴾ وَاللَّهُ جَعَلَ  
 لَكُمْ الْأَرْضَ بِسَاطًا ﴿١٩﴾ لِيَتَسَلَّكُوا مِنْهَا سُبُلًا فَجَاجًا ﴿٢٠﴾

*Mumekuwaje hamuweki hishima ya Mwenyezi Mungu. Na hali yeye amekuumbeni namna baada ya namna? Je hamuoni jinsi Mwenyezi Mungu alivyoziumba mbingu saba tabaka-tabaka(moja juu ya moja). Na Akakaufanya mwezi ndani yake uwe nuru na Akalifanya jua kuwa taa? Na Mwenyezi Mungu amekuotesheni katika ardhi, mimea. Kisha atakurudisheni humo na atakutoeni tena. Na Mwenyezi Mungu amekufanyieni ardhi kuwa busati (kitu kizuri mlichotandikiwa). Ili mtembee humo katika njia zilizo pana. (71:13-20)*

**Pili aliwabashiria malipo au jaza watakayopata endapo watamwamini na kumtii Allah(s.w) ipasavyo. Kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:**

قَالَ يَنْقُومِ إِلَىٰ لَكُمْ نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٢﴾ أَنْ أَعْبُدُوا اللَّهَ وَأَتَّقُوهُ وَأَطِيعُونَ ﴿٣﴾

*Akasema (Nuhu) Enyi watu wangu! Kwa hakika mimi ni mwonyaji niliyedhahiri kwenu. Ya kuwa mwabuduni Allah na mcheni na mnitii. (71:2-3)*

يَغْفِرُ لَكُمْ مِّنْ ذُنُوبِكُمْ وَيُخْرِجُكُمْ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى .....

*Atakusameheni madhambi yenu na atakuakhirisheni (bila ya balaa) mpaka muda uliowekwa.....(71:4)*

يُرْسِلِ السَّمَاءَ عَلَيْكُمْ مِدْرَارًا ﴿١١﴾ وَيُمْدِدْكُمْ بِأَمْوَالٍ وَبَنِينَ وَيَجْعَلْ لَكُمْ جَنَّاتٍ وَيَجْعَلْ لَكُمْ أَنْهَارًا ﴿١٢﴾

*Atakuleteeni mawingu yanyeshayo mvua nyingi. Na atakupeni mali na watoto, na atakupeni mabustani na atakufanyieni mito.*” (71:11-12)

**Tatu** aliwakhofisha watu wake na adhabu ya Allah(s.w) ya hapa duniani na huko akhera, endapo watakataa kumuamini Allah (s.w) na kumuabudu ipasavyo:

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِهِ إِتَىٰ لَكُمْ نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٢٥﴾ أَنْ لَا تَعْبُدُوا إِلَّا اللَّهَ ۗ إِنَّ اللَّهَ ۙ إِلَهٌ ۙ أَحَافٌ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ أَلِيمٍ ﴿٢٦﴾

*Na sisi tulimpeleka (tulimtuma) Nuhu kwa watu wake, (akawaambia): “Mimi kwenu ni Muonyaji anayebainisha (kila kitu). Ya kwamba msimuabudu yoyote isipokuwa Mwenyezi Mungu tu; hakika mimi ninakukhofieni adhabu ya siku (kubwa hiyo) inayoumiza.”* (11:25-26)

إِنَّا أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِهِ أَنْ أَنْذِرْ قَوْمَكَ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١﴾

*“Hakika sisi tulimtuma Nuhu kwa watu wake, ya kwamba waonye watu wako kabla ya kuwajia adhabu iumizayo.”* (71:1)

**Nne** aliwalingania usiku na mchana:

قَالَ رَبِّ إِنِّي دَعَوْتُ قَوْمِي لَيْلًا وَنَهَارًا ﴿٥﴾ فَلَمْ يَزِدْهُمْ دُعَائِي إِلَّا فِرَارًا ﴿٦﴾

*“Akasema (Nuhu): Ee Mola wangu: Kwa hakika nimewalingalia watu wangu usiku na mchana, lakini wito wangu haukuwazidishia ila kukimbia”* (71:5-6)

**Tano**, aliwalingania kwa njia ya muhadhara kwa sauti:

ثُمَّ إِنِّي دَعَوْتُهُمْ جَهَارًا ﴿٨﴾

*Tena niliwaita kwa jahari. (71:8)*

**Sita**, aliwalingania kwa siri kwa kumuendea mmoja mmoja:

ثُمَّ إِنِّي أَعْلَنْتُ لَهُمْ وَأَسْرَرْتُ لَهُمْ إِسْرَارًا ﴿٩﴾

*“Kisha nikawatangazia kwa kelele, tena nikasema nao kwa siri”. (71:9)*

**Saba**, aliwaweka watu wake wazi kuwa hakuwa anawalingania kwenye Dini ya Allah(s.w) kwa kutaraji malipo yoyote kutoka kwao bali alifanya hivyo kwa manufaa yao wenyewe.

وَمَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ إِنْ أَجْرِيَ إِلَّا عَلَى رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٠٩﴾

*“Na sikutakini juu yake ujira, ujira wangu hauko ila kwa Mola wa walimwengu wote.” (26:109)*

**Nane**, alisubiri na kudumu kuwalingania kwa mbinu zilizoainishwa kwa muda wa miaka elfu kasoro hamsini (950).

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِهِ فَلَبِثَ فِيهِمْ أَلْفَ سَنَةٍ إِلَّا خَمْسِينَ

عَامًا فَأَخَذَهُمُ الطُّوفَانُ وَهُمْ ظَالِمُونَ ﴿١٤﴾

*“Na bila shaka tulimtuma Nuhu kwa watu wake na akakaa nao miyaka elfu kasoro hamsini, (wasikubali kumfuata), basi tufani liliwafika, (wakaghariki), na hali walikuwa madhalimu (29:14)*

## **Walimuamini Nabii Nuhu(a.s)**

Walimuamini Nuhu(a.s) walikuwa watu wachache tena wale waliokuwa wanyonge na dhaifu katika jamii. Uchache na udhaifu wa waumini ilitumiwa na makafiri wa wakati wake kama hoja ya kumkataa Nuhu kuwa si Mtume wa Allah(sw).

﴿قَالُوا أَنْتُمْ مِنْ لَدُنْكُمْ وَأَنْتُمْ بَعْدَ الْأَرْذَالِ﴾

“Wakasema: Je, tukuamini wewe hali ya kuwa wanyonge ndio wanaokufuata? (26:111)

Uchache wa waumini waliokuwa pamoja na Nabii Nuhu(a.s) unadhihiri vizuri pale walipo weza kuenea kwenye safina ndogo iliyosheheni mizigo yao na jozi za wanyama mbali mbali kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

حَتَّىٰ إِذَا جَاءَ أَمْرُنَا وَفَارَ التَّنُّورُ قُلْنَا احْمِلْ فِيهَا مِنْ كُلِّ زَوْجَيْنِ اثْنَيْنِ  
﴿وَأَهْلَكَ إِلَّا مَن سَبَقَ عَلَيْهِ الْقَوْلُ وَمَنْ آمَنَ وَمَا آمَنَ مَعَهُ إِلَّا قَلِيلٌ﴾

“Hata ilipokuja amri yetu na ardhi ikaanza kufoka maji tulimwambia (Nuhu) Pakia humo (jahazini) jozi moja katika kila (nyama, jike na dume) na wapakie watu wako wa nyumbani kwako isipokuwa wale ambao imewapitia hukumu (ya Mwenyezi Mungu). Na (wachukue wote) walioamini.” Na hawakuamini pamoja naye ila wachache tu.” (11:40)

## Wapinzani wa Ujumbe wa Nabii Nuhu(a.s) na Vitimbi Vyao

Waliokuwa mstari wa mbele katika kupinga ujumbe wa Nabii Nuhu(a.s), ni viongozi wakuu wa jamii yake.

﴿قَالَ الْمَلَأُ مِنْ قَوْمِهِ إِنَّا لَنَرْنَكَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ﴾

Wakuu wa watu wake wakasema: Sisi tunakuona umo katika upotofu (upotevu) ulio dhahiri (kwa kutukataza haya tuliyowakuta nayo wazee wetu)” (7:60)

Katika kukataa ujumbe wa Nabii Nuhu(a.s), viongozi wa makafiri walitoa hoja dhahifu zifuatazo:



فَقَالَ الْمَلَائِكَةُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَوْمِهِ مَا نَرْنَا إِلَّا بَشَرًا مِثْلَنَا  
 وَمَا نَرْنَا إِلَّا الَّذِينَ هُمْ أَرَادْنَا بِآدِي الرَّأْيِ وَمَا نَرْنَا لَكُمْ عَلَيْنَا  
 مِنْ فَضْلٍ بَلْ نَظُنُّكُمْ كَاذِبِينَ ﴿٢٧﴾

“Na hapa wakasema wakubwa wa wale waliokufuru katika kaumu yake. Hatukuoni ila ni mtu tu sawa nasi; wala hatukuoni ila wamekufuata wale wanaoonekana dhahiri kuwa ni dhaifu (wanyonge) watu, (wamekufuata) kwa fikira ya mawazo tu (bila kupeleleza vizuri) wala hatukuoneni kuwa mnayo ziada juu yetu; bali tunakuoneni kuwa ni waongo. (11:27)

فَقَالَ الْمَلَأُوا الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَوْمِهِ مَا هَذَا إِلَّا بَشَرٌ مِثْلُكُمْ يُرِيدُ أَنْ  
 يَتَفَضَّلَ عَلَيْكُمْ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَأَنْزَلَ مَلَائِكَةً مَا سَمِعْنَا بِهَذَا فِي آبَائِنَا  
 الْأُولَىٰ ﴿٢٤﴾

Wakasema wale wakuu waliokufuru katika watu wake: “Hakuwa huyu (Nuhu) ila ni mtu kama nyinyi. Anataka kujipatia ubora juu yenu. Na kama Mwenyezi Mungu angependa (kukufundisheni), kwa yakini angateremsha Malaika. Hatukusikia haya kwa wazee wetu wa mwanzo.” (23:24)

إِنْ هُوَ إِلَّا رَجُلٌ بِهٖ جِنَّةٌ فَتَرَبُّصُوا بِهٖ حَتَّىٰ حِينٍ ﴿٢٥﴾

Hakuwa huyu ila ni mtu mwenye wazimu. Basi mngojeeni hata muda (wake atakufa).” (23:25)

Kwa mujibu wa aya hizi makafiri walikataa Utume wa Nabii Nuhu(a.s) kwa Sababu:

- Alikuwa mtu kama wao. Walitarajia kutumiwa Malaika.
- Waliomuamini walikuwa watu dhaifu kiuchumi na hadhi.
- Kwa upande mmoja, hawakuona faida yoyote iliyopatikana

kwa waumini kutokana na kuamini kwao na kwa upande mwingine, hawakuona hasara yoyote waliyoipata kutokana na huko kukufuru kwao.

- Walimuita Nabii Nuhu mwenda wazimu:

﴿ كَذَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوحٍ فَكَذَّبُوا عَبْدَنَا وَقَالُوا مَجْنُونٌ وَازْدُجِرَ ﴿٩﴾ ﴾

*Kabla yao watu wa Nuhu walikadhibisha nao. Walimkadhibisha mja wetu na wakasema ni mwendawazimu, na akawa anatolewa maneno makali”. (54:9)*

- Na walimtishia kumuua:

﴿ قَالُوا لَئِن لَّمْ تَنْتَهَ يَنْتُوْحُ لَتَكُوْنَنَّ مِنَ الْمَرْجُوْمِيْنَ ﴿١١٦﴾ ﴾

*“Wakasema: Kama hutaacha, Ewe Nuhu (nasaha zako hizi), bila shaka utakuwa miongoni mwa wanaorujumiwa (wanaopigwa kwa mawe mpaka wafe)”. (26:116)*

## **Msimamo wa Nabii Nuhu(a.s) Dhidi ya Makafiri**

Pamoja na upinzani mkali alioupata kutoka kwa viongozi wa makafiri, Nabii Nuhu(a.s) aliendelea kwa hima kulingania Dini ya Allah(s.w) na kuuweka wazi msimamo wake kama ifuatavyo:

﴿ وَأَنْزَلْنَا عَلَيْهِمْ نَبَأَ نُوحٍ إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ يَنْقُومِ إِن كَانَ كَبُرَ عَلَيْكُمْ

مَقَامِي وَتَذَكِّرِي بِآيَاتِ اللَّهِ فَعَلَى اللَّهِ تَوَكَّلْتُ فَأَجِيعُوا

أَمْرَكُمْ وَشُرَكَاءَكُمْ ثُمَّ لَا يَكُنْ أَمْرُكُمْ عَلَيْكُمْ غُمَّةً ثُمَّ اقْضُوا إِلَيَّ

وَلَا تُنظِرُونِ ﴿٦١﴾ ﴾

*“Wasomee habari za Nuhu alipowaambia watu wake: Enyi watu wangu! Ikiwa kukaa kwangu na nyinyi na kukumbusha kwangu Aya za Mwenyezi Mungu kunakuchukizeni, basi mimi nategemea kwa Mwenyezi Mungu. Nanyi kusanyeni mambo yenu na hao washirika wenu. (Kusanyikeni mje kunidhuru, mimi sijali). Tena*

*shauri lenu hilo lisifichikane kwenu (fanyeniu kwa dhahiri; mimi sijali tu). Kisha mpitisha kwangu (hilo mnalotaka kupitisha). Wala msinipe nafasi (hata kidogo. Mimi sijali, namtegemea Mwenyezi Mungu tu).” (10:71)*

Nabii Nuhu(a.s) aliendelea kuwausia watu wake na kudhihirisha msimamo wake.

وَيَقَوْمٌ لَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مَالًا إِنْ أَجْرِيَ إِلَّا عَلَى اللَّهِ  
وَمَا أَنَا بِطَارِدِ الَّذِينَ آمَنُوا إِنَّهُمْ مُلْمَعُونَ وَلِنُكَبِّنَّ أَرْزَاقَكُمْ  
قَوْمًا تَجْهَلُونَ ﴿٢٩﴾

*“Na enyi watu wangu! Mimi sikuombeni mali juu ya (jambo) hili; sina ujira wangu ila kwa Mwenyezi Mungu; na mimi sitawafukuza walioamini (kama mnavyotaka kwangu niwafukuze hao madhaifu ndipo msilimu nyinyi watukufu. Sitafanya hivyo); maana wao watakutana na Mola wao (awalipe kwa mema yao na mabaya yao). Lakini mimi nakuoneni nyinyi ni watu mnaofanya ujinga. (Mnakataa kuifuata haki kwa kuwa imefuatwa na madhaifu)! (11:29).*

Kwa ufupi tunajifunza kuwa:

- Nabii Nuhu(a.s) hakumchelea yeyote au chochote katika kulingania Dini ya Allah(s.w), bali alimtegemea Allah(s.w).
- Alilingania Dini ya Allah kwa kutarajia malipo kutoka kwake tu.
- Aliwapokea na kuwakumbatia wote waliomuamini bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

## **Ushindi wa Nabii Nuhu(a.s) na Wale Walioamini Pamoja Naye.**

Nabii Nuhu(a.s) alilingania Uislamu katika mazingira magumu ya upinzani mkubwa bila ya kukata tamaa kwa muda wa miaka 950. Alipoona kuwa viongozi wa makafiri wanazidi kuweka mikakati ya

kuzuia watu kusilimu kila uchao na kuwashinikiza kurudi kwenye ukafiri hata wale walioamini kwa kuwafanyia vitimbi mbalimbali, Nabii Nuhu(a.s) alilazimika kuomba msaada wa Allah(s.w) dhidi ya makafiri kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

وَنُوحًا إِذْ نَادَىٰ مِنْ قَبْلُ فَاسْتَجَبْنَا لَهُ فَنَجَّيْنَاهُ وَأَهْلَهُ مِنَ  
 ٱلْكَرْبِ ٱلْعَظِيمِ ﴿٧٦﴾

“Na (wakumbushe) Nuhu alipotulingania zamani (kutuomba) nasi tukamuitikia, na tukamuokoa yeye na watu wake katika shida (msiba) kubwa hiyo.(21:76)

وَنَصَرَ نَوَاحِيَهُ مِنَ ٱلْقَوْمِ ٱلَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا إِنَّهُمْ كَانُوا  
 قَوْمًا سَوِيًّا فَٱعْرَقْنَاهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٧٧﴾

Na tukamnusuru juu ya watu waliozikadhibisha aya zetu. Hakika wao walikuwa watu wabaya. Basi tukawatotesha (gharikisha) wote.” (21:77)

﴿٧٨﴾ كَذَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمٌ نُوحٍ فكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَقَالُوا ٱلْمُجْرِمُونَ ٱلَّذِينَ كَذَّبُوا  
 قَدَّعَارِبًا وَعَٰبِلًا فَٱتَّخَذُوهُم مَّقَابِلًا يُضْرَبُونَ ﴿٧٩﴾

Kabla yao kama tulivyoona watu wa Nuhu walikadhibisha nao. Walimkadhibisha mja Wetu na wakasema ni mwendawazimu; na akawa anatolewa maneno makali. Ndipo akamuomba Mola wake (akasema): “Kwa hakika mimi nimeshindwa, basi ninusuru.(54:9-10)

فَفَتَحْنَا ٱبْوَابَ ٱلسَّمَآءِ بِمَآءٍ مُّثَهِّرٍ ﴿٨١﴾ وَفَجَّرْنَا ٱلْأَرْضَ عُيُونًا فَٱلتَّقَىٰ  
 ٱلْمَآءِ عَلَىٰ أَمْرٍ قَدْفُذِيرٍ ﴿٨٢﴾

Mara tukaifungua milango ya mbingu kwa maji yanayomiminika (kwa nguvu kabisa). Na tukazibubujisha maji chemchem zilizo katika ardhi; na maji (ya juu na chini) yakakutana kwa jambo lililokadiriwa (na Mungu).(54:11-12)

وَحَمَلْنَاهُ عَلَىٰ ذَاتِ الْأَوْجِ وَدُوسِرٍ ﴿١٣﴾ تَجْرِي بِأَعْيُنِنَا جَزَاءَ لِمَن كَانَ

كُفِرَ ﴿١٤﴾

*Na Tukamchukua (Nabii Nuhu) katika ile(jahazi) iliyotenge nezwa kwa mbao na misumari. Ikawa inakwenda mbele ya macho, (hifadhi) Yetu. Hii ni tunzo (tuzo) kwa yule aliyekuwa amekataliwa (amekanushwa). (54:13-14)*

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa Nabii Nuhu(a.s) pamoja na waumini wachache aliokuwa nao walipata ushindi mkubwa juu ya makafiri waliokuwa wengi na uwezo mkubwa kwa msaada wa Allah(s.w). Allah(s.w) alitumia jeshi la “maji” kuwaangamiza makafiri na akawanusuru waumini kwa jahazi. Hii inatukumbusha kuwa:

وَاللَّهُ جُنُودَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿٧﴾

*“Na majeshi ya mbingu na ardhi ni ya Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu, mwenye hikima.” (48:7)*

## **Kuangamia kwa Mtoto na Mke wa Nuhu(a.s)**

Tukirejea Qur’an (11:36-48) na (23:26 -29) tunapata maelezo juu ya mchakato wa kuangamizwa makafiri na kuokolewa waumini katika kaumu ya Nabii Nuhu(a.s). Pamoja na Nabii Nuhu(a.s) kuahidiwa kuwa watu wake wa nyumbani watakuwa miongoni mwa watakaokolewa na gharka, mtoto wake alikataa kuingia kwenye jahazi(safina) na akawa ni miongoni mwa wenye kuangamia kama tunavyo jifunza katika aya zifuatazo.

وَقَالَ ارْكَبُوا فِيهَا بِسْمِ اللَّهِ مَجْرَاهَا وَمُرْسَاهَا إِنَّ رَبِّي لَغَفُورٌ  
 رَّحِيمٌ ﴿٤١﴾ وَهِيَ تَجْرِي بِهِمْ فِي مَوْجٍ كَالْجِبَالِ وَنَادَى نُوحٌ ابْنَهُ  
 وَكَانَ فِي مَعْزِلٍ يَبْنَئِي أَرْكَبَ مَعَنَا وَلَا تَكُن مَعَ الْكَافِرِينَ ﴿٤٢﴾ قَالَ  
 سَاقُوا إِلَى جَبَلٍ يَعْصِمُنِي مِنَ الْمَاءِ قَالَ لَا عَاصِمَ الْيَوْمَ مِنْ أَمْرِ اللَّهِ  
 إِلَّا مَنْ رَحِمْنَا وَحَالَ بَيْنَهُمَا الْمَوْجُ فَكَانَ مِنَ الْمُغْرَقِينَ ﴿٤٣﴾

*Na akasema(Nuhu): "Pandeni humo, kwa jina la Mwenyezi Mungu kuwe kwenda kwake na kusimamma kwake. Hakika Mola wangu ni mwingi wa kusamehe na mwingi wa kurehemu.*

*Ikawa hiyo (jahazi) inakwenda nao katika mawimbi kama milima. Na Nuhu akamwita mwanawe aliyekuwa mbali amekataa kuingia jahazini: "Ewe mwanangu! Panda pamoja nasi wala usiwe pamoja na makafiri". Na akasema (huyo mtoto) "Nitaukimbia Mlima utakaonilinda na maji" Akasema(Nuhu): "Hakuna leo wa kulindwa na amri ya Mwenyezi Mungu isipokuwa yule atakayemrehemu (Mwenyezi Mungu)." Mara mawimbi yakaingia baina yao na akawa miongoni mwa waliogharikishwa. (11:41-43)*

Baada ya gharika kuisha, Nabii Nuhu(a.s) Ilibidi amuelekee Mola wake kutaka kujua ni vipi mwanawe amekuwa miongoni mwa walioangamia.

وَنَادَى نُوحٌ رَبَّهُ فَقَالَ رَبِّ إِنَّ ابْنِي مِنْ أَهْلِي وَإِنَّ وَعْدَكَ الْحَقُّ  
 وَأَنْتَ أَحْكَمُ الْحَاكِمِينَ ﴿٤٥﴾ قَالَ يَبْنَوحُ إِنَّهُ لَيْسَ مِنْ أَهْلِكَ إِنَّهُ  
 عَمَلٌ غَيْرُ صَالِحٍ فَلَا تَسْأَلْنِ مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ إِنِّي أَعْطِكَ  
 أَنْ تَكُونَ مِنَ الْجَاهِلِينَ ﴿٤٦﴾ قَالَ رَبِّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ أَنْ أَسْأَلَكَ مَا لَيْسَ  
 لِي بِهِ عِلْمٌ وَإِلَّا تَغْفِرْ لِي وَتَرْحَمْنِي أَكُنْ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٤٧﴾

*Na Nuhu alimuomba Mola wake (alipomuona mwanawe anaangamia) akasema: Ewe Mola wangu! Mwanangu ni katika watu wa nyumbani kwangu (mbona anaangamia)? Na hakika ahadi Yako ni haki; nawe ni mwenye haki kuliko mahakimu (wote).”Akasema (Mwenyezi Mungu): “Ewe Nuhu! Huyu si miongoni mwa watu wako. Yeye ni (mwenye) mwenendo usikuwa mzuri. Basi usiniombe ambayo huyajui. Mimi nakunasihhi usiwe miongoni mwa wajinga.” (Nuhu) Akasema: Ee Mola wangu! Mimi najikinga kwako nisije kukuambatena nisyoyajua; na kama hutanisamehe na kunirehemu nitakuwa miongoni mwa watakapata khasara.”(11:45-47)*

Pia tunahamishwa juu ya kuangamia mke wa Nuhu(a.s) katika aya ifuatayo:

ضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا لِلَّذِينَ كَفَرُوا امْرَأَتَ نُوحٍ وَامْرَأَتَ لُوطٍ كَانَتَا تَحْتَ  
 عَبْدَيْنِ مِنْ عِبَادِنَا صَالِحَيْنِ فَخَانَتَاهُمَا فَلَمْ يُغَيِّبْنَا عَنْهُمَا مِنَ اللَّهِ شَيْئًا  
 وَقِيلَ ادْخُلَا النَّارَ مَعَ الدَّٰخِلِينَ ﴿١٦﴾

*Mwenyezi Mungu amepiga (anapiga)mfano wa wale wabaya waliokufuru, ni mkewe Nuhu na mkewe Luti. Walikuwa chini ya waja wetu wema wawili hao miongoni mwa waja wetu (wema) lakini(wanawake hao), waliwafanyia khiana (waume zao watukufu hao) na (waume zao hao) hawakuweza kuwasaidia*

*chochote mbele ya Mwenyezi Mungu na ikasemwa: “Uingieni Moto pamoja na hao wanaouingia.” (66:10)*

Kuangamia kwa mtoto na mke wa Nuhu(a.s) pamoja na mke wa Lut(a.s) tunajifunza kuwa mtu hataokoka na ghadhabu ya Allah(s.w) kutokana a unasaba alioona na watu wema na wala hata faidika na malipo ya amali njema walizofanya wengine. Kinyume chake hataadhibiwa mtu mwema kwa kuwa na unasaba na watu waovu maadamu anawafikishia ujumbe na wakamkanusha kama tunavyopigiwa mfano wa mke wa firaun, aliyekuwa mcha-mungu.

وَضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا لِّلَّذِينَ ءَامَنُوا أَمْرَاتَ فِرْعَوْنَ إِذْ قَالَتْ رَبِّ ابْنِ لِي  
عِندَكَ بَيْتًا فِى الْجَنَّةِ وَنَجِّنِي مِّنْ فِرْعَوْنَ وَعَمَلِهِۦ وَنَجِّنِي مِّنَ الْقَوْمِ  
الظَّالِمِينَ ﴿١١﴾

*Na Mwenyezi Mngu amepiga, (anapiga) mfano wa wale walioamini kweli, ni mkewe Firauni, aliposema; “Ee Mola wangu! Nijengee nyumba Peponi karibu yako na uniokoe na Firauni na amali zake (mbovu), na Niokoe na watu madhalimu” (66:11)*

### **Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Nuhu(a.s)**

- (i) Tuanze kulingania kwa Tawhiid – kumjua Allah(s.w) fika na kumuabudu ipasavyo.
- (ii) Tulinganie kwa kutumia hoja na mbinu mbalimbali kulingana na mazingira na wakati.
- (iii) Tutumie hoja kuonesha udhaifu wa hoja za makafiri dhidi ya Uislamu.
- (iv) Tusimchelee yeyote au chochote katika kulingania na kusimamisha Dini ya Allah(s.w).



- (v) Tulinganie Uislamu kwa kutaraji malipo kutoka kwa Allah(s.w)pekee.
- (vi) Waumini hawana budi kushikamana pamoja katika kulingania na kusimamisha Uislamu katika jamii.
- (vii) Mlinganiaji awe na subira na kutowakatia tamaa wale anaowalingania – Nabii Nuhu(a.s) alilingania miaka 950 na kupata wafuasi wachache sana bila ya kukata tamaa.
- (viii) Mlinganiaji amuombe Allah(s.w) na kutegemea msaada kutoka kwake.
- (ix) Hatanusurika mtu muovu na adhabu ya Allah(s.w) kutokana na nasaba yake na Mitume wa Allah(s.w) na watu wema.
- (x) Hatima ya makafiri ni kuhiliki katika maisha ya dunia na akhera.

﴿٥٩﴾ وَلَا يَحْسَبَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا سَبَقُوا إِنَّهُمْ لَا يُعْجِزُونَ

*“Wala wale waliokufuru wasifikiri kwamba wao wamekwi shatangulia (mbele, Allah hawapati), la, wao hawatamshinda (Mwenyezi Mungu). (8:59).*

- (xi) Hatima ya waumini wanaharakati ni kuwashinda maadui zao hapa ulimwenguni na kupata pepo huko akhera.
- (xii) Kushindwa na kuhiliki kwa makafiri wenye nguvu kubwa za kijeshi na kiuchumi na waumini wachache na dhaifu kijeshi nakiuchumi ni alama ya kuwepo Allah(s.w) aliyoahidi kuwatawalisha katika ardhi waumini wanaharakati.(Qur-an 24:55).
- (xiii) Siku zote wanaoongoza katika upinzani ni viongozi wa kikafiri(matwaghuti).

- (xiv) Hatuna mtu atakaye epukana na ghadhabu za Allah(s.w) na kupata pepo kwa amali njema alizofanya mtu mwingine hata akiwa na unasaba au urafiki wa karibu kiasi gani. Mtoto na mke wa Nuhu(a.s) waliangamia kutokana na matendo yao maovu.
- (xv) Hakuna mtu atakaye adhibiwa kwa maovu ya mwingine na huku akiwa ni muumini mtenda mema. Mkewe Firaun ni miongoni mwa wanawake wema waliotajwa katika Qur'an.

## HUD(A.S)

Baada ya Nuhu(a.s) Mtume aliyemfuatia ni Nabii Hud(a.s). Hud(a.s) alitumwa na Mola wake kuwalingania kabila (taifa) la 'Ad. Kabila la 'Ad lilikuwa likijulikana kama 'Ad-al-ram au 'Ad-Ula. 'Ad walikuwa wakiishi kusini ya Bara Arab, eneo la kati ya Oman hadi Hadharamut na Yemen. Akina 'Ad waliongoza katika teknolojia ya kujenga majumba marefu katika makazi yao:

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِعَادٍ ﴿١﴾ إِرَامَ دَاتِ الْعِمَادِ ﴿٧﴾ الَّتِي لَمْ يُخْلَقْ  
مِثْلَهَا فِي الْبَلَدِ ﴿٨﴾

*“Je, hukuona jinsi Mola wako alivyowafanya 'Ad? Iram (waliokuwa) wanamajumba marefu marefu. Ambao hawakuumbwa mfano wao katika miji. (89:6-8)*

Baada ya muda kupita, 'Ad waliacha mafundisho sahihi ya Nabii Nuhu(a.s) ya kumpwekesha Allah(s.w) na wakarejea tena kwenye kuabudia masanamu wakiongozwa na wakuu wa jamii. Ndipo, Hud(a.s) akatumwa na Mola wake kuhuisha tena Uislamu.

﴿١٥﴾ وَإِلَىٰ عَادٍ أَخَاهُمْ هُودًا قَالَ يَا قَوْمِ أَعْبُدُوا اللَّهَ  
مَا لَكُمْ مِّنْ إِلَٰهٍ غَيْرُهُ ۖ أَفَلَا تَتَّقُونَ ﴿١٥﴾

“Na kwa ‘Ad (tulimpeleka) ndugu yao Hud akasema: Enyi kaumu yangu! Muabuduni Allah, nyinyi hamna Mungu ila yeye. Basi hamuogopi?” (7:65)

## Mbinu za Hud(a.s) Katika Kufikisha Ujumbe

Katika kulingania Uislamu kwa watu wake, Hud(a.s) alitumia mbinu zifuatazo:

**Kwanza** alijieleza kwa uwazi na kuwanasihi watu wake:

قَالَ يَتَقَوْمَ لَيْسَ بِي سَفَاهَةٌ وَلَنْ كَيْتِي رَسُولٌ مِّن رَّبِّ الْعَالَمِينَ  
﴿١٧﴾ أُبَلِّغُكُمْ رِسَالَاتِ رَبِّي وَأَنَا لَكُمْ نَاصِحٌ أَمِينٌ ﴿١٨﴾

“Akasema: Enyi kaumu yangu! Mimi sio mpumbavu. Lakini mimi ni Mtume niliyetoka kwa Mola wa walimwengu. Nakufikishieni ujumbe wa Mola wangu. Na mimi kwenu ni (mtu) nasihni muaminifu. (7:67-68)

أَوْعَجِبْتُمْ أَنْ جَاءَكُمْ ذِكْرٌ مِّن رَّبِّكُمْ عَلَى رَجُلٍ مِّنكُمْ لِيُنذِرَكُمْ  
وَأَذْكُرُوا إِذْ جَعَلَكُمْ خُلَفَاءَ مِن بَعْدِ قَوْمِ نُوحٍ وَزَادَكُمْ فِي  
الْخَلْقِ بَصُطَةً فَادْكُرُوا ءَالَآءَ اللَّهِ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿١٩﴾

Mnaona ajabu kukufikieni mawaidha yanayotoka kwa Mola wenu kwa (ulimi wa) mtu aliye mmoja katika nyinyi ili akuonyeni? (Muabuduni Mwenyezi Mungu) na mkumbuke alivyokufanyeni Khalifa baada ya watu wa Nuhu. Na akakuzidisheni sana katika umbo. Basi zikumbukeni neema za Mwenyezi Mungu ili mpate kufaulu.” (7:69)

**Pili** aliwapa hoja kwanini wanalazimika kumuamini Allah na kumuabudu ipasavyo.

وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي أَتَدُّكُمْ بِمَا تَعْلَمُونَ ﴿١٣٣﴾ أَمَدُّكُمْ بِأَنْعَمٍ وَبَيْنَ

﴿١٣٣﴾ وَجَنَّتِ وَعُيُونِ ﴿١٣٤﴾

*Mcheni yule ambaye amekupeni haya mnayoyajua.* “Amekupeni (chungu ya) wanyama na watoto wanaume.” “Na mabustani na chemchem, (mito).” (26:132-134)

**Tatu**, aliwabashiria kupata malipo mema hapa hapa ulimwe nguni endapo watamcha Allah(s.w) ipasavyo:

وَيَنْقُومُ اسْتِغْفِرُوا رَبَّكُمْ ثُمَّ تُوبُوا إِلَيْهِ يُرْسِلِ السَّمَاءَ عَلَيْكُمْ مِدْرَارًا

وَيَرْزُقْكُمْ قُوَّةً إِلَى قُوتِكُمْ وَلَا تَتَوَلَّوْا مُجْرِمِينَ ﴿٥٧﴾

“Enyi watu wangu! Ombeni msamaha kwa Mola wenu (kwa mabaya yenu yaliyopita) kisha mtubie kwake, atakuleteeni mawingu yateremshayo mvua tele, na atakuzidishieni nguvu juu ya nguvu zenu (mlizonazo). Wala msikengeuke kuwa waovu.” (11:52)

**Nne**, aliwahofisha watu wake na adhabu kali ya Allah(s.w) iwapo watamuasi.

فَإِنْ تَوَلَّوْا فَقَدْ أَبْلَغْتُكُمْ مَا أُرْسِلْتُ بِهِ إِلَيْكُمْ وَيَسْتَخْلِفُ رَبِّي قَوْمًا

غَيْرَكُمْ وَلَا تَضُرُّوهُ شَيْئًا إِنْ رَبِّي عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ حَفِيظٌ ﴿٥٧﴾

“Na kama mtarudi nyuma (hainidhurishi kitu); nimekwisha kukufikishieni niliyotumwa nayo kwenu; na Mola wangu atawafanya makhalifa (wakazi wa mahali hapa) watu wengine wasiokuwa nyinyi; wala nyinyi hamtaweza kumdhuru hata kidogo. Hakika Mola wangu ni Mwenye kuhifadhi kila kitu.” (11:57)

إِذْ قَالَ لَهُمْ أَخُوهُمْ هُودٌ أَلَا تَتَّقُونَ ﴿١٣٤﴾ إِبْنِي لَكُمْ رَسُولًا آمِينَ ﴿١٣٥﴾

“(Wakumbushe) alipowaambia ndugu yao Hud. ‘Je, hamtamu ogopa (Mwenyezi Mungu hata nikiputajieni adhabu yote

*itakayokufikieni kwa mabaya yenu mnayoyafanya)? Bila shaka mimi kwenu ni Mtume muaminifu.” (26:124-125).*

**Tano**,aliwafahamisha kwa uwazi watu wake kuwa hakutarajia kupata malipo ya Utume wake kutoa kwao.

يَدْقُومٌ لَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا ۖ إِنِّي أَجْرِي إِلَّا عَلَى الَّذِي فَطَرَنِي ۗ أَفَلَا

تَعْقِلُونَ ﴿٥١﴾

*“Enyi watu wangu! Sikuombeni ujira juu ya haya. Hakuwa ujira wangu ila kwa yule aliyeniumba. Basi hamyatii akilini (haya ninayokuambieni)?” (11:51).*

وَمَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ ۖ إِنِّي أَجْرِي إِلَّا عَلَى رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٢٧﴾

*“Wala sikutakieni juu yake ujira, ujira wangu haupo ila kwa Mola wa walimwengu wote.” (26:127)*

## **Wapinzani wa Ujumbe wa Hud(a.s)**

Waliomuamini Mtume Hud(a.s) walikuwa watu wachache na wengi walipinga ujumbe wake. Waliongozwa na Wakuu wa jamii.

قَالَ الْمَلَأُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَوْمِهِ ۖ إِنَّا لَنَرُكَ فِي سَفَاهَةٍ ۖ وَإِنَّا لَنَنظُنُّكَ

مِنَ الْكَاذِبِينَ ﴿٣١﴾

*“Wakasema wakuu waliokufuru katika kaumu yake, sisi tunakuona umo katika upumbavu na tunakuona u miongoni mwa waongo.” (7:66).*

Katika kuupinga ujumbe wa Mtume Hud (a.s), makafiri walitoa hoja zifuatazo:

**Kwanza**,walidai kuwa hawako tayari kuacha kuabudu yale waliyokuwa wakiabudu wazee wao.

قَالُوا أَجِئْتَنَا لِنَعْبُدَ اللَّهَ وَحْدَهُ وَنَذَرَ مَا كَانَ يَعْبُدُ آبَاؤَنَا فَأَتَيْنَا بِمَا

تَعِدُنَا إِنْ كُنْتَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٧٠﴾

*Wakasema: “Je! umetujia ili tumuabudu Mwenyezi Mungu peke yake na tuache waliyokuwa wakiabudu baba zetu? Basi tulettee unayotuahidi ikiwa ni miongoni mwa wasemao kweli.” (7:70).*

**Pili**,walidai kuwa Hud(a.s) alikuwa mzushi kama wazushi wengine waliotokea katika zama mbali mbali na hasa pale alipowaambia watu watafufuliwa baada ya kufa na kulipwa kwa yale waliyoyafanya hapa duniani.

إِنْ هَذَا إِلَّا خُلُقُ الْأَوَّلِينَ ﴿١٣٧﴾ وَمَا نَحْنُ بِمُعَذِّبِينَ ﴿١٣٨﴾

*“Hayakuwa haya (ya kuja watu kusema kuwa wao ni Mitume) ila ni tabia ya watu wa (tangu) kale. Wala sisi hatutaadhibiwa (kama unavyodai na walivyodai hao).” (26:137-138)*

أَيَعِدُكُمْ أَنْتُمْ إِذَا مِتُّمْ وَكُنْتُمْ تُرَابًا وَعِظَامًا أَنْتُمْ مُخْرَجُونَ ﴿٣٥﴾

﴿٣٦﴾ هِيَ هَاتَ هَيْهَاتَ لِمَا تُوعَدُونَ ﴿٣٦﴾

*“Je anakuahidini ya kwamba mtakapokufa na mkawa udongo na mifupa, kuwa mtatolewa, (mtafufuliwa)?” Hayawi hayo mnayoaahidiwa. (23:35-36).*

إِنْ هُوَ إِلَّا رَجُلٌ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا وَمَا نَحْنُ لَهُ بِمُؤْمِنِينَ ﴿٣٨﴾

*Hakuwa huyu (anayejiita Mtume) ila ni mtu anayemzulia Mwenyezi Mungu uwongo, wala sisi si wenye kumuamini. “(23:38)*

**Tatu**,walidai kuwa Hud (a.s) alikuwa mpumbavu au mjinga.

قَالَ الْمَلَأُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَوْمِهِ إِنَّا لَنَرَنَّكَ فِي سَفَاهَةٍ وَإِنَّا لَنَظُنُّكَ

مِنَ الْكَاذِبِينَ ﴿١١﴾

“Wakasema wakuu waliokufuru katika kaumu yake, “Sisi tunakuona umo katika upumbavu na tunakuona u miongoni mwa waongo”. (7:66).

**Nne**, walidai kuwa hakuwa Mtume kwa kuwa alikuwa mtu ana yekula na kunywa kama wao:

وَقَالَ الْمَلَأُ مِنْ قَوْمِهِ الَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِإِيقَاعِ الْآخِرَةِ وَأَتْرَفْنَاهُمْ  
فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا مَا هَذَا إِلَّا بَشَرٌ مِثْلُكُمْ يَأْكُلُ مِمَّا تَأْكُلُونَ  
مِنْهُ وَيَشْرَبُ مِمَّا تَشْرَبُونَ ﴿٣٣﴾

*Na wakubwa katika watu wake waliokufuru na kukadhibisha makutano ya akhera, na tuliwatajirisha katika maisha ya dunia, walisema: “Hakuwa huyu ila ni mtu kama nyinyi, anakula katika vile mnavyokula na anakunywa katika vile mnavyokunywa.” (23:33)*

## **Msimamo wa Nabii Hud(a.s) Dhidi ya Makafiri wa Kaumu Yake**

Pamoja na kwamba alipingwa na nguvu za Dola ya makafiri wa kaumu yake, Mtume Hud(a.s), hakutetereka katika msimamo wake wa kutangaza Ufalme wa Allah(s.w) na kufikisha ujumbe wake. Hakutetereka kwa sababu alitegemea ulinzi wa yule aliyemtuma, mwenye uwezo juu ya kila kitu kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

..... قَالَ إِنِّي أَشْهَدُ اللَّهَ وَأَشْهَدُوا أَنِّي بَرِيءٌ مِمَّا تُشْرِكُونَ ﴿٥٤﴾  
أَنِّي بَرِيءٌ مِمَّا تُشْرِكُونَ ﴿٥٤﴾ مِنْ دُونِهِ فَكَيْدُونِي جَمِيعًا ثُمَّ  
لَا تَنْظِرُونَ ﴿٥٥﴾

“.....Akasema (Hud) mimi namshuhudia Mwenyezi Mungu, nanyi shuhudieni ya kwamba mimi niko mbali na hao mnaowashirikisha (na Mwenyezi Mungu) mkaacha (kumuabudu)

yeye (pekee). Basi nyote nifanyieni hila (za kunidhuru) kisha msinipe muhula wowote”.(11:54-55).

إِنِّي تَوَكَّلْتُ عَلَى اللَّهِ رَّبِّي وَرَبِّكُمْ مَا مِنْ دَابَّةٍ إِلَّا هُوَ آخِذٌ بِنَاصِيَتِهَا إِنَّ  
رَبِّي عَلَىٰ صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٥٦﴾

Mimi nimentegemea Mwenyezi Mungu, Mola wangu na Mola wenu. Hakuna kiumbe chochote isipokuwa (Mwenyezi Mungu) anamsanifu atakavyo. Bila shaka Mola wangu yuko juu ya njia iliyonyooka.(11:56)

فَإِن تَوَلَّوْا فَقَدْ أَبْلَغْتُكُمْ مَا أُرْسِلْتُ بِهِ إِلَيْكُمْ وَيَسْتَخْلِفُ رَبِّي قَوْمًا  
غَيْرَكُمْ وَلَا تَضُرُّوهُ شَيْئًا إِنَّ رَبِّي عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ حَفِيظٌ ﴿٥٧﴾

Na kama mkirudi nyuma (hainidhurishi kitu); nimekwisha kukufikishieni niliyotumwa nayo kwenu; na Mola wangu atawafanya Makhalifa (wakazi wa mahala hapa) watu wengine wasiokuwa nyinyi wala nyinyi hamtaweza kumdhuru hata kidogo. Hakika Mola wangu ni mwenye kuhifadhi kila kitu.”. (11:57)

## Ushindi wa Nabii Hud(a.s) Juu ya Makafiri

Makafiri walivyozidi kutakabari na kuzidisha fisadi katika ardhi ikiwa ni pamoja na kutaka kumdhuru Nabii Hud(a.s) na wale walioamini pamoja naye, Allah(s.w) alipitisha hukumu yake ya kuwahilikisha makafiri na kuwanusuru waumini kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

وَلَمَّا جَاءَ أَمْرُنَا نَجَّيْنَا هُودًا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ بِرَحْمَةٍ مِنَّا وَنَجَّيْنَا لَهُمْ  
مِّنْ عَذَابٍ غَلِيظٍ ﴿٥٨﴾

Ilipofika amri yetu ya (kuangamizwa) tulimuokoa Hud pamoja na wale walioamini pamoja naye kwa rehema itokayo kwetu. Na tukawaokoa katika adhabu ngumu.(11:58)



وَتِلْكَ عَادٌ جَحَدُوا بِقَابَتِ رَبِّهِمْ وَعَصَوْا رُسُلَهُ وَاتَّبَعُوا أَمْرَ كُلِّ جَبَّارٍ

عِنْدِ ﴿٥٩﴾

*Na hao ndio 'Ad. Walikanusha aya za Mola wao, na wakawaasi Mitume yake na wakafuata amri ya kila jabari mkaidi. (11:59)*

وَاتَّبَعُوا فِي هَذِهِ الدُّنْيَا لَعْنَةً وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ إِلَّا إِنْ عَادَا كَفَرُوا

رَبَّهُمْ إِلَّا بَعْدًا لِعَادِ قَوْمِ هُودٍ ﴿٦٠﴾

*Na wakafuataishiwa laana katika dunia hii na siku ya kiyama. Sikilizeni hakika 'Ad walimkufuru Mola wao. Wakaangamizwa hao 'Ad kaumu ya Hud.' (11:60)*

Jeshi la Allah(s.w) lililotumika dhidi ya makafiri katika jamii ya akina 'Ad ni upepo mkali uliovuma mfululizo kwa siku nane (mausiku Sabaa na michana minane) kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

فَلَمَّا رَأَوْهُ غَارِضًا مَّسْتَقْبِلَ أَوْدِيَّتِهِمْ قَالُوا هَذَا غَارِضٌ مُّطِرْنَا بَلْ هُوَ مَا

أَسْتَعْجَلْتُمْ بِهِ ۗ رِيحٌ فِيهَا عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٧٤﴾ نُدَمِرُ كُلَّ شَيْءٍ بِأَمْرِ رَبِّهَا

فَأَصْبَحُوا لَا يَرَوْنَ إِلَّا مَسَكِنَتَهُمْ ۚ كَذَلِكَ نَجْزِي الْقَوْمَ الْمُجْرِمِينَ ﴿٧٥﴾

*Basi walipoliona wingu likiyaelekea mabonde yao, walisema: "Wingu hili la kutunyeshea mvua." (Wakaambiwa) "Bali haya ni ile mliyokuwa mkitaka ije kwa upesi, (adhabu ya Mwenyezi Mungu). Ni upepo ambao ndani yake iko adhabu iumizayo." "Unaoangamiza kila kitu kwa amri ya Mola wake." Basi wakawa si wenye kuonekana tena ila nyumba zao tu (ndizo zilizosalia). Hivyo ndivyo tuwalipavyo watu waovu. (46:24-25)*

وَأَلْقَدَ مَكَّنْتَهُمْ فِيمَا إِن مَكَّنْتَكُمْ فِيهِ وَجَعَلْنَا لَهُمْ سَمْعًا وَأَبْصَرًا وَأَفْئِدَةً

فَمَا أَغْنَى عَنْهُمْ سَمْعُهُمْ وَلَا أَبْصَرُهُمْ وَلَا أَفْئِدَتُهُمْ مِّنْ شَيْءٍ إِذْ

كَانُوا يَجْحَدُونَ بِآيَاتِ اللَّهِ وَحَاقَ بِهِمْ مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِءُونَ ﴿٢٦﴾

*Na bila shaka tuliwastawisha katika yale tusiyokustawisheni nyinyi, na tuliwapa masikio na macho na nyoyo; lakini masikio yao na macho yao na nyoyo zao hazikuwafaa chochote walipokuwa wakikanusha Aya za Mwenyezi Mungu, na yakawazunguka yale waliyoyafanyia mzaha. (46:26)*

وَلَا تَجْعَلُوا مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ إِنِّي لَكُم مِّنْهُ نَذِيرٌ مُّبِينٌ

﴿٥١﴾ كَذَلِكَ مَا آتَى الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ مِّن رَّسُولٍ إِلَّا قَالُوا سَاحِرٌ أَوْ

مَجْنُونٌ ﴿٥٢﴾

*Na katika (habari za), Adi (ziko alama kadhalika). (Kumbusha) Tulipowapelekea upepo wa papazi uangamizao. Haukuacha chochote ulichokijia ila ulikifanya kama kamba mbovu. (51:41-42)*

كَذَّبَتْ عَادٌ فَكَيْفَ كَانَ عَذَابِي وَنَذِيرِ ﴿١٨﴾ إِنَّا أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ رِيحًا

صَرَصْرًا فِي يَوْمٍ نَّحْسٍ مُّسْتَمِرٍّ ﴿١٩﴾ تَنزِيلُ النَّاسِ كَأَنَّهُمْ أُعْجَازٌ نَّخْلٍ

مُنْقَعِرٍ ﴿٢٠﴾ فَكَيْفَ كَانَ عَذَابِي وَنَذِيرِ ﴿٢١﴾

*Walikadhibisha kina Adi (nao); basi ilikuwaje adhabu Yangu na maonyo Yangu! Hakika tuliwapelekea upepo mkali katika siku ya nuhsi iendeleayo (kwao mpaka leo). Ukiwang'oa watu (katika ardhi kisha unawabwata chini, wamelala, wamekufa) kana kwamba ni magogo ya mitende iliyong'olewa. Basi ilikuwaje adhabu Yangu na maonyo Yangu! (54:18-21).*

وَلِلَّهِ جُنُودُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿٧﴾

*Na majeshi ya mbingu na ardhi ni ya Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu; Mwenye hikima. (48:7)*

## **Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Hud(a.s)**

- (i) Tuanze kulingania kwa kuonesha upweke wa Allah(s.w) na lengo la binaadamu hapa ulimwenguni.
- (ii) Kutomchelea yeyote katika kufanyakazi ya kulingania Uislamu na kuusimamisha katika jamii.
- (iii) Katika kufanyakazi ya kuhuisha Uislamu katika jamii tutarajie malipo kutoka kwa Allah(s.w) peke yake.
- (iv) Katika kufanya kazi ya kulingania na kusimamisha Uislamu katika jamii tumtegemee Allah(s.w) peke yake.
- (v) Waislamu wakijizatiti ipasavyo, watawashinda makafiri. Pamoja na nguvu kubwa walizonazo.

## **SALIH(A.S)**

Nabii Salih(a.s) alifuatia baada ya Hud(a.s) na alitumwa kwa watu wa kabila (Taifa) la Thamud. Makazi yao yalikuwa kaskazini mwa Arabia sehemu iliyojulikana kama al-Hijr Mada'in Salih.

Thamud waliongoza katika teknolojia ya kuchonga majabali na kuyafanya majumba ya fahari kama tunavyofahamishwa katika Qur-an:

وَأَذْكُرُوا إِذْ جَعَلْنَاكُمْ خُلَفَاءَ مِنْ بَعْدِ عَادٍ وَبَوَّأْنَاكُمْ  
فِي الْأَرْضِ تَتَّخِذُونَ مِنْ سُهولِهَا قُصُورًا وَتَنْحِتُونَ الْجِبَالَ بُيُوتًا.....

*“Na kumbukeni (Allah) alivyokufanyeni makhalifa baada ya ‘Ad na kukuwekeni vizuri katika ardhi; mnajenga majumba makubwa ya kifalme katika nyanda zake, na mnachonga majumba katika majabali (yake).....” (7:74)*

Baada ya muda kupita Thamud nao waliacha mafundisho ya Mtume Hud(a.s) kama walivyofanya akina ‘Ad hapo zamani, wakawa wanaabudia masanamu na kufisidi katika ardhi. Ndipo Allah(s.w) akamtuma Nabii Salih(a.s) kulingania Uislamu kwa wakazi wa Hijr.

## Ujumbe wa Nabii Salih(a.s) kwa Watu Wake

Nabii Salih(a.s) aliwalingania watu wa kaumu yake, wamwamini Allah(s.w) na kumuabudu ipasavyo, watubie na waombe msamaha kwa dhambi zao:

﴿وَالَّذِينَ تَمْوَدَّ أَوْلِيَاءَهُمْ صَالِحًا قَالَ يَتَقَوْمَ أَعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِنْ إِلَهٍ غَيْرُهُ ۗ هُوَ أَنْشَأَكُمْ مِنَ الْأَرْضِ وَاسْتَعْمَرَكُمْ فِيهَا فَاسْتَغْفِرْ لَهُمْ ثُمَّ تَوْبُوا إِلَيْهِ إِنَّ رَبِّي قَرِيبٌ مُجِيبٌ ﴿١١﴾﴾

“Na kwa Thamud tukampelekea ndugu yao, Salih, akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Allah; nyinyi hamna Mungu ila yeye. Yeye ndiye aliyekuumbeni katika ardhi, na akakukalisheni humo. Basi muombeni msamaha, kisha mrejee kwake. Hakika Mola wangu ni karibu (na waja wake) anapokea (maombi yao).” (11:61)

Nabii Salih aliendelea kuwalingania

﴿فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا ۗ وَلَا تُطِيعُوا أَمْرَ الْمُسْرِفِينَ ﴿١٥١﴾﴾ الَّذِينَ يُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ وَلَا يُصْلِحُونَ ﴿١٥٢﴾﴾

“Mcheni Mwenyezi Mungu na nitiini.” “Wala msitii amri za wale maasi, (wenye kupindukia mipaka ya Mungu).” “Ambao wanafanya uharibifu tu katika ardhi wala hawaitengenezi.” (26:150-152)

## Mbinu za Mtume Salih(a.s) Katika Kulingania Uislamu

Kama Mitume waliotangulia, Nabii Salih(a.s) naye kwa kuzingatia mazingira ya watu wake, alitumia mbinu zifuatazo katika kuulingania Uislamu:

**Kwanza**, alijieleza kwa uwazi kuwa yeye ni Mtume wa Allah(s.w)

﴿إِنِّي لَكُمْ رَسُولٌ أَمِينٌ ﴿١٤٣﴾﴾

“Bila shaka mimi kwenu ni Mtume mwaminifu.” (26:143)

**Pili**, aliwakumbusha watu wake neema za Allah(s.w) zilizo juu yao ili waone umuhimu wa kumshukuru na kumuabudu ipasavyo:

وَأَذْكُرُوا إِذْ جَعَلْنَاكُمْ خَلْفَاءَ مَنْ بَعْدَ عَادٍ وَبَوَّأَكُمْ فِي الْأَرْضِ تَتَّخِذُونَ مِنْ سُهُولِهَا قُصُورًا وَتَنْجِتُونَ الْجِبَالَ بُيُوتًا فَادْكُرُوا آيَاتِ اللَّهِ وَلَا تَعْتُوا فِي الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ﴿٧٤﴾

“Na kumbukeni (Mwenyezi Mungu) alivyokufanyeni makhalifa baada ya ‘Ad na kukuwekeni vizuri katika ardhi mnajenga majumba makubwa ya kifalme katika nyanda zake, na mnachonga majumba katika majabali (yake). Basi zikumbukeni neema za Mwenyezi Mungu, wala msifisidi katika ardhi kwa kufanya uharibifu.” (7:74)

أَثَرٌ كُونَ فِي مَا هَاهُنَا آمِنِينَ ﴿١٤٦﴾ فِي جَنَّتٍ وَعَيْونٍ ﴿١٤٧﴾ وَرُوعٍ وَنَخْلٍ طَلَعَهَا هَظِيمٌ ﴿١٤٨﴾ وَتَنْجِتُونَ مِنَ الْجِبَالِ بُيُوتًا فَدَرِهِينَ ﴿١٤٩﴾

“Je (mnafikiri kuwa) mtaachwa salama katika haya yaliyopo hapa (kwenu):” “Katika mabustani na chemchem, (mito).” “Na mimea na mitende yenye makole mazuri.” “Na mnachonga milimani majumba mkistarehe tu basi.” (26:146-149)

**Tatu**, aliwanasihi na kuwasisitiza watu wake wamche Allah(s.w) na kumtii yeye badala ya kuwatii watu:

فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا ۖ وَلَا تُطِيعُوا أَمْرَ الْمُسْرِفِينَ ﴿١٥١﴾ الَّذِينَ يُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ وَلَا يُصْلِحُونَ ﴿١٥٢﴾

“Mcheni Allah na mtiini. Wala msitii amri za wale maasi (wenye kupindukia mipaka ya Allah). Ambao wanafanya uharibifu tu katika ardhi wala hawaitengenezi.” (26:150-152)

**Nne**, alisisitiza kutohitajia ujira kwa watu wake, kama walivyozoea kutoa ujira kwa viongozi wao kwa ajili ya manufaa na starehe zao binafsi.

﴿١٤٥﴾ وَمَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ إِنْ أَجْرِيَ إِلَّا عَلَى رَبِّ الْعَالَمِينَ

“Wala sikutakini ujira juu yake, ujira wangu hauko ila kwa Mola wa walimwengu wote.” (26:145)

**Tano**, alionyesha muujiza wa jabali kuzaa ngamia jike kama dalili za Utume wake baada ya watu wake kumtaka afanye hivyo kwa uwezo wa Allah(s.w).

قَالَ يَنْقُومَ آرَاءَيْكُمْ إِنْ كُنْتُمْ عَلَىٰ بَيِّنَةٍ مِّن رَّبِّي وَعَآئِنِي مِّنْهُ رَحْمَةً

﴿١١٣﴾ فَمَنْ يَنْصُرُنِي مِنَ اللَّهِ إِنْ عَصَيْتُهُ ۗ فَمَا تَزِيدُونَنِي غَيْرَ تَخْسِيرٍ

Akasema: “Enyi watu wangu! Mnaonaje, kama ninazo dalili zilizo wazi zitokazo kwa Mola wangu (za kunionyesha ukweli wa haya), naye amenipa rehema kutoka kwake, basi ni nani atakayeninusuru kwa Mwenyezi Mungu kama nikimuasi? Basi hamtanizidishia kwa hayo mnayonitakia ila khasara.(11:63)

وَيَنْقُومَ هَٰذِهِ نَاقَةُ اللَّهِ لَكُمْ آيَةٌ فَمَنْ ذَرَاهَا تَأْكُلْ فَيَرَأِضِ اللَّهُ وَلَا

﴿١٤﴾ تَمْسُوهَا بِسُوءٍ فَيَأْخُذْكُمْ عَذَابٌ قَرِيبٌ

Enyi watu wangu! Huyu ngamia wa Mwenyezi Mungu ni Ishara kwenu (mliyoitaka kwangu ili kuonyesha ukweli wa Utume wangu). Basi muacheni ale katika ardhi ya Mwenyezi Mungu; wala msinguse kwa ubaya isije ikakuangamizeni adhabu iliyo karibu (na kukufikieni).” (11:64)

## Wapinzani wa Ujumbe wa Nabii Salih(a.s)

Baada ya Nabii Salih(a.s) kufikisha ujumbe wa Allah(s.w) kwa ufasaha na kwa uwazi, watu wake waligawanyika makundi mawili.

Wachache wao waliamini, wengi katika hao wakiwa dhaifu. Wengi wao wakiongozwa na wakuu wa jamii walikufuru. Makafiri wa Kithamud waliukataa ujumbe wa Nabii Salih(a.s) kwa sababu zifuatazo:

**Kwanza**, Walimuona Salih(a.s) kuwa ni mwongo, kuwa hapana cha kuwepo Allah wala adhabu kutoka kwake.

قَالَ الَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا إِنَّا بِالَّذِي ءَامَنْتُمْ بِهِ كَافِرُونَ ﴿٧٦﴾ فَعَقَرُوا الثَّاقَةَ  
وَعَتَوْا عَنْ أَمْرِ رَبِّهِمْ وَقَالُوا يُبْصَلِحُ أَتَيْنَا بِمَا تَعِدُنَا إِنْ كُنْتَ مِنَ  
الْمُرْسَلِينَ ﴿٧٧﴾

*Wakasema wale waliotakabari “Sisi tunayakataa yale mnayoyaamini. Na wakamtumbua (wakamuua) yule ngamia na wakaasi amri ya Mola wao na wakasema: “Ee Salih! Tuletee unayotuahidi ikiwa wewe ni miongoni mwa Mitume. (7:76-77)*

فَعَقَرُوهَا فَقَالَ تَمَتَّعُوا فِي دَارِكُمْ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ ذَٰلِكَ وَعَدُوٌّ غَيْرٌ مَّكَذُوبٍ ﴿١٥﴾

*Wakamchinja. Basi (Salih) akasema: “Stareheni katika mji wenu huu (muda wa) siku tatu (tu, kisha mtaadhibiwa); hiyo ni ahadi isiyokuwa ya uwongo.” (11:65)*

**Pili**,hawakuwa tayari kuacha miungu ya Babu zao:

قَالُوا يُبْصَلِحُ قَدْ كُنْتَ فِينَا مَرْجُوًّا قَبْلَ هَٰذَا  
أَتْنَهِنَّا أَنْ نَعْبُدَ مَا يَعْبُدُ ءَابَاؤُنَا وَإِنَّا لَفِي شَكٍّ مِّمَّا تَدْعُونَا إِلَيْهِ  
مُرِيبٍ ﴿١٢﴾

*Wakasema: “Ewe Salih! Bila shaka ulikuwa unayetarajiwa (kheri) kwetu kabla ya haya (Sasa umeharibika). Oh! Unatukataza kuabudu waliowaabudu baba zetu? Na hakika sisi tumo katika shaka inayotusugua (katika nyoyo zetu) kwa haya unayotuitia.” (11:62)*

**Tatu**, walimuona Salih(a.s) kama mtu aliyerogwa na wakamdai kuleta muujiza:

قَالُوا إِنَّمَا أَنْتَ مِنَ الْمُسَحَّرِينَ ﴿١٥٣﴾ مَا أَنْتَ إِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُنَا فَأْتِ بِآيَةٍ إِنْ كُنْتَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿١٥٤﴾

*Wakasema “Hakika wewe ni miongoni mwa waliorogwa (wakakosa akili).” “Wewe si chochote ila ni mtu kama sisi; basi lete muujiza ikiwa ni miongoni mwa wasemao kweli.” (26:153-154)*

**Nne**, walidai kuwa Salih(a.s) na wale waliomuamini pamoja naye wameleta nuksi katika nchi kwa kule kuikataa kwao miungu ya masanamu.

قَالُوا أَطَّيَّرْنَا بِكَ وَبِمَنْ مَعَكَ قَالَ طَئِيرٌ كُمْ عِنْدَ اللَّهِ بَلْ أَنْتُمْ قَوْمٌ تُفْتَنُونَ ﴿٤٧﴾

*Wakasema: “Tumepata bahati mbaya, (ukorofi) kwa Sababu yako na kwa Sababu ya wale walio pamoja nawe.” Akasema: “Ukorofi wenu uko kwa Mwenyezi Mungu (kwa ajili ya ubaya wenu;) lakini nyinyi ni watu mnaojaribiwa (na Mwenyezi Mungu kuwa mtafuata au hamfuati).” (27:47)*

## **Vitimbi vya Makafiri Dhidi ya Nabii Salih(a.s) na Waumini**

Makafiri wa Kithamud hawakuishia tu kwenye kuukataa ujumbe wa Nabii Salih(a.s), bali walidhihirisha jeuri yao kwa kumuua ngamia wa muujiza ili waone hiyo adhabu waliyoahidiwa (Rejea Qur-an 7:77). Baada ya kumuua ngamia walipewa siku tatu kama fursa ya mwisho ya kuamini na kutubia makosa yao. Badala ya kutubia kama vile haitoshi kwa kosa walilolifanya, walikula njama za kumuua Nabii Salih na wale walioamini pamoja naye.



وَكَانَ فِي الْمَدِينَةِ تِسْعَةُ رَهْطٍ يُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ وَلَا يُصْلِحُونَ ﴿٤٨﴾  
 قَالُوا تَقَاسَمُوا بِاللَّهِ لَنُبَيِّتَنَّهُ وَأَهْلَهُ ثُمَّ لَنَقُولَنَّ لِوَلِيِّهِ مَا شَهِدْنَا مَهْلِكَ  
 أَهْلِهِ وَإِنَّا لَصٰدِقُونَ ﴿٤٩﴾

*Na walikuwamo mjini watu tisa wakifanya matata (kabisa) katika ardhi (hiyo) wala hawakusuluhisha (jambo ila kuharibu tu). Wakasema: "Apianeni kwa Mwenyezi Mungu (ya kwamba) tutamshambulia usiku yeye (Salih) na watu wake, kisha tutamwambia mrithi wake; Sisi hatukuona maangamio (yake wala) ya watu wake na bila shaka sisi ni wa kweli kwao. (27:48-49)*

وَمَكْرُؤٌ مَّكْرًا وَمَكْرُؤًا مَّكْرًا وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٥٠﴾

*Basi wakapanga vitimbi (vyao); na sisi tukapanga mipango yetu (tukapangua vitimbi vyao) na hali ya kuwa hawana habari. (27:50)*

## Kuangamizwa Makafiri na Kunusuriwa Waumini

Mwisho wa siku ya tatu makafiri waliangamizwa na wakanusurika Salih(a.s) na wale walioamini pamoja naye kama tunavyojifunza katika Qur-an:

فَلَمَّا جَاءَ أَمْرُنَا نَجَّيْنَا صَالِحًا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ بِرَحْمَةٍ مِنَّا وَمِن  
 خِزْيِ يَوْمِئِذٍ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ الْقَوِيُّ الْعَزِيزُ ﴿١١﴾

*Basi ilipofika amri yetu, tukamuokoa Salih na wale walioamini pamoja naye kwa rehema Yetu; na (pia tukawaokoa) katika hizaya ya siku hiyo. Hakika Mola wako ndiye Mwenye nguvu (na) Mwenye kushinda. (11:66)*

وَأَخَذَ الَّذِينَ ظَلَمُوا الصَّيْحَةَ فَأَصْبَحُوا فِي دِئْرِهِمْ جَثِمِينَ ﴿١٧﴾ كَأَن  
 لَّمْ يَغْنَوْا فِيهَا ۗ آلَآءِ إِنَّ تَمُودًا كَفَرُوا رَبَّهُمْ ۗ أَلَا بُعْدًا لِثَمُودَ ﴿١٨﴾

*Na wale waliodhulumu (nafsi zao) uliwaangamiza ukelele (uliopigwa na Malaika); wakapambazukiwa wametulia tu*

(wamekufa) katika majumba yao. Kama kwamba hawakuwamo humo. Sikilizeni. Hakika Thamud walimkufuru Mola wao; basi Thamud wamepotelea mbali. (11:67-68)

فَأَخَذْنَهُمُ الرِّجْفَ فَأَصْبَحُوا فِي دَارِهِمْ جَنِيثِينَ ﴿٧٨﴾ فَتَوَلَّى عَنْهُمْ  
وَقَالَ إِنَّكُمْ لَقَدْ أَبْلَغْتُكُمْ رِسَالَاتِ رَبِّي وَنَصَحْتُ لَكُمْ وَلَكِنْ لَا تُحِبُّونَ

التَّنصِيحِينَ ﴿٧٩﴾

Mtetemeko wa ardhi ukawanyakuwa (roho zao) na wakawa wamekufa humo katika miji yao. Basi (Salih) akawaacha (akenda zake), na huku anasema: “Enyi kaumu yangu! Nilikufikishieni ujumbe wa Mola wangu na nikakunasihini, lakini nyinyi hamwapendi wenye nasaha.” (7:78-79)

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa jeshi la Allah(s.w) lililotumika kuwaangamiza makafiri wa Kithamud ni tetemeko la ardhi lililosababishwa na ukelele wa Malaika. Kumbuka:

وَلِلَّهِ جُنُودُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿٧٩﴾ إِنَّا  
أَرْسَلْنَاكَ شَاهِدًا وَمُبَشِّرًا وَنَذِيرًا ﴿٨٠﴾

“Na majeshi ya mbingu na ardhini ya Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu, mwenye hikima.” (48:7)

## **Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Salih(a.s)**

Mafunzo tuyapatayo hayatofautiani na yale yatokanayo na Historia ya Nabii Hud(a.s).

Mafunzo ya ziada ni kuwa:

- (i) Maendeleo ya sayansi na teknolojiahayana maana yoyote ya amii kama hayatatumiwakwa ajili ya kusimamisha ukhalifa utakaotengeneza mazingira ya kuwepo kwa amani ya kweli.

- (ii) Hivi leo maendeleo ya sayansi na teknolojia imekuwa ndio silaha ya kuendeleza dhuluma na maangamizi ya mamiloni kwa mamiloni ya watu wasio na hatia.
- (iii) Pamoja na maendeleo ya sayansi na teknolojia waliyonayo matwaghuti hivi leo, Waislamu wakijizatiti na kufanya subira watawashinda matwaghuti na kusimamisha ukhalifa kama ilivyokuwa kwa Nabii Hud(a.s) na Salih(a.s) kwa msaada wa Allah(s.w). Rejea Qur-an (8:59-60, 66)

## **IBRAHIIM(A.S)**

Nabii Ibrahiim(a.s) ni Mtume wa Allah(s.w) aliyemfuatia Salih(a.s) katika wale waliotajwa katika Qur-an. Alizaliwa na kulelewa katika mji wa Ur huko Iraq. Baba yake, Azara, alikuwa akichonga masanamu na kuyauza kwa washirikina waliokuwa wakiyaabudu badala ya Allah(s.w). Hivyo ni wazi kuwa Nabii Ibrahiim(a.s) aliletwa kwa jamii iliyozama katika giza la ushirikina.

### **Kuandaliwa kwa Nabii Ibrahiim(a.s)**

Tangu angali mdogo, Nabii Ibrahiim(a.s) aliyakinisha kuwepo kwa Allah(s.w) kwa kuchunguza dalili zilizomzunguka katika maumbile ya mbingu na ardhi. Baada ya kuyakinisha kuwepo kwa Allah(s.w), alichukua azma ya kumtii kwa unyenyekevu katika maisha yake yote kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

إِذْ قَالَ لَهُ رَبُّهُ أَسْلِمْ قَالَ أَسْلَمْتُ لِرَبِّ

الْعَالَمِينَ ﴿١٣١﴾

*“(Kumbukeni habari hii) Mola wake (Ibrahim) alipomwambia “Silimu” (Jisalimishe) akanena: Nimejisalimisha kwa Mola wa walimwengu wote”. (2:131)*

Imani yake ya kweli juu ya Allah(s.w), ilimpelekea kuwa na tabia njema isiyo na mfano wake katika jamii kama tunavyojifunza katika Qur-an:

إِنَّ إِبْرَاهِيمَ كَانَ أُمَّةً قَانِتًا لِلَّهِ حَنِيفًا وَلَمْ يَكُ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٢٠﴾

*Hakika Ibrahim alikuwa Imamu (mfano mzuri wa wema wa kuigwa), mnyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu, mtii kamili, wala hakuwa miongoni mwa washirikina. (16:120)*

شَاكِرًا لِأَنْعُمِهِ أَجْتَبَنَاهُ وَهَدَيْنَاهُ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿١٢١﴾ وَعَاتَيْنَاهُ فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَإِنَّا فِي الْآخِرَةِ لَمِنَ الصَّادِقِينَ ﴿١٢٢﴾

*(Alikuwa) mwenye kuzishukuru neema Zake (Mwenyezi Mungu zilizo juu yake), akamchagua na kumuongoza katika njia iliyonyooka. Na tukampa wema katika dunia; na hakika yeye katika Akhera atakuwa miongoni mwa watu wema (pia). (16:121-122)*

..... إِنَّ إِبْرَاهِيمَ لَأَوَّاهٌ حَلِيمٌ ﴿١٢٤﴾

*“.....Kwa yakini Ibrahim alikuwa mwingi wa kurejea kwa Mwenyezi Mungu na mvumilivu”. (9:114)*

وَأَذْكُرُ فِي الْكِتَابِ إِبْرَاهِيمَ إِنَّهُ كَانَ صِدِّيقًا نَبِيًّا ﴿٤١﴾

*“Na mtaje Ibrahim katika kitabu (hiki) bila shaka yeye alikuwa mkweli sana, Nabii.” (19:41)*

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa Nabi Ibrahim(a.s) alikuwa Hanifa, yaani aliyejipusha na Dini za upotevu na hakuwa mshirikina. Alikuwa mnyenyekevu kwa Allah(s.w) na mtii kamili. Alikuwa mwenye kushukuru neema za Allah(s.w), alikuwa mkweli, mwingi wa kurejea kwa Allah(s.w) na alikuwa mvumilivu. Pia alikuwa mwepesi katika kukirimu wageni kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

وَلَقَدْ جَاءَتْ رُسُلُنَا إِبْرَاهِيمَ بِالْبُشْرَى قَالُوا سَلَامًا قَالَ سَلَامٌ فَمَا لَبِثَ أَنْ جَاءَ بِعِجْلٍ حَنِيذٍ ﴿١٤﴾

“Na wajumbe wetu walimwendea Ibrahim kwa bishara, (njema) wakasema: “Salaam – amani”, akasema (Ibrahim). “Juu yenu pia iwe amani”. Na hakukaa (Ibrahim) ila mara alileta ndama (aliyechomwa vizuri).” (11:69)

## Nabii Ibrahiim(a.s) Kumlingania Uislamu Baba Yake

Baada ya Nabiilbrahiim(a.s) kutoa shahada ya kweli alipomuahidi Mola wake: “Nimejisalimisha kwa Bwana Mlezi wa Walimwengu Wote” alianza kulingania Tawhiid kwa watu wa jamii yake. Kwa hekima aliona aanze kumlingania baba yake, aliyekuwa mchonga masanamu na kiongozi wa lbada ya masanamu. Alianza kumlingania kwa kutumia hoja zenye mashiko katika akili ya mwanaadamu kama ifuatavyo:

إِذْ قَالَ لِأَبِيهِ يَا أَبَتِ لِمَ تَعْبُدُ مَا لَا يَسْمَعُ وَلَا يُبْصِرُ  
وَلَا يُغْنِي عَنْكَ شَيْئًا ﴿٤٢﴾

(Wakumbushe) alipomwambia baba yake: “Ewe baba yangu! Kwa nini unaabudu visivyosikia na visivyoona na visivyofaa chochote?” (19:42)

يَا أَبَتِ إِذِّي قَدْ جَاءَنِي مِنَ الْعِلْمِ مَا لَمْ  
يَأْتِكَ فَاتَّبِعْنِي أَهْدِكَ صِرَاطًا سَوِيًّا ﴿٤٣﴾

“Ewe baba yangu! Kwa yakini imenijia ilimu isiyokujia. Basi nifuate nitakuongoza njia iliyo sawa.(19:43)

يَا أَبَتِ لَا تَعْبُدِ اللَّهَ يَطْنًا إِنَّ اللَّهَ يَطْنُ كَمَا لِلرَّحْمَنِ  
عَصِيًّا ﴿٤٤﴾

Ewe baba yangu! Usimuabudu Shetani, hakika Shetani ni mwenye kumuasi (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa rehema.(19:44)

يَتَّابَتِ إِيَّيْ أَحَافُ أَنْ يَمْسَكَ عَذَابٌ مِّنَ الرَّحْمَنِ فَتَكُونَ لِلشَّيْطَانِ وَلِيًّا ﴿٤٥﴾

*“Ewe baba yangu! Hakika naogopa kukupata adhabu inayotoka kwa Mwingi wa rehema (Mwenyezi Mungu), (ukifanya hivyo) utakuwa mwenziwe shetani.” (19:45)*

Babu yake, badala ya kuyatia akilini aliyofikishiwa na mwanawe, alimkemea, kumtisha na badaye kumfukuzilia mbali nyumbani kwake.

قَالَ أَرَأَيْبُ أَنْتَ عَنْ آلهَتِي يَا إِبْرَاهِيمَ لَئِن لَّمْ تَنْتَهَ لِأَرْجُمَنَّكَ  
وَأَهْجُرْ نِي مَلِيًّا ﴿٤٦﴾

*“Akasema (yule baba yake) “Je! Unaichukia miungu yangu, ewe Ibrahim? Kama huachi (haya unayosema) lazima nitakupiga mawe. Na niondokelee mbali kwa muda mchache (huu).” (19:46)*

Nabii Ibrahim(a.s)hakutetereka na kurudi nyuma alipofukuzwa nyumbani mwa baba yake. Alibakia na msimamo wake wa kulingania Dini ya Allah(s.w) kwa moyo mkunjufu huku akitarajia msaada kutoka kwake Allah(s.w) pekee.

وَأَعْتَزِلْكُمْ وَمَا تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَأَدْعُوا رَبِّي عَسَىٰ أَلَّا أَكُونَ بِدُعَاءِ  
رَبِّي شَقِيًّا ﴿٤٨﴾

*“Na mimi nakuondokeeni (na kujiepusha) na mnayoyaabudu kinyume cha Mwenyezi Mungu. Hakika sitakuwa mwenye kukhibu (kukosa ninalotaka) kwa kumuomba Mola wangu.” (19:48).*

## **Nabii Ibrahiim(a.s) Kuulingania Uislamu kwa Jamii Yake**

Nabii Ibrahim(a.s), baada ya kupingwa mawe na kufukuzwa na baba yake mzazi, hakukata tamaa bali aliamua kuikabili jamii na kuifikishia ujumbe wa Uislamu kwa hekima kwa kutumia hoja madhubuti.

﴿ وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ لِأَبِيهِ عَازِرْ أَتَتَّخِذُ آلِهَةً إِنِّي أَرَأَيْتَكَ وَقَوْمَكَ

فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٧٤﴾

(Na kumbukeni) Ibrahimu alipomwambia baba yake Azara “Unawafanya masanamu kuwa waungu? Hakika ninakuona wewe na watu wako mumo katika upotofu (upotevu) ulio dhahiri.(6:74)

وَكَذَلِكَ نُرِي إِبْرَاهِيمَ مَلَكُوتَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلِيَكُونَ مِنَ

الْمُوقِنِينَ ﴿٧٥﴾

Na namna hivi tulimwonyesha Ibrahimu Ufalme wa mbingu na ardhi (kuwa ni wa Mwenyezi Mungu), na ili awe miongoni mwa wenye yakini.(6:75)

فَلَمَّا جَنَّ عَلَيْهِ اللَّيْلُ رَأَى كَوْكَبًا قَالَ هَذَا رَبِّي فَلَمَّا أَفَلَ قَالَ لَا أُحِبُّ

الْأَفْلِينَ ﴿٧٦﴾

Na usiku ulipomwingilia (Ibrahimu na hali kaka na makafiri) akaona nyota, alinena “(Nyota) hii ni Mola wangu.” Ilipotua (ikapotea), alisema (kuwaambia wale makafiri kama kwamba yu pamoja nao katika Ibada ile): “Sipendi waola wanaopotea (hawawepo ila wakati makhsusi tu).(6:76)

فَلَمَّا رَأَى الْقَمَرَ بَازِعًا قَالَ هَذَا رَبِّي فَلَمَّا أَفَلَ قَالَ لَئِن لَّمْ يَهْدِنِي رَبِّي

لَأَكُونَنَّ مِنَ الْقَوْمِ الضَّالِّينَ ﴿٧٧﴾

Na (usiku wa pili) alipouona mwezi unachomoza alisema: “Huu (mwezi) ndio Mola wangu.” Ulipotua alisema: “Asiponiongoza Mola wangu, bila shaka nitakuwa miongoni mwa watu wapotofu(Na Mola huyu hawezi kuniongoza kwani anakuwa hayupo wakati mwingine).” (6:77).

فَلَمَّا رَأَى الشَّمْسُ بَارِعَةً قَالَ هَذَا رَبِّي هَذَا رَبِّي هَذَا أَكْبَرُ فَلَمَّا أَفَلَتْ قَالَ يُنْقِوْمِ

إِنِّي بَرِيءٌ مِّمَّا تُشْرِكُونَ ﴿٧٨﴾

*Na (siku ya tatu) alipoliona jua linachomoza alisema (kuwaambia): “Hili (jua) ndilo Mola wangu. Huyu Mola mkubwa kabisa.” Lilipotua alisema “Enyi watu wangu! Mimi simo katika hayo mnayoyashirikisha (na Mungu).(6:78)*

إِنِّي وَجَّهْتُ وَجْهِيَ لِلَّذِي فَطَرَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ حَنِيفًا وَمَا

أَنَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿٧٩﴾

*(Mimi) nimeuelekeza uso wangu kwa yule aliyeziumba mbingu na ardhi. Hali ya kuwa nimewacha dini za upotevu. Mimi (ni Mwislamu) si miongoni mwa washirikina.” (6:79)*

Watu wa jamii yake walimshangaa kwa msimamo wake wa kumpwekesha Allah(s.w) na kujadiliana naye kama ifuatavyo:

وَحَاجَّهُ قَوْمُهُ قَالَ أَتُحَدِّثُونَنِي فِي اللَّهِ وَقَدْ هَدَانِي

وَلَا أَخَافُ مَا تُشْرِكُونَ بِهِ إِلَّا أَنْ يَشَاءَ رَبِّي شَيْئًا وَسِعَ رَبِّي كُلَّ

شَيْءٍ عِلْمًا أَفَلَا تَتَذَكَّرُونَ ﴿٨٠﴾

*Na watu wake wakajadiliana naye (kwa kumwambia Unaacha Ibada ya wazee! Utadhurika)! Akasema: “Je, Mnanihoji juu ya Mwenyezi Mungu, mnaowashirikisha naye. Isipokuwa Mola wangu akipenda jambo (kuwa, basi litakuwa). Mola wangu anakijua vyema kila kitu. Basi je, hamshiki mauidha (6:80)*

وَكَيْفَ أَخَافُ مَا أَشْرَكْتُمْ وَلَا تَخَافُونَ أَنَّكُمْ أَشْرَكْتُم بِاللَّهِ مَا لَمْ يُنَزِّلْ

بِهِ عَلَيْكُمْ سُلْطَانًا فَأَيُّ الْفَرِيقَيْنِ أَحَقُّ بِالْأَمْنِ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٨١﴾

*“Na nitawaogopaje hao mnaowashirikisha, hali nyinyi hamwogopi kumshirikisha Mwenyezi Mungu na kile ambacho*



*hakukiteremshia dalili kwenu (yoyote ya kuonyesha kuwa ni mungu)? Basi kundi gani katika mawili haya (langu au lenu) linastahiki zaidi kupata amani? Kama nyinyi mnajua jambo (lijibuni hili).(6:81)*

الَّذِينَ آمَنُوا وَلَمْ يَلْبِسُوا إِيمَانَهُمْ بِظُلْمٍ أُولَٰئِكَ لَهُمُ الْأَمْنُ وَهُمْ

مُهْتَدُونَ ﴿٨١﴾

*“(Hapana shaka kuwa) wale walioamini na hawakuchanganya imani yao na ushirikina kuwa hao ndio watakapata amani, nao ndio walioongoka.(6:82)*

وَتِلْكَ حُجَّتُنَا آتَيْنَاهَا إِبْرَاهِيمَ عَلَىٰ قَوْمِهِ ۖ نَرْفَعُ دَرَجَاتٍ مَّن نَّشَاءُ ۗ إِنَّ

رَبَّكَ حَكِيمٌ عَلِيمٌ ﴿٨٢﴾

*Na hizi ndizo (baadhi ya) hoja zetu tulizompa Ibrahimu juu ya watu wake. Tunamyanyua katika vyeo yule tumtakaye (kwa kuwa anakwenda mwendo tunaoutaka). Hakika Mola wako ndiye Mwenye hikima (na) ndiye ajuaye. (6:83)*

## **Ujumbe wa Nabii Ibrahiim(a.s) kwa Mfalme Namrudh**

Nabiilbrahiim(a.s) hakuishia kulingania Uislamu kwa baba yake na watu wa kawaida tu bali alisonga mbele na kumkabili Mfalme Namrudh kwa mjadala juu ya upweke wa Allah(s.w). Mfalme Namrudh alikuwa akiwanyonya na kuwadhulumu watu kama ilivyo kawaida ya watawala wa kitwaghuti kupitia kanuni na sharia za dini za kishirikina. Namrudh alijipa uungu kama inavyodhihiri katika majadiliano yake na Ibrahiim(a.s):

أَلَمْ نَرِ إِلَىٰ آلِ الَّذِي حَآجَّ إِبْرَاهِيمَ فِي رَبِّهِ أَنْ آتَاهُ اللَّهُ الْمُلْكَ إِذْ قَالَ  
 إِبْرَاهِيمُ رَبِّيَ الَّذِي يُحْيِي وَيُمِيتُ قَالَ أَنَا أَحْيِي وَأُمِيتُ ۗ قَالَ إِبْرَاهِيمُ  
 فَإِنَّ اللَّهَ يَأْتِي بِالشَّمْسِ مِنَ الْمَشْرِقِ فَأْتِ بِهَا مِنَ الْمَغْرِبِ فَبُهِتَ الَّذِي  
 كَفَرَ ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿٢٥٨﴾

*Hukumsikia yule aliyehojiana na Ibrahimu juu ya Mola wake kwa sababu Mwenyezi Mungu alimpa Ufalme? Ibrahimu aliposema: “Mola wangu ni yule ambaye huhuisha na hufisha,” yeye akasema: “Mimi pia nahuisha na kufisha.” Ibrahimu akasema: “Mwenyezi Mungu hulichomozesha jua mashariki, basi wewe lichomozesha magharibi.” Akafedheheka yule aliyekufuru; na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu madhalimu. (2:258)*

## **Ibrahim(a.s) Avunja Masanamu Kuwatanabahisha Washirikina.**

NabiIbrahiim(a.s) alijitahidi kwa kadiri ya uwezo wake, kuwaonesha watu wake kwa hoja madhubuti udhaifu wa masanamu wanayoyaabudu badala ya Allah(s.w),

﴿وَلَقَدْ آتَيْنَا إِبْرَاهِيمَ رُشْدَهُ مِن قَبْلُ وَكُنَّا بِهِ عَالِمِينَ ﴿٥١﴾ إِذْ قَالَ

لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ مَا هَذِهِ التَّمَاثِيلُ الَّتِي أَنْتُمْ لَهَا عَاكِفُونَ ﴿٥٢﴾

*Na hakika tulimpa Ibrahimu uwongofu wake zamani na tulikuwa tukimjua (vizuri). (Wakumbushe alipowaambia watu wake): “Ni nini masanamu haya mnayakalia wakati wote (kuyaabudu)?” (21:51-52)*

قَالُوا وَجَدْنَا آبَاءَنَا لَهَا عِبَادِينَ ﴿٥٣﴾ قَالَ لَقَدْ كُنْتُمْ أَنْتُمْ وَعِبَائُكُمْ

فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٥٤﴾ قَالُوا أَجِئْتَنَا بِالْحَقِّ أَمْ أَنْتَ مِنَ اللَّاعِبِينَ ﴿٥٥﴾

*Wakasema, “Tuliwakuta babu zetu wakiyaabudu, (basi na sisi tunayaabudu). Akasema: “Bila shaka nyinyi na baba zenu mulikuwa katika upotofu (upotevu) ulio dhahiri.” Wakasema: “Je! Umetujia kwa (maneno ya) haki au umo miongoni mwa wachezaji?” (21:53-55)*

قَالَ بَلْ رَبُّكُمْ رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ الَّذِي فَطَرَهُنَّ وَأَنَا عَلَىٰ ذَٰلِكُمْ

مِّنَ الشَّاهِدِينَ ﴿٥٦﴾

Akasema: “(Siyo! Mimi si mchezaji) Bali Mola wenu ni yule Mola wa mbingu na ardhi ambaye ndiye aliyeziumba. Nami ni miongoni mwa wenye kuyashuhudia haya.” (21:56)

وَأَنْزَلُ عَلَيْهِمْ نَبَأَ إِبْرَاهِيمَ ﴿٦٤﴾ إِذْ قَالَ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ مَا تَعْبُدُونَ ﴿٦٥﴾  
 قَالُوا نَعْبُدُ أَصْنَامًا فَنَنْظِلُ لَهَا عَذَابِينَ ﴿٦٦﴾ قَالَ هَلْ يَسْمَعُونَكُمُ إِذْ

تَدْعُونَ ﴿٦٧﴾

Na wasomee habari za (Nabii) Ibrahimu. Alipomwambia baba yake na kaumu yake: “Mnaabudu nini?” Wakasema: “Tunaabudu masanamu, daima tunawaabudu.” Akasema: “Je, yanakusikieni mnapoyaita?” (26:69-72)

أَوْ يَنْفَعُونَكُمُ أَوْ يَضُرُّونَ ﴿٦٧﴾ قَالُوا بَلْ وَجَدْنَا آبَاءَنَا كَذَلِكَ يَفْعَلُونَ

﴿٦٤﴾ قَالَ أَفَرَأَيْتُمْ مَا كُنْتُمْ تَعْبُدُونَ ﴿٦٥﴾ أَنْتُمْ وَأَبَاؤُكُمْ الْأَقْدَمُونَ ﴿٦٦﴾

Au yanakufaeni (mkiyaabudu) au yanakudhuruni (mkiacha kuyaabudu)?” Wakasema: “(Hayafanyi haya) lakini tumewakuta baba zetu wakifanya hivi.” Akasema: “Je, mumewaona hawa mnaowaabudu” “Nyinyi na wazee wenu waliotangulia?” (26:73-76)

فَأِنَّهُمْ عَدُوٌّ لِي إِلَّا رَبَّ الْعَالَمِينَ ﴿٧٧﴾ الَّذِي خَلَقَنِي فَهُوَ يَهْدِينِ ﴿٧٨﴾

وَالَّذِي هُوَ يُطْعِمُنِي وَيَسْقِينِ ﴿٧٩﴾ وَإِذَا مَرِضْتُ فَهُوَ يَشْفِينِ ﴿٨٠﴾ وَالَّذِي

يُمِيتُنِي ثُمَّ يُحْيِينِ ﴿٨١﴾ وَالَّذِي أَطْمَعُ أَنْ يَغْفِرَ لِي خَطِيئَتِي يَوْمَ الدِّينِ ﴿٨٢﴾

Bila shaka hao ni adui zangu (basi nitawadhuru. Mimi simuabudu) ila Mola wa walimwengu wote. Ambaye ameniumba na Yeye ananiongoza. Na ambaye ndiye anayenilisha na kuninyweshwa, (anayenipa chakula na kinywaji). Na ninapougua; Yeye ndiye anayeniponesha. Na ambaye atanifisha kisha atanihuisha. Na ndiye ninayemtumaini kwamba atanisamehe makosa yangu siku ya malipo. (26:77-82)

Alipoona watu wake hawamuelewi, Nabii Ibrahim (a.s) aliazimia kuvunja masanamu yao atakapopata mwanya ili kuwaonesha kwa vitendo udhaifu wa miungu wanayoiabudu. Alipopata fursa ya kuingia Hekaluni, bila ya kuonekana, aliyavunja masanamu yote yaliyokuwemo na kuacha lile kubwa lao.

أَيْفَكَا ءَالِهَةً دُونَ اللَّهِ تُرِيدُونَ ﴿٨٦﴾ فَمَا ظَنُّكُمْ بِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٨٧﴾  
 فَتَنظَرَ نَظْرَةً فِي التُّجُومِ ﴿٨٨﴾ فَقَالَ إِنِّي سَقِيمٌ ﴿٨٩﴾ فَتَوَلَّوْا عَنْهُ مُدْبِرِينَ ﴿٩٠﴾  
 فَرَاغَ إِلَىٰ ءَالِهِتِهِمْ فَقَالَ أَلَا تَأْكُلُونَ ﴿٩١﴾ مَا لَكُمْ لَا تَنْطِقُونَ ﴿٩٢﴾  
 فَرَاغَ عَلَيْهِمْ ضَرْبًا بِالْيَمِينِ ﴿٩٣﴾

“Oh! Kwa uzushi tu, miungu badala ya Mwenyezi Mungu – ndiyo mnayoitaka?” “Basi nini fikira yenu juu ya Mola wa walimwengu wote? (Mnamuona hatoshelezi ndio mnatafuta waungu wengine?)” Kisha akatazama mtazamo (mkubwa) katika nyota (akasema “Nitachukua fursa ya kuwajulisha uwongo wa Dini yao kwa kuwaonyesha kuchomoza kwake hizo nyota wanazoziabudu na kuchwa kwake).” Akasema: “Hakika mimi ni mgonjwa.” Nao wakamuacha, wakampa kisogo (wakenda zao viungani katika mandari zao). Basi alikwenda kwa siri kwa miungu yao akaiambia (kwa stihzai): “Muna nini? Mbona hamli? (Vyakula hivi vya mihanga mlivyowekewa?)” “Mumekuwaje! Hamsemi?” Kisha akawageukia kuwapiga kwa mkono wa kulia, (kwa mwisho wa nguvu zake). (37:86-93)

فَجَعَلَهُمْ جُودًا إِلَّا كَبِيرًا لَهُمْ لَعَلَّهُمْ إِلَيْهِ يَرْجِعُونَ ﴿٥٨﴾

“Basi akayavunja vipande vipande isipokuwa lile kubwa lao (aliliacha) ili wao walirudie.” (21:58)

قَالُوا مَنْ فَعَلَ هَذَا بِآلِهَتِنَا إِنَّهُ لَمِنَ الظَّالِمِينَ ﴿٥٩﴾ قَالُوا سَمِعْنَا فَتَىٰ يَدُورُهُمْ يُقَالُ لَهُٗٓ إِنَّا إِبرَاهِيمُ ﴿٦٠﴾ قَالُوا فَأْتُوا بِهِ عَلَىٰ أَعْيُنِ النَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَشْهَدُونَ ﴿٦١﴾

Watu wa Nabii Ibrahiim(a.s) walipokuta miungu yao imefanywa vile walihamaki.

Wakasema: “Nani aliyeifanya hivi miungu yetu? Hakika huyo yu miongoni mwa madhalimu (wakubwa)”. Wakasema: “Tulimsikia kijana mmoja akiwataja anayeitwa Ibrahimu.” Wakasema: “Basi mleteni mbele ya macho ya watu, wamshuhudie (kwa ubaya wake huo).” (21:59-61)

Makameo ya Ibrahiim(a.s) dhidi ya masanamu hayo, hayakuwa siri. Hivyo walimtumumu kuwa ndiye aliyeifanya kitendo hicho, wakamkamata na kumshitaki hadharani:

قَالُوا ءَأَنْتَ فَعَلْتَ هَذَا بِآلِهَتِنَا يَا إِبرَاهِيمُ ﴿٦٢﴾

“Wakasema: Je! Wewe umeifanya hivi miungu yetu, ee Ibrahim? (21:62)

Kwa kuulizwa swali hili Nabii Ibrahim (a.s) alipata fursa adhimu aliyokuwa akiitafuta:

قَالَ بَلْ فَعَلَهُ كَبِيرُهُمْ هَذَا فَسَأَلُوهُمْ إِنْ كَانُوا يَنْطِقُونَ ﴿٦٣﴾ فَرَجَعُوا إِلَىٰ أَنفُسِهِمْ فَقَالُوا إِنَّكُمْ أَنْتُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٦٤﴾ ثُمَّ نَكَسُوا عَلَىٰ رُءُوسِهِمْ لَقَدْ عَلِمْتُمْ مَا هَٔؤُلَاءِ يَنْطِقُونَ ﴿٦٥﴾

Akasema: “Siyo, bali amefanya (hayo) huyu mkubwa wao, basi (muulizeni na) waulizeni (pia hao waliovonjwa) kama wanaweza kunena!” Basi wakajirudi nafsi zao, (wakafikiri udhalilifu wa waungu hao walio nao, wasioweza kujipigania) na wakasema: “Hakika nyinyi mlikuwa madhalimu (wa nafsi zenu kwenda kuwaabudu wasiokuwa na maana). Kisha wakainamisha vichwa nyao, (wakasema) “Hakika umekwishajua ya kwamba hawasemi (kwanini unatucheza shere?(21:63-65)

قَالَ أَفَتَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَنفَعُكُمْ شَيْئًا وَلَا يَضُرُّكُمْ ﴿١١﴾ أَفِي

لَكُمْ وَلِمَا تَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿١٧﴾

*Akasema: “Je! Mnaabudu badala ya Mwenyezi Mungu (miungu) isiokufaeni chochote (mnapowaabudu) wala kukudhuruni (chochote mnapoacha kuwaabudu)?” Kefule (udhalilifu) yenu na ya hivyo mnavyoviabudu kinyume cha Mwenyezi Mungu. Je! Hamfikiri? (21:66-67)*

## Allah(s.w) Amnusuru Ibrahim (a.s) na Hila za Makafiri

Pamoja na kudhihirikiwa na ukweli wa udhaifu wa miungu wa kisanamu, watu wa Nabiilbrahiim(a.s) hawakusilimu, badala yake wakapitisha hukumu ya kumteketeza kwa moto wakasema:

قَالُوا حَرِّ قُوَّةٍ وَأَنصُرُوا آلَهُتَكُمُ إِن كُنتُمْ فَاعِلِينَ ﴿١٨﴾

*“Mteketezeni kwa moto na muinusuru miungu yenu, ikiwa nyinyi ni watendao jambo.” (21:68)*

Allah(s.w) alimnusuru Mtume wake kwa kuuamrisha moto uwe “baridi na salama” kwa Ibrahim:

قُلْنَا يَنبَرُ كُونِي بَرْدًا وَسَلَامًا عَلَىٰ إِبرَاهِيمَ ﴿١٩﴾

*Tukasema: “Ewe moto! Kuwa baridi na salama juu ya Ibrahimu.” (21:69)*

وَأَرَادُوا بِهِ كَيْدًا فَجَعَلْنَاهُمُ الْأَخْسَرِينَ ﴿٧٥﴾ وَنَجَّيْنَاهُ وَلُوطًا.....

*“Basi walitaka kumfanyia vitimbi (vya kumchoma moto) lakini tukawafanya wao kuwa wadhalilifu. Na Tulimuokoa yeye na Lut..... (21:70-71)*

## Nabii Ibrahiim(a.s) Kuhama Iraq

Nabii Ibrahiim(a.s) pamoja na jitihada zote alizozifanya za kuulingania Uislamu kwa hekima na kwa hoja madhubuti kwa baba yake, Mfalme na jamii kwa ujumla hakupata watu walioamini ila

mkewe Sarah na mpwawe Lut(a.s). Kwa hali hiyo, Nabii Ibrahiim(a.s) baada ya kupata idhini ya Mola wake, alihama nchini mwake, Iraq, na kwenda katika nchi nyingine za Mashariki ya kati ili kulingania Uislamu humo. Alianza kuhamia Shamu (Syria).

﴿فَقَامَ لَهُ لُوطٌ وَقَالَ إِنِّي مُهَاجِرٌ إِلَىٰ رَبِّي إِنَّهُ هُوَ

الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٢٦﴾

*“Basi Lut akamuamini na akasema (Ibrahiim). Hakika mimi nahamia katika (nchi aliyoni mrisha) Mola wangu, bila shaka yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima.” (29:26)*

﴿وَقَالَ إِنِّي ذَاهِبٌ إِلَىٰ رَبِّي سَيَهْدِينِ ﴿٢٧﴾﴾

*Na (Ibrahiim) akasema: Nakwenda. Mola wangu ndiye atakayeniongoza.” (37:99)*

Nabii Ibrahiim(a.s) baada ya kuhama Iraq alizitungukia nchi nyingi za Mashariki ya kati ikiwa ni pamoja na Misri, Palestina, Trans-jordan na Hijaz. Sehemu zote hizi aliweka vituo vya harakati alivyokuwa akivitembelea. Alimuweka mpwa wake, Lut(a.s), katika kituo cha Trans-jordan. Aliporuzukiwa watoto wema aliwaomba, Ismail(a.s) na Is-haq(a.s) aliwaingiza kwenye harakati, na akamfanya Ismail(a.s) mkuu wa kituo Hijaz na Is-haq(a.s) mkuu wa kituo cha Palestina. Allah(s.w) aliwateua viongozi hawa wa vituo vya harakati kuwa Manabii wa sehemu hizo na Mzee Ibrahiim(a.s) akiwa kiongozi wao.

Mji wa Makka katika nchi ya Hijaz alipokuwa akiishi Ismail (a.s), ulifanywa kuwa makao makuu ya harakati za kuhisha Uislamu. Makka ilianza kutumika rasmi kama kituo kikuu cha harakati pale Mzee Ibrahiim (a.s) walipokamilisha kujenga upya Ka’abah na Allah(s.w) kumuamrisha awatangazie watu kuja kuhiji pale kila mwaka.

وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَاهِيمُ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ وَإِسْمَاعِيلُ رَبَّنَا تَقَبَّلْ  
 مِنَّا إِنَّكَ أَنْتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿١٢٧﴾

“Na Ibrahiim alipoinua kuta za nyumba (hii ya Al-Ka’abah) na Ismail (pia) (wakaomba wakasema:) “Ee Mola wetu! Tutakabalie (amali yetu hii ya kujenga huu msikiti). Hakika wewe ndiye Mwenye kusikia na Mwenye kujua.” (2:127)

وَإِذْ بَوَّأْنَا لِإِبْرَاهِيمَ مَكَانَ الْبَيْتِ أَنْ لَا تُشْرِكْ بِي شَيْئًا وَطَهِّرْ بَيْتِيَ  
 لِلطَّائِفِينَ وَالْقَائِمِينَ وَالرُّكَّعِ السُّجُودِ ﴿١٢٦﴾ وَأَذِّنْ فِي النَّاسِ بِالْحَجِّ  
 يَأْتُوكَ رِجَالًا وَعَلَى كُلِّ ضَامِرٍ يَأْتِينَ مِنْ كُلِّ فَجٍّ عَمِيقٍ ﴿١٢٧﴾

Na (kumbuka) tulipomkalisha Ibrahimu mahali penye ile Nyumba (takatifu na tukamwambia): “Usinishirikishe na chochote na isafishe Nyumba yangu kwa ajili ya waizungukao na wanaokaa hapo (kufanya ibada yao) na wanaorukuu na kusujudu, (wanaosali).” Na (tukamwambia) “Utangaze kwa watu habari za Hija, watakujia, (wengine) kwa miguu na (wengine) juu ya kila mnyama aliyekonda (kwa machofu ya njiani) wakija kutoka katika kila njia ya mbali. (22:26-27)

## Ibrahiim(a.s) Aomba Kupata Kizazi Chema

Nabii Ibrahiim na mkewe Sarah walikaa mpaka wakawa wazee bila ya kupata mtoto. Ibrahim(a.s) alinyoosha mikono ya maombi kwa Mola wake, kuomba watoto wema watakao msaidia katika harakati zake za kusimamisha Uislamu katika jamii. Aliomba:

رَبِّ هَبْ لِي مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿١٠٠﴾ فَبَشَّرْنَاهُ بِغُلَامٍ حَلِيمٍ ﴿١٠١﴾

“Ee Mola wangu! Nipe (mtoto awe) miongoni mwa watenda mema.” Ndipo tukampa habari njema ya (kuwa atapata) mtoto mpole. (Basi akapata. Naye ndiye Nabii Ismaili). (37:100-101)



Aliamua kuoa mke wa pili, Hajirah, aliyekuwa mjakazi wa mkewe Sarah. Dua yake ilipokelewa na Hajirah akajifungua mtoto Ismail (a.s) akiwa mtoto wa kwanza wa Ibrahim (a.s). Baadaye pia Allah(s.w) alimruzuku mtoto wa pili, Is-haqa, kutoka kwa Sarah, wote wawili wakiwa wazee vikongwe:

وَبَشَّرْنَاهُ بِإِسْحَاقَ نَبِيًّا مِّنَ الصَّالِحِينَ ﴿١١٢﴾

“Tena tukambashiria (kumzaa) Is-haqa. Nabii, miongoni mwa watu wema (kabisa)” (37:112)

قَالَتْ يَا وَيْلَتَىٰ أَأَلِدُ وَأَنَا عَجُوزٌ وَهَذَا بَعْلِي شَيْخًا

إِن هَذَا لَشَيْءٌ عَجِيبٌ ﴿٧٢﴾ قَالُوا أَتَعْجَبِينَ مِنْ أَمْرِ اللَّهِ رَحِمَتُ

اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ عَلَيْكُمْ أَهْلَ الْبَيْتِ إِنَّهُ حَمِيدٌ مَّجِيدٌ ﴿٧٣﴾

(Mkewe Ibrahiim akastaajabu) akasema: *Ee mimi We! Nitazaa na hali mimi ni mkongwe, na huyu mume wangu ni mzee sana? Hakika hili ni jambo la ajabu.*” Wakasema (wale wajumbe-Malaiika): *Je! Unastaajabu amri ya Allah? Rehema ya Allah na Baraka zake ziko juu yenu, enyi watu wa nyumba hii! Hakika (Allah) ndiye anayestahiki kusifiwa na kutukuzwa.*” (11:72-73).

Nabii Ibrahiim(a.s) aliwalea watoto wake kiharakati na aliwausia kumcha-Allah na kuendeleza harakati mpaka mwisho wa maisha yao.

إِذْ قَالَ لَهُ رَبُّهُ أَسْلِمْ قَالَ أَسْلَمْتُ لِرَبِّ

الْعَلَمِينَ ﴿١٣١﴾ وَوَصَّىٰ بِهَا إِبْرَاهِيمَ بَيْنَهُ وَيَعْقُوبَ يَنْبِيُّ إِنَّ اللَّهَ

اصْطَفَىٰ لَكُمْ الَّذِينَ فَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنْتُمْ مُسْلِمُونَ ﴿١٣٢﴾

(Kumbukeni habari hii) Mola wake alipomwambia: “Nyenyekea;” akanena “Nimenyenyekea kwa Mola wa walimwengu (wote)”. Na Ibrahimu akawausia haya wanawe; na Yaakubu (pia akawausia wanawe): “Enyi wanangu! Hakika

*Mwenyezi Mungu amekuchaguliwa Dini hii; basi msife ila nanyi mmekuwa wanyenyekevu.” (2:131-132)*

## **Kutahiniwa Nabii Ibrahiim(a.s)**

Tumeona katika historia yake kuwa Nabii Ibrahiim(a.s) alipata majaribu mengi katika harakati za kuhuisha Uislamu alipokuwa nchini mwake Iraq. Baba yake alimfukuza nyumbani na jamii nzima ikamtenga na kumuhukumu kuchomwa moto hadharani. Bila shaka alipata madhila ya aina hiyo hiyo alipokuwa amewalingania Uislamu washirikina wa nchi nyingine alimohamia. Kama hiyo haitoshi Allah(s.w) alimuongezea mingine miwili mizito.

**Mtihani wa kwanza**, ni pale alipoamrisha na Mola wake, kujitenga na mkewe Hajira na mtoto wake mchanga, Ismail, na kuwaacha peke yao jangwani karibu na Ka’abah. Nabii Ibrahiim(a.s) alitii amri hii ya Mola wake na kutegemea msaada wake kwa familia yake huku akiomba dua ifuatayo:

رَبَّنَا إِنِّي أَسْكَنْتُ مِنْ ذُرِّيَّتِي بِوَادٍ غَيْرِ ذِي زَرْعٍ عِنْدَ بَيْتِكَ الْمُحَرَّمِ  
رَبَّنَا لِيقِيمُوا الصَّلَاةَ فَاجْعَلْ أَفْعِدَةً مِنَ النَّاسِ نَهْوِي إِلَيْهِمْ وَأَرْزُقْهُمْ مِنْ  
الثَّمَرَاتِ لَعَلَّهُمْ يَشْكُرُونَ ﴿٣٧﴾ رَبَّنَا إِنَّكَ تَعْلَمُ مَا نُخْفِي وَمَا نُعْلِنُ وَمَا  
يَخْفَى عَلَى اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ ﴿٣٨﴾

*“Mola wetu! Hakika mimi nimewaweka (nimewakalisha baadhi kizazi changu (mwanangu Ismaili na mama yake, Hajrah) katika bonde (hili la Makka) lisilokuwa na mimea yoyote; katika nyumba yako takatifu (Al-Kaaba) Mola wetu! Wajaalie wasimamisha Sala. Na ujaalie nyoyo za watu zielekee kwao (wapende kuja kuka hapa ili pawe mji) na uwaruzuku matunda ili wapate kushukuru.” “Mola wetu! Hakika wewe unajua tunayoyaficha na tunayoyadhihirisha. Na hakuna chochote kinachofichikana kwa Mwenyezi Mungu katika ardhi wala katika mbingu.” (14:37-38)*

**Mtihani wa pili** na mzito zaidi ni pale Nabii Ibrahiim(a.s) alipoamrisha na Allah(s.w) kuwa amchinje Ismail, mtoto wake mmoja pekee, aliyekuwa anamtarajia, amsaidie katika harakati za kusimamisha Uislamu. Vile vile katika hili Nabii Ibrahiim hakusita, bali alitii amri ya Mola wake na kulitekeleza kwa moyo mkunjufu. Pia mtoto wake Ismail, alikuwa radhi kwa hili kwa ajili ya kutafuta radhi za Mola wao.

فَلَمَّا بَلَغَ مَعَهُ السَّعَىٰ قَالَ يَدَّبْتُسَ إِتَىٰ أَرَىٰ فِي الْمَتَامِ أَيُّ أَدْبَحَكَ فَانظُرْ

مَاذَا تَرَىٰ قَالَ يَتَابَتِ أَفْعَلُ مَا تُوَمَّرُ سَتَجِدُنِي إِنْ شَاءَ اللَّهُ مِنَ الصَّابِرِينَ ﴿١١٢﴾

“Basi (Ismail) alipofikia (makamu ya) kwenda na kurudi pamoja naye, alimwambia: Ee Mwanangu! Hakika nimeona katika ndoto ya kwamba ninakuchinja. (Na ndoto za Mitume ni wahay). Basi fikiri, waonaje?” Akasema: Ee baba yangu! Fanya unavyoamrisha utanikuta Insha-Allah miongoni mwa wanaosubiri.” (37:102)

فَلَمَّا أَسْلَمَا وَتَلَّاهُ لِلْجَبِينِ ﴿١١٣﴾ وَتَدَيَّنَهُ أَنْ يَأْبِرَهِيمَ

﴿١١٤﴾ قَدْ صَدَّقْتَ الرُّءْيَا إِنَّا كَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿١١٥﴾

Basi wote wawili walipojialimisha (kwa Mwenyezi Mungu), na akamlaza kifudufudi (amchinje). Pale pale tulimwita: “Ewe Ibrahimu.” “Umekwishesadikisha ndoto. (Usimchinje mwanao).” Kwa yakini hivi ndivyo tunavyowalipa watendao mema. (37:103-105)

إِنَّ هَذَا لَهُوَ الْبَلْتُو الْمُبِينُ ﴿١١٦﴾ وَفَدَيْنَهُ بِذَبْحٍ عَظِيمٍ ﴿١١٧﴾

Bila shaka (jambo) hii ni jaribio lililo dhahiri, (mtihani ulio dhahiri). Basi tukamkomboa kwa mnyama wa kuchinjwa mtukufu. (37:106-107)

## Nabii Ibrahiim(a.s) Afanywa Kiongozi wa Harakati za Uislamu Ulimwenguni

﴿ وَإِذِ ابْتَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ رَبُّهُ بِكَلِمَاتٍ فَأَتَمَّهُنَّ قَالَ إِنِّي جَاعِلُكَ لِلنَّاسِ إِمَامًا ۗ ﴾

﴿ قَالَ وَمِنْ ذُرِّيَّتِي قَالَ لَا يَنَالُ عَهْدِي الظَّالِمِينَ ﴾

“Na (kumbukeni habari hii) Mola wake alipomfanyia mtihani (Nabii) Ibrahiim kwa amri nyingi; naye akazitimiza. Akamwambia: ‘Hakika mimi nitakufanya kiongozi wa watu (wote) (Ibrahim akasema): ‘Je, na katika kizazi changu pia?’ Akasema: “(Ndio lakini) ahadi yangu haitawafikia madhalimu.” (2:124)

Katika aya hii tunajifunza kuwa Nabii Ibrahiim(a.s) alipewa uongozi na kuwa mfano wa kuigwa na walimwengu wote baada ya kufaulu mitihani mingi na mizito iliyomthibitisha kwa ulimwengu kuwa alikuwa mnyenyekevu na mtii kamili kwa Allah(s.w).

﴿ إِنَّ إِبْرَاهِيمَ كَانَ أُمَّةً قَانِتًا لِلَّهِ حَنِيفًا وَلَا مِمَّنْ

﴿ يَكُ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴾

“Hakika Ibrahiim alikuwa Imamu (mfano mzuri wa wema wa kuigwa), mnyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu, mtii kamili, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.” (16:120)

Kutokana na dua yake, Mitume wote waliomfuatia wametokana na kizazi chake. Kupitia kwa Is-haqa(a.s) kuna Mitume wote wa bani Israil, kuanzia kwa Israil (Yaquub(a.s)) mwenyewe hadi kwa Nabii Issa(a.s) na kupitia kwa Ismail(a.s) tunaye Mtume Muhammad(s.a.w), ambaye ni Mtume wa mwisho na Mtume wa walimwengu wote kama alivyokuwa babu yake, Ibrahiim(a.s).Katika Qur-an tunahimizwa kufuata mila ya Nabii Ibrahiim:

وَمَنْ يَرْغَبْ عَنْ مِلَّةِ إِبْرَاهِيمَ إِلَّا مَن سَفِهَ نَفْسَهُ وَلَقَدِ اصْطَفَيْنَاهُ فِي  
 الدُّنْيَا وَإِنَّهُ فِي الْآخِرَةِ لَمِنَ الصَّالِحِينَ ﴿١٣٠﴾ إِذْ قَالَ لَهُ رَبُّهُ أَسْلِمْ قَالَ  
 أَسْلَمْتُ لِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٣١﴾

*Na nani atajitenga na mila ya Ibrahimu (akaichukia Dini hii ya Kiislamu) isipokuwa anayeitia nafsi yake katika upumbavu? Na kwa yakini sisi tulimchagua (Ibrahimu) katika dunia; na kwa hakika yeye katika Akhera atakuwa miongoni mwa watu wema (kabisa). (Kumbukeni habari hii) Mola wake alipomwambia: “Nyenyekea:” Akanena “Nimenyenyekea kwa Mola wa walimwengu (wote)”. (2:130-131)*

وَمَنْ أَحْسَنُ دِينًا مِّمَّنْ أَسْلَمَ وَجْهَهُ لِلَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ وَاتَّبَعَ مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ  
 حَنِيفًا وَاتَّخَذَ اللَّهُ إِبْرَاهِيمَ خَلِيلًا ﴿١٣٥﴾

*Na nani aliye bora kwa Dini kuliko yule ambaye ameuwelekeza uso wake kwa Mwenyezi Mungu, naye ni mwema, na anafuata mila ya Ibrahimu (kuwa Muislamu kweli kweli). Na Mwenyezi Mungu amemfanya Ibrahimu kuwa ni kipenzi chake. (4:125)*

Mila ya Ibrahim(a.s) inayosisitizwa hapa si nyingine ila ni kuwa “Mnyenyekevu na mtii kamili” kwa Allah(s.w), kiasi cha mtu kuwa tayari na kwa moyo mkunjufu kumchinja mwanawe aliye mwema na anayempenda na kumtarajia sana. Pia kufuata mila ya Ibrahim ni kuwa tayari kufanya juhudi za kusimamisha Uislamu katika jamii na kutokomeza ushirikina bila ya kujali lolote litakalotokea hata kama ikibidi kugombana na kutengana na jamii nzima.

قَدْ كَانَتْ لَكُمْ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ فِي إِبْرَاهِيمَ وَالَّذِينَ مَعَهُ إِذْ قَالُوا لِقَوْمِهِمْ  
 إِنَّا بُرَّاءُؤُا مِنْكُمْ وَمِمَّا تَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ كَفَرْنَا بِكُمْ وَبَدَا بَيْنَنَا  
 وَبَيْنَكُمْ الْعَدَاوَةُ وَالْبَغْضَاءُ أَبَدًا حَتَّى تُؤْمِنُوا بِاللَّهِ وَحَدَهُ .....

*Hakika nyinyi muna mfano mzuri (wa kuiga) kwa Ibrahimu na wale waliokuwa pamoja naye, walipowambia jamaa zao (makafiri). “kwa yakini sisi tu mbali nanyi, na mbali na hayo mnayoyaabudu kinyume cha Mwenyezi Mungu; tunakukataeni, umekwisha dhihiri uadui na bughudha ya daima baina yetu na nyinyi mpaka mtakapomuamini Mwenyezi Mungu peke yake.....” (60:4)*

Ili kujikurubisha na mila ya Ibrahimu, Allah(s.w) ametuamrisha na kutufundisha kupitia kwa Mtume(s.a.w) kuwa tumuombe (tumswalie) Mtume na kujiombea sisi wenyewe kwa kusema:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ  
وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ، اللَّهُمَّ بَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ  
مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ.

*“Ee Allah! Mrehemu Muhammad na wafuasi wa Muhammad kama ulivyomrehemu Ibrahim na wafuasi wa Ibrahim. Hakika wewe u mtukufu na msifiwa wa haki. Ee Allah! Mbariki Muhammad na wafuasi wa Muhammad kama ulivyombariki Ibrahim na wafuasi wa Ibrahiim. Hakika wewe u mtukufu na msifiwa wa Haki”.*

## **Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Ibrahiim(a.s)**

Tukimchukua Nabii Ibrahimu kama kiongozi wa kuigwa katika harakati za kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii tunajifunza yafuatayo:

- (i) Mwanaharakati hanabudi kujitakasa yenye binafsi na kuwa mnyenyekevu na mtii kamili kwa Allah(s.w) kabla ya kuiendea jamii.
- (ii) Hatunabudi kuanza kulingania familia zetu kabla ya kuiendea jamii-Nabii Ibrahim alianza kumlingania baba yake Azara.

- (iii) Tulinganie Uislamu kwa kutumia hoja madhubuti na mbinu mbali – Qur-an (16:125).
- (iv) Tulinganie Uislamu kwa watu wa kada zote – kwa raia wa kawaida wa mijini na vijijini, wasomi na maofisa katika sekta mbalimbali na viongozi wa jamii katika ngazi mbalimbali kwa kupanga na kutumia fursa zinazojitokeza – Nabii Ibrahim (a.s) alihojiana na mfalme Namrudh.
- (v) Tusimchelee yeyote katika kulingania Uislamu.
- (vi) Tuwe tayari kukabiliana na machungu ya kutengwa na familia na jamii kwa ujumla kwa ajili ya kusimamisha Uislamu.
- (vii) (a) Tuwe – tayari kutoa nafsi zetu, nafsi za wapenzi na wandani wetu kwa ajili ya Allah(s.w) – Qur-an (9:111).  
 (b) Tumpende Allah(s.w) na Mtume wake na kupigania dini yake kuliko tunavyopenda nafsi zetu na jamaa zetu wa karibu. Qur-an (9:23:24), (58:22).
- (viii) Tuwe na vituo vya harakati vya kistratejia na tuwe na viongozi madhubuti katika vituo hivyo.
- (ix) Tufanye harakati za kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii kistratejia.
- (x) Tuwe tayari kuhama makazi yetu tuliyoyazoea, kuhamia maeneo ya kistratejia kwa ajili ya kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii.
- (xi) Tuandae vizazi vitakavyoturithi katika harakati – Nabii Ibrahim(a.s)aliomba watoto wema watakaomrithi katika harakati.
- (xii) Tuzihusishe familia zetu katika harakati – Bi Hajarrah aliridhia kubaki mwenyewe Makka na kitoto chake kichanga kwa ajili ya kutii amri ya Allah(s.w).

- (xiii) Tuwahusishe jamaa zetu wa karibu katika harakati – Nabii Ibrahim(a.s) alihama kutoka Iraq na mpwa wake Lut (a.s) na kumfanya kuwa kiongozi wa kituo cha harakati cha Transjordan.
- (xiv) Tuwe wepesi wa kumuelekea Allah(s.w) kwa maombi mbalimbali ya kuomba msaada wa Allah(s.w) na kumshukuru kama alivyokuwa akifanya Nabi Ibrahim(a.s) Qur-an.(37:100-101) (14:39)
- (xv) Tumuombe Allah(s.w) aturehemu na kutubariki kama alivyomrehemu na kumbariki Nabii Ibrahim (a.s) kwa kumswalia Mtume(s.a.w) mara kwa mara kama tukavyo mswalia katika swala.

## **LUT(A.S)**

Mtume Lut(a.s) ni mpwawe Ibrahim(a.s) waliohama pamoja yeye kutokea Iraq. Lut(a.s) alitumwa kuulingania Uislamu katika miji miwili ya Sodoma na Gomora katika nchi ya Transjordan.

### **Tabia ya Watu wa Miji ya Sodoma na Gomora**

Jamii aliyoikuta Mtume Lut(a.s) ilikuwa imeanguka sana kimaadili. Walifikia hali ya kuwa waovu zaidi ya wanyama licha ya kuwa maumbile yao yalikuwa ya binaadamu. Walizama kwenye kufanya maovu matatu mazito kama yanavyotajwa katika Qur-an:

وَلَوْطًا إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ إِنَّكُمْ لَتَأْتُونَ الْفَاحِشَةَ مَا سَبَقَكُمْ بِهَا مِنْ أَحَدٍ مِّنَ

الْعَالَمِينَ ﴿٢٨﴾

*Na (wakumbushe Nabii) Lut; alipowaambia watu wake: “Bila shaka nyinyi mnafanya uovu (ambao) hakuna yoyote aliyekutangulieni kwa (uovu) huo katika walimwengu.(29:28)*



أَيُّكُمْ لَتَأْتُونَ الرِّجَالَ وَتَقْطَعُونَ السَّبِيلَ وَتَأْتُونَ فِي نَادِيكُمُ الْمُنْكَرَ  
فَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهِ إِلَّا أَنْ قَالُوا أَئِتَيْنَا بِعَذَابِ اللَّهِ إِنْ كُنْتَ مِنَ

الصَّادِقِينَ ﴿٢٩﴾

*“Je, mnawaendea wanaume, na mnawakatia njia (watu kwa kuwaua na kuwanyang’anya njiani) na mnafanya maovu katika mikusanyiko yenu?” basi halikuwa jawabu ya watu wake ila kusema: “Tuletee adhabu ya Mwenyezi Mungu ikiwa umiongoni mwa wasema kweli!” (29:29)”*

Katika aya hizi tunafahamishwa kuwa watu wa jamii ya Lut (a.s) walikuwa wakifanya maovu mazito yafuatayo:

- 1) Walikuwa wakiwaendea wanaume wenzao katika kutosheleza matamano yao ya ngono.
- 2) Walikuwa wakifanya uharamia na uporaji wa mali za watu.
- 3) Walikuwa wakifanya maovu haya hadharani na kwa ufahari.

لَعَمْرُكَ إِنَّهُمْ لَفِي سَكْرَتِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿٧٢﴾

*Naapa kwa umri wako! Hakika wao walikuwa katika ulevi wao (wa maovu); wanahangaika ovyo. (15:72)*

Je, jamii yetu hivi leo haifanyi haya na zaidi ya haya tena kwa ufahari. Hivi leo kuna mashindano ya U-miss ambayo wasichana vigoli hujitokeza jukwaani mbele ya hadhara ya watazamaji wanaume kwa wanawake wakiwa wamevaa viguo visivyoo sitiri mwili. Hali ni hiyo hiyo kwenye kumbi za dansi, disko na hata kwenye sherehe za kiserikali. Na wengine wameenda mbele zaidi hata kufikia wanawake kusoma taarifa za habari katika television wakiwa uchi wa mnyama na kufikia wengine kucheza sinema za wanawake na wanaume wakifanya ngono hadharani. Leo hii

baadhi ya nchi za magharibi zimepitisha sheria yakuruhusu ndoa baina ya wanaume kwa wanaume wakifanya ushenzi ule ule wa mabaradhuli wa miji ya Sodom na Gomora.

## Nasaha za Lut(a.s) kwa Watu Wake

Nabii Lut(a.s), kama Mitume wengine walivyofanya aliwanasihi watu wake wamuamini Allah(s.w) na wamche ipasavyo na waogope adhabu yake ambayo ikimfika mtu hapana awezaye kuizuia au kuiondisha.

إِذْ قَالَ لَهُمْ أَخُوهُمْ لُوطُ أَلَا تَتَّقُونَ ﴿١١١﴾ إِيَّايَ لَكُمْ رَسُولٌ أَمِينٌ ﴿١١٢﴾  
فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا

*(Wakumbushe) alipowaambia ndugu yao, (Nabii) Lut: “Je, hamuogopi?” “Bila shaka mimi kwenu ni Mtume muaminifu.” “Basi Mcheni Mwenyezi Mungu na nitiini.(26:161-163)*

وَمَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ إِنْ أَجْرِيَ إِلَّا عَلَى رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١١٤﴾ أَتَأْتُونَ  
الذُّكْرَانَ مِنَ الْعَالَمِينَ ﴿١١٥﴾ وَتَذَرُونَ مَا خَلَقَ لَكُمْ رَبُّكُمْ مِنْ أَزْوَاجِكُمْ  
بَلْ أَنْتُمْ قَوْمٌ عَادُونَ ﴿١١٦﴾

*“Wala sikutakini ujira juu yake; ujira wangu hauko ila kwa (Mwenyezi Mungu) Mola wa walimwengu wote.” “Je, mnawaingilia wanaume katika viumbe (vyake Mwenyezi Mungu)!” “Na mnawacha alichokuumbieni Mola wenu katika wake zenu? Kweli nyinyi ni watu mnaoruka mipaka (mliyowekewa).”(26:164-166)*

وَلُوطًا إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ أَتَأْتُونَ الْفِتْيَانَ وَأَنْتُمْ تَبْصُرُونَ ﴿١١٤﴾ أَيْتَكُمْ  
لَتَأْتُونَ الرِّجَالَ شَهْوَةً مِنْ دُونِ النِّسَاءِ ﴿١١٥﴾ بَلْ أَنْتُمْ قَوْمٌ تَجْهَلُونَ ﴿١١٦﴾

*Na (wakumbushe) Lut alipowambia watu wake: “Je, mnaufanya uchafu, na hali mnaona?” Mnawaingilia wanaume kwa*

*matamaniao mabaya badala ya wanawake? Hakika nyinyi ni watu mfanyao ya ujinga kabisa. (27:54-55)*

Pamoja na nasaha hizi nzuri zilizoambatana na hoja madhubuti, hawakumuamini Lut(a.s) ila watu wachache tu.

﴿٣١﴾ فَمَا وَجَدْنَا فِيهَا غَيْرَ بَيْتٍ مِنَ الْمُسْلِمِينَ

*Lakini hatukupata humo ila nyumba moja tu yenye Waislamu. (51:36)*

## **Jawabu la Makafiri Dhidi ya Nasaha za Nabii Lut(a.s)**

Pamoja na Nabii Lut(a.s) kuwanasihia kwa maneno ya hekima na hoja zilizo wazi, watu wake hawakuwa tayari kabisa kuacha maovu yale.

﴿٧٢﴾ لَعْمَرُكَ إِنَّهُمْ لَفِي سَكْرَتِهِمْ يَعْمَهُونَ

*Naapa kwa umri wako! Hakika wao walikuwa katika ulevi wao (wa maovu); wanahangaika ovyo. (15:72)*

Walishakuwa walevi wa machafu hayo na walipania kumfukuza Nabii Lut na wale walioamini pamoja naye ambao huchukia ubaladhuli huo.

﴿٥٦﴾ فَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهِ إِلَّا أَنْ قَالُوا أَخْرِجُوْهُ أَل لَّوِطٍ مِّن قَرْيَتِكُمْ

﴿٥٦﴾ إِنَّهُمْ أَنَاسٌ يَّتَطَهَّرُونَ

“Basi haikuwa jawabu ya watu wake ila kusema: Wafukuzeni wafuasi wa Lut katika mji wenu, hao ni watu wanaojitakasa, (basi wasikae na sisi wachafu)” (27:56)

﴿١٧٧﴾ قَالُوا لَئِن لَّمْ تَنْتَهَ يَنْلُوطٌ لَّتَكُونَنَّ مِنَ الْمُخْرَجِينَ

“Wakasema: Kama usipoacha, ee Lut (kutukataza haya), bila shaka utakuwa miongoni mwa wanaofukuzwa (katika nchi hii).” (26:167)

## Kuangamizwa kwa Watu wa Lut(a.s)

Watu wa Lut(a.s) walipokataa kabisa kuonyeka kwa nasaha na maonyo ya Nabii Lut(a.s) na badala yake wakazidi kushabikia machafu na kupania kuwafanyia ubaya waumini, Allah(s.w) alipitisha hukumu yake ya kuwanusuru waumini na kuwaangamiza makafiri.

قَالُوا يَلُوطُ إِنَّا رُسُلُ رَبِّكَ لَنْ يَصِلُوا إِلَيْكَ فَأَسْرِبَ أَهْلِكَ بِقِطْعٍ مِّنَ اللَّيْلِ  
وَلَا يَلْتَفِتْ مِنكُمْ أَحَدٌ إِلَّا أَمْرَ أَتَكَ إِنَّهُ مُصِيبُهَا مَا أَصَابَهُمْ إِنَّ مَوْعِدَهُمْ  
الصُّبْحُ أَلَيْسَ الصُّبْحُ بِقَرِيبٍ ﴿٨١﴾

(Wale wajumbe) wakasema: “Ewe Lut! Sisi ni wajumbe wa Mola wako (Malaika). Hawatakufikia (kwa baya lolote). Na ondoka pamoja na watu wako katika sehemu ya pingapinga la usiku. Wala yoyote miongoni mwenu asitazame nyuma. Isipokuwa mke wako (mwanamke mbaya huyo hatakufuata). Naye utampata msiba utakaowapata hao. Hakika miadi yao ni asubuhi. Jee, asubuhi si karibu tu? (Basi tuliza moyo wako. Umekwishafika wakatiwao wa kuangamizwa). (11:81)

فَلَمَّا جَاءَ أَمْرُنَا جَعَلْنَا عَالِيَهَا سَافِلَهَا وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهَا حِجَابًا مِّن

سَجِيلٍ مِّنْ سُودٍ ﴿٨٢﴾

Basi ilipofika amri yetu, tulifanya (ardhi hiyo iwe juu chini); juu yake kuwa chini yake, na tukawateremshia mvua ya changarawe za udongo mgumu (wa motoni uliyokamatana). (11:82)

مُسَوَّمَةً عِنْدَ رَبِّكَ وَمَا هِيَ مِنَ الظَّالِمِينَ بِبَعِيدٍ ﴿٨٣﴾

(Changarawe) zilizotiwa alama kwa Mola wako (kila moja kuwa ya mtu fulani). Na (adhabu) hii haiko mbali na madhalimu (wengine kama hawa watu wa umma huu wanaofanya machafu haya). (11:83)

Jeshi la Allah lililotumika kuwaangamiza watu wa Lut(a.s) ni mvua ya changarawe kutokea motoni na kisha ardhi ikapinduliwa juu – chini.

وَلِلَّهِ جُنُودُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿٧﴾

*Na majeshi ya mbingu na ardhi ni ya Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima. (48:7)*

## **Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Lut (a.s)**

Kutokana na historia ya Nabii Lut(a.s) tunajifunza yafuatayo:

- (i) Tujitahidi kwa kadiri ya uwezo wetu kuondoa maovu katika jamii kwa mikono yetu na ikiwa hatuwezi tuyakemee kama alivyofanya Nabii Lut(a.s) na waumini aliokuwa nao.
- (ii) Tusichelee watu katika kukemea maovu.
- (iii) Kila mtu atahesabiwa na kulipwa kulingana na amali zake. Hatafaidika mtu kwa amali njema za mwingine na wala hataadhibiwa mtu kwa matendo mabaya ya mwingine.
- (iv) Tumuogope Allah(s.w), kwani adhabu yake ni kali na hakuna awezaye kujinusuru nayo inapokuja.
- (v) Tujitahidi kusimamaisha Uislamu kwa mali na nafsi zetu bila ya kumchelea yeyote.
- (vi) Hatma ya mapambano dhidi ya makafiri ni Waislamu kuibuka washindi.

## **ISMAIL(A.S)**

Ismail(a.s) ni mtoto wa kwanza wa Mtume Ibrahim(a.s.). Alizaliwa wakati uzee umekwishamfikia Ibrahim(a.s). Kama Qur'an inavyobainisha, katika umri huo wa uzeeni, MtumeIbrahiim(a.s)

alimuomba Mola wake ampe mtoto mwema atakaendeleza harakati za Kiislamu.

رَبِّ هَبْ لِي مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿١٠٠﴾ فَبَشَّرْنَاهُ بِغُلَامٍ حَلِيمٍ ﴿١٠١﴾

*“Ee Mola wangu! Nipe (mtoto awe) miongoni mwa watenda mema.” Ndipo tukampa habari njema ya (kuwa atapata) mtoto mpole. (Basi akapata. Naye ndiye Nabii Ismail).” (37:100-101).*

Mtume Ibrahim(a.s.) aliletewa mitihani migumu miwili juu ya mtoto huyu. Mosi ni kule kuamriwa kumwacha yeye pamoja na mama yake katika bonde kavu lisilo na watu wala maji. Hilo lilikuwa bonde la Makka. Maji ya kisima zamzam yaliyo katika Msikiti wa Makka, aliyabubujisha Allah(s.w) kwa ajili ya Ismail na mama yake. Chem-chem hiyo imedumu hadi leo. Aidha, vilima vya **Safa** na **Marwa** vimepata umaarufu na kuwa miongoni mwa alama muhimu katika Uislamu, kutokana na kitendo cha mama yake Ismail **Hajirah**, kukimbia baina ya vilima hivyo katika jitihada za kumtafutia mwanae Ismail maji.

Mtihani mwingine alioukata MtumeIbrahiim(a.s) juu ya Ismail(a.s) ni kule kuamrisha amchinje. Huu haukuwa ni mtihani kwa baba tu, lakini pia mtoto Ismail(a.s). Hebu fikiri ungekuwa katika hali gani, kama ungekuwa mahali pa Ismail(a.s). Baba yako anakwambia ameamrisha na Allah(s.w.) akuchinje! Hakika ni mtihani mgumu ila kwa wale wanaonyenyekea kikweli kweli kwa Muumba wao.

Qur’an yatufahamisha kuwa Ismail alikuwa mpole na mnyenyekevu kwa Mola wake. Kwa hiyo hakusita kutoa nafsi yake kwa ajili ya Muumba wake. Bali alimhimiza baba yake amchinje kama Allah(s.w) alivyomuamrisha.

فَلَمَّا بَلَغَ مَعَهُ السَّعْيَ قَالَ يَدَّبُّنِي إِنِّي أَرَىٰ فِي الْمَنَامِ أَنِّي أَذْبَحُكَ فَانظُرْ

مَاذَا تَرَىٰ قَالَ يَتَأَبَّتْ أَعْلَىٰ مَا تَوَمَّرُ سَتَجِدُنِي إِنْ شَاءَ اللَّهُ مِنَ الصَّابِرِينَ ﴿١٠٢﴾

*Basi alipofikia (makamu ya) kwenda na kurudi pamoja naye akamwambia: “Ee mwanangu! Hakika nimeona katika ndoto ya kwamba ninakuchinja. (Na ndoto ya Mitume ni Wahayi). Basi fikiriri, waonaje?” Akasema: “Ee baba yangu! Fanya unayoamrish wa, utanikuta Inshallah miongoni mwa wanaosubiri”. (37:102).*

Utii na unyenyekevu huu wa Nabii Ismail(a.s) ni kielelezo muhimu kwetu. Kwamba, amri ya Allah(s.w) ni lazima itiiwe kwa gharama yoyote ile ikiwa ni pamoja na roho zetu.

### **Kuinua Kuta za Ka’bah.**

Kama tulivyoona katika maisha ya Mtume Ibrahim(a.s.), Nabii Ismail (a.s.) alishirikiana na baba yake kuinua kuta za Ka’abah ambayo ndiyo nyumba kongwe ya kufanyia Ibada na kituo kikuu cha kwanza cha harakati za Kiislamu duniani.

..... وَعَهْدَنَا إِلَىٰ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ أَن طَهِّرَا بَيْتِيَ لِلطَّائِفِينَ  
وَالْقَائِمِينَ وَالرُّكَّعِ السُّجُودِ ﴿١٢٥﴾

“.....Na tulimwusia Ibrahim na Ismail (tukawaambia): Itakaseni nyumba yangu kwa ajili ya wale wanaoizunguka kwa ajili ya kutufu na wanaokaa hapo na (kwa ajili ya) wanaorukuu na kusujudu hapo pia” (2:125).

وَإِذ يَرْفَعُ إِبْرَاهِيمُ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ وَإِسْمَاعِيلُ رَبَّنَا تَقَبَّلْ  
مِنَّا ۖ إِنَّكَ أَنْتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿١٢٧﴾

“Na (kumbukeni khabari hii) Ibrahim alipoinua kuta za nyumba (hii ya Al-Ka’bah) na Ismail (pia) (wakaomba, wakasema): “Ee Mola wetu! Tutakabalie (amali yetu hii ya kujenga huu msikiti). Hakika wewe ndiwe Mwenye kusikia, na Mwenye kujua”. (2:127).

## Ismail(a.s) na Taifa la Waarabu

Nabii Ismail(a.s) ndiye chimhuko la kabila la Quraysh. Baada ya kuachwa katika bonde la Makka lililokavu, Allah(s.w) alijaalia kupatikana maji na hatimaye watu kuhamia pale. Uhai wa mji ukaanza na kutokana na kizazi cha Ismail(a.s) wakapatikana Waarabu wa Hijaz (Saudi Arabia) ambao hufahamika kwa jina mashuhuri Banu Quraysh. Qur'an imemtaja Ismail(a.s) kuwa alikuwa Mtume mkweli wa ahadi aliyewausia watu wake swala na zakat.

وَأَذْكُرُ فِي الْكِتَابِ إِسْمَاعِيلَ إِنَّهُ كَانَ صَادِقَ الْوَعْدِ وَكَانَ رَسُولًا نَبِيًّا

وَكَانَ يَأْمُرُ أَهْلَهُ بِالصَّلَاةِ وَالزَّكَاةِ وَكَانَ عِنْدَ رَبِّهِ مَرْضِيًّا ﴿٥٥﴾

*“Na mtaje katika kitabu (hiki) Ismail. Bila shaka yeye alikuwa mkweli wa ahadi, na alikuwa Mtume, Nabii. Na alikuwa akiwaamrisha watu wake Sala na Zakat na alikuwa mridhiwa mbele ya Mola wake”. (19:54-55).*

Qur'an hapa haimtaji Ismail kwa wema kwa vile alikuwa mtoto wa Mtume Ibrahim(a.s.), bali kwa vile alikuwa mtumishi wa Allah aliye mkweli, muamrisha mema na mkataza maovu. Nasaba hapa haikutajwa kabisa.

Baada ya Mtumelbrahiim(a.s) na mwanae Ismail kujenga upya Ka'bah na kutangaza Hija, walimwomba Allah(s.w) alete Mtume atokanaye na kizazi chao ambaye ataendeleza harakati za Kiislamu kama walivyofanya wao. Aidha walikiombea kizazi chao kiwe ni cha watu wanyenyekevu:

رَبَّنَا وَأَجْعَلْنَا مُسْلِمِينَ لَكَ وَمِنْ ذُرِّيَّتِنَا أُمَّةً مُسْلِمَةً لَكَ وَأَرِنَا مَنَاسِكَنَا

وَتُبَّ عَلَيْنَا إِنْكَ أَنْتَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿١٢٨﴾

*“Ee, Mola wetu! Utufanye tuwe wanyenyekevu kwako. Na miongoni mwa kizazi chetu (pia ufanye) umma mnyenyekevu*



*kwako. na utuonyeshe njia ya Ibada yetu na utusamehe. Bila shaka Wewe ndiye Mwenye kusamehe na Mwenye kurehemu.(2:128)*

رَبَّنَا وَأَبْعَثْ فِيهِمْ رَسُولًا مِّنْهُمْ يَتْلُوا عَلَيْهِمْ آيَاتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ  
وَالْحِكْمَةَ وَيُزَكِّيهِمْ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٢٩﴾

*“Ee, Mola wetu! Walettee Mtume anayetokana na wao, awasomee Aya zako, na kuwafundisha kitabu (chako) na hikima na awafundishe kujitakasa (na kila mabaya). Hakika Wewe ndiye Mwenye nguvu Mwenye hikima” (2:129).*

Dua hii ilikuwa kabuili. Ilipofika zama za kuletwa Mtume wa mwisho, Allah(s.w.) akamleta kupitia kizazi cha Bani Quraysh ambao wanatokana na Ismail(a.s). Ndiye Mtume wetu Muhammad (s.a.w.).

## **Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Ismail(a.s)**

Kutokana na Historia ya Nabii Ismail(a.r) tunajifunza yafuatayo:

- (i) Kila Muislamu anatakiwa kumuomba Allah(s.w) amruzuku mtoto mwema atakayesaidia kupeleka mbele harakati za kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii.
- (ii) Mtoto mwema anayependwa na Allah(s.w) ni yule anayewatii wazazi wake katika mambo ya kheri.
- (iii) Mtoto mwema hujitahidi kushiriki katika harakati za kuusimamisha Uislamu katika jamii.
- (iv) Amri ya pili ya Allah(s.w) inayotukabili baada ya ile ya kusoma(kutafuta elimu) ni kusimamisha swala na kutoa katika vile Allah(s.w) alivyoturuzuku, kisha kuamrisha familia

zetu na jamaa zetu wa karibu kufanya hivyo kisha tuilinganie jamii nzima kufanya hivyo.

- (v) Kusema kweli na kutekeleza ahadi ni katika tabia njema anayoiridhia Allah(s.w).
- (vi) Inatupasa kumuomba Allah(s.w) atupe yaliyo mema katika kila jambo tunalolikusudia kufanya.
- (vii) Kuwa tayari kutoa nafsi zetu kwa ajili ya Allah(s.w)kama alivyokuwa tayari Ismail(a.s) kuchinjwa na baba yake katika kutekeleza amri ya Allah(s.w)

## **IS-HAQ(A.S.) NA YA'AQUUB(A.S.)**

Is-haq(a.s) ni mtoto wa pili wa Nabii Ibrahiim(a.s), mama yake akiwa Sarah. Habari njema ya kumzaa Is-haq ilimjia Nabii Ibrahim(a.s.) mara tu baada ya kufuzu mihani wa kumchinja mwanae mkubwa, Ismail(a.s). Alipongezwa kwa kubashiriwa kuzaliwa kwa Is-haq(a.s.):

سَلَّمَ عَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ ﴿١٠٩﴾ كَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿١١٠﴾ إِنَّهُ مِنْ عِبَادِنَا

الْمُؤْمِنِينَ ﴿١١١﴾ وَبَشَّرْنَاهُ بِإِسْحَاقَ نَبِيًّا مِّنَ الصَّالِحِينَ ﴿١١٢﴾

*Amani kwa Ibrahim. Hivi ndivyo tunavyowalipa watendao mema. Bila shaka yeye alikuwa miongoni mwa waja wetu walioamini (kweli kweli).Tena tukambashiria (kumzaa) Is-haq, Nabii miongoni mwa watu wema (kabisa). (37:109-112).*

Maelezo ya kuzaliwa Is-haq na hatimaye Ya'aquub(a.s.) yanapatikana katika kisa cha Malaika waliompa Nabii Ibrahiimu habari za kuangamizwa watu waovu wa Nabii Lut(a.s) na zile za yeye kupata mtoto katika uzee wake.

وَأَمْرَ أَنَّهُ وَقَائِمَةٌ فَأَضْحَيْتَ فَبَشَّرْنَا بِإِسْحَاقَ وَمِنْ وَرَاءِ إِسْحَاقَ

بِعِثْرُوبٍ ﴿٧١﴾

*Na mkewe (Ibrahim - bibi Sarah) alikuwa kasimama wima, akacheka. Basi tukampa habari njema ya (kuwa watazaa mtoto wamwite) Is-haq na baada ya I'shaq (watapata mjukuu wamwite) Yaaquub. (11:71)*

قَالَتْ يَا وَيْلَتَى أَأَلِدُ وَأَنَا عَجُوزٌ وَهَذَا بَعْلِي شَيْخًا

إِنَّ هَذَا لَشَيْءٌ عَجِيبٌ ﴿٧٢﴾

*(Mkewe Ibrahim) akasema: "Ee mimi we! Nitazaa na hali mimi ni mkongwe, na huyu mume wangu ni mzee sana? Hakika hili ni jambo la ajabu." (11:72)*

قَالُوا أَتَعْجَبِينَ مِنْ أَمْرِ اللَّهِ رَحِمَتُ اللَّهِ وَبَرَكَتُهُ

عَلَيْكُمْ أَهْلَ الْبَيْتِ إِنَّهُ حَمِيدٌ مَجِيدٌ ﴿٧٣﴾

*Wakasema (wale Malaika): Je, unastaajabia amri ya Mwenyezi Mungu? Rehema ya Mwenyezi Mungu na Baraka zake ziko juu yenu, enyi watu wa nyumba hii! Hakika Yeye (Mwenyezi Mungu) ndiye anayestahiki kusifiwa na kutukuzwa." (11:73)*

## Shukurani za Nabii Ibrahim(a.s) kwa Allah(s.w)

Kwa neema hii ya kuruzukiwa watoto wawili - Ismail na Is-haqa(a.s), Nabii Ibrahim(a.s.) alimshukuru Allah(s.w) kwa maneno yafuatayo:

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي وَهَبَ لِي عَلَى الْكِبَرِ إِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ

إِنَّ رَبِّي لَسَمِيعُ الدُّعَاءِ ﴿٣٩﴾

“Namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa juu ya uzee (wangu watoto wawili hawa):- Ismail na Is-haqa. Hakika Mola wangu ni mwenye kusikia maombi (ya waja wake)” (14:39).

Is-haqa alipofikia utu uzima naye alipewa Utume na akaruzukiwa mtoto - Ya'aquub(a.s) naye pia akapewa Utume.

..... وَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ ۗ وَكُلًّا جَعَلْنَا نَبِيًّا ﴿٤٩﴾

﴿٥٠﴾ وَوَهَبْنَا لَهُم مِّن رَّحْمَتِنَا وَجَعَلْنَا لَهُم لِسَانَ صِدْقٍ عَلِيًّا ﴿٥٠﴾

.....Tulimpa Is-haqa na Ya'akub, na kila mmoja tukamfanya Nabii.Na tukawapa rehema zetu na tukawafanyia sifa za kweli tukufu(za kusifiwa na viumbe). (19:49-50).

وَجَعَلْنَاهُمْ أَيْمَةً يَهْتَدُونَ بِأَمْرِنَا وَأَوْحَيْنَا إِلَيْهِمْ فِعْلَ الْخَيْرَاتِ وَإِقَامَ

الصَّلَاةِ وَإِيتَاءَ الزَّكَاةِ وَكَانُوا لَنَا عَبِيدِينَ ﴿٧٣﴾

Na tukawajaalia kuwa maimamu wanaoongoza kwa amri yetu, na tukawapelekea wahyi wa kuzifanya kheri na kusimamisha Sala na kutoa Zaka. Na walikuwa kwetu ni wenye kutunyenyekea. (21:73).

Aya tulizozinukuu zaweka wazi kuwa Is-haqa na mwanawe Ya'aquub, walikuwa Mitume na viongozi wa kusimamia utekelezaji wa sheria za Allah(s.w).

## **Mafunzo Yatokanayo na Historia Nabii Is-haqa na Ya'aquub(a.s)**

- (i) Kutenda mema kunampatia muumini faida kubwa hapa duniani na huko akhera.
- (ii) Tunatakiwa tuwachague kuwa viongozi wetu wa jamii wale waliotuzidi katika matendo mema.
- (iii) Ni wajibu wa Waumini kumshukuru Allah(s.w) baada ya kupata ushindi, kufaulu au kupata mafanikio yoyote yale katika mchakato wa maisha.

## YUSUFU(A.S.)

Mtume Yusufu(a.s) alikuwa mtoto wa Mtume Ya'aquub bin Is-haq bin Ibrahiim. Kwa hiyo Yusufu(a.s) ni kijukuu cha (mjukuu wa mtoto wa) Mtume Ibrahiim(a.s) na mjukuu wa Mtume Is-haqa(a.s.).

Mtume Ya'aquub(a.s) alikuwa na watoto 12. Nabii Yusufu(a.s) alichangia mama na mmoja wa hao. Wengine 10 walikuwa na mama zao.

### Ndoto ya Nabii Yusufu(a.s)

Maisha ya Nabii Yusufu(a.s) yanaanza kusimuliwa ndani ya Qur'an pale alipomwambia babake kuwa:

إِذْ قَالَ يُوسُفُ لِأَبِيهِ يَا أَبَتِ إِنِّي رَأَيْتُ أَحَدَ عَشَرَ كَوْكَبًا  
وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ رَأَيْتُهُمْ لِي سَاجِدِينَ ﴿٤﴾

*Yusufu alipomwambia baba yake "Ewe babaangu! hakika nimeona katika ndoto nyota kumi na moja na jua na mwezi. Nimeviona hivi vikinisujudia(12:4)*

Mtume Ya'aquub, kwa ilimu aliyopewa na Mola wake alifahamu tafsiri ya ndoto ile kwamba inabashiri kuwa Yusufu atakuja kuwa mtu mwenye hadhi kubwa na Mtume. Akamtahadharisha kuwa:

قَالَ يَدْبُنِيَ لَا تَقْضُصْ رُءْيَاكَ عَلَيَّ إِخْوَتِكَ فَيَكِيدُوا لَكَ كَيْدًا إِنَّ  
الشَّيْطَانَ لِلْإِنْسَانِ عَدُوٌّ مُّبِينٌ ﴿٥﴾

*Akasema (baba yake): "Ewe mwanangu! Usiwasimulie ndoto yako (hii) nduguzo wasije wakakufanyia vitimbi (kwa ajili ya husuda). Hakika Shetani kwa mwanadamu ni adui aliye dhahiri.(12:5)*

وَكَذَلِكَ يَجْتَبِيكَ رَبُّكَ وَيُعَلِّمُكَ مِنْ تَأْوِيلِ الْأَحَادِيثِ وَيُنْتِمْ نِعْمَتَهُ  
 عَلَيْكَ وَعَلَىٰ آئَالٍ يَعْتَابُوكَ كَمَا أَتَمَّهَا عَلَىٰ أَبَوَيْكَ مِنْ قَبْلُ إِبْرَاهِيمَ  
 وَإِسْحَاقَ إِنَّ رَبَّكَ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٦﴾

*Namna hivi Mola wako atakuchagua na kukufundisha hakika ya mambo. Na atatimiza neema zake juu yako na juu ya kizazi cha Ya'acquub, kama alivyoitimiza zamani juu ya baba zako Ibrahim na Is-haqa. Bila shaka Mola wako ni Mjuzi na Mwenye hikima: (12:6).*

## Njama za Kumuuua Nabii Yusufu(a.s)

Kwa tabia zake njema Yusufu(a.s) alipendwa sana na baba yake. Ndugu zake Yusufu(a.s) wakajawa chuki na husuda wakijadiliana kuwa;

.....لِيُوسُفُ وَأَخُوهُ أَحَبُّ إِلَيَّ أَيْبَانَا مِمَّا وَنَحْنُ عُصْبَةٌ إِنَّ آبَانَا لَفِي  
 ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٨﴾

.....*Hakika Yusufu na nduguye wanapendwa sana na baba kuliko sisi, hali sisi ni kundi lenye nguvu. Hakika baba yetu yumo katika upotofu ulio wazi. (12:8)*

Wakapanga njama za kumhujumu Yusufu (a.s) kwa kumuua ili mapenzi ya baba yao yawageukie wao. Wakapanga na kuazimia kuwa:

أَقْتُلُوا يُوسُفَ أَوْ اطْرَحُوهُ أَرْضًا يَخْلُلْ لَكُمْ وَجْهَ أَبِيكُمْ وَتَكُونُوا  
 مِنْ بَعْدِهِ قَوْمًا صَالِحِينَ ﴿٩﴾

*Muueni Yusufu au mtupeni nchi za mbali ili uso wa baba yenu ukuelekeeni na baada ya haya mtakuwa watu wema. (12:9)*

Hatimaye wakakubaliana kumtumbukiza kisimani badala kumwua,wazo hili lilitolewa na mmoja wao ambaye angalau aliogopa kubeba dhima ya kufanya dhambi kubwa ya kuiua nafsi pasina haki. Akasema;

قَالَ قَائِلٌ مِّنْهُمْ لَا تَعْتَلُوا يُوسُفَ وَالْقَوْهَ فِي غَيْبَتِ الْجُبِّ  
يَلْتَقِطُهُ بَعْضُ السَّيَّارَةِ إِنْ كُنْتُمْ فَاعِلِينَ ﴿١٢﴾

*Msimuue Yusufu lakini mtupeni Yusufu katika(jiwe la ndani) ya kisima kirefu, watamuokota baadhi ya wasafiri, kama ninyi mnataka kufanya kitu. (12:10)*

### **Kutumbukizwa Yusufu(a.s) Kisimani**

Pamoja na kuwa na dhamira ile mbaya ya kutaka kufanya kosa la kuaa mtu asiyekuwa na hatia , wakaongeza kosa lingine la kusema uwongo. Wakasema:

.....يَتَابَانَا مَا لَكَ لَا تَأْمَنَّا عَلَى يُوسُفَ وَإِنَّا لَهُ لَنَنْصِحُونَ ﴿١١﴾ أَرْسِلْهُ  
مَعَنَا غَدًا يَرْتَعْ وَيَلْعَبُ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ ﴿١٢﴾

*.....Ewe baba yetu, mbona hutuamini juu ya Yusufu, hakika sisi ni wenye kumtakia mema. Mruhusu kesho pamoja nasi atakula kwa furaha na kucheza; hakika sisi tutamlinda (12:11-12)*

Ingawa mzee Ya'aquub(a.s) alionyesha wasiwasi,lakini hatimaye aliwaruhusu waandamane naye. Walimtumbukiza Yusufu(a.s) kisimani kama walivyo dhamiria na wakaichukua kanzu yake na kuipakaza damu za uwongo, kisha wakamuongopea baba yao:

.....يَتَابَانَا إِنَّا ذَهَبْنَا نَسْتَبِقُ وَتَرَكْنَا يُوسُفَ عِنْدَ مَتَاعِنَا فَأَكَلَهُ الذِّئْبُ  
وَمَا أَنْتَ بِمُؤْمِنٍ لَّنَا وَلَوْ كُنَّا صَادِقِينَ ﴿١٧﴾

*Ewe baba yetu! Hakika sisi tulikwenda kushindana mbio na tukamuacha Yusufu penye vyombo vyetu, basi mbwa mwitu akamla; lakini hutatuamini ingawa tunasema kweli (12:17)*

Ya'aquub(a.s.) alikuwa na mategemeo makubwa ya kupata mrithi bora atakayeendeleza kazi yake. Hata hivyo hatumwoni mzee Ya'aquub akikata tamaa kwa kufadhaika au kukufuru. Yeye akawajibu;

..... بَلْ سَوَّلَتْ لَكُمْ أَنْفُسُكُمْ أَهَ فَصَبِرْ جَمِيلًا وَاللَّهُ الْمُسْتَعَانُ

عَلَى مَا تَصِفُونَ ﴿١٨﴾

“.....Nafsi zenu zimekushawishini jambo. Basi (langu mimi ni) subira njema; na Mwenyezi Mungu ndiye aombwaye msaada kwa haya mnayomasema” (12:18).

Hii ndio tabia ya Muislamu. Kurejea na kumtegemea zaidi Allah(s.w) afikwapo na msiba.

### Yusufu Aokotwa na Kuuzwa nchini Misri

Huko nyuma wapita njia walikisogelea kisima kwa lengo la kuteka maji. Mmoja wao katika harakati za kuteka maji, alimuibua mtoto akaruka kwa mshangao:

..... قَالَ يَبْشُرِي هَذَا غُلَامٌ .....

.....Akasema: Ee, furaha njema! Huyu hapa kijana mwanaume..... (12:19)

Walimchukua hadi Misri na kumuuzwa kwa Al-Aziz au Waziri,

وَشَرَوْهُ بِثَمَنٍ بَخْسٍ دَرَاهِمَ مَعْدُودَةٍ وَكَانُوا فِيهِ مِنَ الزَّاهِدِينَ ﴿٢٠﴾

Wakamuuzwa kwa thamani chache ya pesa za kuhesabika, na hawakuwa na haja naye (12:20)

### Yusufu(a.s) Apewa Utume na Kukumbana na Mtihani

Alipofikia umri wa utu uzima alipewa hukumu na elimu. Yaani akapewa Utume. Qur'an inasema:-



وَلَمَّا بَلَغَ أَشُدَّهُ عَاتَيْنَاهُ حُكْمًا وَعِلْمًا وَكَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿٢٢﴾

“Na (Yusuf) alipobaleghe, tulimpa hukumu na ilimu. Na namna hivi tunawalipa wanaotenda mema” (12:22).

Katika kipindi hiki cha utu uzima mke wa Waziri alifanya vitimbi na hata kumshika Yusufu kwa nguvu ili azini naye. Lakini Yusufu alikataa kufanya tendo hilo ovu. Alipoambiwa ‘njoo’, Yusufu akasema:

.....مَعَادَ اللَّهِ إِنَّهُ رَبِّي أَحْسَنَ مَثْوَايَ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الظَّالِمُونَ ﴿٢٣﴾

Najikinga kwa Mwenyezi Mungu. Hakika yeye (mumeo) ni bwana wangu, ametengeneza makazi yangu hapa vizuri. Hakika madhalimu hawatengenekewi(12:23)

Al-Aziz, aliyemnunua Yusufu(a.s) alimwangualia vizuri kama mtoto wake wa kulea. Lakini kwa bahati mbaya, Yusufu(a.s)alipofikia baleghe mkeweAl-Aziz alimtamani na kutaka wazini naye. Yusufu(a.s)alimkatalia kwa hoja kuwa kufanya hivyo ni kumwasi Allah(s.w) na pia itakuwa ni kumfanyia khiyana Al-Aziz, ambaye amemkirimu makazi mazuri pale Misri (Rejea Qur’an 12:23).

Mkewe Al-Aziz hakutaka kusikiliza hoja za Yusufu(a.s),bali alimkazania kuwa lazima akubali kufanya kitendo hicho na akafunga mlango.

وَلَقَدْ هَمَّتْ بِهِ وَهَمَّ بِهَا لَوْلَا أَنْ رَأَى بُرْهَانَ رَبِّهِ كَذَلِكَ لِنَصْرِفَ عَنْهُ

السُّوءَ وَالْفَحْشَاءَ إِنَّهُ مِنْ عِبَادِنَا الْمُخْلَصِينَ ﴿٢٤﴾

“Na (mwanamke huyo) akamkazia nia(ya kutaka kumdhuru vile alivyomkataa) na (Yusufu) akamkazia nia (ya kumpiga; akitaka kumpiga). kama (Yusufu)asingaliona dalili za (kufahamishwa na) Mola wake (kuwa kumpiga huyo mwanamke si uzuri, angelimpiga bali alikimbia tu).Tumefanya namna hivi ili Tumwepushie kila jambo la

ubaya na la uovu(kama huko kuzini). Hakika yeye alikuwa katika waja wetu waliosafishwa.(12:24)

Yusufu(a.s) kwa kukwepa shari ile ilibidi akimbilie mlangoni na yule mwanamke akawa anamkimbiza na kuchana kanzu yake kwa nyuma. Kufika mlangoni wakakutana na Al-Aziz na kesi ikaanzia hapo:

وَأَسْتَبَقَا الْبَابَ وَقَدَّتْ قَمِيصَهُ مِنْ دُبُرٍ وَأَلْفَيَا سَيِّدَهَا لَدَا الْبَابِ قَالَتْ مَا جَزَاءُ مَنْ أَرَادَ بِأَهْلِكَ سُوءًا إِلَّا أَنْ يُسْجَنَ أَوْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٢٥﴾

Na (wote wawili) wakakimbilia mlangoni na mwanamke huyo akairarua kanzu yake kwa nyuma. Na wakamkuta mume wake mlangoni; mwanamke akasema (kumwambia mumewe katika kutia chonza za uwongo): “Hakuna malipo ya mwenye kutaka kufanya ubaya na mkeo isipokuwa kufungwa gerezani au kupewa adhabu inayoumiza”(Anamsingizia uwongo Nabii Yusufu kuwa anamtaka). (12:25)

قَالَ هِيَ رَأَوْتَنِي عَنْ نَفْسِي وَشَهِدَ شَاهِدٌ مِّنْ أَهْلِهَا إِنْ كَانَ قَمِيصُهُ قُدَّ مِنْ قُبُلٍ فَصَدَقَتْ وَهُوَ مِنَ الْكٰذِبِينَ ﴿٢٦﴾ وَإِنْ كَانَ قَمِيصُهُ قُدَّ مِنْ دُبُرٍ فَكَذَبَتْ وَهُوَ مِنَ الصّٰدِقِينَ ﴿٢٧﴾

(Yusufu) akasema: “Huyu (mwanamke) ndiye aliyenitaka bila mimi kumtaka.” Na shahidi aliyekuwa katika jamaa za huyu(mwanamke) akatoa ushahidi(akasema): “Ikiwa kanzu yake imechanwa mbele basi (mwanamke huyu amesema kweli, naye (Yusufu) yu katika waongo. “Na kama kanzu yake imechanwa nyuma, basi (mwanamke huyu) amesema uwongo, naye (Yusufu) yu katika wakweli(12:26-27)

فَلَمَّا رَأَى قَمِيصَهُ قَدَّ مِنْ دُبُرٍ قَالَ إِنَّهُ مِنْ كَيْدِكُنَّ إِنَّ كَيْدَكُنَّ عَظِيمٌ ﴿٢٨﴾  
 يُوسُفُ أَعْرَضَ عَنْ هَذَا وَاسْتَغْفِرِي لِذَنبِكِ إِنَّكِ كُنْتِ مِنَ  
 الْخَاطِئِينَ ﴿٢٩﴾

*“Basi (mumewe)alipoona kanzu yake imechanwa kwa nyuma (alijua kuwa Yusufu ndiye aliyekuwa akitaka kukamatwa kwa nguvu) akasema: “Hakika hii ni katika hila zenu wanawake; bila shaka hila zenu ni kubwa. (Wewe ndiye uliyeeazimia mabaya, unakwenda kumsingizia yeye!) “Yusufu! Yaachilie mbali haya (usiyasimulie nje). Na wewe (mwanamke) omba msamaha kwa dhambi zako . Hakika wewe ni katika wanaofanya makosa. (12:28 - 29)*

Mkewe Al-Aziz badala ya kujuta kwa kosa lake lile na kuleta toba, alishabikia kwa kuwaalika wanawake wengine wa mji waliomlaumu kwa kitendo chake kile kiovu cha kutaka kumbaka mtumishi wake. Aliwaalika ili na wao washuhudie uzuri wa Yusufu na kuwahakikishia kuwa yeye hataacha kumtamani Yusufu (a.s)

﴿ وَقَالَ نِسْوَةٌ فِي الْمَدِينَةِ امْرَأَتُ الْعَزِيزِ تُرَاوِدُ فَتَاهَا عَنْ نَفْسِهِ قَدْ شَغَفَهَا حُبًّا إِنَّا لَنَرَاهَا فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٣٠﴾

*Na wanawake wa mji ule (wakapata habari hii) wakawa wanasema:”Mkewe waziri anamtamani mtumishi wake pasi na kutamaniwa naye. Hakika amemuathiri kwa mapenzi, Bila shaka sisi tunamuona (mke wa waziri) yumo katika upotofu ulio dhahiri. (12:30)*

فَلَمَّا سَمِعَتْ بِمَكْرِهِنَّ أَرْسَلَتْ إِلَيْهِنَّ وَأَعْتَدَتْ لَهُنَّ مُتَّكِنًا وَءَاتَتْ كُلَّ  
وَاحِدَةٍ مِّنْهُنَّ سِكِّينًا وَقَالَتِ اخْرُجْ عَلَيْهِنَّ فَلَمَّا رَأَيْتهُنَّ أَكْبَرْنَهُ وَقَطَّعْنَ  
أَيْدِيَهُنَّ وَقُلْنَ حَاشَ لِلَّهِ مَا هَذَا بَشَرًا إِنْ هَذَا إِلَّا مَلَكٌ كَرِيمٌ ﴿٣١﴾ قَالَتْ  
فَذَلِكُنَّ الَّذِي لُمْتُنَّنِي فِيهِ وَلَقَدْ رَاودنَّهُ عَن نَّفْسِيهِ فَاستَعْصَمَ وَلَئِن لَّمْ  
يَفْعَلْ مَا ءَامُرُهُ لَيَكُونَنَّ مِنَّا مِنَ الصَّغِيرِينَ ﴿٣٢﴾

*Basi (mkewe waziri) aliposikia msemu wao huu aliwaita (waje waone uzuri wa Yusufu wajue kuwa mwenye kurukwa na akili kwa kumpenda Yusufu hana lawama) na akawafanyia karamu na akampa kila mmoja katika wao kisu na akamwambia (Yusufu), “Tokeza mbele yao . “Basi walipomuona waliona ni kitu kikubwa kabisa na wakakata mikono yao(kwa vile visu na wenyewe hawana habari kwa kuwa wameshughulika kumtanzama tu huyo Yusufu) hakuwa huyu ila ni malaika mtukufu. (Mkewe waziri) akasema Huyu ndiye mliyenilaumia; na hakika nilimtamani kinyume cha nafsi yake, lakini akajilinda. Na kama hatafanya ninalomuamrisha, bila shaka (nitamfanyia kila vitimbi mpaka) atafungwa gerezani na atakuwa miongoni mwa madhalili (badala ya hii hishima miongoni mwa madhalili (badala ya hii hishima anayoipata. Kisha wakaingia na wale wanawake nao kuwapeleka wajumbe kumtaka)”(12:31 - 32)*

Lengo la mke wa Al-Aziz lilitimia kwa kuwaonesha wanawake wa mji kuwa haipaswi kulaumiwa kwa kumtamani Yusufu.

Ikumbukwe kuwa huyu alikuwa ni mke wa mtu mkubwa. Hivyo hata wanawake walioitwa walikuwa ni wake wa wakubwa au wenye hadhi katika jamii. Wanawake hawa kudhihirisha

matamano yao, bila ya aibu, ni kielelezo cha kuanguka kwa maadili katika jamii hiyo. Yaonesha ufuska ulikuwa umechanua sana kiasi kwamba aibu haikuwa ni kitu chenye nafasi tena katika maumbile yao.

## Yusufu(a.s) Atupwa Gerezani

Mkewe Al-Aziz hakumkatia tamaa Yusufu(a.s). Uovu wake ulimchochea kuzidi kumuandama Yusufu(a.s). Alimpa Yusufu chaguzi mbili: Ama akubali kuzini naye au amfanyie hila atiwe gerezani.

..... وَلَئِن لَّمْ يَفْعَلْ مَا آمُرُهُ لَيُسْجَنَنَّ وَلَيَكُونًا مِنَ الصَّغِيرِينَ ﴿٣٢﴾

.....*Na kama hatafanya ninalomuarisha, hakika atafungwa gerezani na atakuwa miongoni mwa madhalili(12:32)*

Kwa kumukhofu Allah(s.w) na kuchukia tendo chafu la zinaa, Yusufu akasema

..... قَالَ رَبِّ السِّجْنُ أَحَبُّ إِلَيَّ مِمَّا يَدْعُونَنِي إِلَيْهِ

*Ee Mola wangu! Nastahabu zaidi gereza kuliko haya wanayoniitia.....(12:33)*

## Maisha ya Yusufu(a.s.) Gerezani

Yusufu(a.s) alijikuta yupo gerezani, si kama mhalifu bali aliyeonewa kwa uadilifu na uaminifu wake. Lakini pia hakusononenea kwa dhulma ile aliyofanyiwa kwani kuwepo gerezani kulimtenga na watu waovu waliotaka kumtia kwenye uchafu.

Uadilifu na sifa zake njema zilikuwa zimezagaa kila mahali. Hata alipoingia gerezani wafungwa wenzake walimpa heshima ya pekee. Walikiri kwamba Yusufu(a.s) ni miongoni mwa watu wazuri.

## Yusufu Afikisha Ujumbe wa Uislamu kwa Wafungwa

Ilitokea kule gerezani wafungwa wenzake wakaota ndoto na kumtaka Yusufu(a.s) awape tafsiri yake.

وَدَخَلَ مَعَهُ السِّجْنَ فَتَيَانٍ قَالَ أَحَدُهُمَا إِنِّي أَرَدْتُ أُعْصِرَ خَمْرًا وَقَالَ  
الْآخَرُ إِنِّي أَرَدْتُ أَحْمِلُ فَوْقَ رَأْسِي خُبْرًا تَأْكُلُ الطَّيْرُ مِنْهُ نَبِئْنَا  
بِتَأْوِيلِهِ ۗ إِنَّا نَرَاكَ مِنَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٣٦﴾

*Na wakaingia pamoja naye gerezani vijana wawili. Mmoja wao akasema: Hakika nimeona (katika ndoto) nakamua ulevi”; na mwingine akasema: Hakika nimeona(katika) ndoto nabeba mikate juu ya kichwa changu ambayo ndege wanaila. Tuambie tafsiri yake; kwa yakini sisi tunakuona wewe ni miongoni mwa watu wazuri(12:36)*

Yusufu(a.s) aliwakubalia ombi lao lakini kabla ya kuwatafsiria ndoto zao aliwalingania kwa Allah(s.w) kwakuwauliza:

يَنصَحِي السِّجْنَ ۗ رَبَّابٌ مُتَفَرِّقُونَ خَيْرٌ أَمْ اللَّهُ الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ ﴿٣٩﴾

*“Enyi wafungwa wenzangu wawili! Je, waungu wengi wanaofarikiana ndio bora (kuabudiwa) au Mwenyezi Mungu Mwenye nguvu (juu ya kila kitu?)” (12:39).*

مَا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِهِ ۗ إِلَّا أَسْمَاءُ سَمَّيْتُمُوهَا أَنْتُمْ وَآبَاؤُكُمْ مِمَّا أَوْزَلَ اللَّهُ  
بِهَا مِنْ سُلْطَانٍ ۗ إِنْ الْحُكْمُ إِلَّا لِلَّهِ أَمَرَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ ۗ ذَلِكَ الَّذِي يُقِيمُ  
وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٤٠﴾

*Hamuabudu badala yake (Mwenyezi Mungu) ila majina (matupu) mliyopanga nyinyi wenyewe na baba zenu. Mwenyezi Mungu hakuteremsha dalili kwa hayo. Haikuwa hukumu ila hii ya Mwenyezi Mungu tu; ameamrisha msimuabudu yoyote isipokuwa Yeye tu. Hiyo ndiyo Dini iliyonyooka lakini watu wengi hawajui.” (12:40).*

Baada ya kuwafikishia ujumbe huu muhimu, Nabii Yusufu (a.s) akaanza kuwaeleza taawili ya ndoto zao kuwa:

يَنْصَدِحِبِي السِّجْنَ أَمَا أَحَدُكُمْ مَا فَيَسْقَى رَبَّهُ حَمْرًا وَأَمَا الْآخَرَ فَيُصَلِّبُ  
فَتَأْكُلُ الطَّيْرُ مِنْ رَأْسِهِ فُضِيَ الْأَمْرُ الَّذِي فِيهِ تَسْتَفْتِيَانِ ﴿٤١﴾

*Enyi wafungwa wenzangu wawili! Mmoja katika ninyi atarejeshwa kazini kwake akamnyweshe bwana wake ulevi. na yule mwingine atauawa kwa kusulubiwa, na ndege watamla kichwa chake. Limekwishakatwa (huko kwa Firaun) hili jambo mlilokuwa mkiuliza (12:41)*

Kisha Yusufu(a.s) akamuomba yule atakayetolewa gerezani:

.....أَذْكَرْنِي عِنْدَ رَبِّكَ فَأَنْسَنهُ الشَّيْطَانُ ذُكِّرَ رَبِّيهِ فَلَبِثَ  
فِي السِّجْنِ بِضْعَ سِنِينَ ﴿٤٢﴾

*“.....Unikumbuke mbele ya bwana wako;(umwambie kuwa nimeonewa nimefungwa bure); Lakini shetani alimsahaulisha kumkumbusha bwana wake. kwa hivyo akakaa gerezani (Nabii Yusufu) baadhi ya miaka (baada ya hapa)(12:42)*

## **Kufunguliwa Yusufu(a.s) Kutoka Gerezani**

Yusufu(a.s) alisahauliwa gerezani kwa muda mrefu. Kilichopelekea akumbukwe ni ndoto aliyoota Mfalme. Alipoamka aliwaita makuhani na kuwahadithia:

.....إِنِّي أَرَى سَبْعَ بَقَرَاتٍ سِمَانٍ يَأْكُلُهُنَّ سَبْعٌ عِجَافٌ وَسَبْعَ  
سُنْبُلَاتٍ خُضْرٍ وَأُخَرَ يَابِسَةٍ يَتَأْتِيهَا الْمَلَأُ أَفْتُونِي فِي رُءْيَايَ إِنْ كُنْتُمْ  
لِلرُّءْيَا تَعْبُرُونَ ﴿٤٣﴾

*.....Hakika mimi nimeona ng'ombe Saba wanene wanaliwa na ng'ombe Saba ving'onda. Na nimeona mashuke Saba mabichi na mengine yaliyokauka. Enyi wakubwa nitafsirieni ndoto yangu ikiwa ninyi mnaweza kutafsiri ndoto(12:43)*

قَالُوا أَضَعَتْ أَحْلَمٌ وَمَا نَحْنُ بِتَأْوِيلِ الْأَحْلَمِ بِعَدْلِيمِن ﴿٤٤﴾

*Wakasema: ni ndoto iliyovurugika wala sisi hatujui tafsiri ya ndoto hizi(12:44)*

Yule mfungwa aliyefasiriwa ndoto na Yusufu(a.s) kuwa atatolewa gerezani alimkumbuka Yusufu na akawaambia:

..... أَنَا أَنْبِئُكُمْ بِتَأْوِيلِهِ فَأَرْسِلُونِ ﴿٤٥﴾

.....Mimi nitakwambieni tafsiri yake. basi nitumeni (12:45)

Alipofika gerezani, akamwita:

يُوسُفُ أَيُّهَا الصِّدِّيقُ أَفْتِنَا فِي سَبْعِ بَقَرَاتٍ سِمَانٍ يَأْكُلُهُنَّ سَبْعُ عَجَافٍ  
وَسَبْعِ سُنبُلَاتٍ خُضْرٍ وَأُخَرَ يَابِسَاتٍ لَعَلِّي أَرْجِعُ إِلَى النَّاسِ لَعَلَّهُمْ

يَعْلَمُونَ ﴿٤٦﴾

*Yusufu! Ewe mkweli! Tueleze hakika ya ng'ombe Saba wanene kuliwa na ng'ombe Saba dhaifu. Na mashuke Saba mabichi na mashuke makavu, ili nirejee kwa watu wapate kujua. (12:46)*

قَالَ تَزْرَعُونَ سَبْعَ سِنِينَ دَابًّا فَمَا حَصَدْتُمْ فَذَرُوهُ فِي سُنْبُلِهِ إِلَّا قَلِيلًا

مِمَّا تَأْكُلُونَ ﴿٤٧﴾

*Akasema: Mtalima miaka Saba mfululizo kwa juhudi. Na mtakavyovivuna viacheni katika mashuke yake isipokuwa kidogo mnavyokula.(12:47)*

ثُمَّ يَأْتِي مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ سَبْعٌ شِدَادٌ يَأْكُلْنَ مَا قَدَّمْتُمْ لَهُنَّ إِلَّا قَلِيلًا مِمَّا

تُحْصِنُونَ ﴿٤٨﴾

*Kisha itakuja baadaye miaka Saba ya shida itakayokula vile mlivyolima, isipokuwa kidogo mtakachohifadhi (12:48)*



Walipopata taawili ya ndoto hii, Mfalme kwa furaha kubwa kabisa alisema

..... أَتْتُونِي بِهِ ~ أَسْتَخْلِصُهُ لِنَفْسِي ۗ فَلَمَّا كَلَّمَهُ قَالَ إِنَّكَ الْيَوْمَ

لَدَيْنَا مَكِينٌ ۖ أَمِينٌ ﴿٥٤﴾

*Mleteni kwangu nimchague awe mtu wangu mwenyewe. Basi alipozungunza naye (Mfalme) alisema, Hakika wewe leo kwetu umekwisha kuwa ni mwenye hishima na muaminiwa. (12:54)*

Yusufu alimuagiza mjumbe wa mfalme kuwa kabla hajotoka gerezani lijulikane lile shauri la wanawake waliomtaka kwa nguvu na kumchochea aingie katika maasi - Qur'an (12:50). Yusufu(a.s) alitaka hilo lifanyike ili apate kusafika kwa Al-Aziz na kwa jamii nzima kuwa hakumfanyia dhuluma ile aliyosingiziwa.

Mfalme aliwakusanya wanawake na kuwauliza

..... مَا خَطْبُكُنَّ إِذْ رَاوَدْتُنَّ يُوسُفَ عَنِ نَفْسِهِ ۗ قُلْنَ حَاشَ

لِلَّهِ مَا عَلِمْنَا عَلَيْهِ مِنْ سُوءٍ ۗ قَالَتِ امْرَأَتُ الْعَزِيزِ الْقَنَ حَصْحَصَ

الْحَقُّ أَنَّا رَاوَدْتُهُ عَنِ نَفْسِهِ ۗ وَإِنَّهُ لَمِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٥١﴾

*“.....Nini jambo lenu lilikuwa mlipomtamani Yusufu kinyume cha matamania yake? wakasema ‘Hasha lillahi! Sisi hatukujua ubaya wowote kwake. Mkewe Al-Aziz naye akasema: Sasa haki imedhihirika, mimi ndiye niliyemtamani kinyume cha nafsi yake, na bila shaka yeye yu miongoni mwa wa kweli (kabisa)” (12:51)*

Baada ya hapo ndipo Yusufu(a.s) alipokubali heshima ile aliyopewa na kupendekeza awe msimamizi wa hazina ya nchi.

قَالَ اجْعَلْنِي عَلَى خَزَائِنِ الْأَرْضِ ۗ إِنِّي حَفِيظٌ عَلَيْكُمْ ﴿٥٥﴾

*Akasema nifanye niwe mtazamaji wa hazina ya nchi; hakika mimi ni mlinzi mzuri na mjuzi hodari (12:55)*

Tendo hili la Yusufu(a.s) kudai kesi yake na wanawake iangaliwe na Mfalme na haki itolewe, lilinyanyua sana hadhi yake. **Kwanza** aliifasiri ndoto ngumu ya Mfalme ambayo iliwashinda wachawi, wanganga na watabiri wote wa kutegemewa katika nchi. **Pili** alipotakiwa na Mfalme atoke gerezani, alikataa mpaka kesi ifikishwe mahakamani, mkosaji abainishwe. Matokeo ya kesi yakawa wanawake kukiri mbele ya hadhara ya Mfalme kuwa Yusufu(a.s) hakuwa na hatia bali wao ndio waliokuwa waovu.

Ilidhihiri kwa kila mtu kuwa hakuna yeyote miongoni mwao, ila amezidiwa na Yusufu(a.s) kwa uadilifu na tabia njema kwa ujumla. Haiwi ni kitu cha ajabu basi tunapooni Yusufu anapewa dhamana ya kuangalia hazina yote ya nchi. Huu ni wadhifa unaohitajia mtu aliyepewa kwa uadilifu na hakuwepo aliyemzidi Yusufu(a.s).

### **Yusufu(a.s.) Akutana na Ndugu Zake**

Njaa iliitokea na ikawa hapana sehemu nyingine yoyote yenye chakula ila Misri.Watu wakamiminika Misri kuhemea chakula. Miongoni mwao wakawa ni wale ndugu zake Yusufu(a.s).

وَجَاءَ إِخْوَةُ يُوسُفَ فَدَخَلُوا عَلَيْهِ فَعَرَفَهُمْ وَهُمْ لَهُ مُنْكَرُونَ ﴿٥٨﴾

*Wakaja ndugu zake Yusufu, na wakaingia kwake akawajua(12:58)*

Wakapewa chakula na wakarejeshewa bidhaa zao walizoleta kubadilisha na chakula. Kisha Yusufu (a.s.) akawaagiza:

وَلَمَّا جَهَّزَهُمْ بِجَهَّازِهِمْ قَالَ أَذُنُونِي بِأَخٍ لَّكُم مِّنْ أَبِيكُمْ أَلا تَرَوْنَ أَنِّي

أُوفِي الْكَيْلَ وَأَنَا خَيْرُ الْمُنْزِلِينَ ﴿٥٩﴾

*Na alipowapatia chakula chao alisema. (mkinjia mara ya pili) Nijieni na ndugu yenu wa kwa baba. Je hamuoni ya kwamba mimi ninatimiza kipimo, na ni mbora wa wakaribishao. (12:59)*

فَلَمَّا رَجَعُوا إِلَىٰ أَبِيهِمْ قَالُوا يَا أَبَانَا مُنِعَ مِنَّا الْكَيْلُ فَأَرْسِلْ مَعَنَا آخَانَا

نَكْتَلْ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ ﴿٦٠﴾

*Basi waliporejea kwa baba yao, walisema: “Ewe baba yetu! Tutazuliwa (chakula mara ya pili mpaka twende na ndugu yetu); basi mpeleke ndugu yetu pamoja nasi ili tupate kupimiwa; na yakini sisi tutamlinda.” (12:63).*

Mzee Ya‘aquub(a.s), akasema:-

قَالَ لَنْ أُرْسِلَهُ مَعَكُمْ حَتَّى تُؤْتُونِ مَوْثِقًا مِّنَ اللَّهِ لَتَأْتُنَّنِي بِهِ إِلاَّ أَنْ

يُحَاطَ بِكُمْ فَلَمَّا آتَوْهُ مَوْثِقَهُمْ قَالَ اللَّهُ عَلَىٰ مَا نَقُولُ وَكِيلٌ ﴿١١﴾

*Sitampeleka pamoja nanyi mpaka munipe ahadi kwa jina la Allah kwamba lazima mtamrejsha kwangu, isipokuwa nyote mzungukwe (na hatari au kufa). Basi walipompa ahadi yao alisema: Mwenyezi Mungu ndiye mlinzi juu ya haya tuyasemayo (12:66)*

Baada ya kuchukua ahadi hii, Mzee Ya‘aquub aliwaambia wanawe kuwa wasiingie Misr kwa kutumia mlango mmoja, bali kila mmoja apitie mlango wake katika milango inayoingia humo(rejea Qur’an 12:67).

Kwa kuingia milango tofauti, Yusufu(a.s) alipata fursa ya kukutana na ndugu yake, Bin-Amin (wa kwa baba na mama) kabla ya wale wengine na kujitaambulisha kwake kisha kumfahamisha dhamira yake ya kumbakisha Misr-(rejea Qur’an 12:69)

Yusufu(a.s) alifanya hila ya kumbambikizia wizi ndugu yake kwa kuweka pishi ya kupimia ndani ya mzingo wake. Mara tu ya kuchukua mizigo yao na kuaga, palinadiwa kupotea kwa kipimo cha mfalme. Wote ndugu zake Yusufu(a.s) walikataa kuwa hawakuhusika na wizi wa chombo kile. Ikabidi ipitishwe sachi(search) na kikakutwa kwenye mzigo wa Bin Amin ambaye alihukumiwa kifungo cha mwaka mmoja Misr. (rejea Qur’an 12:70-75).

Ndugu zake Yusufu(a.s) waliporejea nyumbani walimfahamisha mzee wao mkasa uliowapata. Mzee Ya‘aquub(a.s) alizidi kupata

majonzi kwa kupotelewa na watoto wawili, lakini baadae alikuwa na matumaini ya kuwapata wote, ndipo akawaagiza wanawe:

يٰۤاٰتِيۡنَا اٰذْهٰبُوۡا فَتَحَسَّسُوۡا مِّنۡ يُّوسُفَ وَاٰخِيۡهِ وَلَا تَاِيۡسُوۡا مِّنۡ رُّوۡحِ اللّٰهِ

اِنَّهٗ وَاٰتِيۡنَا مِّنۡ رُّوۡحِ اللّٰهِ اِلَّا الْقَوْمُ الْكٰفِرُوۡنَ ﴿٨٧﴾

*Enyi wanangu! Nendeni mkamtafute Yusufu na nduguye, wala msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu. Hawakati tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu isipokuwa watu makafiri (12:87)*

Walipofika Misri walimtaka Yusufu(a.s) awafanyie ihsan kwa kuwapa chakula bure kwa vile hawakuwa na fedha ya kulipa huku wakimkumbusha kuwa Mwenyezi Mungu huwalipa watu wanaowatendea wema mwenzao. Hapo Yusufu(a.s) akawakumbusha:

قَالَ هَلْ عَلِمْتُمْ مَا فَعَلْتُمْ بِيُّوسُفَ وَاٰخِيۡهِ اِذْ اَنْتُمْ جٰهِلُوۡنَ ﴿٨٨﴾

*Akasema: Je! Mnajua mliyomfanyia Yusufu na nduguye mlipokuwa ujingani?(12:89)*

قَالُوۡا اٰءِنَّكَ لَآنْتَ يُّوسُفَ قَالَ اَنَا يُّوسُفُ وَهٰذَا اٰخِيۡ قَدْ مَنَّ اللّٰهُ عَلَيْنَا

اِنَّهٗ مَنۡ يَّتَّقِ وَيَصْبِرْ فَاِنَّ اللّٰهَ لَا يُضِيۡعُ اَجْرَ الْمُحْسِنِيۡنَ ﴿٩٠﴾

*Wakasema: Je! Wewe ndiye Yusufu? Akasema: Mimi ndiye Yusufu, na huyu ni ndugu yangu. Mwenyezi Mungu ametufanyia hisani. Hakika anayemcha Mungu na kusubiri , basi Mwenyezi Mungu hapotezi malipo ya wafanyao mema(12:90)*

Nduguze wakakiri makosa yao waliyomfanyia Yusufu(a.s) na kumuomba awasamehe.

قَالُوۡا تَاللّٰهِ لَقَدْ عٰثَرَكَ اللّٰهُ عَلَيْنَا وَاِنۡ كُنَّا لَخٰطِئِيۡنَ ﴿٩١﴾

*Wakasema: Wallahi! Mwenyezi Mungu amekuchagua juu yetu, na hakika sisi tulikuwa wenye makosa. (12:91)*

## Ndoto ya Nabii Yusufu(a.s) Yatimia

Yusufu(a.s.) aliwasamehe na kuwaagiza waende wakamlete baba yao mzee Yaaqub(a.s.) na wao waje wote na familia zao.

قَالَ لَا تَثْرِبَ عَلَيَّكُمْ الْيَوْمَ يَغْفِرُ اللَّهُ لَكُمْ وَهُوَ أَرْحَمُ

الرَّحِيمِينَ ﴿٩٢﴾

*Akasema: “Hakuna lawama juu yenu leo; Mwenyezi Mungu atakusameheni, naye ni Mwenye rehema zaidi kuliko wanaorehemu. (12:92)*

أَذْهَبُوا بِقَمِيصِي هَذَا فَأَلْفُوهُ عَلَىٰ وَجْهِ أَبِي يَأْتِ

بَصِيرًا وَأَنَا مِنِّي بِأَهْلِكُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٩٣﴾

*Nendeni na kanzu yangu hii na muiweke mbele ya uso wa baba yangu: naye atafunuka macho aone. Na nijieni pamoja na watu wenu wote(12:93)*

Waliporudi nyumbani walichukuzana wote, familia nzima akiwemo baba yao, mzee Ya'aquub(a.s),wakahamia Misri.

فَلَمَّا دَخَلُوا عَلَىٰ يُوسُفَ ءَاوَىٰ إِلَيْهِ أَبْوَتِهِ وَقَالَ ادْخُلُوا مِصْرَ إِن شَاءَ اللَّهُ

ءَامِنِينَ ﴿٩٤﴾

*Na walipoingia kwa Yusufu aliwakumbatia wazazi wake na akasema; “Ingieni Misri, Inshaa-Allah mumo katika amani. (12:99)*

وَرَفَعَ أَبْوَتِهِ عَلَىٰ الْعَرْشِ وَخَرُّوا لَهُ سُجَّدًا وَقَالَ يَأْتِيَتِ هَذَا تَأْوِيلُ

رُءْيَايَ مِنْ قَبْلُ قَدْ جَعَلْنَا لِرَبِّي حَقًّا وَقَدْ أَحْسَنَ بِي إِذْ أَخْرَجَنِي

مِنَ السِّجْنِ وَجَاءَ بِكُمْ مِنَ الْبَدْوِ مِنْ بَعْدِ أَنْ نَزَغَ الشَّيْطَانُ

بَيْنِي وَبَيْنَ إِخْوَتِي إِنَّ رَبِّي لَطِيفٌ لِمَا يَشَاءُ إِنَّهُ هُوَ الْعَلِيمُ الْحَكِيمُ ﴿١٠٠﴾

*Aliwainua wazazi wake na kuwaweka katika kiti cha Ufalme. Na wote wakaporomoka kumsujudia. Na Yusufu akasema: “Ewe babangu! Hii ndiyo hakika ya ndoto yangu ya zamani. Hakika Mola wangu ameithibitisha. Na amenifanyia hisani akanitoa gerezani na akakuleteni ninyi kutoka jangwani; baada ya Shetani kuchochea baina yangu na ndugu zangu. Hakika Mola wangu ni mwenye kulifikia alitakalo. Bila shaka Yeye ni Mjuzi na Mwenye hekima.(12:100)*

## **Shukurani za Nabii Yusufu(a.s) kwa Allah(s.w)**

Yusufu(a.s)alimshukuru Mola wake kwa kuleta dua ifuaatayo:

﴿ رَبِّ قَدْ عَاتَيْتَنِي مِنَ الْمُلْكِ وَعَلَّمْتَنِي مِنْ تَأْوِيلِ  
الْأَحَادِيثِ فَاطِرَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ أَنْتَ وَلِيِّ لِي فِي  
الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ تَوَفَّنِي مُسْلِمًا وَأَلْحِقْنِي بِالصَّالِحِينَ ﴾

*“Ee Mola wangu! Hakika umenipa Ufalme na umenifundisha tafsiri ya mambo. Ewe Muumba wa mbingu na ardhi! Wewe ndiye Mlinzi wangu katika dunia na Akhera. Nifishe hali ya kuwa ni Muislamu na unichanganyishe na watendao mema (12:101)*

## **Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Yusufu(a.s)**

﴿ لَقَدْ كَانَ فِي يُوسُفَ وَإِخْوَتِهِ آيَاتٍ لِلْمُتَسَابِلِينَ ﴾

*“Kwa yakini katika (kisa cha) Yusufu na ndugu zake yako mazingatio mengi kwa wanaouliza (mambo wapate kujua)”. (12:7).*

Baadhi ya mazingatio kutokana na kisa hiki ni haya yafuatayo:

- (i) Mitume huzaliwa Mitume na maisha yao yote kuanzia utotoni ni kiigizo cha tabia njema kwa waumini
- (ii) Wazazi hatunabudi kuwafunza watoto wetu tabia njema na kuwalea hivyo mpaka utuuzima wao.

- (iii) Watoto wenye tabia njema tuwapende na tuwashajiishe kubakia na mwenendo huo.
- (iv) Si vema kutangaza neema tulizo nazo kwa watu hata wale wa karibu yetu ili kujikinga na husuda.
- (v) Uislamu ni neema kubwa, hivyo kila atakayejaaliwa kufuata Uislamu vilivyo na kufanya jitihada za kuusimamisha katika jamii,ajiandae kuhusudiwa na makafiri na wanafiki.
- (vi) Hila za watu wenye roho mbaya na husuda dhidi ya watu wema wenye kujitahidi kusimamisha Uislamu katika jamii mwisho wake huwafedhehesha wenyewe hapa hapa duniani kama walivyofedheheka ndugu zake Yusufu na mkewe Al-aziz.
- (vii) Kutenda mema, ukweli na subira humnyanyua mtu daraja hapa duniani na huko akhera.
- (viii) Ukweli ukidhihiri uwongo hujitenga kama tulivyoona kwa nduguze Yusufu na mkewe Al-Aziz.
- (ix) Muungwana katika watu ni yule anayekiri makosa yake na kuomba msamaha kama walivyofanya nduguze Yusufu(a.s).
- (x) Waumini wanatakiwa wamuige Yusufu(a.s) kwa kuwa wepesi wa kusamehe na kulipa wema badala ya kulipiza kisasi baada ya kufanyiwa ubaya na kisha kuombwa msamaha. Pamoja na Yusufu kuwasamehe ndugu zake, aliwapatia chakula wakati wa njaa na kuwakaribisha Misr katika makazi ya Kifalme.
- (xi) Ngao dhidi ya mahasidi, mafatani, n.k. ni kumcha – Mungu, subira,kujitegemeza kwa Allah(s.w) na kuomba kinga yake.
- (xii) Hatunabudi kutumia fursa zinazojitokeza katika kulingania Uislamu, kama Yusufu(a.s) alivyoitumia fursa ile alipokutana na wale wafungwa wawili.

(xiii)Matwaaghuuti daima hawawezi kuhukumu kwa uadilifu na kutoa haki sawa hasa pale kesi itakapokuwa ni baina ya mdau wa nchi na raia wa kawaida. Ilihahirika kwa ushahidi wa wazi kuwa Yusufu(a.s) ndiye aliyekosewa na yule mkewe Al-Aziz, lakini kwa kumlinda na kashfa ile ilibidi Yusufu(a.s) ahukumiwe kwenda gerezani.

(xiv)Waumini wanapobambikiziwa maovu na machafu kutokana na husuda na chuki ya makafiri na wanafiki, wasitengeneze majukwaa ya kujitetea bali waendeleo kufanya wema kama Allah(s.w)anavyoagiza:

وَقُلِ اعْمَلُوا فَسَيَرَى اللَّهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُ وَالْمُؤْمِنُونَ وَسَتُرَدُّونَ إِلَىٰ  
عَدْلِهِمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ فَيُنبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٠٥﴾

*Na sema(uwaambie): “Tendeni mambo (mazuri). Mwenyezi Mungu atayaona mambo yenu hayo na Mtume Wake na Waislamu. Na mtarudishwa kwa Mjuzi wa siri na dhahiri; naye atakwambieni (yote) mliyokuwa mkiyatenda.” (9:105)*

(xv)Tunapokubalika na kuhitajika kuongoza jamii hatunabudi kupendekeza tukabidhiwe kuongoza katika maeneo tunayoyamudu vizuri kitaaluma, kiuzoefu na kiuadilifu na hasa pale tutakapoona hapana watu wengine wa kuongoza kwa uadilifu katika maeneo hayo.

(xvi)Tuchague viongozi waadilifu na wenye tabia njema bila ya kujali ukabila, utaifa, n.k. Yusufu(a.s) alikuwa mtu wa kuja na mtumwa lakini alipewa Uongozi Misr kutokana na elimu yake, tabia yake njema na uadilifu wake.

(xvii)Kiongozi Muumini ni yule anayekumbuka na kuzingatia kuwa wadhifa alionao ni amana aliyokabidhiwa na Allah (s.w) kwa manufaa ya jamii, hivyo hujiepusha na kibri,



majivuno, kujikweza au tabia yoyote inayoashiria dharau kwa wenzake. Funzo hili tunalipata kwenye dua ya Nabii Yusufu(a.s).

## **AYYUUB(A.S)**

Ayyuub(a.s) ni katika Mitume wa Allah(s.w) waliotajwa katika Qur-an kwa umadhubuti wake katika imani juu ya Allah(s.w) na Subira.

Ayyuub(a.s) aliishi Kaskazini Mashariki ya Bara Arabu. Alikuwa tajiri sana mwenye mali nyingi, watoto wengi na watumishi wengi. Lakini hakutakabari bali alimuabudu Mola wake na kumshukuru ipasavyo

### **Mitihani Iliyomfika Ayyuub(a.s)**

Nabii Ayyuub(a.s) alitahiniwa na Mola wake kama ifuatavyo:

- (1) Mali yake, watoto wake na watumishi wake wote walipatwa na majanga wakatoweka. Akabakia yeye na mkewe ambaye naye alikuwa mcha-Mungu.
- (2) Pamoja na kupotelewa na mali yake na watu wake wote, alishikwa na maradhi mabaya ya kuota vidonda mwili mzima kuanzia kichwani hadi miguuni. Alijaribu kutumia dawa zote alizoweza, lakini hakupata nafuu yoyote

Nabii Ayyuub(a.s) hakutetereka katika imani yake kutokana na majanga yaliyomfika bali **alishubiri** na kuwa karibu zaidi na Mola wake kuliko hata wakati alipokuwa katika hali yake ya mwanzo ya utajiri na afya nzuri. Na Allah(s.w) anamsifu mjawake, Ayyuub kama ifuatavyo:

.....إِنَّا وَجَدْنَاهُ صَابِرًا نِّعْمَ إِنَّهُ وَأَب ٤٤

“.... Bila shaka tulimkuta ni mwenye subira mja mwema; kwa hakika alikuwa mnyenyekevu sana.” (38:44)

Nabii Ayyuub(a.s) aliona kuwa aliyempa mali, watoto na wale watumishi aliokuwa nao ni Allah(s.w) kama amana. Hivyo, aliona hapakuwa na kosa lolote kwa Allah(s.w) kuchukua amana yake. Pia aliridhika na hali ya ugonjwa aliyokuwa nayo. Kwa ujumla Nabii Ayyuub (a.s) aliridhika na **kusubiri** juu ya matatizo yote yaliyomfika na kupata matunda ya subira kama Allah(s.w) anavyotubashiria:

وَلَتَبْلُؤَنَّكُمْ بِشَيْءٍ مِّنَ الْخَوْفِ وَالْجُوعِ وَنَقْصٍ مِّنَ الْأَمْوَالِ  
وَالْأَنْفُسِ وَالْأَثْمَارِ<sup>ط</sup> وَبَشِيرِ الصَّابِرِينَ ١٥٥

*Na tutakutieni katika msukosuko wa (baadhi ya mambo haya); hofu na njaa na upungufu wa mali na wa watu na wa matunda. Na wapashe habari njema wanaosubiri.(2:155)*

الَّذِينَ إِذَا أَصَابَتْهُمُ مُصِيبَةٌ قَالُوا إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاغِبُونَ ١٥٦

*Ambao uwapatapo msiba husema: “Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake Yeye tutarejea (atatupa jaza yake).(2:156)*

أُولَئِكَ عَلَيْهِمْ صَلَوَاتٌ مِّن رَّبِّهِمْ وَرَحْمَةٌ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُهْتَدُونَ ١٥٧

*Hao juu yao zitakuwa baraka zitokazo kwa Mola wao na rehema; na ndio wenye kuongoka. (2:157)*

## Dua ya Ayyuub(a.s)

Nabii Ayyuub(a.s) aliendelea na maradhi yale mazito kwa kipindi kirefu (ina semekana miaka saba). Mwishowe akaona amuelekee Mola wake na kumuomba amuondolee maradhi yale kama tunavyojifunza katika ya zifuatazo:

❖ وَأَيُّوبَ إِذْ نَادَى رَبَّهُ أَنِّي مَسَّنِيَ الضُّرُّ وَأَنْتَ أَرْحَمُ

الرَّحِيمِينَ ﴿٨٣﴾

*Na (Mtaje) Ayyubu, alipomwita Mola wake (akasema) “Mimi imenipata dhara, nawe ndiwe Unayerehemu kuliko wote wanaorehemu.” (21:83)*

Dua ya Ayyuub(a.s) ilikuwa makubuli kwa Mola wake kumuelekeza dawa ya matibabu yale:

أَرْكُضْ بِرِجْلِكَ هَذَا مُغْتَسَلٌ بَارِدٌ وَشَرَابٌ ﴿٤٢﴾

*(Mwenyezi Mungu akamwambia):- “Uharikishe mguu wako (patachimbuka chemchem chini yake, maji yake yatakuwa dawa yako). Basi haya maji baridi ya kuogea (koga), na (haya maji baridi) ya kunywa, (yanywe).” (38:42)*

Baada ya kutumia dawa hii Nabii Ayyuub(a.s) alikuwa mzima wa afya kama alivyokuwa hapo awali kabla ya ugonjwa. Furaha zaidi kwake, pamoja kurudishiwa afya yake, pia alirudishiwa mali na watu wake kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

فَأَسْتَجَبْنَا لَهُ فَكَشَفْنَا مَا بِهِ مِنْ ضُرٍّ وَعَآتَيْنَاهُ أَهْلَهُ وَمِثْلَهُم مَّعَهُمْ

رَحْمَةً مِّنْ عِنْدِنَا وَذِكْرَىٰ لِلْعَابِدِينَ ﴿٨٤﴾

*Basi tukamkubalia (wito wake) na tukamuondolea dhara aliyokuwa nayo, na tukampa watu wake na mfano wao pamoja nao. Ni rehema inayotoka kwetu, na ukumbusho (mzuri kwa wafanyao) Ibada. (21:84)*

وَوَهَبْنَا لَهُ أَهْلَهُ وَمِثْلَهُم مَّعَهُمْ رَحْمَةً مِنَّا وَذِكْرَىٰ لِأُولِي الْأَلْبَابِ ﴿٤٣﴾

*Na tukampa watu wake na wengine kama wao pamoja nao, kwa rehema itokayo kwetu, na (ipate kuwa) mauidha kwa watu wenye akili. (38:43)*

## Nabii Ayyuub(a.s) Kutekeleza Kiapo Chake

Mkewe Ayyuub(a.s) alikuwa naye ni mama mcha-Mungu mwenye subira. Alimuuguza mumewe kwa kipindi kirefu kiasi hicho katika hali ngumu bila ya kuchoka. Lakini inasemekana siku moja aliteleza na kutamka maneno ambayo yalimchukiza Nabii Ayyuub(a.s) kwa kuwa yalikuwa yanamtoa katika imani ya Allah(s.w). Inasemekana mkewe aliteleza na kusema, “Hivi huu ugonjwa utaendelea mpaka lini?” Nabii Ayyuub(a.s) alimkemea mkewe juu ya kauli yake hiyo na kumuahidi kuwa akipona atamuadhibu kwa kumcharaza bakora mia.

Baada ya Nabii Ayyuub(a.s) kupona, Allah(s.w) alimuelekeza namna yakutekeleza kiapo cha kumuadhibu mkewe aliyemfanyia ihsani na kuvumilia shida kiasi kile, kwa maelekezo ya Allah(s.w) hakupaswa kumcharaza bakora mia, bali aliagizwa achukue vijiti mia avifunge pamoja kisha ampige navyo mara moja kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

وَخُذْ بِبَيْدِكَ ضِعْفًا فَأَضْرِبْ بِهِ وَلَا تَحْتِثْ إِنَّا وَجَدْنَاهُ صَابِرًا نِعْمَ الْعَبْدُ

إِنَّهُ وَأَوَّابٌ ﴿٤٤﴾

“Na shika kicha cha vijiti tu mkononi mwako, (si fimbo); kisha mpige kwacho (mkeo kwa kiapo ulichoapa kuwa utampiga kwa mabaya aliyoyafanya), wala usivunje kiapo.” Bila shaka tulimkuta ni mwenye subira, mja mwema; kwa hakika alikuwa mnyenyekevu sana. (38:44)

## Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Ayyuub(a.s)

Kutokana na kisha hiki cha Nabii Ayyuub(a.s) tunajifunza yafuatayo:

- (i) Binaadamu hapa ulimwenguni yuko mtihanini kama Qur-an inavyobainisha:

تَبَرَّكَ الَّذِي بِيَدِهِ الْمُلْكُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١﴾ الَّذِي  
 خَلَقَ الْمَوْتَ وَالْحَيَاةَ لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا وَهُوَ الْعَزِيزُ  
 الرَّحِيمُ ﴿٢﴾

*Ametukuka yule ambaye Mkononi mwake umo ufalme (wote);  
 Naye ni mwenye uweza juu ya kila kitu. Ambaye ameumba mauti  
 na uhai ili kukujaribuni (kukufanyieni mtihani); ni nani miongoni  
 mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi. Naye ni Mwenye nguvu na  
 Mwenye Msamaha. (67:1-2)*

إِنَّا خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ مِنْ نُطْفَةٍ أَمْشَاجٍ نَّبْتَلِيهِ فَجَعَلْنَاهُ سَمِيعًا بَصِيرًا ﴿٢﴾

*Kwa hakika tumemuumba mtu kutokana na mbegu ya uhai  
 iliyochanganyika; (ya mwanamume na mwanamke), ili tumfanyie  
 mtihani (kwa amri zetu na makatazo yetu); kwa hiyo tukamfanya  
 ni Mwenye kusikia (na) Mwenye kuona. (76:2)*

Mwanaadamu anachoweza kufanya si kuepa mitihani bali  
 kutekeleza wajibu wake kwa kadiri ya uwezo wake na  
 kufanya subira juu ya mazito mbali mbali yatakayomfika  
 huku akimtegemea Allah(s.w) ipasavyo

(ii) Muumini baada ya kumcha-Allah(s.w) ipasavyo alipokee  
 kwa moyo mkunjufu lolote litakalomfika likiwa la kheri au  
 lenye sura ya shari, kwani Allah yuko pamoja na waja wake.

(iii) Kwa elimu ndogo ya mwanaadamu kuna matukio mengine  
 yanamtokea mwanaadamu kwa sura ya shari, kumbe ni ya  
 kheri kwake na kinyume chake kama Allah(s.w)  
 anavyotutanabahisha katika aya ifuatayo:

كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِتَالُ وَهُوَ كُرْهُ لَكُمْ وَعَسَى أَنْ تَكْرَهُوا شَيْئًا

وَهُوَ خَيْرٌ لَكُمْ وَعَسَى أَنْ تُحِبُّوا شَيْئًا وَهُوَ شَرٌّ لَكُمْ وَاللَّهُ يَعْلَمُ

وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢١٦﴾

*Mmelazimishwa kupigana vita (kwa ajili ya dini). Nalo ni jambo zito kwenu. Lakini huenda mkachukia kitu, nacho ni kheri kwenu. Na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu ndiye anayejua, (lakini) nyinyi hamjui. (2:216)*

- (iv) Muumini wa kweli anatakiwa awe anamkumbuka Allah(s.w) nyakati zote katika hali zote, akiwa na dhiki au wasaa. Na mtu anapokuwa katika dhiki ndio anazijua na kuzithamini vizuri neema mbali mbali alizoneemeshwa na Mola wake na ndio anakuwa na nafasi nzuri ya kushukuru. Kwa mfano ni kweli kuwa mtu hawezi kujua thamani ya shibe kama hajafikiwa na dhiki ya njaa.
- (v) Waumini wanalazimika kutekeleza ahadi au viapo wanavyotoa katika kufanya mambo ya kheri.
- (vi) Hapana kizuizi chochote kiwezacho kuwazuia waumini kumcha-Mola wao na kusimamisha Uislamu katika jamii.
- (vii) Matatizo yanayowafika waumini pasina yale ya kujitakia (ya uzembe), ni nyenzo muhimu za kunoa imaniyao juu ya Allah na kuwapa hamasa na msukumo wa kusimamisha Uislamu katika jamii.

## **SHU'AYB(A.S)**

Nabii Shu'ayb(a.s) alitumwa kwa watu wa Madian waliokuwa wakikaa pande za pwani ya Shamu (Syria). Watu hawa walikuwa wafanyabiashara wakubwa wa zama hizo. Mji wao ulikuwa katika njia kuu (Highway) ya misafara ya biashara kutoka sehemu mbali mbali za Mashariki ya kati kuelekea pwani ya bahari ya Mediterranean.

## Tabia ya watu wa Madian

Wamadian pamoja na kuwa wafanyabiashara mashuhuri walikuwa na tabia ya kupunja vipimo wakati wa kuuza. Pia walikuwa wababe wakifanya uharibifu katika ardhi, walikuwa majambazi wakipora na kunyang'anya watu mali zao. Vile vile walikuwa washirikina na kuzuia watu kufuata Dini ya Allah(s.w).

## Ujumbe wa Nabii Shu'ayb kwa Watu Wake

Nabii Shu'ayb(a.s) kama walivyofanya Mitume waliomtangulia aliwanasihi watu wake kumwamini na kumuabudu Allah(s.w) ipasavyo katika maisha yao ya kila siku na kusimamisha uadilifu katika jamii.

﴿وَاللّٰى مَدْيَنَ اٰخَاهُمْ شُعَيْبًا قَالَ يَدْعُوْكُمْ اَعْبُدُوْا اللّٰهَ  
مَا لَكُمْ مِّنْ اِلٰهٍ غَيْرُهُۥ وَلَا تَنْقُصُوْا الْمِكْيَالَ وَالْمِيزَانَ  
اِنَّىۤ اَرٰنَكُمْ بِخَيْرٍ وَّاِنّىۤ اَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ مُّحِيْطٍ﴾

*Na kwa watu wa Madian (tulimpeleka) ndugu yao, Shuaibu. Akasema: “Enyi watu wangu! Mwabuduni Mwenyezi Mungu, nyinyi hamna Mungu ila Yeye. Msipunguze kipimo (cha vibaba) wala (cha) mizani. Mimi nakuoneni mumo katika hali njema (basi msiiharibu kwa kufanya dhulma).Nami nakukhofieni adhabu ya siku (kubwa) hiyo itakayokuzungukeni.” (11:84)*

Nabii Shu'ayb(a.s) aliendelea kuwaasa watu wake:

﴿وَلَا تَقْعُدُوْا بِكُلِّ صِرَاطٍ تُوعِدُوْنَ وَتَصُدُّوْنَ عَنِ سَبِيْلِ اللّٰهِ مَنْ ءَامَنَ بِهٖ  
وَتَبْعُوْنَهَا عِوَجًا وَّاَذْكُرُوْا اِذْ كُنْتُمْ قَلِيْلًا فَكَثُرْ كُمْ وَاَنْظُرُوْا كَيْفَ كَانَ

عَنْقِبَةُ الْمُفْسِدِيْنَ﴾

“Wala msikae katika kila njia kuogopesha (watu) na kuwazuilia na Dini ya Mwenyezi Mungu (wale) wenye kuamini, na kutaka kuipotisha Na kumbukeni mlipokuwa wachache, Naye akakufanyeni kuwa wengi (sasa).Na tazamneni jinsi ulivyokuwa mwisho wa waharibifu.” (7:86)

## Mbinu Alizozitumia Nabii Shu’ayb(a.s) Katika Kufikisha Ujumbe Wake

Katika kuwafikishia ujumbe watu wake,Nabii Shu’ayb alifanya yafuatayo:

**Kwanza**, kuwafahamisha watu wake kwa uwazi kuwa yeye ni Mtume wa Allah(s.w) aliye mfano wa kuigwa:

قَالَ يَنْقَوْمُ أَرَأَيْتُمْ إِنْ كُنْتُ عَلَىٰ بَيِّنَةٍ مِّن رَّبِّي وَرَزَقَنِي مِنْهُ رِزْقًا حَسَنًا  
وَمَا أُرِيدُ أَنْ أُخَالِفَكُمْ إِلَىٰ مَا أَنهَنكُم عَنْهُ إِنْ أُرِيدُ إِلَّا الْإِصْلَاحَ  
مَا اسْتَطَعْتُ وَمَا تَوْفِيقِي إِلَّا بِاللَّهِ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَإِلَيْهِ أُنِيبُ ﴿٣٨﴾

Akasema: “Enyi watu wangu! Mnaonaje kama ninayo dalili inayotokana na Mola wangu na ameniruzuku riziki njema (ya Utume) kutoka kwake (nitaacha haya, nishike upotofu wenu)? Wala sipendi kukukhalifuni nikafanya yale ninayokukatazeni. Sitaki ila kutengeneza, kiasi ninavyoweza. Na sipati kuwezesha haya ila na Mwenyezi Mungu (Mwenyewe). Kwake ninategemea, na Kwake naelekea.” (11:88)

**Pili**, aliwahofisha adhabu kali ya Allah(s.w) iwapo watakataa kumwamini na kumfuata.

وَإِلَىٰ مَدْيَنَ أَخَاهُمْ شُعَيْبًا فَقَالَ يَنْقَوْمُ أَعْبُدُوا اللَّهَ وَارْجُوا الْيَوْمَ الْآخِرَ  
وَلَا تَعْتَوْا فِي الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ﴿٣٩﴾



*Na kwa Madiani (tulimtuma) ndugu yao, (Nabii) Shu'ayb, naye akasema: "Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu na iogopeni siku ya akhera wala msende katika ardhi mkifisidi." (29:36)*

**Tatu**, aliwatahadharisha watu wake na adhabu ya Allah(s.w) ili yawafika kaumu zilizopita za akina 'Ad, Thamud na kaumu Lut.

وَيَنْقَوْمٍ لَا يُجْرِمُكُمْ شِقَاقِي أَنْ يُصِيبَكُمْ مِثْلُ مَا أَصَابَ قَوْمَ نُوحٍ أَوْ

قَوْمِ هُودٍ أَوْ قَوْمِ صَالِحٍ وَمَا قَوْمُ لُوطٍ مِّنْكُمْ بِبَعِيدٍ ﴿٨٨﴾

*"Na enyi watu wangu! Kukhalifiana nami kusikupelekeeni yakakusibuni kama yaliyowasibu watu wa Nuh au watu wa Saleh na watu wa Luti si mbali nanyi." (Karibuni hivi wameangamizwa; na nchi zao ziko karibu na nyinyi pia). (11:89)*

**Nne**, aliwatumainisha watu wa Madian kuwa endapo wataomba msamaha kwa Allah(s.w) na kutubu juu ya makosa yao, Allah(s.w) atawasamehe na kuwaepusha na balaa lililowafika watu wa kaumu za Mitume waliotangulia.

وَاسْتَغْفِرُوا رَبَّكُمْ ثُمَّ ثَابِرُوا إِلَيْهِ إِنَّ رَبِّي رَحِيمٌ وَدُودٌ ﴿٩٠﴾

*"Na ombeni msamaha kwa Mola wenu (kwa yaliyopita), kisha tubuni kwake. Hakika Mola wangu ni Mwenye kurehemu na Mwenye kuwapenda (waja Wake)." (11:90)*

**Tano**, aliwaonyesha msimamo na utegemezi wake juu ya Allah(s.w).

وَيَنْقَوْمٍ لَا يُجْرِمُكُمْ شِقَاقِي أَنْ يُصِيبَكُمْ مِثْلُ مَا أَصَابَ قَوْمَ نُوحٍ أَوْ

قَوْمِ هُودٍ أَوْ قَوْمِ صَالِحٍ وَمَا قَوْمُ لُوطٍ مِّنْكُمْ بِبَعِيدٍ ﴿٨٩﴾

*"Na enyi watu wangu! Fanyeni (mtakayo) kwa tamkini yenu; na mimi pia ninafanya (yangu kwa tamkini yangu). Karibuni hivi mtajua ni nani itakayemfikia adhabu ifedheheshayo na ni nani aliye muongo. Na ngojeeni; mimi pia ninangoja pamoja nanyi." (11:93)*

قَدِ افْتَرَيْنَا عَلَى اللَّهِ كَذِبًا إِنْ عُدْنَا فِي مِلَّتِكُمْ بَعْدَ إِذْ نَجَدْنَا اللَّهَ مِنْهَا  
 وَمَا يَكُونُ لَنَا أَنْ نَعُودَ فِيهَا إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ رَبُّنَا وَسِعَ رَبُّنَا كُلَّ شَيْءٍ  
 عِلْمًا عَلَى اللَّهِ تَوَكَّلْنَا رَبُّنَا افْتَحْ بَيْنَنَا وَبَيْنَ قَوْمِنَا بِالْحَقِّ وَأَنْتَ  
 خَيْرُ الْفَاتِحِينَ ﴿٨٩﴾

*“Bila shaka tumemtungia Mwenyezi Mungu uwongo ikiwa tutarudi katika mila yenu baada ya Mwenyezi Mungu kutuokoa nayo. Wala haiwi kwetu sisi kurejea mila hiyo. Lakini akitaka (jambo) Mwenyezi Mungu, Mola wetu, (huwa). Mola wetu amekienea kila kitu kwa ilimu yake. Kwa Mwenyezi Mungu tunategemea. Mola wetu! Hukumu baina yetu na baina ya wenzetu (hawa) kwa haki, nawe ndiye mbora wa wanaohukumu.” (7:89)*

## Vitimbi vya Wapinzani Dhidi ya Ujumbe wa Nabii Shu’ayb(a.s)

Kama ilivyokuwa katika kaumu zilizotangulia, waliomuamini Shu’ayb(a.s) na kufuata nasaha zake walikuwa watu wachache tu katika jamii yake. Wengi wao walikaidi mafundisho ya Mtume wao wakiongozwa na wakuu wa jamii. Katika kumkanusha Mtume wao walitumia mbinu mbali mbali.

**Kwanza, walitumia vitisho**

﴿قَالَ الْمَلَأُ الَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا مِنْ قَوْمِهِ لَنُخْرِجَنَّكَ يَشْعِيبُ  
 وَالَّذِينَ آمَنُوا مَعَكَ مِنْ قَرْيَتِنَا أَوْ لَتَعُودَنَّ فِي  
 مِلَّتِنَا قَالَ أَوَلَوْ كُنَّا كَارِهِينَ﴾ ﴿٨٨﴾

*Wakuu waliotakabari katika kaumu yake wakasema: “Ewe Shu’ayb! Tutakutoa wewe na wale walioamini pamoja nawe*

katika mji wetu, au mrejee katika mila yetu.” Akasema: “Je, ingawa tunaichukia?” (7:88)

### **Pili, walitumia mbinu ya kuwakatisha watu tamaa**

وَقَالَ الْمَلَأُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَوْمِهِ لَئِنِ اتَّبَعْتُمْ شُعَيْبًا إِنَّكُمْ إِذًا لَخَسِرُونَ ﴿٩٠﴾

Na wakuu waliokufuru katika kaumu yake wakasema: “Kama nyinyi mkimfuata Shu’ayb, hapo bila shaka mtakuwa wenye kukhasirika.” (7:90)

### **Tatu, walimdhahaki Mtume wao.**

قَالُوا يَشْعَيْبُ أَصْلُوكَ تَأْمُرُكَ أَنْ نَتْرَكَ مَا يَعْبُدُ آبَاؤُنَا أَوْ أَنْ نَفْعَلَ فِي أَمْوَالِنَا مَا نَشَاءُ إِنَّكَ لَأَنْتَ الْحَلِيمُ الرَّشِيدُ ﴿٩١﴾

Wakasema: Ewe Shuaibu! Swala zako zinakuamrisha tuyaache yaliyokuwa wakiyaabudu baba zetu au tuache kufanya tupendavyo katika mali zetu? Bila shaka wewe ni mwenye akili na mnyoofu (11:87)

### **Nne, walitumia mbinu ya kumdhahilisha.**

قَالُوا يَشْعَيْبُ مَا نَفَقَهُ كَثِيرًا مِمَّا تَقُولُ وَإِنَّا لَنَرُكَ فِيْنَا ضَعِيفًا وَلَوْلَا رَهْطُكَ لَرَجَمْنَاكَ وَمَا أَنْتَ عَلَيْنَا بِعَزِيزٍ ﴿٩٢﴾

Wakasema: “Ewe Shu’ayb! Hatufahamu mengi katika hayo unayoyasema. Na sisi tunakuona mdhalilifu kwetu. Lau kuwa si jamaa zako tungekupiga mawe, wala wewe si mtu mtukufu kwetu! (ila tunachunga hishima ya jamaa zako tu).” (11:91)

## Kuangamizwa Waovu na Kuokolewa Waumini

Baada ya kuonywa wasionyeye, Allah(s.w) aliwaangamiza kama walivyoangamizwa akina Ad, Thamud, n.k.

فَأَخَذْتَهُمُ الرِّجْفَةَ فَأَصْبَحُوا فِي دَارِهِمْ جَنَثِيمِينَ ﴿٩١﴾ الَّذِينَ كَذَّبُوا

شُعَيْبًا كَأَن لَّمْ يَعْنُوا فِيهَا الَّذِينَ كَذَّبُوا شُعَيْبًا كَانُوا هُمُ الْخَاسِرِينَ ﴿٩٢﴾

*Basi mtetemeko wa ardhi uliwatoa roho zao, wakawa wasiojimudu, (wamekufa) humo mjini mwao. Wale waliomkadhibisha Shu'ayb wakawa kama kwamba hawakuwako (mahala hapo). Wale waliomkadhibisha Shu'ayb ndio waliokuwa wenye khasara. (7:91-92)*

وَلَمَّا جَاءَ أَمْرُنَا نَجَّيْنَا شُعَيْبًا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ بِرَحْمَةٍ مِنَّا وَأَخَذَتِ

الَّذِينَ ظَلَمُوا الصَّيْحَةَ فَأَصْبَحُوا فِي دِيَارِهِمْ جَنَثِيمِينَ ﴿٩٤﴾

*Na ilipokuja amri yetu, tulimuokoa Shu'ayb na wale walioamini pamoja naye kwa rehema yetu. Na wale waliodhulumu ukelele (wa adhabu) ulinyakuwa roho zao. Wakawa majumbani mwao wametulia tu (wamekufa). (11:94)*

كَأَن لَّمْ يَعْنُوا فِيهَا إِلَّا بُعْدًا لِّمَدْيَنَ كَمَا بَعَدَتْ ثَمُودُ ﴿٩٥﴾

*Kama kwamba hawakuwamo humo. Sikilizeni. Wameangamia (watu wa) Madiana kama walivyoangamia (kina) Thamudu. (11:95)*

Kwa mujibu wa aya hizi, watu wa Madian waliangamizwa kwa ukelele ukifuatiwa na tetemeko la ardhi. Tukikumbuka kuwa:

وَلِلَّهِ جُنُودُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿٧﴾

*Na majeshi ya mbingu na ardhi ni ya Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu; Mwenye hikima. (48:7)*

## **Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Shu'ayb(a.s).**

Kutokana na kisa cha Nabii Shu'ayb(a.s) tunajifunza yafuatayo:

- (i) Waislamu tunadhima ya kusimamisha uchumi halali katika jamii pamoja na kuamrisha mema na kukataza maovu kwa ujumla.
- (ii) Tusimchelee yeyote katika harakati za kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii.
- (iii) Tukisimama kidete kuifuata na kuisimamisha Dini ya Allah (s.w)katika jamii Allah(s.w) atatusuru na kuthubutisha miguu yetu juu ya makafiri.
- (iv) Waislamu wakijizatiti kusimamisha Uislamu katika jamii watawashinda makafiri pamoja na nguvu kubwa za kiuchumi na kijeshi walizonazo.

## **MUSA(A.S) NA HARUN(A.S)**

Nabii Musa(a.s) ni Mtume aliyeandaliwa na Allah(s.w) kuwakomboa Bani Israil (Waisraili) waliofanywa kuwa watumwa nchini Misri. Waisraili ni kizazi cha Nabii Ya'aquub(a.s),Nabii Yusufu(a.s) ndiye alianza kukaa Misri kisha wakafuatia wazazi na ndugu zake wote wakati alipokuwa kiongozi nchini humo.

Allah(s.w) alimtuma Nabii Musa(a.s) kuwakomboa Bani Israil kwasababu haki yao ya kuwa huru ambayo Allah(s.w) amempa kila mwanadamu, iliporwa! Maadamu Bani Israil waliporwa haki hii kuu ya msingi; Allah(s.w) kwa uadilifu wake akamtuma Nabii Musa(a.s) kutekeleza jukumu zito la kuwakomboa na kuwarejeshea haki zao za kibinadamu walizonyang'anywa.

إِنَّ فِرْعَوْنَ عَلَا فِي الْأَرْضِ وَجَعَلَ أَهْلَهَا شِيَعًا يَسْتَضِعُّ طَائِفَةً مِنْهُمْ

يُذَبِّحُ أَبْنَاءَهُمْ وَيَسْتَحْيِي نِسَاءَهُمْ إِنَّهُ كَانَ مِنَ الْمُفْسِدِينَ ﴿٤﴾

*Hakika Firauni alitakabari katika ardhi, na akawafanya watu wa huko makundi mbalimbali. Akalidhoofisha kundi moja miongoni mwao, akiwachinja watoto wao wakiume na kuwa acha hai watoto wao wa kike. Hakika yeye alikuwa miongoni mwa waharibifu (28:4)*

Aya hii zimeweka wazi ukiukwaji wa haki za binadamu walioufanya watawala wa Misri. Lengo la kuhalalisha ukatili na mauwaji hayo lilikuwa kuwadhoofisha wananchi wenye nasaba ya Nabii Yusufu(a.s) wasipate nafasi ya kuongoza tena.

## **Kuzaliwa kwa Musa(a.s)**

Musa(a.s) alizaliwa wakati bado msako unafanywa na askari wa Firauni kumwua kila mtoto wa kiume wa Kiisrail anayezaliwa. Kwa rehema zake Allah(s.w) mama yake Musa alijifungua bila kutambulika kwa askari wa Firauni. Na ili kumlinda zaidi Allah(s.w) alimteremshia Wahy mama yake Musa.

أَنْ أَفْذِيهِ فِي التَّابُوتِ فَأَفْذِيهِ فِي الْيَمِّ فَلْيَلْقِهِ الْيَمُّ بِالسَّاحِلِ

يَأْخُذْهُ عَدُوِّي وَعَدُوُّ لَهُ وَالْقَيْثُ عَلَيْكَ مَحَبَّةٌ مِيَّتِي وَلِيُصْنَعَ

عَلَى عَيْنِي ﴿٣٩﴾

*Ya kwamba mtie sandukuni, kisha litie mtoni, na mto utamtupa ufukoni ili amchukue adui yangu na adui yake (amlee kwa vizuri Naye ni Firaun). Na nimekutilia mapenzi yatokanayo kwangu (ili upendwe na watu wote), na ili ulelewe machoni mwangu.(20:39)*

Baada ya kumtupa mtoni, mama yake akamtuma dada yake Musa kufuatilia:

وَقَالَتْ لِأُخْتَيْهِ فَصِيحَةٍ فَبَصُرَتْ بِهِ عَن جُنُبٍ وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿١١﴾

*Akamwambia dada yake: “Mfuate”. Basi yeye akamwangukia kwa mbali bila wao kumjua (28:11)*

Kitoto Musa kiliokotwa na kufikishwa kwa Firaun. Mkewe Firaun akamrai mumewe kuwa wasimuue bali wamfanye mtoto wao wa kulea.

وَقَالَتْ أُمَّرَأْتُ فِرْعَوْنَ فَرَرْتُ عَيْنَ لِي وَلَكَ لَا تَقْتُلُوهُ عَسَىٰ أَن يَنْفَعَنَا أَوْ نَتَّخِذَهُ وَلَدًا وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٩﴾

*Na mkewe Firauni akasema (Kumwambia mumewe) “Usimuuwe, atakuwa kiburudisho cha macho kwangu na kwako; na msimuuwe; huwenda atatunufaisha, au tumpange kuwa mtoto wetu, walisema haya hali ya kuwa hawatambui (kuwa atakuwa adui yao)” (28:9)*

Watu wa Firauni walipomwokota Musa bila shaka walitambua kuwa ni mtoto wa Kiisrail na walimpeleka kwa Firauni ili auawe kama watoto wengine Wakiisrail. Lakini mke wa Firauni alivutiwa na uzuri wa mtoto Musa. Ambaye kwa kweli Allah(s.w) alimfanya awe ni mwenye kupendeza machoni kwa watu.

## **Allah(s.w) Ajaalia Musa(a.s) Kunyonyeshwa na Mama Yake Mzazi**

Kwa uwezo wake, Mwenyezi Mungu aliharamisha Musa asinyonyeshwe na yeyote yule isipokuwa mama yake. Hivyo, dada yake Musa alijitokeza nyumbani kwa Firauni na kupendekeza:

.....فَقَالَتْ هَلْ أَدُلُّكُمْ عَلَىٰ أَهْلِ بَيْتٍ يَكْفُلُونَهُ

لَكُمْ وَهُمْ لَهُ نَصِیحُونَ ﴿١٢﴾

“.....Basi akasema: Je nikuonesheni watu wa nyumba watakaomlea kwa ajili yenu, na pia watakuwa wema kwake? (28:12)

Dada yake Musa(a.s) alimpendekeza mama yake ambaye Firauni hawakumjua kuwa ndiye mama mzazi wa Nabii Musa(a.s). Ombi hilo lilikubaliwa na Musa(a.s)alirejeshwa kwa mama yake:

فَرَدَّدْنَاهُ إِلَىٰ أُمِّهِ كَىٰ تَقَرَّ عَيْنُهَا وَلَا تَحْزَنَ ۚ وَلِتَعْلَمَ أَنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ

وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٣﴾

Basi tukamrejsha kwa mama yake ili macho yake yaburudike, wala asihuzunike; na ajue ya kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli, lakini watu wengi hawajui (28:13)

## Allah(s.w) Amruzuku Musa(a.s) Elimu

Ili kuweza kutekeleza jukumu la kutetea haki za binadamu na kuwaongoza watu katika njia iliyonyooka, Mwenyezi Mungu akamjaalia Musa elimu ya kutosha na akili yenye upeo mkubwa wa kupembua mambo. Tunafahamishwa kuwa:

وَلَمَّا بَلَغَ أَشُدَّهُ ۖ وَأَسْتَوَىٰ ۖ آتَيْنَاهُ حُكْمًا وَعِلْمًا ۚ وَكَذَٰلِكَ نَجْزِي

الْمُحْسِنِينَ ﴿١٤﴾

Na Musa alipofikia balebale yake na kustawi, tulimpa akili na elimu, na hivi ndivyo tunavyowalipa watu wema (28:14)

## Musa(a.s) Ahamia Madiani

Mchana wa siku moja Musa(a.s) alimuona mtu wa Firauni amemuelemea Muisrail akimtwanga makonde mazito. Musa alichukizwa na kitendo kile, hivyo alipoombwa msaada alijikuta



amemtвика Mmisri huyo ngumi nzito na kumuwa palepale. Hapo Musa(a.s) akashituka na kuleta toba:

قَالَ رَبِّ إِنِّي ظَلَمْتُ نَفْسِي فَاغْفِرْ لِي فَغَفَرَ لَهُ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿١٦﴾

*Mola wangu! Bila shaka nimedhulumu nafsi yangu, basi nisamehe; naye (Allah) akamsamehe. Kwa hakika yeye ni Mwingi wa kusamehe, Mwingi wa kurehemu. (28:16)*

قَالَ رَبِّ بِمَا أَنْعَمْتَ عَلَيَّ فَلَنْ أَكُونَ ظَهِيرًا لِلْمُجْرِمِينَ ﴿١٧﴾

*Akasema: Mola wangu! Kwa kuwa umenineemesha, basi sitakuwa kabisa msaidizi wa watu wabaya. (28:17)*

Habari ile ya kuuliwa mtu na Musa(a.s) ilifika kwa Firaun na ikatoka shauri kuwa Musa(a.s) akamatwe na kuuliwa. Musa(a.s) alipopata habari za kuaminika kutoka kwa mtu mwema, kuhusu hukumu ile, aliamua kutorokea nchini Madian katika mji awa Al-Bid uliopo kilometa 480 hivi mashariki ya Misr. Alipofika Madian hakuwa na pakwenda bali alijipumzisha kisimani ambapo aliwasaidia wasichana wawili kuwanywesha wanyama wao. Wasichana wale hawakuweza kupigana vikumbo na wanaume katika kunywesha wanyama wao, wakawa tu wanabakia pembeni wanaangalia. Kitendo kile kilimfurahisha Mzee wa Madian na akaagiza Musa(a.s) aitwe ili apate ujira wa kazi ile.

فَجَاءَتْهُ إِحْدَاهُمَا تَمْشِي عَلَى اسْتِحْيَاءٍ قَالَتْ إِنَّ أَبِي يَدْعُوكَ لِيَجْزِيَكَ أَجْرَ مَا سَقَيْتَ لَنَا .....

*Basi akamjia mmoja katika (wasichana) wale wawili, anakwenda na huku anaona haya, akasema: “Baba yangu anakuita ili akulipe ujira wa kutunyweshea.....(28:25)*

Musa alipofika kwa yule mzee alimsimulia hali halisi kuhusu dhulma, ukandamizaji na ukiukwaji wa haki za binadamu uliopo nchini Misri, pamoja na kisa kilichompelekea yeye kuhamia Madiani. Yule mzee akamtuliza Musa(a.s), akasema:

..... لَا تَخَفْ نَجَوْتَ مِنَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٢٥﴾

*Usiogope umekwisha kuokoka na watu madhalimu (28:25)*

قَالَ إِنِّي أُرِيدُ أَنْ أُنكِحَكَ إِحْدَى ابْنَتَيَّ هَاتَيْنِ عَلَى أَنْ تَأْجُرَنِي ثَمَنَيْنِ  
حِجَابٍ فَإِنْ أَتَمَمْتَ عَشْرًا فَمِنْ عِنْدِكَ وَمَا أُرِيدُ أَنْ أُلْقِيَ عَلَيْكَ سِتْرًا

إِنْ شَاءَ اللَّهُ مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٢٧﴾

*Akasema: Mimi nataka nikuoze mmoja wapo katika binti zangu hawa wawili kwa kunitumikia miaka minane na kama ukitimiza kumi hiari yako, lakini mimi sitaki kukutaabisha utanikuta Inshaa-Allah miongoni mwa watu wema .(28:27)*

Musa(a.s) aliafiki suala hilo, na mmoja katika wale mabinti aliridhia kuolewa na Musa(a.s) kwa mahari ya kutoa nguvukazi:

قَالَ ذَلِكَ بَيْنِي وَبَيْنَكَ أَيَّمَا الْأَجَلَيْنِ قَضَيْتُ فَلَا عُدْوَانَ

عَلَيَّ وَاللَّهُ عَلَى مَا نَقُولُ وَكِيلٌ ﴿٢٨﴾

*“Akasema(Musa: “Mapatano) hayo yamekwisha kuwa baina yangu na baina yako; muda mmoja wapo nitakaoumaliza, basi nisidhulumumiwe; na Mwenyzi Mungu ni Mlinzi juu ya haya tunayoyasema.”(28:28)*

## Musa(a.s)Kupewa Utume Rasmi

Musa alipotimiza muda, alifunga safari na ahali zake kurejea Misri. Njiani aliona moto upande wa mlimani akawaambia ahali zake:

..... أَمْ كُتِبَ عَلَيْكُمُ النَّارُ إِذْ أَنْتُمْ مِلَّةَ آبَائِكُمُ الَّذِينَ جَاءُوا بِالْحَقِّ كَذِبًا أَوْ كُتِبَ عَلَيْكُمُ النَّارُ إِذْ أَنْتُمْ مِلَّةَ آبَائِكُمُ الَّذِينَ جَاءُوا بِالْحَقِّ كَذِبًا

مِنَ النَّارِ لَعَلَّكُمْ تَصْطَلُونَ ﴿٢٩﴾

.....Ngojeni hakika nimeona moto; labda nitakujieni na habari za huko au kijinga cha moto ili muote (28:29)

فَلَمَّا أَتَاهَا نُودِيَ يَدْمُوسَىٰ ﴿١١﴾ إِنِّي أَنَا رَبُّكَ فَاخْلَعْ نَعْلَيْكَ إِنَّكَ بِالْوَادِ

الْمُقَدَّسِ طَوًى ﴿١٢﴾

*Basi alipofika, aliiitwa: “Ewe Musa! Hakika Mimi ndiye Mola wako. Basi vua viatu vyako. Hakika wewe uko katika bonde takatifu la Tuwa. (20:11-12)*

وَأَنَا أَخْتَرْتُكَ فَاسْتَمِعْ لِمَا يُوحَىٰ ﴿١٣﴾ إِنِّي أَنَا اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا

فَاعْبُدْنِي وَأَقِمِ الصَّلَاةَ لِذِكْرِي ﴿١٤﴾

*Nami nimekuchagua, (uwe Mtume). Basi yasikilize unayoelezwa kupitia wahy. Kwa yakini Mimi ndiye Mwenyezi Mungu, hakuna aabudiwaye kwa haki ila Mimi, Basi niabudu na usimamisha swala kwa kunitaja (20:13-14)*

## Miujiza Kama Ushahidi wa Utume wa Nabii Musa(a.s)

Allah(s.w) alimjaalia Nabii Musa(a.s) miujiza ya kuthibitisha Utume wake. Miujiza si viinimacho kama ilivyo mazingaombwe. Muujiza ni jambo halisi lililola kawaida ambalo hutokea kwa idhini ya Allah(s.w). Musa alipoulizwa na Allah(s.w) kuwa ameshika nini alisema:

.....هِيَ عَصَايَ أَتَوَكَّوْا عَلَيَّهَا وَأَهْشُ بِهَا عَلَىٰ غَنَمِي وَلِيَ فِيهَا مَنَازِبُ

أُخْرَىٰ ﴿١٨﴾

.....Akasema: “Hii ni fimbo yangu, ninaiegemea na ninaangushia majani kwa ajili ya wanyama wangu. Tena ninaitumia kwa mambo mengine.(20:18)

Inadhihirika hapa kuwa Nabii Musa alikuwa na fimbo ya kawaida kabisa, lakini Allah(as) anaigeuza kuwa muujiza.

قَالَ أَلَيْهَا يَدْمُوسَىٰ ﴿١٩﴾ فَالْقَدِّهَا فَإِذَا هِيَ حَيَّةٌ تَسْعَىٰ ﴿٢٠﴾ قَالَ خُذْهَا وَلَا  
تَخَفْ سَنُعِيدُهَا سِيرَتَهَا الْأُولَىٰ ﴿٢١﴾

Allah(s.w) akasema: *Itupe, ewe Musa*". Akaitupa. *Mara ikawa nyoka anayekwenda mbio. Allah akasema: "Ikamate wala usiogope, sasa hivi Tutairudisha hali yake ya kwanza.(20:19-21)*

وَأَضْمَمْ يَدَكَ إِلَىٰ جَنَاحِكَ تَخْرُجَ بَيْضَاءَ مِنْ غَيْرِ سُوءٍ آيَةٌ أُخْرَىٰ ﴿٢٢﴾  
لِنُرِيكَ مِنْ آيَاتِنَا الْكُبْرَىٰ ﴿٢٣﴾

*"Na uambatanishe mkono wako katika kwapa lako; utatoka ukiwa mweupe sana pasipo na ubaya wowote. Huu ni muujiza mwingine. Ili Tukuoneshe miujiza mingine mikubwa (20:22-23)*

Inabainika wazi kuwa chanzo cha miujiza yote aliyokuwa nayo Musa na Mitume wengine, ni Allah(s.w). Hakuna Mtume au Nabii aliyefanya miujiza kwa uweza wake mwenyewe!

## Harun(a.s), Achaguliwa Kuwa Msaidizi Musa(a.s)

Nabii Musa(a.s)alimuomba Allah(s.w) amsaidie(amuwezeshe) kulimudu jukumu zito alilompa na pia alimuomba amfanye Harun(a.s) awe msaidizi wake. Harun alikuwa ndugu yake Musa(a.s)

قَالَ رَبِّ اشْرَحْ لِي صَدْرِي ﴿٢٥﴾ وَيَسِّرْ لِي أَمْرِي ﴿٢٦﴾  
وَأَحْلِلْ عُقْدَةَ مِنِّي لِسَانِي ﴿٢٧﴾ يَفْقَهُوا قَوْلِي ﴿٢٨﴾ وَأَجْعَلْ لِي وَزِيرًا مِّنْ  
أَهْلِي ﴿٢٩﴾ هَٰنُرُونَ أَخِي ﴿٣٠﴾ أَشَدُّ بِهِ أَرْزِي ﴿٣١﴾ وَأَشْرِكُهُ فِي أَمْرِي  
﴿٣٢﴾ كَيْ نُسَبِّحَكَ كَثِيرًا ﴿٣٣﴾ وَنَذْكُرَكَ كَثِيرًا ﴿٣٤﴾ إِنَّكَ كُنْتَ  
بِنَا بَصِيرًا ﴿٣٥﴾

*Akasema: Ewe Mola wangu! Nipanulie kifua changu(nipe subira). Na unifanyie wepesi katika kazi yangu. Na ufungue fundo lililo katika ulimi wangu. Wapate kufahamu maneno yangu. Na unifanyie waziri katika jamaa zangu. Ndugu yangu Harun. Nitie nguvu kwa huyu. Na umshirikishe katika kazi yangu hii. Ili tukutukuze sana. Na tukutaje kwa wingi. Hakika Wewe unatuona (20:25-35)*

Allah(s.w) alilikubali ombi la Nabii Musa (a.s), akamfanya Harun(a.s) kuwa Nabii pamoja naye. Allah(s.w) akasema kumwambia Musa:

قَالَ قَدْ أُوتِيتَ سُؤْلَكَ يَا مُوسَى ﴿٣٦﴾

*Hakika umekubaliwa maombi yako, Ewe Musa (20:36)*

## **Musa na Harun(a.s) Kumkabili Firaun**

Jukumu kubwa la kwanza walilokabidhiwa Musa(a.s) na Harun(a.s) lilikuwa kumwambia Firauni amwamini Allah(s.w) na awache kukiuka haki za binadamu kwa kuwapa Waisraili uhuru wao. Basi wakamkabili Firaun wakamwambia:

.....إِنَّا رَسُولَا رَبِّكَ فَأَرْسِلْ مَعَنَا بَنِيَّ

إِسْرَائِيلَ وَلَا تُعَذِّبْهُمْ قَدْ جِئْنَاكَ بِبَيِّنَاتٍ مِّن رَّبِّكَ وَالسَّلَامُ عَلَيْنَا

مَنْ أَتَّبَعَ الْهُدَىٰ

*.....Kwa hakika sisi ni Mitume wa Mola wako. Basi waachie wana wa Israili watoke pamoja nasi, wala usiwaadhibu. Hakika tumekuletea ishara zitokazo kwa Mola wako. Na amani itakuwa kwa wale wanaofuata uongofu (20:47)*

Firauni kwa jinsi alivyokuwa amezama katika siasa za kidhalimu na unyonyaji hakupenda kabisa kuona Wana Israil wanarejeshewa haki zao za kibinadamu za kuwa huru. Akasema Firauni kwa kibiri na jeuri kubwa kuwa:

.....يَتَأْتِيهَا الْمَلَأُ مَا عَلِمْتُ لَكُمْ مِنْ إِلَهٍ غَيْرِي .....

.....Enyi wakuu! Simjui kwa ajili yenu, mungu asiye kuwa mimi.....(28:38)

﴿٢٤﴾ فَقَالَ أَنَا رَبُّكُمُ الْأَعْلَىٰ

Akasema: Mimi ndiye mola wenu mkuu. (79:24)

Nabii Musa(a.s.) alijitahidi kumuelimisha Firauni na watu wake juu ya Mungu mmoja anayekataza dhulma, ukandamizaji na ukiukaji wa haki za binadamu. Lakini Firauni kwasababu ya kupenda sana dhulma, akazusha uongo akiwatangazia watu kwa kuwaambia:

﴿٢٧﴾ قَالَ إِنَّ رَسُولَكُمْ الَّذِي أُرْسِلَ إِلَيْكُمْ لَمَجْنُونٌ

Bila shaka Mtume wenu aliyetumwa kwenu ni mwendawazimu(26:27)

Pamoja na kujibiwa kwa dharau na kukashifiwa, Musa aliendelea kufafanua zaidi juu ya Mwenyezi Mungu anayemiliki ulimwengu mzima.

..... رَبُّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَمَا بَيْنَهُمَا إِنْ كُنْتُمْ تَعْقِلُونَ ﴿٢٨﴾

.....(Allah ndiye) Mola wa Mashariki na Magharibi na vilivyomo baina yake ikiwa (mna akili) mfahamu (26:28)

Aliposhindwa kujibu hoja hiyo, Firauni akapandwa na hasira na kuanza kumtishia Musa(a.s):

﴿٢٩﴾ قَالَ لَيْنِ اتَّخَذَتِ إِلَهًا غَيْرِي لِأَجْعَلَنَّكَ مِنَ الْمَسْجُودِينَ

Firauni akasema: Kama ukishikilia (kuwa kuna) Mungu mwingine badala yangu, kwa hakika nitakufanya miongoni mwa wenye kufungwa gerezani(26:29)

Lakini Musa(a.s) hakutishika kabisa kwa hizo kauli za Firauni. Badala yake akataka kumdhihirishia kuwa Allah(s.w) ana nguvu na uweza wa kufanya mambo makubwa ya kutisha zaidi kuliko hayo magereza yake.

فَأَلْقَى عَصَاهُ فَإِذَا هِيَ ثُعْبَانٌ مُّبِينٌ ﴿٣٢﴾ وَنَزَعَ يَدَهُ فَإِذَا هِيَ بَيْضَاءُ لِلنَّظِيرِينَ ﴿٣٣﴾

*Basi(Musa) akatupa fimbo yake, mara ikawa nyoka aliye dhahiri. Na akatoa mkono wake, na mara ukawa mweupe (kweli kweli) kwa watazamao(26:32-33)*

Hapo Firaun akatishika na alidhani kuwa ile miujiza aliyokuja nayo Nabii Musa(a.s) ni sawa na mazingaombwe au viinimacho wanavyofanya wachawi.

قَالَ لِلْمَلَآئِكَةِ إِنِّي هَذَا لَسِحْرٌ عَلِيمٌ ﴿٣٤﴾ يُرِيدُ أَنْ يُخْرِجَكُمْ مِنْ أَرْضِكُمْ بِسِحْرِهِ فَمَاذَا تَأْمُرُونَ ﴿٣٥﴾

*Akasema, kuwaambia wakuu waliomzunguka: Hakika huyu ni mchawi ajuae sana. Anataka kukutoeni katika nchi yenu kwa uchawi wake; basi mnasemaje? (26:34-35)*

## Kusilimu kwa Wachawi wa Firaun

Mawaziri waliokuwa washauri wakuu wa Firauni wakataka wakusanywe magwiji waliobobea katika uchawi nchi nzima, kisha wapambanishwe na Nabii Musa(as).

فَلَمَّا جَاءَ السَّحَرَةُ قَالُوا لِفِرْعَوْنَ أَئِن لَّنَا لَأَجْرٌ إِن كُنَّا نَحْنُ الْغَالِبِينَ ﴿٤١﴾ قَالَ نَعَمْ وَإِنَّكُمْ إِذَا لَّمِنَ الْمُقَرَّبِينَ ﴿٤٢﴾

*Basi walipofika wachawi, wakamwambia Firauni: Je, tutapata ujira tukiwa sisi ndio tutakaoshinda. Akasema: Naam, na pia*

*mtakuwa miongoni mwa wale wanaowekwa mbele katika (Serikali) (26:41-42)*

فَأَلْقُوا حَبَالَهُمْ وَعَصِيَّهُمْ وَقَالُوا بِعِزَّةِ فِرْعَوْنَ إِنَّا لَنَحْنُ الْعَالِيُونَ ﴿٤٤﴾

*Basi wakatupa kamba zao na fimbo zao, na wakasema: Kwa nguvu za Firauni sisi tutakuwa ndio wenye kushinda (26:44)*

فَأَلْقَى مُوسَى عَصَاهُ فَإِذَا هِيَ تَلْقَفُ مَا يَأْفِكُونَ ﴿٤٥﴾

*Kisha Musa akatupa fimbo yake, nayo mara ikavimeza(vyote) walivyozusha wachawi (26:45)*

Wachawi walipoona vitu vyao vya kichawi(viini macho) walivyovitupa uwanjani vimemezwa vyote na nyoka(wa muujiza), walisalimu amri na kutoa shahada:

فَأَلْقَى السَّحَرَةُ سَجِيدِينَ ﴿٤٦﴾ قَالُوا ءَأَمْنَا بِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٤٧﴾ رَبِّ

مُوسَى وَهَارُونَ ﴿٤٨﴾

*Hapo wachawi walipinduka wakasujudu. Wakasema: Tumemuamini Mola wa walimwengu wote. Mola wa Musa na Harun (26:46-48)*

Firaun aliwatishia wachawi kuwapa adhabu kubwa kwa kusilimu kwao pasina idhini yake (Qur'an 26:49). Inabainika hapa kuwa uchawi si sawa na muujiza, na ndio maana wachawi walishindwa. Hakika uliwadhihirikia ukweli kwamba Musa(a.s) ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Ndio maana Firauni alipotangaza kuwa atawasulubu kwa kuwakata miguu na mikono yao kwa sababu wamesilimu pasina ridhaa yake; hawakuyumba katika imani yao.

قَالُوا لَا ضَيْرَ إِنَّا إِلَىٰ رَبِّنَا مُنْقَلِبُونَ ﴿٥٠﴾ إِنَّا نَطْمَعُ أَنْ يَغْفِرَ لَنَا

رَبُّنَا خَطَايَنَا أَنْ كُنَّا أَوَّلَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٥١﴾

*Wakasema: Haidhuru, hakika sisi sote tutarejea kwa Mola wetu. Kwa yakini sisi tunatumai ya kwamba Mola wetu atatusamehe*



*makosa yetu, maana sisi tumekuwa wa kwanza wa wenye kusilimu hapa (26:50-51)*

## **Kuangamizwa Firauni na Majeshi Yake**

Baada ya ushindi alioupata Musa(a.s) dhidi ya wachawi, umati wa watu waliokuwa wamekusanyika kushuhudia mapambano baina ya haki na batili, waliona ukweli kuwa Musa(a.s) ndiye kiongozi halali anayepaswa kutiwa, na haifai kabisa kutiwa Firauni dhalimu. Kuanzia hapo waliomuamini Musa wakapata adha na mateso zaidi kutoka kwa Firauni. Ndipo Allah(s.w) alipomuamuru Musa(a.s):

﴿ وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ أَنْ أَسْرِ بِعِبَادِي إِلَيْكُمْ مُتَّبِعُونَ ﴿٥٢﴾ ﴾

*“Nenda na waja wangu wakati wa usiku(mtoke nchini Misri), bila shaka mtafuatwa (26:52)*

﴿ فَلَمَّا تَرَىٰءَ الْجَمْعَانَ قَالَ أَصْحَابُ مُوسَىٰ إِنَّا لَمُدْرِكُونَ ﴿٥١﴾ ﴾ قَالَ كَلَّا ۗ

﴿ إِنَّ مَعِيَ رَبِّي سَيَهْدِينِ ﴿٥٢﴾ ﴾

*Na yalipokutana majeshi mawili. Watu wa Musa walisema. Hakika tutakamatwa. Musa akasema: La, kwa yakini Mola wangu Yu pamoja nami bila shaka ataniongoza.(26:61-62)*

Wanalsrailwalikuwa wamekwama kuendeleana safari kutokana na kuzuiwa na bahari hali ya kuwa Firauni na majeshi yake yamekwisha wakaribia. Kwa huruma na rehema zake, Allah(s.w) akamuongoza Musa kwa kumwambia:

..... أَنْ أَضْرِبَ بِعَصَاكَ الْبَحْرَ ۖ فَانْفَلَقَ فَكَانَ كُلُّ فِرْقٍ

﴿ كَالطَّوْدِ الْعَظِيمِ ﴿٦٣﴾ ﴾

*Piga bahari kwa fimbo yako; basi ikatengana, na kila sehemu ikawa kama mlima mkubwa. (26:63)*

Bahari iligawanyika sehemu mbili na kuwacha njia ambayo Nabii Musa alipita na watu wake kwa salama. Lakini majeshi ya Firaun yalipofika katikati, maji ya bahari yalirudi katika nafasi yake na kuangamizwa yote. Firaun akawa anatapatapa, akijitupa huku na kule na akaona kuwa hapana nusra ila kutoka kwa Allah(s.w) ndipo akatoa shahada kuwa:

.....عَامَنْتُ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا الَّذِي عَامَنْتُ بِهِ بَنُوءَ إِسْرَائِيلَ

وَأَنَا مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿٩٠﴾

.....Naamini ya kwamba hakuna Mola aabudiwaye kwa haki ila Yule wanayemuamini wana wa Israeli, na mimi ni miongoni mwa wanaotii (10:90)

عَالَفَنَ وَقَدْ عَصَيْتَ قَبْلُ وَكُنْتَ مِنَ الْمُفْسِدِينَ ﴿٩١﴾ فَالْيَوْمَ نُنَجِّيكَ

بِبَدَنِكَ لِيَتَكُونَ لِمَنْ خَلَقَكَ آيَةً وَإِنَّ كَثِيرًا مِنَ النَّاسِ عَنْ

آيَاتِنَا لَغَافِلُونَ ﴿٩٢﴾

(Malaika wakamwambia)” Sasa (ndio unaamini)! hali uliasi kabla ya hapo na ukawa miongoni mwa waharibifu. Basi leo tutakuokoa kwa kuuweka mwili wako ili uwe dalili kwa ajili ya wa nyuma yako. Na watu wengi wameghafilika na ishara zetu.(10:91-92)

Huo ukawa ndio mwisho wa utawala wa kifirauni.

## **Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Musa(a.s) na Harun(a.s)**

Kutokana na Historia ya Nabii Musa na Harun(a.s) tunajifunza yafuatayo:

- (i) Tunajifunza kuwa ni muhimu kuweka mipango katika kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii. Allah(s.w) anauwezo wa kukiamrisha kitu “kiwe” na kikawa pale pale, lakini bado tunaona ameweka mpango wa muda mrefu wa kuwaokoa Bani Israil na makucha ya Firaun.

- (ii) Vile vile mpango huu wa Allah(s.w) wa kuwakomboa Bani Israil, unatufunza kuwa kuibadilisha jamii ya kijahili kuwa ya Kiislamu ni jambo linalohitaji muda na subira.
- (iii) Elimu na siha ni nyenzo muhimu za kumuwezesha mtu kuwa khalifa katika ardhi. Nabii Musa alipewa siha nzuri na kuruzukiwa akili na elimu.
- (iv) Hakuna hila wala nguvu zinazoweza kuzuia jambo analotaka Allah(s.w) liwepo au lisiwepo katika jamii, yeye anazo namna nyinyi za kumlinda mja wake na vile vile anaweza kumuangamiza mbabe yeyote awaye.
- (v) Tabia njema na kuwatendea watu wema ni nyenzo muhimu katika harakati za kusimamisha Uislamu katika jamii. Nabii Musa(a.s) kwa wema wake aliletewa taarifa ya mipango ya Firaun dhidi yake; pia kwa huruma yake alipata hifadhi kwa mzee wa Madian.
- (vi) Hakuna binaadamu asiyeteleza na kumkosea Allah(s.w), lakini muumini anakuwa mwepesi wa kurejea kwa Allah (s.w). Musa(a.s) aliteleza kwa kuingilia ugomvi asioujua na kumuua mtu, alirejea kwa Mola wake haraka haraka—Qur-an (28:16).
- (vii) Muumini wa kweli hanabudi kuchukia vitendo vya dhuluma na kuwa tayari kuwatetea wanaodhulumiwa haki zao kwa kadiri ya uwezo wake.
- (viii) Ni muhimu kuwekeana mikataba ya kazi tunapoajiri au kuajiriwa. Nabii Musa(a.s) aliwekeana mkataba wa kazi na mzee wa Madian.
- (ix) Nyanzo muhimu ya kutuwezesha kusimamisha Uislamu katika jamii baada ya Elimu ni kusimamisha Swala za Faradh na sunah, Qiyamullayl na kuleta dhikiri kwa wingi – Qur-an(20:14), (73:1-10), (74:1-7).

- (x) Miujiza ni katika dalili za kuwepo Allah(s.w).
- (xi) Katika harakati za kusimamisha Uislamu katika jamii tunatakiwa tusimvamie tu kila mtu na kumingiza kwenye harakati, bali tuanze na ndugu, jamaa na rafiki wa karibu ambao tunajua fika tabia na mwenendo wao. Nabii Musa (a.s) aliomba ndugu yake Harun awe msaidizi wake si kwa kuwa alikuwa ndugu yake tu, bali alimfahamu fika kwa ucha Mungu wake.
- (xii) Muumini mwanaharakati hahongeki kwa fadhila atakazofanyiwa na madhalimu ili arudi nyuma katika kusimamisha uadilifu. Musa(a.s) alilelewa katika nyumba ya mfalme, lakini hakuacha kudhihirisha kwa matendo udhalimu wa Firaun na serikali yake ikawa ndio sababu ya kuhukumiwa kifo.
- (xiii) Ni kawaida ya matwaghuti kufanya propaganda dhidi ya wanaharakati na kuwapachika majina mabaya. Firaun na serikali yake alimpakazia Nabii Musa(a.s) uwendawazimu na uchawi.
- (xiv) Hapana yeyote wa kumchelea katika kutekeleza amri ya Allah(s.w) ya kusimamisha Uislamu katika jamii. Musa na Harun(a.s) walimkabili Firaun na wakuu wake wa Dola waliozungukwa na majeshi na kuwafikishia ujumbe wa Allah(s.w).
- (xv) Hapana yeyote mwenye uwezo wa kutweza au kutengua maamuzi ya nafsi ya mwanaadamu. Wachawi walipobainikiwa na Haki na wakashilimu, Firaun hakuweza kuwaritadisha pamoja na adhabu kali aliyoitoa dhidi yao – Qir-an (26:49-51).
- (xvi) Toba inayokubalika ni ile inayoletwa haraka kabla ya kufikwa na mauti – Qur-an (4:18).

(xvii)Kuishi nje ya shahada na kutarajia kufa ndani ya shahada ni muhali. Allah(s.w) ametuamrisha tuishi na shahada na tujitahidi kubakia nayo mpaka kufa kwetu– Qur-an (3:102).

## **HISTORIA YA BANI ISRAIL**

Nabii Musa na Harun walikuwa na kazi kubwa mbili; kwanza, kuwakomboa Bani Israil kutokana na dhuluma waliyokuwa wakifanyiwa na Firaun na Serikali yake, na pili, kuwarudisha kwenye nchi yao takatifu ya Palestina. Nchi hii imeitwa takatifu kwa sababu ilikuwa nchi iliyo kaliwa na Mitume watukufu, Ibrahim(a.s),Is-haq(a.s) na Ya'aquub(a.s). Palestina pamoja na kuwa nchi iliyokaliwa na Mitume maarufu kama hao, watu waliofuatia baadaye waliacha mafunzo yao na kuanzisha mifumo ya maisha ya kishirikina. Hivyo Bani Israil walitakiwa warudi nchini mwao wakautawalishe Uislamu juu ya mfumo ya kishirikina uliokuwemo mle.

Kutoka Misr walienda hadi Mlima Sinai. Hapa walikaa kwa muda wa mwaka mmoja ambapo Nabii Musa(a.s) alishushiwa karibu hukumu zote za Taurat.

### **Musa(a.s) Kupewa Taurati**

Musa(a.s) alitwa na Allah(s.w) katika Mlima Sinai ili apewe sharia kwa ajili ya wana wa Israili. Siku arubaini ziliteuliwa ili Mtume aweze kujiandaa mwenyewe kwa kufunga na kuswali kwa ajili ya kazi ngumu inayomsubiri ya kuwaongoza Bani Israil wakasimamisha ufalme wa Allah(s.w) katika nchi ya Palestina. Wakati huu Mtume Musa aliwaacha Bani Israil (Mayahudi) katika sehemu ambayo sasa huitwa Wadiy-Shaikh ambayo ipo kati ya Nubi Salih na Mlima Sinai. Mlima Sinai una urefu wa futi 7,359 toka usawa wa bahari na mara nyingi huwa umefunikwa na mawingu. Kileleni mwa mlima huu lipo pango ambapo Nabii Musa (a.s) alikaa siku arobaini. Leo hii karibu na pango hilo pana msikiti na kanisa.

Habari ya kuitwa Musa katika Mlima Sinai inatajwa katika aya zifuatazo:

﴿وَوَاعَدْنَا مُوسَى ثَلَاثِينَ لَيْلَةً وَأَتَمَّمْنَاهَا بِعَشْرِ فِتْمٍ مِيقَاتٍ رَبِّهِ  
أَرْبَعِينَ لَيْلَةً وَقَالَ مُوسَى لِأَخِيهِ هَارُونَ أَخْلُفْنِي فِي قَوْمِي وَأَصْلِحْ وَلَا  
تَتَّبِعْ سَبِيلَ الْمُفْسِدِينَ ﴿١٤٢﴾﴾

*Na tulimuhidi Musa siku thalathini (afanye ibada, kisha tumpe Taurati) na tukazitimiza kwa kumi ikatimia miadi ya Mola wake siku arubaini. Na Musa akamwambia ndugu yake Haruni: "Shika mahali pangu katika (kuwaangalia) watu wangu na utengeneze wala usifuate njia ya waharibifu" (7:142).*

Kama aya inavyobainisha, ilipotimia miadi Musa alikwenda kupokeasheria.

﴿قَالَ يَمْؤَسَىٰ اِيَّيْ اَصْطَفَيْتَكَ عَلٰى النَّاسِ بِرِسَالَتِي وَبِكَلِمٰى فَاخْذُ مَا  
عَاتَيْتَكَ وَكُن مِّنَ الشَّاكِرِيْنَ ﴿١٤٤﴾ وَكَتَبْنَا لَهُ فِي الْاَلْوَاْحِ مِنْ كُلِّ شَيْءٍ  
مَّوْعِظَةً وَتَفْصِيْلًا لِّكُلِّ شَيْءٍ فَخَذَهَا بِقُوَّةٍ وَاَمْرًا قَوْمَكَ يَأْخُذُوْا بِاَحْسَنِهَا  
سَاُوْرِيْكُمْ دَارَ الْفٰنِيْنَ ﴿١٤٥﴾﴾

*Akasema (Mwenyezi Mungu): "Ewe Musa! Mimi nimekuchagua juu ya watu wote kwa ujumbe wangu na kusema nawe kwangu. Basi pokea haya niliyokupa, na uwe miongoni mwa wanaoshukuru". "Na tulimwandikia katika mbao kila kitu - mawaidha (ya kila namna) na maelezo ya kila jambo. "Basi yashike kwa imara na uwaamrishe watu wako wayashike vema haya. Karibuni nitakuonyesheni miji ya wavunjao amri (zetu namna ilivyoharibika)" (7:144-145).*

## Bani Israil Kuabudu Ndama

Wakati Nabii Musa(a.s) amekwenda kupokea Taurati, katika hizo siku arobaini alizoahidiwa na Mola Wake, Saamiriy alitengeneza sanamu la ndama wa ng'ombe linalotoa sauti unapovuma upepo na kuwashawishi Bani Israil walifanye mungu sanamu hilo la ndama.

وَإِذْ وَعَدْنَا مُوسَىٰ أَرْبَعِينَ لَيْلَةً ثُمَّ اتَّخَذْتُمُ الْعِجْلَ مِن بَعْدِهِ  
وَأَنْتُمْ ظَالِمُونَ ﴿٥١﴾

*"Na kumbukeni tulipomuahidi Musa siku arobaini (afanye ibada mfululizo) Mkamfanya ndama (kuwa Mungu) baada yake, na mkawa madhalimu (wa nafsi zenu)" (2:51).*

Harun(a.s) aliyemkaimu Nabii Musa(a.s) aliwakataza watu wake wasiabudie sanamu la ndama. Baadhi wakamtii na wengine wakamuasi.

وَلَقَدْ قَالَ لَهُمْ هَارُونُ مِن قَبْلُ يَا قَوْمِ إِنَّمَا فُتِنْتُمْ بِهِ  
وَإِنَّ رَبَّكُمُ الرَّحْمَنُ فَاتَّبِعُونِي وَأَطِيعُوا أَمْرِي ﴿٩٠﴾ قَالُوا لَنْ نَبْرَحَ  
عَلَيْهِ عَاكِفِينَ حَتَّىٰ يَرْجِعَ إِلَيْنَا مُوسَىٰ ﴿٩١﴾

*Na Harun aliwaambia zamani (akasema): "Enyi watu wangu! Hakika nyinyi mumefitinishwa tu kwa (kitu) hiki. Na kwa yakini Mola wenu ni yule Mungu Mwenye kurehemu. Basi nifuateni na tiini amri yangu (muache kuabudu Mungu huyu)".  
Wakasema: "Hatutaacha kabisa kumuabudu mpaka Musa arejee kwetu, (aturudie)" (20:90-91).*

Musa(a.s) aliporejea alimlaumu Harun(a.s) kwa kutomfuata huko alikokuwa baada ya watu wake kumuasi. Harun(a.s) alijitetea kuwa hakufanya hivyo kwa kuchelea kuwafarakanisha Bani Israil kwa kuondoka na kundi moja na kuliacha lingine nyuma kabla ya kauli yake (Musa(a.s)) - rejea (Qur'an 2:92-94).

Musa(a.s) aliondoa ile fitina kwa kumuadhibu Saamiriy na walioshirikiana naye na kuliangamiza lile sanamu.

Ikumbukwe kuwa ni muda mfupi sana toka Bani Israil walipokombolewa kutokana na utumwa wa Firauni. Lakini mara wanamsahau Mola wao na kuanza kuabudu ndama. Hii inaonesha ni kwa kiwango gani Bani Israil waliathiriwa na maisha ya ushirikina kwa kipindi walichoishi Misr. Ni muhimu basi tuone jinsi mazingira yanavyoathiri imani, maadili na mwenendo wa mtu.

## Musa(a.s) Kuwaongoza Bani Israil Hadi Palestina

Baada ya matukio haya ndipo Musa(a.s) aliamuriwa kuwaongoza Bani Israil hadi Palestina. Aliwaongoza kupitia Taberah na Hazeroth hadi kwenye jangwa la Paran. Hapo Nabii Musa(a.s) alituma watu mashuhuri kufanya upelelezi Palestina. Baada ya siku arobaini ujumbe huu ulirejea na taarifa yao waliitolea sehemu iitwayo Kadesh. Taarifa za wajumbe wote ila wawili (Joshua na Caleb) ziliwakatisha tamaa. Hivyo wakagoma kuingia Palestina. Hawakutaka kabisa kutoa nafsi zao muhanga. Bali walitaka Allah(s.w) awatengenezee kila kitu wao waje tu kuvuna na kufaidi matunda. Kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

يَنْقُومُ ادْخُلُوا الْأَرْضَ الْمُقَدَّسَةَ الَّتِي كَتَبَ اللَّهُ لَكُمْ  
وَلَا تَرْتَدُّوا عَلَى أَدْبَارِكُمْ فَتَنْقَلِبُوا خَاسِرِينَ ﴿٢١﴾ قَالُوا يَمْوَسَىٰ  
إِنَّ فِيهَا قَوْمًا جَبَّارِينَ وَإِنَّا لَنَنذُرُهَا حَتَّىٰ يَخْرُجُوا مِنْهَا  
فَلَمَّا يَخْرُجُوا مِنْهَا فَإِنَّا دَاخِلُونَ ﴿٢٢﴾ قَالَ رَجُلَانِ مِنَ الَّذِينَ  
يَخَافُونَ أُنْعِمِ اللَّهُ عَلَيْهِمَا ادْخُلُوا عَلَيْهِمُ الْبَابَ فَإِذَا دَخَلْتُمُوهُ  
فَأِنَّكُمْ غَالِبُونَ وَعَلَى اللَّهِ فَتَوَكَّلُوا إِن كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿٢٣﴾



قَالُوا يَمْوَسَىٰ إِنَّا لَن نَّدْخُلَهَا أَبَدًا مَّا دَامُوا فِيهَا فَادْهَبْ أَنتَ وَرَبُّكَ

فَقَدِيلًا إِنَّا هُنَا قَاعِدُونَ ﴿٢٤﴾

“(Musa(a.s) akasema): “Enyi watu wangu! Ingieni katika hiyo ardhi (nchi) iliyotakaswa ambayo Mwenyezi Mungu amekuandikieni. Wala msirudi nyuma, msije mkawa wenye kukhasirika”. Wakasema: “Ewe Musa! Huko kuna watu majabari. Nasi hatutaingia huko mpaka watoke humo, wakitoka humo hapo tutaingia”. Watu wawili miongoni mwa wale waliomwogopa (Allah) ambao Mwenyezi Mungu amewaneemesha, walisema (kuwaambaia wenzao). “Waingilieni katika hilo lango (la nchi yao); maana mtakapo waingilia hapo, kwa yakini nyinyi mtashinda. Na tegemeeni juu ya Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni wenye kuamini”. Wakaema: Ewe Musa! Sisi hatutaingia humo kamwe maadamu wao wamo humo. Basi nenda wewe na Mola wako mkapigane, sisi tutakaa hapa (kungojea nini litakalokuwa)” (5:21-24).

Baada ya ukaidi huu Nabii Musa(a.s) hakuwa na la kufanya tena bali kuleta dua ifuatayo:

قَالَ رَبِّ إِنِّي لَا أَمْلِكُ إِلَّا نَفْسِي وَأَخِي فَافْرِقْ بَيْنَنَا وَبَيْنَ الْقَوْمِ الْفَاسِقِينَ ﴿٢٥﴾

(Musa) akasema: “Mola wangu! Hakika mimi similiki ila nafsi yangu na ndugu yangu; basi tutenge na hawa mafasiki”.(5:25)

Allah(s.w) aliwatia adabu kwa ukaidi wao; wakawa wanatangatanga Jangwani kwa muda wa miaka arobaini.

قَالَ فَإِنَّهَا مُحَرَّمَةٌ عَلَيْهِمْ أَرْبَعِينَ سَنَةً يَتِيهُونَ فِي الْأَرْضِ فَلَا تَأْسَ عَلَى

الْقَوْمِ الْفَاسِقِينَ ﴿٢٦﴾

(Mwenyezi Mungu) akasema: “Basi wameharamishiwa (ardhi) hiyo kwa (muda wa) miaka arobaini, watatangatanga (mumu

*humu) ardhini (jangwani muda wote huo). Basi usihuzunike juu ya watu maasi" (5:26).*

Basi Mayahudi hawa wakadumu kuhangaika majangwani bila kupumua. Kizazi kipya kilichochipuka baadaye wakawa na mwendo mzuri na utii. Wakapigana na majabari wa Palestina na wakatawala wao.

## **Amri ya Kuchinja Ng'ombe**

Kutokana na kuishi kwao Misr kwa muda mrefu, Mayahudi waliathiriwa na ibada za kishirikina za Wamisr. Wakawa nao wanabuni miungu ya vitu vilivyo hai na visivyo hai. Moja ya miungu waliyoibuni ni ng'ombe mwenye sifa maalum. Asiye mzee sana wala mchanga, mwenye rangi ya dhahabu na asiye fanyishwa kazi. Kwa hiyo pamoja na kuwa baadhi ya Mayahudi walifuata sheria ya Musa(a.s), lakini bado athari ya ibada ya ng'ombe ikawa imesalia katika nafsi zao.

Katika mazingira hayo, Nabii Musa(a.s) alipewa amri na Mola wake awaamrishe wachinje ng'ombe. Huu ukiwa ni mtihani wa imani kwao kuthibitisha kwamba kweli wamemuamini Allah(s.w) au la. Mtihani huu ukawa mgumu sana kwao. Wakajaribu kuukwepa kwa kuleta maswali kadhaa ya udadisi. Lakini kila walivyozidi kudadisi juu ya ng'ombe waliyeambiwa wamchinje ndivyo walivyojiingiza mahali pagumu zaidi. Kwani majibu waliyokuwa wakiyapata yaliwataka wamchinje ng'ombe mwenye sifa sawa na yule wanayemuabudu. Basi hatima yake wakamchinja japo kwa shingo upande.

Fundisho lililokusudiwa lilipatikana kwani kile walichokidhania kitakatifu hata kukiabudu walikichinja kwa mikono yao wenyewe na wala hawakupata dhara lolote. Qur'an yabainisha tukio hili katika aya zifuatazo:

وَإِذْ قَالَ مُوسَى لِقَوْمِهِ إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَنْ تَذْبَحُوا بَقَرَةً قَالُوا أَتَتَّخِذُنَا هُزُؤًا قَالَ أَعُوذُ بِاللَّهِ أَنْ أَكُونَ مِنَ الْجَاهِلِينَ ﴿١٧﴾ قَالُوا أَذْعُ لَنَا رَبِّكَ يُبَيِّنُ لَنَا مَا هِيَ قَالَ إِنَّهُ يَقُولُ إِنَّهَا بَقَرَةٌ لَا فَارِصٌ وَلَا بَكَرٌ عَوَانٌ بَيْنَ ذَلِكَ فَافْعَلُوا مَا تُؤْمَرُونَ ﴿١٨﴾ قَالُوا أَذْعُ لَنَا رَبِّكَ يُبَيِّنُ لَنَا مَا لَوْثُهَا قَالَ إِنَّهُ يَقُولُ إِنَّهَا بَقَرَةٌ صَفْرَاءٌ فَاقِعٌ لَوثُهَا تَسْرُ النَّظِيرِينَ ﴿١٩﴾ قَالُوا أَذْعُ لَنَا رَبِّكَ يُبَيِّنُ لَنَا مَا هِيَ إِنَّ الْبَقَرَ تَشَدَّبَ عَلَيْنَا وَإِنَّا إِنْ شَاءَ اللَّهُ لَمُهْتَدُونَ ﴿٢٠﴾ قَالَ إِنَّهُ يَقُولُ إِنَّهَا بَقَرَةٌ لَا ذَلُولٌ تُثِيرُ الْأَرْضَ وَلَا تَسْقِي الْحَرثَ مُسَلَّمَةٌ لَا شِيَةَ فِيهَا قَالُوا الْإِنِّ جِئْتَ بِالْحَقِّ فَذَبَّحُوهَا وَمَا كَادُوا يَفْعَلُونَ ﴿٢١﴾

"Na Musa alipowaambia watu wake: "Hakika Mwenyezi Mungu anakuumrisha ni mchinje ng'ombe". Wakasema: "Je! Unatufanyia mzaha?" Akasema "(La) Najikinga kwa Mwenyezi Mungu kuwa miongoni mwa wajinga. Wakasema: "Tuombe kwa Mola wako atupambanulie ni (wa umri) gani (ng'ombe huyo)?" Akasema: "Hakika Yeye anasema kwamba ng'ombe huyo si mzee wala si mchanga, bali ni wa katikati baina ya hao. Basi fanyeni mnavo arishwa". Wakasema: "Tuombe kwa Mola wako atupambanulie ni vipi hali yake, hakika ng'ombe wanafanana; (basi yupi)? Na kwa hakika kama Mungu akipenda (tutafuata) tuwe wenye kuongoka". Akasema: "Yeye anasema: Kuwa huyo si ng'ombe aliyetiwa kazini kulima ardhi wala kutilia maji mimea, safi kabisa rangi yake, hana kipaku ndani yake". Wakasema: "Sasa umeleta (maneno ya) haki". Basi wakamchinja, na walikuwa mbali na kufanya hayo". (2:67-71).

Pamoja na fundisho kuu tulilolitaja awali la kujenga hoja dhidi ya shirk; lakini pia aya zinatutanabahisha kuwa tusijaribu kuzikwepa amri za Allah(s.w) kwa kuleta maswali ya udadisi na visingizio. Maadhali jambo limethibiti kuwa ni amri ya Allah basi hatuna hiari bali ni kulitekeleza kwa moyo mkunjufu.

## Neema za Allah(s.w) Juu ya Bani Israil.

Katika Qur'an tunakumbushwa neema mbali mbali walizotunukiwa Bani Israil (Mayahudi) na Mola wao ili kuwawezesha kusimamisha Ufalme wa Allah(s.w)katika ardhi takatifu. Lakini ubaya wa bahati, Bani Israil walikhini amana hii na kuwa wezi wa fadhila. Hebu turejee Qur'an tuone baadhi ya neema za Allah juu ya Bani Israil na jinsi walivyofanya ukaidi.

يَذِيبِ إِسْرَائِيلَ أَذْكَرُوا نِعْمَتِي الَّتِي أَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ وَأَنَّى فَضَّلْتُكُمْ عَلٰى

الْعٰلَمِينَ ﴿٤٧﴾

*"Enyi kizazi cha Israili! Kumbukeni neema zangu nilizokuneemesheni na nikakutukuzeni kuliko viumbe wengine (wakati huo)" (2:47).*

وَإِذْ نَجَّيْنٰكُمْ مِّنْ ءَالِ فِرْعَوْنَ يَسُومُونَكُمْ سُوءَ الْعَذَابِ

يُذَيِّبُونَ أَبْنَاءَكُمْ وَيَسْتَحْيُونَ نِسَاءَكُمْ وَفِي ذٰلِكُمْ بَلَاءٌ

مِّنْ رَبِّكُمْ عَظِيمٌ ﴿٤٩﴾ وَإِذْ فَرَقْنَا بِكُمْ الْبَحْرَ فَأَنْجَيْنٰكُمْ

وَأَغْرَقْنَا ءَالِ فِرْعَوْنَ وَأَنْتُمْ تَنْظُرُونَ ﴿٥٠﴾

*Na (kumbukeni) tulipokuokoeni kwa watu wa Firauni waliokupeni adhabu mbaya; wakiwachinja watoto wenu wanaume na kuwawacha hai wanawake; na katika hayo (kuokolewa huko) ilipatikana neema kubwa iliyotoka kwa Mola wenu. Na (kumbukeni) tulipoitenga bahari kwa ajili yenu na tukakuokoeni, na tukawazamisha watu wa Firauni na hali mkitazama" (2:49-50).*

وَإِذْ قُلْتُمْ يَدْمُوسَىٰ لَنْ نُؤْمِنَ لَكَ حَتَّىٰ نَرَىٰ اللَّهَ جَهْرَةً فَأَخَذَتْكُمُ  
 الصَّيْغَةُ وَأَنْتُمْ تَنْظُرُونَ ﴿٥٥﴾ ثُمَّ بَعَثْنَاكُمْ مِنْ بَعْدِ مَوْتِكُمْ لَعَلَّكُمْ  
 تَشْكُرُونَ ﴿٥٦﴾ وَظَلَّلْنَا عَلَيْكُمُ الْغَمَامَ وَأَنْزَلْنَا عَلَيْكُمُ الْمَنَّاءَ وَالسَّلْوَىٰ<sup>ط</sup>  
 كُلُوا مِنْ طَيِّبَاتِ مَا رَزَقْنَاكُمْ وَمَا ظَلَمُونَا وَلَكِنْ كَانُوا أَنْفُسَهُمْ  
 يَظْلِمُونَ ﴿٥٧﴾

*Na (kumbukeni habari hii pia): Mliposema: "Ewe Musa!  
 Hatutakuamini mpaka tumwone Mwenyezi Mungu waziwazi".  
 Yakakunyakueni mauti ghafla na hali mnaona. Kisha  
 tukakufufueni baada ya kufa kwenu, ili mpate kushukuru.  
 Na tukakutilieni kivuli kwa mawingu (mlipokuwa mnakata  
 jangwa kutoka Misri kwenda Palestina) na tukakuteremshieni  
 Manna na Salwa: (Tukakwambieni) "Kuleni katika vitu vizuri  
 hivi tulivyokuruzukuni." Nao hawakutudhulumu sisi  
 (walipokhalifu amri yetu) lakini walikuwa wamejidhulumu nafsi  
 zao." (2:55-57).*

❖ وَإِذِ اسْتَسْقَىٰ مُوسَىٰ لِقَوْمِهِ فَقُلْنَا اضْرِبْ بِعَصَاكَ الْحَجَرَ فَانفَجَرَتْ  
 مِنْهُ اثْنَتَا عَشْرَةَ عَيْنًا قَدْ عَلِمَ كُلُّ أُنَاسٍ مَشْرَبَهُمْ كُلُوا وَاشْرَبُوا  
 مِنْ رِزْقِ اللَّهِ وَلَا تَعَثَوْا فِي الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ﴿٥٦﴾ وَإِذْ قُلْتُمْ يَدْمُوسَىٰ  
 لَنْ نَصْبِرَ عَلَىٰ طَعَامٍ وَاحِدٍ فَادْعُ لَنَا رَبَّكَ يُخْرِجْ لَنَا مِمَّا تُثْبِتُ  
 الْأَرْضُ مِنْ بَقْلِهَا وَقِثَّائِهَا وَفُومِهَا وَعَدَسِهَا وَبَصِلِهَا قَالَ آتَتْكُمْ دُلُورُنَّ  
 الَّذِي هُوَ آذَنِي بِالَّذِي هُوَ خَيْرٌ أَهْبَطُوا مِصْرًا فَإِنَّ لَكُمْ مَّا سَأَلْتُمْ<sup>ط</sup>

وَإِذْ قُلْتُمْ يَا مُوسَىٰ لَنْ نَصْبِرَ عَلَىٰ طَعَامٍ وَاحِدٍ فَادْعُ لَنَا رَبَّكَ يُخْرِجْ  
لَنَا مِمَّا تَنْبِثُ الْأَرْضُ مِنْ بَاطِنِهَا وَقْتَابِهَا وَفُومَهَا وَعَدَسَهَا وَصَلْهَا  
قَالَ أَسْتَبْدِلُونَ الَّذِي هُوَ أَدْنَىٰ بِالَّذِي هُوَ خَيْرٌ أَهْبَطُوا مِصْرًا  
فَإِنَّ لَكُمْ مَّا سَأَلْتُمْ<sup>ط</sup> وَضَرَبْتَ عَلَيْهِمُ الدَّلِيلَ وَالْمَسْكَنَةَ وَبَاءُوا بِغَضَبِ  
مِّنَ اللَّهِ<sup>ط</sup> ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ كَانُوا يَكْفُرُونَ بِآيَاتِ اللَّهِ وَيَقْتُلُونَ  
الَّذِينَ بَغَىٰ لَهُ<sup>ط</sup> الْحَقُّ ذَلِكَ بِمَا عَصَوْا وَكَانُوا يَعْتَدُونَ ﴿١١﴾

*Na (kumbukeni khabari hii nayo): Musa aliomba maji kwa ajili ya watu wake, tukasema: "Lipige jiwe kwa fimbo yako" mara zikabubujika humo chem.-chem kumi na mbili; kila kabila likajua mahali pake pa kunywa. (Tutawaambia) kuleni na kunyweni katika riziki ya Mwenyezi Mungu, wala msiasi katika ardhi mkafanya uharibifu. Na (kumbukeni) mliposema: "Ewe Musa! Hatuwezi kusubiri kwa chakula cha namna moja tu, basi tuombe kwa Mola wako atutolee vile vinavyooteshwa na ardhi, kama mboga zake na matango yake na ngano yake na adesi zake na vitunguu vyake". Akasema (Mwenyezi Mungu): "Mnabadili vitu duni kwa vile vilivyo bora? Nendeni kwenye mji, huko mtapata mlivyoviomba"; Na ikapigwa juu yao (chapa ya) dhila (unyonge) na umaskini; nawakastahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Na haya ni kwa sababu walikuwa wakiyakataa maneno ya Mwenyezi Mungu na wakiwaua manabii pasipo haki. Basi haya ni kwa sababu ya kuasi kwao na kupindukia mipaka (ya Mwenyezi Mungu) (2:60-61).*

Hizo ni baadhi tu ya aya miongoni mwa aya zibainishazo neema za Allah juu ya Bani Israil na ukaidi wao.

## Kulaaniwa Bani Israil

Pamoja na kuteuliwa na Allah(s.w) kuwa taifa bora kuliko mataifa yote ya wakati huo, Allah(s.w) aliwaghadhibikia Mayahudi na kuwalaani kutokana na matendo yao yafuatayo:

(i)Walikuwa ni wezi wa fadhila

- Allah(s.w) aliwatunukia neema mbali mbali ili wasimamishe Ufalme wake katika ardhi na wamuabudu ipasavyo.
- Wengi wao walivitumia vipawa hivi kwa maslahi ya dunia na wakawa miongoni mwa wenye kuzama katika maasi.
- Baadhi ya neema walizotunukiwa Mayahudi zimeainishwa katika Qur-an - Rejea (2:47-53, 60, 122),(45:16-17).

(ii) Walipewa maonyo na mazingatio ili waache makosa na watengenee, lakini hawakuonyeka wala kuzingatia bali walikaidi na kuendelea kuzama katika kumuasi Allah(s.w).  
Rejea Qur-an (2:54-59, 61, 63-74), (5:71), (7:138-141).

(iii)Waliwakadhibisha na kuwaua Mitume wa Allah(s.w) bila ya haki.

لَقَدْ أَخَذْنَا مِيثَاقَ بَنِي إِسْرَائِيلَ وَآرَسَلْنَا إِلَيْهِمُ رَسُولًا  
كُلَّمَا جَاءَهُمْ رَسُولٌ بِمَا لَا تَهْوَىٰ أَنفُسُهُمْ فَرِيقًا كَذَّبُوا  
وَفَرِيقًا يَغْتُلُونَ ﴿٧٠﴾

*"Kwa yakini Tulichukuwa ahadi ya wana wa Israili (Mayahudi kuwa watafuata), na Tukawapelekea Mitume. (Lakini) kila mara alipowafikia Mtume kwa yale zisiyoyapenda nafsi zao, wengine (katika Mitume hao) waliwakadhibisha, na wengine wakawaua (khasa)" (5:70).*

(iv) Walivunja ahadi mbali mbali walizowekeana na Allah(s.w).  
- Rejea Qur-an (2:83-86, 93, 100), (5:12-13, 70).

- (v) Walikuwa na kibri na majivuno kuwa wao ni vipenzi vya Allah (s.w) na kwamba wataingia Peponi bila ya kufanya amali stahiki. Na ikitokea waingie Motoni watakaa muda mchache tu bila ya kujali uovu wanaoufanya:

وَقَالُوا لَنْ نَمَسَّنَا النَّارَ إِلَّا أَيَّامًا مَعْدُودَةً قُلْ أَتَّخَذْتُمْ عِنْدَ اللَّهِ عَهْدًا فَلَنْ يُخْلِفَ اللَّهُ عَهْدَهُمْ أَطَّامُ تَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٨٠﴾

*"Na walisema: Hautatugusa Moto (wa Jahannamu) isipokuwa kwa siku chache tu. Sema: Je! mmepata ahadi kwa Mwenyezi Mungu kwa hivyo hatakalifu ahadi yake? Au mnamsingizia Mwenyezi Mungu mambo msiyoyajua? (2:80).*

- Pia rejea Qur-an (2:88, 91).

- (vi) Wanazuoni wao walikuwa wakificha haki. Pia walikuwa wakichanganya haki na batili.

﴿أَفَتَطْمَعُونَ أَنْ يُؤْمِنُوا لَكُمْ وَقَدْ كَانَ فَرِيقٌ مِّنْهُمْ يَسْمَعُونَ كَلِمَ اللَّهِ ثُمَّ يَلْحَرُونَ مِنْ بَعْدِ مَا عَقَلُوهُ وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿٧٥﴾﴾

*Mnatumaini (nyinyi Waislamu) ya kwamba watakuaminini (hao Mayahudi); na hali baadhi yao walikuwa wanasikia maneno ya Mwenyezi Mungu, kisha wanayabadili baada ya kuwa wameyafahamu; na hali wanajua? (2:75)*

﴿وَلَا تَلْبِسُوا الْحَقَّ بِالْبَاطِلِ وَتَكْتُمُوا الْحَقَّ وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٤٢﴾﴾

*Wala msichanganye haki na batili, na mkaficha haki, na hali mnajua. (2:42)*

- Pia rejea Qur-an (2:76-79).

- (vii) Walibadili vitabu vya Allah(s.w) kwa kupunguza au kuongeza au kuondoa maneno au aya ili kuvuruga maana



halisi ya kile kilichokusudiwa kwa maslahi yao binafsi kwa ajili ya dunia.

(viii) Walikuwa wakiwaamrisha watu kutenda mema ambayo wenyewe walikuwa hawafanyi.

﴿ أَتَأْمُرُونَ النَّاسَ بِالْبِرِّ وَتَنْسَوْنَ أَنْفُسَكُمْ وَأَنْتُمْ تَتْلُونَ الْكِتَابَ أَفَلَا

تَعْقِلُونَ ﴿٤٤﴾

*Je! Mnawaamrisha watu kutenda mema na mnajisahau nafsi zenu, hali mnasoma kitabu (cha Mwenyezi Mungu kuwa kufanya hivyo ni vibaya)? Basi je, hamfahamu? (2:44)*

(ix) Walikuwa wakitekeleza baadhi ya maamrishi ya Allah(s.w) na kukufuru baadhi. Yaani walikuwa wakifuata baadhi ya kitabu na kukufuru baadhi nyingine - Rejea Qur-an (2:85)

(x) Walikuwa wakila riba na kula mali za watu kwa batili - Qur-an (4:161).

(xi) Walikuwa hawaamrishi mema na kukataza mabaya - Qur-an (5:78-79)

(xii) Walikuwa wakifanya urafiki na makafiri - Qur-an (5:80).

(xiii) Walipenda sana kuishi na walikuwa wakiogopa sana kufa kutokana na yale maovu iliyotanguliza mikono yao - Qur-an (2:96), (62:6-8).

(xiv) Waligawanyika katika makundi makundi mbali mbali, kila kundi likiwa dhidi ya lingine japo wote wanasoma kitabu kimoja. Qur'an inawaonya Waislamu juu ya hili katika aya zifuatazo:

إِنَّ الَّذِينَ فَرَّقُوا دِينَهُمْ وَكَانُوا شِيَعًا لَسْتَ مِنْهُمْ فِي شَيْءٍ إِنَّمَا  
 أَمْرُهُمْ إِلَى اللَّهِ ثُمَّ يُنَبِّئُهُمْ بِمَا كَانُوا يَفْعَلُونَ ﴿١٥٩﴾

*Hakika wale waliofarikisha dini yao na wakawa makundi makundi, huna ukhusiano nao wowote. Bila shaka shauri yao (ya kuwaadhibu) iko kwa Mwenyezi Mungu; kisha (hapo wakati wa kuwaadhibu) atawaambia yale waliyokuwa wakitenda (6:159).*

﴿مُتَّبِعِينَ إِلَيْهِ وَاتَّقُوهُ وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَلَا تَكُونُوا مِنَ الْمُشْرِكِينَ﴾

﴿٣١﴾ مِنَ الَّذِينَ فَرَّقُوا دِينَهُمْ وَكَانُوا شِيَعًا كُلُّ حِزْبٍ بِمَا لَدَيْهِمْ فَرِحُونَ ﴿٣٢﴾

*"Nyenyekeeni Kwake na mcheni, na simamisheni Sala, wala msiwe katika washirikina"*

*"Katika wale walioitenga Dini yao na wakawa makundi makundi; kila kikundi kinafurahia kilicho nacho" (30:31-32).*

#### (xv) Waliofanya Viongozi wao Miungu

Juu ya hili Qur'an inatufahamisha katika aya zifuatazo:

وَقَالَتِ الْيَهُودُ عِزَّىٰرُ بْنُ اللَّهِ وَقَالَتِ النَّصَارَى الْمَسِيحُ ابْنُ اللَّهِ ذَلِكَ قَوْلُهُمْ بِأَفْوَاهِهِمْ يُضَاهِئُونَ قَوْلَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَبْلُ قَتَلْتَهُمُ اللَّهُ  
 أَنَّى يُؤْفَكُونَ ﴿٣٠﴾

*"Na Mayahudi wanasema: "Uzeri ni mwana wa Mwenyezi Mungu;" na Wakristo wanasema: "Masih ni mwana wa Mwenyezi Mungu,; haya ndiyo wasemayo kwa vinywa vyao (pasi na kuyapima). Wanayaiga maneno ya wale walio kufuru kabla yao, Mwenyezi Mungu awaangamize. Wanageuzwa namna gani hawa!" (9:30).*

اتَّخَذُوا أَحْبَابَهُمْ وَرُهْبَانَهُمْ أَرْبَابًا مِّن دُونِ اللَّهِ وَالْمَسِيحَ ابْنَ مَرْيَمَ  
وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا إِلَهًا وَاحِدًا لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ سُبْحَانَهُ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٣١﴾

"Wamewafanya wanavyuoni wao na watawa wao kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu na (wamemfanya) Masihi mwana wa Maryamu (pia Mungu), hali hawakuamrisha isipokuwa kumuabudu Mungu Mmoja, hakuna anayestahiki kuabudiwa kwa haki ila Yeye. Ametakasika na yale wanayomshirikisha nayo" (9:31).

(xvi) Walijenga hoja za visingizio.

Mayahudi walikatazwa kufanya kazi Jumamosi. Lakini baadhi yao waliasi ima kwa ujanjaujanja au kwa wazi wazi. Miongoni mwa waliokhalifu kwa unjanja ujanja ni wavuvi wa samaki. Walikuwa wakitega mitego yao Ijumaa jioni na kuchukua samaki Jumamosi jioni au Jumapili asubuhi ili ionekane kuwa Jumamosi hawakufanya kazi. Na wengine waliasi kwa kuleta visingizio kadhaa. Allah(s.w) aliye mjuzi wa nia zao aliwajua kuwa waliamua kumuasi na akawalipa adhabu ya kudhalilisha:

وَلَقَدْ عَلِمْتُمُ الَّذِينَ اعْتَدُوا مِنكُمْ فِي السَّبْتِ فَقُلْنَا لَهُمْ كُونُوا

قِرَدَةً خَاسِئِينَ ﴿١٦﴾

"Na kwa yakini mmekwisha kujua (khabari za) wale walioasi miongoni mwenu katika (amri ya kuihishimu) Jumamosi. Basi Tukawaambia: "Kuweni manyani wadhhalilifu" (2:65).

## **Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Bani Israil**

Kutokana na historia ya Bani Israil (Mayahudi) tunapata mafunzo ya msingi yafuatayo:

- (i) Baada ya Mayahudi kufanya makosa hayo yaliyoainishwa walighadhibikiwa na Allah(s.w) na kunyang'anywa hadhi yao

ya kuwa Taifa teule na kupewa Waumini wa Ummat Muhammad(s.a.w) kama inavyoainishwa katika Qur'an:

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ  
عَنِ الْمُنْكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَلَوْ آمَنَ أَهْلُ الْكِتَابِ لَكَانَ  
خَيْرًا لَهُمْ مِّنْهُمْ الْمُؤْمِنُونَ وَأَكْثَرُهُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿١١٠﴾

*Nyinyi ndio Umma bora kuliko umma zote zilizodhihirishiwa watu (ulimwenguni) - mnaamrisha yaliyo mema na mnakatata yaliyo maovu, na mnamwamini Mwenyezi Mungu. Na kama wale waliopewa Kitabu wangaliamini (kama walivyoamrisha) ingalikuwa bora kwao. (Lakini) miongoni mwao wako wanaoamini; na wengi wao wanatoka katika taa ya Mwenyezi Mungu' (3:110).*

- (ii) Cheo cha kuwa bora walichopewa Waumini kina masharti yale yale ya kusimamisha ufalme wa Allah(s.w) hapa ulimwenguni na kuwa kiigizo chema.

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَاكُمْ أُمَّةً وَسَطًا لِتَكُونُوا شُهَدَاءَ عَلَى النَّاسِ  
وَيَكُونَ الرَّسُولُ عَلَيْكُمْ شَهِيدًا.....

*"Na vivyo hivyo Tumekufanyeni Ummah bora (kama Qibla chenu Tulivyokifanya bora) ili muwe mashahidi juu ya watu na Mtume awe shahidi juu yenu....." (2:143).*

- (iii) Waislamu wa Ummah huu na wao hawatasalimika na ghadhabu pamoja na laana ya Allah(s.w) endapo wataiga mwenendo wa Mayahudi na kurudia makosa yao yaliyoorodheshwa hapo juu na mengineyo yaliyoainishwa katika Qur'an.

## AL-YASA'A(A.S)

Mtume Alyasa'a(a.s) ametajwa mara moja tu katika Qur'an na kubainishwa kuwa ni miongoni mwa watu waliofadhilishwa na Mwenyezi Mungu.

وَإِسْمَاعِيلَ وَالْيَسَعَ وَيُونُسَ وَلُوطًا وَكُلًّا فَضَّلْنَا عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿٨٦﴾

“Na (tukamwongoa) Ismail na Alyasaa na Yunus na Lut. Na wote tukawafadhilisha juu ya walimwengu (wote katika zama zao)” (6:86).

Kufadhilishwa kwa Mitume hawa hakukutokana na nasaba zao wala zama za kuletwa kwao duniani. Bali kwa ujumbe waliopewa na juhudi waliyoifanya katika kuutekeleza ujumbe huo na kuufikisha kwa kaumu zao. Haya yanathibitishwa na aya zinazofuatia:

أُولَئِكَ الَّذِينَ آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ وَالْحُكْمَ وَالنَّبُوءَةَ فَإِنْ يَكْفُرْ

بِهَا هَتُّوْا لَهُمْ فَقَدْ كَلْنَا بِهَا قَوْمًا لَّيْسُوا بِهَا بِكَافِرِينَ ﴿٨٧﴾

“Hao ndio tuliowapa vitabu na hukumu (Ilmu) na utume. Kama hawa (makafiri) wakiyakataa hayo, basi tumekwisha yawekea watu wasioyakataa” (6:89).

أُولَئِكَ الَّذِينَ هَدَى اللَّهُ فَبِهِدَتْهُمْ أَفْتِدَةٌ ۗ فَلَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا ۗ إِنْ هُوَ

إِلَّا ذِكْرٌ لِّلْعَالَمِينَ ﴿٩٠﴾

“Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amewaongoa, basi fuata Uongozi wao” (6:90).

## DHUL-KIFL(A.S).

Mtume Dhul-kifl ananasibishwa na Ezekiel anayetajwa ndani ya Biblia. Ni miongoni mwa Mitume waliopata mateso sana mikononi mwa Bani Israil. Hata hivyo hakuacha kufundisha Ujumbe wa Allah. Tunamsoma Dhul-kifl katika aya zifuatazo:

وَإِسْمَاعِيلَ وَإِدْرِيسَ وَذَا الْكِفْلِ كُلٌّ مِنَ الصَّابِرِينَ ﴿٨٥﴾ وَأَدْخَلْنَاهُمْ فِي رَحْمَتِنَا إِنَّهُمْ مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٨٦﴾

“Na (mtaje) Ismail na Idris na Dhul-kifl – wote walikuwa miongoni mwa wanaosubiri. Na tukawaingiza katika rehema yetu. Hakika wao walikuwa katika watu wema” (21:85-86).

وَإِذْ كُرِيَ إِسْمَاعِيلَ وَالْيَسَعَ وَذَا الْكِفْلِ وَكُلٌّ مِنَ الْأَخْيَارِ ﴿٤٨﴾

“Na mkumbuke Ismail na Alyasaa na Dhul-kifl, na hao wote walikuwa miongoni mwa watu bora” (38:48).

Mtume Dhul-kifl anatajwa kwa wema wake katika kuufuata mwongozo wa Allah(s.w). Na Mwenyezi Mungu anaahidi kuwa marejeo ya watu wema ni mahali pazuri kabisa.

هَذَا ذِكْرٌ وَإِنَّ لِلْمُتَّقِينَ لَحُسْنَ مَقَابٍ ﴿٤٩﴾

“Huu ni ukumbusho (wa watu wema). Na kwa yakini wamchao Mungu mahali pao pa kurudia patakuwa pazuri kabisa” (38:49).

## DAUD(A.S).

Nabii Daudi(a.s) aliishi Bait-UI-Lahm karibu na mji wa Jerusalem zaidi ya miaka 200 baada ya Mtume Musa(a.s). Nasaba yake inatokea kwa Mtume Ya'aquub(a.s). Pamoja na kuwa Mtume wa Allah(s.w), Daudi alikuwa pia mfalme wa Mayahudi (Bani Israil).

## Kupewa Daudi(a.s)Utume na Ufalme

Kiasi cha miaka mia mbili hivi baada ya Mtume Musa (a.s), Mayahudi walipigwa sana na kuonewa na Wafalastin. Waliteka Sanduku takatifu la Waisrail ambamo ndani yake walihifadhi mbao ambazo zimeandikwa amri kumi alizoteremshiwa Nabii Musa (a.s). Aidha yalikuwamo ndani yake masazo mengine ya vitu vitukufu alivyoacha Nabii Musa na Nabii Harun. Sanduku hili Mayahudi walilitukuza sana kiasi kwamba hata wakienda vitani huenda nalo na likiwa mbele ya macho yao huamini kabisa kuwa watahinda vita. Kwa hiyo kunyang'anywa sanduku lao hilo na Wafalastin kuliwavunja nguvu kabisa (Mayahudi).

Ilikuwa ni katika kipindi hicho cha kuzidiwa nguvu na Wafalastin, Mayahudi walitamani wapate mfalme atakaye watawala na awaongoze kaitka vita. Biblia inataja kuwa Mtume wao katika kipindi hicho alikuwa Samuel. Kwa hiyo walimwomba Samuel awateulie mfalme.

Qur'an inataja kuwa Twaluti alichaguliwa kuwa mfalme. Lakini Mayahudi walimkataa. Hata hivyo Twaluti alibakia kuwa kiongozi wao na akawaongoza Mayahudi waliomtii hata wakamshinda adui yao. Qur'an inarejea habari hii katika aya zifuatazo:

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ مَلَآ مِنْ بَنِي إِسْرَائِيلَ مِنْ  
بَعْدِ مُوسَى إِذْ قَالُوا لِنَبِيِّ لَهُمْ أَبْعَثْ لَنَا مَلَكًا يُقَاتِلْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ  
قَالَ هَلْ عَسَيْتُمْ إِنْ كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِتَالُ أَلَّا تُقَاتِلُوا قَالُوا وَمَا لَنَا أَلَّا  
نُقَاتِلَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَقَدْ أَخْرَجَنَا مِنْ دِيَارِنَا وَأَبْنَايَا فَلَمَّا

كُتِبَ عَلَيْهِمُ الْقِتَالُ تَوَلَّوْا إِلَّا قَلِيلًا مِّنْهُمْ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالظَّالِمِينَ ﴿٢٤٦﴾

*"Hukusikia habari ya wakubwa wa Kibanii Israil baada ya Musa walipomwambia Nabii wao: "Tuwekee mfalme ili tupigane katika njia ya Mwenyezi Mungu". Yeye (Mtume wao) akasema:*

"Haielekei ya kuwa hamtapigana ikiwa mtaandikiwa kupigana?"  
 Wakasema: "Itakuwaje tusipigane katika njia ya Mwenyezi Mungu na hali tumetolewa katika majumba yetu na watoto wetu?" Lakini walipoandikiwa kupigana waligeuka, isipokuwa wachache miongoni mwao. Na Mwenyezi Mungu anawajua sana madhalimu". (2:246).

وَقَالَ لَهُمْ نَبِيُّهُمْ إِنَّ اللَّهَ قَدْ بَعَثَ لَكُمْ طَالُوتَ مَلِكًا قَالُوا أَأَتَىٰ يَكُونُ لَهُ  
 الْمُلْكُ عَلَيْنَا وَنَحْنُ أَحَقُّ بِالْمُلْكِ مِنْهُ وَلَمْ يُؤْتَ سَعَةً مِنَ الْمَالِ قَالَ إِنَّ اللَّهَ  
 اصْطَفَاهُ عَلَيْكُمْ وَزَادَهُ بَسْطَةً فِي الْعِلْمِ وَالْجِسْمِ وَاللَّهُ يُؤْتِي مَلَكَهُ مَن  
 يَشَاءُ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٤٧﴾

Na huyo Mtume wao akawaambia: "Mwenyezi Mungu amekuchagulieni Twaluti kuwa mfalme". Wakasema: "Vipi atakuwa na ufalme juu yetu; na hali sisi tumestahiki zaidi kupata ufalme kuliko yeye; naye hakupewa wasaa wa mali?" Akasema: "Mwenyezi Mungu amemchagua juu yenu na amemzidisha wasaa wa **ilmu na kiwiliwili**. Na Mwenyezi Mungu humpa ufalme wake amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa (na) Mwenye kujua". (2:247).

وَقَالَ لَهُمْ نَبِيُّهُمْ إِنَّ آيَةَ مُلْكِهِ أَن يَأْتِيَكُمُ التَّابُوتُ فِيهِ سَكِينَةٌ مِّن  
 رَبِّكُمْ وَبَقِيَّةٌ مِّمَّا تَرَكَ آلُ مُوسَىٰ وَآلُ هَارُونَ تَحْمِلُهُ الْمَلَائِكَةُ إِنَّ فِي  
 ذَٰلِكَ لَآيَةً لِّكُم مِّن كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿٢٤٨﴾

"Na Nabii wao akawaambia: "Alama ya ufalme wake ni kukujieni lile sanduku ambalo mna ndani yake kituliza nyoyo zenu, kitokacho kwa Mola wenu, na mna masazo ya yale waliyoyaacha watu wa Musa na watu wa Harun, walilichukua malaika. Bila shaka katika hayo mna dalili kwenu ikiwa nyinyi mnaamini" (2:248).



Katika jamii za jahiliyah nasaba ya mtu na uwezo wake wa kiuchumi ilikuwa ni vigezo muhimu katika kuteua kiongozi. Mayahudi kwa kuyatupa mafundisho ya Mitume wao na kwa ukaidi wao walivitilia mkazo vigezo hivi vile vile. Kwa hiyo alipoteuliwa Twaluti kuwa kiongozi wao, wakaona hafai kwa kuleta hoja ya mali. Hata hivyo, hoja hiyo inavunjwa na elimu na siha nzuri. Uislamu unasisitiza umuhimu wa kuiboresha akili kwa elimu na kiwiliwili kwa siha nzuri. Katika Uislamu mtu hapewi uongozi kwa sababu ya nasaba au uwezo wake wa kiuchumi bali kwa elimu na Ucha-Mungu wake.

Twaluti baada ya kupewa uongozi aliyaongoza majeshi ya Mayahudi kupambana na Jaluti na majeshi yake. Kundi kubwa katika Mayahudi liliasi. Lakini wachache waliobaki wenye imani thabiti walifanya subira na kwa kumtegemea Allah(s.w) wakamshinda Jaluti. Nabii Daud(a.s) katika mapambano haya alikuwa katika jeshi la Twaluti na ndiye aliyemuua Jaluti. Baada ya ushindi huo Mayahudi walimchagua Nabii Daudi kuwa mfalme wao. Ni katika kipindi hicho hicho cha historia Daudi alipewa Utume kama inavyobainika katika aya zifuatazo:

فَلَمَّا فَصَلَ طَالُوتُ بِالْجُنُودِ قَالَ إِنَّ اللَّهَ مُبْتَلِيكُمْ بِنَهَرٍ فَمَنْ شَرِبَ مِنْهُ  
 فَلَيْسَ مِنِّي وَمَنْ لَمْ يَطْعَمْهُ فَإِنَّهُ مِنِّي إِلَّا مَنِ اعْتَرَفَ غُرْفَةً بِيَدِهِ  
 فَشَرِبُوا مِنْهُ إِلَّا قَلِيلًا مِّنْهُمْ فَلَمَّا جَاوَزَهُ هُوَ وَالَّذِينَ آمَنُوا مَعَهُ قَالُوا لَا  
 طَاقَةَ لَنَا الْيَوْمَ بِجَالُوتَ وَجُنُودِهِ قَالَ الَّذِينَ يَظُنُّونَ أَنَّهُمْ مُلَاقُوا اللَّهَ  
 كَم مِّن فِئَةٍ قَلِيلَةٍ غَلَبَتْ فِئَةً كَثِيرَةً بِإِذْنِ اللَّهِ وَاللَّهُ مَعَ الصَّابِرِينَ

*Basi Taluti alipoondoka na majeshi alisema: "Mwenyezi Mungu atakufanyieni mtihani kwa mto. Basi atakayekunywa humo si pamoja nami, na asiyekunywa atakuwa pamoja nami; ila*

atakayeteka kwa kiasi cha kujaza kitanga cha mkono wake (akanywa hayo tu, huyo hana makosa)". Lakini walikunywa humo isipokuwa wachache tu miongoni mwao. Basi alipovuka yeye na wale walioamini pamoja naye, walisema: "Leo hatumwezi Jaluti na majeshi yake". Wakasema wale wenye yakini ya kukutana na Mola wao: "Makundi mangapi madogo yameshinda makundi makubwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu yu pamoja na wafanyao subira" (2:249).

وَلَمَّا بَرَزُوا لِجَالُوتَ وَجُنُودِهِ قَالُوا رَبَّنَا أَفْرِغْ عَلَيْنَا صَبْرًا وَثَبِّثْ

أَقْدَامَنَا وَانصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ ﴿٢٥٠﴾

Na walipotoka kupambana na Jaluti na majeshi yake, walisema hao watu wa Twaluti: "Mola wetu! Tumiminie subira na uithibitishe miguu yetu, na utusaidie juu ya watu hawa makafiri" (2:250).

فَهَزَمُوهُمْ بِإِذْنِ اللَّهِ وَقَتَلَ دَاوُدُ جَالُوتَ وَءَاتَاهُ اللَّهُ الْمُلْكَ وَالْحِكْمَةَ

وَعَلَّمَهُ مَا يَشَاءُ وَلَوْلَا دَفْعُ اللَّهِ النَّاسَ بَعْضَهُم بِبَعْضٍ لَفَسَدَتِ

الْأَرْضَ وَلَٰكِنَّ اللَّهَ ذُو فَضْلٍ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿٢٥١﴾

Basi (hao watu wa Twaluti) wakawaendesha mbio (hao maadui zao) kwa idhini ya Mwenyezi Mungu; na Daudi akamwua Jaluti, na Mwenyezi Mungu akampa (huyu Daudi) ufalme na hikima (Utume). Na akamfundisha aliyoyapenda" (2:251).

Yapo mambo kadhaa muhimu ya kuzingatia kutokana na mafundisho ya aya hizi. **Kwanza**, ni suala la utii. Kuwa na uongozi madhubuti na utii wa wale wanaoongozwa kwa kiongozi wao ni jambo kubwa sana katika kutengemaa kwa mambo ya watu. Kama hakuna utii kwa uongozi, basi jamii ni yenye kuharibikiwa tu. Twaluti anaondoka na jeshi kubwa kupambana na adui wa kutisha. Twaluti hana hakika na utii wa jeshi lake. Basi Allah(s.w) akamwelekeza awafanyie mihani wa kutokunywa maji hadi kukata

kiu. Wasiotii asiwachukue kwenda nao huko kwenye uwanja wa vita wasije wakakhalifu amri vitani.

Ni dhahiri kuwa kama mtu hawezi kufanya subira na kuvumilia kiu yake kwa muda mdogo tu; basi hawezi kuhimili kishindo cha kutoa roho kwa ajili ya Allah kwenye medani ya vita.

**Pili**, fundisho lingine kubwa linalopatikana ni kuwa katika kuipigania Dini ya Allah(s.w) wingi sio hoja, bali imani thabiti, subira na kumtegemea Mwenyezi Mungu. Watu wachache wa Twaluti walihisi isingekuwa rahisi kulishinda jeshi kubwa la Jaluti. Lakini wale wenye yakini hasa ya kukutana na Mola wao hawakusita. Bali walimkabili Mola wao kumwomba awamiminie subira na ujasiri wa kupambana na adui. Basi kwa idhini ya Mola wao walishinda vita.

Ni ahadi yake Allah(s.w) kwamba wakipatikana waumini wakweli wenye kusubiri, basi watawashinda maadui zao pamoja na wingi wao:

يَتَأَيُّهَا النَّبِيُّ حَرِيصِ الْمُؤْمِنِينَ عَلَى الْقِتَالِ إِنْ يَكُنْ مِنْكُمْ عَشْرُونَ  
صَبْرُونَ يَغْلِبُوا مِائَتِينَ وَإِنْ يَكُنْ مِنْكُمْ مِائَةٌ يَغْلِبُوا أَلْفًا مِّنَ  
الَّذِينَ كَفَرُوا بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَفْقَهُونَ ﴿١٥﴾

*"Ewe Mtume (wa Mwenyezi Mungu)! Wahimizewalioamini wende vitani. Wakipatikana kwenu watu ishirini wanaosubiri watashinda mia mbili (katika hao makafiri. Basi nyinyi mkiwa ishirini lazima msimame mupigane na watu miteni). Na kama wakiwa watu mia moja kwenu watawashinda elfu moja ya wale waliokufuru, maana hao ni watu wasiofahamu (uhai wa Akhera, basi wanaogopa kupigana kwa ushujaa sana wasije wakafa. Basi watu mia katika nyinyi wasiwakimbie watu elfu katika wao)." (8:65).*

Pamoja na ukweli huu, waumini wanatakiwa wafanye juhudi kubwa kukusanya nguvu zao na kusoma mbinu mbali mbali.

وَأَعِدُّوا لَهُمْ مَا اسْتَطَعْتُمْ مِنْ قُوَّةٍ وَمِنْ رِبَاطِ الْخَيْلِ  
 تُرْهَبُونَ بِهِ عَدُوَّ اللَّهِ وَعَدُوَّكُمْ وَعَآخِرِينَ مِنْ دُونِهِمْ لَا تَعْلَمُونَهُمْ  
 اللَّهُ يَعْلَمُهُمْ وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ شَيْءٍ فِي سَبِيلِ اللَّهِ يُوَفِّ إِلَيْكُمْ  
 وَأَنْتُمْ لَا تُظْلَمُونَ ﴿١٦﴾

*Basi waandalieni(wawekeeni tayari)nguvu mziwezazo (silaha) na mafarasi yaliyofungwa(kufuga)tayari tayari(mipakani), ili kwazo nguvu hizi muogopeshe maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui zenu,(mnawajua) na pia (maadui zenu)wengineo wasiokuwa wao, msiowajua nyinyi(lakini) Mwenyezi Mungu anawajua. Na chochote mtakachokitoa katika njia ya Mwenyezi Mungu(kama hii misaada ya vita vya Jihadi)mtarudishiwa (kamili) sawasawa wala hamtadhulumiwa." (8:60).*

Hata hivyo, silaha kubwa zaidi ni kuziunganisha nyoyo za waumini chini ya lengo moja tu la kuihami Dini ya Allah(s.w). Maadui wa Dini ya Mwenyezi Mungu pamoja na wingi wao wanashindwa kuikabili nguvu ya waumini, kwa sababu nyoyo na malengo yao ni mbali mbali.

لَأَنْتُمْ أَشَدُّ رَهَبَةً فِي صُدُورِهِمْ مِنَ اللَّهِ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَفْقَهُونَ  
 ﴿١٣﴾ لَا يَقْدِرُ لَكُمْ جَمِيعًا إِلَّا فِي قَرْيٍ مُحَصَّنَةٍ أَوْ مِنْ وَرَاءِ  
 جُدُرٍ بَأْسُهُمْ بَيْنَهُمْ شَدِيدٌ تَحْسَبُهُمْ جَمِيعًا وَقَلُوبُهُمْ شَتَّىٰ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ  
 قَوْمٌ لَا يَعْقِلُونَ ﴿١٤﴾

*"Hakika nyinyi (Waislamu) mnaogopwa zaidi katika nyoyo zao kuliko wanavyomuogopa Mwenyezi Mungu, maana wao ni watu wasiofahamu (lolote)". "Hawatapigana nanyi kwa mkusanyiko isipokuwa katika vijiji vyoa vilivyohifadhiwa, au nyuma ya kuta. Vita vyao baina yao vikubwa. Utawadhani kuwa wako pamoja, kumbe nyoyo zao ni mbali mbali. Hayo ni kwa sababu wao ni watu wasio na akili" (59:13-14).*

Kwa hiyo suala zima la kuwaelemisha Waislamu na kisha kuwaunganisha chini ya lengo moja tu la kuisimamisha na kuilinda Dini ya Allah, ni jambo la msingi sana.

**Tatu**, jambo lingine la msingi ambalo tunapaswa tulizingatie, ni mazingira yaliyopelekea Nabii Daudi (a.s) kupewa ufalme na utume. Qur'an inatufahamisha kuwa Daudi alipewa Ufalme na Utume baada ya kumwua Jaluti. Hii inatudhihirishia kuwa heshima na jaza njema haipatikani ila kwa juhudi ya mtu binafsi katika kutekeleza majukumu. Hapana heshima pasi na kuwajibika. Aidha katika malipo ya kesho Akhera yatategemea pia juhudi ya mtu na kuwajibika kwake mbele ya Allah(s.w).

## Neema Alizotunukiwa Nabii Daudi(a.s)

### (i)Kupewa Utume na Elimu.

Nabii Daudi pamoja na kupewa utume na ufalme, alifunuliwa elimu kubwa:

يَدَاوُدُ إِنَّا جَعَلْنَاكَ خَلِيفَةً فِي الْأَرْضِ فَاحْكُم بَيْنَ النَّاسِ بِالْحَقِّ  
وَلَا تَتَّبِعِ الْهَوَىٰ فَيُضِلَّكَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ إِنَّ الَّذِينَ يَضِلُّونَ عَنْ سَبِيلِ  
اللَّهِ لَهُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ بِمَا نَسُوا ﴿٦٦﴾

*"Ewe Daudi! Hakika tumekujaalia kuwa khalifa katika ardhi; basi wahukumu watu kwa haki wala usifuate matamania ya nafsi yasije yakakupoteza na njia ya Mwenyezi Mungu" (38:26).*

وَأَقْدَمْنَا دَاوُدَ وَسُلَيْمَانَ عَلِمًا وَقَالَا الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي فَضَّلَنَا عَلَىٰ

كَثِيرٍ مِّنْ عِبَادِهِ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٥﴾

*"Na bila shaka tuliwapa Daudi na Suleiman ilimu (kubwa kabisa) wakasema: "Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu. Aliyetufadhilisha kuliko wengi katika waja wake waliomuamini". (27:15).*

## (ii) Kupewa Zaburi.

Katika Qur'an vinatajwa vitabu vikuu 4 vya Allah(s.w). Vitabu hivyo ni Zaburi, Taurati, Injili na Qur'an. Zaburi alipewa Mtume Daudi (a.s).

وَعَاتَيْنَا دَاوُدَ زَبُورًا ﴿١١٣﴾

“...Na Daud tukampa Zaburi” (4:163).

## (iii) Kipawa cha Mawasiliano na Viumbe Wengine Zaidi ya Wanaadamu.

Ilivyo kawaida wanaadamu huwasiliana wao kwa wao hasa kwa njia ya lugha. Na wanyama na viumbe wengine nao

wana namna ya kuwasiliana wenyewe kwa wenyewe. Lakini Allah(s.w), Muweza wa yote alimjaalia Nabii Daudi kuwa na mawasiliano na viumbe wengine. Aidha alitiishiwa baadhi ya viumbe akawa anashirikiana navyo katika kumdhukuru Allah(s.w).

أَصْبِرْ عَلَىٰ مَا يَقُولُونَ وَلَا تُكْرِهْ عَبْدَنَا دَاوُدَ ذَا الْأَيْدِ إِنَّهُ وَأَوَّابٌ ﴿١٧﴾ إِنَّا  
سَخَّرْنَا الْجِبَالَ مَعَهُ يُسَبِّحْنَ بِالْعَشِيِّ وَالْإِشْرَاقِ ﴿١٨﴾ وَالطَّيْرَ مَحْشُورَةً  
كُلُّ لَهُ وَأَوَّابٌ ﴿١٩﴾

"Subiri juu ya hayo wanayosema, na umkumbuke mja wetu Daudi Mwenye nguvu (ya kuendesha Utume na Ufalme); kwa yakini yeye alikuwa mwelekevu sana". Hakika sisi tuliitiisha milima (iwe) pamoja naye, ikimtukuza (Mwenyezi Mungu pamoja naye) jioni na asubuhi. Na pia Ndege waliokusanywa (makundi kwa makundi), wote walikuwa wanyenyekevu kwake" (38:17-19).

#### (iv)Ustadi Katika Matumizi ya Chuma.

Umuhimu wa matumizi ya chuma hasa katika kuihami Dini ya Allah ni jambo kongwe katika historia ya mwanaadamu. Moja ya neema aliyopewa Nabii Daudi ni ujuzi wa kukifua chuma na kutengeneza zana mbali mbali ikiwa ni pamoja na zana za vita.

﴿وَلَقَدْ آتَيْنَا دَاوُدَ مِنَّا فَضْلًا يَجِبَالٌ أَوْبَىٰ مَعَهُ وَالطَّيْرُ وَالنَّاسُ﴾

لَهُ الْحَدِيدَ ﴿١٠﴾

*"Na kwa hakika Tulimpa Daudi fadhila kubwa kutoka kwetu. (Tuliyaamrisha majabali yawe yanaitikia Dua pamoja naye. Tukayaambia): Enyi milima! Rejezeni sauti pamoja naye. Na (nyie) ndege (pia)". Na tukamlainishia chuma" (34:10).*

﴿وَلَقَدْ آتَيْنَا دَاوُدَ مِنَّا فَضْلًا يَجِبَالٌ أَوْبَىٰ مَعَهُ وَالطَّيْرُ وَالنَّاسُ﴾

لَهُ الْحَدِيدَ ﴿١١﴾

*"(Tukamwambia): Tengeneza (nguo za chuma) pana, na upime vizuri katika kuunganisha; na fanyeni vitendo vizuri, bila shaka Nayaona (yote) msiyoyatenda" (34:11).*

﴿وَعَلَّمْنَاهُ صَنْعَةَ لَبُوسٍ لَّكُمْ لِيُحْصِنَكُمْ مِن بَأْسِكُمْ فَهَلْ أَنْتُمْ شَاكِرُونَ﴾

*"Na tukamfundisha (Daudi) matengenezo ya mavazi ya vita kwa ajili yenu ili yakuhifadhini katika mapigano yenu. Je! Mtakuwa wanaoshukuru?" (21:80).*

#### (v)Hakimu Muadilifu

Nabii Daudi alipewa ilimu na akili ya kukata hukumu:

﴿وَشَدَدْنَا مُلْكَهُ وَآتَيْنَاهُ الْحِكْمَةَ وَفَضَّلَ الْخِطَابَ﴾

*"Na Tukautia nguvu ufalme wake na Tukampa ilimu na (akili ya) kukata hukumu" (38:20).*

Yapo matukio mawili katika historia ya maisha ya Nabii Daudi yanayotoa kielelezo cha unyenyekevu wake katika kuifuata haki. Tukio la **kwanza** ni lile linalobainishwa katika Qur'an Surat Sad aya ya 21 mpaka 25. Katika aya hizi zinatajwa habari za watu wawili waliokuwa wanagombana na kumwendea Nabii Daudi ili awahukumu. Nabii Daudi aliathiriwa mno na maelezo ya upande mmoja kiasi kwamba akatoa hukumu bila ya kusikiliza upande wa pili. Lakini punde akatanabahi na kugundua kosa alilolifanya akarejea kwa Mola wake na kuomba maghfira. Tukio hili linabainishwa katika Qur'an kama ifuatavyo:

﴿٢١﴾ وَهَلْ أَتَاكَ نَبِيُّ الْخَصْمِ إِذْ تَسَوَّرُوا الْمِحْرَابَ

*"Na je imekuwasilia habari ya wagomvi walipopindukia (ukutani kuingia) chumbani kwake (Nabii Daudi?)" (38:21).*

إِذْ دَخَلُوا عَلَى دَاوُدَ فَفَزِعَ مِنْهُمْ قَالُوا لَا تَخَفْ خَصِمَانِ بَعْضُ  
بَعْضُنَا عَلَى بَعْضٍ فَأَحْكُم بَيْنَنَا بِالْحَقِّ وَلَا تُشْطِطْ وَأَهْدِنَا إِلَى سَوَاءٍ

الضَّرِيطِ ﴿٢٢﴾

*Walipomuingilia Daudi na akawaogopa. Wakasema: "Usiogope; (sisi ni) wagombanao wawili, mmoja wetu amemdhulumu mwenziwe; basi tuhukumu, kwa haki wala usipendelee, na utuongoe katika njia iliyo sawa" (38:22).*

إِنَّ هَذَا أَخِي لَهُ تِسْعٌ وَتِسْعُونَ نَعَجَةً وَإِلَى نَعَجَةٍ

وَاحِدَةٍ فَقَالَ أَكْفَلْنِيهَا وَعَزَّنِي فِي الْخِطَابِ ﴿٢٣﴾

*Hakika huyu ni ndugu yangu, yeye ana kondoo majike tisini na tisa, na mimi nina kondoo mmoja tu jike, lakini amesema: "Nipe huyu wako nikufugie, (na mimi mwenyewe sitaki) na amenishinda katika maneno" (38:23).*



قَالَ لَقَدْ ظَلَمَكَ بِسُؤَالِ نَعَجْتِكَ إِلَىٰ نَعَاجِهِ ۗ وَإِنَّ كَثِيرًا  
 مِّنَ الْخُلَطَاءِ لَيَبْغِي بَعْضُهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا  
 وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَقَلِيلٌ مَّا هُمْ ۗ وَظَنَّ دَاوُدُ أَنَّمَا فَتَنَّاهُ فَاسْتَغْفَرَ  
 رَبَّهُ ۗ وَخَرَّ رَاكِعًا وَأَنَابَ ﴿٢٤﴾

*Akasema: "Kweli amekudhulmu kwa kukuomba kondoo wako kuongeza katika kondoo wake, na bila shaka washirika wengi hudhulumiana wao kwa wao, isipokuwa wale walioamini na kutenda mema, na hao ni wachache". Na mara Daudi akaona ya kwamba tumemia mtihanini. Akaomba maghufira kwa Mola wake, na akaanguka kunyenyekea na akaelekea (kwa Mola wake) (38:24).*

فَغَفَرْنَا لَهُ ۗ ذَٰلِكَ وَإِنَّ لَهُ ۗ عِنْدَنَا لَٰزِقًا ۖ وَحَسَنَ مَّآبٍ ﴿٢٥﴾

*"Basi tukamghufiria (tukamsamehe) hayo. Na kwa hakika ana yeye kwetu cheo kikubwa na mahali pazuri (marejeo mazuri)" (38:25).*

Katika tukio hili kosa alilolifanya Nabii Daud ni kule kukata hukumu kabla ya kusikiliza upande wa pili. Kama inavyobainishwa na aya hizi msemaji wa awali alikuwa hodari wa kuyapanga maneno kiasi kwamba alimfanya Nabii Daud amwone ana haki kabla hata hajasikiliza upande wa pili. Lakini hata hivyo kwa ule Ucha-Mungu wake alizindukana na kuomba maghufira.

Hili ni fundisho kubwa sana kwetu kuwa katika hali yoyote itakayokuwa, mtu asipitishie hukumu kwa kutegemea maelezo ya upande mmoja tu.

Katika tukio la **pili** Nabii Daud(a.s) na mwanawe Sulaiman(a.s) waliletewa shauri. Mbuzi wa mtu mmoja waliingia shambani na kuharibu kabisa mimea ya mtu mwingine. Uharibifu huo ulikuwa ni mkubwa kiasi cha kumkosesha kabisa mavuno muhusika kwa mwaka mzima.

Nabii Daud(a.s) alitoa hukumu kuwa mbuzi waliohusika na uharibifu ule, apewe mwenye shamba kama fidia. Lakini mtoto wake Sulaiman aliona hukumu iliyo ya haki zaidi si kumpa mwenye shamba mbuzi wale moja kwa moja. Bali awachukue akae nao anufaike na maziwa, sufi na watoto watakozaliwa kiasi cha kufidia hasara ya mazao yake kisha mbuzi warejeshwe kwa mwenyewe. Nabii Daud kwa vile alikuwa ni mtu wa haki mwenye kusimamia uadilifu hakusita kuchukua rai hii japo imetoka kwa mtoto wake. Tunakumbushwa katika Qur'an:

وَدَاوُدَ وَسُلَيْمَانَ إِذْ يَحْكُمَانِ فِي الْحَرْثِ إِذْ نَفَشَتْ فِيهِ غَنَمُ الْقَوْمِ وَكُنَّا لِحُكْمِهِمْ شَاهِدِينَ ﴿٧٨﴾

*"Na (wakukbushe) Daudi na Suleiman walipokata hukumu juu ya konde, walipolisha humo mbuzi wa watu usiku. Nasi kwa hukumu yao hiyo tulikuwa mashahidi, (tunaona, tunasikia)" (21:78).*

فَفَهَّمْنَاهَا سُلَيْمَانَ وَكُلًّا آتَيْنَاهَا حُكْمًا وَعِلْمًا وَسَخَّرْنَا مَعَ دَاوُدَ الْجِبَالَ يُسَبِّحْنَ وَالطَّيْرَ وَكُنَّا فَاعِلِينَ ﴿٧٩﴾

*Tukamfahamisha Suleiman (kuliko Mzee wake, Daudi). Na kila mmoja tulimpa hukumu na ilimu" (21:79).*

Ikumbukwe Daud(a.s) alikuwa ni Mtume kisha Mfalme wa Wayahudi, lakini hakuwa na takaburi za kifalme. Alikuwa laini katika kusimamia uadilifu. Alikuwa mtu rahisi mbele za watu kiasi kwamba alifanya kazi za mikono ili kujitafutia riziki yake na familia yake

#### **(vi) Mtoto Mwema, Sulaiman (a.s)**

وَوَهَبْنَا لِدَاوُدَ سُلَيْمَانَ نِعْمَ الْعَبْدُ إِنَّهُ أَوَّابٌ ﴿٣٠﴾

*"Na tukampa Daud (Mtoto aliyeyitwa) Suleiman aliyekuwa Mtu Mwema na aliyekuwa mnyanyekevu.(38:30)*

## **Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Daud(a.s)**

Kutokana historia ya Nabii Daud (a.s) tunajifunza yafuatayo

(i) Katika kuchagua kiongozi wa kuendeleza harakati za kusimimisha Uislamu katika jamii hatunabudi kuzingatia sifa nne za msingi zifuatazo:

(a) Elimu ya mwongozo na mazingira – (58:11)

(b) Ucha-Mungu-mwenye kujitahidi kufuata kwa unyenyekevu maamrishi ya Allah(s.w) na Mtume wake na kujitahidi hivyo hivyo kujiepusha na makatazo yao – Qur'an (49:13)

(c) Siha au Afya nzuri na ushupavu. Mtume(s.a.w) amesema:

*“Muumini mwenye afya nzuri (kawiyyu) ni bora zaidi kuliko muumini nyoronyoro (legelege).”*

(d) Mwenye tabia njema – Pia Mtume (s..a.w) kasema;

*“Aliye kipenzi changu kuliko wote katika nyinyi (Waislamu) ni yule aliyewazidi kwa tabia njema” (Al-Bukhari).*

(ii) Utii kwa kiongozi muumini (mcha-mungu) ni msingi wa mafanikio kwa waislamu

(iii) Waumini wachache wenye msimamo na wenye kumtegemea Allah(s.w) wana uwezo wa kusimamisha haki (Uislamu) katika jamii.(2:249)

(iv)Tusitoe hukumu juu ya shutuma kabla hatujapata maelezo na kuyapima kutoka kwa yule anayeshutumumu na anayeshutumiwa.

(v) Tushukuru neema na vipaji vya ziada alivyotutunukia Allah(s.w) na kuwa mstari wa mbele katika kusimamisha uadilifu katika jamii – Nabii Daud (a.s) alikuwa mfalme juu ya watu, milima, upepo na ndege, lakini hakutakabari.

- (vi) Hatunabudi kuwaandalia maadui wa Uislamu silaha zinazolingana na wakati huu wa sayansi na teknolojia – Nabii Daud(a.s)alitumia chuma kuandaa silaha na mavazi ya kivita – Pia rejea agizo la Allah(s.w) (8:60)
- (vii) Hatunabudi kuwa na mazoezi ya kivita yatakayo tuwezesha kuwa jasiri na wavumilivu katika vita dhidi ya maadui wa Haki (Uislamu)
- Mfalme Twalut alilipa jeshi lake zoezi la kutokunywa maji ya mto ule ili kupima utii wao na uvumilivu wao.

## **SULAIMAN(A.S)**

Sulaiman(a.s)alikuwa mtoto wa Nabii Daudi(a.s) na pamoja na kuwa Mtume alirithi pia kiti cha ufalme wa baba yake. Ufalme wake ulidumu kati ya mwaka 965 B.C. hadi 926 B.C. Ufalme wake ulienea Palestina ya leo, Transjordan na baadhi ya eneo la Syria. Qur'an inamtaja Sulaiman kuwa mrithi wa Nabii Daudi(a.s) katika aya zifuatazo:

وَوَرِثَ سُلَيْمٰنُ دَاوُدَ وَقَالَ يَتَّخِئُهَا النَّاسُ غُلْمًا مِّنْطِقِ الطَّيْرِ وَأُوتِينَا  
مِن كُلِّ شَيْءٍ إِنَّ هٰذَا لَهٗوَ الْفَضْلُ الْمُبِينُ ﴿١٦﴾

*"Na Sulaiman alimrithi Daudi na akasema: Enyi watu! Tumefundishwa (hata kutambua) usemi wa ndege na tumepewa kila kitu, hakika hii ni fadhila iliyo dhahiri" (27:16).*

وَوَهَبْنَا لِدَاوُدَ سُلَيْمٰنَ نِعْمَ الْعَبْدُ إِنَّهُٗٓ أَوَابٌ ﴿٣٠﴾

*"Na tukampa Daudi (mtoto anayeitwa) Sulaiman, aliyekuwa mtu mwema, na alikuwa mnyenyekevu mno" (38:30).*

Nabii Sulaiman(a.s) anatajwa katika historia kama mfalme ambaye haujapata kutokea uflame mkubwa kama wake. Mwenyezi Mungu alimpa uwezo hata wa kumiliki majini. Walimtumikia katika

kazi zake mbali mbali. Ufalme huu unatajwa kuwa Nabii Sulaiman(a.s)aliupata baada ya kumuomba Mola wake ampe ufalme ambao hataupata mwingine yoyote baada yake.

قَالَ رَبِّ اغْفِرْ لِي وَهَبْ لِي مُلْكًا لَا يَنْبَغِي لِأَحَدٍ مِّنْ  
بَعْدِي إِنَّكَ أَنْتَ الْوَهَّابُ ﴿٣٥﴾

"Akasema: Mola wangu! Nisamehe na unipe ufalme, asiupate yoyote baada yangu. Bila shaka wewe ndiwe Mpaji" (38:35).

Dua hii Nabii Sulaiman(a.s) anaiomba akiwa tayari ni mfalme. Lakini baada ya hapo ndio ufalme wake ukapanuka, kama aya zinazofuatia aya zinavyobainisha:

فَسَحَّرْنَا لَهُ الرِّيحَ تَجْرِي بِأَمْرِهِ رُخَاءً حَيْثُ أَصَابَ ﴿٣٦﴾ وَالشَّيَاطِينَ  
كُلَّ بَنَاءٍ وَغَوَاصٍ ﴿٣٧﴾ وَعَاخِرِينَ مُقَرَّنِينَ فِي الْأَصْفَادِ ﴿٣٨﴾

"Basi tukamtiishia upepo unaokwenda pole pole kwa amri yake, anakotaka kufika. Pia na (Tukamtiishia) mashetani, kila ajengaye na azamiaye (lulu). Na wengine wafungwao minyororoni (wanapokhalifu amri zake)" (38:36-38).

Pamoja na ufalme na mamlaka makubwa kiasi hiki aliyopewa Sulaiman,lakini pia alipewa elimu ya kumtambua Allah(s.w) na kupewa utume. Kwa hiyo alikuwa ni mja mwenye shukrani kwa neema hizo alizofadhilishwa:

وَلَقَدْ آتَيْنَا دَاوُدَ وَسُلَيْمَانَ عِلْمًا وَقَالَا الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي فَضَّلَنَا عَلَى  
كَثِيرٍ مِّنْ عِبَادِهِ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٥﴾

Na bila shaka tuliwapa Daudi na Sulaiman ilimu (kubwa kabisa na wakamshukuru Mwenyezi Mungu) wakasema: "Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Aliyetufadhilisha kuliko wengi katika waja wake waliomuamini" (27:15).

## Uchambuzi wa Neema Alizopewa Nabii Sulaiman(a.s).

### (i) Kutiishiwa Upepo

Qur'an inatufahamisha kuwa Nabii Sulaiman alitiishiwa upepo akaweza kuutumia apendavyo kwa amri yake.

وَلِسْلِيْمَانَ الرِّيْحَ غُدُوْهَا شَهْرًا وَرَوَاحَهَا شَهْرًا ۗ وَاسْلٰنَا لَهُ وَعِيْنَ  
الْقِطْرِ ۗ وَمِنَ الْجِنِّ مَن يَّعْمَلُ بَيْنَ يَدَيْهِ بِاِذْنِ رَبِّهٖ ۗ وَمَن يَزِغْ مِنْهُمْ  
عَنۢ اٰمْرِ نَا نُنٰذِرُهٗ مِنْ عَذَابِ السَّعِيْرِ ﴿١٢﴾

*"Na kwa Sulaiman (Tukautiisha) upepo wa nguvu uendao kwa amri yake katika ardhi ambayo tumeibarikia. Nasi ndio tunaokijua kila kitu. Na kwa Sulaiman (Tukautiisha) upepo (uliokwenda) safari yake ya subuhi (mwendo wa) mwezi mmoja, na safari yake ya jioni (mwendo wa) mwezi mmoja" (34:12).*

Aya hizi zinaweka wazi kuwa, Nabii Sulaiman aliweza kufanya safari ndefu sana baharini kwa wepesi kabisa kwa vile Allah(s.w) aliutiisha upepo kiasi kwamba ulivuma katika mwelekeo wa vyombo vyake. Kwa hiyo safari ya mwezi mzima aliweza kuifanya kwa masaa machache. Na tukiwa leo katika karne ya sayansi na teknolojia ambapo madege husafiri kwa kasi ya maelfu ya kilometa kwa saa, haiwi viguvmu kwa fahamu zetu kuelewa neema hii aliyopewa Nabii Sulaiman.

### (ii) Kutiishiwa Majini.

Nabii Sulaiman(a.s) alitiishiwa majini ambayo aliyatumikisha kumfanyia kazi mbalimbali.

وَمِنَ الشَّيْطٰنِيْنَ مَن يَّغْوٰصُوْنَ لَهُ وَيَعْمَلُوْنَ عَمَلًا دُوْنَ ذٰلِكَ  
وَكَنَّا لَهُمْ حٰفِظِيْنَ ﴿١٣﴾

*"Na (Tukamtiishia) mashetani wenye kumpigia mbizi (ili wamletee lulu) na wakimfanyia vitendo vingine visivyokuwa hivyo. Nasi tulikuwa walinzi wao" (21:82)*

Tazama pia (34:12-13) na (27:17).

Ilivyokuwa kawaida mwanaadamu huishi na kushirikiana na wanaadamu wenzake. Aidha viumbe wa jinsi nyingine huishi na kuhusiana wao kwa wao. Asili ya umbile la awali la mwanaadamu ni udongo. Majini wao wameumbwa kwa moto.

Katika hali ya kawaida mwanaadamu hakupewa uwezo wa kumwona jinni. Lakini pamoja na tofuati hiyo ya kimaumbile Allah(s.w) Muweza wa yote alimpa Nabii Sulaiman uwezo wa kuyamiliki majini.

### **(iii) Utawala Juu ya Ndege**

Pamoja na kuwa mfalme, mwenye kutiwa na watu, na mwenye uwezo wa kuyatumia majini kufanyia kazi, Nabii Sulaiman alipewa uwezo pia wa kuwatawala na kuwatuma kazi ndege. Hili linawekwa wazi na aya zifuatazo:

وَحْشِرَ لِسُلَيْمَانَ جُنُودَهُ مِنَ الْجِنَّ وَالْإِنْسِ وَالطَّيْرِ فَهَمَّ

يُوزَعُونَ ﴿١٧﴾

*"Na alikusanyiwa Sulaiman majeshi yake katika majini na watu na ndege, nayo yakapangwa makundi makundi" (27:17).*

وَحْشِرَ لِسُلَيْمَانَ جُنُودَهُ مِنَ الْجِنَّ وَالْإِنْسِ وَالطَّيْرِ فَهَمَّ

يُوزَعُونَ ﴿١٧﴾

*"Na akawakagua ndege (na asimuone Hud-Hud) akasema: "Imekuwaje mbona simuoni Hud-Hud, au amekuwa miongoni mwa wasiokuwapo (hapa leo)"? (27:20).*

#### (iv) Uwezo wa kusikilizana na viumbe wengine.

Kama alivyokuwa ameneemeshwa baba yake (Nabii Daudi): Nabii Sulaiman alipewa uwezo wa kusikia lugha za viumbe wengine mbali na binaadamu. Katika Qur'an wanatajwa ndege na wadudu.

وَوَرِثَ سُلَيْمَنُ دَاوُدَ وَقَالَ يَتَأْتِيهَا النَّاسُ عَلِمْنَا مَنْطِقَ الطَّيْرِ وَأُوتِينَا  
مِنْ كُلِّ شَيْءٍ إِنَّ هَذَا لَهُوَ الْفَضْلُ الْمُبِينُ ﴿١٦﴾

*"Na Suleiman alimrithi Daudi na akasema: "Enyi watu! Tumefundishwa (hata kutambua) usemi wa ndege na tumepewa kila kitu; hakika hii ni fadhila iliyo dhahiri" (27:16).*

Habari ya kutambua lugha ya wadudu; inabainishwa katika tukio ambapo Nabii Sulaiman alikuwa akipita mahali na jeshi lake. Wadudu chungu wakapeana taafira wachukue hadhari Nabii Sulaiman asije akawapona hali ya kuwa hana habari. Nabii Sulaiman alifahamu walichokuwa wanaambizana wadudu chungu. Kwa hiyo akalisisimamisha jeshi lake mpaka walipoingia mashimoni mwao. Kisha akamshukuru Mola wake kwa neema hii.

حَتَّىٰ إِذَا أَتَوْا عَلَىٰ وَادِ النَّمْلِ قَالَتْ نَمَلَةٌ  
يَتَأْتِيهَا النَّمْلُ أُدْخُلُوا مَسَكِنَتَكُمْ لَا يَحْطِمَنَّكُمْ سُلَيْمَنُ وَجُنُودُهُ وَهُمْ  
لَا يَشْعُرُونَ ﴿١٨﴾

*Hata walipofika katika bonde la wadudu chungu; alisema mdudu chungu (kuwaambia wenziwe); "Enyi wadudu chungu! Ingieni majumbani mwenu; asikupondeni Sulaiman na majeshi yake, hali ya kuwa hawakuhisini (hawana habari)" (27:18).*



فَتَبَسَّمْ ضَاحِكًا مِّن قَوْلِهَا وَقَالَ رَبِّ أَوْزِعْنِي أَنْ أَشْكُرَ نِعْمَتَكَ  
الَّتِي أَنْعَمْتَ عَلَيَّ وَعَلَىٰ وَالِدَيَّ وَأَنْ أَعْمَلَ صَالِحًا تَرْضَاهُ وَأَدْخِلْنِي  
بِرَحْمَتِكَ فِي عِبَادِكَ الصَّالِحِينَ ﴿١٩﴾

*Basi akatabasamu akilichekea neno lake, na akasema: "Ee Mola wangu! Nipe nguvu nishukuru neema yako uliyonineemsha mimi na wazazi wangu, na nipate kufanya vitendo vizuri uvipendavyo, na uniingize kwa rehema yako katika waja wako wema" (27:19).*

Historia inaonesha kuwa mara nyingi utajiri, wingi wa watoto, uflame na mamlaka makubwa huwa ndio chanzo cha watu kutakabari na kufanya udhalimu na ufisadi katika ardhi. Tunayo historia ya Firauni, Karun, Hamana na wengineo ambao walitakabari na kufanya ufisadi kwa ajili ya utajiri na mamlaka waliyokuwa nayo. Aidha tunao kina Musolin, Stalin, Hitler, Ngueso n.k. Wapo pia Maraisi wengine ambao hawapo katika rekodi za madikteta, lakini huwanyonya, huwatesa na kuwafanyia udhalimu wa kila namna raia zao.

Nabii Sulaiman(a.s) aliwatawala binaadamu wenziwe, majini hadi ndege. Lakini kwa kutambua kuwa yote aliyokuwa nayo ni neema kutoka kwa Allah(s.w) na kwamba ipo siku atasimamishwa katika mahakama tukufu ya Allah(s.w) kujibu jinsi alivyoitumia neema ile; anakuwa mnyenyekevu na mwenye kuchunga mipaka ya Allah(s.w). Anafahamu kuwa kila kiumbe kina lengo la kuumbwa kwake na kina haki ya kuishi. Kwa hiyo anajali hata maisha ya mdugu chungu.

Nabii Sulaiman kwa kutambua kuwa neema zote hizo alizotunukiwa ni mtihani kwake,tunamuona akimuomba Mola wake ampe nguvu ya kuweza kushukuru neema alizompa.(Qur'an 27:19).

Kwa maana amjaaliye asitakabari na kuzitumia neema hizo kwa namna ambayo itawadhuru wengine iwe ni kwa kukusudia au kutokufahamu.

Ardhi yetu hii haitokuwa na amani, uhuru na salama ya kweli mpaka tuwe na viongozi wanaojali haki, uhuru na usalama wa binaadamu wenzao kama Sulaiman alivyo wajali hata wadudu chungu. Na hawa hawawezi kuwa wengine ila wale wanaomtambua Mungu mmoja na kumcha kweli kweli. Viongozi watakoongoza si kwa kufuata miongozo na katiba zilizobuniwa na watu bali kwa kufuata Kitabu cha Allah na Sunna ya Mtume wake (s.a.w).

### **Kisa cha Malkia wa Sabaa.**

Sabaa ulikuwa mji katika nchi inayojulikana leo kama Yemen. Watafiti wa mambo ya historia na geografia wanasema Sabaa ilikuwa kiasi cha umbali wa maili hamsini kutoka mji wa Sanaa. Watu wa Sabaa walikuwa wakiabudu Jua na walimfanya mtawala wao kuwa ni mwanamke - malikia.

Pamoja na ushirikina wao, Allah(s.w) aliwaneemesha watu wa Sabaa kwa kila kitu walichohitajia katika maisha yao.

Nabii Sulaiman aliwafahamu watu wa Sabaa kupitia kwa ndege Hud-Hudi kama aya zifuatazo zinavyobainisha:

وَتَقَفَّدَ الطَّيْرَ فَقَالَ مَا لِيَ لَا أَرَى الْهُدْهُدَ أَمْ كَانَ مِنَ الْغَائِبِينَ ﴿٢٠﴾  
 لِأَعَدَّبْتَهُ وَعَدَابًا شَدِيدًا أَوْ لِأَذْبَحْتَهُ أَوْ لِيَأْتِيَنِي بِسُلْطَنٍ مُّبِينٍ ﴿٢١﴾  
 فَمَكَثَ غَيْرَ بَعِيدٍ فَقَالَ أَحَطْتُ بِمَا لَمْ تُحِطُ بِهِ وَجِئْتُكَ مِنْ سَبَإٍ بِنَبَأٍ  
 يَقِينٍ ﴿٢٢﴾ إِنِّي وَجَدْتُ أَمْرًا تَمَلِكُهُمْ وَأُوتِيَتْ مِنْ كُلِّ شَيْءٍ وَلَهَا عَرْشٌ  
 عَظِيمٌ ﴿٢٣﴾ وَجَدْتُهَا وَقَوْمَهَا يَسْجُدُونَ لِلشَّمْسِ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَزَيَّنَ لَهُمُ  
 الشَّيْطَانُ أَعْمَالَهُمْ فَصَدَّهُمْ عَنِ السَّبِيلِ فَهُمْ لَا يَهْتَدُونَ ﴿٢٤﴾

*"Na akawakagua ndege (na usimuone kidege Hud-Hud) akasema: "Imekuwaje mbona simuoni Hud-Hudi, au amekuwa miongoni mwa wasiokuwepo (hapa leo)". "Kwa yakini nitamuadhibu adhabu kali au nitamchinja au ataniletea hoja iliyo wazi (ya kumzuilia kuja hapa leo)." "Basi hakukaa sana mara (Hud-Hudi akafika) akasema (kumwambia Nabii Suleiman) Nemegundua usilogundua, na ninakujia hivi kutoka (nchi inayoitwa) Sabaa na (nakuletea) habari yenye yakini." "Hakika nimekuta mwanake anawatawalia; naye amepewa kila kitu na anacho kiti cha enzi kubwa". "Nimemkuta yeye na watu wake wanalisujudia jua badala ya Mwenyezi Mungu; na shetani amewapambia vitendo vyao na akawazuilia njia (ya kheri), kwa hivyo hawakuongoka" (27:20-24).*

Baada ya taarifa hizo Nabii Sulaiman alituma ujumbe kumnasihi malkia aingie katika Uislamu. Awali malkia baada ya kushauriana na mawaziri wake aliona apoteze lengo la Sulaiman kwa kumpa zawadi. Lakini lengo la Mitume ni kufikisha ujumbe wa Allah si kuchuma. Kwa hiyo Nabii Sulaiman alimrejeshea zawadi zake na akaendeleza harakati za kumvuta malkia katika haki mpaka akasilimu. Habari hizi zimebainishwa kwa urefu katika aya Qur'an (27:27-44).

Jambo tunalotakiwa tulizingatie hapa ni ule msimamo thabiti wa Nabii Sulaiman katika kazi ya kuwalingania watu. Mara nyingi watawala hulewa tamaa ya kujilimbikizia madaraka na mali wakashau wajibu wao mbele ya Muumba wao. Malkia wa Sabaa alidhani kwa kutumia mali angemtoa Nabii Sulaiman kwenye lengo lake. Lakini haikuwa hivyo.

Hali hiyo si kwa viongozi tu na wakuu wa nchi, bali hata sisi tulio katika harakati za Da'awah tuwe makini tusitolewe kwenye lengo kwa hongo ya mali au wadhifa.

## Kusingiziwa Nabii Sulaiman Uchawi

Pamoja na Ucha-Mungu aliokuwa nao Nabii Sulaiman watu hawakuacha kumsingizia mambo machafu. Na hii imekuwa ni tabia ya watu wabaya kuwasingizia Mitume uovu ili wapate kuwapoteza watu na njia ya Allah. Nabii Suleiman katika jumla ya mambo aliyosingiziwa ni kuwa alikufuru akafundisha watu elimu ya uchawi. Qur'an inajibu shutuma hizo katika aya ifuatayo:

وَاتَّبِعُوا مَا تَتْلُوا الشَّيْطِينُ عَلَىٰ مُلْكِ سُلَيْمَانَ وَمَا كَفَرَ سُلَيْمَانُ وَلَا كَانَ  
 الشَّيْطِينُ كَفَرُوا يُعَلِّمُونَ النَّاسَ السِّحْرَ وَمَا أُنزِلَ عَلَى الْمَلَكَيْنِ بِبَابِلَ  
 هِنْرُوتَ وَمَرْوَتَ وَمَا يَعْلَمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّى يَقُولَا إِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ  
 فَلَا تَكْفُرْ فَيَتَعَلَّمُونَ مِنْهُمَا مَا يُفَرِّقُونَ بِهِ بَيْنَ الْمَرْءِ وَزَوْجِهِ  
 وَمَا هُمْ بِضَارِّينَ بِهِ مِنْ أَحَدٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ وَيَتَعَلَّمُونَ مَا يَضُرُّهُمْ  
 وَلَا يَنْفَعُهُمْ وَلَقَدْ عَلِمُوا لَمَنِ اشْتَرَاهُ مَا لَهُ فِي الْآخِرَةِ مِنْ خَلْقٍ  
 وَلَبِئْسَ مَا شَرَوْا بِهِ أَنْفُسَهُمْ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿١٠٢﴾

*Wakafuata yale waliyoyafuata mashetani (wakadai kuwa yalikuwa) katika uflame wa Sulaiman; na Sulaiman hakukufuru,*

*bali mashetani ndio waliokufuru, waliwafundisha watu uchawi (waliokuwa wakiujua wenyewe tangu zamani) na (uchawi) ulioteremshwa kwa malaika wawili; Haruta na Maruta; katika (mji wa) Babil. Wala (Malaika hao) hawakumfundisha yeyote mpaka wambwambie: "Hakika sisi ni mtihani (wa kutazamwa kutii kwenu); basi usikufuru;" Wakajifunza kwao ambayo kwa mambo hayo waliweza kumfarikisha mtu na mkewe (na mengineyo). Wala hawakuwa wenye kumdhuru yeyote kwa hayo ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na wanajifunza ambayo yatawadhuru wala hayatawafaa. Na kwa yakini wanajua kwamba aliyekhiari haya hatakuwa na sehemu yoyote katika Akhera. Na bila shaka ni kibaya kabisa walichouzia nafsi zao. Laiti wangalijua (hakika wasingefanya hivi). (2:102)*

Pamoja na aya hii kumtakasa Nabii Sulaiman na yale aliyokuwa akisingiziwa, mafundisho yafuatayo hapana budi tuyazingatie. **Kwanza**, tunafahamishwa kuwa elimu ya uchawi ipo; lakini ni mtihani kwa wanaadamu. Kujifundisha na kuufanyia kazi uchawi ni kufuru na atakayehiari kuufuata hatakuwa na sehemu yoyote katika Akhera.

Jambo la **pili** tunalotakiwa tulizingatie ni kuwa Muislamu hana haja ya kubabaika anapopatwa na janga lolote. Mwenyezi Mungu anatufahamisha kuwa huo uchawi hauwezi kumdhuru mtu ila kwa idhini yake Allah(s.w).

..... وَمَا هُمْ بِضَارِّينَ بِهِ مِنْ أَحَدٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ .....

".....Wala hawakuwa wenye kumdhuru yeyote kwa hayo ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu....." (2:102).

Kwa hiyo Muislamu amtegemee Allah(s.w) na alikabili tatizo lolote litakalomtokea kwa kuchunga mipaka ya Allah(s.w) na kuomba msaada wake.

## Kifo cha Nabii Sulaiman

Pamoja na utukufu na umadhubuti wa ufalme wake Nabii Sulaiman muda wake wa kuishi ulipokwisha aliondoka kama walivyoondoka Mitume,wafalme na wanaadamu wengine. Aidha, historia inatuonyesha kuwa kifo chake kilikuwa ndio mwanzo pia wa kuanguka kwa himaya kubwa aliyokuwa amejenga. Tunasoma katika Qur'an:

فَلَمَّا قَضَيْنَا عَلَيْهِ الْمَوْتَ مَا دَلَّهُمْ عَلَىٰ مَوْتِهِ إِلَّا دَابَّةُ الْأَرْضِ

تَأْكُلُ مِنْسَأَتَهُ فَلَمَّا خَرَّ تَبَيَّنَتِ الْجِنُّ أَنْ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ الْغَيْبَ مَا

لَبِثُوا فِي الْعَذَابِ الْمُهِينِ ﴿١٤﴾

*"Na Tulipomkidhia mauti (alipokufa) hakuna aliyewajulisha mauti yake ila mnyama wa ardhi, (mchwa) aliyekula fimbo yake. Basi ilipoanguka, majini walitambua kama wangelijua siri wasingalika katika adhabu hiyo idhalilishayo" (34:14).*

Waliomfuatia Nabii Sulaiman waliendesha maisha ya anasa na ufisadi matokeo yake yakawa ni kuporomoka kwa ufalme kuliko pelekea kuwafanya majini yawe huru.

## Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Sulaiman(a.s)

Kutokana na histoira ya Nabii Sulaiman (a.s) tunajifunza yafuatayo

- (i) Kila muumini anapotunukiwa neema na vipaji vikubwa zaidi kuliko wengine anatakiwa amshukuru Allah(s.w) zaidi kwa kujitahidi kufanya wema zaidi na ibada maalumu za ziada kuliko watu wengine kwani hiyo ni amana na mthiani kwake. Hili alilionna Nabii Sulaiman(a.s) pale aliposema.

هَذَا مِنْ فَضْلِ رَبِّي لِيَبْلُوَنِي.....

أَشْكُرُ أَمْ أَكْفُرُ ۗ وَمَنْ شَكَرَ فَإِنَّمَا يَشْكُرُ لِنَفْسِهِ ۗ وَمَنْ كَفَرَ

فَإِنَّ رَبِّي غَنِيٌّ كَرِيمٌ ﴿٤٠﴾

“.....Haya ni kwa fadhila za Mola wangu, ili anijaribu nitashukuru au nitakuwa mwizi wa fadhila, na anayeshukuru anashukuru kwa manufaa ya nafsi yake; na anayekufuru kwa hakika Mola wangu ni mkwasi, karimu (27:40)

- Mtume(s.a.w) katika kumshukuru Mola wake, alikuwa akisimama usiku mpaka miguuu yake ikawa inavimba. Maswahaba walipomrai kuwa asijitaabishe hivyo, kwani kashasamehewa madhambi yake yaliyopita naya baadaye, aliwajibu: **“Ni siwe mja mwenye kushukuru?”**
- (ii) Waumini wana dhima ya kuulingania Uislamu mijini na vijijini,ufike katika kila kona ya nchi na ulimwengu kwa ujumla tukianza kwenye familia zetu.
- (iii) Kiongozi wa Harakati za Kiislamu katika jamii hanabudi kuwanamtandao wa waumini na wanaharakati watakao muwezesha kupata taarifa za hakika juu ya hali halisi ya Uislamu kutoka kila kona ya jamii husika.
- (iv) Nguvu za elimu, Imani thabit,uchumi na nguvu za kujeshi ni nyenzo muhimu sana katika kusimamisha uislamu katika jamii.
- (v) Hatunabudi kuzichunguza habari tunazozipata juu ya watu kabla ya kuzifanyia kazi- Nabii Suleiman hakumuamini Hud Hud moja kwa moja:-

أَذْهَبْ بِكِتَابِي هَذَا فَأَلْقِهِ إِلَيْهِمْ ثُمَّ تَوَلَّ عَنْهُمْ فَانظُرْ مَاذَا

يَرِجُونَ ﴿٢٨﴾

*“Akasema (Suleiman) Tutatazama kama unasema kweli au umo katika waongo. Nenda na barua yangu hii na uwafikishie, kisha uwaache, na utawatazama wanashauriana vipi” (27:27-28)*

- (vi) Baada ya kupa uhakika juu ya jambo oву, mara moja tuweke mikakati ya kuliondoa kwa kutumia mbinu zinazostahiki.
- (vii) Kutafuta ushauri kabla ya kufikia maamuzi ni katika sifa muhimu za kiongozi wa kiislamu.
- (viii) Pamoja na kutafuta ushauri kwa wadau wa jamii yake, kiongozi mweledi ni yule anayeangalia mbali. Malkia wa Sabaa pamoja na kushauriwa na mawaziri wake kuingia vitani, hakupendelea kwa kuzingatia matokeo. Aliona saluhu ni bora zaidi kuliko vita (27:34 - 35).
- (ix) Nikawaida ya viongozi wa kitwaghuut kuwahonga au kuwarubuni viongozi wa kiislamu kwa kuwakaribisha Ikulu, kuwapa mirunda ya pesa, magari, majumba, vyeo vya bandia n.k.
- (x) Kiongozi au mwanaharakati wa kiislamu anayefanya biashara na Allah(s.w) kwa kutarajia pepo hahongeki au hawezi kurubuniwa kwa namna yoyote ile. Wanaohongeka ni wanafiki wanaopenda maisha ya dunia zaidi kuliko ya akhera.
- (xi) Imekuwa ni tabia ya maadui wa kiislamu, wakiwemo wanafiki, kuwapakazia watu wema makosa mbalimbali na kuwaita majina mabaya ya kuwadhalilisha na kuwafadhehesha ili watu wasiwasikilize na kuwafuata. Hufanya hivyo ili kujenga mazingira ya kuwapoteza watu na Dini ya Allah(s.w)



(xii)Uchawi ni njia ya Shetani na ni haramu kwa muislamu kujifunza na kuifanyia kazi elimu ya uchawi.

- Waislamu wanaelekezwa na Mola wao kuwa mara kwa mara wajikinge na shari za wachawi, mahasidi na shari za viumbe wake wengine wanaoonekana na wasio onekana, kwa kusoma kwa mazinagiatio Suratul-Ikhlash na Al-muwadhatain(Al-Falaq na An-Nas).

## ILYASA(A.S)

Mtume Ilyasa ni mmoja wa Mitume waliotumwa kupitia kizazi cha Bani Israil. Alitumwa kwa watu ambao walitupa mafundisho ya Mitume waliotangulia na badala yake wakawa wanaabudu Mungu-jua waliyemuita - Baal. Mtume Ilyasa(a.s) aliwaita watu wake wamwabudu Mungu Mmoja, Allah(s.w); lakini walimkadhibisha. Kwa ajili hiyo ya kukataa mafundisho ya Mtume wao, wakawa katika kundi la watakaoingia katika adhabu ya Allah(s.w). Isipokuwa kwa wale waliorejea kwa Mola wao wakajitakasa. Kwa muhtasari ujumbe wa Mtume Ilyasa(a.s) unapatikana katika aya zifuatazo:

وَإِنَّ الْيَاسَ لَمِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٣٣﴾ إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ أَلَا تَتَّقُونَ ﴿١٣٤﴾ أَتَدْعُونَ  
بَعْلًا وَتَذَرُونَ أَحْسَنَ الْخَالِقِينَ ﴿١٣٥﴾ اللَّهُ رَبُّكُمْ وَرَبُّ آبَائِكُمُ الْأُولِينَ  
﴿١٣٦﴾ فَكَذَّبُوهُ فَانْتَهُم لَمُحْضَرُونَ ﴿١٣٧﴾ إِلَّا عِبَادَ اللَّهِ الْمُخْلَصِينَ  
﴿١٣٨﴾ وَتَرَكْنَا عَلَيْهِ فِي الْآخِرِينَ ﴿١٣٩﴾ سَلَّمْنَا عَلَىٰ إِلْ يَا سِينِ ﴿١٤٠﴾

*"Na hakika Ilyas alikuwa miongoni mwa Mitume. (Wakumbushe) Alipowaambia watu wake: "Oh! Hamuogopi?" "Mnamuomba (na kumuabudu) Baal na mnamuacha aliye Mbora wa waumbaji (na ndiye Muumbaji peke yake)." "Mwenyezi Mungu, Mola wenu na Mola wa wazee wenu wa mwanzo!" Wakamkadhibisha. Basi bila shaka watarudishwa (adhabuni). Isipokuwa waja wa*

*Mwenyezi Mungu waliosafishwa (na Mwenyezi Mungu). Na tumemuachia (sifa nzuri) kwa (watu wote) Amani kwa Ilyas" (37:123-130).*

## **YUNUS(A.S)**

Nabii Yunus(a.s) ni miongoni mwa Mitume wa Allah(s.w) waliotajwa katika Qur-an. Yunus(a.s) ametajwa katika Qur-an kwa majina matatu:

### **(i) "Yunus" (37:139)**

وَإِنَّ يُونُسَ لَمِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٣٩﴾

*Na hakika Yunus alikuwa miongoni mwa Mitume.*

### **(ii) "Dhun-Nun"**

وَذَا النُّونِ إِذ ذَّهَبَ مُغْرِبًا فَظَنَّ أَنْ لَنْ نَقْدِرَ عَلَيْهِ فَنَادَى فِي الظُّلُمَاتِ  
أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ سُبْحَانَكَ إِنِّي كُنْتُ مِنَ الظَّالِمِينَ ﴿٨٧﴾

*Na (Mtaje) Dhun-Nun (Yunusi) alipoondoka hali amechukiwa, na akadhani ya kwamba hatutamdhikisha. Basi (alipozongwa) aliita katika giza (akasema): Hakuna aabudiwaye isipokuwa Wewe, Mtakatifu "Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu (nafsi zao)." (21:87)*

### **(iii) "Sahibul-Hut" (Mmezwa na Chewa)**

فَأَصْبِرْ لِحُكْمِ رَبِّكَ وَلَا تَكُنْ كَصَاحِبِ الْحُوتِ إِذْ نَادَى وَهُوَ مَكْظُومٌ ﴿٤٨﴾

*Basi subiri kwa hukumu ya Mola wako, wala usiwe kama mmezwa na Chewa (Yunusi). (Kumbuka) alipolingana, (alipomwita Mwenyezi Mungu), na hali ya kuwa amezongwa (barabara).(68:48)*

Majina ya “**Dhun-Nun**” na “**Sahibul-Hut**” yana maana ya “Mwenye kumezwa na samaki (chewa).” Nabii Yunus (a.s) ameitwa majina hayo mawili kutokana na historia ya maisha yake ya Da’awah iliyompelekea mpaka akamezwa na samaki mkubwa (chewa) kisha akatapakwa ufukoni akiwa hai kwa uwezo wa Allah(s.w).

## **Yunus(a.s) Kulingania Uislamu kwa Watu Wake**

Nabii Yunus(a.s) alitumwa kufikisha ujumbe wa Allah(s.w) kwa watu laki moja na zaidi wa mji wa **Ninawah** (Nineveh) katika nchi ya Assyria. Ninawah ni mji wa zamani sana ambao hauko katika ramani hivi sasa. Mji huo ulikuwa kandokando ya mto Tigris sehemu iliyo mkabala na mji wa kisasa, Mosul, kilometa 368 kaskazini ya kaskazini magharibi mwa mji wa Baghdad.

Nabii Yunus(a.s) aliwalingania Uislamu watu wa mji ule, lakini walimkanusha. Allah(s.w) alimuagiza Nabii Yunus awaonye watu wake juu ya adhabu itakayowafika baada ya muda maalumu uliowekwa endapo wataendelea kumuasi. Yunus(a.s) alipoona kuwa muda wa adhabu unakaribia na bado watu wake wameshikilia msimamo wao wa kukanusha ujumbe wake, alikata tamaa na kuamua kuondoka kwenye mji ule kuihami nafsi yake na adhabu ya Allah, bila ya kupewa ruhsa ya kuhama na Mola wake kama walivyopewa ruhsa Mitume wengine.

Watu wa mji ule walipoona adhabu inakaribia, walimuamini Nabii Yunus kuwa ni Mtume wa haki, wakamuamini Allah(s.w) na kumnyenyekeka ipasavyo na kumuomba msamaha kwa maovu yao. Allah(s.w) kwa rehema yake aliwasamehe na kuwaondolea adhabu ile kama tunavyojifunza katika Qur-an:

فَلَوْلَا كَانَتْ قَرْيَةٌ ءَامَنَتْ فَتَنَعَهَا إِيمَانُهَا إِلَّا قَوْمَ يُونُسَ لَمَّا ءَامَنُوا كَشَفْنَا عَنْهُمْ ءَآذَابَ الۡخِزْيِ فِي الۡحَيَاةِ الدُّنْيَا وَمَتَّعْنَاهُمْ إِلَىٰ حِينٍ ﴿٩٨﴾

*Kwanini usiweko mji ulioamini (upesi kabla ya kuadhibiwa), ili imani yake iwafae? Isipokuwa watu wa Yunus (tu ndio walioamini mara walipohisi kuwa adhabu inakuja. Basi wakaokoka). Walipoamini tuliwaondolea adhabu ya hizya katika maisha ya dunia na tukawastarehesha kwa muda (tulioutaka). (10:98)*

Nabii Yunus(a.s) hakujua yaliyopita nyuma yake. Alipoona adhabu haikushuka alichelea kuwa watu wa mji ule watazidi kumkanusha. Akakimbilia Pwani ambako alipata jahazi akaingia. Jahazi ilisheheni kiasi kwamba halikuweza kwenda. Ikapigwa kura ili itakaye muangukia atoswe baharini. Ikamuangukia Nabii Yunus(a.s) akatoswa baharini na kumezwa na chewa (samaki mkubwa)

وَإِنَّ يُونُسَ لَمِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٣٩﴾ إِذْ أَبَقَ إِلَى الْفُلِ الْمَشْحُونِ ﴿١٤٠﴾

*Na hakika Yunusi alikuwa miongoni mwa Mitume. (Kumbukeni) alipokimbilia katika jahazi iliyosheheni.(37:139-140)*

فَسَاهَمَ فَكَانَ مِنَ الْمُدْحَضِينَ ﴿١٤١﴾ فَالْتَقَمَهُ الْحُوتُ وَهُوَ مُلِيمٌ ﴿١٤٢﴾ فَلَوْلَا أَنَّهُ كَانَ مِنَ الْمُسَبِّحِينَ ﴿١٤٣﴾

*Na wakapiga kura. Basi akawa miongoni mwa walioshindwa (ikapasa atupwe baharini). Mara samaki alimmeza hali ya kuwa ni mwenye kulaumiwa. Basi isingelikuwa ya kwamba yeye alikuwa ni miongoni mwa waliokuwa wanamuabudu (Mwenyezi Mungu vilivyo). (37:141-143)*

لَلَّيْتُ فِي بَطْنِهِ ۖ إِلَىٰ يَوْمِ يُبْعَثُونَ ﴿١٤٤﴾

*Bila shaka angalika tumboni mwake mpaka siku watakakayofufuliwa (viumbe). (37:144)*

## **Nabii Yunus(a.s) Amuomba Allah(s.w) Msamaha**

Ndani ya tumbo la samaki, Nabii Yunus(a.s) akiwa hai na akili timamu aligundua kosa lake la kuwakimbia watu wake bila ya ruhusa kutoka kwa Mola wake. Ilibidi Yunus (a.s) alalame ndani ya tumbo la samaki kumuomba msamaha Mola wake na kuomba msaada wake.

وَذَا النُّونِ إِذ ذَّهَبَ مُغْرَضًا فَظَنَّ أَن لَّن نَّجِدَ عَلَيْهِ فَنَادَى فِي الظُّلُمَاتِ  
أَن لَّا إِلَهَ إِلَّا أَنَا أَنتَ سُبْحَانَكَ إِنِّي كُنْتُ مِنَ الظَّالِمِينَ ﴿٨٧﴾

*Na (Mtaje) Dhun-Nun (Yunusi) alipoondoka hali amechukiwa, na akadhani ya kwamba hatutata mdhikisha. Basi (alipozongwa) aliita katika giza (akasema): “Hakuna aabudiwaye isipokuwa Wewe Mtakatifu hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu (nafsi zao).” (21:87)*

Allah(s.w) alimsamehe mja wake Yunus(a.s) na kumuokoa katika janga lile kwa kumuelekeza samaki amrudishe pwani na kumtapika.

فَأَسْتَجَبْنَا لَهُ وَنَجَّيْنَاهُ مِنَ الْغَمِّ وَكَذَلِكَ نُنْجِي الْمُؤْمِنِينَ ﴿٨٨﴾

*“Basi tukampokelea (toba na dua yake) na tukamuokoa katika huzuni ile. Na namna hivyo ndivyo tuwaokoavyo walioamini.” (21:88)*

﴿ فَتَبَدَّدْنَاهُ بِالْعُرَّاءِ وَهُوَ سَقِيمٌ ﴿١٤٥﴾ ﴾

*Lakini tukamtupa ufukoni (kwa kutapikwa na huyo samaki) hali ya kuwa mgonjwa.” (37:145)*

Baada ya kufikishwa pale pwani, Yunus (a.s) alikuwa mgonjwa na dhaifu asiyejiweza kwa lolote. Mola wake alizidi kumrehemu kwa kumuoteshea mti wa **mbarikhi** ambao aliula ukampa afya ya kumuwezesha kuwarudia watu wake ambao aliwakuta wameshaamini na wanamngojea kwa hamu ili awape mafunzo na maelekezo waweze kumuabudu Mola wao inavyostahiki:

وَأَذْبَتْنَا عَلَيْهِ شَجَرَةً مِّن يَّقُطِينٍ ﴿١٤٦﴾

*Na tukamuoteshea mmea wa mbarikhi (akawa anakula). (37:146)*

وَأَرْسَلْنَاهُ إِلَى مِائَةِ أَلْفٍ أَوْ يَزِيدُونَ ﴿١٤٧﴾ فَفَاتَمُوا فَمَتَّعْنَاهُمْ إِلَىٰ حِينٍ ﴿١٤٨﴾

*“Na tulimpeleka kwa (watu) laki moja au zaidi, (wale wale watu wake). Basi wakaamini na tukawastarehesha mpaka muda wao wa kufa.” (37:147-148)*

## **Mafunzo yatokanayo na Historia ya Nabii Yunus(a.s)**

Kutokana na Historia ya Nabii Yunusi(a.s) tunajifunza yafuatayo:

- (i) Allah(s.w) ni mwingi wa kusamehe na mwingi wa kurehemu, hivyo waumini wamuelekee Allah kumuomba msamaha hata kama wamefanya kosa kubwa kiasi gani.
- (ii) Toba inayokubaliwa pamoja na sharti nyingine ni ile inayoletwa kabla ya muda wa hukumu ya adhabu ya Allah (s.w) au kabla ya kufikwa na mauti:

وَلَيْسَتِ التَّوْبَةُ لِلَّذِينَ يَعْمَلُونَ السَّيِّئَاتِ حَتَّىٰ إِذَا حَضَرَ أَحَدَهُمُ الْمَوْتُ قَالَ إِنِّي تُبْتُ الْإِسْمَ وَلَا الَّذِينَ يَمُوتُونَ وَهُمْ كُفَّارًا أُولَٰئِكَ أَعْتَدْنَا لَهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٨﴾

*Hawana toba wale ambao hufanya maovu mpaka mauti*

yamemhudhuria mmoja wao, (hapo) akasema: “Hakika mimi sasa natubu.” Wala (hawana toba) wale ambao wanakufa katika hali ya ukafiri. Hao tumewaandalia adhabu iumizayo. (4:18)

- (iii) Katika kazi ya Da’awah (kulingania Uislamu) tusiwakatie tamaa watu bali tuendeleo nao kwa kubadilisha mbinu mpaka mwisho wa uhai wetu au mpaka Allah(s.w) apitishie hukumu yake. Tumuije Nabii Nuhu(a.s) kwa subira (alilingania kwa miaka 950) na tusirudie kosa la kukosa subira la Nabii Yunus(a.s).
- (iv) Matendo mema na ucha-Mungu, huwa ni sababu ya dua na toba ya mja kuwa kabuli mbele ya Allah(s.w).

﴿١٤٤﴾ فَلَوْلَا أَنَّهُ كَانَ مِنَ الْمُسَبِّحِينَ ﴿١٤٣﴾ لَلَّيْتُ فِي بَطْنِهِ إِلَى يَوْمِ يُبْعَثُونَ ﴿١٤٤﴾

“Basi isingelikuwa ya kwamba yeye (Yunus) alikuwa miongoni mwa waliokuwa wanamuabudu (Allah(s.w) vilivyo) bila shaka angalika tumboni mwaka (huyo samaki) mpaka siku watakatayofufuliwa (viumbe)”. (37:143-144)

## ZAKARIA(A.S) NA YAHYA(A.S)

Nabii Zakaria(a.s) ni miongoni mwa mitume wa Bani Israil (Mayahud) na anatokana na kizazi cha Nabii Sulaiman(a.s). Alikuwa mwangalizi mkuu wa nyumba ya Ibada na alikuwa anapta riziki yake kwa kazi ya useremala.

### Zakaria(a.s) Kumlea Maryam na Kuomba Mtoto Mwema

Zakaria(a.s) alichaguliwa na ukoo kumlea Maryamu, mama yake Nabii Issa(a.s). Alimlea vyema katika malezi ya kiislamu.

Katika kumlea Maryamu, Zakaria(a.s) siku moja alishangaa kumkuta Maryam binti Imraan na vyakula mezani ambavyo hakumpa yeye, ikabidi amuilize:-

.....يَمْرَيْمُ أَنْى لَكَ هَذَا قَالَتْ هُوَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ إِنَّ

اللَّهُ يَرْزُقُ مَنْ يَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٣٧﴾

“.....Ewe Maryam! unapta wapi hivi ? Akasema: Hivi  
vinatoka kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu  
humruzuku amtakaye bila ya hisabu” (3:37)

Jibu hili la Maryamu lilimsisimua na kumuhamasisha Mzee Zakaria kiasi cha kumfanya naye amuelekee Mola wake na kumuomba mtoto mwema atakaye mrithi katika ucha-mungu na kusimamisha Dini ya Allah(s.w) katika jamii. Zakaria(a.s) alimuelekea Mola wake na kulalama.

قَالَ رَبِّ إِنِّى وَهَنَ الْعَظْمُ مِنِّى وَأَسْتَعْلَى الرَّأْسُ شَيْبًا وَلَمْ  
أَكُنْ بِدُعَاؤِكَ رَبِّ شَقِيًّا ﴿٤١﴾ وَإِنِّى خِفْتُ الْمَوَالِىَ مِنْ وَرَأَى  
وَكَانَتِ امْرَأَتِى عَاقِرًا فَهَبْ لى مِن لَّدُنكَ وَلِيًّا ﴿٤٢﴾ يَرِثُنِى وَيَرِثْ مِنِّى  
ءَالَ يَعْقُوبَ وَأَجْعَلْهُ رَبِّ رَضِيًّا ﴿٤٣﴾

Akasema: “Mola wagu. Bila shaka mifupa yangu imekuwa dhaiifu na kichwa kinawaka (kinan’gara) kwa mvi,wala sikuwa mweye bahati mbaya (mwenye kukhasirika) Mola wangu, kwa kukuomba wewe. Na hakika mimi nawahofia jamaa zangu baada yangu(kuharibu Dini). Na mke wangu ni tasa. Basi nipe mrithi (anijie) kutoka kwako. Atakaye nirithi na kuwa na kuwarithi(wazee wake wengine)kizazi cha Ya’aquub. Na umfanye, Mola wangu mwenye kukuridhisha”(19:4-6)



## Yahya(a.s) Jibu la Dua ya Mzee Zakaria(a.s)

Dua ya Zakaria(a.s) ilijibiwa kwa kubashiriwa kupata mtoto, Yahya

يَنْزِكْرِيَا إِنَّا نُبَشِّرُكَ بِغُلَامٍ أَصْمُومٌ يَحْيَىٰ لَمْ نَجْعَلْ لَهُ

مِنْ قَبْلُ سَمِيًّا ﴿٧﴾

(Akaambiwa): “Ewe Zakaria! Tunakupa habari njema ya (kuwa utazaa)mtoto, jina lake ni Yahya: Hatujafanya kabla yake aliye na jina namna hilo.” (19:7)

## Yahya(a.s) Kupewa Utume

Alizaliwa mtoto Yahya na kupewa utume akingali mtoto na akainukia kuwa mtu mwema kwa wazazi wake na kwa walimwengu wote kwa ujumla. Alijitoa muhanga kwa ajili ya kulingania Dini ya Allah(s.w).

يَنْحِىيْ خُذِ الْكِتَابَ بِقُوَّةٍ وَاَتَيْنَاهُ الْحُكْمَ صَبِيًّا ﴿١٢﴾ وَحَنَانًا

مِّن لَّدُنَّا وَرَكُوعًا وَكَانَ تَقِيًّا ﴿١٣﴾ وَبَرًّا بِوَالِدَيْهِ وَلَمْ يَكُن جَبَّارًا

عَصِيًّا ﴿١٤﴾ وَسَلَّمٌ عَلَيْهِ يَوْمَ وُلِدَ وَيَوْمَ يَمُوتُ وَيَوْمَ يُبْعَثُ حَيًّا ﴿١٥﴾

“Ewe Yahya! kishike kitabu (hiki unachopewa) kwa hima kubwa.” Na tulimpa hikima angali mtoto. Na (tukamfanya ni) huruma kutoka kwetu, na utakaso na akawa mcha-Mungu. Na mwema kwa wazazi wake wala hakuwa jeuri ,asi. Na amani ilikuwa juu yake siku aliyozaliwa na siku aliyokufa na siku atakayofufuliwa hai.(19:12-15)

Nabii Zakaria na Yahya(a.s),wote waliuliwa na Mayahud.

## **Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Zakaria(a.s) na Yahya(a.s)**

Kutokana na Historia ya Nabii Zakaria (a.s) na Yahya (a.s) tunajifunza yafuatayo:

- (i) Tuwe makini katika kulea watoto wetu hasa mabinti – Binti akileleka vizuri atakuwa ni chimbuko la malezi bora katika jamii.
- (ii) Tusichoke kumuomba Allah(s.w) jambo lolote la msingi tunalohitajia kwa ajili ya kusimamisha Uislamu na kuendeleza wema katika jamii – Hapana linaloshindikana kwa Allah(s.w).
- (iii) Waumini wanaharakati wa kusimamisha Uislamu katika jamii, waombe watoto wema watakaorithi harakati za Kiislamu na kuziendeleza kwa ari na hima zaidi.
- (iv) Ili watoto wetu waweze kuwa wanaharakati wazuri, hatunabudi sisi wenyewe kuwa mfano mwema wa kuigwa kama alivyokuwa mzee Zakaria(a.s) na kisha tuwafunze kwa kina elimu sahini ya Uislamu inayotokana na Qur-an na Sunnah na tuwape kwa upana elimu ya mazingira.
- (v) toto anayependeka mbele ya Allah(s.w) ni yule anayewafanyia wema wazazi wake kisha kuifanyia wema jamii. Mtu hawezi kuwa mwema kwa jamii yake endapo ameshindwa kuwatendea wema wazazi wake waliomzaa na kumlea kwa taabu.
- (vi) Kila mtoto anazaliwa katika amani, (katika Uislamu). Atabakia kuwa katika amani mpaka kufa kwake na kufufuliwa kwake endapo tutamlea Kiislamu naye akaendelea kubakia kuwa Muislamu mtendaji mwenye kufanya jitihada za makusudi za kusimamisha Uislamu katika jamii baada ya balebhe yake mpaka kufa kwake.

## ISA(A.S)

Nabii Isa(a.s) huitwa “Yesu”, na “Jesus” katika Biblia ya Kiswahili na Kiingereza. Majina yote hayo matatu yanamkusudia mwana wa Maryamu aliyezaliwa bila baba, ambaye ni Mtume wa mwisho kwa Bani Israil.

### Nasaba na kuzaliwa Nabii Isa(a.s)

Nabii Isa(a.s) ni mtoto wa Maryamu aliyekuwa mwana wa Imraani. Kizazi cha Imraani kilichaguliwa na Allah(s.w) kupewa Utume kama tunavyofahamishwa:

﴿۳۳﴾ إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَىٰ آدَمَ وَنُوحًا وَإِبْرَاهِيمَ وَعَالًا عِمْرَانَ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿۳۳﴾

*Hakika Mwenyezi Mungu alimchagua Adamu na Nuhu na kizazi cha Ibrahiimu na kizazi cha Imraani juu ya walimwengu wote(3:33)*

### Kuzaliwa Maryamu, Mama wa Nabii Isa(a.s)

Mke wa Imraani aliweka nadhiri kwa Allah(s.w) kuwa mtoto atakayemzaa atamuweka **wakfu**. Alitarajia kuwa atazaa mtoto wa kiume.

إِذْ قَالَتْ امْرَأَتُ عِمْرَانَ رَبِّ إِنِّي نَذَرْتُ لَكَ مَا فِي بَطْنِي مُحَرَّرًا

فَتَقَبَّلَ مِنِّي إِنَّكَ أَنْتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿۳۵﴾

*Aliposema mke wa Imraani: “Mola wangu! Nimeweka nadhiri kwako aliye tumboni mwangu kuwa wakfu, basi nikubalie, bila shaka Wewe ndiye usikiaye na ujuaye.(3:35)*

فَلَمَّا وَضَعَتْهَا قَالَتْ رَبِّ إِنِّي وَضَعْتُهَا أُنْثَىٰ وَاللَّهُ

أَعْلَمُ بِمَا وَضَعْتَ وَلَيْسَ الذَّكَرُ كَالْأُنْثَىٰ وَإِنِّي سَمَّيْتُهَا مَرْيَمَ

وَإِنِّي أُعِيدُهَا بِكَ وَذُرِّيَّتَهَا مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ ﴿۳۶﴾

*Basi alipomzaa alisema: “Mola wangu! Nimezaa mwanamke”- Na Mwenyezi Mungu anajua sana aliyemzaa -”Na mwanaume si sawa na mwanamke. Na nimempa jina Maryam. nami namkinga kwako, yeye na kizazi chake, uwalinde na shetani aliyewekwa mbali na rehema zako (3:36)*

## **Zakaria(a.s) Akabidhiwa Ulezi wa Maryam**

Baada ya kupigwa kura juu ya nani awe mlezi wa Maryam, Nabii Zakaria akachaguliwa kuwa mlezi wa Maryam. Allah(s.w) akaikubali ile nadhiri na dua ya mama yake Maryam.

فَتَقَبَّلَهَا رَبُّهَا بِقَبُولٍ حَسَنٍ وَأَنْبَتَهَا نَبَاتًا حَسَنًا وَكَفَّلَهَا  
 زَكَرِيَّا كُلَّمَا دَخَلَ عَلَيْهَا زَكَرِيَّا الْمِحْرَابَ وَجَدَ  
 عِنْدَهَا رِزْقًا قَالَ يَمْرِيْمُ أَنَّى لَكَ هَذَا قَالَتْ هُوَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ إِنَّ  
 اللَّهَ يَرْزُقُ مَنْ يَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٣٧﴾

*Basi Mola wake akampokea (mtoto) kwa mapokezi mema na akamkuza kwa makuzi mema, na akamfanya Zakaria awe mlezi wake. Kila mara Zakaria alipoingia chumbani(kwa Maryam) alikuta vyakula pamoja naye. Akauliza: “Ewe Maryam! Unapatawapi hivi? Akajibu: “Hivi vinatoka kwa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu humruzuku amtakaye bila kutarajia(3:37)*

Aya hizi zinatuaonesha kuwa Maryam alikuwa katika malezi mema na uangalizi wa karibu toka kwa Nabii Zakaria(a.s) kiasi cha kuepusha mazingira ya ufuska yasimfikie.Allah(s.w) aliweka maandalizi haya mapema ili atakapoleta muujiza wake kwa Maryam kuzaa mtoto bila ya kuwa na mume isionekane kuwa alikuwa mzinifu, bali iwe ni dalili ya kuwepo Allah(s.w) mwenye nguvu na uwezo wa kila kitu.

Kutokana na mazingira hayo na hifadhi ya Allah(s.w) Maryam akakua vyema na kupata hadhi ya kuwa mwanamke bora kuliko wanawake wote:

وَإِذْ قَالَتِ الْمَلَأِكَةُ يَمْرُؤِمُ إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَاكِ وَطَهَّرَكِ وَأَصْطَفَاكِ عَلَيَّ  
 نِسَاءِ الْعَالَمِينَ ﴿٤٢﴾

“Na (kumbuka) Malaika waliposema: “Ewe Maryamu! Kwa hakika Mwenyezi Mungu amekuchagua na kukutakasa na kukutukiza kuliko wanawake wa ulimwengu (wote).(3:42)

### Maryam Apewa Habari ya Kumzaa Isa(a.s)

Baada ya maandalizi hayo ya kimalezi pamoja na hifadhi ya Allah(s.w) aliyopewa Maryam, Allah(s.w) akamtuma Malaika kumueleza Bi Maryam habari za kumzaa masihi, Isa(a.s) bila ya baba ila kwa amri ya Allah(s.w) ya “Kuwa ikawa”. Malaika akamwambia:

إِذْ قَالَتِ الْمَلَأِكَةُ يَمْرُؤِمُ إِنَّ اللَّهَ يُبَشِّرُكِ بِكَلِمَةٍ مِّنْهُ  
 اسْمُهُ الْمَسِيحُ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ وَجِيهًا فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَمِنَ  
 الْمُقَرَّبِينَ ﴿٤٥﴾

Ewe Maryam! Mwenyezi Mungu anakupa habari njema (za kumzaa mtoto kwa) neno litokalo kwake. Jina lake Masihi Isa bin Maryam, mwenye heshima katika dunia na akhera, na ni miongoni mwa waliotukuzwa.(3:45)

وَيُكَلِّمُ النَّاسَ فِي الْمَهْدِ وَكَهْلًا وَمِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٤٦﴾

Naye atazungumza na watu katika utoto na katika utu uzima wake, na ni katika watu wema (3:46)

قَالَتْ رَبِّ أَنَّى يَكُونُ لِي وَلَدٌ وَلَمْ يَمَسَّسْنِي بَشَرٌ قَالَ كَذَلِكَ أَلَّهُ يَخْلُقُ مَا يَشَاءُ إِذَا قَضَىٰ أَمْرًا فَإِنَّمَا يَقُولُ لَهُ وَكُن فَيَكُونُ ﴿٤٧﴾

*Maryam Akasema: Mola wangu! Nitapataje Mtoto hali mtu yoyote hakunigusa? Akajibu: Ndivyo, vivyo hivyo; Mwenyezi Mungu huumba anavyopenda: anapohukumu jambo, huliambia 'Kuwa', likawa(3:47)*

وَيُعَلِّمُهُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَالتَّوْرَةَ وَالْإِنْجِيلَ ﴿٤٨﴾ وَرَسُولًا إِلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ .....

*Na Mwenyezi Mungu atamfunza kitabu na hekima, na kujua Taurati na Injili. Na ni Mtume kwa wana wa Israili.....(3:48-49)*

## Kuzaliwa Nabii Isa(a.s)

Allah(s.w) anatueleza kuwa Nabii Isa(a.s) alizaliwa chini ya mtende, na wala hakuzaliwa kwenye zizi la ng'ombe lenye najisi kama wanavyodai katika Biblia.

﴿٢٢﴾ فَحَمَلَتْهُ فَانْتَبَذَتْ بِهِ مَكَانًا قَصِيًّا ﴿٢٣﴾ فَأَجَاءَهَا الْمَخَاضُ إِلَىٰ جِذْعِ النَّخْلَةِ قَالَتْ يَدَايَئِي مِثُّ قَبْلَ هَذَا وَكُنْتُ نَسِيًّا مِّنْ نَّسِيًّا ﴿٢٤﴾

*Basi (Maryam) akachukua mimba yake, na akaondoka nayo mahali pa mbali. Kisha uchungu ukampeleka katika shina la mtende, akasema: "Laiti ningekufa kabla ya haya, na ningekuwa niliyesahaulika kabisa. (19:22-23)*

فَنَادَاهَا مِن تَحْتِهَا أَلَّا تَحْزَنِي قَدْ جَعَلَ رَبُّكِ تَحْتَكِ

سِرِّيًّا ﴿٢٤﴾ وَهَرِيءَ إِلَيْكَ بِجِذْعِ النَّخْلَةِ تُسْقِطُ عَلَيْكَ رَطْبًا جَنِيًّا ﴿٢٥﴾

*Mara ikamfika sauti kutoka chini yake inamwambia: "Usihuzunike". Hakika Mola wako amejalia kijito cha maji*

chini yako”. Na litikise kwako shina la mtende, litakuangushia tende nzuri, zilizo mbivu. (19:24-25)

فَكُلِي وَأَشْرَبِي وَقَرِّي عَيْنًا.....<sup>ط</sup>

Basi ule na unywe litue jicho lako.(19:26)

## Nabii Isa(a.s) Azungumza Akiwa Mtoto Mchanga

Maryam akamtwaa mwanawe, akaenda naye kwa jamaa zake amembeba. Watu wakastaajabu na kuwaza, imewezekanaje Maryam asiye mzinzi kumpata mtoto bila kuolewa. Na wengine wakauliza:

يَدْمَرِيْمُ لَقَدْ جِئْتِ شَيْئًا فَرِيًّا .....<sup>٢٧</sup>

يَتَأَخْتِ هُنُورًا مَا كَانَ أَبُوكَ امْرَأَ سَوْءٍ وَمَا كَانَتْ أُمُّكَ بَعْثًا<sup>٢٨</sup>

.....“Ewe Maryam! Hakika umeleta jambo la ajabu: Ewe dada yake Haruni! Baba yako hakuwa mtu mbaya wala mama yako hakuwa hasharati (19:27-28)

Kwa maswali hayo, ikawepo haja ya kumtakasa Maryam kuwa japo hakuolewa, hakumpata mtoto huyo kwa zinaa. Ndipo ikatimia kauli ya Allah(s.w) kuwa Nabii Isa(a.s) atazungumza akiwa kichanga.

فَأَشَارَتْ إِلَيْهِ قَالُوا كَيْفَ نُكَلِّمُ مَنْ كَانَ فِي الْأَمْتِدِ صَبِيًّا<sup>٢٩</sup>

Maryam akaashiria kwake (yule mtoto wamuulize yeye).

Wakasema: “Tutazungumzaje na aliye bado mtoto kitandani?

(19:29)

قَالَ إِنِّي عَبْدُ اللَّهِ ءَاتَنِي الْكِتَابَ وَجَعَلَنِي نَبِيًّا<sup>٣٠</sup> وَجَعَلَنِي مُبَارَكًا

أَيْنَ مَا كُنْتُ وَأَوْصَانِي بِالصَّلَاةِ وَالزَّكَاةِ مَا دُمْتُ حَيًّا<sup>٣١</sup>

(Yule mtoto) akasema: “Hakika mimi ni mja wa Mwenyezi Mungu, Amenipa kitabu na Amenifanya Nabii. Amenifanya

*mbarikiwa popote nilipo. Na ameniusia swala na zaka maadamu ni hai. (19:30-31)*

وَبَرًّا بِوَالِدَتِي وَلَمْ يَجْعَلْنِي جَبَّارًا شَقِيًّا ﴿٣٢﴾ وَالسَّلَامُ عَلَيَّ  
يَوْمَ وُلِدْتُ وَيَوْمَ أَمُوتُ وَيَوْمَ أُبْعَثُ حَيًّا ﴿٣٣﴾

*Na ameniusia kumfanyia wema mama yangu. Wala hakunifanya niwe jeuri, muovu. Na amani iko juu yangu siku niloyozaliwa, siku nitakayokufa na siku nitakapofufuliwa kuwa hai(19:32-33)*

## **Je, Nabii Isa(a.s) ni Mtoto wa Mungu?**

Mwenyezi Mungu si kiumbe. Yeye ndiye Muumba wa kila kitu kilicho na kisicho na uhai. Kuzaa ni sifa za viumbe vya Mwenyezi Mungu, hivyo Mungu si baba mzazi wa Yesu wala si baba wa mwanadamu yeyote. Qur'an tukufu inatuamrisha:

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ﴿١﴾ اللَّهُ الصَّمَدُ ﴿٢﴾ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ ﴿٣﴾ وَلَمْ يَكُنْ  
لَهُ وُكُوفًا أَحَدٌ ﴿٤﴾

*Sema: Yeye Mwenyezi Mungu aliye mmoja (tu). Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kuhitajiwa na viumbe. Hakuzaa wala hakuzaliwa. Na wala hafanani na yeyote(112:1-4)*

Ama katika Biblia, neno Baba limetumika kuonesha sifa ya ulezi wa Mwenyezi Mungu kwa viumbe wake, hivyo, Mwenyezi Mungu kuitwa Baba haimaanishi kuwa kamzaa Yesu au binadamu yeyote miongoni mwetu. Na ndiyo maana akasema:

*Wala msimwite mtu baba duniani, Maana Baba yenu ni mmoja aliye wa mbinguni, wala msiitwe viongozi, maana kiongozi wenu ni mmoja, naye ndiye Kristo(Mathayo 23:9-10)*



Na katika maandiko mengine ya Biblia, Yesu amenukuliwa akisema:

*Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni; Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, hapa duniani kama mbinguni (Mathayo 6:9-10)*

Kwa maana hii, Mwenyezi Mungu ni Baba wa watu wote, si baba wa Yesu tu. Ni Baba yetu, ila si kwamba katuzaa, bali ulezi wake wa kutujaalia riziki za kila aina na kutupatia elimu na teknolojia ya kuweza kuzitumia neema na riziki hizo. Hivyo Isa(a.s) si mwana wa Mungu wa kuzaa, bali ni kiumbe wake aliyemuumba kwa neno la ‘Kuwa’, likawa kama alivyo muumba Adamu.

إِنَّ مَثَلَ عِيسَىٰ عِنْدَ اللَّهِ كَمَثَلِ آدَمَ خَلَقَهُ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ قَالَ لَهُ وَاكُنْ

فَيَكُونُ ﴿٥١﴾

*Bila shaka mfano wa Isa mbele ya Mwenyezi Mungu ni kama Adamu; alimuumba kwa udongo, kisha akamwambia “Kuwa”, akawa.(3:59)*

## **Nabii Isa(a.s) Alitumwa kwa Wana wa Israil.**

Mtume Isa(a.s.)alipewa Utume na kuamrisha kufikisha ujumbe wa Allah(s.w) kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israil. Akibainisha juu ya jambo hili, Nabii Isa(a.s) alisema:

..... يَنْبِئُ إِسْرَائِيلَ إِذْ يَرْسُولُ اللَّهُ إِلَيْكُمْ مُّصَدِّقًا

لِمَا بَيْنَ يَدَيْ مِنَ التَّوْرَةِ وَ مُبَشِّرًا بِرَسُولٍ يَأْتِي مِنْ

أَسْمُهُوَ أَحْمَدٌ فَلَمَّا جَاءَهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ قَالُوا هَذَا سِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿٦١﴾

*“.....Enyi wana wa Israili; Mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, nisadikishaye yaliyokuwa kabla yangu katika Taurati na kutoa habari njema ya Mtume atakayekuja nyuma yangu ambaye jina lake litakuwa Ahmad. (61:6).*

Na katika Biblia tunafahamishwa kuwa Nabii Isa(a.s)alisema kauli hiyo kwamba yeye ni Mtume kwa wana wa Israili tu. Ukweli huu unajitokeza pale Yesu alipojibu, akisema:

*Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israili(Mathayo 15:21-24)*

## **Ujumbe wa Nabii Isa(a.s) kwa Wana wa Israil**

**(i) Mungu ni mmoja,wapekee,si watatu,na yeye si Mungu**

**Kwanza** kabisa, Nabii Isa(a.s) aliwataka watu wamjue na kumuamini Mwenyezi Mungu mmoja aliye wa pekee, na kuwataka wakubali kuwa yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Akawaambia:

إِنَّ اللَّهَ رَبِّي وَرَبُّكُمْ فَاعْبُدُوهُ هَذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ ﴿٥١﴾

*Hakika Mwenyezi Mungu ni Mola wangu na ni Mola wenu. Basi mwabuduni. Hii ndiyo njia iliyonyooka (3:51)*

Ujumbe huu wa Nabii Isa, unapatikana pia katika Biblia. Nabii Isa amenukuliwa katika Bibilia akifundisha Wana wa Israili kuwa yeye si Mungu, ila ni Mtume, na kwamba Mwenyezi Mungu ni mmoja, wapekee na ndiye Mungu wa kweli.

*Na uzima wa milele ndiyo huu, wakujue wewe Mungu wa pekee wa kweli na Yesu Kristo uliyemtuma. (Yohana 17:3)*

Maneno haya ya Nabii Isa(a.s) yanatuonesha ukweli kuwa yeye si mungu, na wale wanaong'ang'ania kumwita, Yesu ni mungu, hawayafuati mafundisho yake, bali wanafuata uzushi wa mafundisho na maagizo ya wanadamu. Hili analithibitisha Yesu katika Biblia:

*Enyi wanafiki, ni vyema alivyotabiri Isaya kwa habari zenu, akisema, Watu hawa wananiheshimu kwa midomo; ila mioyo yao iko mbali nami. Nao wananiabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu. (Mathayo 15:7-9)*

## **(ii) Hakuna dhambi ya asili**

Yesu amefundisha kuwa kila mwanadamu huzaliwa akiwa huru pasina tone lolote la dhambi, na kwamba watoto ndio wakuu katika Ufalme wa mbinguni na Ufalme wa mbinguni ni wao. Na hakuna yeyote atakayeingia katika Ufalme wa mbinguni (peponi) ila atakayejitahidi kutotenda maovu, na kujitahidi kufanya mema akawa safi kama mtoto.

*Saa ile wanafunzi wake wakamwendea Yesu wakisema, Ni nani basi aliye mkuu katika Ufalme wa mbinguni? Akaita mtoto mmoja, akamweka katikati yao, akasema, Amini, nawaambia, Msipoongoka na kuwa kama vitoto, hamtaingia kamwe katika Ufalme wa mbinguni. Basi yeyote ajinyenyekeshaye mwenyewe kama mtoto huyu, huyo ndiye aliye mkuu katika Ufalme wa mbinguni (Mathayo 18:1-4)*

Na katika maandiko mengine ya Biblia, tunasoma:

*Yesu akasema: Waacheni watoto wadogo waje kwangu; wala msiwazuie; kwa maana walio mfano wa hao, Ufalme wa mbinguni ni wao (Mathayo 19:14)*

Kutokana na mafundisho haya ya Yesu, hakuna mtu yeyote muovu atakayeingia katika Ufalme wa mbinguni (Peponi), kwa kuamini kwamba Yesu kafa msalabani kwa ajili ya dhambi zake.

## **(iii) Waumini wanatakiwa kufuata sheria za Mwenyezi Mungu kwa kuweka Ufalme wake hapa duniani**

Nabii Isa (a.s) aliwafundisha watu wamuabudu Mwenyezi Mungu peke yake katika kila kipengele cha maisha yao. Na

kwamba njia ya maisha yenye kuleta amani ya kweli na maisha ya furaha ni kufuata sheria za Mwenyezi Mungu na kuacha mafundisho ambayo ni maagizo ya wanadamu. Katika Qur'an tunafahamishwa kuwa aliwaambia Waisraili.

إِنَّ اللَّهَ رَبِّي وَرَبُّكُمْ فَأَعْبُدُوا اللَّهَ هَذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ ﴿٥١﴾

*Hakika Mwenyezi Mungu ni Mola wangu na ni Mola wenu. Basi mwabuduni. Hii ndiyo njia iliyonyooka. (3:51)*

Na katika Biblia, amenukuliwa akiwataka watu wamuombe Mwenyezi Mungu awezeshe Ufalme wake ustawi duniani kama ulivyo stawi mbinguni ili dunia isitawaliwe na kuongozwa kwa sheria zistawishazo ufuska na ufisadi katika jamii.

*Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni; Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, hapa duniani kama mbinguni (Mathayo 6:9-10)*

### Miujiza Aliyonyesha Nabii Isa(a.s)

Mwenyezi Mungu pekee ndiye aliyewawezesha Mitume na Manabii kufanya miujiza. Allah(s.w) aliwapa mitume miujiza ili kuwa dalili ya kuwathibitishia watu kuwa yeye ndiye aliyewatuma. Hakuna Mtume au Nabii aliyedai kufanya miujiza kwa uwezo wake mwenyewe. Na hivi ndivyo Nabii Isa alivyowaambia wana wa Israili.

.....أَيُّ قَدْ جِئْتُمْ بِآيَةٍ مِّن رَّبِّكُمْ أَيُّ أَخْلُقُ

لَكُمْ مِنَ الطَّيْرِ كَهَيْئَةِ الطَّيْرِ فَأَنْفُخُ فِيهِ فَيَكُونُ طَيْرًا بِإِذْنِ اللَّهِ وَأُبْرِئُ

الْأَكْمَهَ وَالْأَبْرَصَ وَأُحْيِي الْمَوْتَى بِإِذْنِ اللَّهِ وَأُنذِرُكُمْ بِمَا تَأْكُلُونَ

وَمَا تَدْخِرُونَ فِي بُيُوتِكُمْ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لَّكُمْ إِن كُنْتُمْ مُّؤْمِنِينَ ﴿٤٤﴾

*.....Nimekujieni na hoja kutoka kwa Mola wenu, ya kwamba nakuumbieni, katika udongo, kama sura ya ndege, kisha*

*nampuliza, mara anakuwa ndege kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na ninawaponesha vipofu na wenye mabalanga, na ninawafufua waliokufa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu na nitakuambieni mtakavyo vila na mtakavyo weka akiba katika nyumba zenu. Bila shaka katika haya imo hoja (ya kuonesha kuwepo Mwenyezi Mungu) kwenu ikiwa ni watu wa kuamini(3:49)*

Ni dhahiri kuwa miujiza yote aliyoifanya Nabii Isa(a.s), aliifanya kwa lengo la kuwathibitishia watu kuwa yeye ametumwa na Mwenyezi Mungu. Katika Biblia, Yesu alibainisha hili wazi kabla hajafanya muujiza wa kumfufua Lazaro:

*Yesu akainua macho yake juu, akasema: Baba nakushukuru kwa kuwa umenisikia. Nami nalijua ya kuwa wewe wanisikia siku zote; lakini ni kwa ajili ya mkutano huu wanaohudhuria nalisema haya, ili wapate kusadiki kuwa ndiwe uliyenituma. Naye akiisha kusema hayo, akalia kwa sauti kuu, Lazaro, njoo huku nje. Akatoka nje yule aliyekufa, amefungwa sanda miguuni na mikononi, na uso wake umefungwa lesa. Naye Yesu akawaambia, Mfungueni, mkamwache aende zake (Yohana 11:41-44)*

Kwa kuzingatia maandiko haya, utabaini kuwa hawasemi kweli wale wanaodai kuwa Yesu ni Mungu eti kwasababu alifanya miujiza ya kufufua wafu.

## **Wito wa Nabii Isa(a.s) kwa Wanafunzi Wake**

Nabii Isa(a.s) alipoona ukaidi wao umeshitadi, akatoa wito maalum kwa wanafunzi wake ili wajitokeze wale watakaokuwa tayari kuwa naye bega kwa bega kupambana na madhalimu na kuufikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu kwa wengine. Hivyo, akawauliza:

﴿ فَلَمَّا أَحَسَّ عَيْسَىٰ مِنْهُمُ الْكُفْرَ قَالَ مَنْ أَنْصَارِي إِلَى اللَّهِ قَالَ  
 الْحَوَارِيُّونَ نَحْنُ أَنْصَارُ اللَّهِ ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَأَشْهَدُ بِأَنَّكَ مُسْلِمُونَ ﴿٥٢﴾ رَبَّنَا  
 ءَامِنَّا بِمَا أَنْزَلْتَ وَاتَّبَعْنَا الرَّسُولَ فَاكْتُبْنَا مَعَ الشَّاهِدِينَ ﴿٥٣﴾

*Lakini Isa alipoona ukaidi wao, alisema: Nani watakuwa wasaidizi wangu katika kumtangaza Mwenyezi Mungu (mmoja)? Wanafunzi wakasema: “Sisi ni wasaidizi wa Mwenyezi Mungu. Tumemwamini Mwenyezi Mungu na ushuhudie kwamba sisi tumejisalimisha. Mola wetu! Tumeyaamini uliyoyateremsha na tumemfuata Mtume, basi tuandike pamoja na washuhudiao (3:52-53)*

Baada ya hapo, wanafunzi wa Nabii Isa (a.s) wakamtaka awaombe chakula maalumu kutoka kwa Allah(s.w), wakasema:

﴿ إِذْ قَالَ الْحَوَارِيُّونَ يَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ هَلْ يَسْتَطِيعُ رَبُّكَ أَنْ يُنَزِّلَ عَلَيْنَا مَائِدَةً مِنَ السَّمَاءِ قَالَ أَتَقْنَأُوا اللَّهَ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١١٢﴾

*Ewe Isa Mwana wa Maryam! Je Mola wako anaweza kututeremshia chakula kutoka mbinguni? Akasema(Nabii Isa), “Mcheni Mwenyezi Mungu kama kweli ninyi ni wenye kuamini kweli(5:112)*

﴿ قَالُوا نُرِيدُ أَنْ نَأْكُلَ مِنْهَا وَتَطْمَئِنَّ قُلُوبُنَا وَنَعْلَمَ أَنْ قَدْ صَدَقْتُنَا وَتَكُونَ  
 عَلَيْهَا مِنَ الشَّاهِدِينَ ﴿١١٣﴾

*Wakasema: “Tunataka kula katika hicho, na ili nyoyo zetu zitulie na tuwe miongoni mwa wanaoshuhudia(muujiza huo)(5:113)*

﴿ قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ اللَّهُمَّ رَبَّنَا أَنْزِلْ عَلَيْنَا مَائِدَةً مِنَ السَّمَاءِ تَكُونُ لَنَا  
 عِيدًا لِأَوْلَادِنَا وَعَآخِرِنَا وَعَآيَةً مِنْكَ وَأَرْزُقْنَا وَأَنْتَ خَيْرُ الرَّازِقِينَ ﴿١١٤﴾

*Akasema Isa bin Maryamu: “Ewe Mwenyezi Mungu, Mola wetu! Tuteremshie chakula kutoka mbinguni ili kiwe Sikukuu kwa ajili*

ya wa mwanzo wetu, na wa mwisho wetu, na kiwe Ishara itokayo kwako, basi turuzuku, kwani wewe ndiye mmbora wa wanaoruzuku(5:114)

قَالَ اللَّهُ إِنِّي مُنَزِّلُهَا عَلَيْكُمْ فَمَنْ يَكْفُرْ بَعْدَ مِنْكُمْ فَإِنِّي أُعَذِّبُهُ عَذَابًا لَا

أُعَذِّبُهُ أَحَدًا مِّنَ الْعَالَمِينَ ﴿١١٥﴾

Mwenyezi Mungu akasema: “Bila shaka Mimi nitakiteremsha juu yenu, lakini miongoni mwenu atakayekataa baada ya haya, basi Mimi nitamuadhibu adhabu ambayo sijamwadhibu yoyote katika walimwengu(5:115)

## Njama za Mayahudi Kutaka Kumuuu Nabii Isa(a.s)

Njama za kutaka kumuua Nabii Isa(a.s) zilianza kwa kumuuliza maswali ya kumtega na kumfitinisha kwa Serikali ili imuone kuwa anachochea watu wasilipe kodi na kuhatarisha maslahi ya wakubwa Serikalini. Fitina hizi zilifanywa na Mafarisayo na Makuhani, wakamwendea Yesu wakisema:

*Mwalimu, twajua ya kuwa wewe u mtu wa kweli, na njia ya Mungu waifundisha katika kweli, wala hujali cheo cha mtu awaye yeyote, kwa maana hutazami sura za watu. basi utuambie waonaje? Ni halali kumpa kaisari kodi, ama sivyo? (Mathayo 22:16-17)*

Lakini Yesu akaufahamu uovu wao, akasema:

*Mbona mnanijaribu enyi wanafiki? Nionyesheni fedha ya kodi. Nao wakamletea dinari. Akawaambia, Ni ya nani sanamu hii, na anwani hii? Wakamwambia, Ni ya Kaisari. Akawaambia, Basi mlipeni Kaisari yaliyo ya Kaisari, na Mungu yaliyo ya Mungu (Mathayo 22:18-21)*

Baada ya hila hizi kushindwa, zikapangwa njama za kutaka kumuua.

*Basi wakuu wa Makuhani na Mafarisayo wakakusanya baraza, wakasema, Tunafanya nini? Maana mtu huyu anafanya ishara nyingi. Tunamwachia hivi, watu wamwamini. Yafaa mtu mmoja afe kwa ajili ya watu, wala lisiangamie Taifa zima(Mathayo 11:47-48,50)*

## **Ahadi ya Allah(s.w) Kumuokoa Nabii Isa(a.s)**

Nabii Isa(a.s) alimuomba Allah(s.w) amlinde na shari za watu wabaya waliopanga njama dhidi yake. Yesu alikwenda bustani ya Gestmane kuomba. Alipofika, akawaambia wanafunzi wake:

*Roho yangu ina huzuni kiasi cha kufa; kaeni hapa, mkesho pamoja nami. Akaendelea mbele kidogo, akaanguka kifudifudi akaomba, akisema, Baba yangu, ikiwezekana kikombe hiki kiniepuka; walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe.(Mathayo 26:38 39)*

Mwenyezi Mungu alikubali dua ya Nabii Isa (a.s) kwa kumuhakikishia kuwa atamlinda dhidi ya njama za watu madhalimu.

إِذْ قَالَ اللَّهُ يَعْيسَى ابْنُ مَرْيَمَ مَا مَنَنَّا بِكَ وَإِنَّا نَكُونُ مِنَّا  
كَفَرُوا وَجَاعِلُ الَّذِينَ اتَّبَعُوكَ فَوْقَ الَّذِينَ كَفَرُوا إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ ثُمَّ إِلَى  
مَرْجِعِكُمْ فَأَحْكُمُ بَيْنَكُمْ فِيمَا كُنْتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ ﴿٥٥﴾

“Mwenyezi Mungu aliposema: “Ewe Isa! Mimi nitakukamilishia muda wako wa kuishi na nitakuleta kwangu, na nitakutakasa na wale waliokufuru, na nitawaweka wale waliokufuata, juu ya wale waliokufuru mpaka siku ya kiyama. Kisha marejeo yenu yatakuwa kwangu, Nitaku hukumunika tika yale mliyokuwa mkihitilafiana”(3:55)



Katika mahubiri yake huko nyuma, Nabii Isa (a.s) aliwasisitiza sana watu kumtegemea Mwenyezi Mungu kwa kumuomba msaada. Aliwaambia:

*Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa; kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona, naye abishaye hufunguliwa. Au kuna mtu yupi kwenu, ambaye, mwanawe akimwomba mkate, atampa jiwe? Au akiomba samaki, atampa nyoka? Basi ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, Je! si zaidi Baba yenu aliye mbinguni atawapa mema wao wamwombao?*  
(Mathayo 7:7-11)

Kwa mujibu wa Yesu mwenyewe, Mwenyezi Mungu humsikiliza maombi yake na kumkubalia daima. Hebu na tuyarejee maneno yake aliyoyasema pale alipoomba jambo kubwa la kumfufua Lazaro:

*Yesu akainua macho yake juu, akasema: Baba nakushukuru kwa kuwa umenisikia. Nami nalijua ya kuwa wewe wanisikia siku zote; lakini ni kwa ajili ya mkutano huu wanaohudhuria nalisema haya, ili wapate kusadiki kuwa ndiwe uliyenituma. Naye akiisha kusema hayo, akalia kwa sauti kuu, Lazaro, njoo huku nje. Akatoka nje yule aliyekufa, amefungwa sanda miguuni na mikononi, na uso wake umefungwa lesa. Naye Yesu akawaambia, Mfungueni, mkamwache aende zake.*  
(Yohana 11:41-44)

Ndiyo kusema kuwa ikiwa Yesu ametangaza kuwa, "Ombeni, nanyi mtapewa", Na kwakuwa Mungu, huwapa "mema wao wamwombao", na Yesu mwenyewe anakiri kuwa Mungu anamsikia siku zote, haiwezekani kabisa asulubiwe hali ya kuwa Mungu yupo na alishamuomba!

## Si Yesu Aliyesulubiwa

Katika Qur'an tukufu, Mwenyezi Mungu aliye muweza na mjuzi wa mambo anathibitisha kuwa aliyesulubiwa si Nabii Isa(a.s):

وَقَوْلِهِمْ إِنَّا قَتَلْنَا الْمَسِيحَ عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ رَسُولَ اللَّهِ وَمَا قَتَلُوهُ وَمَا صَلَبُوهُ وَلَكِنْ شُبِّهَ لَهُمْ وَإِنَّ الَّذِينَ اخْتَلَفُوا فِيهِ لَفِي شَكٍّ مِّنْهُ مَا لَهُمْ بِهِ مِنْ عِلْمٍ إِلَّا اتِّبَاعَ الظَّنِّ وَمَا قَتَلُوهُ يَقِينًا ﴿١٥٧﴾

*Na kwa kusema kwao: “Sisi tumemuua Masihi Isa, mwana wa Maryam Mtume wa Mungu”, hawakumuua wala hawakumsulubu ila walibabaishiwa (mtu mwingine aliyefananishwa na Nabii Isa). Na hakika wale waliokhitilafiana katika hayo wamo katika shaka nalo. Wao hawana yakini juu ya hili, isipokuwa wanafuata dhana tu. Na kwa yakini hawakumuua(4:157).*

بَل رَفَعَهُ اللَّهُ إِلَيْهِ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿١٥٨﴾

*Bali Mwenyezi Mungu alimnyanyua kwake, Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima (4:158)*

## Kuokolewa Nabii Isa(a.s)

Hukumu ilipitishwa Nabii Issa auawe kwa kusulubiwa. Lakini Allah(s.w)alimnusuru na badala yake akasulubiwa Yuda msaliti aliyefananishwa naye kwa sura na sauti. Kwa hiyo aliyesulubiwa si Yesu bali ni Yuda aliyemsaliti Yesu kama inavyotueleza kwa uwazi Injili ya barnabas katika sura ya 214, 215, 216 na 217.

*“Yesu akatoka nje ya nyumba, akaenda bustanini kusali, kama ilivyokuwa ada yake kusali, kwa kurukuu mara mia na kusujudu kwa paji lake la uso. Yuda, ambaye alipajua mahali alipokuwa Yesu na wanafunzi wake, akaenda kwa kuhani mkuu, na akanena: “Ukinipa kilichoahidiwa, nitakupa mkononi mwako Yesu mnayemtafuta: Kwani yu pekee na wanafunzi kumi na*

*moja'. Kuhani mkuu akajibu: "Wataka kiasi gani?" Akasema Yuda, "Vipande thalathini vya dhahabu."*

*Kisha papo hapo kuhani mkuu akamuhesabia pesa hizo, na akamtuma Mfarisayo kwa gavana kuchukua askari na kwa Herodi, na Wakatoa kikosi chao, kwani waliwahofia watu; wakachukua silaha zao na huku wakiwa na kurunzi na taa ya bakora zao, wakatoka nje ya Yerusalemu.*

*Askari waliokuwa pamoja na Yuda walipokaribia mahali alipokuwa Yesu, Yesu alisikia kishindo cha watu wengi wakija, naye kwa hofu akaingia ndani ya nyumba. Na wale wanafunzi kumi na moja walikuwa wamelala.*

*Kisha Mwenyezi Mungu kwa kuiona hatari iliyomkabili mja wake, akamwamuru Jibrili, Mikaili, Rafaili na Urieli, watumishi wake wamuondoshe Yesu ulimwenguni.*

*Malaika watakatifu wakaja na wakamtoa Yesu nje kupitia katika dirisha la upande wa Kusini. Wakambeba na kumweka katika mbingu ya tatu akiwa katika kundi la Malaika wanaomsabihi Mwenyezi Mungu daima.*

*Yuda akatangulia kuingia kwa ufidhuli, kabla ya wote katika kile chumba ambacho Yesu alikuwamo. Wanafunzi walikuwa wamelala. Hapo Mwenyezi Mungu Mwingi wa miujiza akafanya miujiza, kwani akambadilisha Yuda kwa sauti na sura akawa kama Yesu hadi tukaamini kuwa alikuwa ni Yesu. Naye baada ya kutuamsha akatuuliza Bwana Yesu aliko. Ndipo tukastaajabu na kumjibu: 'Wewe, bwana ndiye bwana wetu; je, sasa umetusahau?'*

Hisia za wanafunzi wa Yesu kama zilivyoielezwa katika Injili ya Barnabas zinafanana na zilizoielezwa katika Injili nyingine. Injili ya Barnabas yasema kama ifuatavyo na hatua za mwisho za kusulubiwa kwa Yuda Iskariot badala ya Yesu:

*“Makuhani Wakuu pamoja na waandishi wa Wafarisayo, walipoona kuwa Yuda hakufa kwa mateso waliyomfanyia na kwa kuhofia kuwa Pilato aweza kumwacha kutundikwa Msalabani. Hivyo wakamhukumu Yuda pamoja na maharamia wawili wafe pamoja naye kifo cha msalabani. Hivyo wakampeleka kwenye Mlima wa Kalvari ambako walikuwa wakinyongwa watu waovu. Wakamsulubisha uchi, ili kumdhalilisha zaidi. Yuda hakufanya chochote isipokuwa kulalamika, “Mwenyezi Mungu kwanini umenitupa, mwovu ametoroka nami nafa, waandishi wa wafarisayo wamchukue Yuda kama mhalifu anayestahili kifo cha msalabani pasi na haki?”*

*Amini nasema kwamba sauti sura na umbo la Yuda vilifanana mno na Yesu kiasi ambacho wanafunzi wake na waumini wengine waliamini kuwa ni Yesu. Hivyo baadhi yao wakayawacha mafundisho ya Yesu kwa kuamini kuwa Yesu alikuwa yu Nabii wa uwongo, na kwamba alifanya miujiza kwa hila za uchawi kwani Yesu aliesema kuwa hatakufa hadi karibu na mwisho wa ulimwengu. Lakini wale waliosimama imara katika mafundisho ya Yesu walisononeshwa sana nyoyo zao kumwona yule aliyefanana kabisa na Yesu (katika hali ile) na wakasahau aliyosema Yesu. Mungu atamfisha karibu na mwisho wa ulimwengu. Ukiwaondoa wafuasi ishirini na watano waliokimbilia Damascus, wengine wote kati ya wale wafuasi 72 walimwona na walikula pamoja na Yesu. Hata hivyo Yesu aliitumia fursa hiyo pia kuwakemea wale ambao waliamini kuwa yeye alikuwa amekufa na kufufuka. “Na aliwakemea wengi ambao waliamini kuwa yeye alikuwa amekufa na kufufuka kwa kusema: ‘Je, mnadhani kuwa mimi na Mwenyezi Mungu tu waongo? Kwani Mwenyezi Mungu amenijaalia mimi kuishi hadi karibu na mwisho wa ulimwengu, kama niliyokwisha kuwaambia. Amin, Amin nawaambia, sikufa bali (alikuwa) Yuda, Msaliti. Jihadharini, kwani shetani atafanya kila jitihada kukudanganyeni. Basi kuweni mashahidi wangu kwa Israeli yote na kwa ulimwengu wote kwa yote mliyoyasikia na*

kuyaona.” Baada ya kusema hayo alimwomba Mwenyezi Mungu awajaalie waumini uokovu, na awajaalie waasi toba. Na alipomaliza dua yake akamkumbatia mama yake, na kusema: ‘Amani iwe juu yako, wewe mama yangu, tulizana kwa Mwenyezi Mungu aliyekuumba wewe na mimi! Baada ya kusema hivyo aliwageukia wanafunzi wake na kusema: ‘Rehema za Mwenyezi Mungu na amani ziwe juu yenu! “Nao wakashuhudia kwa macho yao Malaika wane wakimchukua Yesu hadi mbinguni.” (Injili ya Barnabas, sura ya 221)

Maelezo haya ya Barnabas, aliyekuwa miongoni mwa wale wanafunzi kumi na moja waliokuwa pamoja na Yesu yanathibitishwa na Qur-an pale Allah(s.w) anapotufahamisha:

وَقَوْلِهِمْ إِنَّا قَتَلْنَا الْمَسِيحَ عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ رَسُولَ اللَّهِ وَمَا قَتَلُوهُ وَمَا صَلَبُوهُ وَلَكِنْ شُبِّهَ لَهُمْ وَإِنَّ الَّذِينَ اخْتَلَفُوا فِيهِ لَفِي شَكٍّ مِنْهُ مَا لَهُمْ بِهِ مِنْ عِلْمٍ إِلَّا اتِّبَاعَ الظَّنِّ وَمَا قَتَلُوهُ يَقِينًا ﴿١٥٧﴾ بَلْ رَفَعَهُ اللَّهُ إِلَيْهِ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿١٥٨﴾

Na kwa kusema kwao: “Sisi tumemuua Masihi Isa, mwana wa Maryamu Mtume wa Mungu”, hawakumuua wala hawakumsulubu ila walibabaishiwa (mtu mwingine waliyemdhani Nabii Isa). Na hakika wale waliokhitilafiana katika hayo wamo katika shaka nalo. Wao hawana yakini juu ya hili, isipokuwa wanafuata dhana tu. Na kwa yakini hawakumuua Bali Mwenyezi Mungu alimnyanyua kwake; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na mwenye hekima.” (4:157-158)

Hapa pana fundisho kubwa kwa kila mwenye kupigania na kusimamisha haki. Mateso na magumu yanayompata mtu katika kazi hii isiwe ni sababu ya kukata tamaa. Bali imzidishie imani na kumtegemea zaidi Allah(s.w). Na hatima ya mambo yote ni ushindi kwa waliosimama katika haki.

## Kupotoshwa Mafundisho ya Nabii Isa(a.s)

Pamoja na Isa(a.s) kufundisha tawhiid kwa kauli na vitendo; baada ya kuondoka kwake, mafundisho yake yalipotoshwa. Sura ya 222 ambayo ni ya mwisho katika Injili ya Barnabas inaeleza kama ifuatavyo juu ya kilichotokea baada ya Yesu kuondoka:

*“Baada ya kuondoka kwa Yesu, wanafunzi wakatawanyika katika sehemu mbali mbali za Israeli na za ulimwengu. Na haki inayochukiwa na shetani, ilibughudhiwa, kama ambavyo daima inabughudhiwa na batili. Watu kadhaa waovu kwa kusingizia kuwa walikuwa wanafunzi (wa Yesu), wakahubiri kuwa Yesu alikufa na kufufuka. Na wengine wakahubiri, kwamba Yesu ni mwana wa Mungu, miogoni mwao Paulo. Lakina sisi kama nilivyoandika, tunaohubiri kwa wale wamchao Mwenyezi Mungu, tunahubiri ili waokoke siku ya mwisho na Hukumu ya Mwenyezi Mungu, Amin.”*

Mafundisho ya Nabii Isa(a.s) yalipotoshwa katika maeneo yafuatayo:

### (i) Imani ya Utatu

Imani ya Mungu mmoja aliyofundisha Nabii Isa (a.s) iligeuzwa na kufanywa imani ya Utatu. Mungu mmoja akagawanywa katika sehemu tatu; **Mungu Baba, Mungu Mwana na Roho Mtakatifu**. Hata mafundisho ya Biblia yenyewe yapo kinyume na imani hii. Rejea vifungu vifuatavyo:

*“Yesu akamwambia, kwa nini kuniita mwema? Hakuna aliyemwema ila mmoja ndiye Mungu.” (Marko 10:18)*

*“Yesu akamwambia, Usinishike; kwa maana sijapaa kwenda kwa baba. Lakini nenda kwa ndugu zangu ukawaambie. Ninapaa kwenda kwa Baba yangu naye ni Baba yenu, Mungu wangu naye ni Mungu wenu.” (Yohana 20:17)*

“Kwa Sababu mimi sikunena kwa nafsi yangu tu; bali baba aliyenipeleka, yeye mwenyewe ameniagiza nitakayonena nitakayosema.” (Yohana 10:49)

“Mungu akanena maneno haya yote akasema: Mimi Bwana Mungu wako niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa. Usiwe na miungu mingine ila mimi (Kutoka 20:1-3)

‘Sikiliza Ee Israeli, BWANA, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja.’  
(Kumbukumbu la Taurat) (6:4)

Ama katika Qur-an imani hiyo inakanushwa kabisa na aya zifuatazo:

لَقَدْ كَفَرَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ ثَلَاثَةٌ وَوَمَا مِنَ إِلَهِ إِلَّا إِلَهٌ وَاحِدٌ وَإِن لَّمْ يَنْتَهُوا عَمَّا يَقُولُونَ لَيَمَسَّنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٧٢﴾

Kwa hakika wamekufuru wale waliosema: “Mwenyezi Mungu ni mmoja katika (wale waungu) watatu; (yeye ndiye wa tatu wao).” Na kama hawataacha hayo wayasemayo, kwa yakini itawakamata – wale wanaoendelea na ukafiri miongoni mwao – adhabu iumizayo.(5:73)

## (ii) Imani ya Uungu wa Yesu

Kuhusu imani juu ya Uungu wa Isa(a.s) na mama yake Qur’an inasema:

لَقَدْ كَفَرَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ هُوَ الْمَسِيحُ ابْنُ مَرْيَمَ قُلْ فَمَنْ يَمْلِكُ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا إِنْ أَرَادَ أَنْ يُهْلِكَ الْمَسِيحَ ابْنَ مَرْيَمَ وَأُمَّهُ وَوَمَنْ فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا وَلِلَّهِ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا يَخْلُقُ مَا يَشَاءُ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٧﴾

Kwa yakini wamekwisha kufuru wale waliosema: “Mwenyezi Mungu ni Masihi bin Maryamu.” Sema: “Ni nani atakayemiliki (kuzuilia) chochote mbele ya Mwenyezi Mungu kama yeye angetaka kumwagamiza Masihi mtoto wa Maryam, na mama yake na vyote vilivyomo katika ardhi na Ufalme wa mbinguni na ardhi na vilivyomo kati yake ni vya Mwenyezi Mungu (tu peke yake). Muumba apendavyo, na Mwenyezi Mungu ni muweza juu ya kila kitu. (5:17).

مَا الْمَسِيحُ ابْنُ مَرْيَمَ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ وَأُمُّهُ صِدِّيقَةٌ

كَانَا يَا كَلَانَ الطَّعَامَ أَنْظُرُ كَيْفَ نَبِيْنُ لَهُمُ الْآيَاتِ ثُمَّ أَنْظُرُ أَنِّي يُؤْفَكُونَ ﴿٧٥﴾

Masihi bin Maryamu si chochote ila ni Mtume . (Na) bila shaka Mitume wengi wamepita kabla yake. Na mamake ni mwanamke mkweli, (na) wote wawili walikuwa wakila chakula Tazama jinsi tunavyowabainishia Aya, kisha tazama jinsi wanavyogeuzwa (kuacha haki). (5:75)

### (iii) Imani ya Uwana wa Mungu wa Nabii Isa(a.s)

Kuhusu itikadi ya Wakristo ya Yesu kuwa mwana wa Mungu, Qur’an inatufahamisha:

وَقَالَتِ الْيَهُودُ عُزَيْرٌ ابْنُ اللَّهِ وَقَالَتِ النَّصْرَى الْمَسِيحُ ابْنُ اللَّهِ ذَلِكَ

قَوْلُهُمْ بِأَفْوَاهِهِمْ يُضَاهِئُونَ قَوْلَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَبْلُ قَتَلْتَهُمُ اللَّهُ أَنَّى

يُؤْفَكُونَ ﴿٣٠﴾

Na Mayahudi wanasema: “Uzeri ni mwana wa Mwenyezi Mungu;” na Wakristo wanasema: “Masihi ni mwana wa Mwenyezi Mungu..” haya ndiyo wasemayo kwa vinywa vyao. Wanayaiga maneno ya wale walio kufuru kabla yao, Mwenyezi Mungu awaangamize. Wanageuzwa namna gani hawa! (9:30).

إِنْ هُوَ إِلَّا عَبْدٌ أَنْعَمْنَا عَلَيْهِ وَجَعَلْنَاهُ مَثَلًا لِبَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿٥٩﴾



*Hakuwa (Nabii Issa) ila ni mja tuliyemneemeshwa na tukamfanya mithali (nzuri) kwa wana wa Israili. (43:59).*

#### **(iv) Imani ya kusulubiwa Yesu Msalabani**

Imani ya kufa na kufufuka Nabii Isa(a.s) ni imani ya msingi katika dini ya Ukristo. Imani hii imesimama juu ya dhana zifuatazo:

- Dhambi ya asili.
- Haja ya kuwa na Mpatanishi.
- Kafara ya damu (kifo), kwa ajili ya dhambi.

Wakristo wanaamini kuwa baada ya Adam(a.s) kumkosea Mola wake; kizazi chake chote kilirithi dhambi. Kwa hiyo kila anayezaliwa anazaliwa na dhambi. Ili salama ipatikane kwa mwanaadamu ni lazima apatikane asiye na dhambi awe mpatanishi kati ya Mungu na mwanaadamu. Mtume Isa (Yesu) anadhaniwa ndiye asiye na dhambi na mpatanishi. Lakini ili dhambi za wanadamu zioshwe imekuwa lazima damu ya Yesu imwagike. Kwa hiyo kufa Yesu msalabani ilikuwa hitajio la lazima ili wanaadamu waokolewe na dhambi. Imani hii inasonga mbele na kudai kuwa Mkristo wa leo amepunguziwa kazi. Hana haja ya kufuata sheria. Lililo wajibu juu yake ni kuamini tu kuwa yesu ni Mtoto wa Mungu na alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zake.

Lakini kuhusu dhana ya dhambi ya asili Qur-an inatufunza kuwa Nabii Adam alitubu na Mola wake akapokea toba yake.



فَتَلَقَىٰ آدَمَ مِنْ رَبِّهِ كَلِمَاتٍ فَتَابَ عَلَيْهِ إِنَّهُ هُوَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ

*Kisha Adam akapokea maneno (ya maombi) kwa Mola wake, (akaomba), na Mola wake Akapokea toba yake; hakika Yeye ndiye Mwingi wa kupokea toba (kwa wenye kutubia) na mwingi wa kurehemu (2:37)*

Ama kuhusu mtu kutolewa kafara kwa ajili ya dhambi za mtu mwingine, Biblia ina haya ya kusema:

*“Lakini watoto wao hakuwaua, ila alifanya sawa sawa na alivyo amuru, akisema, mababa wasife kwa makosa ya wana, wala wana wasife kwa makosa ya mababa; lakini kila mtu atakufa kwa dhambi yake mwenyewe. (2 mambo ya nyakati 25:4)*

*Mababa wasiuawe kwa ajili ya watoto wao, wala watoto wasiuawe kwa ajili ya baba zao; kila mtu na auawe kwa ajili ya dhambi yake mwenyewe.” (Kumb, ... 4:16).*

*“Siku zile, hawatasema tena, Baba za watu wamekula zabibu kali, na meno ya watoto wao yametiwa ganzi, Bali kila mtu atakufa kwa Sababu ya uovu wake mwenye; kila mtu alaye zabibu kali meno yake yatakuwa ganzi.” (Yeremia: 31:29-30).*

## **Nabii Isa(a.s) Siku ya Kiyama**

Siku ya kiyama itakuwa nzito sana kwa wale waliokuwa wakiamini na kutangaza kuwa Nabii Isa(a.s) ni Mungu, na kumuabudia kinyume cha alivyofundisha. Allah(s.w) atamuuliza Nabii Isa(a.s)

وَإِذْ قَالَ اللَّهُ يٰعِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ ءَأَنْتَ قُلْتَ لِلنَّاسِ اتَّخِذُونِي وَأُمِّي  
إِلٰهَيْنِ مِن دُونِ اللَّهِ قُلْ سُبْحٰنَكَ مَا يَكُونُ لِيْٓ أَنۢ أَقُولَ مَا لَيْسَ لِيۢ بِحَقِّ  
١١١  
إِن كُنْتَ قُلْتُهُۥ فَقَدْ عَلِمْتَهُۥ تَعَلَّمْ مَا فِي نَفْسِيۡ وَلَا أَعْلَمُ مَا فِي نَفْسِكَ  
إِنَّكَ أَنْتَ عَلَّمُۥمُ الْغُيُوبِ

*Na(Kumbukeni)Mwenyezi Mungu atakaposema: “Ewe Isa bin Maryam! Je wewe uliwaambia watu ‘Nifanyeni mimi na mama yangu miungu badala ya Mwenyezi Mungu?’. Aseme: “Wewe umetakasika na kuwa na mshirika. Hainistahiki mimi kusema ambayo si haki yangu. Kama ningelisema bila shaka ungelijua; unayajua yaliyomo nafsini mwangu, lakini mimi siyajui yaliyo nafsini mwako; hakika wewe ndiwe ujuaye mambo ya ghaibu. (5:116)*

مَا قُلْتُ لَهُمْ إِلَّا مَا أَمَرْتَنِي بِهِ أَن آعْبُدُوا اللَّهَ رَبِّي وَرَبَّكُمْ وَكُنْتُمْ عَلَيْهِمْ شَهِيدًا مَا دُمْتُمْ فِيهِمْ فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِي كُنْتَ أَنْتَ الرَّقِيبَ عَلَيْهِمْ وَأَنْتَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ﴿١١٧﴾ إِنْ تُعَذِّبْهُمْ فَإِنَّهُمْ عِبَادُكَ وَإِن تَغْفِرْ لَهُمْ فَإِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١١٨﴾

*Sikuwaambia lolote ila yale uliyoniamrisha; ya kwamba 'Mwabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu na Mola wenu'. Na nilikuwa shahidi juu yao nilipokuwa nao; na uliponikamilishia muda wangu, Wewe ukawa mchungaji juu yao, na Wewe shahidi juu ya kila kitu. Ikiwa utawaadhibu, basi bila shaka hao ni waja wako; na ukiwasamehe basi kwa hakika wewe ndiwe mwenye nguvu na Mwenye hikima.(5:117-118)*

قَالَ اللَّهُ هَذَا يَوْمُ يَنْفَعُ الصَّادِقِينَ صِدْقُهُمْ لَهُمْ جَنَّاتٌ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ ذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١١٩﴾

*Mwenyezi Mungu atasema: "Hii ndiyo siku ambayo wakweli utawafaa ukweli wao". Wao watapata Bustani zipitazo mito mbele yake. humo watakaa milele. Mwenyezi Mungu amewawia radhi; nao wawe radhi naye. Huko ndiko kufaulu kukubwa(5:119)*

## **Mafunzo Yatokanayo na Historia ya Nabii Isa(a.s)**

Kutokana na Historia ya Nabii Isa(a.s) tunajifunza yafuatayo:

- (i) Mtoto aliyezaliwa ndani ya ndoa ataitwa kwa ubini wa Baba yake na si vinginevyo na mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa ataitwa kwa ubini wa Mama yake.
- (ii) Waumini wanaharakati hawanabudi kumuomba Allah(s.w) awape watoto wema watakaofanya jitihada za makusudi za kuutawalisia Uislamu katika jamii.

- (iii) Tuwalee na kuwaelimisha watoto elimu ya mwongozo na mazingira (elimu juu ya fani mbali mbali) si kwa kutaraji maslahi ya dunia bali kwa ajili ya kusimamisha ukhalifa katika ardhi.
- (iv) Wanaharakati wanaposingiziwa au kupakaziwa maovu wasitengeneze majukwaa ya kujitetea na kujisafisha bali washitakie kwa Allah(s.w) na kumuomba awasafishe na kuwatakasa hapa hapa duniani.

- Allah(s.w) anawaasa waumini wasijali matusi na fitina za wanafiki na makafiri, bali waendeleo kutenda inavyostahiki.

وَقُلِ اعْمَلُوا فَسَيَرَى اللَّهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُ وَالْمُؤْمِنُونَ وَسَتُرَدُّونَ إِلَىٰ

عَلِيمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ فَيُنبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٠٥﴾

*Na sema (uwaambie): “Tendeni mambo (mazuri) Mwenyezi Mungu atayaona mambo yenu hayo na Mtume wake na Waislamu. Na mtarudishwa kwa Mjuzi wa siri na dhahiri; naye atakwambieni (yote) mliyokuwa mkiyatenda.” (9:105)*

- (v) Msingi wa mafundisho ya Uislamu ni Tawhiid. Yaani tunatakiwa tuufundishe Uislamu kwa mujibu wa Qur-an na Sunnah na kwa lengo la kumuabudu Allah(s.w) katika kila kipengele cha maisha ya binafsi na jamii na kusimamisha Ukhalifa katika jamii – Hii ndio njia sahihi ya kufundisha Uislamu.
- (vi) Ukitafakari vizuri utagundua kuwa maumbile yote ya Allah (s.w)yaliyotuzunguka pamoja na nafsi zetu ni miujiza. Hivyo kuletewa muujiza maalumu, haitakuwa ni sababu ya kumfanya mtu amuamini Allah(s.w) ipasavyo kama atashindwa kutafakari maumbile mbali mbali yaliyomzunguka.

- (vii) Kama mbinu ya kulingania Uislamu katika jamii hatunabudi kuunda kundi la harakati litakalokuwa tayari kufundisha Uislamu kwa usahihi wake, kuamrisha mema na kukataza maovu – Qur’an (3:104).
- (viii) Nyakati zote wapinzani wakuu wa kusimama kwa Uislamu katika jamii ni washika dau (Al-Malaau) wa Dola za kitwaaghuut.
- (ix) Tunapoamua kujiingiza kwenye harakati za kuhuisha na kusimamamisha Uislamu katika jamii hatunabudi kujiegemeza (kutawakali) kwa Allah(s.w) na kuomba msaada wake na kutegemea ulinzi wake.
- (x) Mwanaharakati muda wote anatakiwa awe tayari kukabili au kukabiliwa na misukosuko au kufa kwa ajili ya Allah(s.w),Mtume wake na kusimamisha Dini yake.

## **WATU WEMA WALIOTAJWA NDANI YA QUR’AN**

### **Utangulizi:**

Pamoja na Qur’an kutufahamisha Historia ya Mitume hao waliotajwa ndani yake ili tupate mafunzo hayo yaliyoainisha, pia inatufahamisha juu ya watu binafsi na makundi ya watu wema ili vile vile tujifunze kutoka kwao na iwe sababu ya kutuwezesha kusimamisha Uislamu katika jamii yetu. Watu na makundi ya watu wema yaliyoainishwa katika Qur’an ni:

1. Vijana wa Pangoni
2. Al-Khidhr
3. Dhulqarnairn
4. Luqman

## Vijana wa Pangoni

Makafiri wa Kiquraish walikuwa na tabia ya kumghasi Mtume(s.a.w) kwa kumuuliza maswali mara kwa mara. Lengo lao likiwa kumshusha hadhi Mtume(s.a.w) endapo atashindwa kujibu maswali hayo. Mchezo huu walikuwa wakiufanya kwa kushirikiana na Mayahudi. Walikuwa wakijifunza kutoka kwa Mayahudi baadhi ya mambo ya kale kisha hurejea kumuuliza Mtume(s.a.w) maswali. Miongoni mwa maswali waliyomuuliza Mtume(s.a.w) ni juu ya **vijana wa Pangoni** na habari za **Dhulqarnain**.

Vitabu vingi vya historia vinabainisha kuwa kisa cha vijana wa pangoni kilitokea katika mji wa Ephesus uliokuwa ndani ya Ufalme wa Urumi. Mji huu ulijulikana sana kutokana na kushamiri sana dini ya ushirikina. Watu wa huo mji waliabudia masanamu, mwezi, juu na sayari.

Baada ya Nabii Isa(a.s) kuja na mafundisho yake ya kumpwekesha Allah(s.w) yalienea hadi Ephesus. Wakatokea vijana wakayaamini na kuachana na ibada za kishirikina. Hili mfalme akaliona ni hatari kwa maslahi yake. Akawaita vijana hao ili kuwatisha warejee kwenye ukafiri na ushirikina. Lakini vijana hawakukubali kuiacha haki. Baada ya kuonyesha umadhubuti wao Mwenyezi Mungu aliwazidishia imani na kuzitia nguvu nyoyo zao. Qur'an inatuambia:

.....إِنَّهُمْ فِتْيَةٌ آمَنُوا بِرَبِّهِمْ وَزِدْنَهُمْ هُدًى ﴿١٣﴾

“.....*Hakika wao walikuwa ni vijana waliomuamini Mola wao. Basi tukawazidishia uongofu*” (18:13).

وَرَبَطْنَا عَلَى قُلُوبِهِمْ إِذْ قَامُوا فَقَالُوا رَبُّنَا رَبُّ  
السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ لَنْ نَدْعُوَ مِنْ دُونِهِ إِلهًا لَقَدْ قُلْنَا

إِذَا شَطَطًا ﴿١٤﴾

*Na tukazitia nguvu nyoyo zao waliposimama (mbele ya mfalme wao kafiri) wakasema: “Mola wetu ni Mola wa mbingu na ardhi. Hatutamuabudu kabisa Mungu mwingine badala yake. (Hapo) bila shaka tutakuwa tumesema uovu uliopindukia kiasi” (18:14).*

Kwa msimamo wao huo mfalme alitaka kuwadhuru, basi vijana wakakimbilia pangoni. Humo walikaa miaka mia tatu (kwa hesabu ya miaka ya jua) au miaka 309 kwa hesabu ya mwendo wa mwezi.

إِذْ أَوْىُّ الْفِتْيَةَ إِلَى الْكَهْفِ فَقَالُوا رَبَّنَا آتِنَا مِن لَّدُنكَ رَحْمَةً وَهَيِّئْ لَنَا  
 مِنْ أَمْرِنَا رَشَدًا ﴿١٧﴾ فَضَرَبْنَا عَلَيْهِمْ فِي الْكَهْفِ سِنِينَ عَدَدًا ﴿١٨﴾

*Vijana hao walipokimbilia katika pango na wakasema: “Mola wetu; tupe rehema zinazotoka kwako na tutengenezee uwongofu katika (kila) jambo letu”. Tukaziba masikio yao (wakalala hawasikii habri yoyote) katika pango hiyo kwa idadi ya miaka mingi” (18:10 -11).*

وَلَبِثُوا فِي كَهْفِهِمْ ثَلَاثَ مِائَةٍ سِنِينَ وَازْدَادُوا تِسْعًا ﴿٢٥﴾

*“Na walikaa katika pango yao miaka mia tatu na wakazidisha (miaka) tisa” (18:25).*

ثُمَّ بَعَثْنَا لَهُمْ لِنَعْلَمَ أَيُّ الْحِزْبَيْنِ أَحْصَىٰ لِمَا لَبِثُوا أَمَدًا

*Kisha tukawafufua ili tujulishe ni lipi katika makundi mawili lililohisabu sawa sawa muda waliokaa” (18:12).*

Baada ya kulala kwa miaka hiyo 309 ndipo walipozindukana. Mambo yalikuwa yamebadilika katika nchi na mateso kwa ajili ya kufuata mafundisho ya Mwenyezi Mungu yalikuwa hayapo tena. Lakini wao hawakuwa na habari. Walidhani wamelala muda mfupi tu. Hivyo walipoamka wakawa na hofu ile ile iliyowapeleka pangoni. Kuhusu hofu yao na kutokujua muda waliolala Qur’an inasema:

..... قَالَ قَائِلٌ مِّنْهُمْ كَمْ لَبِثْتُمْ قَالُوا لَبِثْنَا  
يَوْمًا أَوْ بَعْضَ يَوْمٍ قَالُوا رَبُّكُمْ أَعْلَمُ بِمَا لَبِثْتُمْ فَابْعَثُوا أَحَدَكُمْ  
بِوَرِقِكُمْ هَذِهِ إِلَى الْمَدِينَةِ فَلْيَنْظُرْ أَيُّهَا أَزْكَى طَعَامًا فَلْيَأْتِكُمْ بِرِزْقِ  
مِّنْهُ وَلْيَتَلَطَّفْ وَلَا يُشْعِرَنَّ بِكُمْ أَحَدًا ﴿١٩﴾ إِنَّهُمْ إِن يَظْهَرُوا عَلَيْكُمْ  
يَرْجُمُوكُمْ أَوْ يُعِيدُوكُمْ فِي مِلَّتِهِمْ وَلَنْ تُفْلِحُوا إِذَا أَبَدًا ﴿٢٠﴾

.....Akasema msemaji wao: “Mumekaa muda gani?”  
Wakasema: “Tumekaa siku moja au sehemu ya siku” (wengine)  
wakasema: “Mola wenu anajuwa zaidi muda mliokaa. Basi  
mtumeni mmoja wenu pamoja na fedha yenu hii mjini na  
akatazame chakula chake kipi ni tahara zaidi akuleteeni katika  
chakula chake. Na afanye mambo haya kwa busara wala  
asikutajeni kabisa kwa yoyote. “Kwani wao wakikujueni mlipo  
watakupigeni mawe au watakurudisheni katika Dini yao; na  
hapo hamtafaulu abadan” (18:19-20).

Historia imebainisha kuwa kipindi hicho vijana hao wanaamka toka usingizini wenyeji wa mji wa Ephesus na Roma yote, walikuwa na ubishani juu ya ukweli wa kufufuka na siku ya malipo. Basi kwa tukio hili ikawa ni fundisho na uthibitisho wa ukweli wa ahadi ya kufufuliwa.

وَكَذَلِكَ أَعْتَرْنَا عَلَيْهِمْ لِيَعْلَمُوا أَن وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ  
وَأَنَّ السَّاعَةَ لَا رَيْبَ فِيهَا .....

“Na namna hivi tuliwatambulisha (kwa watu) ili wapate kujua ya kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu (ya kufufuliwa viumbe) ni kweli, na kwamba Kiama hakina shaka.....” (18:21).

Maelezo zaidi juu ya vijana wa pangoni rejea Qur’an (18:9-26).



## **Mafunzo:**

Kutokana na kisa cha vijana wa pangoni tunajifunza yafuatayo:

### **(i) Alama ya kuwepo Allah(s.w) na Uwezo wake.**

Suala la vijana wa pangoni kulala miaka 309 kisha wakaamka ni la muujiza kama Qur'an yenyewe inavyobainisha:

﴿١﴾ أَمْ حَسِبْتَ أَنْ أَصْحَبَ الْكَهْفِ وَالرَّقِيمِ كَانُوا مِنْ آيَاتِنَا عَجَبًا

*Je! Unafikiri ya kwamba (wale) watu wa pangoni na (wenye habari) zile zilizoandikwa (vitabuni) walikuwa ajabu katika ajabu zetu”? (18:9).*

Si jambo la kawaida mtu kulala kwa muda mrefu (miaka 309) hali wala hanywi na bado akawa hai. Siku 20 zaweza kuwa kiwango cha juu ambazo aweza kukaa mtu bila kula wala kunywa na bado akawa hai. Lakini tunaambiwa vijana wa pangoni walikaa siku 309. Na sio kwamba walikufa wakaoza ndio wakafufuka. Bali walikuwa wazima wakigaragara pangoni.

وَتَحْسَبُهُمْ آيْقَاطًا وَهُمْ رُفُودٌ وَنُقِلَبُهُمْ ذَاتَ الْيَمِينِ وَذَاتَ الشَّمَالِ  
وَكَلَبُهُمْ بِسِطٍّ ذِرَاعِيَهُ بِالْوَصِيدِ لَوِ اطَّلَعَتْ عَلَيْهِمْ لَوَلَّيْت مِنْهُمْ فِرَارًا  
وَلَمَلَّيْت مِنْهُمْ رُعبًا ﴿١٨﴾

*“Na unadhani wamacho na hali wamelala. Na tunawageuza upande wa kulia na upande wa kushoto (wanapogaragara usingizini). Na mbwa wao kanyoosha mikono yake kizingitini. Kama ungewaona hakika ungegeuka upesi kuwakimbia na hakika ungejazwa khofu juu yao” (18:18).*

Huu ni muujiza wa kuonesha kuwepo kwa Allah na Uwezo wake. Aya tuliyoinkuu inatubainishia kuwa Allah(s.w) alijaaliya mazingira walimokuwa wamelala yakawa ni ya kutisha. Kwa hivyo

kwa muda wote wa miaka 309 hakuna aliyethubutu kufika karibu yao, hivyo kutogundila.

## **(ii) Ujasiri**

Imani ya kweli juu ya Allah(s.w) hujenga ujasiri wa hali ya juu. Mtu akishamkubali Allah(s.w) kuwa ndiye Muumba wake na Mwenye Mamlaka yote juu ya Uhai wake hana sababu tena ya kumuogopa na kumtetemekea mwingine. Kufanya hivyo itakuwa ni kwenda kinyume na imani yenyewe ya Kiislamu.

## **(iii) Uwingi na Uzee si Hoja.**

Mara nyingi maadui wa Uislamu wamekuwa wakitumia kisingizio cha vijana na uchache wa watu kutaka kuendesha udhalimu na ukandamizaji dhidi ya Waislamu. Wamekuwa wakisema hao ni vijana wachache. Kana kwamba jambo lolote lifanywalo na vijana ni baya. Lakini habari hizi za vijana wa pangoni zinaweka wazi kuwa vijana walikuwa na imani thabiti na Mwenyezi Mungu akawaongezea uongofu. Aidha wametajwa katika Qur'an ili iwe mfano kwetu.

## **(iv) Uthibitisho wa Utume wa Muhammad (s.a.w).**

Ukizingatia ukweli kwamba habari za vijana wa pangoni zilitokea zaidi ya miaka 309 kabla ya kuja Mtume(s.a.w) na kwamba sehemu ya tukio lenyewe ni mbali sana na mazingira alimokulia Mtume(s.a.w); maelezo ya Mtume ni ushahidi tosha wa utume wake. Katika mazingira alimokulia Mtume(s.a.w) hatutegemei apate taarifa sahihi za vijana wa pangoni kwingine zaidi kuliko kwa Allah(s.w). Na hili Qur'an yenyewe inalishuhudia katika aya ifuatayo:

نَحْنُ نَقُصُّ عَلَيْكَ نَبَأَهُم بِالْحَقِّ إِنَّهُمْ فِتْيَةٌ آمَنُوا بِرَبِّهِمْ وَزِدْنَاهُمْ

هُدًى ﴿١٣﴾

*“Ni sisi tunakusimulia habari zao kwa kweli. Hakika wao wlaikuwa ni vijana waliomuamini Mola wao. Nasi tukawazidisha uwongofu” (18:13).*

## **Al-Khidhri**

Jina Al-Khidhri halikutajwa mahali popote katika Qur’an. Ila Hadith sahihi za Mtume(s.a.w) na vitabu kadhaa ya historia vimentaja mja wa Allah habari zake zilizobainishwa katika Qur’an (18:60-82) kuwa ndiye Al-Khidhri. Upo utata katika kubaini uhakika wa Al-Khidhri kwamba alikuwa binadamu au malaika. Sheikh Abdallah Saleh Farsy katika tafsiri yake ya Qur’an anasema Khidhri alikuwa binadamu na Mtume ila alikuwa amepewa neema ya elimu ya ghaibu. Yaani alipewa uwezo wa kujua mambo yasiyo wazi au yasiyofahamika kwa kutumia uwezo wa milango ya fahamu ya kawaida tuliyonayo.

Sheikh Abul Ala Mauduud, anasema ama Khidhri alikuwa malaika au kiumbe kingine ambacho utendaji wake hauongozwi na sheria hizi za kawaida zinazowaongoza wanaadamu. Hoja zake ni kuwa Khidhri alitoboa jahazi la mtu na akaua kijana. Japo maelezo yanatolewa kuwa alifanya hivyo kwa sababu ya elimu ya ghaibu aliyoletewa na Mwenyezi Mungu kwamba atoboe jahazi ili isije likaporwa kwa kuonekana zuri na pili amuue kijana kwa kuhofia atakuja kuwa mbaya baadae, lakini huo si ushahidi mbele ya sheria za Mwenyezi Mungu zinazowahukumu watu hapa duniani. Kwa hoja hiyo Mauduud anadhani Khidhri alikuwa malaika anayepokea amri na kufanya kama anavyoamrisha na Allah au vinginevyo alikuwa kiumbe wa hali (nature) nyingine lakini si Mtume.

Kisa cha Al-Khidhri kinaanzia pale Mtume Musa (a.s) alipoweka azma ya kufanya safari hadi afikie makutano ya bahari mbili:

وَإِذْ قَالَ مُوسَى لِقَتْنَهُ لَا أَبْرَحُ حَتَّىٰ أَبْلُغَ مَجْمَعَ الْبَحْرَيْنِ أَوْ أَمْضِي

حُفْبًا ﴿١٠﴾

*Na (kumbukeni) Musa alipomwambia kijana wake: “Nitaendelea tu kwenda mpaka nifike katika maungano ya bahari mbili; au niendeleo karne na karne (mpaka nikutane na huyo ninayetaka kukutana naye)” (18:60).*

فَلَمَّا بَلَغَا مَجْمَعَ بَيْنَهُمَا نَسِيَا حُوتَهُمَا فَاتَّخَذَ سَبِيلَهُ فِي الْبَحْرِ

سَرَبًا ﴿١١﴾

*“Basi walipofika wote wawili (mahali) zinapoungana (hizo bahari mbili) walimsahau samaki wao; naye akashika njia yake kwenda baharini; hali ya kuwa inafanya alama” (18:61).*

فَلَمَّا جَاوَزَا قَالَ لِقَتْنَهُ ءَأَتَيْنَا غَدَاءَنَا لَقَدْ لَقِينَا مِنْ سَفَرِنَا هَذَا نَصَبًا ﴿١٢﴾

*Na walipofika mbele (Musa) alimwambia kijana wake: “Tutoo chakula chetu cha asubuhi, maana tumepata uchovu (mkubwa) katika safari yetu hii” (18:62).*

قَالَ أَرَءَيْتَ إِذْ أَوْيَيْنَا إِلَى الصَّخْرَةِ فَإِنِّي نَسِيتُ الْحُوتَ وَمَا أَنسَنِيهِ إِلَّا

الشَّمِيطُنُ أَنْ أَذْكُرَهُ وَاتَّخَذَ سَبِيلَهُ فِي الْبَحْرِ عَجَبًا ﴿١٣﴾

*Akasema: “Unaona! Pale tulipopumzika katika mlima basi hapo nimesahau (kukupua habari za) yule samaki. Na hakuna aliyenisahaulisha isipokuwa shetani, nisikumbuke. Naye akashika njia yake baharini kwa namna ya ajabu” (18:63).*

قَالَ ذَلِكَ مَا كُنَّا نَبْغُ فَارْتَدَّا عَلَىٰ ءَأَنَارِهِمَا قَصَصًا ﴿١٤﴾

*(Musa) akasema: “Hapo ndipo tulipokuwa tunapataka”. Basi wakarudi nyuma kwa kufuata njia yao (ile ile)” (18:64).*

فَوَجَدَا عَبْدًا مِنْ عِبَادِنَا ءَأْتَيْنَاهُ رَحْمَةً مِنْ عِنْدِنَا وَعَلَّمْنَاهُ مِنْ لَدُنَّا عِلْمًا ﴿١٥﴾

*Basi wakamkuta mja katika waja wetu tuliyempa rehema kutoka kwetu na tuliyemuelimisha ilimu (nyingi) zinazotoka kwetu” (18:65).*

قَالَ لَهُ مُوسَىٰ هَلْ أَتَّبِعُكَ عَلَىٰ أَنْ تُعَلِّمَنِي مِمَّا عَلَّمْتَ رُشْدًا ﴿٦٦﴾

*Musa akamwambia: “Je! Nikufuate ili unifundishe katika ule uwongofu uliofundishwa?” (18:66).*

Kwa mujibu wa mafundisho ya aya hizi, yaelekea Mtume Musa(a.s) alikuwa amepewa maelekezo na Allah(s.w) amtafute Khidhri akapate mwongozo na mafundisho kadhaa kupitia kwake. Makutano ya bahari mbili yaelekea ndipo Nabii Musa alipotakiwa akutane na Khidhri.

Mtume Musa(a.s) alikuwa na elimu ya kutosha kufanya kazi yake ya Utume kwa watu wake. Lakini hakuwa na elimu ya mambo yasiyo dhahiri. Kwa sababu hiyo Khidhri alikataa ombi la Mtume Musa la kutaka kuandamana naye. Hata hivyo baadaye alimkubalia ila kwa sharti kuwa asimuulize chochote katika yale atakayomuona anayafanya. Qur’an inabainisha hali hii katika aya zifuatazo:

قَالَ لَهُ مُوسَىٰ هَلْ أَتَّبِعُكَ عَلَىٰ أَنْ تُعَلِّمَنِي مِمَّا عَلَّمْتَ رُشْدًا ﴿٦٦﴾ قَالَ إِنَّكَ

لَنْ تَسْتَطِيعَ مَعِيَ صَبْرًا ﴿٦٧﴾ وَكَيْفَ تَصْبِرُ عَلَىٰ مَا لَمْ تُحِطْ بِهِ خُبْرًا

﴿٦٨﴾ قَالَ سَتَجِدُنِي إِن شَاءَ اللَّهُ صَابِرًا وَلَا أَعْصِي لَكَ أَمْرًا ﴿٦٩﴾ قَالَ فَإِنِ

أَتَّبَعْتَنِي فَلَا تَسْأَلْنِي عَنْ شَيْءٍ حَتَّىٰ أَحْدِثَ لَكَ مِنْهُ ذِكْرًا ﴿٧٠﴾

*Musa akamwambia: “Je! Nikufuate ili unifundishe katika ule uwongofu uliofundishwa?” akasema: “Hakika wewe huwezi kuvumilia kuwa pamoja nami. (Utaona usiyoweza kustahimili kuyaona)”. “Na utawezaje kuvumilia yake usiyojua hakika yake?” Akasema: “Akipenda Mwenyezi Mungu, utaniona mvumilivu, wala sitaasi amri yako”. Akasema: “Basi kama*

*utanifuata, usiniulize kwa lolote (utakaloliona) mpaka mimi nianze kukwambia” (18:66-70).*

Kwa makubaliano hayo Nabii Musa(a.s) akafuatana na Khidhri. Lakini kama Khidhri alivyoonesha wasiwasi, Musa hakuweza kustahimili matendo ya Khidhri. Awali Khidhri alitoboa jahazi waliyopanda. Musa hakustahimili ikabidi aulize kulikoni:

فَأَنطَلَقَا حَتَّىٰ إِذَا رَكَبَا فِي الْأَشْفَيْنِةِ خَرَفَهَا قَالَ أَخَرَفْتَهَا لِتُغْرِقَ أَهْلَهَا

لَقَدْ جِئْتَ شَيْئًا إِمْرًا ﴿٧٦﴾

*Hata walipopanda jahazi (yule Khidhri) aliitoboa. (Musa) akasema, “Je! Umeitoboa ili uwazamishe waliomo? Hakika umefanya jambo baya”. (18:71).*

Khidhri ilibidi amkumbushe sharti la kuandamana naye. Musa akaomba msamaha wakaendelea. Mbele ya safari wakamkuta kijana mdogo Khidhri akamuua. Hili nalo Musa hakuweza kuhimili. Ikabidi amulize Khidhri kwanini amemuua kijana asiye na hatia. Qur’an inatuambia:

فَأَنطَلَقَا حَتَّىٰ إِذَا لَفِيَا غُلَامًا فَفَتَلَهُ قَالَ أَقْتَلْتَنِي نَفْسًا زَكِيَّةً بِغَيْرِ نَفْسٍ

لَقَدْ جِئْتَ شَيْئًا نُكْرًا ﴿٧٤﴾

*Basi wote wawili wakaendelea kwenda. Hata wakamkuta kijana mdogo, na (yule Khidhri) akamuua. (Musa) akasema: “Ala! Umemuua mtu asiye na kosa wala hakumuua mtu? Bila shaka umefanya jambo baya kabisa” (18:74).*

Nabii Musa(a.s) akakumbushwa tena makubaliano yao na akaomba msamaha.

Hatimaye walifika katika mji ambapo waliomba chakula lakini wakanyimwa. Wakakuta ukuta wa moja ya nyumba za mjini hapo

unakaribia kuanguka. Khidhri akausimamisha. Hapa Musa aliuliza tena. Hii ikiwa ni mara ya tatu Musa kukhalifu makubaliano yao; Khidhri hakumsamehe tena. Khidhri akamsimulia hikma na tafsiri ya yote aliyoyafanya kisha wakafarikiana. Qur'an inatuambia:

قَالَ هَذَا فِرَاقُ بَيْنِي وَبَيْنِكَ سَأُنَبِّئُكَ بِتَأْوِيلِ مَا لَمْ تَسْتَطِعْ عَلَيْهِ

صَبْرًا ﴿٧٨﴾ أَمَا السَّفِينَةُ فَكَانَتْ لِمَسْكِينٍ يَعْمَلُونَ فِي الْبَحْرِ

فَأَرَدْتُ أَنْ أَعِيبَهَا وَكَانَ وَرَاءَهُمْ مَلِكٌ يَأْخُذُ كُلَّ سَفِينَةٍ غَصْبًا ﴿٧٩﴾

وَأَمَا الْغُلَامُ فَكَانَ أَبَوَاهُ مُؤْمِنَيْنِ فَخَشِينَا أَنْ يُرْهِقَهُمَا طُغْيَانًا وَكُفْرًا

﴿٨٠﴾ فَأَرَدْنَا أَنْ يُبْدِلَهُمَا رَبُّهُمَا خَيْرًا مِّنْهُ زَكَاةً وَأَقْرَبَ رُحْمًا ﴿٨١﴾

وَأَمَا الْجِدَارُ فَكَانَ لِغُلَامَيْنِ يَتِيمَيْنِ فِي الْمَدِينَةِ وَكَانَ تَحْتَهُ كَنْزٌ لَهُمَا وَكَانَ أَبُوهُمَا صَالِحًا فَأَرَادَ رَبُّكَ أَنْ

يَبْلُغَا أَشُدَّهُمَا وَيَسْتَخْرِجَا كَنْزَهُمَا رَحْمَةً مِّنَ رَبِّكَ وَمَا فَعَلْتُهُ عَنْ

أَمْرِي ذَلِكَ تَأْوِيلُ مَا لَمْ تَسْطِعْ عَلَيْهِ صَبْرًا ﴿٨٢﴾

(Khidhri) akasema: “Huku ndiko kufarikiana baina ya mimi na wewe. Hivi sasa nitakwambia hakika ya yale ambayo hukuweza kuyavumilia”. “Ama ile jahazi, ilikuwa ya masikini wafanyao kazi baharini, na nilitaka kuiharibu kwani mbele yao kulikuwa na mfalme anayekamata kila jahazi (zuri) kwa jeuri”. “Na ama yule kijana, wazazi wake walikuwa Waislamu kamili, tukahofia kwamba asije akawapelekea (wazee wake hao) katika uasi na ukafiri. Basi tulitaka Mola wao Awabadilishie mtoto aliye bora kuliko yeye kwa kutakasika, na aliye karibu zaidi kwa huruma”. Na ama ukuta ulikuwa wa watoto wawili mayatima mjni pale, na chini yake kulikuwa na khazina yao, na baba yao alikuwa

*mwema, kwa hivyo, Mola wako alitaka wafikie baleghe yao na wajitolee khazina yao. Hiyo ni rehema inayotoka kwa Mola wako. Nami sikufanya haya kwa amri yangu. Hiyo ndiyo hakika ya yale ambayo hukuweza kuyavumilia” (18:78-82).*

### **Mafunzo:**

**Kwanza**, Ni hali ya kawaida kwa binaadamu kupitisha maamuzi yake kutokana na taafira za wazi na matukio bayana. Undani na hikma ya matukio hufahamika kwa wale tu waliotunukiwa hikma na fikra zilizotulizana. Katika maisha ya kila siku wafalme na watawala jeuri hupita katika ardhi wakifuja neema za Allah(s.w) huku wakiwadhalilisha wengine kwa jeuri. Watu wema na watiifu kwa Mola wao wakati mwingine waweza kuonekana dhalili wasio na mali wala cheo katika jamii. Wasiomuamini Allah(s.w) wakiwa na mali na vyeo hutakabari na kumkana Mwenyezi Mungu. Wakaona maguvu yao ndio kila kitu kwa hiyo wakazidisha fisadi katika ardhi.

**Pili**, Kwa waumini uangalifu wahitajika vile vile kwa mtu anayetenda mema lakini hali yake kiuchumi kila siku inazidi kushuka ilhali makafiri wanazidi kujilimbikizia mali; aweza kuvunjika moyo na kukata tamaa.

**Tatu**, Kisa hiki cha Musa(a.s) na Khidhri kinatubainishia kuwa zaidi ya elimu hii tunayoidhibiti kwa milango yetu ya fahamu ipo hikma ya mambo mengi ambayo hatuijui mpaka tufunuliwe na Allah(s.w) Mtu aweza kuwa na neema fulani kumbe neema hiyo ni yenye shari na yeye. Na kinyume chake.

**Nne**, Ili Mtume Musa(a.s) apate kufahamu japo sehemu ndogo ya elimu aliyonayo Khidhri ilibidi afunge safari ndefu. Elimu yote ni milki ya Allah na humkunjulia amtakaye kiasi atakacho. Lakini pia juhudi kubwa sana inahitajika katika kutafuta elimu.

**Tano**, Kisa hiki ni kiashiria cha upana wa elimu ya Allah(s.w). Mtume Musa(a.s) alikuwa Mtume na aliletewa Wahay akafahamu



mambo mengi sana. Hata hivyo anakutana na Khidhri mwenye elimu ambayo kwa Musa(a.s) inaonekana kama miujiza.

**Sita**, Mambo matatu aliyoyafanya Khidhri akiwa na Mtume Musa(a.s) yanatupa mafundisho yafuatayo: Mosi; hasara au uharibifu wa jambo fulani yaweza kuwa ndio kheri yenyewe. Kutobolewa kwa jahazi kulilifanya lionekane si zuri. Hii ilifanya kinga kumzuia mfalme asilipore. Pili; ukatili wakati mwingine waweza kuwa ndio amani na msaada kwa watu. Maisha hutolewa muhanga kwa faida ya Ummah. Tatu; matendo ya wema si lazima yazae matunda hapo hapo. Wema unahimizwa hata pale ambapo hakuna dalili ya kulipwa wema.

## **Dhulqarnain**

Dhulqarnain sio jina la mtu bali cheo, maana yake ikiwa: “Mwenye Pembe Mbili”. Qur’an haibainishi Dhulqarnain aliishi wapi na wakati gani wa historia. Lakini kwa vile habari zake zinasimuliwa ndani ya Qur’an kama jibu la Mtume(s.a.w) kwa Maquraish kutokana na swali walilopewa na Mayahudi wamwulize Mtume; ni dhahiri kuwa:

- (a) Dhulqarnain aliishi miaka mingi kabla ya Mtume (s.a.w).
- (b) Historia yake haikuwa inafahimika Arabuni.
- (c) Mayahudi walikuwa wakifahamu historia yake.

Wafasiri wengi wa Qur’an na watu wa historia wanamtaja Dhulqarnain kuwa ni mmoja wa wafalme wa Kifursi ambaye aliungusha ufalme wa Babylon na kuwafanya Waisrail wawe huru. Hii ilitokea kiasi cha maika 1000 kabla ya Mtume(s.a.w). Akiitwa Dhulqarnain (Mwenye Pembe Mbili) kwa vile nchi aliyokuwa anatawala ilikuwa ni nchi mbili zilizoungana na kufanya umbo la Pembe Mbili. Dhulqarnain alikuwa mtawala mwenye nguvu lakini muadilifu pia. Aidha Mwenyezi Mungu alimneemesha kwa kumpa njia za kupatia kila kitu.

إِنَّا مَكَّنَّا لَهُ فِي الْأَرْضِ وَءَاتَيْنَاهُ مِنْ كُلِّ شَيْءٍ سَبَبًا ﴿٨٤﴾

“Sisi Tulimmakinisha katika ardhi na Tukampa njia za kupatia kila kitu” (18:84).

Kwa uwezo aliopewa Dhulqarnain alipanua ufalme wake toka Magharibi kuelekea Mashariki na Kaskazini na Kusini. Haya yametajwa katika Qur’an kwa lugha ya Ishara kuwa alisafiri nchi za Maghabribi, Mashariki n.k. Rejea Qur’an (18:83-93).

فَأَتْبَعَ سَبَبًا ﴿٨٥﴾ حَتَّىٰ إِذَا بَلَغَ مَغْرِبَ الشَّمْسِ وَجَدَهَا تَغْرُبُ فِي عَيْنٍ

حَمِيمَةٍ وَوَجَدَ عِنْدَهَا قَوْمًا قُلْنَا يَبْدَأُ الْقُرْنَيْنِ ۖ إِنَّمَا أَنْتَ تُنذِرُ

فِيهِمْ حُسْنًا ﴿٨٦﴾ قَالَ أَمَّا مَنْ ظَلَمَ فَسَوْفَ نُعَذِّبُهُ ثُمَّ يُرَدُّ إِلَىٰ

رَبِّهِ فَيُعَذِّبُهُ عَذَابًا نُكْرًا ﴿٨٧﴾ وَأَمَّا مَنْ ءَامَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا فَلَهُ

جَزَاءٌ أَلْحَسَنٌ وَسَتَقُولُ لَهُ مِنْ أَمْرِنَا يُسْرًا ﴿٨٨﴾

*Basi akafuata njia. Mpaka alipofika machweo ya jua. (Nchi za Magharibi) aliliona linatua katika chemchem (ziwa) yenye matope mengi. Na pale akawakuta watu. Tukasema: “Ewe Dhulqarnain waadhibu au wafanyie wema”. Akasema: “Ama anayedhulumu basi tutamuadhibu, kisha atarudishwa kwa Mola wake, naye atamuadhibu adhabu mbaya kabisa”. Na yule mwenye kuamini na kufanya vitendo vizuri, atapata ujira mwema, nasi tutamwambia (tutamfanyia) lililo jepesi katika amri yetu” (18:85-88).*

Uadilifu na wema wa Dhulqarnain unaonekana pia pale alipowakuta watu wanaovamiwa na kuonewa na watu wa makabila mengine. Katika Asia ya Kati yalikuwepo makabila yaliyojulikana kama Tartus, Mongolis, Huns na Scythians. Katika hawa baadhi yao ndio waliotajwa kama Yaajuju na Maajuju. Hawa walikuwa wakizivamia baadhi ya tawala na kuleta uharibifu.

Raia wa tawala hizo walimuomba Dhulqarnain awajengee ukuta kuzunguka nchi hizo ili iwe kinga kuwazuia Yaajuju na Maajuju wasiwavamie. Japo walipendekeza wampe ujira Dhulqarnain kwa kazi hiyo, lakini Dhulqarnain hakutaka malipo. Aliwasaidia bure kwa kutaraji malipo bora zaidi kutoka kwa Allah(s.w). Rejea kisa hiki katika aya zifuatazo:

قَالُوا يَبْنَؤُا الْقَرْنَيْنِ إِنِّي يَا جُوجَ وَمَا جُوجَ مُفْسِدُونَ فِي  
الْأَرْضِ فَهَلْ نَجْعَلُ لَكَ خَرْجًا عَلَىٰ أَنْ تَجْعَلَ بَيْنَنَا وَبَيْنَهُمْ  
سَدًّا ﴿٤٤﴾ قَالَ مَا مَكَّنِّي فِيهِ رَبِّي خَيْرٌ فَأَعِينُونِي بِقُوَّةٍ أَجْعَلْ  
بَيْنَكُمْ وَبَيْنَهُمْ رَدْمًا ﴿٤٥﴾ ءَأَثُونِي زُبَرَ الْحَدِيدِ حَتَّىٰ إِذَا سَاوَىٰ بَيْنَ  
الْصَّدَفَيْنِ قَالَ أَنْفُخُوا حَتَّىٰ إِذَا جَعَلَهُ نَارًا قَالَ ءَأَثُونِي أُفْرِغْ عَلَيْهِ  
قَطْرًا ﴿٤٦﴾ فَمَا اسْتَطَعُوا أَنْ يَظْهَرُوهُ وَمَا اسْتَطَعُوا لَهُ نَقْبًا ﴿٤٧﴾

قَالُوا يَبْنَؤُا الْقَرْنَيْنِ إِنِّي يَا جُوجَ وَمَا جُوجَ مُفْسِدُونَ فِي  
الْأَرْضِ فَهَلْ نَجْعَلُ لَكَ خَرْجًا عَلَىٰ أَنْ تَجْعَلَ بَيْنَنَا وَبَيْنَهُمْ  
سَدًّا ﴿٤٤﴾ قَالَ مَا مَكَّنِّي فِيهِ رَبِّي خَيْرٌ فَأَعِينُونِي بِقُوَّةٍ أَجْعَلْ  
بَيْنَكُمْ وَبَيْنَهُمْ رَدْمًا ﴿٤٥﴾ ءَأَثُونِي زُبَرَ الْحَدِيدِ حَتَّىٰ إِذَا سَاوَىٰ بَيْنَ  
الْصَّدَفَيْنِ قَالَ أَنْفُخُوا حَتَّىٰ إِذَا جَعَلَهُ نَارًا قَالَ ءَأَثُونِي أُفْرِغْ عَلَيْهِ  
قَطْرًا ﴿٤٦﴾ فَمَا اسْتَطَعُوا أَنْ يَظْهَرُوهُ وَمَا اسْتَطَعُوا لَهُ نَقْبًا ﴿٤٧﴾

*Wakasema: “Ewe Dhulqarnain! Hakika Yaajuju na Maajuju wanafanya uharibifu katika ardhi. Basi je; tukupe ujira ili utie baina yetu na baina yao kizuizi?” Akasema “Yale ambayo Mola wangu amenimakinishia (amenipa) ni bora (kuliko ujira wenu). Lakini nisaidieni kwa nguvu (kazi). Nitaweka baina yenu na baina yao kizuizi imara”. “Nileteeni vipande vya chuma”. Hata alipoijaza (kwa hicho chuma) nafasi iliyo katikati ya milima miwili alisema: “Pulizeni (moto)” mpaka alipokifanya (kile*

chuma) kuwa (kama) moto alisema: “Nileteeni shaba iliyoyayuka niimwage juu yake”. Basi (Yaajuju na Maajuju) hawakuweza kuukwea wala hawakuweza kuutoboa”. Akasema: “Hii ni rehema itokayo kwa Mola wangu”. Na itakapofika ahadi ya Mola wangu, atauvunjavunja. Na ahadi ya Mola wangu ni kweli tu” (18:94-98).

Katika juhudi za Maquraish kumpinga Mtume(s.a.w) walikuwa wakichukua maswali kutoka kwa Mayahudi na kumuuliza Mtume. Lengo likiwa kupata kisingizio cha kumkana endapo atashindwa kujibu kwa usahihi. Moja ya maswali waliyomuliza ni kutaka kujua juu ya Dhulqarnain.

وَيَسْأَلُونَكَ عَنِ ذِي الْقَرْنَيْنِ ۖ قُلْ سَأَتْلُو عَلَيْكُمْ مِنْهُ ذِكْرًا

“Na wanakuuliza habari za Dhulqarnain. Waambie  
“Nitakusomeeni baadhi ya hadithi yake” (18:83).

Jawabu la Mtume halikuishia kuelezea tu kuwa Dhulqarnain alikuwa mfalme katika zama fulani. Lakini zilimbainisha kama mtu aliyekuwa Mcha-Mungu na Muadilifu. Mfalme aliyenemeshwa kwa mali na nguvu kubwa na juu ya hayo hakutakabari. Bali akawa anamkumbuka Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo maelezo ya Mtume(s.a.w) yakawa yanawaongezea Maquraish ujumbe wa Tawhiid.

Katika zama zetu za leo watawala walio wengi nguvu za kisiasa na kiuchumi walizo nazo, imekuwa ndio sababu ya wao kutakabari na kufanya uufisadi katika ardhi.

Nchi kama Marekani leo hii inaonekana ndio taifa lenye nguvu – “Super Power”, lakini kwa vile limejengwa katika misingi ya kikafiri na ushirikina, viongozi wake wameshindwa kuwa waadilifu kwa amana waliyopewa. Pale wanapotetea maslahi yao ya kidunia hutumia maguvu yao kumwaga damu za watu na kuharibu mali za wengine kwa dhulma. Lakini hawapo tayari kutetea haki ya

mnyonge kama kufanya hivyo hakuna maslahi kwao. Ni tofauti na Dhulqarnain alivyotumia maguvu yake kuwakinga watu walioishi katikati ya milima miwili wasishambuliwe na Yaajuju na Maajuju, bila ya malipo. Hii inatufikisha kwenye fundisho la msingi kuwa, amani, utulivu na utengamano katika jamii, hauwezi kupatikana kwa watu wote bila ya watu kumtambua Muumba wao na kuishi kufuatana na Mwongozo wake.

## Luqman.

Luqman ni katika watu wema kabisa waliopita zama za nyuma. Ingawa zipo simulizi nyingi juu yake katika fasihi na tamaduni za Uarabuni; lakini hapana maelezo ya uhakika juu ya mahali alipoishi wala wakati. Qur'an na Hadith za Mtume(s.a.w) nazo hazigusii lolote juu ya kabila lake, wakati na mahali alimoishi. Hata hivyo muhimu si kujua haya. Ila ujumbe unaopatikana kutokana na mwenendo wake mzuri ndio jambo la msingi.

Luqman ni kigezo cha hikma. Anatubainishia kuwa maisha ya busara yenye kheri na mja ni yale yenye kujengwa juu ya msingi wa kumpwekesha na kumtii Muumba. Kumtambua na kumpwekesha Muumba ndio chimbuko la hikima ya kweli:

وَلَقَدْ آتَيْنَا لُقْمَانَ الْحِكْمَةَ أَنْ اشْكُرْ لِلَّهِ وَمَنْ  
 يَشْكُرْ فَإِنَّمَا يَشْكُرُ لِنَفْسِهِ ۖ وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ حَمِيدٌ ﴿١٣﴾

*Na kwa yakini Tulimpa Luqman hikma tukamwambia:  
 “Mshukuru Mwenyezi Mungu: na atakayeshukuru, kwa yakini anashukuru kwa ajili ya nafsi yake; na atakayekufuru, Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, Asifiwaye” (31:12).*

Ni jambo la lazima watu waelewe uhusiano wao na Mwenyezi Mungu na wamwabudu ipasavyo:

وَإِذْ قَالَ لِقْمَنُ لِبَنِيهِ وَهُوَ يَعِظُهُ وَيَدْبُرُ نَسِيًّا لَا تَشْرِكْ  
بِاللَّهِ إِنَّ الشِّرْكَ لَظُلْمٌ عَظِيمٌ ﴿١٣﴾

*Na (wakumbushe) Luqman alipomwambia mwanawe; na hali ya kuwa anampa nasaha. Ewe mwanangu! Usimshirikishe Mwenyezi Mungu, maana kushirikisha ndio dhulma kubwa” (31:13).*

Katika aya hii kupitia kwa Luqman akimnasihi mtoto wake; Mwenyezi Mungu anatumababisha tuelekane na shiriki. Vipi uumbwe na Mwenyezi Mungu umwabudu mwingine!

Kumuabudu Mwenyezi Mungu kunaandamana vile vile na kufanya wema kwa wanadamu, wazazi wakishika nafasi ya kwanza. Lakini kinyume na utii kwa Allah(s.w); utii kwa wazazi una mipaka. Wazazi na watu wengine hutiiwa tu pale ambapo kutii huko hakumpelekei mtu kumuasi Mwenyezi Mungu:

وَوَصَّيْنَا الْإِنْسَانَ بِوَالِدَيْهِ حَمَلَتْهُ أُمُّهُ وَهَنًا عَلَىٰ وَهْنٍ وَفِصْلَةٌ فِي  
عَامَيْنِ أَنِ اشْكُرْ لِي وَلِوَالِدَيْكَ إِلَيَّ الْمَصِيرُ ﴿١٤﴾

*“Na tumemuusia mwanadamu (kuwafanyia ihsani) wazazi wake mama yake ameichukua mimba yake kwa udhaifu juu ya udhaifu; na (kumnyonyesha na kuja) kumwachisha kunyonya katika miaka miwili – ya kwamba unishukuru Mimi na Wazazi wako, marejeo yenu ni Kwangu” (31:14).*

وَإِنْ جَاهَدَاكَ عَلَىٰ أَنْ تُشْرِكَ بِي مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ فَلَا تُطِعْهُمَا  
وَصَاحِبُهُمَا فِي الدُّنْيَا مَعْرُوفًا وَاتَّبِعْ سَبِيلَ مَنْ أَنَابَ إِلَيَّ ثُمَّ إِلَيَّ  
مَرْجِعُكُمْ فَأُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٥﴾

*“Na (wazazi wako) wakikushurutisha kunishirikisha na (yale) ambayo huna ilimu nayo, usiwatii; lakini kaa nao kwa wema hapa duniani; shika njia ya wale wanaoelekea Kwangu, kisha marejeo yenu ni Kwangu; hapo Nitakwambieni mliyokuwa mkiyatenda” (31:15).*

Akiendelea kumnasihi mwanawe, Mzee Luqman alimsisitizia umuhimu wa swala, kuamrisha mema, kukataza mabaya na kufanya subira katika kuyafanya yote hayo. Aidha alimfahamisha juu ya Ujuzi wa Mwenyezi Mungu kwamba hapana jambo lolote linaloweza kufanyika bila kufahamika mbele ya Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo mwanadamu hawezi kumdanganya wala kumfanyia hila Mwenyezi Mungu.

يَدْبُنِيَّ إِنَّهَا إِنْ تَكُ مِثْقَالَ حَبَّةٍ مِنْ خَرْدَلٍ فَتَكُنْ فِي صَخْرَةٍ أَوْ فِي

السَّمَوَاتِ أَوْ فِي الْأَرْضِ يَأْتِ بِهَا اللَّهُ إِنَّ اللَّهَ لَطِيفٌ خَبِيرٌ ﴿١٦﴾

*Ewe mwanangu! “Kwa hakika jambo lolote lijapokuwa na uzito wa chembe ya hardali, likawa ndani ya jabali au mbinguni au au katika ardhi, Mwenyezi Mungu atalileta (amlipe aliyefanya); bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa mambo yaliyofichikana (na) Mjuzi wa mambo yaliyo dhahiri” (31:16).*

يَدْبُنِيَّ أَقِمِ الصَّلَاةَ وَأْمُرْ بِالْمَعْرُوفِ وَانْهَ عَنِ الْمُنْكَرِ

وَأَصْبِرْ عَلَىٰ مَا أَصَابَكَ ۗ إِنَّ ذَٰلِكَ مِنْ عَزْمِ الْأُمُورِ ﴿١٧﴾

*Ewe mwanangu! “Simamisha Sala, na uamrisha mema; na ukataze mabaya, na usubiri juu ya yale yatakayokusibu. Hakika hayo ni katika mambo yanayostahiki kuazimiwa (na kila mtu)” (18:17).*

Mwisho Mzee Luqman anamuusia mwanawe asiwe na kibiri, jeuri wala dharau. Bali awe mtu mpole na mwenye mwendo wa kati na kati:

وَلَا تُصَعِّرْ خَدَّكَ لِلنَّاسِ وَلَا تَمْشِ فِي الْأَرْضِ مَرَحًا ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ كَلًّا

مُخْتَالًا فَخُورًا ﴿١٨﴾

*“Wala usiwatazame (usiwafanyie watu jeuri) kwa upande mmoja wa uso, wala usende katika nchi kwa maringo, hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila ajivunae, ajifaharishaye” (31:18).*

وَأَقْصِدْ فِي مَشْيِكَ وَأَغْضُضْ مِنْ صَوْتِكَ إِنَّ أَنْكَرَ الْأَصْوَاتِ

لَصَوْتُ الْحَمِيرِ ﴿١٩﴾

*“Na ushike mwendo wa kati na kati, na uteremshe sauti yako, bila shaka sauti ya punda ni mbaya kuliko sauti zote” (31:19).*

Kwa muhtasari Mzee Luqman amempa nasaha mwanawe juu ya mambo ya msingi yafuatayo:

- Kumtambua Allah(s.w) na sifa zake na kumpwekesha ipasavyo.
- Kushukuru neema za Allah kwa kumtii ipasavyo.
- Kufanya jitihada za makusudi za kusimamisha Uislamu katika jamii na kudumu katika jitihada hizo.
- Kujipamba na tabia njema.

Luqman amekuwa ni mfano kwetu juu ya malezi ya watoto. Mzazi pamoja na kuhangaika kumpatia mtoto chakula, malazi na nguo; lakini la msingi zaidi ni kumpa malezi mazuri. Malezi ambayo yatampelekea mtoto kumjua Muumba wake. Malezi ambayo yatamfanya mtoto aelewe na kukifanyia kazi cheo chake cha ukhalifa hapa duniani.

## **WATU WAOVU WALIOTAJWA KATIKA QUR’AN**

Kama ilivyo kwa watu wema, wapo watu waovu wengi waliotajwa ndani ya Qur’an. Hapa tutataja mifano michache kwa lengo la kupata mafunzo yatokanayo na maisha ya watu hao.

### **Watu waliovunja amri ya kuheshimu siku ya Jumamosi.**

Katika zama za kale Mayahudi walikatazwa kufanya kazi siku ya Jumamosi. Siku hiyo ilitengwa iwe ya kufanya ibada tu. Hata hivyo



Mayahudi kidogo kidogo walianza kuivunja amri hii kwa ujanja ujanja na hatimaye wakaivunja kwa dhahiri. Basi Mwenyezi Mungu aliwaadhibu kwa kuwageuza kuwa Manyani.

وَلَقَدْ عَلِمْتُمُ الَّذِينَ أَعْتَدُوا مِنْكُمْ فِي السَّبْتِ فَقُلْنَا لَهُمْ كُونُوا

قِرْدَةً خَاسِئِينَ ﴿١٥﴾ فَجَعَلْنَاهَا نَكَالًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهَا وَمَا خَلْفَهَا

وَمَوْعِظَةً لِّلْمُتَّقِينَ ﴿١٦﴾

*“Na kwa yakini mmekwisha kujua (khabari za) wale walioasi miongoni mwenu katika (amri ya kuihishimu) Jumamosi. Basi tukwaambia: “Kuweni manyani wadhhalifu”. Kwa hiyo tukaifanya (adhabu hiyo) kuwa onyo kwa wale waliokuwa katika zama zao na waliokuja nyuma yao, na (tukaifanya ni) mawaidha kwa wamchao Mwenyezi Mungu” (2:65:66).*

Ni katika utaratibu wa Mwenyezi Mungu kuwapa watu mtihani ili kuwapambanua wale wanaotii kweli na wale wenye kuasi. Kwa hiyo amri ya kutokufanya kazi siku ya Jumamosi iliandamana na mtihani. Ulikuwako mji mmoja wa Kiyahudi ambao wakazi wake kazi yao kubwa ilikuwa uvuvi. Basi Mwenyezi Mungu aliwaletea mtihani. Ikawa ile siku ya Jumamosi waliyokatazwa kufanya kazi samaki walijaa na kuonekana wakichezacheza majini. Hali ikawa hivi siku zote za Jumamosi; lakini siku zingine ikawa taabu kuwapata samaki. Hali hii iliwashinda wengine kustahamili. Wakawa wanakwenda kuvua siku hiyo iliyokatazwa. Wale walioamini kweli kweli kitendo cha wenzao kuvunja amri ya Jumamosi kiliwashtua. Wakawaendea kuwanasihhi na kuwakataza. Wapo waliotii amri ya kutokufanya kazi; lakini wasichukue juhudi yoyote kuwaonya wale waliovunja amri.

Basi ilipokuja amri ya Mwenyezi Mungu ya kuaadhibiwa; walionusurika ni wale waliotii na wakawaonya wenzao. Wale ambao hawakuasi lakini hawakuwanasihhi na kuwakataza wale waliovunja amri, waliadhibiwa pia. Habari hizi zinapatikana kwa urefu kaitka aya zifuatazo:

وَسَأَلَهُمْ عَنِ الْقَرْيَةِ الَّتِي كَانَتْ حَاضِرَةَ الْبَحْرِ إِذْ يَعْدُونَ فِي السَّبْتِ إِذْ  
تَأْتِيهِمْ حِيتَانُهُمْ يَوْمَ سَبْتِهِمْ شُرَّعًا وَيَوْمَ لَا يَسْبِتُونَ لَا تَأْتِيهِمْ كَذَلِكَ  
نَبَأُوهُمْ بِمَا كَانُوا يَفْسُقُونَ ﴿١١٣﴾

“Na waulizeni habari za mji ambao ulikuwa kando ya bahari (watu wa mji huo) walipokuwa wakivunja (sheria ya) Jumamosi (ambayo waliambiwa wasifanye kazi katika siku hiyo, wafanye ibada tu. Na kazi yao ilikuwa uvuvi). Samaki wao walipowajia juu juu siku za Jumamosi zao, na siku isiyokuwa Jumamosi hawakuwa wakiwajia (hivyo). Basi namna hivyo tuliwatia mtihani kwa sababu ya kuasi kwao” (7:163).

وَإِذْ قَالَتْ أُمَّةٌ مِنْهُمْ لِمَ تَعِظُونَ قَوْمًا اللَّهُ مُهْلِكُهُمْ أَوْ مُعَذِّبُهُمْ  
عَذَابًا شَدِيدًا قَالُوا مَعْذِرَةً إِلَىٰ رَبِّكُم وَلَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ ﴿١١٤﴾

“Na (wakumbushe wakati) baadhi ya watu katika wao waliposema (kuwaonya waliovunja hishima ya Jumamosi kwa kuvua, na hali ya kuwa wamekataza, waliposema): “Pana faida gani kuwaonya watu ambao Mwenyezi Mungu atawaua au atawaadhibu kwa adhabu kali (papa hapa)?” Wakasema: “Tupate kuwa na udhuru mbele ya Mola wenu (kuwa tumeonya lakini hatukusikilizwa) na huenda wakaogopa” (7:164).

فَلَمَّا نَسُوا مَا ذُكِّرُوا بِهِ أَنْجَبْنَا الَّذِينَ يَنْهَوْنَ عَنِ السُّوءِ وَأَخَذْنَا الَّذِينَ  
ظَلَمُوا بِعَذَابٍ بَئِيسٍ بِمَا كَانُوا يَفْسُقُونَ ﴿١١٥﴾

“Basi walipoyapuuza waliyokuwa wakikumbushwa, tuliwaokoa wale waliokuwa wakikataza maovu na tukawatesa wale waliodhulumu kwa adhabu mbaya kabisa kwa kuasi kwao” (7:165).

فَلَمَّا عَتَوْا عَنْ مَا نُهُوا عَنْهُ قُلْنَا لَهُمْ كُونُوا قِرَدَةً خَاسِئِينَ ﴿١١٦﴾

“Na walipotakabari wasiache waliyokatazwa, tuliwaambia: “Kuweni manyani madhalilifu” (7:166).

## Mafunzo:

Funzo la **kwanza** tunalopata kutokana na kisa hiki ni kufahamu falsafa na lengo la maisha ya mwanadamu. Tunafahamishwa katika Qur'an kuwa lengo la kuumbwa mwanadamu ni kumwabudu Allah(s.w).

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥١﴾

“Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu” (51:56).

Pamoja na lengo hilo kuu tunafahamishwa kuwa mwanadamu amezungukwa na mitihani ya kila namna. Mitihani hii inadhihiri katika sura ya makatazo na maamrishi ya Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo kipindi cha uhai wetu wote ni kipindi cha mitihani kwetu:

تَبَرَّكَ الَّذِي بِيَدِهِ الْمُلْكُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١﴾ الَّذِي

خَلَقَ الْمَوْتَ وَالْحَيَاةَ لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا وَهُوَ الْعَزِيزُ

الْعَفُورُ ﴿٢﴾

*Ametukuka yule ambaye mkononi mwake umo ufalme (wote). Naye ni Mwenye uweza juu ya kila kitu. Amabaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi. Naye ni Mwenye nguvu na Mwenye Msamaha” (67:1-2).*

Kwa kuzingatia lengo hilo mwanadamu anatakiwa ajichunge katika kuchuma kwake na mengineyo ayafanyayo katika kuendeleza maisha yake asitoke katika lengo kuu. Kama ni kuchuma na kutumia mali basi iwe ni kwa ajili ya kufikia lengo la kuumbwa kwake. Mtu asije kufanya kuchuma na kutumia ndio lengo lenyewe la maisha. Kwa hiyo hata kama ataona mahali pana chumo zuri kiasi gani hatalikimbilia endapo kufanya hivyo kutamtoa katika twaa ya Mwenyezi Mungu.

Jambo la msingi la kuzingatia ni kuwa maisha yamejaa vishawishi vingi sana. Watu waliovunja heshima ya siku ya

Jumamosi walishindwa kuhimili kishawishi cha upatikanaji wa samaki. Leo sisi tumeamriwa inapaoadhiniwa Sala ya Ijumaa tuache shughuli zote tukimilie kwenye Swala. Hapa panahitaji uangalifu. Yawezekana kwa mfanya biashara asubuhi yote ya siku ya Ijumaa asipate wateja. Inapokaribia saa sita mchana ndio wakaanza kumiminika. Bila kuwa makini katika hali kama hiyo mtu atafeli mtihani kama ilivyokuwa kwa wale walioshindwa kuhimili kuwaona samaki nje nje wasiwavue.

Funzo la **pili** na la msingi tunalopata ni kuwa suala la kuamrishana mema na kukatazana mabaya ni muhimu mno. Mtu pekee kuacha mabaya haitoshi. Ni wajibu juu yake pia awaelimishe na kuwahimiza wengine nao wafanye vitendo vizuri. Aidha ni muhimu afanye juhudi kuwaonya na kuwakataza wengine wasifanye maovu.

Katika aya ya 165 ya Sura ya 7 tuliyoinukuu hapo juu imebainishwa wazi kuwa waliokoloewa ni wale waliokuwa wakikataza maovu. Kwa hiyo pamoja na juhudi tunazofanya kuzitakasa nafsi zetu hapana budi juhudi hizo ziende sambamba na harakati za kuelimisha na kuwanasihia wengine. Na kufuzu kwa Muislamu kumeegemea kazi ya kuamrisha mema na kukataza maovu.

وَلْتَكُنْ مِنْكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى الْخَيْرِ وَيَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ  
الْمُنْكَرِ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿١٦٤﴾

*“Na wavewo katika nyinyi watu wanaolingania kheri (Uislamu) na wanaoamrisha mema na wanaokataza maovu. Na hao ndio watakaotengenekewa” (3:104).*

## Firaun, Qarun na Hamana

Karun na Hamana waliishi zama za Mtume Musa(a.s) na walikuwa viongozi waandamizi wa Firaun. Walikuwa ni watu maarufu katika jamii yao na walikuwa mstari wa mbele katika kumpinga Mtume Musa(a.s).

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا مُوسَىٰ بِآيَاتِنَا وَسُلْطَانٍ مُّبِينٍ ﴿٢٣﴾ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ وَهَمَّانَ

وَقَارُونَ فَقَالُوا سَاجِدْ كَذَّابٌ ﴿٢٤﴾

*“Na kwa yakini tulimtuma Musa pamoja na miujiza yetu na hoja (dalili) zilizo dhahiri. (Tulimpeleka) kwa Firauni na Hamana na Karun, wakasema: “(Huyu ni) Mchawi, muongo mkubwa” (40:23-24).*

Katika aya nyingine Mwenyezi Mungu anatumfahamisha kuwa aliwaangamiza Firaun, Hamana na Qarun kwa sababu waliyakanusha mafundisho ya Mtume Musa na wakatakabari:

وَقَارُونَ وَفِرْعَوْنَ وَهَمَّانَ ۗ وَقَدْ جَاءَهُمْ مُوسَىٰ بِالْبَيِّنَاتِ فَاسْتَكْبَرُوا

فِي الْأَرْضِ وَمَا كَانُوا سَابِقِينَ ﴿٢٦﴾ فَكَلَّا أَخَذْنَا بِذُنُوبِهِ ۗ فَمِنْهُمْ مَنْ

أَرْسَلْنَا عَلَيْهِ حَاصِبًا وَمِنْهُمْ مَنْ أَخَذَتْهُ الصَّيْحَةُ وَمِنْهُمْ مَنْ خَسَفْنَا بِهِ

الْأَرْضَ وَمِنْهُمْ مَنْ أَغْرَقْنَا وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُظْلِمَهُمْ وَلَكِنْ كَانُوا أَنْفُسَهُمْ

يَظْلِمُونَ ﴿٤٠﴾

*Na (vile vile) Qarun na Firauni na Hamana (waliangamizwa); na hakika aliwajia Musa kwa miujiza waziwazi, lakini walijivuna katika ardhi, lakini hawakuweza kumshinda Mwenyezi Mungu. Basi kila mmoja tulimtesa kwa sababu ya dhambi zake. Miongoni mwao wako tuliowapelekea kimbunga cha changarawe; na miongoni mwao wako waliotolewa roho kwa ukulele mkubwa, na miongoni mwao wako tuliowadidimiza ardhini na miongoni mwao wako tuliowagharikisha na hakuwa Mwenyezi Mungu*

*Mwenye kuwadhulumu, lakini walikuwa wakijidhulumu (wenyewe) nafsi zao” (29:39-40).*

Qarun alijaaliwa kuwa na mali nyingi sana. Lakini alilisahau lengo la maisha akatakabari. Watu walio karibu naye walimnasih lakini hakuzinduka. Alijivuna na kuona kuwa utajiri aliokuwa nao kaupata kwa juhudi na elimu yake. Alisahau kuwa hiyo ni neema kutoka kwa Allah(s.w).

﴿إِنَّ قَارُونَ كَانَ مِنْ قَوْمِ مُوسَى فَبَغَى عَلَيْهِمْ  
وَأَتَيْنَاهُ مِنَ الْكُنُوزِ مَا إِنَّ مَفَاتِحَهُ لَتَنُوءُ بِالْعُصْبَةِ أُولَى الْقُوَّةِ إِذْ  
قَالَ لَهُ قَوْمُهُ لَا تَفْرَحْ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْفَرِحِينَ ﴿٧٦﴾

*Hakika Qarun alikuwa katika watu wa Musa, lakini aliwafanyia dhulma. Na tulimpa hazina ambazo funguo zake zinawatopeza watu wenye nguvu (kuzichukua). Walimwambia watu wake: “Usijione (usijigambe), hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wanaojigamba” (28:76).*

﴿قَالَ إِذْمَأُوتَيْنَاهُ عَلَىٰ عِلْمٍ بِنَدِيٍّ أَوْلَمْ يَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ قَدَّ  
أَهْلَكَ مِنْ قَبْلِهِ، مِنَ الْقُرُونِ مَنْ هُوَ أَشَدُّ مِنْهُ قُوَّةً وَأَكْثَرَ جَمْعًا وَلَا  
يُسْأَلُ عَنْ ذُنُوبِهِمُ الْمُجْرِمُونَ ﴿٧٨﴾

*Akasema: “Hakika nimepewa haya kwa sababu ya ilimu niliyo nayo”. Je, hakujua ya kwamba Mwenyezi Mungu amewaangamiza kabla yake watu waliokuwa wenye nguvu zaidi kuliko yeye na wenye mkusanyo mwingi zaidi (kuliko wake yeye)?” (28:78).*

Kwa kutakabari kwake huko, Qarun aliangamizwa kwa kudidimizwa ardhini yeye na nyumba yake.

فَخَسَفْنَا بِهِ وَبِدَارِهِ الْأَرْضَ فَمَا كَانَ لَهُ مِنْ فِئَةٍ يَنْصُرُونَهُ مِنْ دُونِ

اللَّهِ وَمَا كَانَ مِنَ الْمُنتَصِرِينَ ﴿٨١﴾

*“Basi tukamdidimiza yeye (Qarun) na nyumba yake ardhini, wala hapakuwa na kundi lolote la kumsaidia kinyume na Mwenyezi Mungu, wala hakuwa miongoni mwa walioweza kujisaidia” (28:81).*

### **Mafunzo:**

Yapo mafunzo mengi kutokana na maisha ya Qarun. Funzo la **kwanza** ni kuwa kama utajiri hautatumiwa vyema, waweza kuzaa maovu yafuatayo:

- (i) Humfanya mwenye mali kujisahau na kutakabari.
- (ii) Humfanya mwenye mali kuwasahau wenye shida na wahitaji. Hali hii huzaa jamii ya wenye mali ambao hula na kusaza wakati wengine hubaki ombaomba wasio na msaada wowote.

Funzo la **pili** linalolandana na maisha ya Qaruni ni kuwa mali, cheo na mamlaka ya mtu hayawezi kumsaidia chochote Mwenyezi Mungu anapopitisha hukumu yake. Qaruni alitamba kwa mali yake, lakini hukumu ya Allah(s.w) ilipofika alididimizwa yeye na mali yake ardhini.

### **Watu wa Mahandaki ya Moto.**

Katika Suratul Buruj, kumetajwa kisa cha makafiri waliowatesa wafuasi wa Mitume waliotangulia kabla ya Mtume Muhammad(s.a.w). Makafiri hao walichimba mahandaki na ndani yake wakawasha moto mkubwa kisha wakawa wanawatosa waumini humo mmoja baada ya mwingine. Dhun-Nuwas mmoja

wa waliokuwa wafalme wa Mayahudi; aliingia Najran akiwa na jeshi kubwa ili awalazimishe watu wa Najran wasifuata mafundisho ya Mitume. Watu wa Najran walipokataa kumfuata, alichimba handaki kubwa akawasha moto akawa anamtumbukiza Muumini mmoja baada ya mwingine huku yeye na watu wake wanachekelea. Habari hii inaelezwa katika Suratul-Buruj, kama ifuatavyo:

قَتِيلَ أَصْحَابِ الْأَخْذُودِ ﴿٤﴾ النَّارِ ذَاتِ الْوَقُودِ ﴿٥﴾ إِذْ هُمْ عَلَيْهَا قُعُودٌ ﴿٦﴾  
 وَهُمْ عَلَىٰ مَا يَفْعَلُونَ بِالْمُؤْمِنِينَ شُهُودٌ ﴿٧﴾ وَمَا نَقَمُوا مِنْهُمْ إِلَّا أَن  
 يُؤْمِنُوا بِاللَّهِ الْعَزِيزِ الْحَمِيدِ ﴿٨﴾ الَّذِي لَهُ مَلِكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ  
 وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ﴿٩﴾

“(Kuwa) wameangamizwa watu waliowaadhibu Waislamu katika mahandaki. Yenye moto wenye kuni (nyingi). Walipokuwa wamekaa hapo (Waliangamizwa makafiri hao pale wakati walipokuwa) wanatazama yale wanayowafanyia hao Waislamu (walipokuwa wakiwaadhibu). Nao hawajaona baya lolote kwao (Waislamu) ila kumuamini Mwenyezi Mungu Mwenye kushinda (na) Mwenye kusifiwa. Ambaye ni Mwenye Ufalme wa mbingu na ardhi; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuona kila kitu” (85:4-9).

Kisa hiki kimesimuliwa kiwape fundisho na kuwaliwaza waumini wa zama zote; kwamba taabu iwapatayo kutoka kwa makafiri imeanza kuwafikia ndugu zao waliotangulia. Aidha, kutokana na kisa hiki Waislamu wanapata funzo kuwa kubakia na Imani Thabiti na suala la kusimamisha Uislamu katika jamii, kwahitaji juhudi na subira kubwa sana.

Mwenyezi Mungu anawaliwaza Waislamu kuwa makafiri wanaowatesa na kuwaghasi Waislamu hivi leo, atawaadhibu na kuwatesa kweli kweli kama alivyowatesa As-habul- Khudud.



إِنَّ الَّذِينَ فَتَنُوا الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ ثُمَّ لَمْ يَتُوبُوا فَلَهُمْ عَذَابُ جَهَنَّمَ

وَلَهُمْ عَذَابُ الْحَرِيقِ ﴿١٥﴾

“*Hakika wale waliowaadhibu Waislamu wanaume na Waislamu wanawake, kisha wasitubie basi watapata adhabu ya Jahanamu na watapata adhabu ya kuungua (barabara)*” (85:10).

إِنَّ بَطْشَ رَبِّكَ لَشَدِيدٌ ﴿١٦﴾

“*Hakika kutesa kwa Mola wako ni kukali (sana)*” (85:12).

Lakini pamoja na kuliwazwa huko; Waislamu hawatakiwi walale usingizi wasubiri nusura ya Mwenyezi Mungu. Ni wajibu wao wajiandae kwa kila mbinu kupambana na vitimvi vya maadui zao.

وَأَعِدُّوا لَهُمْ مَا اسْتَطَعْتُمْ مِنْ قُوَّةٍ وَمِنْ رِبَاطِ الْخَيْلِ

تُرْهِبُونَ بِهِ عَدُوَّ اللَّهِ وَعَدُوَّكُمْ .....

“*Basi waandalieni (wawekeeni tayari) nguvu mziwezao (silaha), mafarasi yaliyofungwa tayari tayari ili kwazo muogopeshe maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui zenu .....*” (8:60).

## **Watu wa Mji Waliomuua Muislamu kwa Kuwa Amewasadikisha Wajumbe wa Allah(s.w).**

Katika Suratul Yassin Allah(s.w) anatufahamisha habari za wale watu wa mji mmoja ambao walikataa kwa takaburi yao kumuamini Allah(s.w) baada ya kufikiwa na Wajumbe wake waliowajia kwa dalili wazi wazi. Wajumbe hao wa Allah(s.w) waliwaambia watu wa mji huo:

.....يَعْلَمُ إِنَّا إِلَيْكُمْ لَمُرْسَلُونَ ﴿١١﴾

“..... *Kwa yakini sisi tumetumwa kwenu*” (36:16).

Watu wa mji huo walikadhibisha na kusema kama kawaida ya wakorofi wa enzi zote walivyosema:

..... مَا أَنْتُمْ إِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُنَا وَمَا أَنْزَلَ الرَّحْمَنُ مِنْ شَيْءٍ إِلَّا أَنْتُمْ إِلَّا

تَكْذِبُونَ ﴿١٥﴾

“.....Nyinyi si chochote ila ni watu kama sisi, wala (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa Rehema hakuteremsha chochote, nyinyi mnasema uwongo tu” (36:15).

Wajumbe wa Allah(s.w) bila ya kukata tamaa waliendelea kuwalingania na kuzidi kuwathibitishia kwa dalili wazi wazi kuwa wao ni wajumbe wa Allah(s.w). Waliwaambia:

..... رَبُّنَا يَعْلَمُ إِنَّا إِلَيْكُمْ لَمُرْسَلُونَ ﴿١٦﴾ وَمَا عَلَيْنَا إِلَّا الْبَلَاغُ الْمُبِينُ ﴿١٧﴾

“.....Mola wetu anajua bila shaka kuwa sisi tumetumwa kwenu. Wala hapana juu yetu ila kufikisha (ujumbe wetu) waziwazi” (36:16-17).

Pamoja na jitihada za Wajumbe hawa kuwalingania watu wa mji huo kwa dalili waziwazi, watu wa mji huo walizidi kutakabari na kuazimia kuwadhuru Wajumbe wa Allah. Walitoa onyo kali kwao na kusema:

..... إِنَّا تَطَيَّرْنَا بِكُمْ لَئِن لَّمْ تَنْتَهُوا لَنَرْجُمَنَّكُمْ وَلَيَمَسَّنَّكُم مِّنَّا عَذَابٌ

أَلِيمٌ ﴿١٨﴾

“.....Hakika sisi tumekorofika kwa ajili yenu. Kama hamtaacha (kusema haya mnayosema) tutakupigeni mawe na itakufikieni kutoka kwetu adhabu iumizayo” (36:18).

Hii ndio tabia ya makafiri wa zama zote. Mara zote huwaona watu wema wanaolingania kheri ili ipatikane furaha na amani katika jamii kuwa ndio wakorofi na wavuruga amani. Huwapachika

majina mbali mbali ili waonekane mbele za watu kuwa wao ni wakorofi kweli ili wapate kisingizio cha kuwasukumiza gerezani au kuwaondoa kabisa katika ardhi. Bali makafiri ndio wakorofi, waharibifu katika ardhi na wavurugaji wakubwa wa amani na furaha katika jamii. Tabia yao hii Allah(s.w) anaidhihirisha katika Qur'an:

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ لَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ قَالُوا إِنَّمَا نَحْنُ مُصْلِحُونَ ﴿١١﴾  
أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ الْمُفْسِدُونَ وَلَكِن لَّا يَشْعُرُونَ ﴿١٢﴾

“Na wanapoambiwa: “Msifanye uharibifu katika ardhi (katika jamii)”, Husema, “hakika sisi ni watengenezaji”. Hakika wao ndio waharibifu lakini hawatambui” (2:11-12).

Katika kisa hiki tunafahamishwa kuwa wale watu wakorofi wa mji ule waliokadhibisha ujumbe wa Allah(s.w) hawakuishia kutoa onyo kali tu bali walitekeleza kwa vitendo kwa mujibu wa habari ifuatayo:

وَجَاءَ مِنْ أَقْصَا الْمَدِينَةِ رَجُلٌ يَسْعَى قَالَ يَنْقُومُ اتَّبِعُوا الْمُرْسَلِينَ  
﴿٢٠﴾ اتَّبِعُوا مَنْ لَا يَسْأَلُكُمْ أَجْرًا وَهُمْ مُهْتَدُونَ ﴿٢١﴾

“Na akaja mtu mbio kutoka upande wa mbali wa mji, akasema (kwaambia watu wa mji ule), “Enyi watu wangu! Wafuateni wajumbe (hawa). Wafuateni hawa wanaokufundisheni bila ya kutaka ujira; na hali ya kuwa wenyewe wameongoka” (36:20-21).

Wakamuuliza, “Kwani wewe umewafuata?” Akawajibu:

وَمَا لِيَ لَا أَعْبُدُ الَّذِي فَطَرَنِي وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٢٢﴾ أَلَتَّخِذُ مِنْ  
دُونِهِ آلِهَةً إِنْ يُرِدْنِ الرَّحْمَنُ بِضُرٍّ لَّا تُغْنِي عَنِّي شَفَاعَتُهُمْ شَيْئًا وَلَا  
يُنقِذُونِ ﴿٢٣﴾ إِنْ أَرَادْتَ إِلَّا لُفِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٢٤﴾ إِنْ أَرَادْتَ إِلَّا آمَنَّا بِرَبِّكُمْ  
فَأَسْمِعُونِ ﴿٢٥﴾

*“Kwanini nisimuabudu yule aliyeniumba (na kukuumbeni nyinyi pia) na kwake mtarejeshwa? Je! Nishike miungu wengine badala yake? Na kama Mwenyezi Mungu akipenda kunidhuru, uombezi wao hautanifaa kitu, wala hawataniokoa! Nikifanya hivyo nitakuwamo katika upotofu ulio dhahiri. Bila shaka mimi nimemuamini Mola wenu, basi nisikilizeni” (36:22-25).*

Badala ya kuuzingatia ushauri wake mzuri na kuufuata, waliamua kumuua Muislamu yule. Mfano huu wa kudhulumiwa Waislamu kwa ajili tu ya kulingania waziwazi ujumbe wa Allah(s.w) na Mitume wake, haukuishia kwa watu wa mji ule tu, bali hiki ni kitendo kinachoendelea mpaka hivi leo. Katika mwaka 1993, tumeshuhudia mauaji ya dhuluma ya aina hii huko Misri, Algeria na Tunisia, kwa kisingizio cha “Waislamu wenye siasa kali”/Waislamu wenye imani kali”.

Kwa upande mmoja, Mola wetu anatupa moyo na motisha kwa ahadi yake ya neema zisizo na kifani za huko peponi, ili tusimame imara na kuwa wagumu dhidi ya makafiri mpaka Dola ya Allah (Dini ya Allah) isimame katika jamii na iwe juu ya Dola ya makafiri japo watachukia mwisho wa kuchukia. Kama mfano kwetu, mara tu ya kuuliwa yule Mujahidina, alikaribishwa Peponi na Mola wake:

قِيلَ ادْخُلِ الْجَنَّةَ قَالَ يَا لَيْتَ قَوْمِي يَعْلَمُونَ ﴿٢٦﴾ بِمَا غَفَرَ لِي رَبِّي

وَجَعَلَنِي مِنَ الْمُكْرَمِينَ ﴿٢٧﴾

*“Akaambiwa: “Ingia Peponi. Akasema, laiti watu wangu wangelijua haya, wangelijua jinsi Mola wangu alivyonisamehe na kunijaalia miongoni mwa waliohishimiwa” (36:26-27).*

Kamwe Muislamu wa kweli hapaswi kuwaogopa makafiri na wapinzani wote wa usimamishaji wa Uislamu katika jamii, kwani hakuna kifo cha heshima na taadhima mbele ya Allah(s.w) kuliko kifo cha Shahidi kiasi kwamba Allah(s.w) anatumataza kumuita mfu aliyekufa shahidi.

وَلَا تَقُولُوا لِمَن يُقْتَلُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَمْوَاتٌ بَلْ أَحْيَاءٌ وَلَٰكِن لَّا تَشْعُرُونَ ﴿١٥٤﴾

*“Wala msiwaite wale waliouawa katika njia ya Mwenyezi Mungu wafu, bali wa hai, lakini nyinyi hamtambui” (2:154).*

Kwa upande mwingine, tunafahamishwa wazi wazi, kwa mifano mingi kuwa hatima ya makafiri na wapinzani wa Uislamu ni kuangamia hapa duniani na huko akhera. Hapa duniani watadhibitiwa au kufutiliwa mbali kabisa na Allah(s.w) kwa urahisi sana. Hahitajii Allah(s.w) kuandaa jeshi kubwa lenye silaha kali katika kuwadhibiti makafiri. Katika kisa hiki, Allah(s.w) anatufahamisha:

﴿ وَمَا أَنْزَلْنَا عَلَىٰ قَوْمِهِ مِن بَعْدِهِ مِن جُنْدٍ مِّنَ السَّمَاءِ وَمَا كُنَّا مُنْزِلِينَ ﴾

﴿ ٢٨ ﴾ إِنْ كَانَتْ إِلَّا صَيْحَةً وَاحِدَةً فَإِذَا هُمْ خَامِدُونَ ﴿٢٩﴾

*“Na hatukuwateremshia watu wake jeshi kutoka mbinguni (kuwaangamiza) baada yake, wala hatukuwa wateremshao (majeshi kutoka mbinguni). Basi hakukuwa (kuangamizwa kwao) ila kwa ukulele mmoja tu, na mara wakawa waliozimika” (36:28-29).*

Kutokana na kisa hiki na visa vingine vilivyohadithiwa katika Qur’an tunajifunza kuwa daima katika kipindi chote cha historia wanaadamu wamekuwa wakigawanyika katika makundi mawili makubwa baada ya kufikiwa na Ujumbe wa Allah(s.w). Kundi la wenye kuwaamini Mitume na kufuata ujumbe wao na kundi la makafiri waliowakataa Mitume na kuukanusha ujumbe wao.

Kundi la waumini huanza na watu wachache na wanyonge, wenye kukandamizwa na makafiri, lakini kila baada ya siku, kulingana na juhudi zao za kuulingania Uislamu na kujitoa muhanga kwao kwa mali na nafsi zao katika kuusimamisha, waliongezeka na kuwa nguvu dhidi ya maadui zao na hatimaye walishinda na kuusimamisha Uislamu katika jamii.

Kundi la makafiri daima huanza na watu wengi wenye mamlaka na hadhi katika jamii, lakini kila baada ya siku, kulingana na ukweli unaodhihirishwa na Uislamu, idadi yao ilizidi kupungua na vitimbwi vyao kubainika na kudhibitiwa na Waislamu hatimaye kuporomoka na kuwa chini ya himaya ya Uislamu na kutoa jizya. Pale ambapo makafiri walipindukia mipaka na kutakabari katika ardhi kiasi cha kutowaruhusu kabisa waumini kuligania Dini ya Allah(s.w) na kuongeza idadi yao, kama walivyokuwa makafiri wa wakati wa Nabii Nuhu, Lut, Salihi, Shuayb(a.s), n.k. Allah(s.w) aliwdhibiti mwenyewe na kuwafuta katika ardhi.

Hivyo, mafunzo haya tunayoyapata kutokana na historia ya mwanaadamu kama inavyodhihirishwa Qur'an, Waislamu wa kweli hatunabudi kufuata vilivyo ujumbe wa Mitume na kufuata nyayo zao na za wale watu wema waliokuwa pamoja nao, katika kuilingania na kuipigania Dini ya Allah(s.w) kwa mali zao na nafsi zao. Kamwe hatutapokelewa mbele ya Allah(s.w) kwa kuwaamini tu Mitume bila ya kufuata nyayo zao na wale watu wema walioamini pamoja nao katika kupigania Dini ya Allah(s.w). Mola wetu anatumkumbusha hili katika Qur'an:

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَأْتِكُمْ مَثَلُ الَّذِينَ خَلَوْا مِنْ قَبْلِكُمْ  
 مَسَّتْهُمُ الْبَأْسَاءُ وَالضَّرَّاءُ وَزُلْزِلُوا حَتَّى يَقُولَ الرَّسُولُ وَالَّذِينَ آمَنُوا  
 مَعَهُ مَتَى نَصْرُ اللَّهِ أَلاَ إِنَّا نَصْرُ اللَّهِ قَرِيبٌ

*“Mnadhani kuwa mtaingia Peponi, na hali hamjajiwa na mfano wa (yale yaliyowajia) wale waliopita kabla yenu? Yaliwapata mashaka na madhara na wakatetemeshwa sana hata Mitume na walioamini pamoja nao wakasema: “Nusura ya Allah itafika lini?” jueni kuwa nusura ya Allah iko karibu” (2:214).*

Hatunabudi kufahamu wazi kuwa, tukifuata vilivyo nyayo za Mitume na wale walioamini pamoja nao katika kumtii Allah(s.w) na kupigania kusimama kwa Uislamu katika jamii kwa mali zetu na

nafsi zetu ushindi ni wetu na makafiri kamwe hawataweza kuufuta Uislamu katika jamii. Hebu tuijee Qur'an kwa makini katika aya zifuatazo:

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظَاهِرَهُد عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ  
 وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٩﴾ يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا هَلْ أَذَلُّكُمْ عَلَىٰ تَجْرَةٍ  
 تُنَجِّيْكُمْ مِّنْ عَذَابِ أَلِيمٍ ﴿١٠﴾ تُوْمِنُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَتُجَاهِدُونَ  
 فِي سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنفُسِكُمْ ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ  
 ﴿١١﴾ يَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَيُدْخِلْكُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا  
 الْأَنْهَارُ وَمَسَاكِينٌ طَيِّبَةٌ فِي جَنَّاتٍ عَدْنٍ ذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١٢﴾  
 وَأُخْرَىٰ تُحِبُّونَهَا نَصْرٌ مِّنَ اللَّهِ وَفَتْحٌ قَرِيبٌ وَبَشِيرٌ لِّلْمُؤْمِنِينَ ﴿١٣﴾

“Yeye ndiye Aliyemtuma (Aliyemleta) Mtume Wake (Nabii Muhammad) kwa uwongofu na kwa Dini ya haki ili kuifanya ishinde Dini zote, ijapokuwa washirikina watachukiwa”.

Enyi Mlioamini! “Je! Nikujulisheni biashara itakayokuo keni na adhabu iumizayo?”. (Basi biashara yenyewe ni hii): Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na piganieni Dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zenu na nafsi zenu, haya ni bora kwenu; ikiwa mnajua (kuwa ni bora, basi fanyeni)”. (Mkifanya haya) Atakusameheni dhambi zenu na atakuingizeni katika Mabustani yapitayo mito mbele yake na (Atakupeni) maskani mazuri mazuri katika Bustani za milele: huku ndiko kufuzu kukubwa”. Na (Atakupeni) kingine mnachokipenda: nayo ni nusura itokayo kwa Mwenyezi Mungu na ushindi ulio karibu! Na wapashe habari njema Waislamu” (61:9-13).

## Zoezi la 2

1. Kwa kurejea Qur'an ainisha asili ya mwanaadamu na Hadhi yake hapa ulimwenguni.
2. Iblis ni nani na ni upi uhusiano wake na mwanaadamu?
3. Nini tofauti ya ukosaji wa Adam(a.s) na Hawwah na ule wa Iblis ?
4. (a) Mwanaadamu hpa ulimwenguni amekusudiwa kuwa Khalifa wa Allah(s.w), lakini si kila mtu atakuwa Khalifa. Fafanua.  
(b) Bainisha nyenzo kuu itakayo muwezesha binaadamu kuwa Khalifa wa Allah(s.w).
5. Kwa kurejea Historia ya Adam(a.s) hakuna dhambi ya asili kama wanavyodai wakristo. Thibitisha kauli hii.
6. Adam(a.s) na mkewe kutolewa peponi baada ya kulaghaiwa na Iblis inatupa fundisho gani?
7. Toa mafunzo matano ya msingi yatokanayo na Historia ya Nabii Adam(a.s).
8. Kwa kurejea Hadith ya Mtume(s.a.w) bainisha asili ya majina ya masanamu matano waliyokuwa wakiyaabudu watu wa Nuhu(a.s)
9. Mitume wote katika kuwalingania watu wao walifanya matano yafuatayo:  
(a) \_\_\_\_\_ (b) \_\_\_\_\_ (c) \_\_\_\_\_ (d) \_\_\_\_\_  
(e) \_\_\_\_\_
10. Takriban Makafiri wa zama zote katika kuwakadhibisha mitume wao walitoa hoja zifuatazo:  
(a) \_\_\_\_\_ (b) \_\_\_\_\_ (c) \_\_\_\_\_ (d) \_\_\_\_\_ (e) \_\_\_\_\_
11. Ainisha mbunu tano alizozitumia Nabii Nuhu(a.s) katika kulingania watu wake.



12. Tofautisha kulingania kwa Nuhu(a.s) na kule kwa Yunusu(a.s)
13. Ainisha mafunzo matano yatokanayo na Historia ya Nabii Nuhu(a.s)
14. Ambapo Salih(a.s) alitumwa kwa Taifa la \_\_\_\_\_  
Hud(a.s) alitumwa kwa akina \_\_\_\_\_
15. Bainisha majeshi ya Allah(s.w) yaliyotumika kuwaangamiza makafiri wa taifa la akina 'Ad na Thamud.
16. Toa mafunzo matano ya ujumla yatokanayo na Historia ya Nabii Hud na Salih(a.s).
17. Kumbukeni habari hii: Mola wake alipomwambia:  
"Nyenyekea", akanena: "Nimenyenyekea kwa Mola wa walimwengu(wote)." (2:131) kwa Nabi Ibrahim(a.s) amefanywa kiigizo kwa waislamu. Toa hoja tano.
18. Bainisha mbinu tano alizotumia Nabi Ibrahim(a.s) katika kuwelingania watu wake.
19. Na(kumbukeni khabari hii) Mola wake alipomfanyia mtihani (Nabii Ibrahim) kwa amri nyingi; naye akazitumiza. Akamwambia: "Hakika mimi nitakufanya kiongozi wa watu (wote)." (2:124) Bainisha mitihani mitano(5) aliyotakihiniwa Nabi Ibrahim(a.s) na namna alivyoishinda.
20. Toa mafunzo matano (5) yatokanayo na Historia ya Nabi Ibrahim(a.s)
21. Maovu yaliyowapelekea kuangamizwa watu wa Lut(a.s) ni haya manne yafuatayo:  
(a) \_\_\_\_\_ (b) \_\_\_\_\_ (c) \_\_\_\_\_ (d) \_\_\_\_\_
22. Na majeshi ya mbinguni na ardhi ni Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu, mwenye hikima  
Bainisha majeshi ya Allah(s.w) yaliyotumika kuwaangamiza watu waovu wafuatao:  
(a) Watu wa miji ya Sodom na Gomora wakati wa Nabii Lut(a.s).

- (b) Makafiri taifa la 'Ad.
  - (c) Makafiri taifa la Thamud.
  - (d) Makafiri wa Madian katika kipindi cha Nabii Shu'ayb(a.s).
  - (e) Firaun na majeshi yake.
23. Ainisha mafunzo matano yatokanayo na Histoira ya Nabii Ayyuub(a.s).
  24. Bainisha maovu manne(4) yaliyopelekea kuangamizwa kwa watu wa Nabii Shu'ayb(a.s).
  25. Kwa yakinikatika (kisa cha) Yusufu na ndugu zake yako mazingatio mengi kwa wanaouliza (mambo wapate kujua)(12:7).
  26. Nabii Musa(a.s)kuandaliwa tangu utotoni kuwakomboa Bani Israil kutokana na mateso ya ya Firaun inatupa funzo moja kubwa Bainisha funzo hili.
  27. Baina mafunzo kumi (10) yatokanayo na Historia ya Nabii Musa(a.s)katika mchakato wa kuwakomboa Bani Israil kutokana na udhalimu wa Firaun.
  28. (a) Bani Israil pamoja na kuwa taifa teule lililo tukuzwa na Allah(s.w)walikuja laaniwa kwa sababu ya kubonea kwao katika kufanya makosa kumi(10) tu.  
(b)Ummah wa Waislamu hivi leo ulio kabidhiwa cheo cha kuwa ummah bora(3:110),unajifunza nini kutokana na kulaaniwa Mayahudi?
  29. Toa mafunzo matano ya ujumla yatokanayo na Historia ya Nabii Daud na Sulaiman(a.s).
  30. Kuna mengi ya kujifunza kutokana na Historia ya Nabii Zakaria na Yahya (a.s). Toa mafunzo matano.
  31. Mkewe Imraan aliweka nadhiri ya kumuweka wakafu mtoto atakaye mzaa. Nini maana ya wakfu kwa mnasaba ya nadhiri hii?
  - 32.(a) Nabii Isa(a.s) kuitwa kwa ubnini wa mama yake kunatupa fundisho gani ?

(b) Toa mafunzo matano yatokanayo na historia ya Nabii Isa(a.s)

33. (a) Toa maelezo mafupi juu ya watu wema wafuatao:

- (i) As-habul-kahf.
- (ii) Luqman
- (iii) Dhurqarnain
- (iv) Hidhri

(b) Tunajifunza nini juu ya Historia ya watu hao wema. Toa mafunzo matatu(3) kwa ila mmoja

34. (a) Toa maelezo mafupi juu ya watu waovu wafuatao:

- (i) As-habul-Khuldud
- (ii) Qarun
- (iii) Hamana
- (iv) Firaun

(b) Toa funzo moja kubwa kutokana na historia ya watu hao waovu waliotajwa hapo juu(a).



## *Sura ya Tatu*

### **HISTORIA YA UISLAMU WAKATI WA MUHAMMAD(S.A.W)**

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظَاهِرَهُ

عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٣٣﴾

*“Yeye ndiye aliyemleta Mtume wake kwa uongofu na Dini ya haki ili aijaalie kushinda Dini zote ijapokuwa washirikina watachukia.” (9:33, 61:9)*

Aya hii inatufahamisha kuwa lengo makhsusi la kuletwa Mtume(s.a.w) ni kusimamisha Dola ya Kiislamu kama alivyofanya. Nasi Waumini tunalazimika kufuata nyayo za Mtume(s.a.w) na kuhakikisha kuwa Uislamu unasimama katika jamii zetu kama inavyosisitizwa katika Qur-an:

لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُوا اللَّهَ وَالْيَوْمَ

الْآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ كَثِيرًا ﴿٣٣﴾

*Bila shaka mnao mfano mwema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwa mwenye kumuogopa Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, na kumtaja Mwenyezi Mungu sana” (33:21)*

Kumuigiza Mtume(s.a.w) ni kufuata Sunnah ya Mtume(s.a.w), kwa kutekeleza yale aliyotumria na kuacha aliyotukataza na kuiga tabia yake adhimu katika kuendesha maisha yetu ya kila siku ya kibinafsi, kifamilia na ya kijamii. Sunnah kuu ni ile ya kumuigiza Mtume(s.a.w) katika kuliendea lengo Makhsus alioletwa kwalo la kuusimamisha Uislamu na kuufanya utawale maisha yote ya jamii. Hapa tutadokeza hatua muhimu alizopitia Mtume(s.a.w) na wale walioamini pamoja naye mpaka kufikia kilele cha kuufanya Uislamu kuwa juu ya Dini zote (mifumo yote ya maisha).

## Zama za Jahiliyyah

Zama za Jahiliyyah ni zile zama ambazo watu walikuwa wakiendesha maisha yao ya kibinafsi na kijamii kwa kufuata matashi yao kinyume na mwongozo wa Allah(s.w) na mitume wake.

Wakati Mtume(s.a.w) anazaliwa katika karne ya Sita (570 A.D) dunia ilikuwa katika giza totoro la ujahili. Wakazi wa Bara Arab, katika kipindi hicho walikuwa chini sana katika maadili. Ubabe, unyang'anyi na uporaji mali ya misafara ya biashara yalionekana matendo ya kishujaa na ya kujivunia. Wanyonge hawakuwa na haki, wanawake walinyanyaswa na kudhalilishwa hadi kufikia watoto wa kike kuzikwa wangali hai na wanawake kurithiwa kwa nguvu kama ilivyorithiwa mali.

Kwa muhtasari hali ya Bara Arab wakati huo ilikuwa kama alivyoeleza Jaffari bin Abu Twalib mbele ya Mfalme Najash wa Uhabesh:

*“Ewe Mfalme, sisi tulikuwa waovu na majahili, tukiabudia masanamu na kula nyamafu hata mizoga ya wanyama waliokufa wenyewe. Tulifanya kila aina ya matendo machafu na ya aibu. Hatukuwa wenye kuwajibika kwa jirani na jamaa zetu. Wenye nguvu miongoni mwetu waliwakandamiza wanyonge. Kisha Allah akamleta Mtume miongoni mwetu ambaye tulimfahamu vema kwa nasaba yake, utukufu wake na uzuri wa tabia yake adhimu. Alituita tumuabudu Mungu mmoja tu na akatukataza kuabudia masanamu na mawe. Alitufundisha kusema ukweli kutunza amana, kuwaangalia ndugu na jamaa na kuwafanyia wema na kuacha maovu. Alituamrisha kusimamisha swala na kutoa Zakat. Alituamrisha kujiepusha na maovu na kujiepusha na umwagaji damu. Alitukataza zinaa, kusema uwongo, kula mali ya yatima na kuwasingizia uovu wanawake watwaharifu. Alitufundisha Qur-an...”*<sup>4</sup> (A Guillaume – The life of Muhammad).

Hali hii ya ujahili haikutawala Bara Arab peke yake, bali katika karne hii ya 6 A.D ulimwengu wote, Mashariki na Magharibi, ulizama katika giza totoro la uovu na ujahili. Ulimwengu katika zama hizo, wanyonge na watu wa chini walikandamizwa na kudhulumiwa pasina chembe ya huruma na wenye uwezo na watukufu miongoni mwao.

Katika kipindi hicho, hata wale waliodai kufuata mafundisho ya Mitume wa Mwenyezi Mungu, Mayahudi na Wakristo, walikuwa katika giza hilo hilo la uovu na ujahili. Mayahudi waliacha mafundisho ya Mtume wao na wakaamua kuishi kulingana na matamania ya nafsi zao. Walipotokea Mitume waliwafanyia maovu mengi kama ilivyobainishwa katika Qur-an. Wakristo nao waliacha mafundisho sahihi ya Nabii Isa(a.s) badala yake wakafuata ushirikina wa Warumi. Walileta uzushi mwingi juu ya Dini ya Allah(s.w) kama tunavyojifunza katika Qur-an:

وَقَالَتِ الْيَهُودُ عُزَيْرٌ ابْنُ اللَّهِ وَقَالَتِ النَّصْرَى الْمَسِيحُ ابْنُ اللَّهِ ذَلِكَ قَوْلُهُمْ بِأَفْوَاهِهِمْ يُضَاهِئُونَ قَوْلَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَبْلُ قَتَلْتَهُمُ اللَّهُ أَنَّى يُؤْفَكُونَ ﴿٣٠﴾

*“Na Mayahudi wanasema: ‘Uzeiri ni Mwana wa Mwenyezi Mungu’ na Wakristo wanasema; ‘Masihi ni Mwana wa Mwenyezi Mungu’; haya ndiyo wayasemayo kwa vinywa vyao. Wanayaiga maneno ya wale waliokufuru kabla yao, Mwenyezi Mungu awaangamize. Wanageuzwa namna gani hawa! (9:30)*

اتَّخَذُوا أَحْبَابَهُمْ وَرُهْبَانَهُمْ أَرْبَابًا مِنْ دُونِ اللَّهِ وَالْمَسِيحَ ابْنَ مَرْيَمَ وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا إِلَهًا وَاحِدًا لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ سُبْحَانَهُ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٣١﴾

*Wamewafanya Wanavyuoni wao na Watawa wao kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu, na wamemfanya Masihi Mwana wa Maryamu (pia Mungu) hali hawakuamrisha isipokuwa kumuabudu Mungu mmoja, hakuna anayestahiki kuabudiwa ila Yeye. Ametakasika na yale wanayomshirikisha nayo.” (9:31).*

﴿ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنَّ كَثِيرًا مِّنَ الْأَحْبَارِ وَالرُّهْبَانِ لَيَأْكُلُونَ أَمْوَالَ

النَّاسِ بِالْبَاطِلِ وَيَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ.....

*“Enyi Mlioamini! Wengi katika Makasisi (Wanavyuoni wa Mayahudi na wakristo) na Watawa (wao) wanakula mali za watu kwa batili na kuwazuilia njia ya Mwenyezi Mungu.....” (9:34)*

Katika kipindi hicho cha historia utawala wa Kikristo Ulaya Magharibi uliwakandamiza na kuwanyonya wanyonge kama utawala wa kishirikina ulivyokuwa ukifanya huko Mashariki ya Kati na Mashariki ya mbali. Katika kipindi hiki wanasayansi walioibuka na ugunduzi ulio kinyume na maelezo ya Wakuu wa Kanisa walisulubiwa na kuuliwa kinyama miongoni mwao ni mwanasayansi maarufu, Galileo.

## **Kuandaliwa Mtume(s.a.w)**

Mitume huzaliwa Mitume. Mitume wa Allah wamekusudiwa kuwa walimu na viigizo katika jamii zao. Hivyo Allah(s.w) Mjuzi Mwenye Hekima, aliwaandaa kuanzia mbali kabisa, ili kuwawezesha kufikia lengo kuu lililo kusudiwa na ili kuifanya kila hatua ya maisha yao iwe ni funzo kwa Umma zao na Umma zilizofuatia.

Tukirejea historia, tunaona kuwa Mtume Muhammad(s.a.w) alipata maandalizi ya aina mbili, Maandalizi ya Ki-il-hamu na Maandalizi ya kufunzwa na kuelekezwa moja kwa moja.

## **Maandalizi ya Ki-il-hamu**

Maandalizi ya Ki-il-hamu ni maandalizi yaliyompitia Mtume (s.a.w) katika kipindi cha miaka 40 kabla ya kupewa Utume rasmi. Katika maandalizi haya hapana maagizo rasmi yanayotolewa bali tunajifunza kutokana na matukio na mazingira kuwa palikuwa na

mpango maalum uliopangwa kumuaanda Mtume(s.a.w). Ili tuone maandalizi haya hebu tuzingatie matukio machache katika maisha ya Muhammad(s.a.w) kabla ya kupewa Utume rasmi ikiwa ni pamoja na:

- (i) Kuzaliwa Makka katika kabila tukufu la Quraish.
- (ii) Kupewa jina la Muhammad.
- (iii) Malezi bora aliyoyapata.
- (iv) Tabia njema isiyo na mfano wake.
- (v) Ndoa yake na Bibi Khadija.
- (vi) Kuchukua maovu na kujitenga pangoni.

### **(i) Kuzaliwa Makka katika kabila la Quraish**

Mtume(s.a.w) kuzaliwa Makkah katika kabila tukufu la Quraish, chini ya ulezi wa Babu yake Abdul-Muttalib, aliyekuwa kiongozi wa Maquraish, ni kielelezo kuwa alistahiki kuchaguliwa kuwa kiongozi wa watu wake. Kabila la Quraish ni katika kizazi cha Nabii Ibrahim(a.s) kupitia kwa Ismail(a.s). Mtume(s.a.w) kuwa Mtume na kiongozi wa Dola ya Kiislamu ni jibu la dua ya Nabii Ibrahimu baada ya kukamilisha kazi ya kujenga upya Ka'abah:

وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَاهِيمُ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ وَإِسْمَاعِيلُ رَبَّنَا تَقَبَّلْ  
مِنَّا إِنَّا نَكْتُبُكَ أَنْتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿١٢٧﴾

*Na (kumbukeni khabari hii pia) Ibrahimu alipoinua kuta za nyumba (hii ya Al-Kaaba) na Ismail (pia); (wakaomba wakasema) “Ee Mola wetu! Tutakabalie (amali yetu hii ya kujenga huu msikiti). Hakika wewe ndiye Mwenye kusikia, na Mwenye kujua.” (2:127)*



رَبَّنَا وَأَبْعَثْ فِيهِمْ رَسُولًا مِّنْهُمْ يَتْلُوا عَلَيْهِمْ آيَاتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ  
وَالْحِكْمَةَ وَيُزَكِّيهِمْ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٢٩﴾

*“Ee, Mola wetu! Waletee Mtume anayetokana na wao, awesomee Aya Zako, na kuwafundisha Kitabu (chako) na hikima na awafundishe kujitakasa (na kila mabaya). Hakika Wewe ndiye Mwenye nguvu, na ndiye Mwenye hikima. (2:129)*

## (ii) Kupewa jina la Muhammad(s.a.w)

Kuzaliwa kwa Mtume(s.a.w) na kupewa jina la Muhammad na Babu yake, lililo na maana sawa na lile la Ahmad alilooteshwa mama yake ni jambo jingine linalothibitisha maandalizi haya. Jina la Ahmad lenye maana ya “mwenyekushukuriwa” lilitabiriwa katika Taurat na Injili kama tunavyojifunza katika Qur-an:

وَإِذْ قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ يَدَّبَّيْنَ إِسْرَائِيلَ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ  
إِلَيْكُمْ مُّصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيَّ مِنَ التَّوْرَةِ وَمُبَشِّرًا بِرَسُولٍ يَأْتِي مِنْ  
بَعْدِي اسْمُهُ أَحْمَدٌ فَلَمَّا جَاءَهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ قَالُوا هَذَا سِحْرٌ مُّبِينٌ

*“Na (wakumbushe) aliposema Issa bin Maryamu, ‘Enyi wana wa Israil! Mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, nisadikishaye yaliyokuwa kabla yangu katika Taurat, na kutoa habari njema ya Mtume atakayekuja nyuma yangu ambaye jina lake litakuwa Ahmad. Lakini alipowajia kwa hoja zilizowazi walisema, ‘huu ni udanganyifu uliodhahiri’. (61:6).*

## (iii) Malezi bora aliyoyapata

Pamoja na kuwa Muhammad(s.a.w) alizaliwa akiwa yatima, alipata malezi bora na ya huruma kupitia kwa mama yake wa kunyonya- Bibi Halima bint Abi-Dhuaby. Mama huyu wa kabila la Bani Khawaizin ambalo lina sifa ya usafi na lugha fasaha ya

Kiarabu alitokea Taifu mji wenye hali nzuri ya hewa kwa kulelea watoto. Mtume alipata bahati ya kukaa miaka mine badala ya miwili kutokana na magonjwa ya mlipuko yaliyojitokeza Makkah jambo ambalo lilimuwezesha kuzungumza kiarabu kwa ufasaha zaidi kuliko watu wengine wa Makkah. Mama yake Amina bint Wahhab alimlea mpaka alipofikisha umri wa miaka 6 akafariki. Babu yake Abdul-Muttalib aliendelea kumlea na alipofikisha umri wa miaka 8 akafariki. Kisha alilelewa na ‘Ami yake, Abu - Talib ambaye aliendelea kuwa naye mpaka alipopewa utume na alikuwa akimlinda mpaka alipofariki, Mtume(s.a.w) akiwa na miaka kumi ya utume. Hii haikutokea tu kwa bahati nasibu, bali tunafahamishwa katika Qur-an kuwa ni maandalizi maalum aliyoyapanga Allah(s.w).

أَلَمْ يَجِدْكَ يَتِيمًا فَآوَىٰ ۝٦

*Je! Hakukukuta yatima akakupa makazi (mazuri ya kukaa)? (93:6).*

**(iv) Tabia yake njema isiyo na mfano wake**

Tabia nzuri ya Mtume(s.a.w) haikuishia utotoni mwake tu bali iliendelea kwa umri wake wote. Tunajifunza katika historia kuwa hata alipokuwa mtoto hakuwahi kufanya vitendo vya kipuuzi vya kitoto na alikuwa ni mwenye haya sana. Wakati fulani kuta za Ka’abah zilifanyiwa ukarabati. Wavulana wadogo wadogo nao wakashiriki katika kazi ya ukarabati. Wavulana hawa walizitoa nguo zao za kiunoni na kuziweka mabegani ili kubebea mawe. Abu Talib alimshauri Mtume(s.a.w) naye ajiunge na watoto wenziwe. Mtume(s.a.w) alikubaliana na ushauri wa Ami yake, lakini alikuwa na haya sana hata katika umri ule wa utotoni. Hivyo, alipojaribu naye kuvua nguo yake na kubaki uchi, alishikwa na bumbuazi (butwaa) na kuanguka chini.

Mtume(s.a.w) tangu utotoni mwake aliepukana na tabia zote chafu zenye kuchukiza watu kwa ujumla. Pia aliepushwa na matendo yote maovu yenye kumchukiza Allah(s.w) ambayo

yalionekana mazuri mbele za watu wa jamii yake. Kwa mfano katika umri wa ujana wake aliazimia mara mbili kuhudhuria mikeshwa ya ngoma za harusi za rafiki zake wawili lakini Allah(s.w) alimwepusha na mikeshwa hiyo kwa kumpa usingizi mzito mpaka asubuhi kwa safari zote mbili.

Tangu utotoni mwake Mtume(s.a.w) alichukia sana lbada ya masanamu. Hakupata kuhudhuria hata mara moja ibada za masanamu wala hakupata kula kilichoandaliwa kwa ajili ya masanamu. Moyo wake pia ulichukia maovu yote mengine yaliyofanywa matendo ya kawaida na watu wa jamii yake kama vile ulevi, uzinifu, uchezaji kamari, ulaji riba, udhalimu, ulaji wa vyakula haramu, n.k.

Tangu utotoni mwake, Muhammad(s.a.w) alisifika kwa kila sifa nzuri zilizobainishwa katika Qur'an. Bibi 'Aisha(r.a) alipoulizwa juu ya tabia ya Mtume(s.a.w) alijibu kuwa tabia yake ni Qur'an. Yaani Mtume(s.a.w) amejipamba na vipengele vyote vya tabia njema vilivyobainsihwa katika Qur'an tangia utotoni mwake. Qur'an yenyewe katika miongoni mwa aya zake za mwanzo mwanzo kushuka, inamsifu Mtume(s.a.w) kwa tabia yake tukufu:

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقِي عَظِيمٍ ﴿٤﴾

*“Na bila shaka unatabia njema kabisa” (68:4)*

Aya hii haielezi kuwa tabia yake ilikuwa njema tu pale alipopata utume bali inaashiria kuwa tabia yake njema anayo tangu utotoni mwake. Muhammad(s.a.w) tangu utotoni mwake tumeona kuwa alikuwa mpole, mtulivu, mwenye huruma, mwenye haya na mwenye sifa zote nzuri zilizowapendeza watu na kuwavutia. Alikuwa mashuhuri Bara Arab nzima kwa ukweli na uaminifu wake. Alikuwa mkweli mno mpaka akaitwa, **“As-Sadiq”** – **“mkweli”** na alikuwa mwaminifu mno mpaka akapewa jina la **“Al-Amin”**. Muhammad(s.a.w) alikuwa haitwi ila kwa majina haya: **As-Sadiq Al-Amin**. Wakubwa na wadogo walimheshimu na walimpa amana zao kuwawekea hata baada ya kupewa Utume. Tabia yake njema

isiyo na mfano wake katika jamii yake ni uthibitisho kuwa Mtume(s.a.w) aliandaliwa ki-il-hamu kabla hajapewa utume.

Tabia yake njema isiyo na mfano wake kuanzia utotoni hadi utuuzima wake inaashiria wazi kuwa hakuwa zao la jamii yake, bali aliandaliwa na Mola wake awe vile ili awe kiigizo chema kwa watu wa Umma wake na walimwengu kwa ujumla.

### **(v) Ndoa yake na Bibi Khadija**

Umaarufu wa Muhammad(s.a.w) kutokana na tabia yake tukufu ulienea Bara Arab nzima. Bibi Khadijah, mwanamke mjane miongoni kwa matajiri wakubwa wa Makkah, alivutiwa na tabia ya Muhammad(s.a.w). Bibi Khadijah alimtaka Muhammad ampelekee bidhaa zake Yemen kwa ujira wa ngamia wawili. Muhammad(s.a.w) alikubali na alirejea na faida kubwa zaidi kuliko matazamio ya Bibi Khadijah. Bibi Khadijah alivutika kwa faida hiyo kubwa na ikambidi tena amuombe Muhammad(s.a.w) ampelekee bidhaa zake Sham(Syria)kwa malipo ya ngamia wanne. Katika msafara huu, Muhammad(s.a.w) alimletea Bibi Khadijah faida kubwa zaidi ya mategemeo yake. Khadijah alikuwa hajawahi kupata faida kubwa kiasi kile tangu aanze kufanya biashara katika misafara ya Sham. Pamoja na furaha ya kupata faida kubwa kiasi hicho, Bibi Khadijah alizidi kufurahi na kuvutiwa na Muhammad aliposikia sifa zake za ajabu kutokana na taarifa ya mtumishi wake Maisarah, waliyeongozana naye. Kutokana na mvuto ule Bibi Khadijah hakuweza kustahamili kukaa mbali na Muhammad(s.a.w). Hivyo alimtaka radhi Muhammad na kuomba amuo. Bibi Khadijah wakati huo alikuwa mjane mwenye umri wa miaka 40, aliyewahi kuolewa mara mbili na kujaaliwa kupata watoto watatu, wawili wanaume na mmoja mwanamke. Kabla ya hapo matajiri na machifu wengi wa Makkah walipeleka posa zao kwa Bibi Khadijah lakini aliwakatalia. Muhammad(s.a.w) akiwa na umri wa miaka 25, alikubali ombi la Bibi Khadijah baada ya kushauriana na ami yake, bila ya kujali tofauti kubwa ya umri iliyokuwepo.

Baada ya kuoana, Bibi Khadijah alimuingiza Muhammad kwa ukamilifu katika biashara, akiwa si mwajiriwa tena kama ilivyokuwa katika safari mbili za mwanzo, bali baba na kiongozi wa familia. Muhammad(s.a.w) alifika sehemu mbali mbali za Bara Arab kwa shughuli ya biashara ikiwa ni pamoja na Bahrain na Yemen. Muhammad(s.a.w), kwa kushauriana na mkewe, alitumia sehemu ya utajiri wao katika kuwakomboa watumwa na vijakazi waliokuwa wakifanyiwa ukatili na mabwana zao. Bibi Khadijah alimzawadia Mtume(s.a.w) mtumwa wake aliyeitwa Zaid bin Harith. Mtume(s.a.w) alimpa Zaid uhuru wake na kumfanya mtoto wake wa kupanga. Pia walitumia utajiri wao katika kuwasaidia maskini na kuwalipia madeni wale waliokuwa hawana uwezo wa kulipa madeni yao.

Mtume(s.a.w) na mkewe Khadijah waliishi maisha mazuri ya kifamilia yaliyokuwa mfano bora wa kuigwa. Upendo, huruma na wema wa Mtume(s.a.w) kwa kila mtu, licha kwa familia yake, unafahamika. Bibi Khadijah naye, kwa kumjua Mtume(s.a.w) kuwa ni mtu mtukufu hata kabla hajatangaziwa utume rasmi, alikuwa ni kiliwazo cha Mtume kabla na baada ya utume. Alimfariji na kumpa ushauri mzuri kwa kila gumu lililomfika Mtume(s.a.w) katika maisha yote walipokuwa pamoja. Katika watoto saba wa Mtume(s.a.w), watoto sita wamezaliwa na Khadijah nao ni: Qasim, Zaynab, Ruqyyah, Umm Kulthum, Fatimah na 'Abdullah. Watoto wote isipokuwa 'Abdullah, walizaliwa kabla ya utume. Wanawe wa kiume walifariki wakiwa bado watoto katika kipindi cha utume cha Makkah. Mtoto wa saba wa Mtume(s.a.w) ni Ibrahim aliyezaliwa na mjakazi wake, Mariam bint Kibtiyah katika kipindi cha utume cha Madinah. Naye alifariki angali mtoto.

Hivyo ndoa ya Mtume(s.a.w) na Bibi Khadijah haikutokea kwa bahati nasibu tu, bali ulikuwa mpango madhubuti wa Allah(s.w) ili kumtajirisha Mtume ili aweze kutoa mchango wake katika kuwahurumia na kuwasaidia madhaifu katika jamii yake, na ili awe mfano wa kuigwa na matajiri katika kutoa mali kwa ajili ya Allah katika kuwahurumia wanajamii. Qur-an inatufahamisha:

وَوَجَدَكَ عَابِلًا فَأَغْتَى ﴿٨﴾

*Na akakukuta fakiri akakutajirisha?” (93:8)*

Muhammad(s.a.w) alikuwa fakiri kabla ya kumuoa Khadija na kuwa tajiri mkubwa baada ya kumuoa Khadija

### **(vi) Kuchukia maovu na kujitenga pangoni**

Kuchukia maovu na kujitenga pangoni, ni tukio lingine linaloonesha kuandaliwa kwa Mtume(s.a.w) ki-il-hamu. Muhammad(s.a.w) tangu angali kijana alijihusisha mno na masuala ya kijamii na alikuwa akikereka sana kuona wanyonge wakidhulumiwa. Akiwa na umri wa miaka 20 alijiunga na Chama cha kuwatetea wanyonge dhidi ya Madhalimu. Mtume(s.a.w) alikosa usingizi kwa Sababu ya matatizo ya wengine na alikuwa na shauku kubwa ya kutafuta njia ya kuitoa jamii yake kwenye uovu na upotofu na kuipeleka kwenye wema na uongofu. Katika hali hiyo ilibidi ajitenge pangoni ili kutafuta msaada kwa Muumba Wake na aliupata kwa njia ya ndoto na baadaye kutumiwa Malaika Jibril. Allah(s.w) anamkumbusha Mtume wake juu ya maandalizi haya:

أَلَمْ تَشْرَحْ لَكَ صَدْرَكَ ﴿١﴾ وَوَضَعْنَا عَنكَ وِزْرَكَ ﴿٢﴾ الَّذِي أَنْقَضَ

ظَهْرَكَ ﴿٣﴾

*“Je! Hatukukupanulia kifua chako. Na tukakuondolea mzigo wako (mzito) uliovunja mgongo wako?” (94:1-3)*

وَوَجَدَكَ ضَالًّا فَهَدَىٰ ﴿٧﴾

*“Na akakukuta hujui kuongoza njia akakuongoza?” (93:7).*

Mzigo uliovunja mgongo wa Muhammad(s.a.w) kipindi kile si mwingine ila ile hali ya udhalimu na uovu iliyoshamiri katika jamii yake. Alikuwa na ari kubwa ya kuiondoa ile hali na kusimamisha uadilifu katika jamii lakini hakujua ni vipi atafanikisha hilo.

## **Mafunzo Yatokanayo na Maandalizi ya Ki-il-hamu**

Kutokana na matukio haya yanayoashiria kuandaliwa kwa Mtume(s.a.w) kabla ya kupewa Utume rasmi, tunajifunza kuwa katika kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii hatuna budi kuzingatia haya yafuatayo:

**Kwanza**, hatunabudi kuwaandaa watoto wetu kuwa Makhaliifa wa Allah(s.w) mapema kabla hata hawajazaliwa. Maandalizi haya yanawezekana pale wazazi wote wawili watakapokuwa na mtazamo huo wa Ukhalifa. Kisha baada ya watoto kuzaliwa tuwaadhinie na kuwakimbia,tuwafanyie aqika na kuwapa majina mazuri, tuwalee kwa mapenzi na huruma na kuwafunza tabia njema tangu wangali wachanga. Tuwasomeshe watoto wetu katika shule na vyuo vyenye kufuata mfumo wa elimu wa Kiislamu wenye lengo la kuandaa Makhaliifa wa Allah(s.w).

**Pili**, hatunabudi kuandaa Waalimu na Madaiyah watakao fundisha Uislamu na taaluma nyingine kwa lengo la kusimamisha Ukhalifa katika jamii.

**Tatu**, Mume na Mke (Baba na Mama) katika familia hawanabudi kushirikiana na kusaidiana kwa huruma na mapenzi ili kupata uwezo wa kuwalea watoto vilivyo na kupata wasaa wa kuyaendea masuala ya jamii.

**Nne**, Wanawake wa Kiislamu, hawanabudi kumfanya Bibi Khadijah, Mkewe Mtume(s.a.w), kuwa kiigizo chao katika kuwasaidia na kuwaliwaza waume zao hasa wanapokuwa katika harakati za kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii.

**Tano**, hatunabudi kuchukia maovu na dhulma wanazofanyiwa wanyonge na madhaifu wengine katika jamii na kuwa tayari kuondoa maovu na dhulma kwa mikono yetu pale tunapoweza. Na pale ambapo hatuna uwezo wa kutumia mikono, tutoe makemeo, vinginevyo tuingie “Pangoni Hira” tutafute msaada wa Allah(s.w).

**Sita**, hatunabudi kujipamba na tabia njema kwa kadiri iwezekanavyo. Mtu mwema hutambulika na kukubalika kwa watu kwa urahisi.

**Saba**, hatunabudi kuimarisha uchumi wetu kwani uchumi ndio nyenzo kuu ya kuusimamisha Uislamu katika jamii.

**Nane**, Katika kuchagua viongozi wa jamii hatunabudi kuzingatia historia zao pamoja na kuzingatia sifa nyingine za kiongozi bora.

## Maandalizi ya Kimafunzo

Ni maandalizi yaliyompitia Mtume(s.a.w) pale alipoanza kuletewa wahyi na Malaika Jibril(a.s). Maandalizi haya tunayapata katika Qur-an katika wahay wa mwanzo mwanzo kumshukia Mtume(s.a.w) katika Suratul ‘Alaq (96:1-5), Suratul-Muzzammil (73:1-10) na Suratul-Muddaththir (74:1-7).

### (i) Suratul- ‘Alaq (96:1-5)

أَفْرَأُ بِاسْمِ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ ① خَلَقَ الْإِنْسَانَ مِنْ عَلَقٍ ② أَفْرَأُ ③ وَرَبُّكَ  
الْأَكْرَمُ ④ الَّذِي عَلَّمَ بِالْقَلَمِ ⑤ عَلَّمَ الْإِنْسَانَ مَا لَمْ يَعْلَمْ ⑥

*“Soma kwa jina la Mola wako aliyeeumba Aliyemuumba mwanaadamu kwa ‘alaq. Soma na Mola wako ni karimu sana. Ambaye amefundisha kwa msaada wa kalamu. Amemfundisha mwanaadamu mambo aliyokuwa hayajui.” (96:1-5)*

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa Amri ya kwanza aliyopewa Mtume(s.a.w), na kwa hiyo waumini wote wa Ummah wake, ni kusoma au kutafuta elimu kwa ajili ya Allah(s.w). Kusoma kwa jina la Allah ni kusoma kwa lengo la kumuwezesha muumini kumjua na kumuabudu Mola wake vilivyo kisha kusimamisha Ukhalifa katika jamii.



Katika mazingira ya kupewa amri hii ya kwanza, pale pangoni Hira katika kilima cha Nuur (Jabal-Nuur), Mtume(s.a.w) alishinikizwa kusoma na Malaika Jibril kwa kumbana (kumkumbatia kwa nguvu) mara tatu pale alipojitetea kuwa hajui kusoma. Kubanwa huku kwa Mtume(s.a.w) na Malaika Jibril kunaashiria kuwa elimu kwa waumini ni amri ya kwanza inayotakiwa kutekelezwa kwa hima na kwa taklifu kubwa.

Hivyo Elimu ni amri ya kwanza inayotakiwa itekelezwe kwa juhudi na bidii zote. Ndiyo silaha kuu itakayowawezesha waumini kupata ushindi wa kusimamisha Uislamu katika jamii. Tukirejea nyuma katika historia, takrima ya kwanza aliyofanyiwa Adam(a.s) na Mola wake, ili kuandaliwa kuwa khalifa wa Allah(s.w) hapa duniani ni kufundishwa majina ya vitu vyote. Majina ya vitu vyote inaashiria fani zote za Elimu anazohitajia binaadamu ili aweze kuwa kiongozi wa dunia kwa niaba ya Allah(s.w). Pia tunajifunza kuwa chanzo cha fani zote za elimu ni Allah(s.w).

**(ii) Suratul-Muzzammil (73:1-10)**

يَتَأْتِيهَا الْمُرْمِلُ ﴿١﴾ فَمِ الْإِيلِ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٢﴾ نِصْفَهُ أَوْ انْقُصَ مِنْهُ قَلِيلًا ﴿٣﴾  
 أَوْ رَدَّ عَلَيْهِ وَرَتَّلِ الْقُرْآنَ تَرْتِيلًا ﴿٤﴾

*“Ewe uliyejifunika maguo simama usiku kucha (kuswali) ila muda mdogo (tu hivi). Nusu yake au upunguze kidogo au uzidishe na soma Qur-an vilivyo. (73:1-4)*

إِنَّا سَنُلْقِي عَلَيْكَ قَوْلًا ثَقِيلًا ﴿٥﴾ إِنَّ نَاشِئَةَ الْإِيلِ هِيَ أَشَدُّ وَطْأًا وَأَقْوَمُ قِيلًا ﴿٦﴾ إِنَّ لَكَ فِي النَّهَارِ سَبْحًا طَوِيلًا ﴿٧﴾ وَأَذْكُرِ اسْمَ رَبِّكَ وَتَبَتَّلْ إِلَيْهِ تَبْتِيلًا ﴿٨﴾

*Hakika sisi tutakuteremshia kauli nzito. Hakika kuamka usiku kunawafikiana zaidi na moyo na maneno yake yanatuwa zaidi. Hakika mchana unashughuli nyingi. Na litaje jina la Mola wako na ujitupe kwake kwa kweli. (73:5-8)*

رَبُّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ فَاتَّخِذْهُ وَكِيلًا ﴿١٠﴾ وَأَصْبِرْ عَلَىٰ مَا  
يَقُولُونَ وَأَهْجُرْهُمْ هَجْرًا جَمِيلًا ﴿١١﴾

*(Yeye Ndiye)Mola wa mashariki na magharib, Hapana Mola ila yeye, basi mfanye kuwa mlinzi wako. Na subiri juu ya hayo wayasemayo na uwaepuke mwepuko mwema.” (73:9-10)*

Aya ya kwanza ya sura hii inaashiria kuwa huu ni wahyi wa mwanzo mwanzo uliofuatia wahyi wa kwanza. Katika Hadith iliyosimuliwa na Bibi Aysha(r.a), tunafahamishwa kuwa Mtume(s.a.w) alistushwa sana na lile tukio la Pangoni Hira, la kulazimishwa kusoma na Malaika Jibril ambaye ilikuwa ni mara yake ya kwanza kukutana naye. Mtume(s.a.w) alirudi nyumbani akiwa anatetemeka kama mtu mwenye homa kali. Alimuomba mkewe Khadija amfunike nguo nzito(shuka). Baada ya muda hali ile ya khofu iliisha na kuweza kumhadithia mkewe yale yaliyomtokea. Alipomuona tena Jibril(a.s) anamjia kumletea wahay uliomo mwanzoni mwa sura hii (73:1-10) Mtume(s.a.w) alistuka tena na kujaribu kujihami asijefikwa na yale yaliyo mfika pangoni kwa kujifunika tena nguo. Lakini bado Jibril alimuendea Mtume(s.a.w) katika hali ile ile ya kujifunika na kumfikishia ujumbe huu wenye kumuamrisha kufanya yafuatayo:

1. Kusimama kwa swala ya usiku kwa kitambo kirefu kati ya saa 4 au theluthi ( $1/3$ ) hadi saa 8 au theluthi mbili ( $2/3$ ) za usiku.
2. Kusoma Qur-an kwa mazingatio.
3. Kumdhukuru au kumkumbuka Allah(s.w) kila wakati.
4. Kujitupa kwa Allah kikweli (kumtii Allah kwa unyenyekevu)
5. Kumfanya Allah kuwa mlinzi (wakili) pekee.
6. Kufanya subira juu ya yale wayasemayo makafiri na kuwaepuka mwepuko mwema.

Imebainishwa wazi kuwa Mtume(s.a.w) amepewa amri hizi ili iwe maandalizi ya kupokea kauli nzito. Kauli nzito si nyingine ila lile lengo alioletwa kwalo la kusimamisha Uislamu katika jamii.

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ ۗ  
 وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٣٣﴾

*Yeye ndiye aliyemleta Mtume wake kwa uongofu na Dini ya haki ili aijaalie kushinda (Dini hii) Dini zote, ijapokuwa watachukia hao washirikina. “(9:33)*

Kuchukia kwa washirikina kunaashiria mapambano.

**(iii) Suratul-Muddaththir (74:1-7)**

يَتَأْتِيهَا الْمُدْتِرُّ ﴿١﴾ ثُمَّ فَاَنْذِرْ ﴿٢﴾ وَرَبِّكَ فَكَبِيرٌ ﴿٣﴾ وَثِيَابَكَ فَطَهِّرْ ﴿٤﴾  
 وَالرُّجُزَ فَاهْجُرْ ﴿٥﴾ وَلَا تَمُنْ بِتَسْتَكْبِرُ ﴿٦﴾ وَلِرَبِّكَ فَاصْبِرْ ﴿٧﴾

*Ewe uliyejifunika maguo. Simama uonye (viumbe). Na Mola wako umtukuze. Na nguo zako uzisafishe. Na Mabaya yapuuze, (endelea kuyapuuzza). Wala usiwafanyie ihsani (viumbe) ili upate kujikithirishia (wewe hapa duniani). Na kwa ajili ya Mola wako fanya subira (kwa kila yatakayokufika). ( 74:1-7)*

Muda mfupi baada ya kupewa amri sita zilizomo katika suratul-Muzzammil(73:1-10) na kuanza kuzitekeleza, Mtume (s.a.w)akiwa katika hali ile ile ya kujifunika funika aliamrishwa tena na Mola wake, ili kumalizia kazi ya maandalizi, kufanya yafuatayo:

1. Kusimama na kuonya – kulingania Uislamu.
2. Kumtukuzza Allah.
3. Kutakasa nguo.
4. Kupuuza mabaya.
5. Kufanya ihsani kwa ajili tu ya kutafuta radhi za Allah(s.w).
6. Kufanya subira kwa ajili ya Allah.

## **Mafunzo Yatokanayo na Maandalizi ya Kimafunzo**

Kutokana na maandalizi haya ya awali aliyopewa Mtume(s.a.w) mwanzoni mwanzoni mwa Utume wake tunajifunza kuwa ili tuweze kusimamisha Uislamu katika jamii kama alivyofanikiwa kuusimamisha Mtume(s.a.w) na maswahaba zake , tunajifunza yafuatavyo:

### **(i) Elimu katika Fani zote**

Ukiacha ila ya uchawi iliyoharamishwa,ndio nyenzo ya msingi ya kutuwezesha kusimamisha Uislamu katika jamii. Hivyo Waislamu hawanabudi kutilia mkazo suala la elimu na kuandaa mitaala na mazingira yatakayowezesha kuielimisha jamii kwa lengo la kusimamisha Ukhalifa katika ardhi.

### **(ii) Kisimamo cha usiku**

Ni nyenzo kuu ya pili inayofuatia katika maandalizi ya kusimamisha Uislamu katika jamii. Allah(s.w) anatubainisha kuwa hekima ya kupewa amri ya kisimamo cha usiku (Qiyamullayl) ni ili tupate maandalizi ya “**Ukomando**” (Ujasiri wa nafsi) yatakayotuwezesha kukabiliana na suluba (misuko suko) ya kusimamisha Uislamu katika jamii. Allah(s.w) anabainisha pia kuwa maandalizi haya hayafai mchana ila usiku kwa sababu kuna mazingira mazuri ya utulivu yatakayompelekea huyu askari wa Allah kuwa na **khushui** (unyenyekavu) ya hali ya juu inayohitajika kuomba hidaya na msaada kutoka kwa Allah(s.w). Pia kuamka usiku na kukatisha utamu wa usingizi katika theluthi ya mwisho ya usiku, humpa Muislamu zoezi la uvumilivu na subira. Hivyo, ni wazi kuwa, **kisimamo cha usiku**, kikitekelezwa vilivyo, kinauwezo mkubwa wa kumfanya Muislamu awe na ujasiri wa kusimamisha Uislamu katika jamii kwa hali yoyote iwayo. Hivyo kwa waumini wa kweli, wanaojua kuwa wanadhima ya kuusimamisha Uislamu katika jamii na kuuhami usiporomoke baada ya kusimama, **kisimamo cha usiku**, si jambo la khiari kwao kama Mola wao anavyowatanabahisha:

أَمَّنْ هُوَ قَدِنتُ إِانَاءَ اللَّيْلِ سَاجِدًا وَقَائِمًا يَحْذَرُ الْآخِرَةَ وَيَرْجُوا رَحْمَةَ رَبِّهِ ۗ قُلْ هَلْ يَسْتَوِي الَّذِينَ يَعْلَمُونَ وَالَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ۗ إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿٩﴾

*Je, afanyae Ibada nyakati za usiku kwa kusujudu na kusimama na kuogopa Akhera na kutarajia rehema ya Mola wake (ni sawa na asiyejanya hayo)? Sema: “Je, wanaweza kuwa sawa wale wanaojua na wale wasiojua?” Wanaoatanabahi ni wale wenye akili tu. “(39:9)*

Pia tunafahamisha katika Qur’an kuwa miongoni mwa sifa za waja wa Allah(s.w) ni kusimama usiku.

وَالَّذِينَ يَبِيتُونَ لِرَبِّهِمْ سُجَّدًا وَقَائِمًا ﴿١٤﴾

*“Na wale wanaopitishas baadhi ya saa za usiku kwa ajili ya Mola wao kwa kusujudu na kusimama” (25:64)*

إِنَّمَا يُؤْمِنُ بِآيَاتِنَا الَّذِينَ إِذَا ذُكِرُوا بِهَا خَرُّوا سُجَّدًا وَسَبَّحُوا بِحَمْدِ رَبِّهِمْ وَهُمْ لَا يَسْتَكْبِرُونَ ﴿١٥﴾ تَتَجَافَى جُنُوبُهُمْ عَنِ الْمَضَاجِعِ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ خَوْفًا وَطَمَعًا وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ ﴿١٦﴾

*Hakika wanao ziamini aya zetu ni wale tu ambao wanapokumbushwa kwazo huanguka kusujudu na kumtukua Mola wao kwa sifa zake, nao hawatakabari. Huinuka mbavu zao kutoka vitandani wakati wa usiku ili kumuambudu Mola wao kwa kuogopa moto na kutarajia pepo; na kutoa katika yale tuliowapa.” (32:15-16)*

Pia tunafahamishwa na Mola wetu kuwa kuamka usiku hupandishwa cheo.

وَمِنَ اللَّيْلِ فَتَهَجَّدُ بِهِ نَافِلَةً لَّكَ عَسَىٰ أَن يَبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَّحْمُودًا ﴿٧٤﴾

*Na katika usiku jiondoshee usingizi(kidogo) kwa kusoma hiyo Qurani ndani ya Sala). Hiyo ni (ibada) zaidi kwako. Huenda Mola wako akakuinua cheo kinichosifika. (17:79)*

### **(iii) Kusoma Qur-an kwa mazingatio**

Kusoma Qur'an kwa mazingatio kwa lengo la kuifanya kuwa dira pekee ya maisha yetu ya kila siku, ni nyenzo nyingine itakayotuwzesha kusimamisha Uislamu katika jamii. Uislamu ni mfumo wa maisha wa kutii na kufuata utaratibu wa kuendesha maisha ya kibinafsi na ya kijamii anaouridhia Allah(s.w).

Utaratibu huu wa maisha anaouridhia Allah(s.w) umeainishwa na Qur-an, kitabu chake cha mwisho. Hivyo, waumini wa kweli; ili waweze kusimamisha Uislamu katika jamii, hawanabudi kuisoma Qur-an kwa mazingatio kiasi cha kuweza kuelewa vilivyo na kuifanya mwongozo wa kukiendea kila kipengele cha maisha ya kibinafsi na ya kijamii. Vile vile jamii ya Waislamu hainabudi kuandaa mtaala wa kufundisha Qur-an kwa lengo la kuwaandaa wasomaji wa rika zote kuwa Makhalifa wa Allah(s.w).

### **(iv) Kumdhukuru na kumtukuza Allah(s.w)**

Kumdhukuru Allah(s.w) na kumtukuza ni nyenzo nyingine muhimu itakayowawezesha waumini kusimamisha Uislamu katika jamii. Ili Waislamu wawe na msimamo thabiti, hawanabudi kuwa na yakini juu ya kuwepo Allah(s.w) na sifa zake tukufu. Imani ya kweli juu ya Allah(s.w) inathibitishwa na matendo ya Muumini ya kila siku pale atakapofuata maagizo na kuchunga mipaka ya Allah(s.w) katika kukiendea kila kipengele cha maisha yake.

### **(v) Kujitupa kwa Allah kwa kweli**

Kujitupa kwa Allah kwa kweli au kumtii Allah(s.w) kwa unyenyekevu, ni nyenzo nyingine ya kumuwezesha Muumini kusimamisha Uislamu katika jamii. Pamoja na kuwa kusimamisha

Uislamu ni “kauli nzito” (jambo zito), Muumini mwenye kujitupa kwa Allah kwa kweli, hatamchelea yeyote awaye au lolote zito liwalo, katika kutekeleza amri ya Allah(s.w) iliyoumbele yake.

### **(vi)Kumfanya Allah kuwa Mlinzi Pekee**

Kumfanya Allah(s.w) kuwa Mlinzi Pekee ni nyenzo nyingine inayompa Muumini ujasiri wa kusimamisha Uislamu katika jamii. Kuwa tegemezi kwa Allah(s.w) ambaye ni **Al-qahhaaru** (mwenye nguvu juu ya kila kitu) humfanya Muislamu asichelee kizuizi au nguvu yoyote inayozuia Uislamu kusimama.

### **(vii)Kusimama na kuonya**

Kusimama na kuonya ni amri ya kuwalingania watu juu ya upweke wa Allah(s.w) kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah na kisha kuwafahamisha namna ya kumuabudu Allah(s.w) pekee katika kila kipengele cha maisha. Baada ya kufikisha ujumbe huu wa Tawhiid, kwa hekima na mawaidha mazuri (rejea Qur-an 16:125), Mtume na Waumini kwa ujumla wanaamrisha kuwaonya watu juu ya adhabu kali itakayowafika wale wote watakaoishi kinyume cha Tawhiid – katika maisha ya akhera.

Pia amri hii ya kuwaonya watu inakwenda sambamba na kuwabashiria malipo mema watakayopata wasimamishaji wa Tawhiid katika maisha ya akhera. Kuufundisha Uislamu na kuweka wazi faida itakayopatikana kwa wale watakaoufuata vilivyo na hasara itakayowafika wale watakaoukanusha, ni hatua muhimu na ya msingi mno katika harakati za kusimamisha Uislamu katika jamii.

### **(viii)Kutakasa nguo**

Kutakasa nguo ni amri inayoashiria kuwa mwenye kulingania Uislamu anatakiwa awe mfano wa kuigwa kwa tabia njema.

Pamoja na mlinganiaji kutekeleza amri ya kutakasa nguo zake na mwili wake ili awe kivutio kwa watu atakaokutana nao katika harakati za kulingania Uislamu, anatakiwa awe na tabia njema itakayovuta usikivu wa watu. Katika kutekeleza amri hii Mtume(s.a.w) alikuwa akipendelea vazi jeupe na kujipaka manukato ili asiwe kero kwa watu kutokana na harufu mbaya inayotokana na nguo chafu na majasho.

Sambamba na usafi huu wa nguo na mwili, Mtume(s.a.w) alikuwa na tabia njema kabisa.

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ ﴿٤﴾

“Na bila shaka una tabia njema kabisa.” (68:4)

Mlinganiaji kuwa kiigizo kwa tabia inasisitizwa katika aya zifuatazo:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لِيَمَّ تَقُولُونَ مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿٣﴾ كَبِيرَ مَقْتًا عِنْدَ اللَّهِ أَنْ تَقُولُوا مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿٣﴾

*Enyi mlioamini! Mbona, (kwa nini) mnasema msiyoyatenda? Ni chukizo kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu kusema msiyoyatenda. (61:2-3)*

### **(ix)Kupuuza Mabaya**

Kupuuza Mabaya ni pamoja na kutojali au kutokatishwa tamaa na mabaya unayofanyiwa na maadui wa Uislamu. Pia amri hii ya kupuuza mabaya ni pamoja na kujiepusha kuyafanya, kutoyathamini maovu hatakama yanafanywa na watu maarufu na kuyachukia. Kupuuza mabaya ni nyenzo nyingine muhimu katika kusimamisha Uislamu. Kama muumini hatakuwa na tabia ya kupuuza mabaya anayofanyiwa na maadui wa harakati za kusimamisha Uislamu, atafikishwa mahali pakukatishwa tamaa na kususa harakati.



**(x) Kufanya ihsani kwa ajili tu ya kutafuta radhi za Allah(s.w)**

Kufanya ihsani kwa ajili tu ya kutafuta radhi za Allah(s.w) ni amri inayowataka wanaharakati wa kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii wasitegemee malipo ya kazi hii kutoka kwa watu bali wategemee malipo yao kutoka kwa Allah(s.w). Kazi ya kusimamisha Uislamu katika jamii, Allah(s.w) ameifaninisha na biashara kati yake na waumini ambapo waumini wanamuuzia Allah(s.w) mali zao na nafsi zao, naye Allah awalipe malipo makubwa yanayobainishwa katika aya zifuatazo:

﴿إِنَّ اللَّهَ اشْتَرَىٰ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَنفُسَهُمْ وَأَمْوَالَهُم بِأَنَّ لَهُمُ الْجَنَّةَ يُقَدِّتُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيَقْتُلُونَ وَيُقْتَلُونَ وَعَدًّا عَلَيْهِ حَقًّا فِي التَّوْرَةِ وَالْإِنْجِيلِ وَالْقُرْآنِ وَمَنْ أَوْفَىٰ بِعَهْدِهِ مِنَ اللَّهِ فَاسْتَبْشِرُوا بِبَيْعِكُمُ الَّذِي بَايَعْتُمْ بِهِ وَذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١١١﴾﴾

*Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waumini nafsi zao na mali zao (watoe nafsi zao na mali zao katika kupigania Dini) ili na yeye awape Pepo. Wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu; wanaua na wanauawa. Hii ndiyo ahadi aliyojilazimisha (Mwenyezi Mungu) katika Taurati na Injili na Qur-an. Na ni nani atelezaye zaidi ahadi yake kuliko Mwenyezi Mungu? Basi furahini kwa biashara yenu mliyofanya naye (Mwenyezi Mungu). Na huko ndiko kufuzu kukubwa. “(9:111)*

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا هَلْ أَذُكُّكُمْ عَلَىٰ تَجَارَةٍ تُنْجِيكُمْ مِّنْ عَذَابِ أَلِيمٍ ﴿١١٠﴾ تُوْمِنُونَ بِاللّٰهِ وَرَسُوْلِهِ وَتَجَاهِدُونَ فِي سَبِيْلِ اللّٰهِ بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنفُسِكُمْ ذٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ

*Enyi mlioamini! Je! Nikujulisheni biashara itakayokuo kweni na adhabu iumizayo? (Biashara yenyewe ni hii) Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na piganieni Dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zenu na nafsi zenu. Haya ni bora kwenu ikiwa mnajuwa (61:10-11)*

## (xi) Kufanya Subira kwa ajili ya Allah

Kufanya Subira kwa ajili ya Allah ni nyenzo nyingine ya msingi itakayowawezesha Waumini kusimamisha Uislamu katika jamii. Katika harakati za kusimamisha Uislamu katika jamii, kuna kero na bughudha nyingi zinazoandaliwa na kusimamiwa na wapinzani wa Uislamu. Ukirejea historia ya Mtume(s.a.w), kero hizi huanza na kujenga mazingira ya kukatisha tamaa. Katika mazingira hayo, Mtume(s.a.w) alitwa mwongo, mwenda wazimu, mtunga mashairi, mchawi, aliyepagawa, mkatikiwa na kheri (Abtari), n.k.

Katika mazingira ya sasa makafiri wanajitahidi kuwa katisha tamaa wanaharakati kwa kuwaita siasa kali (fundamentalist), mashabiki wa Kidini (fanatics), magaidi (terrorists), n.k. Allah(s.w) anatuamrisha tusbiri juu ya hayo wayasemayo dhidi yetu na tuwaepuke mwepuko mwema. Kuwaepuka mwepuko mwema ni kuyapuza hayo wayasemayo dhidi yetu na tusilumbane nao ili wasije kuttoa katika agenda yetu. Jibu la tusi kwa muungwana ni “**hewala**” na jibu la muumini kwa jahili ni “**salama**”.

وَعِبَادُ الرَّحْمَنِ الَّذِينَ يَمْشُونَ عَلَى الْأَرْضِ هَوْنًا وَإِذَا خَاطَبَهُمُ

الْجَاهِلُونَ قَالُوا سَلَامًا ﴿١٣﴾

*“Na waja wa Rahmani, ni wale wanaokwenda ulimwenguni kwa unyenyekevu; na majahili wakisema nao (maneno mabaya) huwajibu (maneno ya) salama.” (25:63).*

Tukirejea historia, baada ya makafiri kushindwa kuzuia harakati za kusimamisha Uislamu kwa maneno ya kukatisha tamaa, waliandaa nguvu za kuzuia Uislamu kwa matendo kama vile kutesa, kufunga gerezani, kufukuza nchini na kuua. Haya ndiyo mazingira halisi katika harakati za kusimamisha Uislamu na ndiyo sunnah ya harakati aliyoiweka Allah(s.w) kama anavyotukumbusha:

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا شَيْطِينِ الْإِنْسِ وَالْجِنِّ يُوحِي بَعْضُهُمْ  
إِلَى بَعْضٍ زُخْرُفَ الْقَوْلِ غُرُورًا وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ مَا فَعَلُوهُ فَذَرْهُمْ وَمَا  
يَفْتَرُونَ ﴿١١٢﴾

*Na namna hii tumefanyia kila Nabii maadui; (nao ni) mashetani katika watu na (mashetani katika) majini. Baadhi yao wanawafunulia wenziwao maneno ya kupambapamba ili kuwadanganya. Na kama Mola wako angalipenda wasingalifanya hayo, (angewalazimisha kwa nguvu kutii). Basi waache na uwongo wao. (6:112)*

## **MTUME(S.A.W) KULINGANIA UISLAMU MAKKA**

Historia ya harakati za Mtume(s.a.w) za kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii yake zimegawanyika katika vipindi viwili – kipindi cha **Makka** na kipindi cha **Madinah**. Kipindi cha Makka kilichukua muda wa miaka kumi na tatu(13) kuanzia pale Mtume(s.a.w) alipoanza kupokea wahayi wa kwanza wa Qur'an mpaka alipoondoka kuhamia Madinah. Kipindi cha Madinah kilianza pale alipopokelewa Madinah na Answar mpaka mwisho wa uhai wake. Kipindi hiki kilichukua muda wa miaka kumi (10).

Mazingira ya **Makka** na **Madinah** yalikuwa tofauti. Hivyo hata mbinu za kuhuisha na kusimamisha Uislamu zilitofautiana. Pia hata mbinu za wapinzani wa Uislamu zilitofautiana.

## **Kuanza Kulingania kwa Siri**

Baada ya Mtume(s.a.w) kupewa amri ya “simama uonye (watu)” aliamua kuanza kulingania kwa siri. Bila ya kutangaza hadharani kuwa yeye sasa ni Mtume wa Allah(s.w), alianza kumuendea mtu mmoja mmoja katika wale waliokuwa karibu naye kifamilia na kirafiki. Mtume(s.a.w) alianza kuutangaza Utume wake

kwa mkewe Khadija na watoto kisha kwa wale waliokuwa chini ya ulezi wake, ndugu yake, Ally bin Abu-Talib na huru wake, Zaid bin Harith. Baada ya hapo Mtume(s.a.w) aliwaendea rafiki na jamaa zake wa karibu na kuwafikishia ujumbe wa Utume. Miongoni mwa rafiki zake waliokuwa karibu ni Abubakar(r.a). Rafiki zake nao waliufikisha ujumbe wa Uislamu kwa familia zao na rafiki zao wa karibu kiasi kwamba ujumbe ulitambaa chini kwa chini mpaka ukaingia takriban katika kila nyumba ya wakazi wa Makka.

Katika kipindi hiki cha kufikisha ujumbe kwa siri, kilicho dumu kwa miaka mitatu, Mtume(s.a.w) alikuwa akikutana na Waislamu kwa siri katika nyumba ya Bwana **Arqam bin Abi Arqam** iliyojulikana kwa jina maarufu, "**Darul-Arqam**".

Mtume(s.a.w) alikuwa anakutana na waumini Darul-Arqam ili kuwafundisha Uislamu na kuwapa waumini maelekezo ya namna ya kuutekeleza katika maisha ya kibinafsi na ya kijamii. Alikuwa akiwasomea aya za Qur-an alizokuwa anashushiwa kila mara na kuwaelekeza namna ya kuzitekeleza katika maisha yao ya kila siku. Kila Muislamu wakati ule aliujua Uislamu na kuutekeleza vilivyo katika maisha yake ya kila siku. Kwa mujibu wa Hadith, iliyo simuliwa na Ibn Masu'ud(r.a), kila Muislamu aliisoma Qur-an kwa lengo la kuifanya mwongozo wa maisha yake ya kila siku.

Wengi waliosilimu katika kipindi hiki cha awali walikuwa watumwa, maskini, vijana na wale wasiokuwa maarufu katika jamii. Kilichowafanya hawa watu wa mwanzo kusilimu haraka haraka bila ya kusita, ni ule ukaribu wao na Muhammad(s.a.w) ambao uliwawezesha kuifahamu vyema tabia yake tukufu. Walimfahamu kuwa alikuwa mwaminifu mno na hawakuwahi kamwe kumsikia akisema uwongo. Kwa ukweli wake na uaminifu uliopea, walimuita "**As-Sadiq Al-Amin**" (Mkweli Mwaminifu) hata kabla ya kutangaza ujumbe wa Uislamu. Pia, hata kabla ya kuanza kutangaza ujumbe wa Utume wake, alikuwa mpole na mwenye kuwahurumia mno wanyonge hasa watumwa na maskini. Hivyo, alipowatangazia hao

rafiki zake na jamaa zake wa karibu kuwa yeye ni Mtume wa Allah, wote waliitikia wito wake wakasilimu isipokuwa wale waliokuwa na matatizo yao ya ubinafsi kama ami yake, **Abu-Lahab**.

### **Mafunzo:**

Kutokana na Mtume(s.a.w) kuanza kulingania ujumbe wa Uislamu kwa siri, tunajifunza yafuatayo:

**Kwanza**, baada ya kuukiri Uislamu na kuutekeleza kimatendo, hatunabudi kuufikisha Uislamu huo kwa familia zetu, rafiki na jamaa zetu wa karibu. Hawa watakuwa wepesi kutusikiliza na kutufuata kwa kuwa wanatufahamu vyema. Tabia njema ni nyenzo muhimu sana.

**Pili**, ni muhimu kuwa wasiri na waangalifu katika hatua za mwanzo mwanzo za kuuhuisha Uislamu katika jamii ili maadui zetu wasije kutuzima kabla ujumbe haujasambaa kwa watu wengi. Baada ya miaka mitatu ya Mtume(s.a.w) kutangaza ujumbe kwa siri, takriban katika kila familia ya wakazi wa Makka palikuwa na mtu aliyesilimu. Jambo hili liliwaudhi na kuwahuzunisha sana wakuu wa jamii ya Kiquraish.

**Tatu**, kuujua Uislamu vilivyo kwa kila Muislamu ni jambo muhimu sana. Hata katika kipindi hiki cha kutangaza ujumbe kwa siri, Mtume(s.a.w) hakuacha kuwakusanya Waislamu kisiri siri katika kituo cha Darul-Arqam kuwafundisha Uislamu na kuwapa maelekezo ya utekelezaji wake katika maisha ya kila siku. Uislamu hautoweza kusimama katika jamii iwapo wanaojiita Waislamu watakuwa wameridhika kuishi kwa kufuata upepo kama bendera. Waislamu wa kufuata mkumbo (norminal Muslims) mara nyingi hutumiwa na maadui na kuupiga vita Uislamu na Waislamu bila kujitambua. Aidha, Waislamu wa mkumbo mara nyingi huwa rahisi kukumbwa na propoganda za maadui wa Uislamu. Vile vile Waislamu wa aina hii ni rahisi kuathiriwa na mila na desturi za makafiri.

## Kulingania Uislamu kwa Jamii Nzima

Baada ya miaka mitatu ya Utume, Muhammad(s.a.w) aliamuriwa na Mola wake kuutangaza ujumbe kwa uwazi kwa watu wote.

فَأَصْدَعْ بِمَا تُؤْمَرُ وَأَعْرِضْ عَنِ الْمُشْرِكِينَ ﴿٩٤﴾ إِنَّا كَفَيْنَاكَ  
الْمُسْتَهْرَجِينَ ﴿٩٥﴾

*“Basi yatangaze uliyoamrisha (wala usijali upinzani wao) na ujitenge mbali na hao washirikina. Hakika sisi tunatosha kukuingia (shari ya) wanaofanya dhahaka”. (15:94-95)*

وَأَنْذِرْ عَشِيرَتَكَ الْأَقْرَبِينَ ﴿٩٦﴾ وَأَخْفِضْ جَنَاحَكَ لِمَنِ اتَّبَعَكَ مِنَ  
الْمُؤْمِنِينَ ﴿٩٧﴾ فَإِنْ عَصَوْكَ فَقُلْ إِنَّي بِرِيءٍ مِّمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٩٨﴾ وَتَوَكَّلْ  
عَلَى الْعَزِيزِ الرَّحِيمِ ﴿٩٩﴾

*Na uwaonye jamaa zako walio karibu (nawe). Na uinamishe bawa lako kwa yule anayekufuata katika wale walioamini. Na kama wakikuasi, basi sema: “Mimi ni mbali na hayo mnayoyafanya.” Na umtegemee (Mola wako) Mwenye nguvu, Mwenye rehema. (26:214-217)*

Mtume(s.a.w) alianza kutekeleza amri hii kwa kutumia nyenzo ya **“tabia yake njema”**. Aliita kwa jina ukoo moja moja mpaka kumaliza koo zote kumi na nne za kabila la Quraysh akiwa juu ya kilima cha Safa, karibu na Ka’abah. Baada ya koo zote kuhudhuria chini ya kilima cha Safa, Mtume(s.a.w) aliwaomba jamaa zake wa karibu, banu ‘Abdul-Manaf, wasogee karibu naye kisha akaanza kutoa khutuba yake ya kwanza:

*“Mnaonaje! Kama nikiwapa taarifa kuwa kunajeshi kubwa linalokuja kukupigeni kutoka chini ya mlima huu, je, mtaniamini?” Wakajibu wote kwa pamoja, “Naam, bila shaka*

*tutakuamini, kwani hatujawahi kusikia kutoka kwako ila ukweli”.* Kisha Mtume(s.a.w) akasema, “Hakika mimi kwenu ni kama mtu aliyemuona adui, kwa hiyo akaenda kuwaonya watu wake, lakini akahofu kwamba adui anaweza kumuwahi kabla hajafikisha habari kwa watu wake, kwa hiyo akaanza kupiga kelele: ‘Tahadharini na mashambulizi ya asubuhi’. Hakika mimi ni muonyaji kwenu juu ya adhabu kali iliyo mbele yenu. Enyi wana wa Abdul-Muttalib, Enyi wana wa ‘Abdul-manaf, Enyi wana wa Zuhr, (mpaka akamaliza kuziita koo zote za Quraysh), hakika Allah ameniamrisha kuwaonya jamaa zangu wa karibu. Na hakika mimi sina cha kuwanufaisha katika maisha haya ya dunia na ya huko akhera ila mtakapokiri kuwa “Hapana Mola ila Allah”<sup>5</sup>

Baada ya kwisha kwa khutuba hii, Maquraish walikasirika sana wakawa wanapiga kelele “*umekuwa mwendawazimu!*” Ami yake Mtume, Abu Lahab, alimuapiza: “*langamie mikono yako miwili siku ya leo. Hili ndilo ulilotuitia hapa? Heshima yote tuliyokuwa tukikupa sasa umeikosa. Ondokeni, mwacheni mpuuzi huyu.*”

Mtume(s.a.w) alihuzunishwa sana na maneno ya Abu Lahab, ami yake. Allah(s.w) alimfariji Mtume wake kutokana na hali ile kwa kumshushia Suratul-Lahab:

تَبَّتْ يَدَا أَبِي لَهَبٍ وَتَبَّ ۝ مَا أَغْنَىٰ عَنْهُ مَالُهُ وَمَا كَسَبَ ۝ سَيَصْلَىٰ  
 نَارًا ذَاتَ لَهَبٍ ۝ وَأَمْرًا تُهْرَعُونَ ۝ حَمَلَةَ الْخَطَبِ ۝ فِي جِيدِهَا حَبْلٌ مِّن  
 مَّسِينٍ ۝

*Pana kuangamia mikono miwili ya Abu Lahab! Naye amekwisha angamia. Hayatamfaa mali yake wala alivyovichuma. (Atakapokufa) atauingia Moto wenye mwako (mkubwa kabisa). Na mkewe, mchukuzi wa kuni (za fitina, fattani, anayefitinisha*

watu wasiingie katika Dini; ataungia naye Moto huo). (Kama kwamba) shingoni mwake iko kamba iliyosokotwa (anayochukulia kuni za fitina hizo). (111:1-5)

Siku chache baada ya tukio la Safa, Mtume(s.a.w) aliwaalika jamaa zake wa karibu kwa chakula. Baada ya kumaliza kula Mtume(s.a.w) alisimama na kuwafikishia ujumbe ufuatao:

*“Enyi kizazi cha wana Abdul-Muttalib, hakika Allah amenituma kuwa Mtume kwenu nyinyi na kwa watu wote kwa ujumla. Kwa hiyo ameniamrisha: “Na uonye jamaa zako walio karibu.” Na ninawaiteni kwenye maneno mawili ambayo ni mepesi sana katika ulimi na mazito sana katika mizani, nayo ni “Kushuudia kuwa hapana Mola ila Allah na kwamba mimi ni Mtume wake.” Nani atakayeniitikia na kunisaidia katika kazi hii? Alijibu ‘Ali (r.a), “Nitakusaidia Ewe Mtume wa Allah”. Mtume akamwambia: “Kaa chini”. Mtume(s.a.w) alirudia tena kuuliza swali lile. Lakini wote walinyamaza kimya, ila ‘Ali bin Abu-Talib alisimama tena akasema: “Nitakusaidia Ewe Mtume wa Allah. Kisha alimuamuru tena kukaa chini. Kisha alirudia tena swali lile kwa mara ya tatu. Lakini hapana aliyejibu. Ndipo ‘Ali alisimama tena na kujibu, ‘Nitakusaidia Ewe Mtume wa Allah. Mtume akamwambia: “Kaa chini, wewe ndugu yangu.”<sup>6?</sup>*

### **Mafunzo:**

Kutokana na hatua hii ya Mtume(s.a.w) kufikisha ujumbe kwa uwazi na kwa watu wote tunajifunza yafuatayo:

**Kwanza**, baada ya kuuhuisha Uislamu katika nafsi zetu na watu wetu wa karibu, familia, ndugu na rafiki, hatuna budi kutanua wigo wa ulinganizi mpaka kufikia ngazi ya Kitaifa na hatimaye ya Kimataifa. Uislamu ni Dini ya ulimwengu mzima na waumini wote ni ummah mmoja na ndugu moja.



**Pili**, hapana yeyote wa kumchelea katika kutekeleza amri ya Allah(s.w). Baada ya Mtume(s.a.w) kupewa amri ya kufikisha ujumbe kwa kila mtu wa kabila lake (jamaa zake wa karibu), alifanya hivyo bila ya kujali upinzani aliokuwa akiutarajia.

**Tatu**, subira na kutokata tamaa ni nyenzo muhimu mno katika kulingania Uislamu. Baada ya kupuuzwa ujumbe wake katika hadhara ya mlima Safa, Mtume(s.a.w) aliendelea mbele na kazi yake kwa kuwaita peke yao watu wake wa karibu zaidi – Wana Abdul-Muttalib.

**Nne**, hatunabudi kutumia mbinu mbali mbali katika kulingania Uislamu. Mtume(s.a.w) alitumia mbinu ile ya kuwaita Maquraish wote kwenye kilima cha Safa na kuchagua kuwafikishia khutuba ile. Kisha akatumia mbinu ya kuwaalika chakula watu wa ukoo wake wana Abdul-Muttalib.

## **Upinzani Dhidi ya Ujumbe wa Mtume(s.a.w)**

Mtume(s.a.w) alipoanza kutangaza ujumbe kwa watu wote alipata upinzani mkali. Wapinzani wakuu walikuwa wakuu au watu maarufu wa jamii yake(wadau) miongoni mwa viongozi, matajiri na mamwinyi wa Kiquraysh. Upinzani wao ulisababishwa na hofu ya kuponyokwa na maslahi yao waliyokuwa wakiyapata kwa njia za batili kupitia mkondo wa siasa kandamizi, uchumi haramu na itikadi za kishirikina. Makafiri wa Kiquraysh waliongozwa na wakuu wa jamii yao, walifanya juhudi kubwa katika kuuzima Uislamu kwa kufanya vitimbi vifuatavyo:

### **(i) Kukatisha tamaa**

Makafiri walitumia mbinu ya kumkatisha tamaa Mtume na waumini wachache aliokuwa pamoja nao kwa kumdhihakiki Mtume(s.a.w) na kumuita majina mabaya. Walimuita muongo, mwenda wazimu, mtunga mashairi, mchawi, Abtar (mkatikiwa na

kheri), aliyepagawa na shetani, n.k. Mbinu hii haikusaidia kitu kwani Mtume na waumini walibakia na msimamo wao kwa kuzingatia agizo la Allah(s.w):

﴿وَأَصْبِرْ عَلَىٰ مَا يَقُولُونَ وَاهْجُرْهُمْ هَجْرًا جَمِيلًا﴾

*“Na subiri juu ya hayo wasemayo (hao makafiri) na uwaepuke mwepuko mwema.” (73:10)*

## **(ii) Kumkataza Mtume kulingania kwa kumtumia Abu-Talib**

Wakuu wa Maquraish, walimtaka Abu-Talib, ami yake Mtume(s.a.w) na mlezi wake, amkataze Mtume asiendelee na harakati zake za kuulingania Uislamu. Maquraish walipoona Abu-talib hamkatazi Mtume(s.a.w) walimuendea kwa vitisho na kumtaka achague moja katika matatu-amkataze Mtume kulingania Uislamu au akubali apewe kijana mbadala, ‘Umairah ibn Al-Walid; na wao wamchukue Mtume wamuue au akikataa mapendekezo hayo mawili wamshambulie pamoja na Mtume(s.a.w).Abu-Talib alipofikishwa hapo ilibidi amuendee Mtume(s.a.w) na kumnasihi:

*“Ewe Muhammad! Ujutie nafsi yangu na nafsi yako, pia usinitwike mzigo nisiuweza, acha hii kazi yako.” ?*

Mtume(s.a.w) alimjibu ami yake kwa majonzi makubwa:

*“Ewe mpendwa Ami yangu! Sitaacha kazi hii hata kama wataliweka jua katika mkono wangu wa kulia na wakauweka mwezi katika mkono wangu wa kushoto. Ama Allah atanipa ushindi au nitakufa katika kazi hii.<sup>7?</sup>*

Mbinu hii nayo haikufanikiwa, kwani Abu Talib baada ya kuguswa na yale maneno mazito ya Mtume (s.a.w), aliamua kumuunga mkono na kumuahidi:

*“Ewe Mwana wa ndugu yangu, endelea na Dini yako na sema unalotaka. Naapa kwa jina la Allah, sitakutoa kwa maadui na hapana yeyote atakayekudhuru.”<sup>8</sup>*

### **(iii)Kutaka kumhonga (kumrubuni) Mtume(s.a.w)**

Makafiri wa Kiquraish baada ya vitimbi vya mwanzo kufeli walibuni mbinu nyingine ya kumzuilia Mtume(s.a.w) asiendelee na kazi ya kuulingania Uislamu. Safari hii walibuni mbinu ya kumnunua au kumhonga Mtume(s.a.w). Maquraish walimtuma mwanadiplomasia wao, ‘Utbah bin Rabiah, kuwa amrai Muhammad(s.a.w) aache kazi yake ya Utume na apokee malipo yoyote anayotaka ikiwa ni mali, Ufalme au mwanamke mzuri. ‘Utbah alipofika kwa Mtume(s.a.w) alimnasih:

*“Ewe Muhammad! Usiwagawanye watu katika nchi, waache Maquraish waendeleo na mila zao na uchukue chochote unachokitaka badala yake. Kama ni fedha (utajiri) chukua kiasi chochote unachokitaka (tutakupa); kama ni mwanamke mzuri; chagua kigori mzuri kuliko wote miongoni mwa waarabu (tutakuoza); kama ni madaraka, basi tuko tayari kukufanya Mfalme – wetu. Chukua unachokitaka katika hivi (hata ukitaka vyote) lakini uache kazi yako hii ya kutangaza Uislamu.”<sup>9</sup>*

Mtume(s.a.w) alimjibu ‘Utbah kwa kumsomea aya za Qur-an katika Surat Haamym Sajdah (41) na alipofika kwenye aya ya 37 isemayo:

وَمِنْ آيَاتِهِ اللَّيْلُ وَالنَّهَارُ وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ لَا تَسْجُدُوا لِلشَّمْسِ وَلَا  
لِلْقَمَرِ وَأَسْجُدُوا لِلَّهِ الَّذِي خَلَقَهُنَّ إِن كُنتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ ﴿٣٧﴾

*Na katika alama zake (za Uungu wake Mwenyezi Mungu) ni (huku kupatikana) usiku na mchana na jua na mwezi; basi msilisujudie jua wala mwezi; bali msujudieni Mwenyezi Mungu aliyeviumba; ikiwa nyinyi mnamuabudu Yeye (basi fanyeni hivi). (41:37)*

‘Utbah alitetemeka na kumuomba Mtume(s.a.w) asiendelee kusoma. Alirejea kwa wakuu wa Maquraish na kutoa ripoti:

*“Naapa kwa jina la Allah, haya maneno (ya Muhammad) sio mashairi. Mwacheni na Dini yake. Kama akishinda hiyo itakuwa ni heshima yenu na akishindwa, basi huo utakuwa ndio mwisho wa kazi yake hiyo.”*

Lakini Maquraish hawakutaka kusikiliza rai ya ‘Utbah, bali walimcheka na kumdhihaki kuwa amelogwa (amechawiwa). Hivyo, mbinu hii pia haikufanikiwa.

#### **(iv) Kutaka Kumlaghai Mtume(s.a.w)**

Walipoona mbinu zote zimefeli, walibuni mbinu nyingine ya kidiplomasia vile vile. Safari hii walikuja na mbinu mbili za ulaghai.

**Kwanza**, walimuendea Mtume(s.a.w) na kumuomba kuwa waondoe uhasama kati yao kwa kushirikiana katika Ibada. Wafanye makubaliano kuwa mwaka mmoja Mtume(s.a.w) pamoja na wao waabudu masanamu yao na mwaka unaofuatia washiriki pamoja na Mtume(s.a.w) kumuabudu Allah(s.w) pekee. Mtume(s.a.w) aliagizwa na Mola wake kuwa awajibu kwa kuwasomea Suratul-Kaafiruun:

قُلْ يَتَّيِّبُهَا الْكٰفِرُونَ ﴿١﴾ لَا اَعْبُدُ مَا تَعْبُدُونَ ﴿٢﴾ وَلَا اَنْتُمْ عٰبِدُونَ مَا  
اَعْبُدُ ﴿٣﴾ وَلَا اَنَا عٰبِدُ مَا عٰبَدْتُمْ ﴿٤﴾ وَلَا اَنْتُمْ عٰبِدُونَ مَا اَعْبُدُ ﴿٥﴾  
لَكُمْ دِيْنَكُمْ وَّلِيّ دِيْنِ ﴿٦﴾

*Sema: Enyi makafiri. Siabudu mnachoabudu. Wala nyinyi hamuabudu ninayemuabudu. Wala sitaabudu mnachoabudu.. Wala Nyinyi hamtaabudu ninayemuabudu. Nyinyi mna Dini yenu nami nina Dini yangu (109:1-6)*

**Pili**, Maquraish walimuendea Mtume(s.a.w) na kumpa masharti kuwa kama anataka Maquraish wasilimu, alete ujumbe mwingine usiwe ule wa Qur-an anaowasomea au abadilishe aya za Qur-an zilandane na matashi yao. Mtume(s.a.w) aliwakatalia ombi hili kwa kuwasomea Qur-an:

وَإِذَا تُلَىٰ عَلَيْهِمْ آيَاتُنَا بَيِّنَاتٍ قَالَ الَّذِينَ لَا يَرْجُونَ لِقَاءَنَا أُمِّتٌ بِفُرْعَانٍ  
 غَيْرِ هَذَا أَوْ بَدَّلَهُ قُلْ مَا يَكُونُ لِي أَنْ أُبَدِّلَهُ مِنْ تِلْقَائِي نَفْسِي  
 إِنِ اتَّبَعُ إِلَّا مَا يُوحَىٰ إِلَيَّ إِنِّي أَخَافُ إِنْ عَصَيْتُ رَبِّي عَذَابٌ يَوْمٍ  
 عَظِيمٍ ﴿١٥﴾

*Na wanaposomewa Aya zetu zilizo wazi, wale wasiogopa kukutana nasi husema: “Lete Qur-an isiyokuwa hii (ambayo haitatukataza haya tunayoyapenda), au ibadilishe (kidogo hii).” Sema “Sivezi kuibadilisha kwa khiari ya nafsi yangu; sifuati ila yanayofunuliwa kwangu (ninayoletewa Wahyi). Hakika mimi naogopa-nikimuasi Mola wangu, - adhabu ya siku (hiyo) iliyo kuu.” (10:15)*

**(v) Kuwatesa na Kuwaua Waislamu**

Maquraish walipoona wameshindwa kuzima Uislamu usiendelee kwa kutumia diplomasia, waliamua kutumia mbinu ya mabavu ya kuwapiga waumini, kuwatesa mateso ya kila namna, kuwatenga kijamii na kuwaua baadhi yao. Hebu turejee historia tuone mifano michache ya mateso kwa ajili ya Uislamu waliyopata Maswahaba na Mtume mwenyewe.

**Mtume(s.a.w) mwenyewe**

Mtume mwenyewe alifanyiwa kila aina ya mateso. Pamoja na kutukanwa na kuitwa muongo, mwendawazimu, mchawi, mkiwa na kuzomewa mitaani, alipigwa mawe (rejea safari yake ya Taif), Abu

Jahl (adui yake mkubwa) alimbandika shingoni mwake kinyesi cha ngamia wakati alipokuwa katika sijida (katika swala), Utbah bin Abi Mu'it alimniga Mtume shingo na shuka iliyosokotwa, n.k.

### **Abu Bakar(r.a)**

Mara tu Mtume(s.a.w) alipodhihirisha utume wake hadharani, Abu Bakar alikwenda kwenye Ka'bah akatoa khutuba juu ya Uislamu. Watu wote waliokuwa pale walimvamia na kuanza kumpiga. Baada ya kuanguka chini, 'Utbah bin Rabi'ah alimpiga kwa viatu mpaka akazirai. Hakupata fahamu mpaka jamaa zake wakampeleka nyumbani kwake, na alikaa kitandani kwa masiku kutokana na kipigo. Mtume(s.a.w) alipokuwa kwenye Ka'bah, Abu Jahl alikuja na kumtia shingoni kamba ya nguo iliyosokotwa. Aliinyonga ile kamba na kuikaza ili kumniga Mtume mpaka afe. Abu Bakar(r.a) alipoona kitendo kile anafanyiwa Mtume alienda mara moja kumuokoa kwa kumsukumiza Abu Jahal pembeni na kuitoa ile kamba shingoni mwa Mtume, kisha akasema: "Unataka kumuua mtu mzuri kama huyu ambaye ni Mtume wa Allah anayemtangaza Allah kwa sifa zake tukufu? Kisha Abu Jahl na maadui wengine wa Uislamu walimgeuekia Abu Bakar na kumpiga kikatili.

### **Bilal(r.a)**

Bilal alikuwa Muhabeshia na mtumwa wa Umayyah bin Khalaf, adui mkubwa wa Uislamu. Umayyah alikuwa akimpiga sana Bilal kisha alikuwa akimfunga kamba za mikononi, miguuni na shingoni kisha kuwaambia watoto wamburure njiani. Mara nyingine alikuwa akimshindisha na kumlaza njaa, kisha siku ya pili yake alikuwa akimtoa nje na kumlaza chali uchi katika jua kali juu ya mchanga wa moto na kumuwekea jiwe kubwa la moto juu ya kifua chake na kumwambia, "**Utasalia vivi hivi mpaka ufe au uache Dini ya Muhammad**". Bilal alikuwa akisema, "**Ahad**", "**Ahad**" – yaani Naabudu Mungu mmoja tu. Alitaabishwa hivyo hivyo mpaka Abu Bakar alipomkomboa. Abu Bakar aliwakomboa watumwa wengi waliokuwa wakiteswa kwa ajili ya Uislamu wao.

### **Abu-Fukayha(r.a)**

Alikuwa akitaabishwa na kuteswa na mtoto wa Umayyah kwa namna ile ile alivyokuwa akitaabishwa Bilal(r.a).

### **Bibi Anira(r.a)**

Abu Jahl alikuwa akikiunguza chuma motoni kisha akimgandamiza nacho machoni mpaka akapofuka.

### **Khabbab(r.a)**

Alikuwa mtumwa wa mwanamke katili kweli kweli, alikuwa akinyolewa nywele kisha akichomwa kwa bapa la chuma chenye moto juu ya kichwa. Akawa na madonda mengi kichwani.

### **Ammar bin Yasir(r.a)**

Baba yake na ndugu yake walikuwa wakipigwa kwa majani ya mitende kila siku mpaka wakajaa madonda mwili mzima. Baba yake na ndugu yake waliuliwa katika mateso hayo na akabakia Ammar.

### **Mama yake Ammar(r.a)**

Pamoja na mateso mengi aliuliwa kikatili mno. Alichomwa mkuki tumboni.

### **Amir bin Fuhayra(r.a)**

Aliadhibiwa kikatili mno mpaka akarukwa na akili.

### **Bibi Lubayna(r.a)**

Alikuwa akiadhibiwa kwa ukatili mno na 'Umar bin Khattab kabla hajasilimu. 'Umar alikuwa akimchapa bakora mpaka achoke.

### **(vi)Kuwasusia Waislamu na Banu Hashim**

Ni katika kipindi hiki cha mateso, Mtume(s.a.w) aliwashauri

waumini hasa wale wanyonge waliokuwa wakipata mateso makubwa zaidi, kuwa wa hajiri kwenda Uhabeshi (Ethiopia) ili kusalimisha maisha yao kwa Mfalme muadilifu, Najash. Najash alikuwa Ahlal-Kitaab (Mkristo) na baadaye alisilimu.

Maquraish walipong'amua kuwa baadhi ya Waislamu wamehamia Uhabeshi na Mfalme anawapokea, walifanya jitihada za kuwarudisha lakini ilishindikana. Hii iliwapandisha hasira zaidi na kuamua kuzidisha mateso kwa Mtume na Waislamu waliobakia Makka. Katika kuzidisha mateso, Maqurash waliamua kuwasusia Waislamu na watu wa ukoo wa Mtume (Banu, Hashim na Banu Muttalib) kiuchumi na kijamii. Banu Hashimu na Banu Muttalib walichanganywa na Waislamu kwa kuwa walipinga rai ya kuuliwa ndugu yao, Muhammad(s.a.w). Mkataba wa kuwasusia Waislamu na ukoo wa Mtume(s.a.w) uliwakataza Maquraish kufanya yafuatayo:

- (1) Kusema na Banu Hashimu yeyote wala banu Muttalib akiwa Muislamu au si Muislamu.
- (2) Kuwauzia chochote wala kununua kitu kwao.
- (3) Kuoana nao.
- (4) Kuwasaidia kwa njia yoyote ile.
- (5) Kukaa pamoja nao.

Baada ya mkataba huu kupitishwa, ilibidi Waislamu, Banu Hashim na Banu Muttalib watoke Makka na kuhamia kwenye bonde moja lililokuja julikana kwa jina la Shi'b Abu Talib (Makazi ya Abu Talib). Waislamu na watu wa ukoo wa Mtume(s.a.w) walikaa pale bondeni kwa dhiki kubwa ya chakula kiasi cha watu kula majani na ngozi, kwa muda wa miaka mitatu baada ya mkataba kuvunjwa na baadhi ya Maquraish kwa misingi ya ubinaadamu. Baadhi yao waliona si sahihi kuwatesa watu kiasi kile kwa sababu



tu ya itiqadi yao.

Pamoja na mateso haya, Mtume(s.a.w) na wale waliomuamini walibakia na msimamo wa Dini yao pasina kutetereka hata chembe. Ni katika mazingira haya Allah(s.w) anatumuambia:

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَأْتِكُمْ مَثَلُ الَّذِينَ خَلَوْا مِنْ قَبْلِكُمْ  
مَسَّتْهُمُ الْبَأْسَاءُ وَالضَّرَّاءُ وَزُلْزِلُوا حَتَّى يَقُولَ الرَّسُولُ وَالَّذِينَ آمَنُوا

مَعَهُ مَتَى نَصْرُ اللَّهِ الْآلَاءُ إِنَّ نَصْرَ اللَّهِ قَرِيبٌ ﴿٢١٤﴾

*Mnadhani kuwa mtaingia Peponi, na hali hamjajiwa na mfano wa (yale yaliyowajia) wale waliopita kabla yenu? Yaliwapata mashaka na madhara na wakatetemeshwa sana hata Mitume na walioamini pamoja nao wakasema: “Nusura ya Mwenyezi Mungu itafika lini?” Jueni kuwa nusura ya Mwenyezi Mungu iko karibu. (2:214)*

### (vii) Kuazimia Kumuua Mtume(s.a.w)

Mtume(s.a.w) baada ya mikataba ya ‘Aqabah, aliwaamuru Waislamu wahamie Yathrib (Madinah). Maquraish waling’amua kuhama kwa Waislamu na walimtarajia Mtume(s.a.w) naye kuhama. Wakuu wa Maquraish waliona kuwa wakimuachia Mtume(s.a.w) kuhamia Madinah, Uislamu utapata nguvu na itakuwa ni hatari kwa maslahi yao ya kiitiqadi, kisiasa na kiuchumi. Hivyo wakuu wa Maquraish walikutana “**Dar-al-Nadwa**” na kupitisha uamuzi wa kumuua Mtume(s.a.w) kama Qur-an inavyotukumbusha:

وَإِذْ يَمْكُرُ بِكَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِيُثْبِتُوكَ أَوْ يَقْتُلُوكَ أَوْ يُخْرِجُوكَ ﴿٣٠﴾

*Na (kumbuka Ee Nabii Muhammad) walipokufanyia hila wale waliokufuru ili wakufunge au wakuue au wakutoe (kwa hali mbaya katika Makka)“(8:30)*

Mbinu hii nayo ilifeli pale Allah(s.w) alipomnusuru Mtume

wake, alipokuwa na sahibu yake, Abubakar, katika pango la Jabal Thaur, kituo cha mwanzo cha safari yao ya kuhajiri kwenda Madinah.

إِلَّا تَنْصُرُوهُ فَقَدْ نَصَرَهُ اللَّهُ إِذْ أَخْرَجَهُ الَّذِينَ كَفَرُوا  
ثَانِيَ اثْنَيْنِ إِذْ هُمَا فِي الْغَارِ إِذْ يَقُولُ لِصَاحِبِهِ لَا تَحْزَنْ إِنَّ اللَّهَ  
مَعَنَا فَأَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَيْهِ وَأَيَّدَهُ بِجُنُودٍ لَمْ تَرَوْهَا  
وَجَعَلَ كَلِمَةَ الَّذِينَ كَفَرُوا السُّفْلَىٰ وَكَلِمَةُ اللَّهِ هِيَ الْعُلْيَا وَاللَّهُ  
عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٤٠﴾

*Kama hamtamnusuru (Mtume), basi Mwenyezi Mungu alimnusuru walipomtoa wale waliokufuru; alipokuwa (mmoja tu na mwenziwe) wa pili wake, (peke yao) walipokuwa wote wawili katika pango; (Mtume) alipomwambia sahibu yake; “Usihuzunike, kwa yakini Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi.” Mwenyezi Mungu akamteremshia utulivu wake, na akamnusuru kwa majeshi msiyoyaona, na akafanya neno la wale waliokufuru kuwa chini; na neno la Mwenyezi Mungu ndilo la juu. Na Mwenyezi Mungu ndiye anayeshinda na ndiye Mwenye hikima. (9:40)*

**Mafunzo:**

Kutokana na upinzani dhidi ya ujumbe wa Mtume(s.a.w) katika kipindi cha Makka, tunajifunza yafuatayo:

**Kwanza**, hatunabudi kukumbuka kuwa upinzani dhidi ya Uislamu haukutokea tu wakati wa Mtume(s.a.w) bali hii ni katika Sunnah ya Allah(s.w), kuwa amejaalia Uislamu uwe na upinzani katika zama zote.

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا شَيَاطِينَ الْإِنْسِ وَالْجِنِّ يُوحِي بَعْضُهُمْ  
إِلَى بَعْضٍ زُخْرُفَ الْقَوْلِ غُرُورًا وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ مَا فَعَلُوهُ فَذَرْهُمْ وَمَا

يَفْتَرُونَ ﴿١١٢﴾

*Na namna hii tumemfanyia kila Nabii maadui; (nao ni) mashetani katika watu na (mashetani katika) majini. Baadhi yao wanawafunulia wenziwao maneno ya kupambapamba ili kuwadanganya. Na kama Mola wako angalipenda wasingalifanya hayo, (angewalazimisha kwa nguvu kutii). Basi waache na uwongo wao. (6:112)*

Hivyo, ili tuweze kusimamisha Uislamu katika jamii hatunabudi kuwa tayari kupambana na wapinzani wa Dini ya Allah(s.w).

**Pili**, mbinu walizozitumia Makafiri wa Kiquraysh, katika kutaka kuuhilikisha Uislamu, zinafanana mno na hizi wanazozitumia makafiri wa leo.

**Tatu**, siri ya mafanikio ya Mtume(s.a.w) na Maswahaba zake, ya kubakia katika Uislamu, kuulingania na hatimaye kuusimamisha kule Madinah pamoja na upinzani mkubwa kiasi hicho, ni kule kufuatilia kwao kwa makini mafundisho ya awali waliyopewa katika A'laq (96:1-6), Muzzammil (73:1-10) na Muddaththir (74:1-7).

**Nne**, wakati wowote Waislamu watakapojitahidi kulingania na kusimamisha Uislamu kwa kadiri ya uwezo wao wa mali na nafsi, pamoja na upinzani mkubwa dhidi yao, nusura ya Allah(s.w) itakuwa pamoja nao alimradi tu wamtii Allah(s.w.) na Mtume wake ipasavyo. Ahadi ya Allah(s.w) iko wazi

يُرِيدُونَ لِيُطْفِئُوا نُورَ اللَّهِ بِأَفْوَاهِهِمْ وَاللَّهُ مُتِمُّ نُورِهِ

وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُونَ ﴿٨﴾

*Wanataka kuzima nuru ya Mwenyezi Mungu (ya Uislamu) kwa vinywa vyao; na Mwenyezi Mungu atakamilisha nuru yake ijapokuwa makafiri watachukiwa. (61:8)*

## **Mtume(s.a.w) Kulingania Uislamu Katika Mji wa Taif**

Baada tu ya Mtume(s.a.w) na Waislamu kurejea Makka kutoka kule Shi'b Abu Talib, Abu Talib na Bibi Khadijah walifariki ikiwa ni mwaka wa 10 baada ya Utume sawa na mwaka 620 A.D. Umuhimu wa wawili hawa kwa Mtume na Waislamu unafahamika. Japo kuwa Abu-Talib hakusilimu, alijitoa muhanga kumlinda na kumhifadhi Mtume(s.a.w) kutokana na shari za Makafiri wa Makka. Mchango wa bibi Khadijah, mke wa kwanza wa Mtume(s.a.w), unafahamika. Tangu mwanzo wa Utume, bibi Khadijah alikuwa kiliwazo kikubwa cha Mtume(s.a.w). Alimfariji Mtume(s.a.w) kwa kila gumu lililomfika na alijitahidi kwa hali na mali kumsaidia Mtume(s.a.w) katika kazi yake. Kutokana na kipigo cha vifo hivi, Mtume(s.a.w) aliuita mwaka ule wa 10 B.U (620 A.D) “**Ani al-Huzn**” – mwaka wa huzuni.

Baada ya kufariki Abu-Talib na Bi Khadijah Maquraish walizidisha jeuri zao dhidi ya Mtume(s.a.w) na Waislamu kanakwamba wanamuambia Mtume(s.a.w), “Ni nani atakayekusaidia sasa”. Mtume(s.a.w) alipoona kuwa Makka imechafuka kiasi hicho, aliamua kwenda mji wa Taif kuwalingania Uislamu watu wa huko, **Banu Thaqif** na **Banu Khawaizin**, kabila la Bibi Halima, mama yake Mtume(s.a.w) wa kunyonya. Alitarajia kuwa kutokana na uhusiano wake na watu wa kabila hilo, watampokea vizuri atakapokwenda huko. Baada ya siku 10 kupita tangu afariki Bibi Khadijah, Mtume(s.a.w) alifunga safari ya kwenda Taif akiongozana na Zaid bin Harith. Alipowasili Taif aliwaendea wakuu wa mji ule na kuwafahamisha lengo la safari yake. Wakuu hawa walimpuuza na kumvunja sana moyo. Aliamua kuwaendea watu wa kawaida lakini nao pia walimpuuza. Hata hivyo, Mtume(s.a.w) hakukata tamaa, bali aliendelea kuwalingania Uislamu watu wa mji ule.

Walipoona Mtume(s.a.w) haondoki pamoja na kumkatisha tamaa kiasi hicho, wakuu wa mji ule walitoa amri kuwa watu wampige mawe popote watakapomuona mpaka aende zake. Watu walipopata amri ile, waliwaelekeza watoto na wahuni wa mji wampige Mtume(s.a.w) mawe mpaka aondoke. Bila ya huruma walimpopoa Mtume(s.a.w) mawe na kumsindikiza nayo kwa umbali wa maili mbili. Zaid alijitahidi sana kumkinga Mtume kwa mwili wake lakini haikusaidia kitu kwani wote walibubujikwa na damu mwili mzima kuanzia kichwani hadi miguuni.

Wale watoto na wahuni wa mji walipoacha kuwapiga na kurudi zao, Mtume(s.a.w) na Zaid walikaa kujipumzisha katika shamba la 'Utbah bin Rabi'ah. 'Utbah na ndugu yake walipomuona Mtume katika hali ile walimhurumia na wakamtuma mtumwa wao kuwaletea Mtume vishada vya zabibu na vyakula vingine. Yule mtumwa alimsaidia Mtume(s.a.w) juu ya safari yake na juu ya ujumbe wake. Yule mtumwa alisilimu baada ya kupata maelekezo yale kutoka kwa Mtume(s.a.w) na Bwana wake alijuta sana kwa nini alimtuma pale. Katika hali ile ya udhaifu, Mtume(s.a.w) alimuomba mola wake dua ifuatayo:

*“Ya Allah! Kwako nashitakia udhaifu wa nguvu zangu na udhalilifu wangu katika macho ya watu. Ewe mwingi wa Rehema na Huruma kuliko wote wenye huruma! Wewe ndiye Bwana wa wanyonge na wewe ndiye Bwana wangu. Ni kwa watu gani umenipeleka? Kwa adui asiye na huruma anayenikunjia uso au kwa mgeni uliyempa uwezo juu ya jambo langu hili? Sijali lolote kunitokezea isipokuwa naomba ulinzi wako. Naomba hifadhi na nuru ya uso wako – nuru iangazayo mbinguni na kuondosha aina zote za giza na nuru iongozayo na kudhibiti mambo yote ya hapa duniani na akhera. Naomba uninusuru na ghadhabu zako au kutokuwa radhi na mimi. Sina budi kuondosha Sababu ya wewe kutokuwa radhi na mimi ili hatimaye uwe radhi na mimi. Hapana nguvu wala uwezo ila kutoka kwako” (Sahihi – Muslim).*

Mara baada ya dua yake alimjia Jibril (a.s) na baada ya kumpa salamu alisema:

*“Allah anajua yote yaliyotokea kati yako na watu hawa. Anamtuma Malaika wa milima kuwa chini ya amri yako”.*<sup>10</sup>

Mara tu baada ya Jibril(a.s) kumaliza ujumbe ule, Malaika muhusika alisimama mbele ya Mtume na kusema:

*“Ee Mtume wa Allah, niko chini ya utumishi wako (niko tayari kukutumikia utakavyonituma). Kama unataka naweza kuvigonganisha vilima viwili vilivyoutazama mji huu na watu wote ndani yake wahiliki au unaweza kuamua adhabu yoyote unayotaka wapate.”*<sup>11</sup>

Mtume(s.a.w) aliye rehema kwa viumbe alijibu:

*Hata kama watu hawa hawatakubali Uislamu, ninategemea kwa Allah kuwa watatokea watu katika kizazi hiki watakaomuabudu Allah na kupigania Dini yake”.*<sup>12</sup>

Tukio hili la Taif linatuonesha jinsi Mtume(s.a.w) alivyokuwa Rehema kwa viumbe na mvumilivu katika kazi yake. Pamoja na kufanyiwa ukatili mkubwa kiasi kile na watu wa mji wa Taif, bado hakuwalaani au kuwataka waangamizwe, bali bado alikuwa na tamaa kuwa watatokea watu wazuri katika kizazi chao watakaokuwa Waislamu na kuipigania Dini ya Allah(s.w) inavyostahiki.

## **Mafunzo Yatokanayo na Kufariki Bibi Khadija, Abu Twalib na Tukio la Taif**

Kufariki kwa Bibi Khadija na Abu Twalib na tukio la Taif tunajifunza yafuatayo:

- (i) Hatuna budi kutambua na kulipa fadhila angalau ya kihali (appreciation) kwa kila mtu aliyetoa mchango wa kuusukuma mbele Uislamu.
  - Mtume(s.a.w) katika maisha yake yote hakusahau mchango wa Bibi Khadijah na pia hakusahau mchango wa ami yake katika kuuhami Uislamu pamoja na kwamba hakusilimu. Kwa kuwaenzi mwaka walio fariki akauita “**Amul-al-Huzn**”(mwaka wa huzuni)
- (ii) Hatuna budi kutafuta fursa zitakazo pelekea kuulingania Uislamu kwa wepesi, Mtume(s.a.w) alienda Taif kutumia fursa ya udugu wa kunyonya. Mtume(s.a.w) alinyonyeshwa na Bibi Halima wa ukoo wa Saad kutoka mji wa Taif katika kabila la Bani Khawaizin.
- (iii) Tuwe na subira na kumuelekee Allah(s.w) tunapokumbana na misukosuko katika mchakato wa kulingania na kusimamisha Uislamu katika jamii. Mtume(s.a.w). Pamoja na madhila yaliyomfika hakukata tamaa bali alimuelekea Mola wake na kuleta dua ile.
- (iv) Tujiepushe na kuwalaani watu na kutaka waangamizwe kutokana na jeuri zao dhidi ya Uislamu, kwani asaa baada ya muda wanaweza, kwa rehema za Allah(s.w) kubadilika na kuufia Uislamu au kizazi chao kikaibukia kuupenda Uislamu na kuusimamisha katika jamii.

## **Safari ya Mi'raj**

Katika mwaka wa 12 B.U(Baada ya Utume) sawa na Oktoba, 621, Mtume(s.a.w) alichukuliwa usiku na malaika Jibril na Mikailu

kwa safari ndefu sana lakini iliyochukua muda mfupi sana. Safari hii iligawanyika kaitka sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni safari ya hapa ardhini kutoka msikiti mtukufu wa Makka, Masjidil-Haram mpaka msikiti mtukufu wa Jerusalem, Baitul-Muqaddas, (Masjidul-Aq-Swaa). Safari hii ya hapa ardhini inajulikana kwa jina la Israa ambayo imetajwa katika Qur'an:

سُبْحَانَ الَّذِي أَسْرَىٰ بِعَبْدِهِ لَيْلًا مِّنَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ  
إِلَى الْمَسْجِدِ الْأَقْصَا الَّذِي بَنَىٰ كُنَا حَوْلَهُ وَ لِيُرِيَهُ  
مِنَ آيَاتِنَا إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ ﴿١٧﴾

*"Utukufu ni wake yeye ambaye alimpeleka mja wake usiku kutoka msikiti mtukufu (wa Makkah) mpaka msikiti wa mbali (wa Baytul Muqaddas - Jerusalem) ambao (tumeubariki na) tumevibariki vilivyomo pembezoni mwake. (tulimpeleka hivyo) ili tumuonyeshe baadhi ya alama zetu. Hakia yeye (Mwenyezi Mungu)ni Mwenye kusikia (na) Mwenye kuona". (17:1).*

Sehemu ya pili ni safari ya mbinguni inayoanzia Baitul-Muqaddas mpaka mbingu ya Saba. Safari hii ya sehemu ya pili imeelezwa kwa urefu kaitka vitabu vya Hadithi. Kutokana na Bukhari na Muslim, Mtume(s.a.w) alielezea kisa hiki kama ifuatavyo:

*Nililala Makka katika nyumba ya Umm Haani Binti Abu Talib dada wa Ally bin Abu Taalib, wakati Jibril aliponijia. Alinichukua mpaka kwenye kisima cha Zam-zam karibu na Ka'abah. Alinipasua kifua changu katika upande wa moyo, akautwaa moyo na kuuosha kwenye beseni la dhahabu, akaujaza hekima, huruma na imani na kisha akaurudishia mahali pake na kufunga kifua. Kisha akaleta mnyama kama farasi (Burak) mweroro na mweupe, mwenye umbo la kadiri, mdogo kuliko nyumbu na mrefu kuliko punda, mwepesi na mwenye mwendo wa kasi sana ambaye huweka kwato zake kila mwisho wa upeo wa*



*macho. Nilimpanda mpaka Baytul-Muqaddas-Jerusalem na kumfunga mahali walipokuwa wakiwafunga wanyama wao Mitume. Niliingia Msikitini na kuswali rakaa mbili pamoja na mitume wote, nilikuwa Imamu wao. Baada ya kutoka nje, Jibril aliniletea vyombo viwili, kimoja cha mvinyo na kingine cha maziwa. Nilichaguwa mazima na Jibril akasema umechagua kinywaji asilia. Kisha alinichukua mbinguni juu ya mnyama yule (Burak). Jibrili aliomba afunguliwe. Ikaulizwa: Wewe ni nani? Akajibu Jibril. Kisha aliulizwa: Nani uliyeongozana naye? Alijibu (Jibril): Muhammad. Ikaulizwa: Ameitwa? Jibril akajibu: Naam, hakika ameitwa. Mbingu ya kwanza ilifunguliwa kwa ajili yetu na lo: Tunamuona Adam(a.s). Alinikaribisha na kuniombea kheri. Kisha tulipanda mpaka uwingu wa pili ambapo Jibril aliomba kufuguliwa na akaulizwa kuwa yeye ni nani? Akajibu Jibril; na aliulizwa tena: Ni nani mliye wote? Alijibu Muhammad. Ikaulizwa: Ameitwa? Akajibu: Naam, hakika ameitwa. Mbingu ya pili ilifunguliwa, na nilipoingia nilikaribishwa na Issa bin Maryam na Yahya bin Zakariya mabinamu kwa upande wa mama walinikaribisha na kunitakia rehema. Kisha nilichukuliwa mpaka mbingu ya tatu na Jibril aliomba ifunguliwe. Aliulizwa: Nani wewe? Alijibu: Jibril. Aliulizwa tena: Nani anayeongozana na wewe? Alijibu Muhammad. Ikaulizwa je, ameitwa? Alijibu: Naam, hakika ameitwa. Tulifunguliwa na nilimuona Yusuf (a.s) aliyepewa nusu ya urembo na uzuri wa sura wa dunia nzima. Alinikaribisha na aliniombea kheri kisha tuliongozana mpaka uwingu wa nne. Jibril aliomba afunguliwe. Iliulizwa kuwa yeye ni nani. Alijibu: Muhammad. Ikaulizwa: Je, ameitwa? Alijibu: Naam, hakika ameitwa. Mlango ulifunguliwa kwa ajili yetu, na lo! Idris (a.s) alikuwa pale. Alinikaribisha na kuniombea kheri. Na Allah (s.a.w) amesema: "Na tulimuinua (Idris) daraja ya juu kabisa" (Qur'an: 19:57). Kisha tulipanda naye mpaka uwingu wa tano na Jibril aliomba (mlango) ufunguliwe. Iliulizwa tena: Ni nani mliyeongozana? Alijibu: Muhammad. Ikaulizwa: Je, ameitwa? Akajibu: Naam, hakika ameitwa. Tulifunguliwa na Lo! Nikawa*

na Haruun (a.s). Alinikaribisha na akaniombea kheri. Kisha nilichukuliwa mpaka uwingu wa sita. Jibril aliomba ifunguliwe. Ikaulizwa; nani wewe? Akajibu: Jibril. Ikaulizwa tena; nani uliye pamoja naye? Alijibu: Muhammad. Kisha ikaulizwa: Ameitwa? Akajibu: Naam, hakika ameitwa. Tulifunguliwa na kumkuta Mussa(a.s). Alinikaribisha na kuniombea kheri. Kisha nikapelekwa mpaka uwingu wa saba. Jabir aliomba pafunguliwe. Ikaulizwa: Nani wewe ? Akajibu: Jibril. Ikaulizwa tena: Ninani uliyeongozana naye? Akajibu: Muhammad. Ikaulizwa: Ameitwa? Akajibu: Hakika ameitwa. Tulifunguliwa na nikamuona Ibrahim akiwa ameegemea Baitul'Ma'muur na kunaingiwa humo na malaika elfu sabini (70,000) kila siku ambao hawatazuru tena sehemu hiyo milele. Kisha nilipelekwa "Sidratul-'Muntahaa, (Mti wa Kivuli) ambao majani yake mapana kama masikio ya tembo na matunda yake kama vyombo vikubwa vya udongo. Na ulipofunikwa kwa amri ya Allah ulibadilika kwa kiasi ambacho hakuna yeyote katika viumbe anayeweza kuusifu uzuri wake; (Qur'an 53:16). Kisha Allah(s.w) aliniletea (alinishushia) wahyi na akanipa amri ya **Swala hamsini** kwa kila mchana na usiku.

Kisha nilishuka kwa Musa (a.s) (uwingu wa sita) akaniuliza: Ni kitu gani Mola wako alichokiamrisha kwa Umma wako? Nikajibu: Swala hamsini. Akasema (Musa): Rejea kwa Bwana wako umuombe akupunguzie (idadi ya swala hizo) Umma wako hautaweza kulibeba jukumu hilo. Nimewajaribu wana Israil (nikawakuta dhaifu mno kiasi cha kutoweza kubebe jukumu hilo). Nilirudi kwa Bwana wangu na kumuomba Ee Mola wangu, Nifanyie tahfifu kwa Umma wangu. Allah(s.w) akanipunguzia swala tano zikabakia arobaini na tano). Nikaenda chini kwa Musa(a.s) na kumueleza: Allah amenipunguzia swala tano. Akasema (Musa a.s): Hakika Umma wako hautaweza kubebe jukumu hili, rejea kwa Bwana wako umuombe akufanyie tahfifu. Nilibakia kwenda na kurudi kati ya Allah(s.w) na Musa(a.s) mpaka Allah(s.w) akasema: "Kuna swala tano kwa kila mchana

*na usiku wake (kwa kila siku). Ee Muhammad, kila moja italipwa kama kumi, kwa hiyo inafanya idadi ya swala hamsini (5 x 10 = 50). Yule atakayenuia kufanya kitendo kizuri na asikifanye atalipwa au ataandikiwa jaza ya jema moja na akifanya atalipwa kama mtu aliyetenda kitendo hicho mara kumi; ambapo yule atakayenuia kufanya kitendo kiovu na asikifanye, hatalipwa chochote, na kama atakifanya, atalipwa jaza ya kitendo kibaya kimoja tu". Kisha nilishuka chini na nilipompitia Musa(a.s) na kumueleza, alisema: Rudi kwa Bwana wako umuombe tahfifu. Juu ya jambo hili nilisema: "Naona haya kurudi tena kwa Bwana wangu". (Bukhari na Muslim).*

Katika Qur'an sehemu ya safari inagusiwa katika aya zifuatazo:

وَلَقَدْ رَعَاهُ إِذْ نَزَلَ مِنَ السَّمَاءِ نَزْلًا أُخْرَىٰ ۖ ۝١٣ عِنْدَ سِدْرَةِ الْمُنْتَهَىٰ  
 ۝١٤ عِنْدَهَا جَنَّةُ الْمَأْوَىٰ ۖ ۝١٥ إِذْ يَغْشَى السِّدْرَةَ مَا يَغْشَىٰ ۝١٦  
 مَا زَاغَ الْبَصَرُ وَمَا طَغَىٰ ۝١٧ لَقَدْ رَأَىٰ مِنْ آيَاتِ رَبِّهِ  
 الْكُبْرَىٰ ۝١٨

*"Na (Mtume) akamuona (Jibril) mara nyingine (kwa sura yake ya kimalaika katika usiku wa Mi'raj). Penye mkunazi wa kumalizikia (mambo yote). Karibu yake ndio kuna hiyo Bustani (Pepo) itakayokaliwa (daima na hao watu wema). Kilipoufunika mkunazi huo kilichoufunika (katika mambo ya kiajabu ya huko mbinguni). Jicho halikuhangaika wala halikuruka mipaka. Kwa yakini aliona (Nabii Muhammad) mambo makubwa kabisa katika alama za Mola wake". (53:13-18).*

Safari ya Mi'raj kama ilivyoelezwa katika Qur'an na Hadith yaonesha ilikuwa na malengo mawili makubwa.

**Kwanza**, yaonyesha ilikuwa na lengo la kumpa Mtume(s.a.w) mafunzo zaidi juu ya kazi yake kutokana na alama mbali mbali

alizokusudiwa kuonyeshwa na Mola wake. Qur'an inatufahamisha juu ya lengo hili na inatuhakikishia kufikiwa kwake kama ifuatavyo:

..... لِنُرِّيَهُ مِنْ آيَاتِنَا.....

".....li tumuonyeshe baadhi ya alama zetu....." (17:1)

لَقَدْ رَأَى مِنْ آيَاتِ رَبِّهِ الْكُبْرَى ﴿١٨﴾

"Kwa yakini aliona mambo makubwa kabisa katika alama za Mola wake". (53:18).

Mtume(s.a.w) akiwa ni mwalimu wetu na kiigizo chetu, pamoja na kupewa miongozo na kufahamishwa juu ya mambo mbali mbali kwa njia ya wahay kupitia kwa malaika Jibril, bado Mola wake alimtaka aone alama mbali mbali katika mambo ya ghaibu ili ziwe msaada kwake katika kufikisha ujumbe wake kwa watu. Kuona na kutafakari juu ya alama za Allah(s.w) hukomaza zaidi imani ya mja na hivyo humfanya awe madhubuti zaidi katika kufikisha na kusimamisha ujumbe wa Allah(s.w) katika jamii. Izingatiwe kuwa Muhammad(s.a.w) ni Mtume wa mwisho na ujumbe wake unatakiwa udumu mpaka siku ya mwisho. Kwa hiyo Mtume(s.a.w) ilibidi awe madhubuti na mfanyaji kazi zaidi katika kufikisha ujumbe wake kuliko mitume wengine. Si hivyo tu bali alitakiwa ahakikishe kuwa watu wanaupokea na kuuelewa vilivyo ili na wao waufikishe vilivyo kwa watu wengine watakaomendelea na kazi hiyo mpaka siku ya mwisho.

**Pili**, yaonyesha pia safari hii ilikuwa na lengo la kuwatahini watu. Katika hali ya kawaida, ni jambo lisilowezekana kwa mtu kusafiri kutoka Makka hadi Jerusalem kwa masaa machache ya usiku katika enzi hizo ambapo hapakuwa na vyombo vya usafiri vya kileo. Hivyo Mtume(s.a.w) kusafiri hadi Jerusalem na kwenda mbinguni kisha akarejea Makka katika usiku mmoja ulikuwa ni mtihani mkubwa kwa watu, hasa kwa Waislamu, kama wataamini uwezo wa Allah, au la. Asubuhi iliyofuatia usiku wa safari yake,

Mtume(s.a.w) aliwafahamisha watu waliokusanyika katika eneo la Ka'abah kuwa usiku alikwenda Baitul-Muqaddas na kurudi na hakutaka kuwatajia kwanza safari ya mbinguni. Alipowapa habari hii Maquraish wakiwemo baadhi ya waislamu walimzomea na kumwita mwongo. Mara akaja Mut'im bin Adi yule aliyempa Mtume hifadhi ya kukaa Makka, pale alipokataliwa kuingia Makka baada ya safari ya Taif, akamwambia:

*"Muhammad! Mambo yote kabla ya leo yalikuwa mepesi. Ama ya leo uwongo wako ni dhahiri. Mimi nashuhudia kuwa wewe ni mwongo. Baitul Muqaddas tunakwenda na kurudi kwa muda wa miezi miwili, iweje udai kuwa umekwenda huko na kurudi kwa usiku mmoja? Leo mwisho wangu na wewe, huna hifadhi yangu katika mji wa Makka"*<sup>13</sup>

Wakatoka wale Waislamu waliorejea ukafirini (kutokana na safari hii, wakaenda kumhadithia Abubakar juu ya maelezo ya Mtume(s.a.w) juu ya safari yake ili naye apate kurejea ukafirini kama wao. Abubakar akawajibu, *"Kama Muhammad anadai hayo, basi mimi nimemsadiki. Namsadiki kwa habari za mbinguni anazoshushiwa na Allah kila siku, seuze za hapo Baitul-Muqaddas"*? Abubakar alikwenda pale alipokuwa Mtume(s.a.w), akamkuta anaelezea ulivyo msikiti wa baitul-Muqaddas, baada ya kutakiwa afanye hivyo na wapinzani wake waliokuwa wamemzonga pale. Baada ya kumaliza maelezo yake juu ya msikiti wa Baitul-Muqaddas, Abubakar alisema, *"Sadakta, Sadakta"* - umesema kweli, umesema kweli". Kuanzia siku hiyo Mtume(s.a.w) alimpa jina la Abubakar *"al-Saddiq"* - yaani Abubakar *"Msadikishaji kuliko watu wote"*.

Baada ya kuuelezea msikiti wa Baitul-Muqaddas ulivyo, Maquraish walimtaka aeleze juu ya misafara yao, Muhammad(s.a.w)alitoa habari zote za misafara yao na alama alizowaachia wasafiri mahali alipowakuta. Maquraish wakasema

*"Ngojea ikija misafara hiyo na yakathibitika haya unayotueleza, papo hapo tutakuamini sote".* Hata siku ilipokuja misafara hiyo na yakathibitishwa yale aliyoyaeleza Mtume(s.a.w) aliruka Walid bin Mughira akasema, "Wallah" huyu ni mchawi mkubwa, wala hatumuamini mchawi sisi". Wote waliokuwa hapo walisema, *"kasema kweli Walid, sisi hatumwamini mchawi"*.

Safari hii ya Mi'raj, ilikuwa ni kichujio cha kuwatenganisha waumini wa kweli na waumini waliokuwa na ati-ati (wasiwasi) na kuamini uwezo wa Allah(s.w) na sifa zake zote. Kweli hapana linaloshindikana kwa Allah(s.w). Akitaka jambo liwe hauliamrisha *"kuwa"* na likawa ple pale. Mtihani huu haukuishia kwa Waislamu wa wakati ule tu bali mpaka leo hii kuna baadhi ya watu wajiitao waumini wa Allah(s.w), lakini bado hawaamini kuwa safari ya Mi'raj ilikuwa ya kimwili kama ilivyoelezwa katika Qur'an na Hadithi Sahihi. Wao wanadai kama walivyodai Maquraish, kuwa haiwezekani ikawa safari ya kimwili, bali ya kiroho. Maquraysh baada ya ushahidi wa kutosha walidai kuwa safari ile ilikuwa ya kichawi. Je, wale wanaodai kuwa safari ya Mtume(s.a.w) ya Mi'raj ilikwa ya kichawi au ya kiroho, wanaamini kuwa pia hizi television,internet,umeme, safari katika anga na vitu vingine vya kiteknolojia ya hivi leo, navyo ni vitu vya kichawi au vya kiroho?

## **Mtume(s.a.w) Kulingania Uislamu Siku za Hija**

Baada ya Mtume(s.a.w) kupewa amri ya kuutangaza Uislamu kwa wazi, alitumia kila fursa aliyopata katika kufikisha ujumbe wa Allah(s.w) kwa watu. Alianza na jamaa zake wa karibu, Maquraish, wakasilimu wachache na wengi wao wakawa maadui wakubwa dhidi yake na Uislamu. Pamoja na upinzani mkubwa uliokuwepo, Mtume(s.a.w) na Waislamu hawakukata tamaa bali walijaribu kutumia kila fursa iliyopatikana kuufikisha ujumbe wa Uislamu kwa kila ambaye haujamfikia na kuendelea kuwaasa wale uliowafikia lakini hawajaukubali. Katika kutumia fursa, Mtume(s.a.w) aliamua kutumia msimu wa Hija, kufikisha ujumbe wa Uislamu kwa watu wa mbali na Makka.

Tukumbuke kuwa Ibada ya Hija, pamoja na kupotoshwa mafundisho yake, ilikuwa utamaduni wa Waarabu uliodumu tangu wakati wa Nabii Ibrahim(a.s) pale alipoamrisha:

وَأَذِّنْ فِي النَّاسِ بِالْحَجِّ يَأْتُوكَ رِجَالًا وَعَلَىٰ كُلِّ ضَامِرٍ يَأْتِينَ مِنْ كُلِّ فَجٍّ

عَمِيقٍ

*Na (tukamwambia:) “Utangaze kwa watu habari za Hija, watakuja, (wengine) kwa miguu na (wengine) juu ya kila mnyama aliyekonda (kwa machofu ya njiani) wakija kutoka katika kila njia ya mbali; (22:27)*

Hata hivyo, Maquraish hawakumuachia Mtume(s.a.w) kutumia fursa hii. Wakuu wa Maquraish walikutana “**Dar-al-Nadwa**” kuweka mikakati ya kuwazuia wageni (mahujaji) kukutana na Mtume(s.a.w). Waliamua kutuma wajumbe wasimame katika kila njia ya kuingilia Makka kuwatahadharisha wageni kuwa:

*“Mabwana wa Kiquraysh wametutuma kuwaambia kwamba huko Makka kuna mtu jina lake, Muhammad ambaye amezua Dini mpya ambayo wao hawaikiri kuwa ni Dini; na mtu huyo kapewa ufasaha wa kuzungumza usiokuwa na mfano. Humvuta mtu mara moja kwenye Dini yake kiasi cha kumsikiliza tu. Basi Maquraish wanakuhadharisheni na kumsogelea, licha ya kumsikiliza maneno yake. Akitaka kukusemezeni, mfukuzeni na zibeni masikio yenu. Lau kuwa hayo anayosema yangelikuwa kweli, wao wangelikuwa wa kwanza kumfuata, kwani wao wanamjua zaidi kuliko nyinyi.”<sup>14</sup>*

Kila mahujaji walipokuja Mtume(s.a.w) alichukua fursa ile na kuingia kila hema la kila kabila na kuwalingania Uislamu. Lakini hakupata mapokezi mazuri kutokana na ile ilani iliyotangulizwa na wajumbe wa Maquraish. Kila alipojaribu kuzungumza nao walimpuuza. Kila akisema humzomea, hujifunika nguo usoni na kuziba masikio yao ili wasimuone wala kumsikia ili wasije kutekwa

na maneno yake yenye mvuto wa kichawi. Na anapofika mwisho wa mazungumzo yake humuambia:

*“Jamaa zako wanakujua zaidi, nao hawakukufuata. Basi hii ni alama kubwa ya kuwa wewe ni mwongo. Wala sisi hatutaacha Dini ya wazee wetu kwa Sababu yako? Abdul-Muttalib mbona hakuwaambia watu kuwa Dini hii (ya wazee) ni uwongo? Ingekuwa kweli Allah anataka kuleta Mtume, angelipewa Walid bin al-Mughira, Bwana wa Maquraish wote au angelipewa Urwa, Bwana wa Banu Thaqif wote. Unafikiri angelikuletea wewe yatima wa Abdul-Muttalib?”<sup>15</sup>*

Pamoja na mikakati hiyo ya makafiri wa Makka ya kuzuia watu wasiingie Dini ya Allah(s.w), palitokea watu ambao hawakutosheka na ile ilani ya Maquraish, bali waliamua kumsikiliza Mtume(s.a.w) na kujionea wenyewe ukweli wa mambo. Katika mwezi wa Rajab, mwaka wa 11 B.U. sawa na Oktoba 620 A.D walikuja kuhiji Makka watu sita (6) kutoka Yathrib (Madinah), katika kabila la Khazraj. Yathrib wakati huo ilikuwa ikikaliwa na Mayahud na makabila mawili ya Waarabu, Aus na Khazraj. Makabila ya Aus na Khazraj yalipasimiana na yalikuwa katika vita baina yao kwa muda mrefu. Kwa bahati nzuri Mtume(s.a.w) alipita Jamaratul-‘Aqabah, katika mji wa Minaa, akakutana na hao watu sita wa Yathrib. Baada ya Mtume(s.a.w) kuwafikishia ujumbe wa Uislamu na baada ya kuwajibu maswali yao waliyomuuliza, wale watu sita walisilimu wote na wakamuahidi Mtume(s.a.w) kuwa watajaribu wawezavyo kufikisha ujumbe wa Uislamu kwa wenzao wa Yathrib. Walitekeleza ahadi yao na watu wengi wa Yathrib walisilimu.

## **Mikataba ya ‘Aqabah**

Katika Hija iliyofuatia katika mwaka wa 621 A.D, walikuja kama wageni wa Mtume(s.a.w) Waislamu 12 kutoka Yathrib, 10 kutoka katika kabila la Khazraj na 2 kutoka katika kabila la Aus.



Katika hawa 12, Waislamu 5 walikuwa katika wale waliosilimu mwaka uliopita na 7 walikuwa wapya. Walimuomba Mtume(s.a.w) awapelekee mtu wa kuwafundisha Uislamu na kuutangaza Uislamu kwa watu wa Yathrib. Mtume(s.a.w) alikubali ombi lao na akampeleka huko **Mus'ab bin 'Umair**. Baada ya Hija Mtume(s.a.w) aliagana na wale wageni na akawataka watoe ahadi mbele yake kuwa:

*(i) Hawataabudu chochote kingine ila Allah pekee.*

*(ii) Hawataiba wala hawatapokonya misafara njiani.*

*(iii) Hawatazini.*

*(iv) Hawatawaua watoto wao tena.*

*(v) Hawatasema uwongo wala hawatawasingizia watu wengine uovu.*

*(vi) Hawatamuasi Mtume kwa kila atakalowaamrisha na watakuwa waaminifu kwake kwa hali yoyote iwayo.*

Huu unajulikana kama mkataba wa kwanza wa 'Aqabah uliokuwa kati ya Mtume(s.a.w) na wale wageni 12 wa Yathrib. Waliporejea Yathrib walitekeleza ahadi ile na muda si mrefu watu wengi wa kabila la Aus na Khazraj walisilimu.

Labda ni vyema tujiulize ni kwanini waarabu wa Yathrib waliitkia wito wa Mtume(s.a.w) kwa wepesi kiasi hicho ambapo waarabu wengine wote walikuwa wagumu sana. Bila shaka ni kutokana na historia ya Yathrib yenyewe. Tumeona kuwa Yathrib ilikaliwa na mchanganyiko wa Mayahudi na waarabu.

Waarabu wa Yathrib hawakuwa wamezama sana katika kuyaabudu masanamu kutokana na athari ya mafundisho ya Dini ya kiyahudi na baadhi ya waarabu waliacha Dini za wazee wao na kufuata Dini ya kiyahudi. Pia waarabu wa Yathrib walizoea kusikia

kutoka kwa Mayahudi juu ya Utabiri wa kuja kwa Mtume na dalili zake. Hivyo walipokutana na Mtume(s.a.w) na kumuuliza maswali mbali mbali yaliyowapelekea kuhakikisha zile alama za Utume wake na Mtume(s.a.w) akawajibu maswali yao vilivyo, walidhihirikiwa kuwa bila shaka yeye ndiye yule Mtume aliyetabiriwa katika vitabu vya Mayahudi. Ajabu ni kwamba Mayahudi wenyewe hawakumkubali Mtume(s.a.w) na waliungana na washirikina kumpiga vita .

Hija iliyofuatia, mnamo Machi 622 A.D, walimjia Mtume(s.a.w) Waislamu 75 kutoka Yathrib, wawili wakiwa wanawake, wakiongozana na mwalimu wao, Mus'ab bin 'Umair. Baada ya Hija Mtume(s.a.w) alikutana na kikundi hiki cha Waislamu usiku wa manane katika sehemu ya siri nyuma ya mlima. Kutoka Makka Mtume aliongozana na Abubakar, Aly na ami yake Abbas (ambaye alikuwa bado hajasilimu). Mtume(s.a.w) alitoa khutuba ndefu, akiwasomea aya za Qur-an na kuwatofautishia Uislamu na Ukafiri. Kisha akawataka wamuahidi kuwa akienda kwao watamuhifadhi yeye na wafuasi wake kama wanavyowahifadhi watoto wao na wake zao wakati wa vita. Aliposikia ombi hili, **Barq bin Marur**, aliyekuwa mkubwa wao, alisimama na kumhakikishia Mtume(s.a.w) kwa niaba ya watu wake kuwa wako tayari kumlinda Mtume na watu wake. Kabla ya kufunga mkataba wa ahadi ya kumlinda Mtume(s.a.w), Abbas, aliwaomba watafakari na kuelewa vizuri uzito wa ahadi wanayotaka kuichukua na kuwaambia:

*“Enyi watu wa Khazraj! Mnaifahamu nafasi aliyoshika Muhammad hapa kwetu. Tumekuwa tukimlinda na shari za watu wetu kwa kadiri tulivyoweza. Ni mtu mwenye kuheshimiwa sana na wafuasi wake na yuko salama kabisa hapa. Sasa mnataka akaishi nanyi huko kwenu. Kama mnafikiri mnaweza kutekeleza kama mnavyoahidi kwamba mtamlinda kwa namna yoyote iwayo, basi mnaweza kumchukua vinginevyo ni vema mumuache hapa”<sup>16</sup>.*

**Barq bin Marur** alisimama tena na kusisitiza kuwa wako tayari kumlinda Mtume na watu wake kwa nafsi zao, mali zao, wake zao, watoto wao na kwa nyumba zao. Baada ya kutoa ahadi hii kila mmoja katika wale wanaume 73 alimpa Mtume mkono wa ahadi(**Bai’ayah**),Barq akiwa ndiye wa kwanza kumpa Mtume(s.a.w) mkono.

Huu ni mmkataba wa pili wa ‘Aqabah. Kisha Mtume(s.a.w) aliwachagua viongozi 12, 9 kutoka katika kabila la Khazraj na 3 kutoka katika kabila la Aus. Kila kiongozi alimpa ukoo utakaokuwa chini ya uongozi wake. Jukumu kubwa la viongozi hawa lilikuwa kuwafundisha watu Uislamu na kuwaelekeza kuishi Kiislamu. Baada ya hapo walimuaga Mtume na kumsisitizia kuwa wanamngojea yeye pamoja na Waislamu kwa hamu kubwa.

**Mafunzo Yatokanayo na Mikataba ya ‘Aqabah**

Tunajifunza yafuatayo kutokana na mikataba ya ‘Aqabah: **Kwanza**, Waislamu wanapoazimia kufanya jambo au kuchukua njia fulani itakayowapelekea kusimamisha Uislamu hawanabudi kujifunga katika utekelezaji wa azimio hilo kwa kupeana kiapo cha ahadi. Kiapo cha ahadi kitawalazimisha kutekeleza azimio lile wakikumbuka kuwa:

..... إِنَّ الْعَهْدَ كَانَ مَسْئُولًا ﴿٣٤﴾

*Kwa hakika ahadi itaulizwa (Siku ya Kiyama) (17:34)*

إِنَّ الَّذِينَ يُبَايِعُونَكَ إِنَّمَا يُبَايِعُونَ اللَّهَ يَدُ اللَّهِ فَوْقَ أَيْدِيهِمْ فَمَنْ نَكَثَ فَإِنَّمَا يَنْكُثُ عَلَىٰ نَفْسِهِ ۗ وَمَنْ أَوْفَىٰ بِمَا عَاهَدَ عَلَيْهِ اللَّهُ فَمَسْئُولٌ بِهِ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٣٥﴾

*Bila shaka wale wanaofungamana nawe, kwa hakika wanafungamana na Mwenyezi Mungu. Mkono wa Mwenyezi Mungu uko juu ya mikono yao. Basi avunjaye ahadi (hizi) anavunja kwa kudhuru nafasi yake; na atekelezaye aliyomuahidi Mwenyezi Mungu, (Mwenyezi Mungu) atamlipa ujira mkubwa.(48:10)*

Hivyo, kwa kujua uzito wa ahadi, hapana budi kwa kila mwenye kuchukua ahadi ya utekelezaji wa azimio fulani, kuvifahamu vyema vipengele vya azimio hilo, ugumu wa utekelezaji wake na athari yake baada ya utekelezaji kabla hajachukua ahadi ya kulitekeleza. Muislamu asije kujichukulia tu ahadi ya kutekeleza jambo bila ya kujua vyema dhima anayoichukua.

**Pili**, tunajifunza pia kuwa Waislamu wanapopanga mambo yao hawanabudi kuhakikisha kuwa wanayapanga kwa siri ili wasijejulikana kwa maadui zao hata kabla ya kuanza kuyatekeleza. Mtume(s.a.w) alikutana na wale Waislamu 75 kutoka Yathrib katika sehemu ya siri usiku wa manane, si Waislamu wote wa Makkah waliohusika. Makka iliwakilishwa na watu wanne tu, Mtume mwenyewe, Abubakar, Aly na Abbas, wote hawa watatu wakiwa ni wandani wa Mtume(s.a.w)

Usiri huu ulisaidia sana wakati wa kuhamia Madinah. Maquraish walistukia kuhama kwa waislamu baadaye kabisa, baada ya watu wengi kuhama. Kuhama kwenyewe kulifanyika kwa siri sana.

**Tatu**, tunajifunza kuwa katika kusimamisha Uislamu uongozi bora ni kitu cha msingi na cha awali. Tumeona kuwa hata kabla hajahamia Madinah, Mtume(s.a.w) aliteua viongozi wa kumsaidia kuwaweka sawa watu wa Madinah kwa kuwaelimisha juu ya Uislamu na juu ya majukumu yao kama Waislam. Uongozi bora wa Kiislamu ulijenga umoja miongoni mwa watu wa Madinah na hii ilisaidia sana katika kuanzisha Dola ya Kiislam Madinah.

## **Kuhajiri Waislamu wa Makka Kwenda Madinah**

Baada ya mikataba miwili ya 'Aqabah na baada ya Waislamu 75 kufika Yathrib salama, Mtume(s.a.w) aliwaita Waislamu na kuwapa habari njema, akawaambia:

*“Allah(s.w) keshakupeni mahala pazuri pa amani pa kukaa na kuendesha Dini yenu bila ya kuteswa na yeyote. Mahali penyewe ni Yathrib. Nimekwisha pata habari kuwa ndugu zenu wako tayari kukupokeeni kwa hali na mali. Basi kila aliyetayari aondoke leo asingoje kesho, kwani ndugu zenu huko wamesimama mikono wazi, wanangoja kukupokeeni.”<sup>17</sup>?*

Mtume(s.a.w) alitoa amri ya kuhama mnamo April, 622 A.D. mwaka wa 13 B.U na Waislamu katika makundi makundi walianza kuhama kwa siri kuelekea Yathrib. Ili maadui wasije ng’amua kuhama kwao, Waislamu walisafiri usiku na mchana walijipumzisha mafichoni. Walihama na mali ile tu iliyokuwa nyepesi kuchukulika. Vitu vyao vingine vyote waliviacha Makka ikiwa ni pamoja na nyumba zao, vikachukuliwa na jamaa zao waliobakia katika ukafiri. Ni ‘Uthman bin Affan peke yake aliyeweza kuchukua mali yake yote. Mali ya ‘Uthman isiyochukulika ilinunuliwa na jamaa zake kwa fedha taslimu.

Baada ya miezi miwili hivi, takriban Waislamu wote walikwisha hamia Yathrib. Waislamu wachache, akiwemo Abubakar na ‘Ali bin Abu Talib, walibakia Makka na Mtume(s.a.w) ili kufanikisha maandalizi ya kuhama kwake pale atakapopewa ruhusa ya kuhama na Mola wake.

## **Hijra ya Mtume(s.a.w) Kwenda Madinah**

### ***Njama za Kumuuu Mtume(s.a.w)***

Maquraish walikasirika sana walipogundua kuwa takriban Waislamu wote wameshamia Yathrib na walihofia kuwa wakimwacha Muhammad naye akahamia Yathrib, atajiimarisha na Uislamu utakita mizizi. Hata hivyo, tetesi kuwa Mtume naye atahamia Yathrib zilishaenea miongoni mwa Maquraish, ikabidi wakutane waamue la kufanya kabla jambo hilo halijatokea. Abu Jahl, adui mkubwa wa Uislamu, aliitisha mkutano wa vijana 14 wa koo zote za Quraysh isipokuwa vijana wa Banu Hashim tu. Katika

mkutano wao huo uliofanyika katika “Dar al-Nadwa”, yalitolewa mapendekezo yafuatayo dhidi ya Muhammad(s.a.w)

- (1) Wamfunge Mtume peke yake katika chumba
- (2) Wamzibe mcho na wamfunge mikono barabara kisha wampandishe juu ya ngamia aliyetiwa vitunga vya kuziba macho, aachwe ahangaike naye jangwani mpaka afe kwa kiu, njaa na jua kali.
- (3) Mtu mmoja ampige panga ya shingo amuulie mbali
- (4) Wachaguliwe vijana watukufu kutoka katika kila tumbo la Quraish kisha kila mmoja apewe upanga mkali; wakusanyike alfajiri moja makhsus wamuue wote kwa pamoja, ili lawama ziangukie koo zote za Quraish. Hapo Banu Hashim hatakuwa, na la kufanya ila kupokea diya tu.

Hizi ndizo njama za Maquraish dhidi ya maisha ya Mtume(s.a.w) ambazo pia zinabainishwa katika Qur-an:

وَإِذْ يَمْكُرُ بِكَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِيُثْبِتُوكَ أَوْ يَقْتُلُوكَ أَوْ يُخْرِجُوكَ  
وَيَمْكُرُونَ وَيَمْكُرُ اللَّهُ وَاللَّهُ خَيْرُ الْمَكْرِينَ ﴿٣٠﴾

“Na (kumbuka Ee Muhammad) walipokufanyia hila wale waliokufuru ili wakufunge au wakuue au wakutoe (Makkah kwa namna mbaya); na wakafanya hila (za barabara). Na Mwenyezi Mungu akapindua hila hizo. Na Mwenyezi Mungu ni mbora wa kupindua hila (za watu wabaya)”. (8:30)

Walikubaliana na ile rai ya nne, wakachaguliwa vijana watukufu kutoka kila ukoo wa kabila la Quraish na wakaizunguka nyumba ya Mtume(s.a.w) usiku ili akitoka alfajiri wamvamie wote kwa pamoja.

Katika mchana ule ambao usiku wale vijana wa Kiquraish waliazimia kumuua Mtume(s.a.w), alikuja Jibril(a.s)akamueleza

Mtume(s.a.w) njama za Maquraish dhidi yake na akampa amri ya kuhamia Yathrib katika usiku ule ule. Pale pale Mtume alimwendea Abubakar na kumfahamisha kuwa safari imeshawiva na atampitia usiku wa manane waende zao.

Mtume(s.a.w) na Abubakar walishaandaa safari kabla ya amri hii ya kuhama. Walishapanga njia watakayopita na pango watakamojificha katika siku za kutafutwa. Walipanga kukaa siku tatu pale pangoni, Abubakar alikwisha nunua ngamia wawili kwa ajili ya safari; alimchukua binti yake mkubwa, Asma, kwa siri mpaka kwenye pango la Thawr mahali watakapojificha ili awalettee chakula humo usiku usiku; aliamuru mchungaji wake wa mbuzi, Bwana Amr bin Fuhayra awe akiwaletea maji na maziwa kwenye hilo pango; aliamuru mwanawe mdogo, Abdallah, awalettee habari yoyote itakayowahusu watakapokuwa pangoni na alisha mkodi Bedui mmoja, Abdullah bin Uraiqit, kwa dinar 300, atakayewaongoza kwenda Yathrib kwa njia ya siri isiyotumiwa na yeyote.

Mtume baada ya kutoka kwa Abubakar, alimwita Aly bin Abu Talib, akamfahamisha habari ya safari yake na akamkabidhi amana zote za watu alizokuwa nazo ili azirudishe kwa wenyewe na akamtaka alale kitandani mwake. Pamoja na kujua kuwa Mtume(s.a.w) atazingirwa usiku ule ili auawe, 'Ally alilala mle kitandani mwake badala yake bila ya wasiwasi wowote.

Wakati wa kuondoka ulipofika, Mtume(s.a.w) alitoka nje akawakuta maadui zake wamelala fofofu, akawanyunyizia mchanga vichwani mwao, huku akisoma Surat Yaasin, aya ya 1-9, kisha akaondoka zake salama salimini. Ieleweke hapa kuwa kilichomkinga Mtume(s.a.w) si Surat Yaasin kama wengi wanavyoitakidi bali anayemkinga mja na janga lolote lile ni Allah(s.w). Bila shaka Mtume(s.a.w) alisoma aya hizo ili kujikumbusha na kujiliwaza kutokana na ujumbe unaopatikana humo. Mtume(s.a.w) hakuwa na wasiwasi wowote kwa kuwa alikuwa na yakini juu ya ulinzi wa Allah(s.w).

Baada ya kutoka nyumbani kwake, Mtume(s.a.w) alimpitia Abubakar wakaanza safari yao mpaka kwenye pango la mlima Thaur lililopo maili mbili kusini mwa Makka.

Huko Makka, Maquraish walipoona njama yao haikufanikiwa walikasirika sana wakawa wanakwenda huku na kule katika harakati za kumtafuta Mtume(s.a.w). Kabla hawajaenda mbali walipita kwa Abubakar wakakuta naye hayupo. Wakaamua kumkodi Bedui mmoja **Abu Kurz al-Khizai**, aliyekuwa hodari sana wa kutafuta nyayo za mwenye kutafutwa. Wakafuata nyuma yake wakaikagua Makka yote. Hatimaye aliweza kuitambua njia waliyoifuata Mtume(s.a.w) na mwenzake, wakaanza kutafuta kwa hadhari kubwa hata wakapanda juu ya ule mlima wenye pango walimojificha Mtume(s.a.w) na Abubakar. Walipofika juu, yule Bedui mfuata nyayo, aliwaashiria kwenye lile pango lililokuwa kiasi cha futi 40 hivi kutoka pale walipo. Abubakar alipowaona wamewakaribia kiasi kile alipatwa na wasi wasi kuwa labda wataonekana. Mtume alimtuliza na kumwambia:

..... لَا تَحْزَنُ إِنَّ اللَّهَ مَعَنَا .....<sup>ط</sup>

.....*Usihuzunike, kwa yakini Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi.....*”  
(9:40).

Vijana wa Kiquraish walipotaka kuliendea lile pango, Umayyah bin Khafaf, mmoja wa mabwana wakubwa wa kiquraish, alipiga kelele kwa ukali na hasira akasema,

*“Hamna akili nyinyi kama huyu tuliyepoteza fedha zote kumkodi? Vipi mtu ataweza kupita katika pango lile pasina kuharibu utando wa mabubui wale waliotanda pale, au vipi njiwa wataweza kukaa pale na kulalia mayai yao ikiwa pana mtu ndani ya pango lile? Wallah! Mabuibui wamelitanda pango hili hata kabla ya kuzaliwa mwenyewe Muhammad! Hajui chochote mfuataji huyu”.*



Ukweli ni kwamba buibui na njiwa wale hawajakuwepo zamani kama anavyodai Humayyah bali wote walikuja alfajiri ya siku ile ili wapate kuwaziba macho Maquraish wasimwone Mtume na mwenzake. Buibui na njiwa walikuwa miongoni mwa askari wa jeshi la Allah(s.a.w) katika kumnusuru Mtume na Dini yake kama anavyotukumbusha katika Qur-an:

إِلَّا تَنْصُرُوهُ فَقَدْ نَصَرَهُ اللَّهُ إِذْ أَخْرَجَهُ الَّذِينَ كَفَرُوا  
ثَانِيًا أَتَيْنِي إِذْ هُمْ فِي الْغَارِ إِذْ يَقُولُ لِصَاحِبِهِ لَا تَحْزَنْ إِنَّ اللَّهَ  
مَعَنَا فَأَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَيْهِ وَأَيَّدَهُ بِجُنُودٍ لَمْ تَرَوْهَا  
وَجَعَلَ كَلِمَةَ الَّذِينَ كَفَرُوا السُّفْلَىٰ وَكَلِمَةُ اللَّهِ هِيَ الْعُلْيَا وَاللَّهُ

*“Kama hamtamnusuru (Mtume) basi Mwenyezi Mungu alimnusuru walipomtoa wale waliokufuru, alipokuwa (mmoja tu na mwenziwe) wa pili wake (peke yake); walipokuwa wote wawili katika pango; (Mtume) alipomwambia sahibu yake: ‘Usihuzunike, kwa yakini Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi. Mwenyezi Mungu akamteremshia utulivu wake, na akamnusuru kwa majeshi msiyoyaona, na akafanya neno la wale waliokufuru kuwa chini, na neno la Mwenyezi Mungu ndilo la juu. Na Mwenyezi Mungu ndiye anayeshinda na ndiye mwenye hekima”. (9:40).*

Maquraish walipokata tamaa kuwa hawataweza kumuona Mtume(s.a.w) katika viunga vya Makka walitangaza kuwa atakayemleta Muhammad akiwa hai au akiwa amekufa atapata zawadi ya ngamia 100.

Mtume(s.a.w) na Abubakar walibaki mle pangoni kwa muda wa siku tatu kisha waliendelea na safari yao ya Yathrib na mambo yakaenda kama walivyopanga. Katika msafara wa kwenda Yathrib Mtume(s.a.w) aliongozana na Abubakar, huru wa Abubakar, Bwana Amir bin Fuhayra, na yule Bedui aliyekodiwa kuwa mwongozaji wa msafara.

Huko Makka kila shujaa alikwenda huku na kule kumtafuta Muhammad ili aweze kujipatia ile zawadi nono ya ngamia 100. Shujaa mmoja **Suraqah bin Malik** alifanikiwa kuufuatia msafara wa Mtume(s.a.w), lakini kabla hajaukaribia farasi wake alijikwaa akaanguka. Alijaribu kumuinua na kuendelea kumfuatilia lakini farasi wake alianguka tena. Akamuinua tena na kukazana tena kuwakimbilia lakini farasi wake alijikwaa tena na safari hii miguu yake ilizama ardhini akazuiliwa, hawezi kuchopoka. Ilipofikia hali hiyo, Suraqah alipiga makelele ya kuomba amani na Mtume akampa.

Pale pale akachopoka akasimama pembezoni mwa Mtume na kuwaambia, “Mimi nina yakini kuwa jambo lako hili litaenea Bara Arab yote. Basi naomba unipe barua yako ambayo nikimuonyesha mtu yoyote atanipa amani na atanisaidia “. Mtume alimuamuru, Amir bin Fuhayra amuandikie barua hiyo ya amani. Suraqah alirejea Makkah na walipokutana na Abu Jahl alimpa habari juu ya yote yaliyomtokea na akamtaka Abu Jahl asilimu kama yeye alivyosilimu baada ya kuyakinisha kuwa kweli Muhammad ni Mtume wa kweli. Abu Jahl alimshangaa akamwambia; “masikini Roho yako! ndio kwanza sasa unajua kwamba Muhammad ni Mtume wa Haki?”

Mimi tangu zamani najua kuwa yeye ni Mtume wa Haki lakini sitaki kumfuata tu. Kwa nini kila utukufu wawe nao Banu Hashim peke yao? Banu Hashim wanatoa watukufu na sisi Banu Makhzum tunatoa: wanatoa mashujaa na sisi tunatoa. Hata leo farasi wao na wetu wanagusana magoti kwa kukaribiana, anatokea kwao Mtume aliyeletwa na Allah! wallah sitamfuata! Tutapata wapi Mtume wa kumlinganisha na wao? Kwa hiyo sitamuamini. Kwanini wakapewa cheo hiki Banu Hashim peke yao?

## **Mafunzo Yatokanayo na Hijra ya Mtume(s.a.w) na Maswahaba zake**

Kutokana na Hijira ya Madinah ya Mtume(s.a.w) na maswahaba zake tunajifunza yafuatayo:

- (i)Tunaona umuhimu wa kutunza na karejesha amana kwa wenyewe. Pamoja na mazingira yale ya hatari bado Mtume(s.a.w) alimbakisha Ally(r.a) ili arudishe amana za watu.
- (ii)Ni muhimu kuweka mipango ya mambo tunayotaka kuyafanya kabla ya utekelezaji. Mtume(s.a.w) na Abubakar(r.a) wasingaliweka mpango wa safari yao mapema wangelikwama.
- (iii)Hatunabudi kuchukua tahadhari katika kuendea harakati za kiislamu tukizingatia kuwa dini hii ina maadui wengi.
- (iv)Baada ya kuchukua tahadhari kwa kadiri ya uwezo wetu, tujitegemeze (tutawakal) kwa Allah(s.w) kwani ahadi ya kuwanusuru wanaonusuru dini yake ni ya kweli.(Qur-an 47:7)
- (v) Waislamu wanalazimika kufanya jitihada za makusudi za kuusimamisha Uislamu katika jamii ili waweze kumuabudu Allah(s.w) katika kila kipengele cha maisha yao ya kibinafsi na ya kijamii.
- (vi)Kama Waislamu baada ya kujitahidi mwisho wa uwezo wao, watahindwa kupata mazingira yatakayowawezesha kuishi Kiislamu katika kila kipengele cha maisha, hawana budi kuhajiri kwenye eneo lingine katika ardhi ambapo wataweza kumuabudu Mola wao vilivyo.Vinginevyo hawatakuwa na udhuru mbele ya

Allah(s.w) kama tunavyojitunza katka aya zifuatazo:

إِنَّ الَّذِينَ تَوَفَّيْنَاهُمْ لَمَلَكَةٌ ظَالِمِي أَنْفُسِهِمْ قَالُوا فِيمَ كُنْتُمْ قَالُوا كُنَّا  
 مُسْتَضْعَفِينَ فِي الْأَرْضِ قَالُوا أَلَمْ تَكُنْ أَرْضَ اللَّهِ وَسِعَةً فَتُهَاجِرُوا فِيهَا  
 فَأُولَئِكَ مَا لَهُمْ جَهَنَّمُ وَسَاءَتْ مَصِيرًا ﴿٩٧﴾ إِلَّا الْمُسْتَضْعَفِينَ  
 مِنَ الرِّجَالِ وَالنِّسَاءِ وَالْوِلْدَانِ لَا يَسْتَطِيعُونَ حِيلَةً وَلَا يَهْتَدُونَ  
 سَبِيلًا ﴿٩٨﴾ فَأُولَئِكَ عَسَى اللَّهُ أَنْ يَعْفُوَ عَنْهُمْ وَكَانَ اللَّهُ عَفُورًا غَفُورًا ﴿٩٩﴾

*"Wale ambao Malaika wamewafisha, hali wamedhulumu nafsi zao, (kwa kutohajiri; Malaika) watawaambia: "Mlikuwa katika hali gani (katika jambo la dini yenu?" watasema: "Tulikuwa madhaifu katika ardhi hiyo (kwa hivyo hatukuweza kufanya ibada yetu Malaika watasema: "Ardhi ya Mwenyezi Mungu hakuwa na wasaa na nyinyi kuhamia humo?" Basi hao makazi yao ni Jahanamu; nayo ni marejeo mabaya kabisa. Isipokuwa wale waliokuwa madhaifu kweli; katika wanaume na wanawake na watoto wasio na uweza wa hila yoyote wala hawawezi kuongoza njia (kwenda Madina) Basi hao huenda Mwenyezi Mungu akawasamehe; Mwenyezi Mungu ni mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kughufiria. (4:97-99)*

- (vii) Kuhajiri sio ukimbizi bali ni kuhamia sehemu nyingine yenye mazingira yatakayo wezesha kusimamisha Uislamu pale na kupata nguvu ya kusimamisha Uislamu kule mlipotoka na sehemu nyingine ambapo uislamu hauja simama. Ikumbukwe kuwa Waislamu wa ummah huu wana dhima ya kusimamisha Uislamu kote ulimwenguni.
- (viii) Hijra ya Madinah inatupa funzo la wazi kuwa Waislamu ni ndugu moja bila ya kujali ukabila, utaifa, rangi, n.k.
- (ix) Uislamu hautasimama mpaka Waislamu wewe tayari kujitoa muhanga kwa mali zao na nafsi zao. **Muhajirina** waliacha makazi yao waliyoyazoea, majumba yao na kila chao wakaenda watupu kwenye makazi mapya ya ugenini. **Ansari** nao waliwanusuru ndugu zao kwa mali zao na makazi yao.

- (x) Muislamu ni haramu kabisa kuishi katika nchi ya kikafiri ila kwa sababu mbili tu; moja, iwapo yupo katika juhudi za kuondoa ukafiri na kuutawalisha Uislamu, pili, iwapo yumo katika matayarisho ya kufanya Hijra (kuhama).

## **MTUME(S.A.W) KUSIMAMISHA DOLA YA KIISLAMU MADINAH**

Safari ya Mtume(s.a.w) na sahibu wake, Abubakar na wale walioandamana nao, ilichukua siku 7 na waliwasili Quba siku ya Jumatatu mwezi 18 Rabi al-awwal sawa na 20 Septemba, 622 A.D. Quba ni kimji kilichopo maili tatu au kilomita 4.8 kusini mwa mji wa Yathrib (Madinah). Waislamu wote wa Yathrib, wakubwa kwa wadogo, wake kwa waume, walimiminika kwenda kumpokea Mtume(s.a.w) kwa shangwe na furaha kubwa. Mtume(s.a.w) alijipumzisha Quba kwa muda wa siku nne katika nyumba ya Bwana Kulthum bin Hadm, mkubwa wa Banu Amr katika kabila la Aus. Bwana huyu hakuwa amesilimu, bali alisilimu katika siku hizo alizokaa na Mtume wa Allah.

Baadaye Waislamu walipendekeza kuwa tarehe ya Kiislamu ianzie pale Waislamu walipoanza kuhamia Madinah, mpaka sasa hivi tunahesabu tarehe ya Kiislamu kuanzia kipindi hicho na tunatofautisha na miaka ya Kikristo kwa kuongeza A.H. (Al-Hijra) mbele ya mwaka wa Kiislamu.

## **Kujengwa Msikiti wa Quba**

Katika siku ya pili ya kukaa kwake Quba, Mtume(s.a.w) aliamuru kujengwe msikiti katika uwanja uliotolewa na mwenyeji wake, bwana Kulthum bin Hadm. Mtume mwenyewe alishiriki katika kujenga msikiti huu wa kwanza. Aliwaachia Waislamu wa pale kuumaliza alipoondoka kuelekea mjini Yathrib. Msikiti huu umetajwa katika Qur'an kwa heshima kubwa kama ifuatavyo:

..... لَمَسَّجِدٍ أُسِّسَ عَلَى التَّقْوَىٰ مِنْ أَوَّلِ يَوْمٍ أَحَقُّ أَنْ تَقُومَ

فِيهِ فِيهِ رِجَالٌ يُحِبُّونَ أَنْ يَتَطَهَّرُوا وَاللَّهُ يُحِبُّ الْمُطَهَّرِينَ ﴿١٠٨﴾

*"..Msikiti uliojengwa juu ya msingi wa Ucha-Mungu tangu siku ya kwanza (ya kufika Mtume Madinah) unastahiki zaidi wewe usimame humo. Humo wamo watu wanaopenda kujitakasa. Na Mwenyezi Mungu anawapenda wajitakasao." (9:108)*

Kila mara Mtume(s.a.w) alikuwa akiuzuru msikiti huu kama tunavyofahamishwa katika Hadhith:

*"Ibn 'Umar ameeleza kuwa Mtume wa Allah alikuwa akiuzuru msikiti wa Quba kwa miguu au akiwa juu ya mnyama, kila Jumamosi na alikuwa akiswali huko raka mbili." (Bukhari na Muslimu).*

Ujenzi wa msikiti kuwa ndilo jambo la kwanza alilolifanya Mtume(s.a.w) mara tu ya kuingia Madinah, inatupa picha juu ya umuhimu na nafasi ya msikiti katika Uislamu.

### **Yathrib Inakuwa Al-Madinah al-Munawwarah**

Siku ya Ijumaa, mwezi 22 Rabi 'al-awwal sawa na 24 Septemba, 622 A.D, Mtume(s.a.w) aliondoka Quba kuelekea Yathrib. Swala ya Ijumaa ilimkuta njiani katika sehemu ya Banu Salim, ambapo alishuka na kuswali swala hiyo pamoja na Waislamu wote waliokuwa panoja naye. Hii ilikuwa ndio swala ya kwanza ya Ijumaa. Mtume(s.a.w) na Waislamu hawakuwa wakiswali swala hii walipokuwa Makka. Khutuba yake ya Ijumaa hii ya kwanza ilizivuta na kuziteka sana nyoyo za wakazi wa Yathrib. Mtume(s.a.w) aliitoa hutuba yake kama ifuatavyo:

*Kila sifa njema zinamstahikia Allah, ninamtakasa, nataka Msaada wake, Msamaha wake na Mwingozo wake.*

*Ninamuamini Yeye, wala simkufuru. Nashuhudia kuwa Muhammad ni mja wake na Mtume wake. Amemtuma na mwongozo, Imani ya kweli, mwanga na hekima na akamtuma kwa watu katika wakati ambapo Mitume wamekoma kuja na watu wamesahau mafundisho ya Mitume waliotangulia na hivyo wakawa ni wenye kupotea.*

*Kiyama kinakaribia na inakaribia siku ya malipo. Yeyote anayemtii Allah na Mtume wake hupata uongofu na anayekataa kuwatii, hupotea upotevu wa mbali. Nawausia kumcha Mwenyezi Mungu. Kwani ushauri mwema kuliko ushauri mwingine wowote ambao muislamu angeweza kumpa ndugu yake Muislamu ni kumuusia akumbuke maisha ya akhera na kumtaka amche-Mwenyezi Mungu. Hapana ukumbusho (mawaidha) ulio bora kuliko huu na hakuna kukumbuka kuliko bora kuliko huku. Hakika kumuogopa Allah kwa kutenda na kuchunga mipaka ya Allah, ni nyenzo ya kweli ya kukupelekea kupata maisha mazuri ya akhera. Yeyote yule anayeteteleza lile lililo kati yake na Allah, kwa siri au kwa dhahiri, kwa tegemeo tu la kupata radhi za Allah, atapata heshima katika muda mfupi ujao na atapata malipo makubwa huko akhera ambapo mwanaadamu atahitajia kupata kila amali njema aliyoichuma na atatamani kuwa mbali na amali nyingine yoyote ile.*

*Allah anawatanabahisha juu yake na Allah ni mpole kwa waja wake. Yeye ni yule ambaye maneno yake ni ya kweli na yule atetelezaye ahadi yake. Hapana mabadiliko katika ahadi yake na hakika amesema: "Neno langu halibadiliki na mimi si dhalimu kwa waja! Kwa hiyo muogope Allah katika mambo yako sasa na baadaye yakiwa ya siri au ya wazi. Kwani kwa yule amuogopaye Allah, Allah atamsamehe dhambi zake na kukuza malipo yake. Yeyote yule amuogopaye Allah atafuzu kufuzu kukubwa. Hakika kumcha-Allah (kumuogopa Allah) kutakupepusha na ghadhabu zake na kutakuweka mbali na adhabu yake na laana yake. Na hakika kumuogopa Allah kunaung'arisha uso, kunamridhisha*

*Allah na kunapandisha daraja.*

*Kwa hiyo, kamata sehemu yako na usichupe mipaka katika dini ya Allah ambayo amekufundisheni kwa kuwaletea kitabu na amewaandalia njia (amekuongozeni katika njia) inayokufikisheni kwake, ili awatambue waumini wa kweli na wale wasioamini.*

*Kwa hiyo, fanya wema kama Allah alivyokufanyia wema. Kuwa katika uadui na maadui zake na pigana katika njia ya Allah kama inavyostahiki. Ni yeye aliyekuchagueni na kukuiteni Waislamu, ili wale wanaotaka kuangamia waangamie baada ya kuwafikia dalili zilizowazi. Hapana hila wala nguvu, ila itokanayo na Allah. Na ili wale wanaoishi baada ya kuwafikia dalili zilizo wazi wazi waishi. Hapana hila wala nguvu ila itoknayo na Allah.*

*Hivyo mkumbukeni Allah mara kwa mara kwa kadiri ya uwezo wenu na jiandaeni kwa maisha ya Akhera. Kwani anayetengeneza yake yaliyo baina yake na Allah(s.w), atamtosheleza kwa yale yaliyo kati yake na watu. Hii ni kwa sababu mamlaka ya Allah yako juu ya watu na wao hawana nguvu yoyote juu yake. Allah ni mkubwa, na hapana uwezo au nguvu, ila itokanayo na Allah, Aliye juu, Aliye Mkuu".<sup>18</sup>*

Hutuba hii ya mwanzo katika kipindi cha Madinah imesisitiza Waislamu kumcha-Allah(s.w) na kupigania dini yake kwa matarajio ya kupata malipo mema ya huko akhera. Pamoja na maudhui ya hutuba hii pia tunapata funzo la tabia anayotakakiwa awe nayo mlinganiaji Uislamu. Kwa kipindi cha miaka 13 Mtume(s.a.w) aliteseka sana kutokana na vitimbi vya maquraish, ikiwa ni pamoja na kumtukana na kumkatisha tamaa, kumpiga, kumtenga na kula njama za kumuua. Mateso yote haya hayakumfika kwa kosa lolote lile zaidi ya kuwaita watu kwenye dini ya Allah(s.w). Kutokana na mateso aliyopata yeye na Waislamu waliokuwa pamoja naye, kibinaadamu baada ya kupata makazi ya salama, Mtume(s.a.w) angetegemewa aseme lolote juu ya maovu aliyofanyiwa katika hutuba yake hii ya kwanza. Lakini twaona katika hutuba hii Mtume(s.a.w) hakutoa neno lolote la ukali wala la shutuma dhidi ya



makafiri wa Makka. Si hivyo tu, hakuzungumzia kabisa lolote lililomhusu yeye kama Muhammad (kama mtu binafsi). Muda wake wa hutuba aliutumia katika kuwahimiza watu wamuamini Allah na kumcha inavyostahiki, wapigania dini ya Allah kwa kutarajia malipo ya akhera.

Jambo la kuzingatia hapa ni kuwa Muislamu katika kuufikisha ujumbe wa Allah kwa watu anatakiwa ajali zaidi kuona ujumbe unawafikia watu kuliko kujali hali yake binafsi. Kama kudhurika Muislamu binafsi kutakuwa ndio sababu ya kufanikisha kazi ya kuufikisha ujumbe wa Allah, basi hanabudi kujitoa muhanga kuikabili dhana hiyo.

Baada ya swala ya Ijuma Mtume(s.a.w) aliendelea na safari yake. Kila ukoo ulimkaribisha Mtume akakae kwao, lakini aliwajibu kwa wema kuwa mahali atakaposhukia pameelekezwa na Allah(s.w) na ni pale atakaposimama ngamia wake. Mtume(s.a.w) alipokaribia kufika pale mahali palipokusudiwa, aliachia huru khatamu za ngamia wake ili aende mwenyewe mpaka alipoelekezwa na Mola wake. Ngamia wa Mtume alisimama mbele ya nyumba ya Abu Ayyub Ansari ambapo mbele yake palikuwa na kiwanja kikubwa kilichokuwa wazi. Kiwanja hicho kilikuwa cha yatima wawili, Sahl na Suhail. Mtume(s.a.w) aliamuru kiwanja hicho kununuliwe baada ya kukubaliana na wenyewe kwa ajili ya msikiti na makazi yake.

Abu Ayyub alifurahi sana kushukiwa na bahati hiyo ya kuchaguliwa na Allah(s.w) kukaa pamoja na Mtume wake. Alimpokea Mtume kwa furaha na alijitahidi kumtendea Mtume kila linalomfurahisha. Nyumba yake ilikuwa na ghorofa moja na akamuomba sana Mtume akae sehemu ya juu. Mtume(s.a.w) alimtaka radhi na kumwambia kwamba yeye mwenye nyumba ndiye mwenye kustahiki zaidi kukaa sehemu ya juu, pia alipendelea sehemu ya chini kwa ajili ya urahisi wa kuwapokea wageni wake tukizingatia kuwa nyumbani kwake sasa ndio ikulu ya

muda. Mtume(s.a.w) alikaa kwa Abu Ayyub kwa kipindi cha miezi saba, baada ya ujenzi wa msikiti na nyumba za Mtume kukamilika. Alikaa kwa Abu Ayyub na familia yake ikiwa ni pamoja na mkewe, Bibi Sauda (aliyemuoa akiwa Makka baada ya kufariki Bibi Khadijah) na binti zake, Fatimah na Umm Kulthum.

Tokea siku ile Mtume(s.a.w) alipoanza kuishi mjini Yathrib mji huo ulipewa majina mapya. Kuanzia pale uliitwa **Madinatun-Nabii** (mji wa Mtume) na **al-Madinah al-Munawarah** (mji ung'arao). Hivi sasa inajulikana kwa ufupi kama mji wa "**Madinah**".

## **Mambo ya Msingi Aliyofanya Mtume(s.a.w) Katika Kuanzisha Dola ya Kiislamu Madinah.**

Mtume(s.a.w) alipofika Madinah alitumia fursa ile ya mazingira ya amani na kuanzisha Dola ya kiislamu kwa kufanya yafuatayo:

- (i) Kujenga msikiti wa Madina
- (ii) Kujenga ummah wa kiislamu
- (iii) Kuweka mkataba wa Madinah(Madina Cherter)
- (iv) Kuweka mikataba ya amani na makabila ya Kiyahudi pembezoni mwa Madinah.
- (v) Kuandaa Ummah kijeshi na kiusalama.
- (vi) Kuimarisha uchumi.
- (vii) Kuunda(kuanzisha) sekretarieti.
- (viii) Kuteua shura.

### **(i) Kujenga Misikiti wa Madinah**

Jambo la kwanza alilolifanya Mtume(s.a.w) alipoingia Madinah ni kujenga msikiti uliojulikana kwa jina la "**Msikiti wa Mtume**" au "**msikiti wa Madinah**". Msikiti ulijengwa katika uwanja

ulionunuliwa kutoka kwa yatima mawili, Sahl na Suhail. Mtume(s.a.w) alipowaeleza vijana hawa juu ya nia yake ya kutaka kununua uwanja wao, si tu kwamba walikubali kwa furaha, bali walimtaka Mtume(s.a.w) awakubalie wautoe bure. Mtume(s.a.w) hakukubali ombi lao, bali alimuamuru Abubakar anunue uwanja ule kwa niaba yake.

Msikiti wa Mtume(s.a.w) ulitumika kwa kazi nyingi. Ulitumika kama mahali pa kuswalia swala za jamaa, darasa, Ikulu ya Mtume, Mahakama, ukumbi wa bunge (shura), kituo cha jeshi, mapokezi ya wageni, makazi ya maskini, n.k. Kwa ufupi **Msikiti wa Mtume** ulikuwa kituo cha harakati za kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii.

## **(ii) Kujenga Ummah wa Kiislamu**

Kabla ya Hijira, Yathrib ilikaliwa na Mayahud na Waarabu wa Kabila la Aus na Khazraj. Aus na Khazraj daima walikuwa katika uhasama na vita visivyokatika wakichochea na Mayahud ili waweze kuwa juu yao na kuwanyonya kiuchumi. Baada ya Aus na Khazraj kuwa Waislamu, walisahau kabisa tofauti zao zote na wakashikamana pamoja na kuwa kundi moja la **Answar** (wenye kunusuru Uislamu) kama Mtume(s.a.w) alivyowaita. Hali kadhalika watu wa Makka nao waliposilimu walitupilia mbali ukabila na kushikamana na udugu wa Kiislamu. Waislamu wa Makka walipohamia Madinah, kama kundi waliitwa **Muhajirina** (waliohamia).

Baada ya ujenzi wa msikiti, jambo la pili alilolishughulikia Mtume(s.a.w), ni namna ya kutatua tatizo la kiuchumi lililokuwa likiwakabili Muhajirin. Takriban Waislamu wote waliohamia kutoka Makkah walikuwa na hali mbaya kiuchumi kwa vile nyumba zao na mali yao nyingi isiyochukulika ilibakia Makkah. Hivyo wengi wa Muhajirina walifika Madinah wakiwa masikini hohe-hahe. Hawakuwa na makazi, chakula, nguo na mahitaji mengine muhimu ya maisha. Mtume(s.a.w), akiwa kiongozi mweledi wa Dola ya

Kiislamu, aliona utatuzi pekee wa tatizo hili ni kuuingiza udugu wa Kiislamu katika matendo. Aliwakusanya Muhajirina wote na akachagua wanaojiweza kidogo kiuchumi miongoni mwa Answar kiasi cha ile idadi ya Muhajirina. Kisha akapiga kura na kila mmoja katika wale Answar likamuangukia jina la mmoja wa Muhajir ili awe ndugu yake wa Kidini. Udugu huu wa Kidini uliofungamana na mapenzi na huruma ulikuwa mzito kuliko udugu wa damu kiasi kwamba ndugu wa upande wa Answar alikuwa radhi kutoa nusu ya kila alichomiliki ampe ndugu yake wa upande wa Muhajirina kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*“Amesimulia Anas (r.a), Abdur-Rahman bin ‘Auf alipokuja kwetu (Madinah) Mtume wa Allah aliunganisha udugu baina yake na Sa’d bin Ar-Rabi aliyekuwa tajiri: Sa’d akasema: Answar wananifahamu kuwa mimi ni tajiri mkubwa kuliko wao wote, hivyo nitagawanya mali yangu katika sehemu mbili, yako na yangu, na nina wake wawili, chagua umpendaye, Ili nimpe talaka na baada ya kipindi cha eda umuo” Abdur-Rahman alisema: “Allah akubariki wewe na familia yako (wake zako). (Badala yake aliomba aonyeshwe sokoni akafanye biashara) alikwenda kufanya biashara sokoni na siku ile akarudi na faida ya mkate wa Yoghurt na siagi...” (Sahih na Bukhari).*

Hadithi hii ni kielelezo cha ukarimu wa Answar kwa ndugu zao Muhajirina na Allah(s.w) amewasifu kwa ukarimu wao huo katika aya zifuatazo:

لِلْفُقَرَاءِ الْمُهَاجِرِينَ الَّذِينَ أُخْرِجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ وَأَمْوَالِهِمْ يَبْتَغُونَ

فَضْلًا مِنَ اللَّهِ وَرِضْوَانًا وَيَنْصُرُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ أُولَئِكَ هُمُ الصَّادِقُونَ ﴿٥٩﴾

*(Basi) wapewe (mali) mafakiri wa miongoni mwa Muhajirin ambao walifukuzwa katika nyumba zao na mali zao (wakakhiari kuacha hayo) kwa ajili ya (kutafuta) fadhila za Mwenyezi Mungu na radhi (yake) na kuinusuru (Dini ya) Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Basi hao ndio Waislamu wa kweli.(59:8)*

وَالَّذِينَ تَبَوَّءُوا الدَّارَ وَالْأَيْمَانَ مِنْ قَبْلِهِمْ يُحِبُّونَ مَنْ  
هَاجَرَ إِلَيْهِمْ وَلَا يَجِدُونَ فِي صُدُورِهِمْ حَاجَةً  
مِمَّا أُوتُوا وَيُؤْثِرُونَ عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ وَمَنْ يُوقِ  
شَحْحَ نَفْسِهِ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٩﴾

*Na (pia wapewe) wale waliofanya maskani yao hapa (Madinah) na wakautakasa Uislamu (wao) kabla ya kuja (hao Muhajirin) na wakawapenda hao waliohamia kwao, wala hawaoni dhiki nyoyoni mwao kwa hayo waliyopewa (hao Muhajir), na wanawapendelea kuliko nafsi zao ingawa wenyewe wana hali ndogo. Na waepushwao na ubakhili wa nafsi zao hao ndio wenye kufaulu kweli kweli". (59:9).*

Kwa muunganisho wa udugu, Waislamu kutoka Makkah walijisikia kama wapo nyumbani na walipata fursa nzuri ya kujijenga upya kiuchumi. Hata hivyo kutokana na tabia nzuri ya Kiislam waliyokuwa nayo, Muhajirin hawakutaka kuwa mzingo kwa ndugu zao na walijitahidi kutokubali kupokea msaada mwingi kupita kiasi kutoka kwa ndugu zao na walijitahidi kujitegemea kwa kufanya kazi mbali mbali, hasa biashara, kwa kadiri walivyoweza kama tunavyojifunza katika Hadithi ifuatayo:

*“Amesimulia Abu Hurairah (r.a): Answar walimwambia Mtume (s.a.w), “Tafadhali gawanya mashamba yetu ya mitende kati yetu na Muhajirin. Mtume(s.a.w) alikataa. Answar wakasema (katika pendekezo lingine): “Muhajirin wafanye kazi katika bustani (zetu za mitende) kisha tutagawana matunda yatakayopatikana.” Muhajirin wakasema, “Hili tunakubaliana nalo” (Sahih Bukhari).*

Udugu wa Kidini kati ya Muhajirin na Answar, unabainishwa pia katika aya ifuatayo:

إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَهَاجَرُوا وَجَاهَدُوا بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَالَّذِينَ ءَاوَأُوا وَنَصَرُوا أَوْلِيَّكَ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَلَمْ يُهَاجِرُوا مَا لَكُمْ مِّنْ وَلِيَّتِهِم مِّن شَيْءٍ حَتَّىٰ يُهَاجِرُوا.....

*Hakika wale walioamini na wakahama na wakapigania Dini ya Allah kwa mali zao na nafsi zao (Nao ni wale Muhajirin). Na waliowapa (Muhajirin) mahali pa kukaa (nao ni Answar) na wakainusuru Dini ya Allah; hao ndio marafiki wao kwa wao. Na wale walioamini lakini hawakuhama nyinyi hamna haki ya kurithiana nao (mpaka wahame).....” (8:72)*

Udugu wa Kidini baina ya Answar na Muhajirin, ulikuwa mzito kiasi kwamba mwanzoni ndugu hawa wawili walirithiana. Baada ya Uislamu kuimarika na kuenea kote Bara Arab na watu wengi kusilimu ikiwa ni pamoja na watu wa Makka, sharia ya kurithiana kwa misingi ya udugu wa Kidini iliondolewa na Waislamu wakawa wanarithiana kwa sharia ya mirathi tunayoifuata hivi leo . Sharia ya kurithiana baina ya Answar na Muhajirin ilifutwa na aya ifuatayo:

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مِن بَعْدُ وَهَاجَرُوا وَجَاهَدُوا مَعَكُمْ فَأُولَٰئِكَ مِنكُمْ وَأُولَٰئِكَ الْأَرْحَامُ بَعْضُهُمْ أَوْلَىٰ بِبَعْضٍ فِي كِتَابِ اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ

عَلِيمٌ ﴿٧٥﴾

*“Na wale watakaoamini baadaye, wakahajiri nao, wakapigania pamoja nanyi (katika kupigania Dini) basi hao ni katika nyinyi. Na ndugu wa nasaba wanastahikiana wenyewe kwa wenyewe (katika kurithiana. Ndivyo vilivyo) katika kitabu cha Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa kila kitu” (8:75).*

Muhajirina walikuwa wakifanya biashara walipokuwa Makka, hivyo walijiingiza katika biashara na katika muda mfupi wengi wao waliinukia kuwa wafanya biashara wakubwa kama ‘Uthman bin

Affan na Abdur-Rahman bin ‘Auf. Ansvari nao kulingana na mazingira ya Madinah walipendelea kilimo zaidi. Ni dhahiri kuwa kwa kuchangaya kilimo na biashara, uchumi wa Madinah uliinuka haraka haraka. Uchumi wa Madinah ulizidi kwenda juu kutokana na ngawira walizozipata Waislamu kutokana na ushindi walioupata katika vita mbali mbali vya jihad. Kwa mara ya kwanza ulianzishwa mfuko au hazina ya Serikali – Baitul Mal – kwa ajili ya kuendesha shughuli za Serikali ya Kiislamu na kwa ajili ya kuwasaidia wasiojiweza, hasa wale wakazi wa Suffah. Waislamu walichangia mfuko huu kwa kutoa zakat na Sadaqat.

**(iii) Kuweka Mkataba wa Madinah**

Mtume(s.a.w) aliona kuwa, ili kuhakikisha mji wa Madinah unakuwa na amani, hapanabudi kuandikiana mkataba wa amani na Mayahudi. Mtume(s.a.w) aliwaendea Mayahudi na kuwafahamisha kuwa yeye ni Mtume wa Allah(s.w) kama Mitume wengine waliomtangulia na kuwa anakuja kuthibitisha Dini ya Mitume hao na sio kuipinga. Aliwathibitishia kuwa yeye ni Mtume aliyeletwa kwa upande wa Waarabu kama Musa(a.s) alivyoletwa kwa upande wa wana Israil (Mayahudi).

إِنَّا أَرْسَلْنَا إِلَيْكُمْ رَسُولًا شَاهِدًا عَلَيْكُمْ كَمَا أَرْسَلْنَا إِلَىٰ فِرْعَوْنَ  
رَسُولًا

*“Hakika sisi tumekuleteeni Mtume aliyeshahidi juu yenu, kama tulivyompeleka Mtume kwa Firaun”. (73:15).*

Mayahudi walipoona kuwa Mtume(s.a.w) na Waislamu wanafunga pamoja siku ya Ashura na wanaelekea Qibla kimoja cha Yerusalem (Masjidul-Aqswaa) wakati wa kuswali, walihisi kuwa Waislamu wako pamoja nao. Ni katika kipindi hiki cha awali Mtume(s.a.w) alifunga nao mkataba wa amani na ukawekwa wazi katika katiba ya Dola ya Kiislamu. Mkataba wa Madinah uliainisha mahusiano mema baina ya Waislamu na wasiokuwa Waislamu

katika mji wa Madinah. Katika mkataba huu kila kundi la watu, Waislamu, Mayahudi na Washirikina (Waarabu waliokuwa hawajasilimu), walikuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa mji wa Madinah unakuwa katika amani na wote waliwajibika kuuhami endapo utavamiwa na maadui zao. Kila watu walikuwa na uhuru wa kufuata Dini waipendayo.

**(iv) Mikataba ya Amani na Makabila ya Kiyahudi pembezoni mwa Madinah**

Pamoja na mkataba wa Madinah, Mtume(s.a.w) aliweka mikataba ya amani na makabila mbali mbali yaliyo pembezoni mwa mji wa Madinah. Miongoni mwa koo za Kiyahudi zilizokuwa zikiishi pembezoni mwa mji ni **Banu Quraizah, Banu Qainuqa na Banu Nadhir**. Hizi zilikuwa koo maarufu za Kiyahudi zenye nguvu. Mtume(s.a.w) alifunga nazo mikataba ya amani.

**(v) Kuandaa Ummah Kijeshi na Kiusalama**

Mtume(s.a.w) aliwahimiza Waislamu kuwa wakakamavu, kujifunza shahaba na mieleka na kuwa na silaha. Kila Muislamu mwanamume alikuwa mpiganaji na mpelelezi dhidi ya maadui wa Uislamu na njama zao.

**(vi) Kuimarisha Uchumi**

Pamoja na Mtume(s.a.w) kuweka mazingira ya kusaidiana kiuchumi kwa kuunganisha udugu baina ya Answar na Muhajirina aliwahimiza Waislamu kufanya kazi kwa bidii na kujiimarisha kiuchumi. Utoaji wa Zakat na Sadaqat ulihimizwa ili kuondoa umaskini na kuimarisha huduma za jamii. Ilianzishwa Baitul-mal(Hazina ya Dola).

**(vii) Kuteua Sekretarieti**

Mtume(s.a.w) aliteua waandishi maalumu ambao walikuwa wakiandika na kuweka kumbukumbu ya mambo mbali mbali. Pamoja na waandishi wa Qur-an waliokuwepo tangu Makka,



alikuwa na waandishi wa mikataba, idadi ya watu, idadi ya mitende na mifugo, n.k. Palikuwa na taarifa na rikodi ya kila kitu.

### **(viii) Kuteua Shura**

Pia Mtume(s.a.w) aliteua Waislamu weledi na wazoefu kuwa washauri wake katika mambo mbali mbali. Waliokuwa safu ya mbele katika washauri wake ni Abu bakar(r.a), 'Umar bin Khattab(r.a), 'Uthman bin Affan(r.a), 'Ali bin Abu-Talib(r.a), Hamza bin Abdul-Muttalib na wengineo. Wengi wao walikuwa Muhajiriina. Hata hivyo Mtume(s.a.w) alipohitaji rai kutoka kwa watu wote, alipendelea sana kuanza kupata rai kutoka kwa Answar.

### **Mafunzo Yatokanayo na mambo Aliyofanya Mtume (s.a.w) Katika Kuanzisha Dola ya Kiislamu**

**Kwanza**, ili tuweze kusimamisha Uislamu katika jamii hatunabudi kuanzisha na kuendeleza vituo vya harakati, misikiti ikiwa ndio vitovu. Kila palipo na fursa nzuri ni muhimu kuibadili misikiti iliyopo na kuifanya vituo vya harakati. Lakini ichukuliwe tahadhari kubwa ili tusije tumbukia kwenye kosa la kuvamia misikiti ya watu kabla ya kufikia kipindi cha kuikomboa – Fat-h-Makka.

**Pili**, hatunabudi kujenga mshikamano wa Waislamu kwa njia ya kupendana na kuhurumiana na hasa kwenye matatizo na shida. Rejea udugu baina ya Answar na Muhajiriina. Hatunabudi kujenga mazingira na tabia ya kufanya kazi za bega kwa bega (za kitamasha) katika kuendeleza shughuli mbali mbali kwa ajili ya maendeleo ya Uislamu.

**Tatu**, hatunabudi kukaa vizuri na wasiokuwa Waislamu hasa wale wasiotupiga vita bayana. Tuwaheshimu, tuwatendee haki na tusiwatukanie miungu yao wala kuidhihaki dini yao. Tuwalinganie kwa hekima na tuwape changamoto ya hoja na mawaidha mazuri.

أَدْعُ إِلَى سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحُكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ وَجَدِلْهُمْ بِالَّتِي هِيَ  
 أَحْسَنُ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِمَنْ ضَلَّ عَنْ سَبِيلِهِ ۗ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ ﴿١٢٥﴾  
*Waite (waite watu) katika njia ya Mola wako kwa hikima na mauidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora (siyo kwa kuwatukana wao au kutukana Dini yao. Kwa njia hii huwezi kumvuta mtu). Hakika Mola wako ndiye anayemjua aliyepotea katika njia yake, naye ndiye anayewajua walioongoka. (16:125)*

**Nne**, hatunabudi kuwajua vema maadui wa Uislamu na Waislamu na kuzijua vyema hila na mbinu zao katika kuuhujumu Uislamu. Kila Muislamu anatakiwa awe msalama kwa kumjua ni nani adui wa Uislamu, yuko wapi na anafanya nini dhidi ya Uislamu.

**Tano**, kila Muislamu mwanamume hanabudi kuwa mkakamavu na jasiri aliyetayari kuingia vitani ili kuihami Dini ya Allah(s.w).

وَأَعِدُّوا لَهُمْ مَا اسْتَطَعْتُمْ مِنْ قُوَّةٍ وَمِنْ رِبَاطِ الْخَيْلِ  
 تُرْهِبُونَ بِهِ عَدُوَّ اللَّهِ وَعَدُوَّكُمْ وَعَآخِرِينَ مِنْ دُونِهِمْ لَا تَعْلَمُونَهُمُ  
 اللَّهُ يَعْلَمُهُمْ ۗ وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ شَيْءٍ فِي سَبِيلِ اللَّهِ يُوَفَّ إِلَيْكُمْ  
 وَأَنْتُمْ لَا تُظْلَمُونَ ﴿٦١﴾

*Basi waandalieni (wawekeeni tayari) nguvu mziwezazo (silaha), na mafarasi yaliyofungwa tayari (mipakani), ili kwazo (nguvu hizi) muogopeshe maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui zenu, (mnaowajua) na pia (maadui zenu) wengine wasiokuwa wao, msiowajua nyinyi (lakini) Mwenyezi Mungu anawajua. Na chochote mtakachokitua katika njia ya Mwenyezi Mungu (kama hii misaada ya vita vya Jihadi) mtarudishiwa kamili wala hamtadhulumiwa. (8:60)*

**Sita**, ili tuweze kusimamisha Uislamu katika jamii yetu, hatuna budi kuimarisha uchumi wetu. Uchumi ndio raslimali kuu ya kusimamishia Uislamu katika jamii. Kila kitu cha kimaendeleo kinahitaji matumizi ya mali. Hatunabudi kuhuisha na kuimarisha ukusanyaji na ugawaji wa Zakat na Sadaqat kijamii.

## **Mapambano Dhidi ya Maadui wa Dola ya Kiislamu**

Katika miaka yote kumi ya kipindi cha Madinah, Mtume(s.a.w) alipambana mfululizo na maadui wa Dola ya Kiislamu. Mtume(s.a.w) mwenyewe akiwa Amir Jeshi na kamanda mkuu aliongoza vita 27, vikubwa 7 na vidogo 20 katika kipindi hicho cha miaka kumi. Maadui wakubwa waliopambana na Waislamu katika kipindi cha Madinah ni:

- Makafiri wa kabila la Qiquraish.
- Wanafiki.
- Mayahudi.
- Makabila mengine ya Waarabu.
- Warumi (wakristo).

## **Makafiri wa Kabila la Qiquraish**

Pamoja na vitimbi vyao vikubwa walivyovifanya Makka dhidi ya Mtume(s.a.w) na Waislamu, Makuraysh waliamua kuwafuatilia Waislamu Madinah kuendeleza vitimbi vyao kama vifuatavyo:

**Kwanza**, walimuandikia barua kiongozi wa wanafiki, ‘Abdullah bin Ubayyi, ili amfukuze au kumuua Mtume(s.a.w) na kumtishia vita endapo hatatekeleza:

*“Kwa kumpa mtu wetu(Muhammad) hifadhi (ya kiasiasa) tunakutaka kwa jina la Allah ima umuue au umfukuze Madinah lau sivyo, tutakushambulieni, tutakumalizeni na kuwateka wake zenu.”<sup>19</sup>*

**Pili**, Maquraish waliyatishia vita makabila yaliyokuwa yakiishi kati ya Makka na Madinah ili yasije silimu na kuyachochea yawe dhidi ya Waislamu.

**Tatu**, Bwana mkubwa wa Maquraish, Kurz bin Jabir na wenzake walikuja kwa siri, Madinah, na kupora mifugo ya ngamia, mbuzi na kondoo na kukimbia nayo Makka.

**Nne**, mabwana wakubwa wa Maquraish, Habbar bin 'Aswad na Nafii bin Qays walimchocha chocha mikuki, bibi Zaynab bint Muhammad(s.a.w) alipokuwa akihamia Madinah kumfuata baba yake. Bibi huyu aliyekuwa mja mzito aliathirika sana na ikawa ndio Sababu ya kifo chake.

Hujuma kama hizi za Maquraish za kuhatarisha usalama wa Waislamu na uchumi wao zilikithiri na ikawa ndio Sababu ya Waislamu kuruhusiwa rasmi na Mola wao kuingia vitani dhidi ya maadui zao.

أَذِنَ لِلَّذِينَ يُقْتَلُونَ بِأَنَّهُمْ ظَلَمُوا وَإِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ نَصْرِهِمْ لَقَدِيرٌ ﴿٣٩﴾

*Wameruhusiwa (kupigana) wale waliopigwa, kwa Sababu wamedhulumiwa. Na kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuwasaidia. (22:39)*

وَقَدِّلُوهُمْ حَتَّىٰ لَا تَكُونَ فِتْنَةٌ وَيَكُونَ الدِّينُ كُلُّهُ لِلَّهِ فَإِنَّ آنتَهُوْا

فَإِنَّ اللَّهَ بِمَا يَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٣٩﴾

*Na piganeni nao (makafiri) mpaka yasiweko mateso (nyinyi kuteswa na wao kwa ajili ya dini kama wanavyokuteseni sasa); na dini iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Lakini wakiacha, basi hakika Mwenyezi Mungu anayaona wanayoyatenda. (8:39)*

Ruhusa hii iliwafanya Waislamu walijizatiti kivita kupambana na maadui zao hawa na wengine wote walioibuka baadaye.

Mtume(s.a.w) na jeshi lake alipambana na Maquraish katika vita vikubwa vya Badr, Uhud na Ahzab. Waislamu walipata ushindi mkubwa katika vita vya Badr pamoja na udhaifu waliokuwa nao ukilinganisha na nguvu ya jeshi la Maquraish. Ushindi wa Badr ni bishara njema kwa Waislamu wa zama zote kuwa watapata ushindi dhidi ya maadui wa Dini ya Allah(s.w) pale watakapojizatiti kwa kadiri ya uwezo wao kupambana na maadui hao huku wakitegemea msaada kutoka kwa Allah(s.w).

إِذْ تَسْتَعِيثُونَ رَبَّكُمْ فَاسْتَجَابَ لَكُمْ أَنِّي مُمِدُّكُمْ بِآلِيفٍ مِّنَ الْمَلَائِكَةِ

مُرْدِفِينَ ﴿١٠١﴾

(Kumbukeni) mlipokuwa mkiomba msaada kwa Mola wenu, naye akakujibuni kuwa: “Kwa yakini Mimi nitakusaidieni kwa Malaika elfu moja watakaofuatana mfululizo (wanaongezeka tu)(8:9)

وَمَا جَعَلَهُ اللَّهُ إِلَّا بُشْرَىٰ وَلِتَطْمَئِنَّ بِهِ قُلُوبُكُمْ وَمَا النَّصْرُ إِلَّا مِنْ عِنْدِ

اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿١٠٢﴾

Na Mwenyezi Mungu hakufanya haya ila iwe bishara (habari ya furaha) na ili nyoyo zenu zitue kwayo. Na hakuna msaada (wa kufaa) ila utokao kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu (na) Mwenye hikima. (8:10)

وَلَقَدْ نَصَرَكُمُ اللَّهُ بِبَدْرِ وَأَنْتُمْ أَذِلَّةٌ فَاتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ

تَشْكُرُونَ ﴿١٢٣﴾

Na Mwenyezi Mungu alikunusuruni katika (vita vya) Badri, hali nyinyi mlikuwa dhaifu. Basi mcheni Mwenyezi Munguili mpate kushukuru (kila wakati kwa neema zinazokujieni).(3:123)

إِذْ تَقُولُ لِلْمُؤْمِنِينَ أَلَنْ يَكْفِيَكُمْ أَنْ يُمِدَّكُمْ رَبُّكُمْ

بِثَلَاثَةِ آلَافٍ مِّنَ الْمَلَائِكَةِ مُنَزَّلِينَ ﴿١٢٤﴾

(Alikunusuruni katika vita vya badr) ulipowaambia Waislamu:  
“Je! Haitakutosheni Mola wenu atapokusaidieni kwa Malaika  
elfu tatu watakaoteremshwa?” (3:124)


فَلَمْ تَقْتُلُوهُمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ قَتَلَهُمْ وَمَا رَمَيْتَ إِذْ رَمَيْتَ وَلَكِنَّ اللَّهَ  
رَمَىٰ وَلِيُبْلِيَ الْمُؤْمِنِينَ مِنْهُ بَلَاءً حَسَنًا إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١٧﴾

*Hamkuuwa nyinyi lakini Mwenyezi Mungu ndiye aliyewaua; na hukutupa wewe (Mtume ule mchanga wa katika gao la mkono wako), ulipotupa (ukawaingia wote machoni mwao); (hukufanya wewe haya) walakini Mwenyezi Mungu ndiye aliyeutupa, (yaani ndiye aliyefikisha katika macho yao wote yakawa yanawawasha kuliko pilipili, wakenda mbio) Alifanya haya Mwenyezi Mungu ili awape walioamini hidaya nzuri itokayo kwake. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye asikiaye na ajuaye. (8:17)*

Pamoja na udhaifu wa baadhi ya Waislamu walioonyesha kwa kuhlifu amri ya Mtume(s.a.w) katika vita vya Uhud bado Waislamu baada ya kurudi katika twaa ya Mtume(s.a.w) waliwashinda Maquraish na kuwarejesha Makka mbio mbio.

Katika vita vya Ahzab, maquraish walikusanyana na makundi mengine ya maadui wa Uislamu ili kuunda nguvu kubwa itakayo wafuta Waislamu na Uislamu kwenye uso wa dunia. Waislamu walifanya jitihada kubwa ya kujihami kwa kuchimba handaki kubwa kuzunguka mji wa Madinah. Angalia ramani ya uwanja wa vita vya Handaq.

## RAMANI YA VITA VYA HANDAQ



Maadui kwa uwezo wa Allah walishindwa kulivuka lile handaki, wakabakia wakiwazingira Waislamu kwa takriban mwezi mmoja. Baadaye Allah(s.w) alileta majeshi yake ya mbinguni na ardhini kuwanusuru Waislamu. Allah(s.w) anatumkumbusha:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَذْكُرُوا نِعْمَةَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ جَاءَتْكُمْ جُنُودٌ  
فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ رِيحًا وَجُنُودًا لَمْ تَرَوْهَا وَكَانَ اللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرًا

*Enyi mlioamini! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu; lilipokujieni jeshi; basi tukatuma upepo dhidi yao na majeshi msiyoyaona; na Mwenyezi Mungu amekuwa ni mwenye kuyaona mnayoyatenda. (33:9)*

Hali ngumu ya Ahzab, iliwafanya Waislamu kuwa imara na wagumu zaidi kwa maadui zao:

وَلَمَّا رَأَى الْمُؤْمِنُونَ الْأَحْزَابَ قَالُوا هَذَا مَا وَعَدَنَا اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَصَدَقَ

اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَمَا زَادَهُمْ إِلَّا إِيمَانًا وَتَسْلِيمًا ﴿٢٢﴾

*Na Waislamu (wa kweli) walipoyaona majeshi (ya makafiri yamewashambulia hivyo), walisema, “Haya ndiyo Aliyotuahidi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (kuwa tutapata misukosuko, kisha tutashinda). Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wamesema kweli;” na (jambo hili) halikuwa zidishia ila imani na utii. (33:22)*

Hivyo Maquraish hawakuwa na uwezo tena wa kukabiliana na Waislamu na hatimaye wenyewe waliomba suluhu iliyopelekea kupatikana kwa mkataba wa amani wa Hudaybiya uliopelekea kuwashinda Maquraish na kupatikana “*Fat-h Makkah*”..

## **Wanafiki**

Muda mfupi baada ya Mtume(s.a.w) kuhamia Madinah, ukiwaacha Mayahud, takriban watu wengi wa Madinah walisilimu. Hata hivyo si wote waliosilimu kwa dhati. Baadhi ya watu walisilimu tu kuwaonyesha watu, lakini hawakufurahia kabisa mafanikio ya ujumbe wa Mtume(s.a.w). ‘Abdullah bin Ubayyi aliyekuwa anatazamia kuvishwa taji la Ufalme kabla ya Mtume(s.a.w) kuhamia Madinah alikuwa ndiye kiongozi wa wanafiki. ‘Abdullah bin Ubbayyi na kundi lake pamoja na kutoa kwao shahada walikuwa na chuki dhidi ya Mtume(s.a.w) na Waislamu. Kundi hili lilidhihirisha chuki yao dhidi ya Uislamu kama ifuatayo:

**Kwanza** katika siku za mwanzo mwanzo za kipindi cha Madinah, Abdullah bin Ubayyi alitumiwa barua na Maquraish ili amue Mtume(s.a.w) au amfukuze Madinah. ‘Abdullah hakuweza kufanya chochote kwa kuhofia kuwa watu wake wa Madinah watakuwa dhidi yake, hasa pale Mtume(s.a.w) alipomwambia:

*“Unataka kuzusha vita dhidi ya ndugu zako na vijana wako?”<sup>20</sup>*



**Pili**, wanafiki walishirikiana na Mayahudi katika kuwatia wasiwasi waumini juu ya mabadiliko ya Qibla.

**Tatu**, walishirikiana na Mayahudi na maadui wengine wa Uislamu katika njama za kutaka kumuua Mtume(s.a.w) na kuhilikisha Uislamu. Kwa mfano, Mayahudi wa Banu Nadhir walipopewa amri na Mtume(s.a.w) ya kuondoka Madinah, ‘Abdullah bin Ubayyi, kiongozi wa wanafiki, aliwatumia ujumbe kuwa wasikubali kuhama na akawaahidi kuwa atawasaidia katika mapambanao dhidi ya Mtume(s.a.w) na Waislamu.

﴿ أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ نَافَقُوا يَقُولُونَ لِإِخْوَانِهِمُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَئِنْ أُخْرِجْتُمْ لَنَخْرُجَنَّ مَعَكُمْ وَلَا نُطِيعُ فِيكُمْ أَحَدًا أَبَدًا وَإِنْ قُوتِلْتُمْ لَنَنصُرَنَّكُمْ وَاللَّهُ شَهِدٌ لِمَن كَذَبُونَ ﴾

*Huwaoni wale wanafiki wanawaambia ndugu zao walio makafiri miongoni mwa watu waliopewa Kitabu kabla yenu (Mayahudi) (Wanawaambia): “Kama mkitolewa, (mkifukuzwa hapa) tutaondoka pamoja nanyi, wala hatutamtii yoyote kabisa juu yenu. Na kama mkipigwa vita lazima tutakusaidieni.” Na Mwenyezi Mungu anashuhudia ya kuwa wao ni waongo. (59:11)*

**Nne**, wanafiki 300 wakiongozwa na ‘Abdullah bin Ubayyi walijiangua katika jeshi la Waislamu katika vitu vya Uhud.

**Tano**, katika msafara wa vita vya Banu Mustaliq, ‘Abdullah bin Ubayyi alichocha ugomvi baina ya Answar na Muhajirina na kutishia kuwafukuza Muhajiriina watakaporejea Madinah.

﴿ يَقُولُونَ لَئِنْ رَجَعْنَا إِلَى الْمَدِينَةِ لَيُخْرِجَنَّ الْأَعَزُّ مِنْهَا الْأَذَلَّ وَلِلَّهِ الْعِزَّةُ وَلِرَسُولِهِ وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَلَكِنَّ الْمُنَافِقِينَ لَا يَعْلَمُونَ ﴾

*Wanasema: “Tukirudi madina, Mwenye utukufu atamfukuza mnyonge,” (yaani Abadallah bin Ubay atamfukuza Mtume). Na utukufu hasa ni wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Waislamu; lakini wanafiki hawajui. (63:8)*

**Sita**, wanafiki chini ya uongozi wa ‘Abdullah bin U bayyi, walimzulia mkewe Mtume(s.a.w), Aysha bint Abubakar, kitendo kichafu cha zinaa ili kumuudhi Mtume(s.a.w) na Waislamu na kuupaka Uislamu matope.

**Saba**, wanafiki walikuwa wakitoa nyudhuru za uwongo ili kuepa jukumu la kuupigania Uislamu. Kwa mfano katika msafara wa Tabuuk, wanafiki kutokana na ugumu wa safari, hali ya njaa iliyokuwepo na woga wa kupambana na jeshi kali la Warumi, walitoa nyudhuru za uongo mbele ya Mtume(s.a.w) ili wasiende vitani.

لَوْ كَانَ عَرَضًا قَرِيبًا وَسَفَرًا قَاصِدًا لَاتَّبَعُوكَ وَلَكِنْ  
 بَعَدَتْ عَلَيْهِمُ السُّجَّةُ وَسَيَحْلِفُونَ بِاللَّهِ لَوِ اسْتَطَعْنَا لَخَرَجْنَا  
 مَعَكُمْ يُهْلِكُونَ أَنْفُسَهُمْ وَاللَّهُ يَعْلَمُ إِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ ﴿٤٧﴾

*Kama ingalikuwa faida iliyo nyepesi (kapatikana) na safari fupi, kwa yakini wangalikufuata (hao wanaojipa Uislamu wa uwongo). Lakini safari hii ya taabu imekuwa ndefu kwao. Nao wataapa kwa Mwenyezi Mungu, “Kama tungaliweza bila shaka tungelitoka pamoja nanyi.” Wanaangamiza nafsi zao; na Mwenyezi Mungu anajua (kwa hakika) kuwa hao ni waongo (tu). (9:42)*

Pia wanafiki walikuwa wakiwashawishi Waislamu wasiende vitani, wakawahofisha adha na madhara watakapopata.

فَرِحَ الْمُخَلَّفُونَ بِمَقْعَدِهِمْ خِلَافَ رَسُولِ اللَّهِ وَكَرِهُوا أَنْ يُجَاهِدُوا  
بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَقَالُوا لَا تَنْفِرُوا فِي الْحَرِّ قُلْ نَارُ  
جَهَنَّمَ أَشَدُّ حَرًّا لَوْ كَانُوا يَفْقَهُونَ ﴿٨١﴾

*Walifurahi walioachwa nyuma (wasende vitani. Walifurahi) kwa kule kukaa kwao nyuma ya Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na walichukia kupigana kwa mali zao na nafsi zao katika njia ya Mwenyezi Mungu, na wakasema (kuwaambia wenzao): “Msende (vitani) katika joto hili.” Sema (uwaambie): “Moto wa Jahanamu una joto zaidi. Laiti wangepahamu.” (9:81)*

**Nane**, Wanafiki walijenga msikiti wakishirikiana na maadui wengine wa Uislamu, ili uwe kichaka cha kupanga njama za kuhujumu Uislamu.

وَالَّذِينَ اتَّخَذُوا مَسْجِدًا ضِرَارًا وَكُفْرًا وَتَفْرِيْقًا بَيْنَ الْمُؤْمِنِينَ وَإِرْصَادًا  
لِّمَنْ حَارَبَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ مِنْ قَبْلُ وَلَيَحْلِفُنَّ إِنْ أَرَدْنَا إِلَّا الْحُسْنَى وَاللَّهُ  
يَشْهَدُ إِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ ﴿١٠٧﴾

*Na wako (wanafiki wengine) waliojenga msikiti wa (kuleta) udhia na kutia nguvu ukafiri, na kuwafarikisha walioamini na kuufanya mahali pa kuwangojea wale waliomfanyia vita Mwenyezi Mungu na Mtume wake zamani. Na bila shaka wataapa (waseme): “Hatukukusudia ila wema.” Lakini Mwenyezi Mungu anashuhudia kuwa wao ni waongo. (9:107)*

Katika kuondosha chokocho na taathira ya wanafiki katika jamii ya Kiislamu, Mtume(s.a.w) aliamrisha na Mola wake kuwa mgumu kwao:

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ  
وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٩﴾

*Ewe Nabii! Shindana na makafiri na wanafiki na uwe mgumu kwao; na makazi yao ni Jahanamu; nayo ni marejeo mabaya kabisa. (66:9)*

Katika kuwa mgumu kwao, Mtume(s.a.w) alivunja msikiti wao kwa amri ya Allah(s.w).

لَا يَزَالُ بُنِيتُهُمُ الَّذِي بَنَوْا رِيبَةً فِي قُلُوبِهِمْ إِلَّا أَنْ تَقَطَّعَ قُلُوبُهُمْ وَاللَّهُ  
عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿١١٠﴾

*Jengo lao hilo walilolijenga (likavunjwa na Mtume) litakuwa Sababu ya kutia wasi wasi (uchungu) nyoyoni mwao (siku zote), mpaka nyoyo zao zikatike vipande vipande. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi (na Mwenye hikima. (9:110)*

Vile vile Mtume(s.a.w) aliwatenga wanafiki na jamii ya Waislamu, alipoamriwa na Mola wake kutomswalia na kumuomba msamaha mmoja wao akifa.

أَسْتَغْفِرُ لَهُمْ أَوْ لَا تَسْتَغْفِرُ لَهُمْ إِنْ تَسْتَغْفِرْ لَهُمْ سَبْعِينَ مَرَّةً فَلَنْ  
يَغْفِرَ اللَّهُ لَهُمْ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ كَفَرُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي  
الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ ﴿٨٠﴾

*(Ewe Mtume)! Waombee msamaha (hao wanafiki) au usiwaombee; (yote sawa sawa). Hata ukiwaombee msamaha mara sabiini, Mwenyezi Mungu hatawasamehe. Hayo ni kwa Sababu ya kuwa wao wamemkataa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu wavunjao amri (Zake). (9:80)*

وَلَا تَصَلِّ عَلَى أَحَدٍ مِّنْهُمْ مَّتَّاتَ أَبَدًا وَلَا  
تَقُمْ عَلَى قَبْرِهِ ۗ إِنَّهُمْ كَفَرُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ۗ وَمَاتُوا وَهُمْ  
فَاسِقُونَ ﴿٨٤﴾

*Wala usimsalie kamwe mmoja wao yoyote yule akifa, wala usisimame kaburini kwake (kumuomba dua). Hakika hao wamemkataa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na wakafa, na hali ni wenye kuvunja amri (za Mwenyezi Mungu). (9:84)*

## Mayahud

Mwanzoni Mayahud walipoona kuwa Waislamu wanafunga siku ya Ashura pamoja nao na wanaelekea Qibla cha Baitul-Muqaddas pamoja nao hawakuonyesha chuki ya dhahiri dhidi ya Mtume(s.a.w) na Waislamu. Chuki yao dhidi ya Uislamu ilibainika pale Allah(s.w) alipowabadilishia Waislamu Qibla.

قَدْ نَرَى تَقَلُّبَ وَجْهِكَ فِي السَّمَاءِ فَلَنُوَلِّيَنَّكَ قِبْلَةً تَرْضَاهَا فَوَلِّ وَجْهَكَ  
شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَحَيْثُ مَا كُنْتُمْ فَوَلُّوا وُجُوهَكُمْ شَطْرَهُ ۗ وَإِنَّ  
الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ لَيَعْلَمُونَ أَنَّهُ الْحَقُّ مِنْ رَبِّهِمْ ۗ وَمَا اللَّهُ بِغَفِيلٍ عَمَّا  
يَعْمَلُونَ ﴿١٤٤﴾

*Kwa yakini tukiona unavyogeuzageuza uso wako mbinguni. Basi tutakugeuza kwenye Qibla ukipendacho. Basi geuza uso wako upande wa Msikiti Mtakatifu (Al-Kaaba); na po pote mnapokuwa zielekezeni nyuso zenu uliko (msikiti huo); na hakika wale waliopewa Kitabu wanajua kwamba hiyo ni haki itokayo kwa Mola wao; na Mwenyezi Mungu si Mwenye kughafilika na yale wanayoyatenda. (2:144)*

Jambo hili la kubadilishwa Qibla liliwachoma sana Mayahud na lilijenga chuki na husuda dhidi ya Waislamu. Waliona kuwa kubadilishwa Qibla ni dalili ya Waislamu kufanywa umma bora na teule badala ya Mayahudi. Walihisi kuwa wamenyang'anywa cheo chao. Katika kudhihirisha chuki yao. Mayahud walifanya vitimbi vifuatavyo dhidi ya Mtume(s.a.w) na Waislamu:

**Kwanza**, Mayahudi walishirikiana na wanafiki kuwachochea Waislamu juu ya mabadiliko ya Qibla mpaka baadhi yao wakaanza kuwa na wasi wasi na kusema: “Inakuaje kwamba watu wakati mmoja wanaelekea huku (Baitul-Muqaddas) na wakati mwingine wanabadilisha tena wanaelekea huku (Baitul-Haraam)”. Allah(s.w) aliondoshwa wasi wasi huu kwa Waislamu kwa kushusha aya ifuatayo:

﴿سَيَقُولُ السُّفَهَاءُ مِنَ النَّاسِ مَا وَلَّيْنَاهُمْ عَنْ قِبْلَتِهِمُ الَّتِي كَانُوا عَلَيْهَا قُلْ

لِلَّهِ الْمَشْرِقُ وَالْمَغْرِبُ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ﴾

*Karibuni wapumbavu miongoni mwa watu watasema: "Nini kilichowageza kutoka kibla chao walichokuwa wakikielekea?"*

*Sema: (uwambie) "Mashariki na Magharibi ni ya Mwenyezi Mungu; humwongoza amtakae katika njia iliyonyooka." (2:142)*

**Pili**, Mayahudi walitumia kifo cha Swahaba Amama, kutangaza kuwa Muhammad(s.a.w) si Mtume wa kweli, kwani angelikuwa Mtume wa kweli wa Allah(s.w) angelizuia kifo cha Amama.

Pia Mayahudi walipita wakitangaza kuwa Mtume(s.a.w) ni Mtume wa uongo pale Mtume(s.a.w) alipobadilisha Qibla.

**Tatu**, Mayahud waliifanyia Qur-an stihizai. Iliposhuka aya 245 ya Suratul-Baqarah:

مَنْ ذَا الَّذِي يُقْرِضُ اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا فَيُضْعِفُهُ لَهُ وَأَضعَافًا كَثِيرَةً وَاللَّهُ

يَقْبِضُ وَيَبْضُطُ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٢٤٥﴾

*Ni nani atakayemkatia Mwenyezi Mungu sehemu bora (ya mali yake kwa kuwapa masikini na kwa kutoa katika mambo mengine ya kheri) ili Mwenyezi Mungu amzidishie mzigidisho mwingi, na Mwenyezi Mungu ndiye anayezuia na ndiye anayetoa, na Kwake (nyote) mtarejeshwa. (2:245)*

Mayahudi walipita mitaani wakisema kuwa Allah(s.w) ni maskini anawaomba mali yao:

لَقَدْ سَمِعَ اللَّهُ قَوْلَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ فَقِيرٌ

وَنَحْنُ أَغْنِيَاءُ سَنَكْتُبُ مَا قَالُوا وَقَتَلَهُمُ الْأَنْبِيَاءُ بِغَيْرِ حَقٍّ وَنَقُولُ

ذُوقُوا عَذَابَ الْحَرِيقِ ﴿١٨١﴾

*Mwenyezi Mungu amekwisha sikia kauli ya wale (Mayahudi) waliosema: "Mwenyezi Mungu ni fakiri, na sisi ni matajiri." Tumeyaandika haya waliyoyasema, na (tumeandika) kuua kwao Manabii bila ya haki, na tutawaambia (Siku ya Kiyama): "Onjeni adhabu ya kuungua." (3:181)*

**Nne**, walimjaribu Mtume(s.a.w) kwa kumuuliza maswali ya kubabaisha yasiyo na majibu ya dhahiri. Katika mkusanyiko wa Waislamu, Mayahudi walimuuliza Mtume:

"Kama Allah amewaumba binaadamu, yeye ameumbwa na nani?"

Mtume(s.a.w) alijibu swali hili kwa kuwasomea Suratul Ikhlas:

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ① اللَّهُ الصَّمَدُ ② لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ ③ وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ ④

*Sema: Yeye ni Mwenyezi Mungu Mmoja (tu). Mwenyezi Mungu (tu) ndiye anayestahiki kukusudiwa (na viumbe vyake vyote kwa kumuabudu na kumuomba na kumtegemea). Hakuzaa wala Hakuzaliwa. Wala hana anayefanana Naye hata mmoja. (112:1-4)*

Siku moja kundi la wanachuoni (Rabb) wa Kiyahudi walimwendea Mtume(s.a.w) na kumwambia kuwa endapo atajibu kiasi cha kuwatosheleza maswali yao watasilimu. Miongoni kwa maswali waliyoyauliza ni haya yafuatayo:

Usingizi wako ukoje? Ni vitu gani Israil (Nabii Yaquub) alivyojiharamishia mwenyewe na kwa nini? Ni Malaika yupi anayekuletea wahay. Maswali yote Mtume(s.a.w) aliyajibu vilivyo, bali kuhusu swali la nne walisema:

*“Lakini, Ewe Muhammad! Jibril ni adui yetu. Kila anapokuja anakuja na makamio ya adhabu na maangamizi dhidi yetu. Hatuna maelewano mazuri na yeye. Kama si huu uadui kati yetu na yeye bila shaka tungalikuja kwako na kukutii”.*

Mtume(s.a.w) aliwajibu kwa kuwasomea aya ifuatayo:

قُلْ مَنْ كَانَ عَدُوًّا لِجِبْرِيلَ فَإِنَّهُ نَزَّلَهُ عَلٰى قَلْبِكَ بِإِذْنِ اللَّهِ .....

*“Sema: Anayemfanyia ushinde Jibril (kwa kuwa ndiye aliyemletea utume Nabii Muhammad na asiwapelekee Mayahudi bure, hana kosa Jibril) hakika yeye ameteremsha Qur-an moyoni mwako kwa idhini ya Mwenyezi Mungu .....” (2:97)*

مَنْ كَانَ عَدُوًّا لِلَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَرُسُلِهِ وَجِبْرِيلَ وَمِيكَالَ

فَإِنَّ اللَّهَ عَدُوٌّ لِلْكَافِرِينَ ④



*Anayemfanyia ushinde Mwenyezi Mungu na Malaika wake na mitume wake na Jibril na Mikail (anatafuta kuangamia) kwani Mwenyezi Mungu atakuwa mshinde wa makafiri hao". (2:98)*

**Tano**,kuwanyanyasa na kuwadhallisha waislamu kutokana na hali duni ya uchumi waliyokuwanayo. Kila mwanzo mgumu. Waislamu walipoanzisha Dola ya Kiislamu ya Madinah, hali yao haikuwa nzuri kutokana na sababu mbali mbali za msingi. Muhajirina walikwenda Madinah mikononi mitupu na mali yao yote wakaibakisha mikononi mwa makafiri wa Makka.

Answar waliwapokea ndugu zao kwa mapenzi na udugu na kuwasitiri kwa mali zao kwa kadiri ya uwezo wao. Pamoja na hivyo makafiri wa Makkah waliwafuata Waislamu wa Madinah na kuhujumu uchumi wao kwa kuiba mifugo, kuchoma mashamba n.k. Mayahudi walitumia udhaifu huu wa uchumi wa Dola ya Kiislam katika kuwanyanyasa na kuwavunja moyo Waislamu. Walikuwa wakiwakopesha Waislamu na kuwadai hadharani popote pale watakapowakuta na wakati wowote hata kabla ya muda walioahidiana kufika. Kwa mfano Bilal alikopeshwa fedha na Mayahudi. Siku moja Bilal(r.a) alipokuwa anataka kutoa adhana kwa ajili ya swala, huyu myahudi alimuita kwa sauti na kumwambia kuwa kama hatalipa deni lile atachukuliwa tena utumwani. Bilal(r.a) alisononeshwa sana na tukio lile na alikwenda kumhadithia Mtume(s.a.w) ambaye alifanya mpango wa kulipwa kwa deni lile.

Kuna matukio mengi ya namna hii waliyofanyiwa Waislamu pamoja na Mtume mwenyewe. Mwishowe, Mayahudi wakishirikiana na wanafiki pamoja na matajiri wengine wa Madinah wasiokuwa Waislamu waliweka mikakati wa kutowakopesha Waislamu au kuwapa msaada wowote wa kifedha, ili wafilisike kabisa na waamuea kuacha Uislamu. Qur-an inabainisha njama hizi kama ifuatavyo:

هُمَّ الَّذِينَ يَقُولُونَ لَا تُنْفِقُوا عَلَيَّ مِنْ عِنْدِ رَسُولِ اللَّهِ  
 حَتَّى يَنْفَضُوا ۗ لِلَّهِ خَزَائِنُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلَكِنَّ الْمُنْفِقِينَ لَا  
 يَفْقَهُونَ ﴿٧﴾

*“Wao ndio wanaosema: “Msitoe mali kwa ajili ya wale walioko kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ili waondokelee mbali (hapa nchini kwetu, Madinah) . Na hazina za mbingu na ardhi ni za Mwenyezi Mungu; lakini wanafiki hawafahamu” (63:7).*

**Sita,** Walifanya jitihada za kuwachochea na kuwafarakanisha Waislamu. Mayahudi daima hawakulala katika jitihada zao za kutaka kuuhilikisha Uislamu na kuuvuruga udugu wa Waislamu. Walijaribu kuyachonganisha makabila mawili ya Aus na Khazraj, ambayo yaliishi kwa uadui baina yao kabla ya Uislamu kuingia Madinah. Siku moja walipokuwa katika mkutano wao, Mayahudi waliingia mle na kupenyeza habari zenye lengo la kukumbushia kisa cha vita vya Bua’ath, vita vikubwa vya kihistoria vilivyopiganwa kati ya Aus na Khazraj. Mayahudi hao waliendelea kuwachochea na kuwakumbusha uadui baina yao wa miaka iliyopita. Kutokana na uchochezi huu Answar walianza kukasirikiana wao kwa wao na panga zikawa nje nje. Habari za tukio hili zilimfikia Mtume(s.a.w) na akaja kuamua. Kutokana na tukio hili Allah(s.w) aliwaonya Waislamu kwa aya ifuatayo:

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنْ تُطِيعُوا فَرِيقًا مِّنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ يَرُدُّوكُمْ  
 بَعْدَ إِيمَانِكُمْ كَافِرِينَ ﴿١٠٠﴾

*“Enyi mlioamini mkiwatii baadhi ya wale waliopewa kitabu (Mayahudi) watakurudisheni kuwa makarifi baada ya Uislamu wenu” (3: 100).*

**Saba**, Walishirikiana na wanafiki katika njama za kutaka kumuua Mtume na kuuhilikisha Uislamu. Wanafiki wa Madinah, chini ya kiongozi wao ‘Abdullah bin Ubayy, walikuwa wakila njama dhidi ya Mtume na dhidi ya Waislamu wakishirikiana bega kwa bega na Banu Qainuqa’, kabila la kwanza la Mayahudi kufukuzwa Madinah, katika kumnyanyasa na kumuudhi Mtume na Uislamu.

**Nane**, Walivunja au kusaliti mikataba ya amani waliyowekeana na Mtume (s.a.w).

Mtume(s.a.w) alichukua hatua kali dhidi ya kila kitimbi walichokifanya Mayahudi dhidi ya Uislamu. Mtume(s.a.w) alitoa hukumu ya vifo kwa wale waliosimama kidete binafsi kuupiga vita Uislamu. Aliyafukuza Madinah makabila ya Banu Nadhir, Banu Qainuqa na Banu Quraizah baada ya kuvunja mikataba ya amani na kumpiga vita Mtume na Waislamu.

Mayahudi baada ya kuhamishwa Madinah walijikusanya Khaibar, kilomita 320 Kaskazini ya Madinah, Mayahud wa Khaibar wakishirikiana na rafiki zao, wanafiki na washirikina, waliazimia kuivamia Dola ya Kiislamu Madinah mwaka 7 A.H. Mtume(s.a.w) alipopata taarifa juu ya azma hiyo, aliwaendea huko huko Khaibar kwenye ngome yao na kuwacharaza vibaya na huo ukawa ndio mwisho wa chokochoko za Mayahudi katika kipindi cha Mtume(s.a.w).

### ***Makabila Mengine ya Kiarabu***

Makabila mengi ya Kiarabu yaliyoleta chokochoko dhidi ya Dola ya Kiislamu ya Madinah, Mtume(s.a.w) aliyashughulikia mpaka yakasalimu amri na kulipa jizya. Ukiacha Maquraish makabila ya Kiarabu yaliyokuwa na nguvu sana na kujiamini ni makabila ya Khawaizin na Thaqif yaliyokuwa yakiishi katika maeneo ya mji wa Taif. Makabila haya yalipambana na jeshi la Mtume(s.a.w) katika vita vya Hunain vilivyopiganiwa mwaka wa 8 A.H. mwezi mmoja baada ya Fat-h-Makka. Waislamu walipata

ushindi mkubwa sana katika vita hivi vilivyokuwa mwisho wa mapambano na makabila ya Kiarabu kwani yote yalikuja silimu na kuwa chini ya Dola ya Kiislamu. Vita vya Hunain vinaelezwa katika Qur-an:

لَقَدْ نَصَرَ كُمْ اللَّهُ فِي مَوَاطِنَ كَثِيرَةٍ وَيَوْمَ حُنَيْنٍ إِذْ أَعْجَبَتْكُمْ كَثْرَتُكُمْ فَلَمْ تُغْنِ عَنْكُمْ شَيْئًا وَضَاقَتْ عَلَيْكُمْ الْأَرْضُ بِمَا رَحُبَتْ ثُمَّ وَلَّيْتُمْ مُدْبِرِينَ ﴿٧٥﴾ ثُمَّ أَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَى رَسُولِهِ وَعَلَى الْمُؤْمِنِينَ

وَأَنْزَلَ جُنُودًا لَمْ تَرَوْهَا وَعَذَّبَ الَّذِينَ كَفَرُوا وَذَلِكَ جَزَاءُ الْكَافِرِينَ ﴿٧٦﴾

*Bila shaka Mwenyezi Mungu amekunusuruni katika mapigano mengi, na siku ya Hunayni (pia); ambapo wingi wenu ulikupandisheni kichwa, lakini haukukufaeni chochote, na ardhi ikawa dhiki juu yenu; ingawa ilikuwa yenye wasaa, kisha mkageuka mkarudi nyuma (mnakimbia). Kisha Mwenyezi Mungu akateremsha utulivu wake juu ya Mtume wake na juu ya walioamini. Na akateremsha majeshi (ya Malaika) ambayo hamkuyaona, na akawaadhibu wale waliokufuru; na hayo ndiyo malipo ya makafiri. (9:25-26)*

Aya hizi zinatupa picha halisi ya tukio la Hunain. Baadhi ya Waislamu mwanzo mwa vita walitelezeshwa na sheitani wakawa na fikra mbaya kuwa watashinda kutokana na ukubwa wa jeshi lao lililokuwa na askari 12,000 waliojizatiti vizuri, wakasahau kuwa ushindi wote unatoka kwa Allah(s.w). Mazingira ya vita yaliwadhihirishia kuwa wingi wao haukuwasaidia chochote. Mwanzoni wengi wa Waislamu walisambaratishwa na maadui na kumuacha Mtume(s.a.w) na waumini wachache kwenye uwanja wa mapambano wakiwa wamezungukwa na jeshi kubwa la maadui. Mtume(s.a.w) na waumini wachache aliokuwa nao walipigana kwa ujasiri wakiwa na yakini kuwa Allah(s.w) yuko

pamoja nao. Waislamu waliokimbia walipokumbushwa kuwa wamemuacha Mtume wa Allah na waumini wachache kwenye uwanja wa vita, walitanabahi na kujitupa tena kwenye uwanja wa vita bila ya woga wowote kwa kutegemea radhi za Allah(s.w) peke yake. Walipofanya hivyo, Allah(s.w) aliwasaidia kwa kuwashushia jeshi la Malaika na wakapata ushindi mkubwa kwa namna ya ajabu kabisa.

### **Warumi (Wakatoliki)**

Warumi mpaka kufikia 7 A.H. sawa na 629 A.D. walikuwa ni Taifa kubwa (super Power) lililokuwa likitamba kwa nguvu za kishindo katika ulimwengu wa wakati huo. Baada ya mkataba wa Hudaybiyah Mtume(s.a.w) alituma wajumbe katika nchi mbali mbali za ndani na nje ya Bara Arabu. Miongoni mwa watawala waliopelekewa ujumbe na Mtume(s.a.w) ni mfalme wa Basra aliyepelekewa barua na Haarith bin 'Umar Azid. Haarith alipofika **Muttah** aliuliwa na Shurahbil Ghassaany aliyekuwa Gavana wa **Dola ya Kirumi** chini ya Mfalme Heracleus.

Kumuua mjumbe lilikuwa ni kosa kubwa sana kwa sheria ya makabila ya Kiarabu wakati ule. Hivyo , Mtume(s.a.w) alipopata habari ya kuuliwa mjumbe wake, aliandaa jeshi la watu 3,000 chini ya Uamiri wa Zaid bin Harith kwenda Muttah kupambana na Gavana wa Warumi, Shurahbil Ghassaany. Wakati Mtume anatuma jeshi hili aliagiza:

*“Kama Zaidi atauliwa, Ja’far bin Aby Taalib atakuwa Kamanda wenu, na kama naye atauliwa, ‘Abdullah bin Rawahah atachukua ukamanda. Kama naye atakufa mumchague kamanda kutokana na nyinyi.”*

Shurahbil alipopata habari za kuja kwa jeshi la Waislamu aliandaa jeshi la askari laki moja (100,000) Jeshi la waislamu lilipofika njiani lilipata uvumi kuwa Heracleus anakuja na jeshi

lingine la askari 100,000. Jeshi la Waislamu lilisita njiani siku mbili ili kuweka mikakati ya namna ya kupambana na jeshi kubwa kiasi hicho. Baada ya kushauriana Waislamu wote 3,000 katika kikosi kile waliamua kupambana na maadui zao na maadui wa Allah(s.w) kwa gharama yoyote ile.

Zaid aliongoza vita na mapambano makali yakaanza. Si muda mrefu kaka wa Shurahbil aliuliwa na yeye mwenye akakimbilia mafichoni kwenye ngome. Shurahbil alituma ujumbe kwa Mfalme Heracleus ambaye mara tu alituma jeshi lenye nguvu la askari 100,000 kujiunga katika mapambano dhidi ya Waislamu 3,000 tu. Waislamu wachache sana (3,000) wakawa wanapigana na jeshi kubwa sana (200,000) lenye nguvu na uzoefu wa vita. Uwiano wa jeshi la Waislamu na jeshi la Warumi ulikuwa  $3,000:200,000 = 3:200 \approx 1:67$

Zaid bin Harith aliuliwa na Ja'afar akachukua nafasi yake. Naye alipiganisha kwa ushujaa mpaka akafa shahidi. Baada ya Ja'afar, 'Abdullah bin Rawahah alichukua bendera ya vita naye akafa shahidi. Baada yake Waislamu walimchagua Khalid bin Walid kuwa kamanda wao. Waislamu chini ya uongozi wa Khalid waliendelea kupigana kwa ushujaa mkubwa. Katika mchana mmoja wa mapigano Khalid alichakaza panga nane na katika usiku wake, ilibidi Warumi waombe kuakhirisha vita mpaka kesho yake.

Siku iliyofuatia Khalid aliwapanga askari wake katika mstari mrefu kama vile anataka kuwazingira maadui na kuwaweka katikati. Warumi waliogopa kujitokeza kwenye uwanja wa mapambano siku ile. Naye Khalid kama mbinu ya kivita, alilirejesha jeshi lake Madina. Warumi walifurahi sana kuona vita vimekwisha, kwani hawakuwa na nguvu tena ya kupambana na Khalid. Kwa upande mwingine, Waislamu wa Madina hawakufurahishwa na kitendo cha jeshi la Waislamu kuacha mapigano na kurudi Madinah bila ya kupata ushindi. Waliwatupia michanga ya usoni huku wakiwasimanga.

*“Enyi mliokimbia vita! Mnakimbia njia ya Allah”!*

Mtume(s.a.w) aliwaliwaza na kujibu mashambulizi kwa niaba yao, “Sio wakimbizi, Inshaa Allah watarudi tena”. Ni kweli kuwa hawakuwa na dhamira ya kukimbia vita bali walirejea Madina ili kukusanya nguvu upya. Mtume(s.a.w.) na Waislamu walipata majonzi makubwa kwa kuwapoteza mashujaa wengi na hasa wale makamanda watatu.

## **Mafunzo Yatokanayo na Vita vya Muttah**

Waislamu hawakufurahia kuwaona wenzao wanarudi bila ya ushindi. Kwa Waislamu, walikuwa na mawili tu ya kupata katika vita, ushindi au kufa shahidi katika njia ya Allah. Hawakuzoea kabisa kurudi nyuma, ila iwe kama mbinu ya kivita ili kutafuta nguvu zaidi kama alivyofanya Khalid ambayo inaruhusiwa:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا لَقَيْتُمْ الَّذِينَ كَفَرُوا زَحْفًا فَلَا  
تُوَلُّوهُمْ إِلَّا ذُبَابًا ۝١٥

*“Enyi mlioamini! Mkutanapo vitani na wale waliokufuru basi msiwageuzie migongo (mkakimbia). (8:15)*

وَمَنْ يُؤَلِّمْ يَوْمَئِذٍ دُبُرَهُ إِلَّا مُتَحَرِّفًا لِّقِتَالٍ أَوْ  
مُتَحَرِّرًا إِلَىٰ فِتْنَةٍ فَكَدُّ بَاءٍ بِغَضَبٍ مِّنَ اللَّهِ وَمَأْوَاهُ جَهَنَّمُ  
وَبئس المصير ۝١٦

*Na atakayewageuzia mgongo wake siku hiyo – isipokuwa amegeuka kwa kushambulia au amegeuka akaungane na sehemu nyingine ya jeshi hili hili la Waislamu (ikiwa si hivyo) – atatahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu na mahali pake ni Jahanamu. Napo ni mahali pabaya pa kurejea (mtu). (8:16)*

Wakristo katoliki (Warumi) hawakujiona kuwa wameshinda wala kushindwa. Hawakushinda kwa sababu wao ndio waliogopa kukabiliiana na Waislamu na wakakataa kujitokeza kwenye uwanja wa mapambano. Hawakushindwa kwa sababu Waislamu hawakuendelea kupambana nao mpaka kuwafikisha katika kilele cha kushindwa. Hata hivyo Warumi (Wakristo) walishangazwa sana na ushujaa wa Waislamu. Waliona kuwa ni jambo la hatari kubwa kupigana na Waislamu ambao walishambulia kama simba na kila mmoja alikuwa kama vile ana maisha mengi (uhai mwingi).

Walishuhudia nguvu za Waislamu kwa mifano waliyoipata kwa watu kama Ja'far ambaye aliendelea kupigana baada ya mikono yake yote miwili kukatwa; na Khalid ambaye alichakaza panga nane katika kipindi kifupi cha mchana mmoja wa mapambano. Hivyo, walishafikia hatua ya kukata tamaa na walipendelea kuomba suluhu lakini kutokana na kibri chao waliona haya kufanya hivyo. Kwa hiyo walifurahi sana walipoona Waislamu wenyewe wameamua kuondoka na hawakuamini macho yao.

Kwa upande mwingine, Mayahudi na washirikina walifurahi sana kwa msiba uliowapata Waislamu. Walifikia hatua ya kujiwa na mawazo kuwa nuru ya Uislamu itazimwa na Wakristo (Warumi). Wakati vita baina ya Waislamu na Warumi vinaendelea, Mayahudi na washirikina walikuwa wakifanya njama za kuwahujumu Waislamu.

## **Msafara wa Tabuk Dhidi ya Warumi**

Ukombozi wa mji wa Makka (Fat-h Makka) mwaka 8 A.H. uliwezesha Uislamu kuenea kwa kasi kubwa Uarabuni kote. Nchi jirani za wakristo, hasa katika Himaya ya Warumi, zilishikwa na wivu mkubwa kutokana na kuimarika kwa Uislamu hasa kwa kasi kubwa kiasi kile. Pia waliona hatari iliyopo mbele yao kutokana na kuibuka nguvu kubwa ya Uislamu. Waliona hapana budi kuandaa mashambulizi ya nguvu ili kupunguza kasi ya nguvu ya Uislamu.



Hivyo, Warumi chini ya uongozi wa Heracleus, waliandaa jeshi kubwa sana dhidi ya Dola ya Kiislamu, wakishirikiana na nchi nyinginezo za wakristo.

Kama kawaida yake, Mtume(s.a.w) alipohakikisha juu ya maandalizi ya Warumi na nchi za Kikristo dhidi yake, hakusubiri mpaka wamvamie, bali aliandaa jeshi kubwa la Waislamu na kuelekea Syria kupambana na jeshi la Warumi.

Baada ya wiki mbili (siku 14) jeshi la Waislamu lilipiga kambi. Tabuk, mji ulioko kati ya Madinah (mji mkuu wa Dola ya Kiislamu) na Damascus (mji mkuu na mkongwe wa Syria), likingojea lisikie zaidi juu ya miondoko ya jeshi la maadui. Warumi walipopata habari juu ya maandalizi ya kivita ya Mtume(s.a.w), wakikumbuka matokeo ya vita vya Muttah, waliogopa na kurudi ndani ya mipaka yao.

Kwa kuwa lengo la jeshi la Mtume(s.a.w) lilikuwa kuihami Dola ya Kiislamu na wala sio kuvamia Syria, alibakia pale Tabuk, kilometa 700 kutoka Madinah, na kuendelea na kazi ya Da'awah. Makabila mengi ya Wakristo yalijisalimisha kwa dola ya Kiislamu na kuwa tayari kulipa Jizya. Huo ukawa ndio mwisho wa 'U-super power' wa dola ya Kirumi na Uislamu ukachukua nafasi yake na kutimia neno la Allah(s.w):

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ

وَكَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا ﴿٢٨﴾

*Yeye ndiye aliyemtuma, (aliyemleta) Mtume wake kwa uwongofu na dini iliyo ya haki, ili ishinde juu ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Shahidi. (48:28)*

## **Mafunzo Yatokanayo na Mapambano Dhidi ya Maadui wa Dola ya Kiislamu.**

**Kwanza**, kila Uislamu unavyopiga hatua ya maendeleo ndivyo maadui wake wanavyozidi kuwa wengi na kujiimarisha. Katika kipindi cha Makkah, ambapo Waislamu walikuwa katika hali ya udhaifu, adui alikuwa mmoja tu, Makafiri wa Kiquraish. Katika kipindi cha Madinah ambapo Dola ya Kiislamu ilianzishwa na kuendelea kila uchao, maadui nao waliongezeka mpaka ikabidi Waislamu waingie vitani kupambana na kuwashinda maadui watano walioainishwa.

**Pili**, Waislamu watakapojitahidi kupigania Uislamu kwa kadiri ya uwezo wao kwa kutoa mali zao na nafsi zao, Allah atawawezesha kupata ushindi kwa hali yoyote iwayo.

**Tatu**, Siri ya mafanikio ya Waislamu ya kusimamisha na kuendeleza Dola ya Kiislamu ni kule kumtii kwao Allah(s.w) na Mtume wake katika kila waliloamrisha na kila walilokatazwa kwa shauku kubwa ya kupata radhi za Allah(s.w) na kuepukana na ghadhabu zake.

## **Mkataba wa Hudaybiyah**

Mkataba wa Hudaybiyah ni mkataba uliofungwa baina ya Waislamu na Makafiri wa Kiquraish katika kitongoji cha Hudaybiyah kilicho karibu na Makka. Katika mwaka 6 A.H. Mtume(s.a.w) aliota kuwa anafanya 'Umrah katika nyumba takatifu ya *Al-Ka'abah*. Kwa kuwa ndoto za Mitume ni agizo la moja kwa moja kutoka kwa Allah(s.w), Mtume(s.a.w) ilibidi atekeleze agizo hilo kwa kuwakusanya Waislamu wapatao 1,400 wa kuongozana naye kwenye msafara wa kuelekea Makka kwa ajili ya 'Umarah. Makafiri wa Kiquraish waliwazuia Waislamu hao pamoja na Mtume(s.a.w) kuingia Makkah, katika kitongoji cha *Hudaybiyah*. Mtume(s.a.w) alituma wajumbe wawili, mmoja baada ya mwingine,

kuwaomba wakuu wa Maquraish kuwa wawaruhusu waingie Makka na kuwahakikishia kuwa wanaingia kwa amani kwa ajili tu ya kufanya Umarah na hawakuwa na silaha yoyote. Baada ya wajumbe hawa kukataliwa na Maquraish, Mtume(s.a.w) alimtuma mjumbe wa tatu, 'Uthman bin Affan, ambaye kulingana na heshima yake kwa Maquraish, ilitarajiwa kuwa ujumbe wake ungelikubaliwa. Kinyume chake, 'Uthman alishikiliwa kwa kitambo kirefu na zikaja tetesi kuwa ameuliwa. Baada ya kupata tetesi hizi Mtume(s.a.w) aliwaita Waislamu chini ya mti na kuchukua ahadi (Bai'yah) kwao ya kulipiza kisasi cha kuuliwa 'Uthman. Allah(s.w) aliitilia mkazo ahadi hii kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

إِنَّ الَّذِينَ يُبَايِعُونَكَ إِنَّهُمْ بَايَعُوا اللَّهَ يَدُ اللَّهِ  
 فَوْقَ أَيْدِيهِمْ فَمَنْ نَكَثَ فَإِنَّمَا يَنْكُثُ عَلَىٰ نَفْسِهِ ۗ وَمَنْ أَوْفَىٰ بِمَا  
 عَاهَدَ عَلَيْهِ اللَّهُ فَسَيُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿١٠﴾

*Bila shaka wale wanaofungamana nawe, kwa hakika wanafungamana na Mwenyezi Mungu. Mkono wa Mwenyezi Mungu uko juu ya mikono yao. Basi avunjaye ahadi (hizi) anavunja kwa kuidhuru nafsi yake; na atekelezaye aliyomuahidi Mwenyezi Mungu, (Mwenyezi Mungu) atamlipa ujira mkubwa. (48:10)*

﴿لَقَدْ رَضِيَ اللَّهُ عَنِ الْمُؤْمِنِينَ إِذْ يُبَايِعُونَكَ تَحْتَ الشَّجَرَةِ فَعَلِمَ مَا فِي

قُلُوبِهِمْ فَأَنْزَلَ السَّكِينَةَ عَلَيْهِمْ وَأَثَبَهُمْ فَتْحًا قَرِيبًا ﴿١٨﴾﴾

*Kwa hakika Mwenyezi Mungu amewapa radhi Waislamu walipofungamana nawe chini ya mti; na alijua yaliyomo nyoyoni mwao. Basi akateremsha utulivu juu yao, na akawapa kushinda kwa zama za karibu. (48:18)*

Baada ya Waislamu kuchukua bai'yah kwa Mtume(s.a.w) iligundulika kuwa zile tetesi za kuuliwa 'Uthman zilikuwa za uwongo na 'Uthman alirudi kutoka kwa Maquraish akiwa salama. Hata hivyo, ilikuwa dhahiri kwa Maquraish kuwa kamwe

hawanauwezo wa kuwazuia Waislamu kuingia Makka wakiyakumbuka vyema matukio ya Badr, Uhud na Handaq.

Hivyo waliamua kumtuma **Suhail bin 'Amr**, kwa niaba yao aje kuweka mkataba wa amani na **Mtume(s.a.w)** kwa niaba ya Waislamu. Baada ya mjadala mrefu pande zote mbili ziliafikiana kuweka mkataba wa amani wa miaka kumi (10) wenye masharti yafuatayo:

- (i) Waislamu warudi Madinah bila ya kufanya 'Umrah.
- (ii) Waislamu wanaweza kurudi mwakani (7 A.H) kufanya 'Umrah lakini wakae Makka siku tatu tu.
- (iii) Wakija Makka kufanya 'Umrah wasije na silaha yoyote ila panga ndani ya ala.
- (iv) Waislamu hawataenda nao Madinah Waislamu wanaoishi Makka na wala hawatamzuia yeyote miongoni mw ao anayetaka kubakia Makka.
- (v) Kama yeyote wa Makka atatoroka kwenda Madinah kusilimu Waislamu hawanabudi kumrudisha(wasimmpokee), lakini yeyote kutoka Madinah akitoroka kwenda Makka Maquraish hawatapaswa kumrudisha Madinah (watampokea).
- (vi) Makabila ya Kiarabu yatakuwa huru kufanya Itifaki (urafiki) na upande wowote ule (wa Maquraish au wa Waislamu) wanaoupendelea.
- (vii) Pasiwe na vita kwa kipindi cha miaka kumi baina ya Waislamu na Maquraish na baina ya Waitifaki (Allies) wa Waislamu na waitifaki wa Maquraish.
- (viii)Hapana ruhusa ya kutengua hata shuruti moja katika hizi kabla ya miaka kumi kupita.

Mkataba huu ulitiwa sahihi na **Muhammad bin ‘Abdullah (s.a.w)** kwa niaba ya **Waislamu** na **Suhail bin ‘Amr** kwa nia ya Maquraish. Baadhi ya Waislamu walichukizwa sana na mkataba kutokana na mazingira ya ushabiki na unyanyasaji yaliyodhihirishwa na Maquraish. Suhail alikataa mkataba usianzwe kwa **Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim**, kama ilivyo Sunnah kwa Waislamu katika kuanza kila jambo lao. Pia Suhail alikataa mkataba usiwe baina yake na “**Muhammad Rasuulullah**”, wao hawamtambui kuwa ni “Rasuulullah” (Mjumbe wa Allah), bali wanamtambua kuwa ni “**Muhammad bin Abdullah bin Abd-al-Muttaalib**”. Baadhi ya Waislamu pia waliona kuwa baadhi ya vipengele vya masharti ya makataba, hasa kipengele cha tano (5), vilikuwa vikiwanyanyasa na kuwakandamiza Waislamu, kiasi kwamba wengine walifikia hatua ya kumshawishi Mtume(s.a.w) kuwa waukatae mkataba ule. Kwa mfano kabla mkataba kutiwa sahihi na pande zote mbili, Abu Jandal bin Suhail, aliyekuwa akipata mateso kwa ajili ya kusilimu kwake, alimkimbilia Mtume(s.a.w) ili apate salama. Suhail alidai kuwa Abu Jandal arudishwe, kwa mujibu wa kipengele cha tano (5) cha mkataba. Aliporudishwa Suhail alimcharaza viboko vya miba pale pale kadamnas: Umar bin Khattab hakuweza kuvumilia hali ile na alimuuliza Mtume(s.a.w) kwa uchungu: “Wewe si Mtume wa kweli wa Allah(s.w)? Je, sisi hatuko katika njia ya haki?” Mtume(s.a.w) alijibu kuwa yeye ni Mtume wa Allah(s.w) na kuwa wao wako katika njia sahihi, pia alimfahamisha kuwa anafanya kila jambo kama alivyoamrisha na Allah(s.w).

Kwa upande mwingine, machoni mwa Allah(s.w) na Mtume wake na kwa baadhi ya waislamu wenye uoni wa mbali, mkataba ule ulikuwa ni ushindi kwa Waislamu. Mkataba kutoandikwa “**Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim**” na “**Muhammad Rasuulullah**”, hakukuwapunguzia Waislamu chochote. Vile vile kuteswa kwa akina Abu Jandal ni jambo la muda mfupi. Hivyo, Mtume(s.a.w) alitia sahihi mkataba na akawaamuru Waislamu wachinje na kunyoa pale pale na kurejea zao Madinah. Njiani, kabla ya

Waislamu hawajafika Madinah, Mtume(s.a.w) alishushiwa wahay wa kuwapongeza Waislamu kwa ushindi watakaoupata kutokana na mkataba wa Hudaybiyah.

إِنَّا فَتَحْنَا لَكَ فَتْحًا مُّبِينًا ﴿١﴾ لِيُغْفِرَ لَكَ اللَّهُ مَا

تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِكَ وَمَا تَأَخَّرَ وَيُتِمَّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكَ وَيَهْدِيَكَ

صِرَاطًا مُسْتَقِيمًا ﴿٢﴾

*Bila shaka tumekwisha kupa kushinda kuliko dhahiri. Ili Mwenyezi Mungu akusamehe makosa yako yaliyotangulia na yanayokuja, na kukutimizia neema zake na kukuongoa katika njia iliyonyooka(48:1-2).*

## **Kusibu kwa Bishara ya Ushindi**

“Kushinda kuliko dhahiri” kunakotokana na mkataba wa Hudaybiyah kunabainika katika matukio ya fuatayo:

**Kwanza**, kuwapa fursa Waislamu wa Madinah kubakia Makka au kuja Makka mara kwa mara kufanya Da’awah. Kwa mujibu wa wanahistoria, katika kipindi cha miaka miwili tu ya mkataba wa Hudaybiyah, watu waliosilimu Makka ni wengi zaidi kuliko wale waliosilimu katika miaka yote ya nyuma. Ni katika kipindi hiki walisilimu majemadari wa Kiquraish, Khalid bin Walid na ‘Amr bin al-‘As pamoja na Suhail bin Amr mwenyewe.

**Pili**, maquraish wenyewe waliomba lile sharti la kuwazuia watu wa Makka waliosilimu kwenda Madinah liondolewe kwa sababu wale wote waliokataliwa kujiunga na Waislamu wenzao Madinah, Ibn Abu Jandal na wenzake, waliweka kambi njiani na kuwa kikwazo kikubwa kwa misafara ya biashara ya Maquraish. Maquraish wakaomba waruhusiwe kuingia Madinah ili nao wawe ndani ya mkataba wa amani wa Hudaybiyah.

**Tatu**,Mtume(s.a.w) na Waislamu kwa ujumla walipata fursa ya kulingania Uislamu kwa watu wa karibu na mbali. Ni katika kipindi cha mkataba, Mtume(s.a.w) alituma wajumbe na barua kwa falme mbali mbali za Bara Arab na nje ya Bara Arab. Alikumbusha Waislamu kuwa jukumu la kuufikisha Uislamu kwa watu si lake peke yake bali ni la kila Muislamu. Katika kuwakumbusha hili Mtume(s.a.w) aliwahutubia Waislamu:

*“Enyi watu! Allah(s.w) amenituma kuwa Rehema kwa wanaadamu (wote) na kuwa Mtume wa ulimwengu mzima. Kwa hiyo, linganieni Uislamu kwa niaba yangu na Allah atakurehemuni. Kwa hiyo nakuusieni msifarikiana kama (watu wa) Isa mwana wa Mariam”<sup>21</sup>*

Baada ya khutuba hii, Mtume(s.a.w) aliteua wajumbe wenye akili (intelligent) na uwezo wa kujieleza, miongoni mwa maswahaba wake na kuwapa barua za kupeleka kwa tawala mbali mbali za nchi za Mashariki ya kati ikiwa ni pamoja na Misri na Uhabeshi. Takriban barua zote zilikuwa na maudhui moja zikizingatia mazingira ya mtawala anayepelekewa. Kwa mfano barua aliyopelekewa Heracleus, mfalme wa Warumi iliandikwa kama ifuatavyo:

*Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu;*

*Kutoka kwa Muhammad bin ‘Abdullah kwenda kwa Heracleus, mfalme wa Warumi (Eastern Roman Empire). Amani iwe juu ya yule anayefuata mwongozo. Baada ya hayo ninakuitia kwenye Uislamu. Ukisilimu utakuwa katika amani na Allah(s.w) atakulipa mara dufu. Lakini ukikataa wito huu madhambi ya raia zako utayabeba. Akanukuu aya ya Qur-an ifuatayo:*

قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ تَعَالَوْا إِلَى كَلِمَةٍ سَوَاءٍ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ أَلَّا نَعْبُدَ إِلَّا اللَّهَ  
وَلَا نُشْرِكَ بِهِ شَيْئًا وَلَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضًا أَرْبَابًا مِّن دُونِ اللَّهِ فَإِن تَوَلَّوْا  
فَقُولُوا أَشْهَدُوا بِأَنَّا مُسْلِمُونَ ﴿١٤﴾

“Sema: Enyi watu waliopewa kitabu (Mayahud na Manasara) njooni katika neno lililo sawa baina yetu na baina yenu, ya kwamba tusimuabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu wala tusimshirikishe (Mwenyezi Mungu) na chochote; wala baadhi yetu tusiwafanye wengine kuwa waungu badala ya Mwenyezi Mungu (au pamoja na Mwenyezi Mungu). Wakikengeuka semeni: Shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu.” (3:64)

**Nne**, Waislamu walipata fursa ya kujiimarisha kiuchumi. Kwa kuondokewa na adui yao mkubwa, makafiri wa Kiquraish, Waislamu waliweza kufanya biashara zao za masafa marefu kwa amani.

**Tano**, Waislamu walipata fursa ya kujizatiti kijeshi na kuwashughulikia maadui zao wengine waliokuwa wakiwakera mara kwa mara. Ni katika kipindi hiki waliwashinda Mayahudi kimoja katika vita vya Khaybar. Pia waliwaonyesha Warumi cha “Mtema kuni” katika vita vya Muttah vilivyopiganwa 7 A.H. Kumbukizi za vita hivi ziliwatia Warumi khofu na woga. Pamoja na ushujaa wao uliofahamika katika ulimwengu wa enzi hizo, waliwakimbia Waislamu katika vita vilivyokuwa vipiganwe Tabuuk.

**Sita**, Waislamu 2,000 walifanya ‘Umrah pamoja na Mtume (s.a.w), mwaka wa 7 A.H. na ndoto ya Mtume ikawa imesadifu:



لَقَدْ صَدَقَ اللَّهُ رَسُولَهُ الرُّسُلَ بِالْحَقِّ لَتَدْخُلُنَّ الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ إِنِ شَاءَ

اللَّهُ عَامِنِينَ مُحَلِّقِينَ رُءُوسَكُمْ وَمُقَصِّرِينَ لَا تَخَافُونَ فَعَلِمَ مَا لَمْ تَعْلَمُوا

فَجَعَلَ مِنْ دُونِ ذَلِكَ فَتْحًا قَرِيبًا ﴿٢٧﴾

*Kwa yakini Mwenyezi Mungu amemhakikishia Mtume wake ndoto yake ya haki; Bila shaka nyinyi mtaingia katika Msikiti Mtukufu Insha-Allah kwa salama; mkinyoa vichwa vyenu na mkipunguza nywele (kama ilivyo wajibu kufanya hivyo wakati wa Hija). Hamtakuwa na hofu (wakati huo). Na (Mwenyezi Mungu) anajua msiyoyajua. Basi kabla ya haya atakupeni kushinda (kwanza) kuliko karibu (kuwashinda Mayahudi). (48:27)*

Ni ushindi kwa sababu Mtume(s.a.w) katika ndoto yake hakufahamishwa ni lini atafanya 'Umrah, japo alijiandaa kuitekeleza katika mwaka wa 6 A.H. Vile vile ni ushindi kwa sababu idadi ya Waislamu waliofanya 'Umrah mwaka 7 A.H. ni kubwa zaidi kwa watu 600 kuliko wale waliokuwa kwenye msafara wa mwanzo ambao walikuwa 1,400 tu.

**Saba**, baada ya muda mfupi Maquraish waling'amua kuwa mkataba wa Hudaybiyah haukuwa unawanufaisha wao bali kinyume chake. Hivyo waliamua kuuvunja baada ya miaka miwili tu. Mtume(s.a.w) alichukua fursa ile ya kuvunjika kwa mkataba kuikomboa Makka. Katika kuikomboa Makka hapakutakiwa kutokee mapigano, kwani ingelikuwa vigumu kuwatambua Waislamu walioko Makka ambao walisilimu katika miaka miwili ya mkataba na wale walioshindwa kuhamia Madinah kutokana na sababu za msingi. Hivyo Mtume(s.a.w) aliandaa jeshi kubwa la askari 10,000 kwa siri kisha likaja kuzingira Makka ghafla bila Maquraish kupata habari. Abu Sufyan, kiongozi wa Makka wakati huo, Ramadhani, 8 A.H, ilibidi asalimu amri na kuwaachia Waislamu kuikomboa na kuitwahirisha Ka'abah bila ya upinzani.

**Nane**, ukombozi wa Makka,(Fat-h Makka) ulikuwa ndio kilele cha ushindi kwani, takriban viongozi wote wa Maquraish walisilimu, akiwemo Abu Sufyan na mkewe Hindu bint ‘Utbah aliyekuwa adui nambari “one” wa Mtume(s.a.w). Kusilimu kwa viongozi wa Makka kulichangiwa sana na ile tabia ya usamehevu na huruma aliyoonesha Mtume(s.a.w). Baada ya kuikomboa Makka alitangaza kuwa wamesamehewa wote kwa yale yote waliyowafanyia Waislamu kwa kipindi cha miaka 21 iliyopita kama Nabii Yusufu(a.s) alivyowasamehe ndugu zake.

قَالَ لَا تَثْرِيْبَ عَلَيْكُمْ اَلْيَوْمَ يَغْفِرُ اللّٰهُ لَكُمْ وَهُوَ اَرْحَمُ

الرَّحِيْمِ ﴿٩٢﴾

*Akasema (Yusufu): “Hakuna lawama juu yenu leo; Mwenyezi Mungu atakusameheni, naye ni Mwenye rehema zaidi kuliko wanaorehemu (wote).” (12:92)*

Kwa msamaha huu viongozi wa maquraish waliyakinisha kuwa Muhammad(s.a.w) ni Mtume wa Allah aliye rehema kwa walimwengu wote.

وَمَا اَرْسَلْنَاكَ اِلَّا رَحْمَةً لِّلْعٰلَمِيْنَ ﴿١٠٧﴾

*Nasi hatukukutuma, (hatukukuleta) ila uwe rehema kwa walimwengu (wote). (21:107)*

Kusilimu kwa wakuu wa kabila tukufu la Quraish, kulipelekea makabila mengi ya Kiarabu kuja kusilimu kwa Mtume(s.a.w) makundi kwa makundi.

**Tisa**, Baada ya **Fat-h Makka** dola ya Kiislamu ilitanuka. Katika kuimarisha Dola, Mtume(s.a.w) aliigawanya katika majimbo matano na kwa kila jimbo aliteua viongozi watatu wafuatao:

- (1) Mkuu wa Jimbo - Walii (Gavana)
- (2) Kadhi – Hakimu.
- (3) Amil – Mkusanyaji na mgawaji Zakat

Mtume(s.a.w) alikuwa mkuu wa Jimbo la Madinah.

## **Mafunzo Yatokanayo na Mkataba wa Hudaybiyah.**

Kutokana na mkataba wa amani wa Hudaybiyah tunajifunza kuwa:

- (i) Mazingira ya amani ni jambo muhimu mno katika kuleta maendeleo ya aina yoyote. Hivyo, ni vyema kukimbilia mapatano kuliko mapambano.
- (ii) Katika kutafuta suluhu, lazima tuwetayari kupoteza maslahi madogo madogo kama vile kuacha “**Bismillah**” na “**Rasuulullah**” kwenye mkataba wa Hudaybiyah, ili kujenga mazingira yatakayotuwzesha kufikia lengo kuu la Uislamu kuwa juu ya tawala zote:

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظَاهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ ۗ

وَكَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا ﴿٢٨﴾

*Yeye ndiye aliyemtuma, (aliyemleta) Mtume wake kwa uwongofu na dini iliyo ya haki, ili aishindishe juu ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Shahidi. (48:28)*

- (iii)Waislamu tuwe wepesi katika kutumia fursa zinazopatikana. Mtume(s.a.w) alikuwa mwepesi mno katika kutumia fursa. Kwa mfano Mtume(s.a.,w) alitumia fursa ya kuvunjika mkataba wa Hudaybiyah kuikomboa Makka kabla Maquraish hawajajiweka sawa.

## Hija ya Kuaga

Mwaka mmoja baada ya msafara wa Tabuuk Bara Arab zima ilikuwa chini ya Dola ya Kiislamu. Kutokana na ujumbe wa Suratun-Nasr, sura ya mwisho kushuka, iliyoshuka baada ya Fat-h-Makka, na ukizingatia makundi ya watu kutoka makabila mbali mbali yalivyomininika Madinah kuja kusilimu na kujifunza Uislamu, baada ya msafara wa Tabuuk, ilikuwa wazi kwa Mtume(s.a.w) kuwa ujumbe wake umekamilika na kazi yake ya Utume imekaribia kwisha.

إِذَا جَاءَ نَصْرُ اللَّهِ وَالْفَتْحُ ① وَرَأَيْتَ النَّاسَ يَدْخُلُونَ فِي دِينِ اللَّهِ

أَفْوَاجًا ② فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَأَسْتَغْفِرْهُ إِنَّهُ كَانَ تَوَّابًا ③

*Itakapofika nusura ya Mwenyezi Mungu na kushinda. Na ukawaona watu wakiingia katika dini ya Mwenyezi Mungu makundi makundi. Basi hapo mtakase Mola wako pamoja na kumsifu, umuombe maghufira (msamaha); hakika Yeye ndiye Apokeaye toba. (110:1-3)*

Mtume(s.a.w) hakuweza kushiriki kwenye Hija ya kwanza iliyofanyika 9 A.H. kutokana na shughuli nzito aliyokuwa nayo ya kupokea makundi kwa makundi ya makabila mbali mbali yaliyomininika Madinah kuja kusilimu. Badala yake alimteua Abubakar kuongoza msafara wa Hija hiyo. Mwaka 10 A.H. Mtume(s.a.w) alinuia kufanya Hija kubwa na kuwajumuisha Waislamu wengi iwezekanavyo. Alituma wajumbe kwenda kwenye kona zote za Bara Arab kuwatangazia Waislamu kuwa waje kujiunga naye kwenye msafara wa Hija. Waislamu waliitikia wito na waliojiunga na msafara wa Hija ya Mtume kutoka Madinah ni 100,000 na jumla ya Waislamu waliosimama Arafa mwaka ule ni 120,000.

## **Hutuba ya Mtume(s.a.w) Katika Uwanja wa ‘Arafa, 9 Dhul-Hijjah 10 A.H.**

Mchana wa 9 Dhul-Hijjah, Mtume(s.a.w.) akiwa juu ya ngamia wake alitoa hutuba ya kihistoria kwa mkusanyiko wa Waislamu laki moja na zaidi kama ifuatavyo:

*“Sifa zote anastahiki Allah, Tunamshukuru na tunamtaka msaada na msamaha na tunatubu kwake, Tunajikinga kwa Allah (s.w.) kutokana na uovu wetu na kutokana na ubaya unaotokana na matendo yetu (maovu). Hapana awezaye kumpoteza aliyeongozwa na Allah na hapana awezaye kumuongoza aliyepotezwa na Allah. Ninashuhudia kuwa hapana Mola ila Allah pekee asiye na mshirika. Ninashuhudia kuwa Muhammad ni mja na Mtume wake. Ninawausia enyi waja wa Mwenyezi Mungu, kumcha Mwenyezi Mungu na ninakusisitizeni kumtii Allah. Ninafungua khutuba yangu hii, na lile lililo zuri”.*

*“Enyi watu, sikilizeni ujumbe ninaokupeni. Sijui kama nitapata fursa nyingine ya kukutana na nyinyi baada ya mwaka huu.*

*“Enyi watu, hakika damu yenu (yaani uhai wenu), mali zenu na heshima yenu ni vitu vitukufu, katu visiharibiwe hadi mtakaposimamishwa mbele ya Mola wenu, kwani utukufu wa vitu hivyo ni kama ilivyo utukufu wa siku hii, wa mwezi huu na wa mji huu. Kwa hakika mtakutana na Mola wenu na atakuulizeni juu ya vitendo vyenu. Je, nimefikisha ujumbe? Ewe Mwenyezi Mungu shuhudia”.*

*“Hivyo, kila aliye na amana yoyote, hana budi kumrejeshea mwenyewe”*

*“Kumbukeni, hakuna atakayebeba lawama kwa kosa lolote isipokuwa yule aliyelitenda kosa hilo. Mtoto hawezi kulaumiwa kwa kosa la baba wala baba kwa kosa la mwanawe”.*

*“Enyi watu, yasikilizeni maneno yangu na yazingatieni. Fahamuni kuwa Muislamu ni ndugu wa Muislamu, na Waislamu wote ni ndugu wamoja. Si halali kwa Muislamu kuchukua chochote kutoka kwa nduguye Muislamu isipokuwa kile alichoruhusiwa. Hivyo msioneane. Yaa Allah, nimefikisha ujumbe?”*

*“Fahamuni, mambo yote ya ujahili yamewekwa chini ya nyayo zangu. Visasi vya damu vya zama za jahiliya vimeondolewa. Hakika, kisasi cha damu cha kwanza ninachokifuta ni kile cha Ibn Rabi’ah ibn Harith aliyelelewa na kabila la Sa’d na ambaye Wa-Hudhail walimwua.*

*Riba za kipindi cha jahiliya zimefutwa. Lakini mtapata mtaji wenu. Msidhulumu nanyi hamtadhulumiwa. Allah amekataza riba. Riba ya kwanza ninayoifuta ni ile ya Abbas ibn Abdul Muttalib. Imefutwa moja kwa moja.*

*“Enyi watu, mcheni Allah kuhusiana na wanawake. Mmewaoa kwa amana ya Allah na mnawaingilia kwa amri ya Allah.*

*Hakika mnazo haki kutoka kwao na wanawake wanazo haki kutoka kwenu. Haki zenu kwao ni kwamba wasimruhusu mtu yeyote kuvuruga vitanda vyenu na wasimruhusu mtu yeyote msiyemridhia kuingia katika nyumba zenu. Wakifanya hivyo Allah amewaruhusu nyinyi kuwakemea, kutengana nao vitanda na kuwapiga lakini siyo kwa nguvu, wakijirekebisha basi na wapewe kwa haki chakula chao na mavazi yao kutoka kwenu.*

*Yapokeeni kwa wema mafundisho haya juu ya wanawake. Kwani wao ni wasaidizi wenu. Hawamiliki kwa ajili ya nafsi zao chochote, nanyi hamwezi kumiliki chochote kutoka kwao kisichokuwa hicho. Wakikutiini basi kaeni nao kwa wema. Je, sijafikisha ujumbe?*

*“Enyi watu, msikilizeni na mtiini Amiri anayetokeleza kitabu cha Allah miongoni mwenu hata kama atakuwa ni mtuwa wa Kihabeshi”.*

*“Enyi watu, hakika Allah amekadiria kila mtu riziki yake. Wasia haujuzu kwa mrithi na wasia si halali ukiwa zaidi ya theluthi ya mali”.*

*“Mtoto ni wa kitanda cha halali na mzinifu arujumiwe. Mtu anayejinasibisha (ukoo wake) kwa asiyekuwa baba yake humshukia laana ya Allah, Malaika na watu wote. Allah hatakubali kutoka kwa mtu kama huyo toba wala amali njema. Enyi watu, shetani amehuzunishwa sana kwa kutoabudiwa tena katika hii nchi yenu. Lakini anatosheka na kule kutiwa katika mambo ambayo nyinyi mnadhani ni madogo. Hivyo kuweni waangalifu sana katika dini yenu.*

*Kwa hakika nimekuachieni vitu viwili ambavyo iwapo mtavishika katu hamtapotea – Kitabu cha Allah na Sunnah za Mjumbe wake.*

*“Enyi watu, Jibril amenijia, amenisomea salaam kutoka kwa Mola wangu na amesema, Hakika Allah amewasamehe watu wa ‘Arafat na wa Ka’abah na amechukua dhamana ya kuwasamehe upungufu wao”.*

*‘Umar-ibnul Khattab akasimama na kuuliza: “Ya Rasulullahi, msamaha huo ni kwa ajili yetu sisi tu?” Akajibu: “Ni kwa ajili yenu na kwa ajili ya wale watakaokuja baada yenu hadi siku ya Kiyama”.*

*“Na mtaulizwa juu yangu, mtajibu vipi?” Wakasema: “Tunashuhudia kwamba umefikisha ujumbe, umetimiza wajibu wako na umetunasihi.”*

*Halafu akasema hali ya kuwa amekiinua kidole chake cha pete na kukielekeza mbinguni: “Ya Allah shuhudia, Yaa Allah, Shuhudia, Yaa Allah, Shuhudia”.<sup>22</sup>*

Baada ya hutuba hii Mtume(s.a.w.) alimuamuru Bilal atoe adhana kisha wakaswali jamaa ya Adhuhuri pamoja na Asr kwa rakaa mbili mbili (Qasr). Baada ya swala Mtume(s.a.w.) alishushiwa Wahay unaokamilisha kazi yake na akasoma aya hiyo mbele ya watu wote waliohudhuria Hija mwaka ule:

....الْيَوْمَ يَئِسَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِن دِينِكُمْ فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَاخْشَوْنَ الْيَوْمَ  
أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتَمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيْتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا...

“.....Leo waliokufuru wamekata tamaa katika dini yenu, basi msiwaogope bali niogopeni mimi. Leo nimekukamilishieni dini yenu na kukutumizieni neema yangu, na nimekupendeleeni Uislamu uwe Dini yenu.....” (5:3)

Pamoja na nasaha nzito alizotuachia katika khutuba yake ya kuaga, Mtume(s.a.w) alimalizia kwa kuwatumainisha Waislamu wa zama zote:

“Kwa hakika nimekuachieni vitu viwili ambavyo iwapo mtavishika katu hamtapotea – Kitabu cha Allah na Sunnah za mjumbe wake.”

## **Ugonjwa wa Mtume(s.a.w) na Kufariki kwake**

Miezi miwili baada ya Hijjat-al-Wada, Mtume(s.a.w.) alishikwa na ugonjwa wa kuumwa kichwa na homa. Lakini muda wote alikuwa akijitokeza kufanya shughuli zake kama kawaida. Katika hali hiyo hiyo ya kuumwa, alikwenda Uhud na kuwaombea dua mashahidi waliozikwa mle. Pale alitoa khutuba ifuatayo:

“Siwahofii kuwa mtajihusisha na kuabudu masanamu baada yangu, lakini nahofia kuwa mtajihusisha sana na dunia kiasi cha kufikia hatua ya kuuana wenyewe kwa wenyewe. Kisha, mkishafanya hivyo, mtaishia kwenye maangamivu kama



*walivyoangamia wa kabla yenu”.*

Mtume(s.a.w.) pamoja na maradhi yake aliendelea kuswalisha swala za jamaa msikiitni na bado alikuwa akitimiza ngono za wake zake wote tisa. Ugonjwa ulipozidi kushitadi, aliwaomba wakeze kuwa waje kumuuguza kwa Bibi Aysha(r.a.) palipo kuwa karibu na msikiti. Wakeze walikubali kwa moyo mkunjufu. Ugonjwa ulivyoendelea Mtume(s.a.w.) alizidi kuwa dhaifu na hatimaye alishindwa hata kuhudhuria swala za jamaa msikitini. Aliposhindwa kuhudhuria msikitini alitoa amri Abubakar awe anaongoza swala ya jamaa, alifanya hivyo kwa siku kadhaa.

Siku nne kabla ya kufariki kwake, Mtume(s.a.w.) alijisikia nafuu kidogo na akakoga kabla ya swala ya Dhuhuri. Baadaye alikuja msikitini akiwa amesaidiwa na watu wawili, Abbas(r.a.) na Ally(r.a.). Abubakar alikuwa anaendelea kuongoza swala kama kawaida. Alipomuona Mtume(s.a.w.) anakuja alianza kuondoka, lakini Mtume alimuambia abakie pale pale naye akakaa pembeni mwake. Baada ya swala alihutubia kama ifuatavyo:

*“Allah amempa mja wake achague kati ya dunia na akhera. Akachagua akhera. Ninawausia, Enyi Waislamu (Muhajirina) muwe wema kwa Ansar. Hakika wameteteleza wajibu wao vizuri. Waislamu kwa ujumla wao idadi yao itaongezeka lakini Ansar watafungua na kuwa kama chumvi katika chakula. Zimeangamia umma zilizotangulia ambazo ziliabudu makaburi ya Mitume wao na ya watu wema. Ninawakatazeni kufanya hivyo. Nina deni kubwa (la Ihsani) kwa Abubakar. Kama ingekuwa nimfanye yeyote kuwa rafiki yangu, angalikuwa Abubakar, lakini uhusiano (udugu) wa Uislamu unatosha. Ee, binti yangu Fatimah na Ee, shangazi yangu mpendwa, Swafiyah, fanyeni amali kwa ajili ya akhera kwani sitaweza kuwasaidia chochote dhidi ya hukumu ya Allah.”<sup>23</sup>*

Hii ilikuwa khutuba ya mwisho ya Mtume (s.a.w.). Kisha ugonjwa ulishitadi. Alijisikia nafuu kidogo asubuhi ya Jumatatu ya

mwezi 12 Rabi'ul-Awwal, 11 A.H, lakini ilipofika aduhuri hali ilibadilika tena kuwa mbaya. Alikuwa akizimia kila baada ya muda mfupi. Hata alipokuwa katika hali hii ya sakaratul-maut, bado hakumsahau Mola wake. Muda wote alikuwa akisema “Nisamehe Bwana wangu”. Wakati wa alasiri alipokuwa anapumua pumzi za mwisho mwisho, alisikika kwa sauti ndogo akisema:

*“Shikamana na swala na wafanyieni wema watumwa (wafungwa)”.*

Palikuwa na beseni la maji lililowekwa karibu na Mtume (s.a.w.). Alikuwa akilowesha viganja vyake mara kwa mara kwenye maji haya na kufuta uso wake, huku akisema, *“Enyi watu! Hakika kutoka roho kuna machungu makubwa”*. Wakati huo aliingia mtu mmoja na mswaki mkononi mwake. Mtume akaashiria apewe mswaki huo. Alitafuniwa na Bibi Aysha, ambaye alimpakata mapajani mwake, na kumpa akawa anaswakia kidogo kidogo. Kisha akiwa ameashiria kwa kidole (cha shahada) na huku ametazama juu alisema mara tatu:

*“Nakwenda kwa rafiki yangu mtukufu,  
Nakwenda kwa rafiki yangu mtukufu,  
Nakwenda kwa rafiki yangu mtukufu”.*

Roho yake ilirudi kwa Bwana na Mola wake mtukufu wakati wa jioni ya Jumatatu ya mwezi 12 Rabi'ul Awwal, 11 A.H, Sawa na tarehe 8 Juni 632 A.D. Mtume(s.a.w.) alifariki akiwa na umri wa miaka 63. Mazishi yake yalifanyika siku iliyofuatia. Waliomwosha ni jamaa zake wa karibu – Fadhil bin Abbas, Ally bin Abu Talib na Usamah bin Zaid(r.a.). Kisha alizikwa kwenye chumba cha Bibi Aysha(r.a.) pale pale alipofia. Hivi sasa kaburi la Mtume(s.a.w.) limo ndani ya Msikiti wa Madinah.

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ  
 وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ، اللَّهُمَّ بَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ  
 مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ.

*“Ee Allah! Mrehemu Muhammad na wafuasi wa Muhammad kama ulivyomrehemu Ibrahim na wafuasi wa Ibrahim. Hakika wewe U-mtukufu na Msifiwa wa haki “Ee Allah! mbariki Muhammad na wafuasi wa Muhammad kama ulivyombariki Ibrahim na wafuasi wa Ibrahim. Hakika wewe U-mtukufu na Msifiwa wa haki.*

### **Zoezi la 3**

1. (a) Mtume(s.a.w) alizaliwa katika kipindi cha Jahiliya:  
 Kipindi cha Jahiliya ni kipindi gain ?  
 (b) Nini tofauti ya Jahili na Kafiri?  
 (c) Toa maelezo mafupi juu ya tabia ya wakazi wa Bara Arab katika kipindi cha Jahiliya.
2. Nukuu aya ya Qur’an inayobainisha lengo la kuletwa Mtume Muhammad(s.a.w) na kisha unukuu aya inayothibitisha kuwa Mtume(s.a.w) alifikia lengo hilo.
3. (a) Mtume(s.a.w) aliandaliwa ki-il-hamu na kimafunzo. Toa ufafanuzi juu ya kauli hii.  
 (b) Bainisha matukio matano(5) yanayothibitisha kuwa Mtume(s.a.w) aliandaliwa ki-il-hamu.  
 (c) Wanaharakati wa kiislamu wanajifunza nini kutokana na kuandaliwa Mtume(s.a.w) ki-il-hamu na kimafunzo?

4. (a) Mtume(s.a.w) alianza kulingania uisImau kwa siri: Fafanua.  
 (b) Toa mafunzo matano(5) yatokanayo na Mtume(s.a.w) kuanza kulingania Uislamu kwa siri kish akwa dhahiri.
5. *Wanataka kuzima Nuru ya Mwenyezi Mungu(ya Uislamu) kwa vinywa vyao; na Mwenyezi Mungu atakamilisha Nuru yake ijapokuwa makafiri watachukia.(61:8)*  
 Chambua mbinu walizozitumia makafiri wa Makka katika kutaka kuzima nuru ya Allah(s.a.w) wakati wa Mtume(s.a.w)
6. Bainisha mchango wa Bibi Khadijah, mkewe Mtume(s.a.w) na Abu Twalib katika kuuhami Uislamu katika kipindi cha Makka cha utume.
7. (a) Toa maelezo mafupi juu ya Israa na Mi'raj.  
 (b) Safari ya Mtume(s.a.w) ya Israa na Mi'raj ilikuwa na malengo mawili: Bainisha malengo haya
8. (a) Kwanini waarabu kutoka Yathri'b waliukubali Uislamu kwa wepesi ukiwalinganisha na wakabila mengine ya waarabu?  
 (b) Toa maelezo mafupi juu ya mikataba miwili ya 'Aqabah.
9. (a) Hijrah ya Mtume(s.a.w) na Abubakar(r.a) inatupa mafunzo yafuatayo:  
 (i) \_\_\_\_\_ (ii) \_\_\_\_\_ (iii) \_\_\_\_\_ (iv) \_\_\_\_\_ (v) \_\_\_\_\_  
 (b) Ni upi umuhimu wa Hijrah katika Uislamu?
- 10.(a) Bainisha maadui wakuu watano(5) na vitimbi vyao dhidi ya Dola ya kiislamu Madinah wakati wa Mtume(s.a.w).  
 (b) Onesha namna Mtume(s.a.w) alivyowashughulikia maadui wa Dola ya Kiislamu Madinah

11. (a) Mkataba wa Hudaybiyah ni \_\_\_\_\_
- (b) Ni mazingira yapi yaliyopelekea kupatikana kwa mkataba wa Hudaybiyah.
- (c) Orodhesha vipengele vya mkataba wa Hudaybiyah.
- (d) *“Bilashaka tumekwishakupa kushinda kuliko dhahiri.(48:1)*  
Pambanua matukio manane(8) yanayodhihirisha ushindi uliotokana na mkataba wa Hudaybiyah.
- (e) Tunajifunza nini kutokana na mkataba wa Hudaybiyah ?
12. (a) Toa maelezo mafupi juu ya Hijatul-wadaa (Hija ya kuaga).
- (b) Chambua Hutuba ya Mtume(s.a.w) aliyoitoa siku ya Arafa, 9Dhul-Hija 11A.H kisha bainisha mambo kumi(10) aliyowausia waumini kuyatekeleza.



## *Sura ya Nne*

### **UONGOZI WA DOLA YA KIISLAMU WAKATI WA MAKHALIFA WA MTUME(S.A.W)**

#### **Utangulizi**

Kifo cha Mtume(s.a.w) kiliacha pengo la kiongozi wa Dola ya Kiislamu. Muhammad(s.a.w) ni Mtume wa mwisho na hakuwa na naibu wake kama Haruna(a.s) alivyokuwa naibu wa Musa(a.s). Isitoshe, Mtume(s.a.w)hakuacha usia wowote wa nani awe kiongozi baada yake, sio kwa kauli wala maandishi. Hivyo ilibidi waislamu wazibe pengo la uongozi kwa kufuata utaratibu wa kuchagua viongozi wa Dola kwa kuzingatia mwongozo wa Qur'an na Sunnah. Kiongozi aliyechaguliwa kuchukua nafasi ya Mtume(s.a.w) aliitwa Khalifa wa Mtume yaani kiongozi anayeongoza kwa niaba ya Mtume(s.a.w). Katika Historia ya Uislamu makhalifa waongofu waliongoza Dola ya kiislamu nyayo kwa nyayo kama alivyofanya Mtume(s.a.w) ni wanne wafuatao:

- (1) Abubakar bin Qahafu(r.a) - 11-13AH(632-634)
- (2) Umar bin Khattab (r.a) - 14 - 24A.H(634 - 644 A.D)
- (3) Uthman bin Affan (r.a) - 24 - 36 A.H (644 - 656 A.D)
- (4) Ali bin Abu Twalib(r.a) - 36 - 41 A.H (656 - 661 A.D)

#### **Uchaguzi wa Abubakar Kuwa Khalifa**

Mara tu habari za kutawafu kwa Mtume(s.a.w) zilipoenea maswahaba waliokuwa wajumbe wa shura wakati wa uhai wa Mtume(s.a.w) walisahau wajibu wao wa kudhibiti pengo la uongozi lililojitokeza. Hali hii iliwapa nafasi Answar kukutana kwenye ukumbi wa “**Thaqifah Bani Saidah**” na kuanza kuzungumzia

uongozi. **‘Umar na Abubakar** walipopata taarifa hii nao walienda kujiunga katika ukumbi huo. Wakati huo huo bani Hashim nao walikuwa wanakutana nyumbani kwa Fatma bint Muhammad kuzungumzia ukhalifa. Pale “Thaqifa Bani Saidah” mjadala mrefu ulipita, wapo waliotaka khalifa atoke upande wa Answar, wapo waliotaka khalifa atoke upande wa Muhajirina na wapo waliopendekeza kuwe na khalifa na naibu khalifa. Hatimaye walikubaliana kuwa pawe na khalifa mmoja ndipo Abubakar akampendekeza ‘Umar bin Khattab upande wa Muhajirina na **Saad bin Ubaidah** upande wa Answar. Wote kwa pamoja (‘Umar na Saad) wakasema hawana kifua cha kusimama katika jambo la ukhalifa badala ya Abubakar. Baada ya kauli hii ‘Umar alimpendekeza Abubakar na akampa mkono wa ahadi ya utii (Ba’iyah). Ndipo wote waliokuwepo kwenye ukumbi ule wakampa Abubakar mkono wa ahadi ya utii.

Siku ya pili jambo hili lilipelekwa msikitini kupata ridhaa ya Waislamu wote. Takriban watu thelathini na tatu elfu (33,000) walimkubali Abubakar awe khalifa na kumpa mkono wa ahadi ya utii. Lakini Ali bin Abutalib aliendelea na kikao cha ukoo wa bani Hashim na hakuwepo msikitini wakati Abubakar amepewa Ba’iyah na Waislamu 33,000 waliokuwemo. Ali alichukua miezi kabla ya kumpa khalifa Abubakar ahadi ya utii.

Abubakar alipewa ofisi ya ukhalifa kwa kufuata misingi ya Uislamu ya watu kumchagua kiongozi kwa kuzingatia sifa stahiki. Abubakar alistahiki kuchukua nafasi ya ukhalifa kwa sifa zifuatazo:

**Kwanza**, alikuwa na sifa zote za kiongozi wa Dola ya Kiislamu. Sifa hizi ni: Ucha-Mungu, ujuzi wa Qur-an na Sunnah, siha nzuri na tabia njema. Sifa zote hizi alikuwa nazo Abubaka(r.a)

**Pili**, Abubakar alikuwa karibu na Mtume(s.a.w) pengine kuliko swahaba yoyote. Hili linadhihirika zaidi katika msimamo wake wa kufuata hatua kwa hatua kila ambalo Mtume(s.a.w) amelifanya au

kuliruhusu katika uhai wake alipokuwa akiendesha Dola ya Kiislamu. Usahibu wa Mtume(s.a.w) na Abubakar umetajwa katika Qur-an kuhusiana na tukio la pangoni Thaur, wakati wa kuhajiri Mtume:

إِلَّا تَنْصُرُوهُ فَقَدْ نَصَرَهُ اللَّهُ إِذْ أَخْرَجَهُ الَّذِينَ كَفَرُوا  
ثَانِيًا أَتْنَيْنِ إِذْ هُمَا فِي الْغَارِ إِذْ يَقُولُ لِصَاحِبِهِ لَا تَحْزَنْ إِنَّ اللَّهَ  
مَعَنَا فَأَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَيْهِ وَأَيَّدَهُ بِجُنُودٍ لَمْ تَرَوْهَا  
وَجَعَلَ لِكَلِمَةِ الَّذِينَ كَفَرُوا السُّفْلَىٰ وَكَلِمَةُ اللَّهِ هِيَ الْعُلْيَا وَاللَّهُ

عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٤٠﴾

*Kama hamtamnusuru (Mtume), basi Mwenyezi Mungu alimnusuru walipomtoa wale waliokufuru; alipokuwa (mmoja tu na mwenziwe) wa pili wake, (peke yao); walipokuwa wote wawili katika pango; (Mtume) alipomwambia sahibu yake: “Usihuzunike, kwa yakini Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi.” Mwenyezi Mungu akamteremshia utulivu wake, na akamnusuru kwa majeshi msiyoyaona, na akafanya neno la wale waliokufuru kuwa chini; na neno la Mwenyezi Mungu ndilo la juu. Na Mwenyezi Mungu ndiye anayeshinda na ndiye Mwenye hikima. (9:40)*

**Tatu**, Abubakar ndiye aliyeteuliwa na Mtume(s.a.w) kuongoza swala kwa niaba yake alipokuwa anaumwa karibu na kutawafu kwake. Katika siku hizo ambazo Abubakar aliteuliwa kuwa Imamu kwa niaba ya Mtume(s.a.w) ilitokezea siku moja akachelewa akaswalisha Imamu mwingine (aliswalisha ‘Umar bin Khattab). Mtume(s.a.w) aliposikia sauti isiyo ya Abubakar aliuliza juu ya Imamu (Abubakar) ambaye hakuwepo. Mtume hakupendezwa na akasema: “asiswalishe mtu mwingine ila Abu Qahafu (Abubakar). Baada ya hapo akaitwa Abubakar lakini wakati huo Imamu (‘Umar) alikwisha maliza swala. Mtume(s.a.w) aliamuru swala ile irudiwe nyuma ya Imamu Abubakar(r.a)



**Nne**, Abubakar alikuwa mtu mashuhuri anayekubalika, mtaratibu, mwenye istiqama na Ikhlas, mpevu wa uoni na mwenye uamuzi na alikuwa mfuasi wa Mtume(s.a.w) wa nyayo kwa nyayo.

Sifa zote hizi ukichanganya na umri wake, kwa wale waliokuwa kwenye ukumbi wa **Thaqifa Bani Saidah** hapana aliyemzidi kiumri, utaona kuwa Abubakar alistahiki kuwa Khalifa na hakuwa na upinzani kisifa.

Pia hutuba ya Abubakar aliyoitoa katika kupokea Ukhalifa nayo inaumuhimu wake katika kuonyesha wajibu wa kiongozi wa Dola ya Kiislamu, pale aliposema:

*“Enyi watu mmenichagua niwe mdhamini wenu ingawa mimi sio bora kuliko wengi miongoni mwenu. Nikiwa sahihi nitiini. Nikipotoka nirekebisheni kwani ukweli ni uaminifu na uwongo ni kutoaminika. Aliyedhaiifu atakuwa na nguvu mbele yangu mpaka nishindwe kumpatia haki zake Insha-Allah na mwenye nguvu mbele yangu atakuwa dhaiifu mpaka alipe haki za wengine Insha-Allah. Allah huteremsha Nakama kwa watu walioacha Jihad katika njia yake. Vile vile Allah huteremsha maafu kwa watu ambao hufanya maovu”.*

## **Mawazo Tofauti Kuhusiana na Uchaguzi wa Abubakar**

Zipo tofauti za kimawazo kuhusiana na uchaguzi wa Khalifa wa kwanza, Abubakar(r.a.) mara baada ya kutawafu Mtume (s.a.w.).

Wapo wasemao uchaguzi ule ulifanyika katika mazingira ya kuchanganyikiwa, kwani mkutano haukuwa rasmi. Maelezo ya kundi hili yameegemea kauli zisemazo kuwa Abubakar(r.a.) na Umar(r.a.) walistushwa na taarifa kuwa Ansar walikuwa wamekutana kwenye ukumbi wa mikutano wa **Thaqifa Bani**

*Saidah*, kumchagua kiongozi anayetokana na wao ambaye angeshika uongozi wa dola ya Kiislamu baada ya Mtume(s.a.w.). Kwa mujibu wa kauli hizo, Abubakar(r.a.) na Umar(r.a.) walilazimika kwenda kwenye mkutano huo wakiwa na dhamira ya kuzuia usiendelee, hasa ikizingatiwa kuwa Mtume alikuwa bado hajazikwa na hilo ni suala zito lilohitajia muafaka wa Waislamu wote.

Kundi jingine lina mawazo kuwa, pamoja na kuwa mkutano wa Ansar haukuwa rasmi, lakini kuchaguliwa Abubakar(r.a.) kuliwafiki, kwa kuzingatia dokezo za Mtume(s.a.w), ishara zitokanazo na Qur'an na aliyokuja kuyafanya Abubakar(r.a.) wakati wa uongozi wake, ambayo yalidhihirisha usahihi wa chaguo la mkutano wa Thaqifa Bani Saidah.

Wapo wanaosema kuwa kutokuwepo kwa watu wa nyumba ya Mtume (Ahlul-Bayt) katika mkutano ule, kunabatilisha zoezi zima la uchaguzi wa Khalifa wa kwanza. Maelezo ya kundi hili yanatiwa tashdid na usia, unaodaiwa kuachwa na Mtume(s.a.w.) kwa "Ahlul-Bayt" muda mfupi kabla ya kutawafu kwake; unaosema kwamba haki ya uongozi wa ummah huu baada yake ni ya "Ahlul-Bayt". Kwa hivyo Ali(r.a.) ndiye aliyestahiki nafasi hiyo, na warithi baada yake ni wanawe Hassan na Hussein kwa kuwa ni wajukuu wa Mtume(s.a.w.). Kundi hili linadai Ukhalifa wa Abubakar(r.a.), Umar(r.a.) na Uthman(r.a.) ni **batili** kwa kuwa hao si katika watu wa nyumba ya Mtume(s.a.w.) na walipewa uongozi katika mikutano isiyo rasmi. Aidha hatua ya kuwafanya Makhalisa ni kudhulumu haki ya Ali(r.a.) akiwa ndugu wa Mtume.

Na kuna wasemao kwamba, kwa kuwa Uislamu ni dini ya Mwenyezi Mungu si ya ukoo, kabila au Taifa fulani, na kwa kuwa hakuna aya katika Qur'an inayomwamrisha Mtume(s.a.w.) kurithisha dhima ya uongozi baada yake kwa watu wa nyumbani kwake (Ahlul-Bayt), basi jukumu la uongozi wa ummah limeachwa mikononi mwa waumini wenyewe. Kiongozi atachaguliwa kwa

kuzingatia sifa mbali mbali zikiwemo uoni, ucha Mungu, siha n.k. Sifa zote hizo zimpelekee kuongoza kwa haki na uadilifu. Kwa hiyo Ukhalifa wa Abubakar, Umar na Uthman si suala la kubishaniwa.

### **Tukio la kartasi**

Tukio la ‘kartasi’ lililonakiliwa katika vitabu vya Muslim na Bukhari kuwa siku tatu kabla ya kutawafu Mtume (s.a.w.) alitamka: *“Nipeni peni na wino ili niwaandikie maelekezo yatakayowafanya watu wasipotee”*, halina ukweli. Kutokana na kauli hii inadaiwa kuwa Umar alihutubia watu na kusema *“Mtume yuko katika maumivu makali, Qur’an kama muongozo unatosha kwa watu. Baadhi ya watu wakasema Mtume amepoteza fahamu. Ipo kauli pia isemayo maneno haya yamesemwa na Umar (Khalifa wa pili)!”*

Moja ya Hadithi hizo imo katika kitabu cha Bukhari juzuu ya Hadithi namba 114 katika ukurasa wa 86 tafsiri ya Kiarabu Kingereza isemayo hivi:

*Amesimulia Ubaidullah bin Abdullah kuwa Ibn Abbas amesema:*

*Hali ya Mtume (s.a.w.) ilipokuwa mbaya alisema: “Nileteeni karatasi ya kuandikia, na nitawaandikia tamko litalowapelekea kutopotea”. Lakini Umar akasema; “Mtume anaumwa sana na tuna kitabu cha Mwenyezi Mungu ambacho kinatosheleza. Lakini Maswahaba wa Mtume wakatofautiana juu ya jambo hili. Kutokana na zogo hili Mtume akawaambia; “Ondokeni (na niacheni peke yangu) sio sahihi mbishane mbele yangu. Ibn Abbas akatoka nje na kusema: Imekuwa bahati mbaya na msiba mkubwa kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amezuiwa kuandika tamko kwa Sababu ya kutokubaliana kwao na makelele yao.*

### **Zingatia**

Kutokana na Hadithi hii ni dhahiri kuwa Ibn Abbas ameshuhudia tukio hili na akatoka nje na kusema kauli hii. “Ukweli

sio huu kwa Sababu Ibn Abbas alikuwa anatamka kauli hii alipokuwa anasimulia Hadithi hii, lakini yeye binafsi hakushuhudia tukio hili. Kwa maelezo zaidi juu ya hili rejea Fat-h al-Barr juzuu ya I, ukurasa wa 220).

Pamoja na kuwepo kwa maandishi juu ya tukio hili na wanahistoria kuwa na mifano na tafsiri tofauti, hakuna ushahidi wa kutosha kama tukio hili limetokea kweli au ni maandishi tu yenyewe yaliyopachikwa ili kukidhi haja ya waliyobuni tamko hili. Tukio hili halina ukweli wa kihistoria kwa sababu zifuatazo:

Ni muhali kudhania kuwa Mtume anaweza kuzuiwa na swahaba au na yeyote asiye Allah(s.w.) kutekeleza jambo la Utume wake; inashangaza zaidi kuwataja maswahaba kuwa wanaweza kumpinga Mtume katika Utume wakati huu akiwa katika kitanda cha mauti. Linaloshangaza zaidi ni lengo la tukio hili: Kwa mujibu wa maelezo yaliyopo ni kuwa Mtume(s.a.w.) hakuandika tamko alilokusudia ingawa aliishi siku nne baada ya tukio hili akiwa katika hali isiyo mbaya sana hata Abubakar akarudi kitongojini kwake, kulipokuwa na umbali wa maili mbili hivi kutoka mjini Madina. Kama hali ilikuwa hii kwa nini basi usia huu usiandikwe?

Hivyo Mtume(s.a.w.) kwa makusudi hakuacha uteuzi wowote wa nani ashike uongozi baada ya kutawafu kwake kwa kuwa ameacha mafunzo ya kudumu ya namna ya kupata viongozi, watu wachague wenyewe kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu.

## **Uchaguzi wa ‘Umar bin Khattab kuwa Khalifa wa Pili.**

Mtume(s.a.w.) kumchagua Abubakar kuwa Imam wa msikiti na kutoruhusu mtu mwingine kuswalisha na aliposwalisha mtu mwingine swala ilirudiwa ni dhahiri, kwa maoni yetu, Mtume(s.a.w.) aliashiria kuwa kiongozi awe Abubakar na akawaachia Waislamu waamue kumkubali au kumkataa. Tunaamini kuwa Abubakar alimuelewa hivi Mtume(s.a.w.) ndio maana alipokuwa anakaribia

kutawafu aliwaita wajumbe wa Shura na kushauri kuwa yeye anampendekeza Umar awe ndiye Khalifa baada ya kifo chake. Wajumbe wa Shura walipokubali ndipo akamwambia Ali aandike usia huo. Abubakar alifanya hivi kwa jitihadi yake ambayo inakubalika katika Uislamu na hasa akizingatia hali ilivyokuwa mara Mtume alipofariki, Waislamu walipogawanyika makundi matatu yaani ukoo wa mtume, Muhajirin na Answari.

Hivyo alitumia njia hii ambayo ni ya Kiislamu, hakuiburuza Shura na kulikuwa na mjadala kabla ya kukubalika rai hiyo. Wajumbe maarufu wa Shura walikuwa 'Umar, Uthman, Ali, Talha, Abdul Rahman bin Auf, Muadh bin Jabal, Ubay bin Kaab, Zaid bin Thabit na wajumbe wengine mashuhuri kutoka Muhajirin na Ansar. Abubakar alitoa pendekezo lake la kumteua Umar kuwa Khalifa wa pili, wote walikubali ila walieleza wasi wasi wao juu ya ukali wa Umar, hii ndio hoja pekee iliyotolewa na Ali na Talha. Abubakar aliikataa hoja hii kwa kuwafahamisha kuwa Ukhalifa utamfanya asiwe mkali. Kwa kuwa hoja dhidi ya Umar ilikuwa hii tu basi pendekezo likakubalika.

Hatua iliyofuata ambayo imeimarisha uhuru wa kuchagua viongozi ni kuwahutubia waumini katika msikiti wa Mtume, akisaidiwa na jamaa zake, alisimama kwenye mimbari, kwanza alitaka ule usia usomwe mbele ya watu wote waliokuwa msikitini na yeye azungumze nao.<sup>9</sup> Usia wenyewe ulikuwa kama ifuatavyo:

*Bismillahir Rahmanir Rahiim. Hili ni tamko linalofanywa na Abubakar bin Abi Qahafu ambaye yuko karibu ya kwenda akhera. Wakati wa kuwa katika hali ya kufa hata kafiri humuamini Mwenyezi Mungu, na hata mfanya madhambi hutubia (hurudi kwenye imani yake) na kafiri humtegemea Mwenyezi Mungu. Nimefanya kila jema kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kwa kuboresha dini yake na kwa manufaa ya Waislamu na kwa mimi mwenyewe katika kumteua Umar kuwa Khalifa. Nategemea atakuwa muaminifu na*

*mtekelezaji haki lakini akibadilika na kuwa dhalimu mimi sina lawama kwa kuwa sina elimu ya ghaibu. Kila mmoja anawajibika kwa afanyayo*<sup>24</sup>

Baada ya usia huu kusomwa, Abubakar alipanda kwenye mimbari huku akisaidiwa na kuuhutubia umma kama ifuatavyo:-

*Enyi ndugu zangu, sikumchagua kuwa Khalifa ukoo wangu au ndugu zangu. Nimemteua aliyebora miongoni mwenu mnakubaliana na uteuzi wangu? Wote waliitikia kwa kukubali*<sup>11</sup>

## **Uchaguzi wa Uthman bin Affan Kuwa Khalifa wa Tatu**

Uislamu sio dini iliyofungwa katika mabano bali ina sifa ya kwenda na wakati kwa maana kuwa maamuzi yake ilimradi yamo katika mfumo wa Uislamu yanakubalika. Hali ilivyokuwa wakati alipotawafu Mtume(s.a.w) imetofautiana na ile ya wakati alipotawafu Abubakar. Wakati wa kifo cha Abubakar, Umar alikuwa amejitokeza kuwa ndiye Khalifa bila upinzani lakini wakati wa kifo cha Umar hali ilikuwa tofauti. Walikuwepo watu wengi wenye sifa zinazolingana hivyo alichokifanya Umar ni kuteua jopo la wagombea sita wa ukhalifa ambao walikuwa Uthman, Ali, Saad bin Waqqas, Talha, Zubair na Abdur-Rahman bin Auf.<sup>26</sup> Agizo lingine alilotoa ni kuwa katika muda wa siku tatu baada ya kifo chake wawe wameshaamua wao wenyewe nani miongoni mwao awe Khalifa.

Jopo hili lilikaa kwa muda mrefu bila kufikia uamuzi ndipo Abdur-Rahman bin Auf aliposhauri kuwa kati yao mmoja ajitoe ili aweze kutoa uamuzi. Alipokosa jibu alijitoe mwenyewe na akaanza kazi ya kutafuta maoni ili kukamilisha uteuzi. Talha hakuwepo hivyo wagombea walibaki wanne. Imetokea kuwa Ali alimpendekeza Uthman na Uthman alimpendekeza Ali. Zubair na Saad walimpendekeza Uthman. Baada ya kushauriana na

Maswahaba wengine na kwa kuzingatia muda wa siku tatu Abdur-Rahman bin Auf alitoa uamuzi asubuhi ya siku ya nne na kumtangaza Uthman kuwa ndiye Khalifa. Abdur-Rahman bin Auf (r.a.) alianza kumpa bai'at (mkono wa ahadi ya utii) na kutambua Ukhalifa wake ndipo Waislamu waliokuwa msikitini wakafuatia na kwa namna hii Uthman akawa Khalifa wa tatu. Talha aliporudi Madinah, Uthman alimshauri achague moja kati ya mawili, achukue nafasi ya Ukhalifa au ampe mkono wa ahadi ya utii. Talha alikubali kumpa mkono wa ahadi ya utii.

Utaratibu huu pia umo katika mkondo wa Uislamu na ni aina ya tatu ya utaratibu unaokubalika wa kupata viongozi katika Uislamu.

### **Uchaguzi wa Ali bin Abu Twalib kuwa Khalifa wa nne**

Mkondo wa historia ya Kiislamu juu ya utaratibu wa kuingia kwenye mamlaka umechukua sura mpya, pale alipouliwa Khalifa wa tatu na wapinzani, na kundi hili la wapinzani likamtaka Ali awe ndiye Khalifa wa nne. Kwa hali ilivyokuwa naye akakubali kuchukua nafasi hiyo. Jambo hili lilipelekwa msikitini na wapo waliokubali Ukhalifa wa Ali bila masharti, wapo waliokubali kwa sharti kuwa wahalifu waadhibiwe na wapo waliokataa kumpa mkono wa ahadi ya utii miongoni mwao ni Muhammad bin Muslimah, Usamah bin Zaid, Hassan bin Thabit, Ka'ab bin Malik, Abu Said Khudri, Numan bin Bashir, Zaid bin Thabit, Mughirah bin Shubah na Abdullah bin Salama.<sup>27</sup> Wengine waliokataa ni ndugu na jamaa wa ukoo wa Uthman. Baadhi ya waliokataa Ukhalifa wa Ali walihamia Syria. Kwa ujumla uchaguzi wa Ali(r.a) uliwagawa waislamu kwenye makundi manne yafuatayo:

- (i) Wafuasi wa Uthman (Uthmanis), ambao walitaka dola iwaadhibu wauwaji. Watu wengi wa msimamo huu walikuwa wakazi wa Syria na Basra. Wasiria walimtaka Muawiyah ndiye awe Khalifa na sio Ali. Lakini Wabasra walitaka awe Talha au Zubeir.

- (ii) Marafiki wa Ali (Shian-i-Ali). Watu hawa hawakumuona kuwa Uthman angefaa kuwa Khalifa. Hivyo wakajiita wenyewe Shia-i-Ali (marafiki wa Ali) watu wa mji wa Kufa (Wakufa/Kufans) na Wamisri ndio waliokuwa na msimamo huu. Inaaminika kuwa kundi hili ndilo lililomuua Uthman.
- (iii) Mashibah: Watu hawa walikuwa kwenye Jihad wakati Uthman anauliwa. Hawakuwaunga mkono Uthmanis wala Shias.
- (iv) Ahli-Sunnah wal Jamaah: Kundi hili lilikuwa lenye maswahaba wengi na lilienea Dola yote ya Kiislamu. Hawa wanasema tunawapenda wote Uthman na Ali. Wote ni Maswahaba waongofu. Kama kuna aliyefanya makosa ni kutokana na ijtihada, yake. Tunafuata Sunnah za Mtume na Sunna za Jamaa waongofu yaani kundi la Maswahaba.<sup>28</sup>

Utaratibu huu, ingawa kuna baadhi ya wanachuoni wanaokubali lakini hauhitaji mjadala wowote, ni wazi kuwa hauna nafasi katika Uislamu. Kwa hakika watu wa Madina walikuwa na khofu na kundi hili la wauwaji hivyo kukubali kwao ule Ukhalifa wa Ali kwa mfumo ule yawezekana ni matokeo ya woga tu na siyo hiyari yao. Majibu ya Zubeir na Talha walipoulizwa na mjumbe wa Gavana wa Basra katika msafara wa Bibi Aisha kwa nini wanavunja Ahadi ya utii kwa Khalifa walisema. “Ba’iyah ilifanywa mbele ya ncha ya upanga na ahadi ya kuwaadhibu wauwaji.”<sup>29</sup>

Inawezekana pia hata kule kukubali kwa Ali kuwa Khalifa kunatokana na woga kwa sababu walipomtaka mara ya kwanza awe Khalifa kabla ya hao wauwaji kumuua Khalifa Uthman alikataa.<sup>30</sup> Si hivyo tu lakini alipoona wanamsonga kutaka kumshirikisha katika mzozo wao alihama Madina na kwenda Ahjar sehemu maili chache kutoka Madina.<sup>31</sup> Ingawa pia tukio hili linaonekana kumuweka Ali mahali pabaya.



Utaratibu wa kuingia katika uongozi wa dola ulizidi kuharibika alipouwawa Ali na mwanae mkubwa, Hassan akateuliwa kuwa Khalifa wa tano. Lakini Muawiyah alipopata habari hizi aliivamia Iraq. Hassan nae kwa upande wake alimteua Qays kuongoza majeshi ya kupigana na Muawiyah. Kulitokea uvumi kuwa Qays ameuwawa na hali hii ilipelekea majeshi ya Khalifa kumgeukia mwenyewe. Hassan alielewa hali ilivyokuwa mbaya hivyo alisalimu amri kwa Muawiyah, akaacha Ukhalifa kwa makubaliano kuwa atapofariki amuachie nduguye, Hussein ukhalifa. Baada ya makubaliano haya na Muawiyah, Hassan alirudi Madinah lakini aliuliwa kwa sumu aliyolishwa na mmoja wa wake zake kutokana na ushawishi wa Yazid.<sup>32</sup> Huu ndio ulikuwa mwisho wa Hassan mjukuu wa Mtume.

Taratibu zote hizi ni za kupora madaraka kama alivyofanya Muawiyah ingawa alishinda kivita, kuwekeana makubaliano na watoto wa Ali, Hassan kuwa atamwaachia madaraka Hussein baada ya kufa kwake, na utaratibu wa kurithishwa, taratibu zote hizi, hazikubaliki katika Uislamu ingawa mfumo huu wa mwisho ndiyo uliyotumika katika utawala wa Banu Umayya, Banu Abbasi na Fatimiya.

## **Kuzuka Imani ya Kishia**

Baada ya kuuwawa Ali(r.a), kundi la marafiki wa Ali(Shi'a Ali) lilianzisha imani mpya ya ushia. Walifuata itikaqadi iliyo buniwa na 'Abdallah bin Sabaa kuwa Ali ni Mrithi wa Mtume(s.a.w) kama Haruna(a.s) alivyokuwa mrithi Musa(a.s). Hivyo kundi hili liliitaqidi kuwa Ali(r.a) ndiye aliyekuwa Khalifa halali pekee na kuwaona Abubakar, 'Umar na Uthmani kuwa walikuwa madhalimu waliopora nafasi hiyo. Siku zilivyosonga mbele mashia waliandika vitabu vyao vya sheria, Hadith, Historia ya Uislamu na ufafanuzi wa Qur'an unaolandana na imani yao mpya. Kwa mujibu wa Imani ya kishia, kiongozi wa jamii lazima awelmam ambaye uteuzi wake

unatokana na Mtume (s.a.w). Baada yakutawafu Mtume(s.a.w),kulingana na Imani ya kishia Uimamu ulimshukia Ali(r.a) kupitia kwa mkewe Fatma bint Muhammed(s.a.w). Baada ya kuuliwa Ali(r.a) Uimamu uliwashukia watoto wa kiume wa Fatma hadi akafikia Imam wa kumi na moja anayeitwa Hassan al-Askari ambaye alifariki 874 A.D./260 A.H. katika utawala wa Abasi, ambao Khalifa wake alikuwa Matamid. Alipofariki Imam Hassan al-Askari Uimam ulimshukia mwanae Muhammad anayejulikana kwa jina la Mahdi, Imam wa mwisho. Tarekh ya maimamu wa nyumba ya Mtume (Ahlul-Bayt) inatatanisha. Inaaminika Baba yake Hassan aliamishwa kutoka Madinah na kupelekwa Summara na dikteta Mutawakkil aliyekuwa Khalifa wakati huo, aliwekwa kizuizini huko Summara hadi akafa. Hassan naye aliwekwa kizuizini na aliyechukua nafasi ya Mutawakkil, mtoto wa Hassan aliyekaribia umri wa miaka mitano alianza kumtafuta baba yake katika pango lililokuwa karibu ya nyumba yao. Mtoto huyu hakurudi kutoka pangoni. Tukio hili limewapelekea Mashia kujaa matumaini kuwa mtoto huyu atarudi kuja kuikoa dunia kutokana na mzigo wa madhambi na uonevu.

Mtindo huu haumo katika mfumo wa Uislamu ingawa wafuasi wake wanatumia jina la Uislamu. Kwa nini mtindo huu haumo katika Uislamu tumeshazitaja sababu zake kuwa utume haurithiwi ila hapa tunataka kuongezea kuwa Imani hii ambayo ilipandikizwa baadaye katika historia ya Uislamu ina mizizi ya dini ya Uzoroastrian na Ukristu, dini ambazo zote zinamshirikisha Mwenyezi Mungu.

### **Angalizo(Tanbih)**

Kwa Waislamu hivi leo, mfumo wa usia kama wanavyofanya wafuasi wanaojiita Mashia si katika utaratibu unaokubalika katika Uislamu. Mtume hakulifanya, na hata Ali alipokuwa katika kitanda cha mauti baada ya kujeruhiwa aliulizwa na mtu mmoja kuwa

Waislamu wampe mkono wa ahadi ya utii mwanae mkubwa, Hassan, awe Khalifa? Ali alijibu, “**Nawaachia Waislamu waamue**”. Au mfumo wa ufalme (Royal Family) kama ule wa Saudia Arabia, Moroko, Oman, Qatar au mfumo wa vyama vingi au kimoja kama Pakistan, Misri, Libya, Syria n.k. siyo mifumo ya Kiislamu na nchi zinazofuata mifumo hiyo si za Kiislamu.

Hivyo ni dhahiri wajumbe wa Shura katika dola ya Kiislamu wanalazimika kwa kushirikiana na kiongozi aliyepo madarakani kumteua anayefaa kuwa kiongozi kisha jina liwasilishwe kwa waumini kwa ajili ya kupitishwa au kukataliwa. Hivyo ni kweli kuwa jina linalotolewa na utaratibu unaotumika sasa wa chama kuteua mgombea katika chaguzi za Marais duniani kote ni mawazo yaliyoazimwa kutoka katika mfumo huu wa Kiislamu.

## UENDESHAJI WA DOLA YA KIISLAMU WAKATI WA MAKHALIFA

### Kazi na Wajibu wa Khalifa

Khalifa katika Serikali ya Kiislamu ndiye mtendaji mkuu wa Serikali kama alivyokuwa Mtume(s.a.w). Akiwa mtendaji mkuu wa Serikali, kwa ujumla Khalifa atasimamia utekelezaji wa madhumuni ya kuwepo Dola ya Kiislamu ambayo ni

- (1) Kuhuisha, kuendeleza na kudumisha maadili mema ambayo hupelekea watu katika jamii kuishi kwa furaha na amani.
- (2) Kuzuia na kukomesha maovu ambayo huleta vurugu, mashaka na huzuni katika jamii,

الَّذِينَ إِن مَّكَّنَّاهُمْ فِي الْأَرْضِ أَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ وَأَمَرُوا

بِالْمَعْرُوفِ وَنَهَوْا عَنِ الْمُنْكَرِ ۗ وَاللَّهُ عَنِقَبَةُ الْأُمُورِ ﴿٤١﴾

*Wale ambao tukiwamakinisha, (tukiwaweka uzuri) katika ardhii husimamisha Sala na wakatoa Zaka na wakaamrisha yaliyo mema na wakakataza yaliyo mabaya. Na marejeo ya mambo ni kwa Mwenyezi Mungu. (22:41)*

Katika kutekeleza madhumini haya ya Dola ya Kiislamu, Khalifa aliwajibika kufanya yafuatayo:

- (i) Kujenga maisha ya binaadamu juu ya msingi wa ucha-Mungu na matendo mema. Kuyasafisha maisha ya binaadamu kutokana na maasi, kudumisha haki na usawa, kukomesha ukatili, ukandamizaji, utabaka, uonevu, unyonyaji, udhalimu n.k.

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ  
لِيُقِيمُوا النَّاسَ بِالْقِسْطِ.....<sup>ط</sup>

*“Kwa hakika tuliwapeleka Mitume wetu kwa dalili wazi wazi na kuteremsha vitabu na uadilifu pamoja nao, ili watu wasimamie uadilifu.....” (57:25)*

- (ii) Kutumia uchumi wa Taifa kwa kukuza na kuendeleza maadili mema kwa raia wake.
- (iii) Kuamrisha mema na kukataza mabaya. Hatua nne zilichukuliwa katika kufanikisha jukumu hil:
  - (a) Kuteua mahakimu wacha-Mungu wa kusimamia haki na sheria.
  - (b) Kuteua Madai’yah (Waalimu) wa kuwaelekeza watu yepi mema na namna ya kuyaenda na yepi maovu na namna ya kuyaepuka.
  - (c) Hutuba za Ijumaa, Idd na Hijja zilitumika kukazia wema na ucha-Mungu.
  - (d) Kuteua tume ya kufuatilia tabia za watu na kuadhibu hapo hapo kwa makosa yasiyohitaji kwenda mahakamani.
- (iv) Kulinda mipaka ya dola kwa gharama yoyote. Mipaka ya Dola ililindwa ama kwa vita au kwa diplomasia.
- (v) Pamoja na kulinda na kutekeleza madhumuni ya dola ya

Kiislamu, Khalifa akishirikiana na Shura yake, aliteua viongozi mbali mbali wa Serikali ikiwa ni pamoja na wakuu wa majimbo (Walii au Gavana), Mahakimu, (Makadhi) wakusanya kodi, (maamil) majemedari, makatibu, wakuu wa polisi, n.k.

Kwa mfano Khalifa Abubakar aliteua magavana 17 kuongoza majimbo (mikoa) 17 ya Serikali yake. Naye 'Umar aliteua Magavana 15 katika Serikali yake.

(vi) Khalifa alikuwa ndiye mkuu wa majeshi. Aliamuru vita vipiganwe au visipiganwe, alisaini mikataba, aliteua maamiri jeshi na kupeleka maelekezo katika uwanja wa vita. Abubakar na Ali waliongoza mapigano kama Mtume (s.a.w) alivyofanya, lakini 'Umar na 'Uthuman hawakujaaliwa fursa hii lakini wamekufa mashahidi kwa kuuliwa na wapinzani.

(vii) Khalifa alikuwa ndiye mwanasheria mkuu wa Serikali. Alisikiliza kesi na kutoa hukumu na yeye ndiye aliyekuwa mahakama ya rufaa. Mikoani waliteuliwa makadhi walioendesha kesi na kutoa hukumu kwa niaba yake.

### ***Malipo ya Khalifa***

Abubakar alipochaguliwa kuwa Khalifa aliendelea na kazi yake ya biashara. Alipokuwa anakwenda sokoni kuuza nguo alikutana na Umar na Abu Ubaida ambao walimkataza. Ndipo shura ikakaa na kuamua kuwa apewe kiwango maalum cha posho kutoka katika Baitul-Mali cha kumuwezesha kuishi maisha ya kawaida. Zaidi ya kasma hii hakuruhusiwa kuchukua zaidi. Hata hivyo Khalifa Abubakar alirudisha kwenye Baitul Mali posho yote aliyopewa kutokana na maelekezo yake alipokuwa anafariki Dunia. Katika Ukhalifa wa Umar mishahara ilipangwa kwa wafanyakazi na viongozi wa Serikali. Hivyo Khalifa Umar na Ali walichukua posho zao ila Uthman alitumia pesa zake kwa vile alikuwa na uwezo wa kiuchumi.

## ***Khalifa na Utungaji Sheria***

Khalifa kama ilivyokwishaoneshwa sio mtungaji wa sheria kama ilivyo kwa marais wa leo na mabunge yao. Khalifa ni mtekelezaji wa sheria za Mwenyezi Mungu na msimamizi mkuu wa sheria za Mwenyezi Mungu. Katika kipindi cha Ukhalifa vyanzo vya sheria vilibakia kuwa **Qur'an, Sunnah** na **Ijmaa** na baadaye Umar, Khalifa wa pili, aliongeza **Qiyas**. Kwa hali hii Ufalme katika Dola ya Kiislamu ulibaki kuwa ni wa Mwenyezi Mungu tu.

Siku za mwanzo za ukhalifa kuliundwa tume ya sheria (Ofisi ya Mufti) ilipotokea haja. tume hii iliitwa na kupitisha uamuzi. Tume ya sheria ya Khalifa ilifanya kazi kwa kutegemea vyanzo vya sheria vilivyotajwa katika masuala ya kawaida, maamuzi ya tume yalilikidhi haja. Lakini yalipotokea masuala yasiyo ya kawaida na yenye umuhimu wa kitaifa ilikaa majlis ya Answar, Muhajirin, wawakilishi wa Aus na Khazraj na kupitisha maamuzi; kwa mfano baada ya kutekwa kwa Iraq na Syria wapo maswahaba waliotaka ardhi igawiwe kwa askari waliopigana. Majlis iliyojumuishia Ansar, Muhajirin na watu mashuhuri watano watano kutoka makabila ya Aus na Khazraj ilifanyika kuamua suala hili. Baada ya mjadala mrefu Khalifa Umar alifanikiwa kuwaelewesha wajumbe wa majlis kwa kunukuu aya nyingi kuthibitisha kuwa katika ardhi hata vizazi vijavyo vina hisa kwa hiyo ardhi isigawiwe kwa askari waliopigana lakini waachiwe wenyewe waliotekwa na kodi itakayotokana na ardhi hii wagawiwe askari katika mfumo wa kiinua mgongo cha kila mwaka.

Hivyo ni dhahiri mkono wa Khalifa haukuwa juu ya sheria bali chini ya sheria ya Mwenyezi Mungu, kwa namna hii haikuwezekana kupendelea kundi au mtu yeyote au kuipinda sheria kwa kumpendelea kundi fulani. Hivyo kulikuwa na usawa kamili mbele ya sheria. Hali kadhalika katika masuala ya kodi kulikuwepo usawa na haki za kiraia. Hali hii ilipelekea mshikamano miongoni mwa waumini, uhuru wa maoni, haki katika jamii na kubwa kabisa ni kuwavumilia wafuasi wa dini nyingine.

## ***Khalifa na Mahakama***

Kabla ya kuangalia suala la mahakama katika Uislamu, tuanze na mtazamo wa Uislamu juu ya uhalifu, makosa au hatia. Makosa katika Uislamu yapo katika mafungu matatu:

- (i) Makosa yanayomuhusu Mwenyezi Mungu kama vile uzinzi, ambao adhabu yake ni bakora mia moja, kumsingizia mtu kuzini, ambako adhabu yake viboko themanini, kuritadi adhabu yake ni kifo, kunywa vileo adhabu yake viboko themanini, wizi ambao adhabu yake ni kukatwa mkono na unyang'anyi au ujambazi ambao adhabu yake ni kukatwa mkono na miguu. Makosa haya yanajumuishwa katika istilahi moja kuwa ni **Al-Hudud**. Khalifa hawezi kusamehe makosa haya. Kazi yake ni kutekeleza hadd (adhabu). Kwa wasio Waislamu makosa haya husameheka endapo atasilimu.
- (ii) Makosa dhidi ya mwanadamu yanayohitaji fidia **al-qisas**. Mengi ya makosa haya kama kuuwa, kuumiza, kumtukana mtu n.k yanaweza kumalizwa kwa makubaliano kwa mujibu wa sheria lakini Khalifa hana mamlaka ya kusamehe ila aliyekosewa. Hali kadhalika makosa haya hayahesabiwi kuwa makosa dhidi ya Serikali.
- (iii) Yapo baadhi ya makosa kama, uasi (Rebellion), kula mali ya umma yamehesabika kama makosa dhidi ya Serikali. Kwa kuzingatia haya, kazi za Khalifa kimahakama ni za aina tatu. **Kwanza** kuhakikisha kuna amani katika himaya yake, maendeleo kwa tabaka zote za watu na kuwalinda wanyonge mbele ya wenye kujiweza. **Pili** ni kutekeleza adhabu, kuratibu na kutekeleza haki za wanaodhulumiwa. Na **tatu** ni kuteua mahakimu wa kusimamia haki.

Mahakimu hawa walikuwa watu wazima, waadilifu, waliobobea katika sheria ambao kazi zao ni pamoja na kuhukumu kesi, kusuluhisha magomvi, kurudisha amana za watu, ulipaji wa

zaka, utekelezaji wa usia, utekelezaji wa adhabu, kusimamia mipango ya ndoa, mirathi, talaka, na haki za wanyonge.

Katika kuhakikisha kuwa haki inatendeka kwa wote, tangu wakati wa Ukhalifa wa Abubakar ilianzishwa ofisi ya mufti au taasisi ya mufti au tume ya uchambuzi wa sheria. Ofisi hii ndio pekee iliyoruhusiwa kutoa uchambuzi wa kina wa Fatwa za mamlaka mbali mbali. Hakuruhusiwa mtu mwingine kutoa uchambuzi wa sheria. Walioteuliwa wakati wa Abu bakar kushika wadhifa huu ni Umar, Ali, Uthman, Abul Rahman bin Auf, Ali bin Kaab, Zaid bin Thabit na Abu Huraira - Mufti hawa walisaidia kuwafahamisha watu kuhusu sheria na kuwashauri bila malipo. Serikali ilifanya hivi ili kupunguza makosa kwani kwa kujua sheria watu walijizuia kufanya makosa.

Waraka, Khalifa Umar, aliowatumia mahakimu ni kielelezo cha utaratibu wa mahakama ulivyokuwa wakati wa makhalifa ambao leo hii unafuatwa duniani kote. waraka huo tunaufupisha kama ifuatavyo:

- (i) Utawala wa haki ni amri ya Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume wake, hivyo ni lazima kufuatwa.
- (ii) Mashtaka yanapowasilishwa ipitishwe hukumu kwa uangalifu.
- (iii) Mshitaki na mshitakiwa wote watendewe haki ili maskini asikate tamaa ya kufanyiwa haki na wenye uwezo wasifikirie kupendelewa.
- (iv) Ushahidi ni juu ya mlalamikaji na anayelalamikiwa anaweza kukana anacholalamikiwa kwa kuapa.
- (v) Suluhu inaweza kufikiwa nje ya mahakama lakini mazingira ya suluhu yasichupe mipaka ya maamrishi na makatazo ya Mwenyezi Mungu.
- (vi) Hukumu inaweza kubadilishwa katika jambo lililodhahiri, kwani kubadilishwa hukumu ni bora kuliko kuendelea na uonevu.



- (vii) Ikitokea kesi isiyo angukia kwenye sheria wala hukumu iliyoitangulia, ilinganishwe na kesi zinazofanana kisha deduction itumike kupitisha hukumu inayompendeza Mwenyezi Mungu na ya haki.
- (viii) Mlalamikaji apewe muda wa kutolea ushahidi kesi yake ataposhindwa kesi inaweza kufutwa.
- (ix) Hakimu asijione wala kuonyesha kuchukia inaposemwa kweli.

Watu wote ni sawa mbele ya sheria ndio mafunzo ya Qur'an. Uislamu hauruhusu ule msemu wa “**Mfalme hakosei**”. Hakuna mwanadamu aliyekamilika asiyekosea kabisa. Mtume (s.a.w.) aliweka mfano pale alipowataka watu wenye madai dhidi yake wajitokeze. Maswahaba wake nao walifuata nyayo zake kama mtu angewashitaki kama ilivyotokea kwa Umar au wao pia wangeshitaki kama ilivyotokea kwa Ali.

Khalifa Umar na Ubayy ibn Kaab, walikuwa na tofauti zao. Ubayy ibn Kaab alikwenda kumshtaki Khalifa kwenye mahakama ya Zayd bin Thabit. Hivyo Khalifa aliingia mahakamani kwa kujitetea. Alipokuwa anaingia mahakamani Zayd alisimama. Hapa Khalifa alisema hili ni tendo la kwanza la kuvunja haki. Kwa kufuata nafasi ya Khalifa kuwa alikuwa anajitetea alilazimika kuapa. Hakimu Zayd alimuomba Ubayy aondoe haki yake ya kumtaka Khalifa aape. Khalifa Umar aliingilia kati na kusema “*kama Umar na watu wengine siyo sawa mbele yako, hufai kuwa Hakim.*”<sup>33</sup>

## **Khalifa na Uendeshaji wa Dola kwa ujumla**

Khalifa ndiye mtendaji mkuu wa Serikali. Kwa hiyo jukumu lake la kwanza lilikuwa kuhakikisha kuwa maelekezo na amri za mamlaka kuu ya uendeshaji zinatekelezwa. Katika kuendesha shughuli za kila siku za Serikali alisaidiwa na shura – ambayo mfano wake katika Serikali za leo ni **Baraza la Mawaziri** au

**Cabinet.** Majlisi shura au Tume ya ushauri ilitumiwa na kila Khalifa katika makhalifa wanne wa Mtume(s.a.w). Hakukua na idadi maalumu ya wajumbe wa shura. Wajumbe hawa waliteuliwa na khalifa kwa misingi ya ucha Mungu na mchango wao katika Uislamu na kujitoa muhanga kwao. Miongoni mwao walikuwemo maswahaba maarufu wakiwemo Abubakar, Umar, Uthman, Ali Abdurahman bin Auf, Talha, Zubair, Saad Ibn Waqqas, Abu Ubaidah Ibn Jarrah na Said Ibn Zaid. Viongozi maarufu kutokana Muhajirin na Answar walijumuishwa kwenye shura.

## **Haki za wasiokuwa Waislamu chini ya uongozi wa Khalifa.**

Uislamu una vumilia dini nyingine ingawa ni za kishirikina. Kwa hiyo wasio Waislamu, walitekeleza sheria zao kwa mujibu wa dini zao hasa katika masuala ya urithi, ndoa, talaka, namna ya kupata viongozi wao, uendeshaji wa ibada zao n.k. Kwa kweli walikuwa na uhuru kamili. Vile vile kama wangependa walikuwa na uhuru wa kupeleka kesi zao kwaKadhi(hakimu).Kesi inapopeleka kwa hakimu haikuruhusiwa kuiondoa mahakamani.

Sheria ya makosa ya jinai, sheria ya ushahidi na mikataba iliwahusu Waislamu na wasio Waislamu. Katika kuwaadhibu wahalifu dhidi ya ubinaadamu kama uzinzi, mauaji, wizi, kupora, n.k. sheria ya Kiislamu ilitumika kwa Waislamu na wasio Waislamu.

Kama mzozo ulizuka baina ya Muislamu na asiye Muislamu kesi ya namna hii ilipeleka mahakamani na utaratibu ulikuwa kama ifuatavyo: Katika masuala ya ubinaadamu asiye Muislamu alihukumiwa sawa na Muislamu. Kwa mfano kama asiye Muislamu amemuua Muislamu adhabu atayopewa ni sawa na ile, kama kosa lile lingefanywa na Muislamu.

Tukio la kihistoria lifuatalo linaonesha haki ilivyo katika Uislamu hata kama asiye Muislamu alimkosea Khalifa.

Wakati Khalifa Ali alipokuwa anaondoka kwenda katika vita vya Siffin - alipoteza *zira* yake. Aliporudi toka vitani alimuona Myahudi mmoja na *zira* yake. Khalifa alimuuliza yule Myahudi aliipataje ile *zira* wakati ni yake na hajampa mtu wala hajaiuza. Yule Myahudi alijibu kijeuri: “*Kwa kuwa ninayo mimi basi kiasili ni mali yangu*”. Khalifa pamoja na kuwa ndiye mkuu wa Serikali hakuwa na jinsi isipokuwa kulikepeleka suala hili mahakamani. Kadhi Shurayb alimuuliza Khalifa aliyekuwa pamoja naye sababu ya kuwepo kwake pale mahakamani. Ndipo Khalifa akaeleza: “*zira* aliyonayo huyu Myahudi ni yangu kwa vile sijampa mtu yeyote na sijaiuza”. Yule Myahudi alipotakiwa kujieleza alieleza kuwa kwa kuwa *zira* iko mkononi mwake basi ni mali yake. Hapo ndipo hakimu alipomtaka Khalifa atoe ushahidi, lakini alipotaka kuwaleta mwanae Hassan na mfanyakazi wake Qanbar kama mashahidi hakimu hakukubali ushahidi wao kutokana na uhusiano wao na Khalifa. Kwa hali hii Myahudi alishinda kesi na akaachiwa aende na ile *zira*. Myahudi huyu alishangazwa na hali hii ya Khalifa kusimama mahakamani na raia wake tena wa dini nyingine na hata hivyo akashindwa kesi na akaridhika. Hali hii ilimfanya akiri kuwa ile *zira* ni ya Khalifa akamrudishia na yeye akasilimu”.<sup>34</sup>

## **Kuanzishwa kwa Polisi.**

Kuanzishwa kwa Polisi Wakati wa ukhalifa wa Umar ilikuwa hatua nyingine ya kupunguza makosa na kusimamia haki katika jamii. idara hii iliitwa Ahdath na mkuu wake aliitwa Sahib Al-Ahdath (mkuu wa Polisi) Maafisa kadhaa waliteuliwa katika sehemu kadhaa ili kudhibiti makosa; kwa mfano kudhibiti vipimo na mizani, usalama wa barabara kama kutojenga nyumba barabarani, kuzuia kuwabebesha mizigo mikubwa wanyama, kuzuia uuzaji wa pombe, nakadhalika. Wakati wa Makhalifa wanne polisi hawakuendesha mashitaka mahakamani.

## **Kuanzishwa kwa Magereza**

Sambamba na kuwepo kwa polisi yalianzishwa magereza (jela) wakati wa Khalifa wa pili. Mwanzoni makosa ya jinai tu ndiyo yaliyowapeleka watu jela. Lakini siku zilivyosogea hata makosa

kama kurudiarudia pombe yaliwapelekea walevi kufungwa badala ya kuchapwa bakora.

Masuala mengi kuhusiana na Dola kama vile kupanga mishahara ya wanajeshi, kuanzisha idara mbali mbali, kuwapa vibali wageni kufanya biashara katika Dola ya Kiislamu na kiwango cha kodi wanachotakiwa kulipa, n.k. yaliamuliwa na Khalifa baada ya kushauriwa na kamati yake ya utendaji. Kamati hii ilikuwa ikikutana kila siku katika msikiti wa Mtume (s.a.w). Taarifa za wilayani na mikoani zilizowasilishwa kwa Khalifa zilijadiliwa na kupitishiwa maamuzi.

Baadhi ya wanakamati wa kamati hii ya utendaji walipewa nyadhifa mbali mbali; kwa mfano – Abubakar alimteua ‘Umar kuwa Jaji Mkuu na msimamizi wa kugawa zaka. Ali aliteuliwa kuwa mkuu wa mawasiliano; kusimamia wafungwa wa kivita, fidia yao na n.k.

Mbali ya shura teule, makhalifa wote walitumia shura ya watu wote msikitini kama chombo cha kusaidia uendeshaji. Uteuzi wa majaji, wakuu wa mikoa, n.k. ulifanywa hadharani (msikitini) ili kama kuna upinzani wowote juu ya mteuliwa, raia walikuwa huru kupinga kwa hoja wazijuazo. Si hivyo tu hata kama kiongozi ameteuliwa bado raia walikuwa na fursa ya kuwasilisha malalamiko dhidi ya kiongozi muhusika.

Ili kujua ukweli na malalamiko ya watu na kufanya uchunguzi, Tume ya kufuatilia malalamiko ya raia dhidi ya viongozi wao iliundwa. Malalamiko yalipomfikia Khalifa, alitwa kiongozi muhusika kwa kuhojiwa au tume ilimuendea.

Chombo kingine cha utawala kilikuwa mkutano wa watendaji wote wa Serikali waliokuwa wanakutana baada ya Hija. Wakati huu Khalifa alikuwa anamsikiliza kila mwenye malalamiko dhidi ya Serikali. Kwa namna hii kila mwananchi alihusika na uendeshaji.

Si hivyo tu bali Khalifa Uthman alianza utaratibu wa kusikiliza malalamiko ya wananchi kila Ijumaa.

Jambo lingine muhimu katika uendeshaji ni kuwa Serikali ilitoa mishahara iliyokidhi mahitaji ya watendaji ili kuzuia rushwa na mambo yanayolingana.

Kama ilivyokuwa wakati wa Mtume(s.a.w) kuitawala Dola iligawanywa kwenye majimbo na wilaya. Idadi ya majimbo na wilaya ilitegemea kupanuka kwa mipaka ya Dola. Kila jimbo au wilaya ilikuwa na viongozi watatu. Gavana au Walii, mkusanyaji mapato ya Serikali (Amil) na mwanasheria (Kadhi). Gavana alifanya kazi zote za Khalifa mkoani kwake. Aliendesha swala za kila siku ya Ijumaa, Idi zote mbili, na kuongoza msafara wa Hija wa watu wa mkoa wake. Alisimamia amani na utulivu mkoani kwake, pale ambapo kamanda wa kijeshi wa mkoa hakuwepo mkuu wa mkoa ndiye aliyejaza nafasi hiyo na kuwa kamanda wa majeshi ya mkoa na mara nyingine kuongoza mapigano dhidi ya maadui.

Pamoja na Gavana viongozi wengine waliokuwa mkoani ni Sheikh Ul-Kharaj au msimamizi wa mapato ya Serikali. Sahib Ahdath (mkuu wa polisi), Kadhi na Kamanda wa majeshi. Wakati wa ukhalifa wa Umar kiongozi alipoteuliwa aliorodhesha mali zake na itapoonekana anaongezeko lisiloleweka aliulizwa na mali yake kutaifishwa.

## **Pato la Serikali**

Moja ya shughuli muhimu katika uendeshaji wa Serikali ni namna Serikali ilivyopata mapato yake na ilivyotumia. Wakati wa Mtume(s.a.w) vyanzo vya pato la Serikali vilikuwa zaka, jizya, kharaj, khums na fay. Katika kipindi cha makhalifa wanne vyanzo vya pato la Serikali viliongezeka kama ifuatavyo;

**Ushr;** Ushr ni kodi ya mazao kutoka katika ardhi ya Waislamu iliyotekwa kivita na kugawiwa askari waliopigana au ardhi ya Serikali iliyoandaliwa kwa kilimo au mifugo. Kwa ardhi inayotegemea mvua ya asili, mabwawa na mito ya asili kima chake ni  $\frac{1}{10}$  (10%) ya mazao na kwa mashamba yanayomwagiliwa kiwango cha ushuru ni  $\frac{1}{20}$  (5%) ya pato la mwaka.

**Kharaj au kodi ya Ardhi:** Kodi hii iliwahusu wasio waislamu ambao ardhi yao ilitakwa kivita lakini wenyewe wameruhusiwa kuedelea kutumia ile ardhi iliyotekwa ambayo ni mali ya dola ya Kiislamu. Kodi hii iliwekewa kima maalum baada ya tathmini ya ardhi na ililipwa kwa mwaka.

**Jizya;** ilikuwa chanzo kingine cha pato la Taifa. Kodi hii iliwahusu wasio waislamu tu, waliojulikana kwa jina la “**Dhimmi**”. Serikali ya Kiislamu inachukua dhamana ya kuwalinda wasio Waislamu, wao na mali zao. Wasio Waislamu wanalipa kodi hii ya jizya ikiwa ni malipo ya kazi ya ulinzi wanayofanyiwa na Serikali. Kodi hii pia iliwekewa kiwango maalum na haikuwahusu vikongwe, watoto, walemavu na wanawake.

**Zaka na Sadaqa** nazo zilibakia kuwa vyanzo vya msingi vya pato la Serikali.

**Ngawira** ni mali inayopatikana kwa kumshinda adui. Hii nayo ilitumika kama chanzo cha pato la Serikali. Wapiganaji walichukua asilimia 80 au ( $\frac{4}{5}$ ) na pato la serikkali lilikuwa asilimi 20 au ( $\frac{1}{5}$ ) ya ngawira.

**Fay** kilikuwa ni chanzo kingine cha pato la Serikali katika kipindi cha Makhalfa. Fay ni mali iliyotolewa na adui hata bila ya kupigana.

**Zaraib** ni kodi za muda zilizotozwa na serikali kwa maslahi ya nchi Mapato mengine ya Serikali yalitokana na **wakfu, kodi za madini, kodi ya mali inayoingia nchini** au **inayopitishwa**, n.k.

Kwa vyanzo hivi Serikali iliweza kukusanya mapato yaliyoweza kuendesha Serikali bila matatizo. Palikuwa na Baitil-Mali(Hazina). Mali ya Serikali ilitumika kwa mujibu ya maelekezo ya mafungu yake, maendeleo ya nchi na wananchi kwa ujumla.

Maendeleo ya nchi yaliyopatikana wakati wa Makhalifa ni pamoja na ujenzi wa mifereji(Canals). Katika Ukhalifa wa 'Umar(r.a)ulijengwa mfareji kutoka mto Euphrates hadi Basra kuliko kuwa na ukame wa maji. Mfereji huu uliitwa kwa jina la Gavana wa Basra, "**Canal Abi Musa**". Mifereji mingine iliyojengwa kutoka Mto Euphrates ni "Canal Maakal na Canal Saad" iliyopeleka maji sehemu mbali mbali zilizokuwa kame.

Mfereji mwingine maarufu ni ule uliunganisha mto Nile na Red See (Bahari ya Shem) ambao uliitwa kwa jina la "Canal Amirul-Muuminina".

Maendeleo mengine yaliyofanywa kutokana na pato la Serikali katika kipindi cha Makhalifa ni ujenzi wa barabara na madaraja, majengo ya ofisi, nyumba za wafanyakazi, ngome na kambi za jeshi, nyumba za wageni, majengo madhubuti ya Baitul-Mali na magereza. Visima na vituo kadhaa baina ya Makkah na Madina vilijengwa. Miji nayo ilianzishwa na maarufu katika hiyo ni Basra, Kufa, Fustat na Mosul.

Kazi ya ujenzi wa misikiti na upanuzi wa misikiti ya Makkah na Madinah ilishamiri katika kipindi cha Makhalifa. Misikiti elfu nne (4,000) inakadiriwa kujengwa katika Ukhalifa wa 'Umar(r.a). Misikiti ya Makkah na Madina ilipanuliwa kwa kununua nyumba za majirani katika kipindi cha 'Umar na 'Uthman(r.a).

## Ulinzi na Usalama

Wakati wa Ukhalifa wa Makhalifa wanne ulinzi uliimarishwa kwa kiwango kikubwa. Wakati wa Mtume(s.a.w) hakukua na jeshi maalum. Kila mtu alikuwa askari na vita ilipofika Waislamu walijitokeza wakapewa mafunzo na kwenda vitani. Ni kweli pia kuwa katika Dola ya Kiislamu kila Muumin ni askari wa Allah(s.w) na wakati wowote anapotakiwa ni lazima awe tayari kupigania dini ya Mwenyezi Mungu.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ آمَنُوا هَلْ أَدُلُّكُمْ عَلَىٰ تَجْرَةٍ تُنْجِيكُمْ

مِّنْ عَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿١٠﴾

*“Enyi mlioamini Je! Nikujulisheni biashara itayokuo keni na adhabu iumizayo(61:10).*

تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ۖ وَتُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنفُسِكُمْ.....

*Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake na piganieni dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zenu na nafsi zenu.....” (61:11)*

﴿إِنَّ اللَّهَ اشْتَرَىٰ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَنفُسَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ بِأَنَّ لَهُمُ الْجَنَّةَ

يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيَقْتُلُونَ وَيُقْتَلُونَ.....﴾

*Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waislamu nafsi zao na mali zao ili nae awape Pepo. Wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu wanauwa na wanauwawa.....” (9:111)*

Ni dhahiri Waislamu ni askari wa Mwenyezi Mungu. Pamoja na hivi tangu wakati wa Khalifa wa pili Umar, liliundwa jeshi kama yalivyo majeshi ya kileo. Khalifa ndie aliyekuwa mkuu wa majeshi, aliteua kamanda wa jeshi na makamanda wa mikoa na wilaya.

Idara ya ulinzi ilianzishwa na askari wote waliorodheshwa na utaratibu wa mshahara na posho ulianza kutumika kwa askari wa kudumu, wakujitolea na wale waliopigana vita vya awali kama Badr, Uhud, n.k.



Nchi iligawanywa kwenye maeneo ya kiulinzi, makao makuu ya maeneo haya yakawa Madina, Kufa, Basra, Mosul, Fustat, Damaskas, Hems, Jordan na Palestine. Katika sehemu zote hizi kambi zilijengwa kwa ajili ya askari. Mashamba ya mifugo yalipanuliwa kwa matumizi ya farasi na ngamia wa vita.

Pamoja na askari wa farasi na wa miguu jeshi la maji lilianza katika Ukhalifa wa Uthman. Vita vya kwanza vya majini vilipiganwa na Muawiya alipovamia Cyprus mnamo mwaka wa 28 A.H. Makao makuu ya Jeshi la maji yalikuwa Alexandria Misri.

## **Usalama wa Taifa**

Idara ya usalama ilikuzwa. Ilianza tangu wakati wa Mtume(s.a.w) na kuendelezwa wakati wa Makhalfifa wanne. Walitumika wanajeshi na wasio wanajeshi katika kazi ya kupata habari ndani na nje ya Dola na hasa kujua mwenendo wa adui. Wapo Machief, kwa mfano Syria, waliochaguliwa kuwa wanausalama, kuchunguza mwenendo wa Warumi. Palestine lilikuwepo kundi la Wayahudi lililojulikana kwa jina la Samara lilijizatiti katika upelelezi. Khalifa Umar(r.a) aliweka wapelelezi ndani ya jeshi (military intelligence) ili apate habari zote. Hivyo idara hii nayo ilisaidia sana katika ulinzi na usalama wa Dola ya Kiislamu.

Hivi ndivyo Serikali ya Kiislamu ilivyoendeshwa kwa muda wa miaka 40 kuanzia kwa Mtume(s.a.w) hadi Makhalfifa wake wanne na imekuwa ndio msingi wa uendeshaji wa Serikali zote za leo Duniani.

## **Upinzani Dhidi ya Dola ya Kiislamu Wakati wa Makhalfifa**

Katika kipindi cha Makhalfifa wanne wa Mtume (s.a.w), maadui wa Dola ya Kiislamu ni wale wale waliokabiliana na Mtume na

kuainishwa katika Qur-an japo walitofautiana kimbinu kulingana na mazingira. Maadui wakubwa walioainishwa katika Qur-an ni:

- (i) Adui mkubwa – Sheitwaan (katika Majini na Watu) anayepambana kwa kuishawishi na kuipambia nafsi ya mtu ili imuasi Mola wake.
- (ii) Makafiri na Washirikina – Wanaotaka mifumo yao ya maisha iwe juu ya Uislamu.
- (iii) Wanafiki – wanaotaka kuishi maisha ya mseto baina ya Uislamu na ukafiri kwa ajili ya maslahi ya dunia.
- (iv) Mayahudi - husuda na chuki yao dhidi ya Uislamu ilibainika tangu wakati wa Mtume(s.a.w) - kwa ajili ya kuipenda dunia kuliko akhera.
- (v) Wakristo wanachuki na husuda dhidi ya Uislamu kama Mayahudi.

## **Uasi wa Dola (Riddah)**

Habari za kutawafu kwa Mtume(s.a.w) zilipelekea makabila mengi ya Kiarabu yaliyokuwa chini ya himaya ya Dola ya Kiislamu kuasi. Tukio hili katika vitabu vya tarekh huitwa **Riddah** kwa Kiarabu na **apostasy** kwa Kiingereza.

Kwa ujumla dola ya Kiislamu wakati wa ukhalifa iligawanyika katika makundi sita ya watu. kuna waliobakia na Uislamu wao bila kutetereka hasa watu wa Madina, Taif na Makka. Wanafiki ni kundi lililokuwepo na hila zao za mwisho ziligonga ukuta mwaka mmoja tu kabla ya kutawafu kwa Mtume(s.a.w). Hivyo walikuwa macho kuvizia fursa yoyote iliyopatikana waitumie. Kulizuka kundi la Waislamu waliobakia Waislamu lakini walikataa kupeleka Zaka Madina kwa hoja kuwa itumike kuwasaidia wasiojiweza katika eneo lao.

Wapo waliobaki Waislamu lakini walikataa kulipa Zaka kabisa. Kundi lingine ni lile lililoritadi na kurudia dini zao za asili. Kundi lingine ni wale mitume wa uwongo alioanza tangu wakati wa Mtume na sasa wakaongezeka kufikia wanne. Ikumbukwe pia wakati wa majilio ya wajumbe mbali mbali kwa Mtume(s.a.w) yapo makabila ambayo hayakusilimu ila yaliitambua Dola ya Kiislamu wakawa wanalipa Jizya. Mfano ni kabila la Hanifa la sehemu ya Arabia ya kati. Wayahudi nao ambao siku zote walikuwa maadui wa Mtume(s.a.w) si kuwa tu wametolewa Madina lakini hata huko Khaibar walikohamia walishindwa na kulazimishwa kuutambua utawala wa Kiislamu na kulipa Jizya.

Sio Wayahudi tu bali Wakristu wa Najran na Urumi waliazimia kuiangamiza dola ya Kiislamu kwa vile wote walikuwa wanalipa Jizya. Hivyo ni dhahiri uasi katika dola ya Kiislamu ulikuwa mkubwa. Dola yote ya Kiislamu ilisambaratika, maadui walikuwa wengi na waliobakia na utii kwa Dola ni miji baina ya Madina, Makka na Taif. Kabla ya kutazama hatua alizochukua Abubakr Siddiqi ni vyema kwanza tuchambue sababu zilizopelekea uasi huu.

### **Sababu zilizopelekea Uasi**

Kwa wale waliosilimu kisha baada ya kutawafu Mtume walikataa kulipa Zaka na wale waliokubali kulipa Zaka lakini wakajenga hoja kuwa hawatapeleka Madina lakini itumike kwa watu wao; makundi yote haya Sababu yao kubwa ya kufanya hivi ni udhaifu wa Imani kama isemavyo Qur'an:

﴿ قَالَتِ الْأَعْرَابُ ءَأَمَّا قُلٌّ لِّمَ تُوْمِنُوْا وَلَكِنْ قُوْلُوْا أَسْلَمْنَا وَلَمَّا يَدْخُلِ

الْإِيْمَانُ فِيْ قُلُوْبِكُمْ .....

*Walisema wanaokaa jangwani (kumwambia Mtume) “Tumeamini” Sema uwaambie Hamjaamini, Lakini semeni Tumesilimu maana imani haijaingia nyoyoni mwenu bado..... (49:14).*

Ama kwa wale waliorudia dini zao za awali walikuwa na sababu mbili, moja ya kiuchumi ya kulinda biashara zao na mali zao kwa kuondokana na kulipa Jizya na pili kulinda hadhi zao na nafasi zao katika koo na mila . Sababu hizi pia ndizo zilizopelekea uasi kwa wale waliokuwa hawakusilimu lakini walikuwa wanalipa Jizya. Na kwa wale waliodai utume na walioungana nao pamoja na sababu zilizotajwa walikuwa na husda na uroho wa mamlaka. Bado ipo hoja inayowahusu Waarabu wote, wengi wao walizoea maisha yasio na mpangilio maalum, yasiyo na nidhamu na hawakuzoea kutoa utii wao nje ya koo zao au makabila yao. Mabadiliko yaliyoletwa na Mtume(s.a.w) yaliwaweka katika mfumo wa maisha wenye nidhamu wasioitaka. Waliukubali wakati wa Mtume(s.a.w) kwa kuwa walikuwa hawana jinsi. Kutawafu kwa Mtume(s.a.w) kulitoa nafasi siyo tu ya kujitenga na utawala wa Madina bali walikusudia kuuhilikisha kabisa. Kwa upande wa Wayahudi na Wakristu ni kweli waliasi kulinda tawala zao na utukufu wao lakini kulinda dini (itikadi) zao pia kulitoa msukumo mkubwa. Sababu hizi na nyinginezo ambazo huenda hatukuzitaja zaweza kuwa ndio chimbuko la “**Riddah**”.

## **Kukomeshwa kwa Riddah na Chokochoko Nyingine**

Miongoni mwa makabila yaliyovamia Madina ni Bani Abbas na Zukian. Makabila haya yalipokuwa yanakimbilia Rabaza baada ya kushindwa kuivamia Madina waliwaua kikatili watu wa makabila yao ambao hawakuasi. Khalifa Abubakar aliongoza msafara wa kuwafukuza. Adui alishindwa, wengi waliuliwa na baadhi yao kuchukuliwa mateka. Khalifa Abubakar, kwa ujumla aliendesha vita dhidi ya makundi yote ya waasi na muda mfupi akaurudisha utulivu wa Dola ya kiislamu kama alivyoiacha Mtume(s.a.w). Si tu kuirudisha Dola katika hali ya utulivu, basi huifanya Dola kuimarika zaidi kijeshi na kiusalama.

Mitume wa uongo nao ambao idadi yao ilikuwa wanne walinyamazishwa. Mitume bandia hawa ni Aswad Ausi, Tulaiha,

Sajah bint Alharith na Musailamah Al-kadh-dhab(mzandiki). **Aswad** alitangaza utume wake Yemen baada ya kukusanya jeshi kubwa. Mtume huyu wa uwongo aliyekuwa anajitanda uso wote hata akaitwa mtume anayejitanda aliuliwa na Qais ibn Makshuh aliyekuwa chifu wa Waarabu akishirikiana na Feroze Dailme na Darweih.

**Tulaiha** anatoka katika kabila la Bani Asad kaskazini mwa Arabia. Mara baada ya kifo cha Mtume, alijitangazia utume. Khalifa Abubakar alimtuma Khalid bin Walid kuzima uasi huu. Khalid alikuwa jemadari mwenye kipaji cha kupigana na amerikodiwa kuwa miongoni mwa majemadari wa dunia. Mtume(s.a.w.) kwa uhodari wake alimwita “**Upanga wa Mwenyezi Mungu**”. Khalid alishinda makabila yote yaliyokuwa yanamuunga mkono Tulaiha, wakiwemo Bani Tay, Bani Ghatfan na Bani Asad. Katika vita vilivyopiganiwa mahali paitwapo Bozakha, Jeshi la adui liliongozwa na Uyeina. Tulaiha alikimbilia Syria na mkewe, Uyeina alikamatwa mateka na kupelekwa Madina pamoja na watemi wengine wawili ambako baada ya kuomba msamaha walisamehewa.

**Sajah bint Al-Harith** anatoka katika kabila la Bani Tamim. Baada ya kifo cha Mtume(s.a.w.) watemi wengi wa kabila hili waliritadi ndipo Sajah akajitangazia utume. Sajah alikusanya watu elfu nne tayari kuelekea Madinah. Alipokuwa anakwenda Madina akapata habari za jeshi la Khalid bin Walid lililomuungamiza Tulaiha. Aliingiwa na khofu kwenda Madinah. Kwa udhuru huu akamuandikia **Musailamah Mzandiki** washirikiane ambaye naye alikwisha tangaza utume wake. Sajah aliungana na Musailamah mzandiki na kutambua utume wake. Wakati huo huo, Khalid bin Walid alifika makao makuu ya kabila la Bani Tamim na kutuliza uasi. Baada ya kutuliza fujo za kabila la Bani Tamim Khalid alimgeukia Musailimah Al-kadh-dhab.

Katika siku za mwisho za Utume katika mwaka wa kumi Hijriya(10 A.H.) Musailimah aliyeishi katika kitongoji cha Yamen (kakatikati ya Bara Arab) katika kabila la Bani Hanifa alijitangazia utume na akamuandikia Mtume (s.a.w.) juu ya utume wake na kumtaka wagawane Dunia nusu kwa nusu katika kuiendesha. Mtume (s.a.w.) alimjibu:

*“Kutoka kwa Muhammad, Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenda kwa Musailimah alkadhab (mzandiki). Dunia iko chini ya ufalme wa Mwenyezi Mungu na humuachia kuitawala amtakaye. Na mwisho mwema ni wa wakweli.”<sup>35</sup>*

Musailimah alikuwa na wafuasi wengi. Hivyo alikusanya jeshi la watu arobaini elfu lililopigana na jeshi la Waislamu la watu elfu kumi na tatu liliongozwa na Khalid bin Walid. Ikrima na Shurahbil walitangulia lakini walishindwa. Kuwasili kwa Khalid kuliwapelekea kukusanya nguvu na kufikia askari kumi na tatu elfu dhidi ya adui aliyekuwa na jeshi la watu arubaini elfu. Pambano hili ambalo matokeo yake yalikuwa **“Bustani ya Vifo”**, lilikuwa kali sana na lenye matokeo ya kuelemeza kwa adui. Waislamu waliwaangamiza Bani Hanifa na wasaidizi wao, wakawauwa adui 21,000<sup>46</sup> (ishirini na moja elfu) pamoja na Musailimah aliyeuiliwa na Wahshiy aliyemuua Hamza katika vita vya Uhud. Waislamu waliouawa ni mia nane (800) wakiwemo maswahaba 360 (mia tatu sitini) wengi wao wakiwa mahifadhi wa Qur’an. Vita hivi vilipiganwa mnamo mwaka 633 A.D. au 11 A.H. vilichukua miezi Saba. Vita vya Yamama vilimalizia uasi wa Riddah na Dola ikarudia utulivu.

Chokochocho nyingine dhidi ya uongozi wa Abubakar zilitoka kwa Waajemi (Persians) waliokuwa washirikina na Warumi au Dola ya Wakristo wa Kirumi. Abubakar, aliwahamasisha Waislamu kuingia katika Jihad ili kuihami Dola ya Allah(s.w). Moja ya barua aliyoundika katika kuhamasisha Waislamu ni hii:

*Kutoka kwa Khalifa wa Mtume(s.a.w) kwenda kwa Waislamu wote wanaume na wanawake wa Yemen. Nawasalimia wote wanaosomewa barua hii. Namshukuru Mwenyezi Mungu anayepaswa kuabudiwa. Mwenyezi Mungu ameifaradhisha Jihad na kuwaamuru (waumini) waitekeleze wakiwa katika halinzuri au hali ngumu, wanatakiwa wajitokeze kwenda katika Jihad kwa mali zao na nafsi zao. Jihad ni wajibu na malipo yake ni makubwa. Nawasihi Waislamu mjitokeze kwenda kwenye Jihad dhidi ya Warumi wa Syria. Enyi waja wa Mwenyezi Mungu, shirikini katika Jihad kwa ikhlaswi. Hamtakosa moja ya zawadi hizi, ama kufa Shahid au ushindi na ngawira .....<sup>36</sup>*

Waislamu walihamasika na kujitokeza kwa wingi na kuwashinda maadui zao ushindi wa kishindo katika Ukhalifa wa Abubakar, 'Umar na Ukhalifa wa 'Uthman pale Waislamu walipokuwa hawajaanza kugombana wenyewe kwa wenyewe.

## **KUPOROMOKA KWA DOLA YA KIISLAMU ALIYOICHA MTUME(S.A.W)**

Dola ya Kiislamu ilianza kuporomoka katikati ya Uongozi wa Khalifa 'Uthman palipotokea fitna iliyowapelekea Waislamu kugombana wenyewe kwa wenyewe kiasi cha kuwafikisha mama wa waumini, Aysha (r.a) mkewe Mtume(s.a.w)na Ali bin Abu Taalib kupambana kijeshi. Fitina hii ilipelekea kuuliwa kwa Uthman na Ali na kusambaratika kwa Dola ya Kiislamu na kuanza uongozi wa Kifalme. Mzizi wa Fitna hii ni Myahudi '**Abdallah bin Sabaa**' wa Yemen aliyesilimu kinafiki. Ili kupata mafunzo ya kina Waislamu hatuna budi kuipitia kwa makini historia hii ya kusikitisha, iliyopelekea kusambaratika kwa dola ya Kiislamu, katika kipindi cha Khalifa 'Uthman na Ali.

## **Upinzani Kutoka Miongoni mwa Waislamu**

Ukhalifa wa Uthman ulichukua miaka 12. Katika miaka sita ya kwanza Dola ya Kiislamu iliimarika na mipaka yake kupanuka . Katika miaka sita aliyomalizia ukhalifa wake kulikuwa hakuna utulivu: Miongoni mwa Waislamu walizusha malalamiko ya uongo dhidi ya Khalifa na Serikali yake. Kiongozi wa kundi hili la wapinzani ni **Abdullah Ibn Sanda** alijulikana sana kwa jina la **Ibn Sanda** au **Ibn Sabaa**. Ibn Sanda alikuwa Myahudi anayetoka Yemen, alisilimu kinafiq kama alivyosilimu Abdallah bin Ubay wa Madinah, lakini ibn Sabaa tangu aliposilimu alikuwa tayari na mpango wake wa kuudhuru Uislamu hatua kwa hatua. Kundi la wanafiqi lililoongozwa na Ibn Sabaa lilitumia shutuma dhidi ya Khalifa na Serikali yake kuficha unafiki wao kwa sababu madai yao yalikuwa ni ya uongo na pale walipopewa maelezo ya kweli waliyafumbia macho na hawakuyakubali.

## **Madai Dhidi ya Khalifa ‘Uthman**

Upinzani mkubwa ulitokea Misri ambapo Abdallah bin Sa’ad aliteuliwa badala ya Amri bin al As. Abdallah hapana shaka ni ndugu wa Uthman lakini mchango wake katika Uislamu ulikuwa mkubwa sana. Ndiye aliyeanzisha jeshi la majini la Dola ya Kiislamu na ushindi wake Afrika ya kaskazini. Ushindi huu ulionesha kuwa Abdallah bin Sa’ad alikuwa na uwezo wa kuongoza hivyo Khalifa alikuwa sahihi kumpa ugavana na hapana upendeleo hapa. Hata hivyo wanafiki hawa alipovamia Madinah na kudai kuwa hawamtaki Gavana Sa’ad; Khalifa alimbadilisha na kumuweka mtu wanayemtaka, Muhammad bin Abubakar.

Kutokana na maelezo haya ni dhahiri kuwa Khalifa Uthman hakuwa na upendeleo kwa ndugu zake kwa kuwapa nafasi za ugavana. Kama angekuwa nao ni dhahiri asinge waachisha kazi na pale walipokosea kuwachapa. Isitoshe magavana hawa waliteuliwa mwanzoni mwa ukhalifa wake wakati akipendwa kama



Khalifa Umar. Ni kweli Uthman aliwawua madaraka baadhi ya magavana kama alivyofanya Umar kwa manufaa ya uislamu.

Dai lingine lililopikwa na wanafiki wa kundi la Sabaa ni matumizi mabaya ya pesa za Serikali (Baitul-mal). Khalifa alisingiziwa kuwa anatumia vibaya pesa za Serikali na kuwapa ndugu zake. Dai hili halikuwa la kweli kabisa kwa Sababu zifuatazo:

Uthman alikuwa tajiri mkubwa Arabia hata akaitwa **“Ghanir”** (mtu tajiri). Lakini hakuwa tajiri tu lakini anajulikana kwa mchango wake katika njia ya Uislamu wakati wa Mtume(s.a.w.) na baada ya Mtume(s.a.w.) wema wake uliendelea. Katika Ukhalifa wake alitumia mali yake mwenyewe kusaidia maskini na ndugu zake. Katika ukhalifa wake kwa muda wote wa miaka 12 hakuchukua posho kwa ajili ya ukhalifa wake kutoka kwenye Baitul-Mal. Kulikuwa na zogo kubwa wakati Khalifa alipotamka kumpa zawadi Abi Sarh  $\frac{1}{5}$  ya ngawira ya Afrika ya kaskazini kwa kazi nzito aliyoifanya ya kuteka Afrika kaskazini kama motisha. Jambo hili lilipolalamikiwa na watu, Khalifa alimtaka Sarh arudishe ile ngawira na akafanya hivyo. Vile vile ikasemwa kuwa amemruhusu mpwae Marwan anunue kasma ya Serikali ya mateka. Jambo hili na mengine kuhusu tuhuma hii kama kweli au sikweli tusome hotuba ya Khalifa mwenyewe.

*Watu wa Madina wanasema, nina pembe laini kwa ajili ya ndugu zangu na ninawafanyia wema (ninawapendelea ndugu zangu). Lakini kuwapenda kwangu hakuathiri haki ya mtu yeyote. Ninawapa wanachostahili kutokana na mali yangu. Sijafikiria kujihalalishia mali ya Serikali kwa ajili yangu au mtu mwingine yeyote. Wakati wa Mtume, Abubakr na Umar nilitoa mali nyingi ingawa nilikuwa naipenda na bakhili. Hivi sasa niko ukingoni mwa uhai wangu na nimewaachia watoto na ukoo wangu, makafiri wanaeenza madai ya uzushi dhidi yangu. Hakuna mji*

*uliotozwa kodi kwa ajili ya kufuja mali, bali kwa manufaa ya wananchi, Nina hisa ya moja ya tano, lakini sichukui kitu chochote kwa ajili yangu, inatumiwa na Waislamu wanaostahili. Katika mali ya Mwenyezi Mungu hakuna kinachoibwa wala sichukui kitu. Ninaishi kwa kutegemea kipato changu.*<sup>37</sup>

Shutuma nyingine aliyotupiwa Khalifa Uthman ni kuchoma moto Qur'an. Dai hili pia si la kweli. Ukweli ni kuwa Uthman alituma nakala za Qur'an inayotokana na ule msahafu asili na kuamuru nakala nyingine zote zichomwe moto. Alichukua hatua hii kwa sababu zilikuwepo naksi za Qur'an zisizokuwa na mpangilio wa Mtume kwa mujibu wa aya na sura kama Jibrili alivyomuelekeza Mtume. Baadhi ya nakala zilizokuwa nje ya Madina zilikuwa hazikukamilika. Hali kadhalika miandiko tofauti ilileta tofauti. Tofauti nyingine ilikuwa ile ya usomaji. Hivyo ni dhahiri misahafu haikuchomwa na dai hili kama mengine ni la uongo kwani kwa kazi hii Uthman amepewa jina la **Jami-ul-Quran** (mkusanyaji wa Qur'an).

Hata kazi ya kupanua eneo la Kaaba, na msikiti wa Madina ililaumiwa. Kazi ya upanuzi wa eneo la Kaaba ilianzwa na Umar na Uthman aliendeleza. Wenye nyumba za karibu zilizovunjwa walikataa kuchukua fidiya, na kuanza kulalamika. Baadhi ya maswahaba walipinga kutumia fedha za Serikali kupanulia msikiti wa Madina na uwanja wa Kaaba. Hata hivyo mnamo mwaka 29 A.H. Uthman aliamua kupanua msikiti wa Madina kwa pesa zake. Magogo ya miti yaliondolewa na kuta zikajengwa kwa matofali. Hebu ona kama sio unafiki na ukafiri kazi ya kurekebisha msikiti na upanuzi wa uwanja wa Kaaba ni vya kulalamikiwa, tena kwa gharama ya Khalifa mwenyewe ?

Lawama nyingine ambayo ni kuhusu mjomba wa Uthman Hakam Ibn Al-Aas ambae alikuwa akiwatendea vibaya jirani zake na kumcheza shere Mtume. Alihamishwa Madina. Baada ya

miaka michache Uthman alimuomba kwa Mtume na baada ya kuombwa mara nyingi Mtume aliahidi kulitazama upya suala hilo. Mtume alipokufa jambo hili lilikuwa halijapatiwa ufumbuzi. Uthman aliwaomba Abubakr na Umar wamrejeshe kutoka uhamishoni katika ukhalifa wao, lakini hawakuruhusu. Katika ukhalifa wa Uthman alimrudisha mjomba wake baada ya miaka 17 ya kuishi uhamishoni. Hili nalo limumfanya Khalifa kulaumiwa.

Hadithi zikavumishwa kuwa Khalifa amewanyanya baadhi ya maswahaba mfano unaotolewa ni wa Abu Dharr Ghifari. Swahaba huyu alikuwa mchamungu kama maswahaba wengine ila yeye alichukua muelekeo wa kisufi. Kwa imani yake hii alilaumu waliokuwa wanaishi maisha ya kujiweza hasa baada ya watu kupata utajiri kutokana na ngawira. Hali kadhalika alitaka Baitul Mal, pasiwe na salio. Fedha au mali igawiwe na itumike kadiri inavyokuja. alianza kueneza imani yake hii Syria. Gavana wa jimbo la Syria, Amir Muawiya alimuandikia Khalifa kumfahamisha juu ya shughuli za Abu Dharr Ghifari. Khalifa Uthman alimwita Abu Dharr Madinah. Abdallah bin Sabaa alijaribu kumuomba alipokuwa Syria lakini Gavana Muawiya alimwambia imani anayofundisha ni mpya katika Uislamu na nia yake nikuleta mtafaruku miongoni mwa Waislamu.

Abu Dhar alipofika Madinah alijadiliana na Khalifa. Khalifa alimuuliza Abu Dhar: “Watu wakashatekeleza wajibu wao mimi nina mamlaka gani ya kuwataka watoe zaidi?” Abu Dhar alipoona hakuweza kumbadili Khalifa alikwenda kuishi kijiji cha Rabdhah karibu na Madinah na alifia hapo. Wanafiki waligeuza maneno na kusema kuwa Abu Dhar alitakiwa aishi kijijini hapo kwa amri ya Serikali hivyo alinyanyaswa. Ni dhahiri Khalifa hata kama alifanya hivyo alikuwa sahihi kwa vile ni kweli imani ya Abu Dharr haikuwa ya Kiislamu. Inasemekana pia kuwa maswahaba aliowanyanya ni pamoja na Ammar bin Yasir na Abdullah bin Masud. Dai hili ni la uongo kama tulivyoonesha. Lakini linathibitika zaidi wakati Abu Ammar alipoteuliwa kuwa miongoni mwa wajumbe wa kwenda mikoani kuchunguza matatizo ya magavana.

Khalifa Uthman anatoka ukoo wa Banu Umayyah wa makureish. Kabla ya kuzaliwa Mtume kulikuwa na kutoelewana baina ya ukoo wa Banu Ummayah na ukoo wa Banu Hashim anaotoka Mtume ambao nao ni wa Kikureish. Wasabaai waliwashawishi ukoo wa Banu Hashim kuwa Khalifa anapendelea ukoo wa Banu Ummaya kwa kuwapa nafasi za juu na kuwaondoa madarakani ukoo wa Banu Hashim.

Dai lingine ambalo halina msingi kama mengine linahusu mashamba ya Serikali ya kuchungia wanyama. Mtume(s.a.w.) alianzisha mashamba ya Serikali ya kuchungia wanyama. Umar aliongeza mawili. Wakati wa Uthman Farasi na ngamia wa Serikali waliongezeka. Kwa sababu hii Khalifa aliongezea mashamba ya kuchungia wanyama ya Serikali. Uzushi ukawa Khalifa ameruhusu ukoo wake wa Banu Ummaya uchungie wanyama wao katika shamba la Serikali.

Wingi wa vita ulilazimisha matumizi makubwa ya fedha kwa kuimarisha jeshi kwa kununua zana na vifaa vya jeshi la majini. Pamoja na ngawira iliyokuwa inatumika kwa kuimarisha jeshi. Uthman alitumia Zaka na Sadaka kuimarisha ulinzi. Wapinzani wake wakashutumu kuwa, Zaka na Sadaqa zina matumizi yaliyotajwa kwenye Qur'an hivyo haikuwa sahihi kutumia kwa kuimarisha jeshi. Hiki ni kichekesho kwani moja ya matumizi ya Zaka na Sadaqa ni kuimarisha dini ya Allah(s.w). Ulinzi nao huimarisha dini ya Allah(s.w). Hata hivyo Khalifa alieleza kuwa alitumia fungu kwa kuliazima na atalirudisha.

Malalamiko mengine yaliyotolewa na wanafiki wale ni kuswali swala kamili bila kupunguza katika Hija, kupiga mahema Minna na kutoza Zaka farasi - mambo ambayo wakati wa Mtume(s.a.w.) wala wa Abubakar na wa Umar hayakufanywa. Kuhusu kutopunguza swala Khalifa alipoulizwa alisema nimefanya hivyo ili wakazi wa maeneo hayo wasidhanie kuwa kupunguza swala ndio utaratibu. Ama kuhusu mahema ni suala la maendeleo na kwa

watu wa leo ni jambo halina msingi kabisa. Kwa vile mahema na nyumba za kitalii zinatumiwa sio Minna tu bali hata Makka. Ama kuhusu farasi kutozwa au kutotozwa Zaka wakati wa Mtume na makhalifa wawili wa mwanzo yaweza kuwa uchache wao na kushiriki kwao kwenye vita. Wakati wa Khalifa Uthman na baada ya mfululizo wa vita hali ya uchumi ya Waarabu ilibadilika na Khalifa aliona ni Busara Zaka pia itolewe kwa farasi kama ilivyo kwa ngamia.

Sababu hasa ya chanzo cha ghasia hatimaye kumuua Khalifa Uthman hazikuwazi wakati wa Uthman bali zilianza wakati wa Mtume(s.a.w.). Maadui wa Uislamu wakati wa Mtume walikuwa Maqureysh, Waarabu, Wayahudi, Wapersia na Wakristu wa Kirumi. Baada ya kutekwa Makka koo na makabila mengi yalisilimu, lakini walisilimu kwa nia mbali mbali ambapo hapa hatutazitaja. Linalohibitisha hili ni kule kuukana Uislamu kulikotokea mara tu baada yakutawafu Mtume(s.a.w), uasi ambao uliikumba karibu Arabia yote. Wapinzani hawa walishindwa nguvu wakati wa Abubakar halikadhalika wakati wa Umar. Lakini haiyumkini kuwa walikuwa wameridhika na ustawi wa uislamu. Kwa hiyo hili ni kundi moja ambalo miongoni mwao walitokea wapinzani.

Kundi la pili la wapinzani linatoka kwa wanafiki ambao njama yao ya kumuua Mtume ilitajwa kwenye Qur'an na hila zao kubainishwa mwaka wa 9 Hijria na hiki kilikuwa kipigo kikubwa kwao. Kubadilika kwa sera ya kuwataja wanafiki bayana na Mtume kukatazwa kuwaombea na kuwazika na kutotambulika katika jamii ya Waislamu kulistawisha chuki dhidi ya viongozi wa Waislamu.

Kifo cha Mtume kiliwagawa Waislamu katika makundi matatu. Ukoo wa Mtume(Ahlul Bayt), Muhajirin na Ansaar. Pamoja na kuwekwa sawa hali hii wapo walioendeleza vikundi vyao nyoyoni na hasa pale upinzani ulipochukua umbo la kuonesha makosa Serikalini. Bado lilikuwepo tatizo la watu binafsi. Wapo Waislamu

waliojiingiza katika upinzani kwa maslahi yao binafsi. Mfano mzuri ni Muhammad bin Abubakar na Muhammad bin Hudhaifa.

Wayahudi nao hawakusahau kutolewa kwao Madinah na hata huko Khaibar walikohamia bado walitezwa nguvu na kulazimika kulipa Jizya. Makundi yote haya yaliungana kwa kujuana na kutokujuana kwa kusimamisha upinzani dhidi ya Khalifa Uthman na Serikali yake na hatimaye kumuua.

### **Fitna za Abdullah bin Sabaa**

Pamoja na makundi mengi haya, kiongozi wa udhia wote huu ni Myahudi aliyekuwa mkazi wa Yemen aliyejulikana kwa jina la Abdullah bin Sabaa. Sabaa hakuwa anautaka Uislamu na alipanga mpango wa kuudhuru. Mbinu aliyotumia ni kuingia katika Uislamu na kuupiga vita kutoka ndani.

Kwa kutumia hali ya mazingira ya wakati ule alitunga na kuhubiri imani zisizokuwemo katika Uislamu ambazo ni kila Mtume aliacha “Wasi” (mrithi wake katika ujumbe wake) na wasi wake alikuwa ndugu yake, kwa mfano Mtume Musa(a.s) alimfanya Haruna kuwa “Wasi” na Mtume(s.a.w) wasi wake ni ndugu yake Ali. Na Ali alikuwa mtu pekee aliyestahili kupewa Ukhalifa. Sabaa alifikia kiwango cha kusema kuwa makhalifa watatu waliotangulia Abubakar,Umar na Uthman sio halali. Namna pekee ya kurekebisha mambo ni kumuondoa Khalifa Uthman madarakani:

Ibn Sabaa pia alifundisha imani ya kurudi kwa Mtume(s.a.w). Alikuwa akishangaa kuwa ni ajabu kuamini kuwa Nabii Isa(a.s) atakuja kutoka mbinguni ili afuate Uislamu na kuupigania dhidi ya maadui na kuamini kuwa Mtume Muhammad(s.a.w) hatarudi. Ibn Sabaa aliamini na kufundisha kuwa kwa kuwa Mtume Muhammad(s.a.w) ni bora kuliko Isa(a.s) na kwa kuwa yeye Muhammad(s.a.w) ndiye Mtume wa mwisho, basi atarudi. Hali kadhalika Ibn Sabaa alitoa tafsiri potofu za aya za Qur’an ili kubatilisha itiqadi zake.

Madina hakupata wafuasi, hivyo alikwenda Basra na kuendesha shughuli zake za upinzani dhidi ya Serikali. Gavana wa Basra Abdallah bin Amir alimwita na kumhoji kwa sababu hii Ibn Sabaa aliogopa akaondoka Basra na kuwacha wafuasi wake chini ya uwongozi wa Hakim Hublah adui wa Gavana.

Kutoka Basra alikwenda Kufa ambako alipata wafuasi wengi. Gavana, wa Kufa, Sa'd bin al As alimwita Ibn Sabaa na kumuonya juu ya udhalimu anaoufanyia Uislamu. Hatua hii ilimfanya ahame Kufa aende Damascus ambako hakufanikiwa lakini alimteua Ashtar kuwa naibu wake na kuacha maelekezo kuwa ujumbe wake uendelee chini chini na yeye akahamia Misri. Ambako kwa kuwa Gavana wa Misri Abdallah bin Sarah alikuwa katika vita vya Warumi, Ibn Sabaa alipata muda wa kupandikiza fikra zake potofu akapata wafuasi wengi na kuweza kuwasiliana na vituo vyake vya Kufa na Basra.

Wafuasi wa uasi huu, walitumia mikakati mingi ya kujiimarisha. Walijionesha kuwa ni wacha Mungu na kushawishi watu waunde malalamiko dhidi ya Maafisa wa Serikali, Magavana na Khalifa. Walitawanya barua za kuonesha udhalimu wa Serikali hali ni madai ya uzushi. Barua hizi zilitumwa kwa wafuasi wa Ibn Sabaa nao wakawa wanazisoma hadharani. Walionesha kuwa Ali, Talha na Zubair, Maswahaba maarufu kwa wakati ule, waliwaunga mkono ili kuunda taswira ya kuonesha kuwa kweli Serikali ina matatizo.

Pamoja na barua watu walijiriwa kuendeleza madai dhidi ya Serikali na Khalifa. Hapo awali tulieleza kuwa wapo watu waliojiunga na ghasia za Ibn Sabaa kwa sababu zao binafsi wakiwemo Ammar bin Yasir, Muhammad bin Abu Hudhaifah na Muhammad bin Abubakar. Muhammad bin abu Hudhaifa alilelewa na Uthman tangu udogo kwa kuwa alikuwa yatima. Alitegemea apate nafasi kubwa katika Serikali alipoona hapati akaenda Misri kujiunga na wahaini. Ni hivyo hivyo kwa mtoto wa Abubakar. Alikuwa na kesi ya kudaiwa. Khalifa Uthman alihukumu kwa haki

dhidi ya Muhammad bin Abubakar. Muhammad akaona kaonewa akaenda Misri kujiunga na Ibn Sabaa. Ammar alikuwa miongoni mwa maswahaba wanne waliotumwa kusikiliza malalamiko mikoani. Alipofika Misri alishawishiwa na akakubali kujiunga na wanafiki wa kundi la Ibn Sabaa. Abu Sarah Gavana wa Misri alimfahamisha Khalifa kushiriki kwa Maswahaba hawa katika ghasia za Ibn Sabaa na kushauri wachukuliwe hatua. Lakini Khalifa alikataza kuwachukulia hatua yoyote.

Kutokana na harakati hizi za wapinzani, wasiwasi ulienea nchi nzima na serikali sasa ikalazimika kuchukua hatua, ili kudhibiti hali ya nchi.

## **Hatua ya Serikali Dhidi ya Waanzilishi wa Fitna na Farka**

Hatua ya kwanza ilikuwa kuwahamishia Syria viongozi 10 wa upinzani kutoka Kufa. Wakorofi hawa walipopelekwa Syria, Amir Muawiya alizungumza nao na kusikiliza mafundisho yao lakini alipowasahi waache kupoteza watu walijifanya hawamuelewi kwa sababu hii Gavana Muawiya alimuandikia Khalifa Uthman kumuomba awarudishe walikotoka ili wasiwaharibu watu wa Syria kwa vile wanazungumza lugha ya shetani na lengo lao ni kuwagawa watu na kuunda fitna. Watu hawa walirudishwa Kufa na walipoendelea na shughuli zao walihamishiwa Hirus ambako walidhibitiwa kwa muda na gavana Abdur-Rahman mtoto wa Khalid.

Hatua ya pili iliyochukuliwa na Khalifa pamoja na Shura yake ni kutuma wajumbe wanne(4) kutembelea Dola nzima na kusikiliza malalamiko ya wananchi. Maswahaba waliotumwa ni Muhammad bin Muslimah, Usamah bin Zaid, Ammar bin Yasir na Abdullah bin Umar. Wajumbe hawa ambao walirudi watatu walitoa taarifa kuwa hakukua na malalamiko. Ammar bin Yasir alibakia Misr na kujiunga na wapinzani.



## **Kuwasilisha Malalamiko Kwenye Kikao cha Magavana**

Kama kawaida magavana walikutana kila mwaka baada ya Hija. katika mwaka ule taarifa zilitolewa kuwa wenye malalamiko waende kuwasilisha malalamiko yao kwenye kikao hicho. Lakini hakuna aliyejitokeza. Si hivyo tu lakini Khalifa Uthman alitimiza dai la wapinzani hawa kwa kumuweka Gavana wanayemtaka Kufa. Walichokifanya wapinzani ni kuwa walikusanya kundi la watu wapatao elfu moja na kumzuia Gavana wa Kufa asirudi madarakani alipokwenda Madinah mkutanoni. Walimzuia mahali paitwapo Ajara, mtumishi wake aliuliwa na yeye akarudi Madinah. Khalifa akamthibitisha Abu Mussa kuwa gavana wa Kufa baada ya kutakiwa na wapinzani. Hapa Khalifa alionesha udhaifu, watu hawa walistahili kuadhibiwa kinyume na kukubali dai lao baada ya uhaini uliowazi.

Katika kikao cha Magavana Khalifa alitaka ushauri wa kuzima uasi nchini. Saad alishauri wapinzani wakamatwe na kuadhibiwa. Abu Sarah alishauri wasipewe posho; Ibn Aamir alitaka wapinzani wauawe; Muawiya pia alitaka zichukuliwe hatua kali. Kutokana na maoni haya Khalifa alijibu:

*Ukatili sitoruhusu, kama mapinduzi yakija sitaki kulaumiwa.  
Ukianza hivi mwisho wake mbaya. Ingekuwa vyema pale  
mapema wakati uasi haujaenea. Sasa hakuna la kufanya ila  
kukaa kimya na kusubiri bila kumkosea mtu yeyote.*

Muawiya alipokuwa anaondoka Madina alimsihi Khalifa akubali kuhama Madina lakini alikataa, na kusema hata kama ni kuokoa maisha yangu sitaondoka katika ardhi ambayo Mtume aliishi na kuzikwa.

Kisha Muawiya akamuomba akubali kuletewa jeshi lilinde mji wa Madina. Hali kadhalika Khalifa alikataa na kusema; “Sitawaweka askari wanaokaa karibu na nyumba ya Mtume”. Kwa

hali hiyo Muawiya akajibu “Sioni kinachokusubiri ila umauti; “Mwenyezi Mungu ndie mlinzi wangu,” alisema Khalifa Uthman.<sup>38</sup> ambaye alikuwa mzee wa miaka 82.

Uthman bin Affan, alijua hatari iliyokuwa inamkabili lakini hakutaka kutumia nguvu kuwaadhibu wapinzani wake kwa kuhofia kuzuka vita vya wenyewe kwa wenyewe, alihiyari afe yeye kuliko kuzusha vita ambavyo vingegarimu roho nyingi.

## **Khalifa Uthman Kufa Shahidi**

Ni dhahiri wahaini wa Serikali waliona wakati umefika wa kufanya lile walilokusudia tangu pale walipoweza kumtoa Gavana wa Kufa na kumuweka wanayemtaka bila kuadhibiwa. Wakaibua mbinu ya kutuma watu watatu kwenda Madinah kuwasilisha malalamiko yao. Watatu hao walitoka Misri, Basra na Kufa. Walipofika Madinah baadhi ya maswahaba walimshauri Khalifa kuwa wauwawe lakini kwa msimamo ule ule wa kutotaka kumwaga damu ya Waislamu, Khalifa alikataa na kusema nitawasikiza. Khalifa aliwasikiliza kisha akatoa hutuba ndefu ambayo ndani yake alijibu shutuma zote. Baadhi ya sehemu ya hutuba hiyo ya kihistoria ni kama ifuatavyo:

*Ninalaumiwa kwa kuwapenda ndugu zangu. Sio dhambi kwa mtu kumpenda ndugu yake. lakini sijamfanyia mtu udhalimu kwa sababu ya kupenda ndugu. Sijatumia chochote kwa ajili ya ndugu zangu kutoka kwenye mfuko wa Serikali...*

*Imesemwa kuwa nimewateua vijana wadogo maafisa. nimefanya hivyo kwa kuzingatia mchango wao katika uislamu. Hakuna anayekanusha uaminifu wao na mchango wao katika Uislamu, na Waislamu. Kuteuliwa kwa Usamah na Mtume (s.a.w.) kuwa kamanda wa jeshi ni ushahidi kuwa ujana sio kipingamizi cha kupewa uafisa.*

*Imedaiwa nimempa gavana wa Misri ngawira yote ya Afrika kaskazini kama zawadi. Ni kweli lakini niliposikia jamii haikupendezwa na jambo hili nimezichukuwa fedha zote kutoka kwa gavana na kuziweka kwenye mfuko wa Serikali (Baitul Mal).*

*Inadaiwa kuwa nimetenga mbuga za malisho ya Serikali kwa ajili ya wanyama wangu. Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, sitafanya hivyo. Katika mbuga hizo (mashamba hayo) ni wanyama wa Serikali tu (Baitul-Mal) ndio wanaolishwa humo, wote mnafahamu kuwa nilipopewa ukhalifa nilikuwa na wanyama wengi kuliko yeyote Arabia nzima. Leo nina ngamia wawili niliowaacha ili wanisaidie wakati wa Hija. Ingekuwaje, nitenge malisho ya Serikali kwa ajili yangu wakati wanyama wenyewe sina.*

*Watu wananilaumu kwa kuchoma nakala za Qur'an. Qur'an tukufu ni kitabu cha Mwenyezi Mungu aliteremshiwa Mtume (s.a.w.). Maswahaba waliokiandika chini ya usimamizi wa Mtume wako hai. Nimepeleka ile nakala ya Qur'an iliyokusanywa na maswahaba.*

*Inasemwa kuwa nimemrudisha Hakam Madina ambaye alipeleka uhamishoni na Mtume. ukweli ni kwamba Mtume alimhamisha Hakam kutoka Makka kwenda Taif. Baada ya kumwomba Mtume alimruhusu aishi Madina. Nimetekeleza ruhusa iliyotolewa na Mtume (s.a.w.)....”*

*(Mwisho wa Hotuba yake akasema). Niambieni kama kuna kitu kisichokuwa cha kweli kati ya niliyosema.....<sup>39</sup>*

Ingawa Khalifa alijibu shutuma zote kwa ufasaha, ukweli na uwazi, wawakilishi wa wapinzani walirudi na kusema uongo kuwa Khalifa amepuuza madai yao.

Ndipo wakaja makundi ya watu elfu, elfu kutoka Misr, Basra na Kufa na kupiga kambi karibu na Madina. Waliotoka Basra

walipiga kambi Dhikhasha, waliotoka kufa walikaa ‘Awas na waliotoka Misri walikaa Dhi-Murwah. Makundi ya wahaini hawa walishindwa kuingia Madina moja kwa moja kwa sababu walipokuwa wanakaribia Madina, Khalifa alikusanya wakazi wa Madina na kuwahutubia kuwa:

*Wananikusudia mimi, karibuni hivi watakumbuka wakati wa ukhalifa wangu na kuujutia, wataona siku moja ni kama mwaka kwa sababu ya vurugu umwagaji damu na uasi utaoenea nchi nzima.*<sup>40</sup>

Wananchi walichukua silaha na kuzuia uvamizi wa mji wao. Hali hii ndiyo iliyolazimisha wahaini kukaa nje ya Madina.

Wahaini hawa walikuwa na agenda moja tu, ya kumwondoa Khalifa madarakani kwa hiyari au kwa nguvu. ndiyo maana walipofika tu Madina kila kikundi kilimkabili waliyemtaka awe Khalifa kwani katika hili walitofautiana. Ibn Sabaa na Wamisri walimtaka Ali. Watu wa Kufa walimtaka Zubair na watu wa Basra walimtaka Talha. Maswahaba wote hawa walikataa na kuwaambia kuwa Mtume (s.a.w.) aliwaambia makundi ya Dhikhasha, ‘Awas na Dhi-murwah yamelaaniwa.<sup>41</sup>

Khalifa aliwatuma maswahaba maarufu akiwemo Ali kusikiliza malalamiko yao. Waliwakilisha matakwa yao pamoja na kutaka Muhammad Ibn Abubakar awe gavana wa Misri badala ya Abu Mussa. Khalifa alikubali bila kuuliza kisha akawaahidi kuwa atatekeleza maombi yao. Ali naye akasisitiza hivyo hivyo. Pamoja na kuwakubalia matakwa yao walivamia msikiti na kumuua Khalifa Uthman akiwa nasoma Qur’an.

## **Vita vya Wenyewe kwa Wenyewe**

Kipindi cha Ukhalifa wa Ali hakikuwa na wapinzani kutoka nje ya Dola ya Kiislamu. Na inaweza kusemwa kuwa hakukuwa na

upinzani kwa sababu hapakuwa na kiongozi aliyechaguliwa kwa utaratibu unaokubalika na kwa sababu hii inakuwa vigumu kusema kulikuwa na upinzani ila kulikuwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe. Ni vigumu kusema kuwa Ali alikuwa ameteuliwa kwa utaratibu wa Uislamu kuwa Khalifa. Wahaini wale baada ya kumuua Khalifa Uthman, mji wa Madinah na Serikali yake ilikuwa chini yao kwa muda wa siku sita na swala ya Ijumaa waliendesha wao.

Siku ya sita Ali alitangazwa kuwa Khalifa na wauwaji. Wauwaji hawa hawa ndio waliofundisha kuwa Ali ni “wasi” wa Mtume. Aisha, Talha na Zubeir ni vigumu kusema kuwa waliupinga Uislamu walipopigana na Ali katika vita vya Ngamia. Vile vile ni vigumu na haiwezekani Muawiya alipokataa kumtii Ali alikuwa amekosea hivyo alipinga Uislamu alipopigana na Ali katika vita vya Siffin. Tunachoweza kusema wakati wa Ali kulikuwa vita vya wenyewe kwa wenyewe. Katika vita hivyo, nani alipigania Uislamu, nani alipigania kundi lake, au ukoo wake au udugu au kabila lake n.k. ni maoni ya kila mwana historia baada ya kujua mkondo wa matukio ya kihistoria.

Jambo la kusikitisha ni kuwa kipindi cha Khalifa Ali kilitawaliwa na mapigano baina ya wenyewe kwa wenyewe. Baina ya Khalifa na Aisha, Talha na Zubair, Khalifa na Khawarij na Khalifa na Muawiya Gavana wa Syria. Matukio yalichukua mkondo ufuatao.

Baada ya kuuawa kwa Khalifa Uthman na kutawazwa kwa Ali baadhi ya jamaa wa Khalifa walikwenda Makka kueleza tukio lilivyokuwa, mama wa waumini Bi Aisha alistushwa sana na tukio hili, lakini lililotisha zaidi ni hatua ya Khalifa ya kuahirisha adhabu ya waliyomuua Khalifa Uthman kwa hoja kuwa kwanza arudishe amani nchini kisha ndipo awaadhibu wauwaji. Hoja hii ilikuwa ni ngumu kueleweka hasa ukizingatia mambo matatu. **Kwanza** muanzilishi wa ghasia na hatimaye kufikia kifo cha Khalifa Uthman

alifundisha imani ya “wasi” wa Ali. **Pili** hilo ndilo lililomuweka Ali madarakani na **tatu**, wauwaji hawa pamoja na kuambiwa waondoke Madina siku ya tatu ya Ukhalifa wa Ali kundi la Ibn Sabaa lilikhalifu amri ya Khalifa na kuendelea kubaki Madina kwa kisingizio cha urafiki. Mama wa waumini ambaye alikuwa anarudi Madinah kutoka kwenye Hija, alirudi Makka na kuwaomba watu kwenda kulipiza kifo cha Khalifa. Maswahaba maarufu Talha na Zubeir walimuunga mkono na wakawa naye. Wapiganaji 2,000 walipatikana. Lakini walipokuwa wanakwenda Madinah wakapata wazo la kupitia Basra kupata watu wengi. Walipokuwa njiani kuelekea Basra watu wengi wakaungana naye na alipofika Basra alikuwa na watu 3,000 chini ya Bendera yake.

Gavana wa Basra, Uthman bin Hunif alituma watu ili kujua lengo la ziara ya Bibi Aisha Basra. Wajumbe wa Gavana walifahamishwa kuwa yeye mama Aisha na Waislamu wengine walitaka kuwakumbusha Waislamu juu ya wajibu wao kwa Khalifa aliyeuawa. Na dhima yao ni kuwaadhibu wauwaji. Kusikia hivi Gavana alizuia msafara usiingie Basra. Kwa hiyo akaita mkutano na kuwaamuru watu wake wawapige Mama Aisha na wenzake baada ya kupata maelekezo kutoka kwa Khalifa Ali. Watu wake waligawanyika, kuna waliomuunga mkono yeye na wapo waliomuunga mkono Aisha. Mama Aisha alitoa Hotuba ambayo iliwezesha kuwateka nusu ya watu ambao mwanzoni walimuunga mkono Khalifa. Kuona hivi mama Aisha alitaka suluhu, lakini upande wa gavana kulikuwa na watu wa Ibn Sabaa ambao suluhu hawakuitaka - Hakim bin Hublan akiwa kiranja wa kundi hili lisilotaka suluhu alivamia jeshi la Mama Aisha(r.a) hata kabla ya ruhusa ya gavana wake na uchokozi huu vita vikaanza, gavana akatekwa, Hublan na wenzake wengi wapatao 600 wakauawa na Basra ikatekwa na kuwa chini ya Bibi Aisha, Talha na Zubeir.

## **Vita Kati ya Bibi Aisha na Khalifa Ali**

Khabari za kutekwa Basra zilimchukua kwa mshangao mkubwa Khalifa Ali ambaye alikuwa aende Syria kumrudi Muawiya lakini alilazimika kwenda Basra kwanza kutuliza hali ya kule.

Alipofika Dhi-Qar'a mahali karibu na Basra-alituma ujumbe kwa Aisha, Talha na Zubeir wafanye mazungumzo ya amani. Nafasi ilipatikana mazungumzo yakafanywa na wakawa karibu kukubaliana baada ya Ali kuahidi kuwa atawaadhibu wauwaji wa Uthman Dola itakapokuwa na amani. Lakini mpango wa amani haukuwa na maslahi kwa lile kundi la Ibn Sabaa ambalo lilifanya sehemu ya jeshi la Ali. Walinong'onezana kuwa Ali anataka kufikia makubaliano ya amani na ameahidi kuwaadhibu waliomuua Uthman. Kundi hili lilikuwa ndilo lililomuua Khalifa Uthman halikupendezwa na mpango huu, wakaunda hila iliyochochea kutokea vita. Mbinu mbili walizitumia. Kwanza walipeleka umbea Basra kuwa Ali akiingia Basra atawafanya watumwa wakazi wote na atawaua vijana wote. Kwa sababu hii watu wa Basra lazima wapigane.<sup>66</sup> Ibn Sabaa na wachochezi wake usiku usiku walivamia jeshi la mama Aisha ambaye aliarifiwa na kwa namna hii vita vikaanza. Vita hivi vinajulikana kwa jina la **Vita vya ngamia**.

Vita vilikuwa vikali kwa vile ukubwa wa jeshi ulilingana. Baada ya mapigano makali na kuuawa Waislamu wapatao elfu kumi, Talha aliuwawa na , Zubair aliacha kupigana na akawa anaelekea Madina ndipo akauliwa njiani. Wakati wote wa vita mama Aisha alikuwa katika sehemu ya uwanja wa vita akiwa amepanda ngamia. Kuwepo kwake kulifanya mapigano yaendeleo kwa kasi kubwa, bila kukoma, ndipo Ali alipoamuru ngamia wake akatwe miguu ya nyuma. Ngamia aliangukia miguu yake ya mbele na kwa heshima zote akatolewa mama Aisha ndani ya kikatio cha ngamia na vita vikaisha. Mama Aisha akasindikizwa Madinah na kaka yake Muhammad bin Abubakar.

Baada ya vita, Ali alizungumza na Waislamu katika msikiti wa Basra na Waislamu wakampa mkono wa utii. Alipoondoka alimuacha Abdallah bin Abbas kuwa Gavana wa Basra.

## **Vita Kati ya Khalifa Ali na Gavana Muawiya**

Vita vya pili vya wenyewe kwa wenyewe ni vile vilivyopiganwa baina ya Khalifa Ali na Gavana Amir Muawiya wa Syria - vita hivi vinaitwa **Vita vya Siffin**.

Sababu hasa ya vita hivi ni vigumu kuitamka kuwa ni hii au ni ile. Kwa vyovyote ilivyokuwa ni vita ambavyo vingeweza kuepukika katika kiwango kikubwa kama viongozi wawili hawa wangetanguliza Uislamu kuliko vinginevyo.

## **Yaliyopelekea Kuzuka kwa Vita vya Siffin**

Khalifa Ali alipopewa ukhalifa na wale wauwaji na kukubali kuwa Khalifa wapo maswahaba waliokataa kumtambua mpaka awaadhibu wauwaji. Ali alidai kuwa atawashughulikia nchi itakapotulia. Kinyume na ushauri wa maswahaba wakongwe wengi Ali aliamua kubadilisha Magavana wote. Gavana wa Kufa na Syria walikubali kwa sharti kuwa endapo atawaadhibu waliomuua Khalifa Uthman wangempa mkono wa utii na kuacha ugavana. Ammarah bin Hassan alipokwenda Kufa kuchukua nafasi ya ugavana alilazimishwa kurudi kwa vile watu wa Kufa hawakutaka gavana wao Musa Ashari abadilishwe. Ama yule aliyepangiwa Syria alipofika Tabuk, majeshi ya Muawiya yalimuamuru arudie pale pale.

Ali alituma wajumbe maalum Kufa na Syria. Gavana wa Kufa, Abu Mussa Ashari, alituma jibu la kuridhisha na kumuarifu Khalifa kuwa watu wa Kufa wamekubali kumtii na hivyo Gavana alichukua kiapo cha utii kwa niaba yake. Jibu hili lilimpendeza Ali, alimuacha Abu Mussa aendelee kuwa Gavana na yeye mwenyewe akahamisha makao makuu ya Serikali kutoka Madinah na kuyapeleka Kufa. Sababu inayotajwa katika vitabu vya historia ni kuepuka umwagaji damu katika msikiti na mji mtakatifu wa Mtume (s.a.w.) kama ilivyotokea kwa Khalifa Uthman.



Lakini maoni ya kutoungwa mkono sana Madinah na Kufa ndiko kulikokuwa chimbuko la wauwaji na kuwa jeshi lake lilikuwa na wachochezi wa Ibn Sabaa ambao inadhaniwa walikuwa na hisa kubwa katika uamuzi huu, havitajwi wala kuongelewa. Hata hivyo umwagaji damu katika mji na msikiti mtakatifu wa Madinah pengine na hata wa Makka hauepukiki kwa kuhama Madinah. Umwagaji damu unaepukika kwa kutekeleza haki. Vile vile ghasia hazina mahali na damu siyo ya Khalifa tu bali damu ya yeyote siyo ya kumwagwa bila sababu za Kiislamu ambazo ni kuuu au uhaini. Halafu hakuna mahali ambapo kumwaga damu ni halali na pengine ni kharamu. Ni haramu kumwaga damu iwe Madinah, Maka, Taif, Kufa, Basra, n.k. Hivyo hoja inayotolewa katika vitabu vya historia kuwa imempelekea Khalifa Ali kuhamishia makao makuu ya Serikali kutoka Madinah kwenda Kufa uzito wake ni hafifu na inakanganya.

Pamoja na Gavana wa Kufa kutambua Ukhalifa wa Ali na Khalifa akapeleka makao makuu ya Serikali Kufa, mambo hayakuwa hivyo kwa Syria. Kabla ya kuuuwa kwa Khalifa Uthman, Amir Muawiya, gavana wa Syria alimuomba Khalifa akubali kwenda Syria au amletee jeshi la kumlinda. Maombi yote haya yalipokataliwa Muawiya alimwambia nduguye Uthman sioni kitu kinachokutokea ila kifo. Isitoshe Muawiya aliwafukuza mkoani kwake wachochezi wa ghasia. Ndiyo kusema alikuwa anafuatilia wimbi la upinzani na hakuridhika na kuuuwa kwa Khalifa. Pia alishangazwa na Khalifa aliposhindwa kuwarudi wauwaji kwa hoja ya kuleta amani. Kilichotokea ni kuwa watu waliokuwa wanaona Uthman kaonewa walikimbilia Syria.

Pamoja nao wakaenda na vidole vilivyokatwa, vya mke wa Khalifa, Nailah, pamoja na shati lenye misindosindo ya damu ya Khalifa Uthman. Vitu hivi vikatungikwa nje ya msikiti wa mji wa Damascus, Syria. Wasiria walishikwa na uchungu mkubwa wakalia kwa machozi na kwikwi kwa kishindo kikubwa kwa kifo hiki cha kikatili cha Khalifa Uthman na kudai kulipiza kisasi kwa wauwaji. Hii

ndiyo hali waliyokuwa nayo watu wa Syria. Hivyo Khalifa Ali alipotuma mjumbe wake maalumu kwa Muawiya, alichokifanya Muawiya ni kumuweka kizuizini mjumbe yule na baada ya miezi mitatu alituma mjumbe wake na barua yenye anuani “*Kutoka kwa muawiya kwenda kwa Ali.*”

Barua hii ilipofunguliwa haikuwa na kitu ila Bismillahir-Rahmanir Rahiim. Isitoshe mjumbe yule alimwambia Ali kuwa; watu 50,000 wanaomboleza kifo cha Uthman na wako tayari kupigana mpaka wauwaji wa Khalifa wapatikane. Tukio hili linafanya sababu ya vita vya Sifin isieleweke. Khalifa Ali kusema kama alikuwa anawaogopa wahaini kwa sababu yoyote ile iwe wamo kwenye jeshi lake, au ndio waliomuweka madarakani au nyingine yoyote lakini bado ni kweli wamefanya kosa lisilovumilika kuwa nao. Ni kweli pia wapo wanaoleta hoja kuwa kwa sababu ya kujenga amani unaweza kuakhirisha adhabu ya watu, lakini kwa kiwango chochote kiwacho haki haiwezi kuahirishwa. Khalifa Ali aliahirisha haki ya kuwaadhibu wahalifu. Isitoshe wahalifu hawa walikuwa ndani ya jeshi lake. Tunachokisema ni kuwa kama hali ilikuwa hivi angeweza kutumia Wasyria kuzima uasi huu watu ambao walikuwa tayari kuwarudi wauwaji. Badala ya kuchukua njia hii ambayo inaonekana ingekuwa nyepesi na fupi, Khalifa alitangaza vita dhidi ya Gavana Muawiya kwa kile kilichodaiwa utovu wa nidhamu wa kutomtii Khalifa. Lakini hoja hii pia hairuhusu kumwaga damu ya Waislamu. Khalifa akamhukumu gavana kuwa ni mkorofi na anatomia kifo cha Uthman kama kisingizio tu. Gavana naye ambae amekaa Syria kwa miaka ishirini akamuona Khalifa kakumbatia wauwaji. Ameshindwa kuwaadhibu, kwa vile ndiwo waliomuweka madarakani na wamo katika jeshi lake. Gavana hakuona sababu ya kumtii.

Misingi hii ya tofauti za misimamo ndizo zilizopelekea vita vya Sifin ambavyo kwa kweli vingeweza kuepukika. Jambo hili linadhihirika tena Ali alipomuandikia barua Muawiyah ya kumtaka amtii na Muawiyah akamtuma mjumbe wake kwa Khalifa kumtaka

kwanza wapatikane wauwaji wa Uthman. Watu 10,000 waliokuwa na Khalifa walijibu kuwa wote ndio waliomuua Uthman.

Hali hii ikamfanya Khalifa aende kumrudi Muawiyah na Muawiyah naye kwa upande wake akajiandaa. Wote wakapiga kambi mahali paitwapo Siffin wakiwa na idadi ya askari inayolingana ya 50,000 Katika uwanja huu wa vita Ali alijaribu tena kumtaka Muawiyah ajiuzulu na amtii. Muawiyah naye kwa upande wake alimtaka Ali amkabidhi waliomuua nduguye Uthman. Na anataka hivyo akiwa Walii wa Uthman kabla ya makubaliano yeyote. Dai hili lilikataliwa na mapigano ya wenyewe kwa wenyewe yakaanza.

Mapigano haya yalianza Dhul-Hijah 36 A.H. Lakini katika mwezi wote huo, mapigano yalikuwa mepesi. Ulipofika Muharram wote wakakubaliana kuahirisha vita.

Vita vilianza tena mnamo mwezi wa Safar 37 A.H. Vilichukua muda wa zaidi ya juma moja Waislamu wakiuana bila huruma. Kutokana na wingi wa maiti waliozagaa katika uwanja wa vita, vita vilisitishwa kidogo kwa ajili ya kuzika na kuwaondoa waliojeruhiwa katika uwanja wa vita. katika kipindi hiki Muawiya alimuandikia Ali kama ifuatavyo:

*“Kama wewe au mimi tungefahamu kuwa vita hivi vingechukua muda mrefu hivi hakuna ambaye angevianzisha. Tuache vita hivi viharibifu. Wote sisi tunatokana na ukoo wa Manafi na hakuna mbora mbele ya mwenzie. Makubaliano yanayolinda heshima na nafasi zetu lazima yafikiwe”.*<sup>42</sup>

Ali alikataa kufanya makubaliano yoyote. Baadhi ya wanahistoria wanamshutumu Muawiya kuwa ni mjanja mjanja na hasa mshauri wake Amr bin al As kwa kubuni njia ya kumaliza vita kwa kufunga karatasi za Qur’an katika ncha ya majambia yao ikimaanisha kuwa vita viishe na suluhu ipatikane kwa kutumia Qur’an. Inadaiwa kuwa Muawiya alifanya hivi kwa kuona kuwa

alikuwa anakaribia kushindwa. Lakini ama ushahidi wa vyanzo vya historia unapingana au vinginevyo kwa sababu watu wa Khalifa nao hawakutaka kupigana tena. Kwani yasemekana pia “Ali alikuwa anazungumza na watu wake kirafiki katika namna ya kuhoji tendo la Muawiya. Ni mbinu ya watu waovu, wanaogopa kushindwa, wamefunika uasi wao kwa neno la mwenyezi Mungu! Watu wake wakajibu; ‘Tunaitwa kwenye Qur’an na hatuwezi kuidharau”. Katika mkutano wa hadhara walimtishia Khalifa kuwa kama hata kubali watamtoroka, kumkamata na kumkabidhi kwa adui. Walimlazimisha Khalifa amwite Usstur aliyekuwa kwenye mapigano.

### **Suluhu**

Watu wawili waliteuliwa, Musa Ashari kutoka upande wa Khalifa Ali na Amr bin al As kutoka upande wa Gavana Muawiya wafanye suluhu kwa mujibu wa Qur’an.

Wasipokubaliana uamuzi utolewe kwa kupiga kura na mshindi awe yule ambaye atapata kura nyingi. Kila upande ungetoa watu mia nne (400) na kufanya jumla ya watu 800. Majaji hawa wawili pamoja na watu 800 hawa wakutane Damat-ul-Jandal mahali palipo kati kati ya Syria na Iraq katika mwezi wa Ramadhani kufanya suluhu hii na Kikao hiki kitangazwe. Hivyo, Ali na Muawiya walifanya makubaliano ya Muda. Mapigano yakasitishwa na majeshi yakaondoka kwenye uwanja wa mapambano.

### **Kuibuka kwa Khawarij**

Baada ya makubaliano, Ali aliwatangazia makubaliano haya wapiganaji wake. Lakini ndugu wawili wa kabila la Azza walisimama kupinga suluhu kwa hoja kuwa wanazo hukumu za Mwenyezi Mungu katika Qur’an hivyo hawahitaji wasuluhishi. Watu wengi waliunga mkono rai hii na kufikia 12,000. Wao hawakurudi Kufa, walipiga kambi mahali paitwapo Harorah. Walimteua Sheikh bin Rabi kuwa kamanda wao na Abdullah bin Kawa kuwa Imam wa kuongoza Swala. Walitangaza imani yao ambayo ilikuwa:

*“Ba’iyah iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu, yeye tu ndiye wa kutiwa. Kuhubiri mema na kukataza mabaya. Hakuna Khalifa au Amir. wote Ali na Muawiyah wana makosa, Muawiyah anamakosa kwa kutomtii Ali, na Ali anamakosa kwa kukubaliana na Muawiyah juu ya suluhu. tutaposhika mamlaka tutaanzisha mfumo wa maisha ya jamii uliojengwa juu ya Qur’an”.*<sup>43</sup>

Ali aliporudi Kufa alimtuma Abdullah bin Abbas, Harorah kuzungumza na Khawarij. Aliweza kuwavuta na wakakubaliana na Khalifa baada ya mazungumzo ya muda mrefu. Hata hivyo kukubali huku kulikuwa kwa muda tu.

## **Tamko la Wapatanishi**

Baada ya mazungumzo marefu wapatanishi walikubaliana kuwa wote wawili Ali na Muawiyah hawafai kugombea nafasi ya ukhalifa. Amr bin al- As alimtegea Abu Mussa aanze yeye kusema msikitini juu ya maazimio yao. Abu Muusa akasema; “Enyi watu tumelizingatia vyema suala linalotukabili. Hatukuona njia nyingine ya kuleta amani miongoni mwa watu ila kuwaondoa wote katika nafasi ya kugombea Ukhalifa. Baada ya hivi mchague Khalifa anayefaa.”<sup>44</sup> Hii ndio hukumu yangu.

Alipopanda jukwaani Amr bin al As alibadili maneno na kusema maneno wasiyokubaliana na mwenziwe kwa kusema; “Mmesikia hukumu ya Abu Mussa. Amemuondoa mtu wake nami pia ninamuondoa. Lakini kwa chifu wangu Muawiyah, yeye ninamthibitisha, ni mrithi wa Uthman, mlipiza wa damu yake, ni bora kuliko wote kwa kuchukua nafasi yake.”<sup>45</sup>

Wajumbe wote walichanganyikiwa kwa kauli hii na kukawa hakuna maelewano. Nusra Amr bin al-As auliwe na askari wa Ali. Uamuzi huu haukufuata Qur’an hivyo haukukubalika. Khawarij walijikusanya na kuanza uasi. Walihama Harorah na kwenda

Nahruwan. Katika eneo hili waliuwa watu na kufanya ukatili. Khalifa Ali alizungumza na Khawarij hawa ili waache vitendo vyao na imani yao potofu.

Lakini hawakukubali, kwa hali hii mapigano yakawa lazima, hata hivyo walishindwa vibaya. Baada ya hapa Khalifa Ali aliamuru jeshi lake liende Syria kupambana na Amir Muawiya kwa sababu suluhu haikuwa katika Qur'an. Lakini kabla ya kwenda Syria Khalifa Ali alipiga kambi mahali paitwapo Nakhila karibu na mji wa Kufa. Askari wake waliomba kwenda makwao na akawaruhusu, wengi hawakurudi na safari ikavunjika. Alijaribu mara mbili kukusanya askari kwenda Syria bila mafanikio na kutokana na hali hii suala zima la kupigana tena na Muawiya akaliacha.

## **Muawiyah Ateka Jimbo la Misri**

Khalifa Ali alimteua Qais bin Sad awe gavana wa Misri. Qais alichukua ahadi ya utii kwa niaba ya watu wa Misri, lakini watu wa jimbo la Khartaban hawakutoa ahadi ya utii kwa Khalifa Ali na Qais aliwaacha kwa kuwa kulikuwa na amani.

Hali hii ya kuwaacha watu wa Khartaban iliwafanya baadhi ya watu wamuone Qais sio mtiifu kwa Khalifa. Khalifa alikusudia kumjaribu Qais kwa kumuamuru awapige vita watu wa Khartaban. Qais hakuona sababu ya kupigana na watu wa Kharaban hivyo akaondolewa kwenye ugavana na nafasi yake akateuliwa Muhammad bin Abubakar.

Muhammad alikuwa kijana hivyo aliwalazimisha watu wa Khartaban wakubali Ukhalifa wa Ali. Watu wa Khartaban hawakukubali na walisubiri hadi vita vya Siffin vilipomalizika waliamua kujilinda dhidi ya majeshi ya gavana Muhammad bin Abubakar na mapigano yakazuka. Majeshi ya gavana yakashindwa mara mbili. Khalifa aliamua kumbadilisha Muhammad na kumtuma Ushtar kuwa gavana wa Misri. Lakini

Ushtar alikufa alipofika mpakani mwa Misr hivyo Khalifa alimtaka Muhammad aendeleo kushikilia ugavana wa Misri akamtumia askari 2,000 ambao aliwapata kwa taabu. Lakini kabla askari wa Khalifa hawajafika Muawiya alimtuma Amri bin al As na jeshi la kutosha, likayashinda majeshi ya gavana na yeye mwenyewe kuuliwa. Kwa ushindi huu Misri ikawa chini ya Muawiyah na Amr bin al As akawa gavana wa Muawiyah Misri. Hii ilikuwa katika mwaka wa 38 A.H.

## **Ghasia Sehemu Mbali Mbali za Dola ya Kiislamu**

Misri kuwa mikononi mwa Muawiyah kulichochea upinzani dhahiri baina ya Ali na Muawiyah. Mnamo mwaka 38 A.H. gavana wa Basra Abdallah bin Abbas alikwenda Kufa kumzuru Khalifa. Wakati huu Basra ilikuwa na wafuasi wa Ali, hali kadhalika wafuasi wa Muawiyah. Kutokuwepo kwa Gavana kulipelekea Ubaidullah Ibn Hadrami mfuasi wa Muawiyah kushawishi watu na kuunda jeshi la kulipiza kisasi dhidi ya mauaji ya Uthman. Alipata jeshi na akavamia Basra. Ziyad ibn Abi Sufiyan aliyekuwa amemshikia ugavana akashindwa kuyamudu majeshi ya Hadrami na kukimbia. Hata hivyo Khalifa aliposikia uasi huo alimtuma Jariah ibn Gudumah na jeshi ambalo liliweza kuzima upinzani. Hadrami na watu wengine sabini walijificha ndani ya nyumba ambayo wafuasi wa Ali waliichoma moto.

Khawarij nao waliendesha upinzani dhidi ya Serikali ya Ali. Upinzani mkali uliendesha na Khirrt ambae alipigana na Ali katika vita vya **ngamia** na vita vya **Siffin** akiongoza kabila lake la Bani Najia. Jitihada za kumteka katika vita hivi zilishindikana na alikimbilia Ahwaz na Ran Hermuz. Aliwashawishi, Waajemi (Persians), Wakurd (Kurds) na Wakristo wasilipe kodi, akiwa na kundi la wafuasi wake aliendesha uasi Faris na Kirman. Khalifa alituma jeshi ambalo liliweza kuzima uasi huu, katika mapigano haya Khirrt aliuliwa. Kwa ushindi huu jimbo la kusini mwa Persia likarudia utulivu na Ziyad akateuliwa Gavana wa jimbo hili.

Muawiya bado aliendelea kutumia vikundi vya askari katika sehemu mbali mbali za Dola ya Kiislamu. Numan ibn Bashir alitumwa Ain al-Tamr lakini alishindwa na gavana wa Ali, Maliki bin Kab. Kundi lingine la watu elfu sita chini ya uongozi wa Sufiyan ibn Auf lilikwenda Ambar na Madain (Madian), walifanikiwa kumuua kiongozi wa Ambar. Khalifa Ali alimtuma Said Ibn Auf na jeshi ambalo lilimfanya adui akimbie. Askari wengine elfu tatu chini ya uongozi wa Dahak ibn Qais walikaribia Basra. Mapigano yalitokea baina ya majeshi ya Khalifa na Waasi. Waasi 19 waliuliwa na wengine wakakimbia.

Ghasia zote hizi zilitokea katika mwaka wa 39 A.H. Katika mwaka huo huo wa 39 A.H. Ali alipeleka mwakilishi wake Ibn Abbas awe kiongozi wa Hijja, na Muawiyah naye alimpeleka Yazid ibn Sanjar, awe muwakilishi wake. Ugomvi baina yao ulizuka na suluhu ikawa wote wawili wasiongoze Hijja na Shaiban ibn Uthman ibn Abi Talha aliteuliwa kuongoza Hijja. Hali hii ilidhoofisha nafasi ya Ali kama Khalifa.

## **Kutekwa kwa Makka, Madina na Yemen**

Katika mwaka wa 40 A.H. Amir Muawiya alimtuma Busr Ibn Abi Artat na watu elfu tatu kwenda Hijazi ambako aliiteka Madina, Makka na mji wa Sanaa, Yemen na kuwataka wamtii Muawiyah. Huko Yemen aliua watoto wadogo wawili wa Gavana wa jimbo hilo Ubaidullah ambaye alikimbilia Kufa. Vile vile aliwaua wafuasi wengi wa Ali. Jariah Ibn Qudamah akiwa na askari elfu mbili alitumwa kurudisha maeneo yaliyotekwa. Alifanikiwa kuirejesha Sanaa mikononi mwa Khalifa kwani wakati huu Busr alikwisharudi Syria. Lakini alipofika Makka alipata taarifa ya kuuwawa kwa Ali na huu ukawa ndio mwisho wa Ali.

## **Kuuwawa kwa Ali**

Baada ya vita vya Nahrwan, Khawarij waliendesha mambo yao chini chini. Inadaiwa waliendelea kuisakama Serikali.



Hawakumpenda Ali wala Muawiyah kwa sababu wao ndiyo chanzo cha kugawanyika kwa Waislamu, katika kundi la Muawiyah na kundi la Ali. Amr bin al As naye walimuona ana makosa kwa vile ndiye mshauri na afisa mipango wa Muawiya. Hivyo walipanga kuwaua wote watatu alfajiri ya mwezi 17 Ramadhan 40 A.H. wakati wa swala ya Alfajiri. Iipangwa Ali auliwe na Abdur-Rahman Muljam. Muawiya auliwe na Bark Ibn Abdullah na Amr bin al As auliwe na Amr ibn Bark. Wauwaji hawa walitia sumu kali katika majambia yao na wote wakafanya kazi yao kama walivyopanga Misri, Syria na Kufa. Lakini matokeo hayakuwa mia kwa mia. Ali alijeruhiwa vibaya na jeraha lilisababisha kifo chake kilichotokea jioni ya mwezi 20 Ramadhan 40 A.H. Muljam alikamatwa na kuhojiwa. Kabla hajafa Khalifa Ali aliwaita watoto wake na kuwauusia kumcha Mungu. Lakini alipoulizwa kama Hassan atawazwe Ukhalifa alisema, "Nawaachia Waislamu waamue". Khalifa Ali alitawala kwa miaka mine na miezi tisa. Alikufa akiwa na miaka 63.

Baada ya Khalifa Ali kuuliwa, mtoto wake, Hassan, alichaguliwa kuchukua nafasi ya Ukhalifa lakini Muawiyah aliasi na kuandaa jeshi dhidi yake. Baada ya mapigano kidogo, Hassan alizidiwa nguvu na akaona amwachie Muawiyah Ukhaifa kwa makubaliano kuwa baada yake uongozi uchukuliwe na ndugu yake, Hussein bin Ali. Kinyume na makubaliano hayo, ambayo pia hayakuwa ya Kiislamu, Muawiyah kabla hajafa, alimteua mtoto wake, Yazid bin Muawiyah kushika uongozi wa Dola baada yake.

## **Kuanzishwa Ufalme.**

Muawiyah kwa kumrithisha mtoto wake, Yazid, uongozi wa Dola, bila kuzingatia utaratibu wa kuchangua viongozi kutokana na sifa stahiki, alivunja maongozi ya Kiislamu na kuasisi utawala wa kifalme au utawala wa kiukoo ambao mpaka leo unaendelezwa katika nchi nyingi za Arabia(Bara Arab), Saud Arabia ikiwa miongoni.

Dola ya kifalme aliyoiasisi Muawiya ilitafautiana na Dola ya Kiislamu aliyoiasisi Mtume(s.a.w) na kuendelezwa na Makhaliifa wanne waongofu, Abubakar, ‘Umar, Uthman na Ali, kwa sababu:

- (i) Taasisi ya shura ilivyunjwa na raia walipokonywa uhuru wao wa kutoa maoni na kukosoa viongozi
- (ii) Hazina ya Dola – Baitul-Mali, ilifanywa mali ya nyumba ya mfalme ambapo mfalme aliitumia atakavyo kwa maslahi yake binafsi na familia ya kifalme.
- (iii) Tabia za kijahili za majivuno ya kikabila na nasaba ziliibuka na kustawishwa na ufalme.
- (iv) Watawala (viongozi mbali mbali wa dola) walianza kuishi kwenye mahekalu na nyumba za kifahari za Kifalme.
- (v) Suala la kutenganisha maongozi ya **Serikali** na **Dini** liliibuka. Masheikh wazuri waliokuwa waadilifu walitengwa na kundi la watawala. Wao wakawa wanajitahidi kuirekebisha jamii lakini wakiwa ndani ya kuta nne za msikiti na nje ya vyombo vya dola.

## **Zoezi la 4**

- 1. (a) Wabainishe Makhaliifa wanne waongofu wa Mtume(s.a.w) na muda aliiodumu katika uongozi kila mmoja wao.  
(b) Eleza kwa ufupi namna kila Khalifa wa Mtume(s.a.w) alivyochaguliwa na kuingizwa kwenye uongozi.
- 2. Uchaguzi wa Ali(r.a) kuwa Khalifa wa nne wa Mtume(s.a.w) ulikuwa na utata. Jadili.
- 3. (a) Ainisha madhumuni ya Dola ya Kiislamu.  
(b) Katika kutakeleza madhumuni ya Dola ya Kiislamu Khalifa aliwajibika kufanya yafuatayo:  
(i) \_\_\_\_\_ (ii) \_\_\_\_\_ (iii) \_\_\_\_\_ (iv) \_\_\_\_\_ (v) \_\_\_\_\_

4. Ainisha vyanzo saba vya pato la serikali katika kipindi cha makahalifa wa Mtume(s.a.w).
5. Onesha kuwa wakati wa makhalifa ulinzi na usalama uliimarishwa zaidi kuliko kipindi kile cha Mtume(s.a.w). Kwanini ?
6. (a) Eleza juu ya uasi wa Dola(Riddah) uliotokea mara tu ya kutawafu Mtume(s.a.w)  
(b) Ni sababu zipi zilizopelekea kutokea kwa “riddah”  
(c) Onesha namna Khalifa Abubakar Siddiq(r.a) alivyokomesha riddah.
7. Toa maelezo mafupi juu ya:  
(a) Vita vya ngamia  
(b) Vita vya Siffin
8. Nikipi kilichopelekea kutokea kwa mapigano ya waislamu kwa waislamu wakati wa uongozi wa Khalifa Ali bin Abu Talib(r.a)”
9. Ni sababu zipi zilizopeleka kuuliwa:  
(a) Khalifa ‘Uthman bin Affani  
(b) Khalifa Ali bin Abu Twalib.
10. (a) Eleza hatua kwa hatua namna Dola ya Kiislamu aliyoasisi Mtume(s.a.w) ilivyoporomoka na kuzuka Dola za kifalme.  
(b) Toa mafunzo matano(5) yatokanayo na kuporomoka kwa Dola ya Kiislamu aliyoiasisi Mtume(s.a.w)

## *Sura ya Tano*

### **KUHUISHA UISLAMU WAKATI WA TABIINA**

#### **Utangulizi**

Pamoja na kuporomoka kwa dola ya Kiislamu, waumini wa kweli wamekuwepo na kujitahidi hapa na pale, kwa mmoja mmoja na katika vikundi, kwa kadiri ya uwezo wao kuurudisha Uislamu katika ile hali aliyoiacha Mtume(s.a.w). Kwa mfano, pamoja na kuporomoka kwa Dola ya Kiislamu na maadili yake katika utawala wa kifalme wa Banu Umayyah, ulioasisiwa na Mu'awiya, aliibuka 'Umar bin Abdul Aziz aliyekuwa Muislamu mcha Mungu, ambaye alipopata tu fursa ya kuteuliwa kuwa Kiongozi wa Dola, aliirejesha dola kwenye Uislamu. Pia walitokea maimamu mashuhuri wa fiqh ambao walifanya jitihada kubwa na kuyatoa muhanga maisha yao yote katika kuurudisha Uislamu katika nafasi yake ya kutawala kila kipengele cha maisha yakibinafsi na kijamii. Maimamu hawa ni: Abu Hanifa, Maliki, Shafii na Hambali. Tabiin niwafusi wa maswahaba.

#### **Khalifa 'Umar bin Abdul Aziz**

Wakati watu wakiendelea kukata tamaa na utawala mbaya wa Banu Umayya aliibuka Umar bin Abdul Aziz mwaka 99 A.H(717A.D). 'Umar alizaliwa mwaka 61 Hijriya. Wakati wa utawala wa Suleiman Ibn Abdul Malik, akawa gavana wa Madina. Alikuwa kijana mtanashati na mwenye tabia nzuri. Kwa vile uongozi ulikuwa ukienda kiukoo, 'Umar hakuwa miongoni mwa waliotarajiwa kushika Ukhalifa. Hata hivyo Suleiman hakuwa na mtoto mkubwa hivyo ikatokea Umar kupendekezwa kuchukua uongozi na akakubalika.

Baada ya kushika uongozi, ‘Umar alibadili maisha yake yakawa rahisi zaidi na ya uadilifu. Aliwaondoa magavana wote waliokuwa katili. Akarejesha hadhi ya Baitul-Mal, ikawa fedha ya umma inakusanywa na kutumiwa kwa uadilifu. Pamoja na yeye mwenyewe kujichunga katika kutumia Baitul-Mal, alikuwa mkali pia kufuatilia maafisa waliofuja mali ya umma. ‘Umar bin Abdul Aziz hakuishia hapo, alitoa amri na kusimamia marekebicho ya vipimo(mizani, ili raia wasipunjwe). Aidha ardhi ambayo ilitengwa kwa ajili ya wakubwa aliichukua na kuwagawia raia. ‘Umar bin Abdul Aziz alikuwa kiongozi rahim na mtu mpenda watu, asiye na makuu. Alikuwa karibu na watu akisikiliza maoni yao juu ya uendeshaji wa dola, akitatua shida na matatizo ya raia. Kabla yake, Serikali zilizotangulia hazikujali hali wala hisia za raia. Zilikusanya kodi na kuendesha dola kwa misingi ya kujali zaidi familia na koo za wakuu. Hazikuwa zikijishughulisha kubadili tabia na mienendo ya watu. Kadhalika hazikuwa zikiwajenga watu kimaadili. Kazi hiyo waliachiwa masheikh. Uongozi wa ‘Umar ulibadili mtazamo huo potofu wa kutenganisha Dini na Serikali badala yake ukasimamia kikamilifu kazi ya kuamrisha mema na kukataza maovu huku ukiboresha hali na maisha ya watu. Kauli ya kukumbukwa ya ‘Umar bin Abdul Aziz juu ya wajibu wa kiongozi wa kiislamu ilikuwa: **“Muhammad alitumwa kama Mtume sio mkusanya kodi”**. Akiwa na maana wajibu wa kiongozi wa dola ya kiislamu haukomei katika kukusanya kodi tu bali anawajibika pia kuangalia maadili ya jamii.

Katika kujenga udugu miongoni mwa raia wake, Serikali ya ‘Umar ilipiga marufuku mila zote za kijahili ikiwa ni pamoja na mishikamano ya kikabila na kiukoo. Baadhi ya waliokuwa machifu wa makabila wakati wa utawala wa Banu Umayya walipotaka kufufua mila zao, ‘Umar bin Abdul Aziz aliwakemea vikali kwa kuwaambia: “Mila hizo za ukabila zinavuruga maana ya udugu wa kiislamu na mshikamano wa kijamii uliojengwa miongoni mwa raia (Waislamu). Akisisitiza msimamo huo, ‘Umar alionya kuwa yeyote ambaye angekutwa na tabia hiyo angekabiliwa na adhabu. Katika waraka wake kwa Dhahaakak Ibn Abdul Rahaman, Amiril Muuminina ‘Umar bin Abdul Aziz aliandika:

*“Shukrani zote anastahiki Allah na rehemu iwe kwa Mtume wake. Baada ya hayo, mnapaswa kujua kwamba Allah haikubali dini nyingine yoyote zaidi ya Uislamu ambayo amewachagua waja wake wema. Mwenyezi Mungu ameitukiza dini hii ya Uislamu kwa kuiwekea mwongozo unaoitofautisha na dini nyingine. Mwenyezi Mungu mtukufu amempa utume Muhammad na amemfunulia kitabu. Nye Waarabu, kama mnavyoyua, mliishi kwenye ujahili, ushirikina na kila aina ya uchafu, mambo ambayo yalikuwamisheni kwenye ufukara, vurugu na machafuko ya mara kwa mara miongoni mwenu. Mlikuwa watu wa kudharauliwa mbele ya wengine, uhai wenu ukiwa chini ya ujahili na ushirikina ambapo umauti wenu usingekuwa na mafikio mengine ila motoni. Mwenyezi Mungu amewaokoeni kutoka lindi la maovu, kuabudu masanamu na umwinyi, kuchukiana na migongano miongoni mwenu. Ingawa wengi miongoni mwenu mlimkataa Mtume wa Mwenyezi Mungu lakini aliendelea kuwaita katika uongofu. Mtume wa Mwenyezi Mungu ameondoka katika ulimwengu akiwa amekamilisha ujumbe aliotumwa na Allah.....”*

*“Nimeelezwa kwamba baadhi ya watu wamekuwa wakijikusanya kimakabila wa kujisaidia wao kwa wao kama ilivyokuwa zama zilizopita. Wanafanya hivyo wakijuwa wazi kuwa Mtume(s.a.w) alipiga marufuku ushirikiano huo. Mtume amesema hakuna utaiifa au ukabila katika Uislamu. Hakuna mtu kutukiza eneo analotoka juu ya wengine. Zama za ujahili, watu walikuwa wakishirikiana hata katika mambo maovu bila ya kujali athari kwa wasio na mahusiano nao. Watu walikuwa wakikandamizana, kubaguana, kuchukiana na kufanyiana machafu kwa sababu ya tofauti hizo. “Namuasa kila atakayesoma au kusikia waraka huu ajipambe na vazi la Uislamu na asiwe na ndugu ila na yule aliyeshikamana na Allah na Mtume wake. Narudia tena kuonya kwa kumshuhudisha Mwenyezi Mungu dhidi ya atakayekiuka maamrisha hayo ya Allah na Mtume wake, kwani Mwenyezi Mungu ni mwenye uwezo na yuko karibu na yeyote kuliko mshipa wake mkuu wa damu”.*

Kwa upande wa uchumi Amiril Muuminina ‘Umar bin Abdul Aziz alisimamia nguzo ya zaka na ukusanyaji wa kodi mbali mbali. Kutokana na uadilifu uliokuwepo katika ukusanyaji na utumiaji wa mapato ya umma, ilifikia mahali ndani ya dola ya Kiislamu kukawa hakuna maskini wa kupewa zaka.

UchaMungu wa Ibn Abdul Aziz ulijitokeza hata alipokuwa akiyaamuru majeshi yake kupambana na maadui. Hakuwa tayari kuona askari wa kiislamu akikiuka mipaka kwa kisingizio cha “vita haina macho”. Moja ya maelekezo yake kwa makamanda walioongoza misafara ya kijeshi, ‘Umar Abdul Aziz aliwataka wajiegemeze kwa Allah(s.w) katika kila wanapokabilia na maadui. Aliwataka wasipindukie mipaka katika kushambulia. Sehemu ya Waraka wake mrefu kwa makamanda wa Jeshi hilo umenukuliwa kama ifuatavyo:

*“Haya ni maelekezo kutoka kwa mja wa Allah na kamanda wa Waumini kwenda kwa Mansur Ibn Ghalib kamanda wa jeshi la kiislamu. Kamanda wa Waumini(Umar bin Abdul Aziz) anamuamuru Mansur kumpiga vita yule anayesimama kupambana naye. Aidha Mansur anaamriwa kumcha Mwenyezi Mungu katika kutekeleza wajibu huo na hiyo ndiyo stratejia na nguvu halisi ya kijeshi. Dhambi ni hatari zaidi kuliko silaha ya adui. Kamanda wa Waumini anamuamuru Mansur badala ya kumuhofu adui anapaswa kuhofu kukiuka mipaka ya Allah. Tumekuwa tukiwashinda maadui zetu vitani si kutokana na uhodari mkubwa wa kijeshi tulionao bali ni kutokana na dhambi na maovu yao, ingelikuwa si hivyo tusingekuwa na ujasiri wa kupambana nao. Hatuwezi kuwa na jeshi linalolingana na lao kiidadi na kisilaha. Kwa hiyo iwapo tutakuwa watenda maovu kama maadui zetu bila shaka watatushinda kwa mapambano ya silaha. Tambueni, iwapo hatutamcha Mwenyezi Mungu hatutaweza kuwashinda maadui zetu kivita. Tuwe waangalifu zaidi wa matendo yetu. Msijiweke kwenye aibu ya kukiuka mipaka ya Allah. Kuweni wakarimu na wenye huruma, mkizingatia kuwa mmewaacha wapenzi wenu na majumba yenu*

*kwa ajili ya Allah. Msijifakharishe mbele ya maadui zenu. Kamanda wa Waumini vile vile anamtaka Mansur Ibn Ghalib awaongoze wapiganaji kwa upole na kujali hisia zao. Asiwe mkali na katili kwao. Na iwapo Mansur hatajali ubinadamu itakuwa nafasi nzuri kwa maadui kupata ushindi dhidi yake. Kamanda wa waumini anawaelekezeni kuwa waangalifu katika maeneo ya maadui, wekeni wapelelezi miongoni mwa maadui baada ya kuwachunguza na kuwaona ni waaminifu kwenu ili mpate ripoti kutoka upande wa adui. Hata hivyo, ripoti zilizo na udanganyifu ni za hatari kwenu katika uchukuaji wa hatua, lazima muhakiki ripoti zao. Watakaowapeni habari kutoka kambi ya adui lazima nao muwatazame kama wapelelezi dhidi yenu. Amani ya Mwenyezi Mungu iwe juu yenu”.*

Kwa uadilifu na utendaji wake mzuri katika kuendesha Serikali, ‘Umar alifananishwa na Abubakar na alitwa Khalifa wa tano wa Dola ya Kiislamu. ‘Umar bin Abdul Aziz alifariki mwaka 101Hijriya baada ya kutawala kwa miaka miwili na miezi mitano. Baada ya kufariki ‘Umar Abdul Aziz, ulifuatia msururu wa utawala wa Kifalme.

## **Maimamu Wanne wa Fiq-hi**

Pamoja na kutokea mara kwa mara viongozi wema waliojitahidi kuirejesha jamii ya Kiislamu katika sura yake asilia, kama alivyojitahidi ‘Umar bin Abdul Aziz, viongozi wengi waliendelea kuutawala ulimwengu wa Waislamu kwa kuimarisha Ufalme na Udikteta zaidi kuliko Uislamu. Lakini, pamoja na kuwepo hawa watawala waovu, bado palikuwepo watu wema katika miji mbali mbali ya Dola hizo za Kifalme. Kwamfano, mji wa Baghdad ulijaa watu ambao walikamatana na Uislamu. Aidha walikuwepo viongozi wa dini ambao, pamoja na kutotambuliwa na watawala, walisimama imara kuwaongoza Waislamu. Pamoja na maguvu na vyombo vya Dola vya kutisha walivyokuwanavyo watawala bado, raia waliwaheshimu na kuwatii zaidi viongozi wao wa kiislamu.



Katika kupanuka dola ya Kiislamu, tangu wakati wa Makhalifa wanne wa Mtume(s.a.w), matatizo kadhaa yaliibuka ambayo yalihitaji ufumbuzi. Dola ilipanuka toka mashariki ya kati hadi Asia yote, sehemu za Afrika ya kaskazini na Hispania (Spain) huko Ulaya. Yaliibuka matatizo ya kisheria, taratibu za kibiashara na uchumi kwa ujumla na mila na desturi za watu mbalimbali . Uislamu ulitakiwa utoe fa-twa. Vinginevyo zingeibuka sheria na kanuni tofauti na Uislamu. Juhudi za mwanzo zilizofanywa ilikuwa ni utungaji na utoaji wa Fat'wa juu ya masuala mbalimbali kulingana na Qur'an na Sunnah. Hiki ndicho kipindi cha "Tabiina" ambacho waliibuka Maimamu wanne waliotumia uhai wao wote katika kutoa ufafanuzi, rai na Fat'wa juu ya sheria za Kiislamu katika mas'ala mbalimbali ya maisha. Hawa ni mabwana: Nu'man Ibn Thabit Abu Hanifa, Malik Ibn Anas, Muhammad Ibn Idris al-Shafii na Abu Abdallah bin Muhammad Ahmad Ibn Hambal. Wote hawa walitoa mchango mkubwa sana katika sheria ya Kiislamu na walikubaliana katika mambo yote ya msingi (Usul). Hawakufarakana kwa tofauti za maoni zilizojitokeza katika mambo madogo madogo.

**Imam Abu Hanifa** (80-150 A.H) na **Imam Malik Ibn Anas** (93-179 A.H) walirithi elimu ya moja kwa moja toka kwa masahaba iliyoegemea Qur'an na Sunnah. Aidha wao wenyewe walifanya juhudi kungeza ujuzi wao kulingana na mazingira mapya yaliyokuwa yakijitokeza.

**Imam Shafii** (150 - 204 A. H) aliendeleza juhudi za Abu Hanifah na Malik kwa kufanya utafiti zaidi wa ukusanyaji na uchujaji wa Hadith, na maoni ya wataalamu mbalimbali wa sheria.

**Imam Ahmad bin Hambal** (164-204 A.H) aliandika Musnad ambacho ndicho kitabu mashuhuri kabisa cha Sunnah.

Maimamu wote hawa ama wamesoma na kufundishana au kusoma kwa Waalimu sawa. Imam Malik na Abu Hanifa wote

walisoma Hadith kutoka kwa Imam Muhammad Ibn Shihab al-Zuhr. Imam J'afar al-Sadiq aliwahi kuwa mwalimu wa wote Imam Abu Hanifa na Imam Malik. Aidha, wote hawa walisomeshwa pia na "Tabii" mashuhuri Muhammad bin al-Mukadir al-Madani.

Imam Abu Hanifah pamoja na utu uzima wake, alikuwa akihudhuria darasa hasa la Hadith la Imam Malik. Imam Shafii pia alisoma kwa Imam Malik. Kwa ujumla Maimamu wote wanne walihusiana sana katika kusoma kwao na japo walitofautiana katika maoni juu ya mambo kadhaa, walikuwa wamoja katika Uislamu na wakiheshimiana.

Hivi leo wapo watu wanaojinasibisha na madhehebu ambao hudai yapo madhehebu manne ndani ya Sunni wal-Jamaa, kila madhehebu ikinasibishwa na mmoja wa Maimamu hao wanne. Na japo haisemwi wazi wazi, lakini zipo hisia kwa mfano wanaojiita Shafii kuwaona wale wa Hambal, Hanafi na Malik kuwa hawapo sawa. Pengine na kinyume chake. Lakini hakika ya mambo na ushahidi wa vitabu vya historia haioneshi popote mabwana hawa kuhusika na fikra hizi za kuwa na madhehebu yasiyochanganyika. Kazi yao kubwa waliyofanya ni kutoa ufafanuzi wa kifiqh juu ya mas'ala mbalimbali na sio kuwagawa Waislamu kwenye madhehebu. Katika Uislamu suala la madhehebu ni uzushi. Labda ni vyema tuangalie kwa ufupi maisha na mchango wa kila Imam katika kuhuisha Uislamu.

## **Imam Abu Hanifah**

Imam Abu Hanifah ndiye anayenasibishwa na madh'hab ya Hanafi. Jina lake kamili ni **Nu'man bin Thabit Abu Hanifah**. Imam Abu Hanifah alizaliwa Kufa, Iraq katika mwaka wa 80 baada ya Hijrah. Yeye ni katika watu wa kipindi cha Tabiin kwani aliwashuhudia maswahaba wa Mtume ikiwa ni pamoja na Khalifa bin Abu Taalib, Anas bin Malik na Sahl bin Sa'd. Alipata elimu katika miji ya Kufa na Basra kisha Makka na Madinah. Miongoni

mwa waalimu wake alikuwa Abdallah bin Umar mtoto wa Khalifa Umar bin Khattaab. Pamoja na kujikusanyia elimu nyingi na umaarufu kutokana na elimu na ucha Mungu wake; Imam Abu Hanifah alibakia kuwa mnyenyekevu na mwenye msimamo usiotetereka.

Mwaka 146 A.H Khalifah Mansur alimteua Abu Hanifah awe Kadhi; lakini alikataa akitoa hoja kuwa nafasi hiyo ni nzito kuliko uwezo wake. Mansur alikasirika na kumwambia Imam Abu Hanifah kuwa ni mwongo. Imam Abu Hanifah alimjibu, “kama mimi ni mwongo basi kauli yangu kuwa safai ni sahihi kwani mwongo hawezi kuchaguliwa kuwa Kadhi”. Mansur alikasirika zaidi na kumtupa gerezani Imam Abu Hanifah.

Hata hivyo, kutokana na vilio vya watu ilibidi Mansur aruhusu Imam Abu Hanifah aendeshe darsa hapo hapo jela. Lakini alivyoona watu wanazidi kufurika jela kuhudhuria darsa, alimpa sumu Abu Hanifah akafa katika mwezi wa Rajab 150 A.H., miaka kumi na nane (18) tangu Abbasids kushika mamlaka.

Jeneza lake liliswaliwa mara sita na kila mara watu zaidi ya hamsini elfu walisimama kumswalia. Na hata baada ya kuzikwa watu toka sehemu mbalimbali duniani walifurika kuja kuswali swala ya jeneza.

## **Imam Malik bin Anas**

Kwa mujibu wa “Kitab al-Ansab na Dhahabi, Tadhkirah al-Huffaz” juzuu ya kwanza, Imam Malik alizaliwa mwaka 93 A.H. Baadhi ya vitabu vimetaja pia mwaka 94 na 95 A.H. Wazazi wa Imam Malik walitoka katika familia ya kifalme ya Kiarabu toka Yemen ambayo iliamia Madinah. Wakati anazaliwa Imam Malik dola ya Kiislamu ilikuwa chini ya uongozi wa Khalifa Walid bin Abd-al-Malik na japo makao makuu ya dola yalikuwa yamehamishiwa Damascus, Syria, lakini mji wa Madinah ulibakia mashuhuri na

kitovu cha elimu ya Uislamu. Familia ya Imam Malik ilizungukwa na ndugu na jamaa wa karibu waliokuwa na elimu ya kutosha. Hivyo alianza kupata elimu yake katika mazingira ya nyumbani. Zaidi ya hapo alisoma kwa waalimu wengine saba mashuhuri wa fani mbalimbali, miongoni mwao alikuwa Jafar al-Sadiq, kitukuu cha Imam Hussein. Pamoja na kujikusanyia elimu nyingi, umaarufu wa Imam Malik ulizidi kuvuma kutokana na unyenyekevu na ucha Mungu wake. Watu walitoka masafa ya mbali kuja Madina kuhudhuria darsa za Imam Malik.

Sehemu kubwa ya muda wake aliitoa kwa kufundisha na akiifurahia kazi hii. Japo Imam Malik alikuwa mtaalam mzuri wa Hadith, lakini alikuwa dhaifu kidogo katika mambo ya sheria na kutoa fa-twa za kifiqh. Hata hivyo alikuwa mtu madhubuti na mwenye msimamo. Hakukubali kutolewa katika haki kwa hali yoyote iwayo. Wakati fulani alitoa fa'twa ambayo ilikuwa kinyume na matakwa ya Gavana wa Madinah. Gavana alimuonya asitoe fa'twa hiyo hadharani, lakini kwa kuridhika kuwa ndio haki, Imam Malik alitoa maoni yake hadharani na akachapwa viboko hadharani kwa tendo hilo. Katika kazi muhimu alizoziacha Imam Malik ni kitabu chake **al-Muwatta** chenye mjumuiko wa Hadith na mafundisho ya Mtume(s.a.w) ya ibada na mas'ala mbalimbali ya Kiislamu. Imam Malik alitawafu mwaka 179A.H.Madinah.

## **Imam Muhammad Idris al-Shafii**

Imam Shafii alizaliwa mwaka (150 A.D.) huko Gaza katika ukanda wa Pwani ya bahari ya Meditteranean. Yeye ni wa kabila la Quraysh. Akiwa bado kijana, Imam Shafii alihifadhi Qur'an na Kitabu cha Imam Malik, al-Muwata. Alisoma elimu ya sheria ya Kiislamu toka kwa mwanachuoni mashuhuri na Mufti wa Makka Muslim bin Khalid al-Zanji. Baada ya kifo cha Khalid, alikwenda Madinah ambapo alisoma kwa Imam Malik bin Anas. Wakati Imam Malik anafariki tayari Imam Shafii alikuwa ashavuma ndani ya Arabuni na kwingineko kwa ujuzi wake wa elimu ya sheria na Uislamu kwa ujumla.

Kutokana na elimu na uadilifu wake, Imam Shafii aliteuliwa kufanya kazi Serikalini. Hata hivyo hakudumu kwani kwa uadilifu na utendaji wake wa kazi kwa haki aligongana na wakuu wa Serikali wasiotaka haki. Alikamatwa na kuhamishiwa Iraq akiwa amefungwa minyororo kwa tuhuma kuwa anafanya uchochezi dhidi ya Serikali. Huo ulikuwa mwaka 187 A.H. (803 A.D.) wakati wa utawala wa Harun al-Rashid. Baadae aliachiwa huru kwa kuonekana hana hatia. Alibaki kwa muda Baghdad akisoma chini ya wanafunzi wa Imam Abu Hanifah. Alifanya kazi ya kudarasisha Makka na akapata wasikilizaji wengi akiwemo Imam Ahmad bin Hambal ambaye wakati huo alikuwa anasoma Makka. Pamoja na kuwa alikuwa na maoni ya kifiqh tofauti na yale ya Imam Malik na Abu Hanafi, aliwaheshimu na kuthamini juhudi na michango yao. Hakujenga kundi la Shafii dhidi ya Maimamu wengine kama ambavyo baadhi ya Masheikh hufanya hivi leo.

Maimamu ambao tunajinasibisha nao hivi leo wao walikuwa wamoja katika Uislamu. Pale walipokuwa na maoni tofauti katika ufahamu wa baadhi ya mambo walikubaliana kutofautiana, wakazikubali tofauti zao, lakini walibaki kuwa wamoja walioshikamana katika kamba (dini) ya Allah(s.w).

Kazi kubwa ya kufundisha na uandishi, Imam Shafii aliifanyia Misri katika mji wa Cairo ya leo. Huko alizungukwa na wanafunzi na wanachuoni toka sehemu mbalimbali. Walijifunza na kuandika kila alichosema. Imam Shafii alikuwa na kawaida ya kuwaamrisha wanafunzi wake kusoma kwa sauti kila walichoandika ili apate kusahihisha. Kazi kubwa muhimu za Imam Shafii ambazo zinaendelea kutoa mchango mkubwa katika elimu ya Fiqh na sheria ya Kiislamu mpaka hivi leo ni **Kitab al-Umm** na **Kitab al-Risalah Fi-Usul-al Fiqh** (al-Risalah). Imam Shafii alifariki na kuzikwa Cairo mwezi Rajabu mwaka 204 A.H/201/820 A.D.

## Imam Ahmad bin Muhammad bin Hambal

**Imam Abu Abdallah Ahmad bin Muhammad bin Hambal** alizaliwa huko Marwa mwezi 20 Rabi-al-Awwal 164 A.H. Baba yake Muhammad alikuwa mujahid aliyesifika wakati akiishi Basra, Iraq. Baba yake alihamia Baghdad ambapo alifariki muda mfupi baadae na kumuacha Ahmad bin Muhammad akiwa bado mchanga. Pamoja na uyatima wake, kijana Ahmad alikuwa mwenye akili na akautumia ujana wake wote katika kujielimisha. Alisoma zaidi Hadith na akawa mwanasheria na mtaalam wa fiqh katika zama zake. Kwa hiyo Imam Shafii na Imam Ahmad Hambal walikuwa karibu sana. Imam Hambal alimheshimu mwalimu wake Shafii, na Imam Shafii alimheshimu mwanafunzi wake mashuhuri Hambal.

Imam Ahmad Hambal alikuwa mwanachuoni Mcha Mungu sana aliyejitoa maisha yake yote kusoma na kufundisha Hadith na Fiqh. Kwa ucha Mungu wake alikataa kufanya kazi Serikalini, kwani aliona Serikali ilikuwa haiongozwi kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah. Zaidi ya hivyo alivunja uhusiano wa karibu na wote wale waliokubali kuwa ndani ya Serikali ya kidhalimu. Alikataa hata kupokea fedha au chakula kutoka kwa mtoto wake ambaye alikuwa akifanya kazi katika Serikali ile ya kidhalimu. Hata wakati alipokabiliwa na hali ngumu ya uchumi hakukubali kupokea msaada wowote ila kwa kuufanyia kazi.

Katika kipindi cha uhai wa Imam Ahmad waliibuka wanafalsafa waliokuja na falsafa iliyoitwa **Mu'tazili**. Falsafa hii iliwaita watu wawe huria katika fikra. Walichanganya imani na kufr hata kufikia kuleta hoja kuwa Qur'an imetengenezwa tu. Harakati hizi za kuleta kufr ndani ya Uislamu zilitokana na athari ya falsafa za Wagiriki zilizowalevya baadhi ya Waislamu wa zama hizo.

Bahati mbaya watawala wa zama hizo nao waliathiriwa na falsafa hizo za Kigiriki na wakataka kuifanya kuwa imani rasmi ya dola ya Kiislamu. Viongozi waliotaka kuisimika imani hiyo ni Khalifa Ma'mun al-Rashid; Mu'taslim Billah na Al-Wathiq. Imam Ahmad bin

Hambal alikataa kuikubali imani hiyo mpya ya watawala na akaendesha harakati kuipinga. Mtaawala Mu'taslim alitoa amri akamatwe afungwe minyororo na kuhamishiwa Tarsus toka Baghdad. Huko alitupwa gerezani na kuteswa sana mpaka viungo vyake vingi vikavunjika. Imam Ahmad aliachwa adumu amefungwa minyororo mizito ndani ya chumba chenye giza gerezani. Pamoja na kuteswa sana ikiwa ni pamoja na kuchapwa mpaka kutoka damu, Imam Ahmad hakutetereka katika msimamo wake. Msimamo huu wa Imam Ahmad ulimstua Khalifa Mu'taslim. Aliikumbuka Akhera akahofia khatima yake. Aliamuru Imam Ahmad atolewe gerezani mwezi 25 Ramadhan mwaka 221 A.H na akamuomba msamaha, Imam Ahmad akamsamehe.

Miongoni mwa kazi muhimu alizofanya Imam Ahmad ni kuandika vitabu vifuatavyo: Kitab al-Amal al-Tafsir; **Kitab al-Nasikh wal-Mansukh** na kadhalika. Lakini kazi muhimu zaidi aliyoiacha Imam Ahmad ni ukusanyaji wa Hadith elfu nyingi na kuandika kitabu cha Hadith cha **Musnad ya Ibn Hambali**. Ulipofika mwaka wa 241 A.H Imam Ahmad alifariki dunia. Maelfu ya watu wa Baghdad walifurika kumzika.

### **Hitimisho**

Maimamu wote wanne walikuwa wanachuoni wacha Mungu na waadilifu katika zama zao. Walifanya juhudi kubwa kusoma na kufanya ijtihada ya kutafsiri na kutoa maoni yao juu ya sheria na masuala mbalimbali ya Fiqh. Ni vizuri tunufaike na matunda ya juhudi zao, lakini tusigawike wala kubaguana kutokana na maoni tofauti ya Maimamu hao juu ya masuala mbalimbali. Wao wenyewe walisoma pamoja au kusomesha na wakaheshimiana na wakaafikiana kutofautiana katika mambo ya msingi bila ya kugombana.

Jambo jingine la msingi la kuzingatia ni kuwa Maimamu hawa walipata mateso makubwa kutokana na misimamo na juhudi zao katika kuuhuisha na kuusimamisha Uislamu katika

jamii. Walichapwa viboko, walifungwa gerezani na kufungwa minyororo na watawala madhalimu. Zaidi ya hivyo hawakukubali kununuliwa na Serikali. Walikataa kabisa kuwa vibaraka wa Serikali. Je, wakati tunafuata Fiqh na Fat'wa zao tunao pia uadilifu kama wao? Misimamo yetu juu ya Serikali za kidhalimu ni kama wao? Je, hatununuliwi na Serikali na kuifanyia kazi kinyume na maslahi ya Uislamu? Je, tupo tayari kufungwa na kuchapwa viboko kwa ajili ya kusimamisha haki kama Imam Abu Hanifa, Malik, Shafii na Hambal?

## **Zoezi la 5**

1. 'Umar bin Abdul-Aziz ameitwa 'Umar wa pili au Khalifa wa Tano wa Mtume(s.a.w). Jadili.
2. Tunajifunza nini kutokana na Historia ya 'Umar ibn Abdul-Aziz?
3. Bainisha maimamu wanne wa Fiqh wa wakati wa Tabiin na mchango wa kila mmoja katika kuhuisha Uislamu katika jamii yake.
4. Kwa kuzingatia wasifu wa maimamu wanne wa fiqh na ushirikiano wao katika kusoma na kusomesha tunajifunza nini juu ya suala la madhahabi waliyonasibishwa nayo?
5. Kwa kurejea historia ya maimamu wanne wa fiqh una maoni gani juu ya madha-hab manne yanayofuatwa na baadhi ya waislamu ?





## *Sura ya Sita*

# KUHUISHA UISLAMU WAKATI WA TABII TABIINA

### Utangulizi

Tabii Tabiina ni wafuasi wa Tabiin au wafuasi wa wajukuu wa maswahaba.

Wanazuoni katika kipindi cha Tabiina, wakiwemo maimamu wanne wa Fiq-h, walijitahidi sana kukusanya Hadith za Mtume (s.a.w) lakini kazi zao hazikuweza kukidhi mahitaji yote ya kuendea kila kipengele cha maisha ya kibinafsi na kijamii. Kwa mfano kitabu cha Imamu Malik, **Al-muwatta**, kilichokuwa mashuhuri sana katika enzi hizo kiligusia baadhi ya mambo tu yakiwemo yale ya Ibada maalumu za swala, swaumu, Zakat na Hija. Pamoja na mapungufu haya pia iligundulika kuwa katika kipindi cha Tabiina zilizushwa Hadith za uwongo maelfu kwa maelfu.

Katika kupunguza mapungufu haya wanazuoni katika kipindi cha Tabii Tabiin walijishughulisha sana na kukusanya na kuandika Hadith kuhusu nyanja zote za maisha ya muiislamu. Pia ili kuhakikisha usahihi wa Hadith walizozikusanya na kuziandika walichukua tahadhari kubwa sana katika kuzichuja. Katika kipindi hiki walitokea maimamu mashuhuri sita waliojitahidi na kutumia sehemu kubwa ya maisha yao katika kukusanya, kuchuja na kuandika Hadith. Maimamu hawa ni: **Bukhari, Muslim, Abu Daud, Nasai, Ibn Majaha na Tirmidh**. Walisafiri masafa marefu kwa ajili ya kazi hii ya ukusanyaji Hadith na ilibidi wajifunze tabia ya wapokezi kadhaa wa Hadith kabla hawajaiandika. Sio kila Hadith waliyoambiwa waliiandika bali kulikuwa na utaratibu wa kuchambua Hadith iliyo sahihi na isiyo sahihi kwa kuzingatia tabia za wasimulizi na vigezo vya matini ya Hadith. Kutokana na jitihada

zao za uchujaji wa Hadith, vitabu vyao vilijulikana kwa jina la “Sitta Sahihi”. Kila Imamu wa Hadith alivyozidi kuwa muangalifu katika uchujaji wa Hadith zake alizozikusanya ndivyo kitabu chake kilivyopewa daraja ya juu ya usahihi. Vitabu sita mashuhuri vya Hadith sahihi vilivyoandikwa na maimamu hao ni:

## **Sahihi al-Bukhari**

Sahihi al-Bukhari ni kitabu cha **Muhammad bin Isma'il Abu 'Abdallah al'Ju'fi** anayejulikana kwa jina la "**Imamu al-Bukhari.**" Alizaliwa 13 Shawwal, 194 A.H./21 Julai, 810 A.D. katika mji wa Bukhara huko Urusi, na alifariki 30 Ramadhan, 256 A.H./31 Agosti 870 .D.

Hamu yake ya kuhifadhi Hadith aliipata bado akiwa mtoto wa umri wa miaka kumi na moja. Alipofikia umri wa miaka kumi na sita alikwenda kuhiji Makka na kubakia humo humo kujifunza Hadith kwa wanazuoni mbali mbali. Baada ya kutoka Makka alikwenda Misr kisha Basra na sehemu nyingine za Asia ambapo alitembea huku na huko katika kujifunza na kukusanya Hadith kwa muda wa miaka kumi na sita.

Kazi yake ya miaka kumi na sita inaonekana katika kitabu chake mashuhuri kijulikanacho kwa jina la "**Al-Jami'u al-Sahih au Sahihi al-Bukhari**". Kitabu hiki ndio kitabu cha kwanza cha Hadith kinachotemgemewa na Umma wa Waislamu baada ya Qur-an, kwa sababu ya uangalifu mkubwa uliochukuliwa na Imamu Bukhari katika ukusanyaji na uchambuzi wa Hadith zake. Jumla ya Hadith alizokusanya ni 600,000 na katika hizo alihifadhi Hadith 200,000. Lakini kutokana na uangalifu na tahadhari kubwa aliyoichukua katika kuhakiki usahihi wa Hadith alizozipokea, ni Hadith 7,275 tu zilizotokea katika kitabu cha **Sahihi al-Bukhari**. Kabla hajaikubali Hadith kuwa ni sahihi, ilibidi kwanza achunguze historia ya maisha ya kila mpokeaji wa Hadith hiyo kutokea kwa Mtume(s.a.w) mpaka kumfikia.

Imamu Bukhari amezipanga Hadith katika kitabu chake kufuatana na mada za fiq-h. Ameigawanya kazi yake katika juzuu tisini na saba na katika milango (sura) 3,450.

## **Sahihi Muslim**

Sahihi Muslim ni kitabu cha Hadith sahihi kinachofuatia sahihi al-Bukhari kilichokusanywa na **Abul Husain Muslim bin al-Hajjaj** anayejulikana kwa jina la **Imamu Muslim**. Imamu Muslim alizaliwa katika mji wa Misabur, 202 A.H./817 A.D. na alifariki 261 A.H./875 A.D. katika mji huo huo. Kama alivyokuwa Imamu Bukhar, naye alisafiri sana huku na huko katika nchi za Uarabuni, Misr, Syria (Sham) na Iraq ambapo alipata fursa ya kusoma kwa wanazuoni wengi waliokuwa mashuhuri. Miongoni mwa wanazuoni mashuhuri ambao alisoma kwao ni Ahmad bin Hambal, mwanafunzi wa Imam Shafii.

Imam Muslim alikusanya Hadith 300,000 na katika hizo ni Hadith 9,200 tu alizoziandika katika kitabu chake kinachojulikana kwa jina mashuhuri "**Sahihi Muslim**". Alimpenda sana Imam Bukhari na kazi yake. Kama imam Bukhari, Muslim naye amekifuma kitabu chake kulingana na mada za fiq-h. Naye alichukua uangalifu mkubwa mno katika kuchagua Hadith zilizo sahihi kwa kiasi ambacho Hadith zake nyingi zimeku baliana na zile za Al-Bukhari. Alikuwa mwangalifu sana katika kuchambua sehemu ya upokezi (isnad) kwa kiasi ambacho Hadith moja ilikuwa na isnad nyingi (misururu mingi ya wapokeaji). Kwa msomaji, Sahihi Muslim imekuwa katika mpango mzuri zaidi kuliko ule wa Sahihi al-Bukhari.

## **Sunnan Abu Daud**

Sunnan Abu Daud ni kitabu cha Hadith cha Abu Daud. Imamu Abu Daud alizaliwa 203 A.H. na akafiriki 275 A.H. Elimu yake ya mwanzo aliipata Khurasan. Alisafiri sehemu mbali mbali ambazo

zilikwa mashuhuri kwa kuwa na wanazuoni wa Hadith. Ni miongoni mwa wanafunzi wa Imam Ahmad bin Hambali. Alikusanya Hadith 500,000 na alizoziandika katika kitabu chake cha Hadith kinachojulikana kwa jina la "**Sunnan**" ni Hadith 48,000 tu.

Japo hakuwa mkali sana katika uchambuzi na uhakiki wa Hadith zake kama walivyokuwa Bukhari na Muslim, Sunan yake imekuwa ni kitabu cha Hadith mashuhuri sana kwa Umma wa Kiislamu na imeshika daraja la 2 kwa usahihi baada ya sahihi mbili. Hapana shaka kitabu hiki kimejaza mapengo ya mambo yale ambayo hayakugusiwa na Imam Bukhari na Imamu Muslim. Pia Abu Dawud naye alipanga Hadith zake kulingana na vichwa vya habari vya mada mbali mbali.

### **Jami'u at-Tirmidh**

**Abu Isa Muhammad bin 'Issa bin Sarwa bin Shaddad** anayejulikana kwa jina la at-Tirmidh. Alisoma kwa Imamu Bukhari, Ahmad bin Hambali na Abu Daud al-Sijistani. Alizaliwa katika mji wa Tirmidh mnamo 209 A.H. na akafariki mwaka wa 279 A.H.

**Imamu Tirmidh** alikuwa mwanazuoni mkubwa. Pamoja na kitabu chake cha Hadith aliandika vitabu vingine vya Sharia na Tarekh. Alisafiri sana katika kukusanya Hadith katika nchi za Khurasan, Iraq na Hijaz.

Kitabu chake cha Hadith kinachojulikana kwa jina la **Jami'u** kimemfanya kuwa maarufu sana. Alikuwa mwanazuoni wa kwanza kuchambua Hadith kutokana na majina ya wasimulizi. Alizingatia majina yao, majina yao ya ukoo, majina ya utani, n.k. Jami'u ina Hadith chache zaidi ukilinganisha na **Sahihi Bukhari** na **Sahihi Muslim**.

## **Sunnan Ibn Majah**

Sunnan Ibn Majah ni miongoni mwa vitabu sita vya Hadith sahihi kilichoandikwa na **Muhammad bin Yazid** anayejulikana kwa jina la Ibn Majah aliyezaliwa 209 A.H. na akafariki 295 A.H. Katika kukusanya Hadith alisafiri nchi mbali mbali palimokuwa na vituo vya elimu kama Basra, Kufa, Baghdad, Makka, Syria (Sham) na Misr.

Kitabu chake cha Hadith kinachojulikana kwa jina la "**Sunnan**" kimejishughulisha na Hadith zinazohusu sharia zinazoonyesha halali na haramu. Katika uchambuzi wa Hadith sahihi hakuwa makini sana kama walivyokuwa Maimam wawili wa mwanzo. Hivyo Hadith zake zimewekwa kwenye daraja la pili la usahihi. Hadith za daraja la kwanza ni Hadith za Bukhari na Muslim.

## **Sunan ya an-Nasai**

An-Nasai ambaye jina lake kamili ni **Abu 'Abdur-Rahman Ahmad bin an-Nasai** alizaliwa katika mwaka 214 A.H na kufariki 303 A.H./315 A.D. An-Nasai alikuwa mwanafunzi wa Abu Dawud na Hadith za kitabu chake kinachojulikana kwa jina la "**Sunnan**" amezipanga katika muundo alioutumia mwalimu wake. Kazi ya an-Nasai katika ukusanyaji Hadith imekuwa ni kazi muhimu sana kwa Uma wa Kiislamu lakini kwa kuwa hakuwa mwangalifu sana katika uchujaji wa Hadith sahihi, kazi yake imeangukia katika kundi la Hadith za daraja la pili. Baadhi ya Hadith za kitabu hiki ni dhaifu na zenye kutiliwa mashaka zilizo simuliwa na watu wanaotiliwa mashaka.

## **Zoezi la 6**

1. Onesha tofauti kubwa mbili(2) ya vitabu vya Hadith vilivyoandikwa na maimu wa Tabiina na vile vitabu Sitta Sahihi vilivyoandikwa na maimumu wa Hadith wa Tabii Tabiin.
2. Katika vitabu “Sitta Sahihi” vimegawanyika kwenye daraja la kwanza na la pili. Pambanua vitabu vya daraja la kwanza na vile vya daraja la pili.
3. Kwanini maimamu wa Hadith katika kipindi cha Tabii Tabiina walichukua tahadahri kubwa katika ukusanyaji wa uchujaji Hadith ?
4. Vigezo vipi maimamu wa Hadith katika kipindi cha Tabii Tabiina walivitumia katika kuhakiki Hadith?



## *Sura ya Saba*

### KUHUISHA UISLAMU KATIKA KARNE YA 20 A.D

#### **Utangulizi**

Katika sura hii tutapitia harakati za baadhi ya vikundi mashuhuri vilivyojitahidi kuhuisha Uislamu katika karne ya 20 A.D. ambapo nchi nyingi za Waislamu zilikuwa chini ya ukoloni wa Wakristo wa Ulaya Magharibi zikiongozwa na Magavana au vibaraka wao. Vikundi vinne (4) mashuhuri vya harakati za kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii vilivyojitokeza katika karne ya 20 A.D ni:

- 1) Kikundi cha Badee – U-Zaman Said Nursi wa Uturuki.
- 2) “Ikhwan Muslimiin” kilichoasisiwa na Hassan al-Banna wa Misri.
- 3) “Ikhwani Muslimiin” kilichoasisiwa na Hassan al-Turabi wa Sudan.
- 4) Jama’atil Islamy kilichoasisiwa na Abul A’la Maududi wa Pakistan.

#### **Badee – U-Zaman Said Nursi**

Imekuwa ni ada ya historia kwamba kila baada ya kipindi fulani hutokea muhuishaji (Mujadid) wa harakati za Kiislamu. Kama hivyo ndivyo; basi hapana shaka **Badee-U-Zaman Said Nursi** wa Uturuki alikuwa Mujadid aliyekuja kupambana na maovu ya utawala dhalimu wa Mustafa Kamal Atatürk. Pamoja na vipingamizi vingi bado wafuasi wa Badee-U-Zaman wanafanya juhudi kubwa kuuhuisha Uislamu hivi leo kupitia program mbali

mbali. Badee-U-Zaman ni Mkurd aliyezaliwa huko Hizan jimbo la Bitlis Uturuki mwaka 1873. Ujana wake alikutumia kikamilifu katika kutafuta elimu. Awali, alisoma Qur-an, Sheria, Falsafa, Historia na Geografia. Baadaye aliona umuhimu wa kusoma Sayansi asilia. Kwa hiyo akasoma Hisabati, Baolojia na Lugha kadhaa za kigeni. Maisha yake yalikuwa rahisi na ya uadilifu. Qur-an na Sunnah vilikuwa ndio dira ya kila jambo lake. Alikuwa tayari kubaki njaa kama alikuwa na wasi wasi juu ya uhalali wa chakula kilicho mbele yake. Ilikuwa kawaida yake kuwapa chakula sisimizi na alipoulizwa kwanini anafanya hivyo alijibu kuwa ile ilikuwa zawadi yake kwa moyo wa kidemokrasia na utaratibu mzuri wa kazi wa wadudu hao wadogo.

## Mwanzo wa Harakati Zake

Siku moja Badee-U-Zaman alishtushwa na kauli ya Muingereza aliyekuwa Waziri wa Makoloni aliposema: ***“Muda wa kuwa Waislamu wanayo Qur-an basi watakuwa kikwazo kwetu. Kwa hiyo ni lazima tuiondoe kutoka maishani mwao.”*** Kutoka hapo akaamua kupambana bila ya kujali hatari yoyote itakayo mkabili. Alihamia Istambul na kuandaa mipango ya kuanzisha chuo Kikuu cha **Zuhra** mfano wa **al-Azhar**.

Baada ya mapinduzi ya mwaka 1908 ambapo Sultan Abdul Hamid II alipinduliwa: Badee-U-Zaman, alipambana na chama cha kisiasa kilichojulikana kama Kamati ya Umoja na Maendeleo. Chama hiki kilikuwa kimedhibitiwa na majasusi wa Kizayuni (Freemasons).

Katika kupambana na Chama hicho, Badee-U-Zaman, alianzisha Chama cha upinzani alichokiita ***Ittihadil-Muhammad*** kikiwa na malengo ya kuleta Umoja, Uhuru na kusimamisha Uislamu. Aliandika na kusambaza makala ambazo zilielezea malengo na program za chama chake. Aidha aliwaonya Waislamu kuwa endapo watatafuta mwongozo wa maisha zaidi ya Qur-an na Sunnah, basi wajue wanakaribisha maangamizi.



Viongozi wa Kamati ya Umoja na Maendeleo hawakuweza kumvumilia Badee-U-Zaman. Walimkamata mnamo Machi 1909. Kumi na tisa kati ya wafuasi wake wakauawa. Badee-U-Zaman alifikishwa mahakamani. Baada ya hakimu Khurshid Pasha kupitisha hukumu ya kifo kwa wafuasi kumi na tano wa Badee-U-Zaman; alimgeukia na kumuulizia:

*“Wataka pia kutekelezwa kwa sheria ya Kiislamu?” Badee-U-Zaman alijibu; “Endapo ningepewa uhai elfu, ningeutoa muhanga uhai huo kwa furaha, mmoja baada ya mwingine kwa ajili ya Uislamu. Jambo lolote geni katika Uislamu halikubaliki kwangu. Kwa hakika nangojea katika Barzakh kipando kitakacho nipeleka Akhera. Nipo tayari kwa safari ya kuungana na wenzangu ambao wamekwisha epukana na ukatili wako kupitia kitanzi.”*

Badee-U-Zaman alimalizia kwa kusema: *“Utamaduni na mfumo wa maisha ya Ulaya hauwafai watu wa Istambuli. Sifa zote ni zake Allah na ushindi ni kwa Uislamu”*.<sup>46</sup>

Tunapozungumzia mwanaharakati, huyu ndiye mwanaharakati. Tunapozunguzia Mujahidin, hizi ndizo sifa za Mujahidin. Tunapozunguzia subra na uvumilivu, basi kipimio chake ni hiki. Huku ndiko kujitoa muhanga kwa ajili ya Allah (s.w). Mahakama ilimwachia huru Badee-U-zaman kutokana na malalamiko ya wafuasi wake.

Baada ya kukaa kidogo Istambul, alikwenda Damascus, ambapo alitoa nasaha katika misikiti kuelezea matatizo yanayo ukabili Ummah wa kiislamu. Aliyataja matatizo hayo kuwa ni mifarakano ya kijamii na siasa, ubinafsi na kukata tamaa. Tatizo lingine alilolitaja kuwa linatishia Ummah ni kukua kwa tawala za ukandamizaji na kidhalimu.

Aliwahimiza Waarabu na Waturuki wajenge Umoja madhubuti kwani kushinda katika mapambano baina ya Waislamu na makafiri kunategemea sana Umoja wa Waislamu.

Baada ya safari yake ya Damascus alitumia muda wake mwingi kuanzisha Chuo Kikuu ambacho Mitaala na Mihutasari yake ingeweka pamoja mafundisho ya Uislamu na elimu ya Sayansi asilia na Sayansi ya jamii. Hata hivyo kabla lengo lake halijatimia vita kuu ya kwanza ya dunia lililipuka.

Badee-U-Zaman akaingia vitani akiungana na jeshi la Kituruki. Kutokana na ujasiri wake alipewa Uafisa. Katika kambi yake alijenga mazingira ya kufanya Ibada na kusomesha Qur-an. Askari wengi wakawa wanafika kambini kwake kusoma.

Kwa bahati mbaya kikosi chake kilizidiwa sana nguvu na Warusi, ambapo karibu askari wenzake wote waliuawa na yeye mwenyewe kupelekwa mateka Urusi.

Siku moja Generali wa Kirusi; Generali Nicholas alitembelea kambi (jela) yao. Wafungwa wote walisimama na kumpigia saluti isipokuwa Badee-U-Zaman peke yake. Generali Nicholas akamshangaa na kumuuliza endapo anamfahamu yeye ni nani. Badee-U-Zaman alijibu: *“Ndio nakujua u Generali Nicholas Nikolarich. Lakini hiyo si hoja kwangu. Mimi ni Muislamu. Kwangu Muislamu ni bora kuliko kafiri. Namuabudu Allah peke yake. Siwezi kukutukuza.”*

Maneno haya ya kijasiri na pengine yanayoweza kuitwa ya kijeuri yalimfikisha Badee-U-Zaman kwenye mahakama ya kijeshi ambapo alizawadiwa adhabu ya kifo. Aliomba apewe fursa apate rakaa mbili kisha wampige risasi. Baadhi ya marafiki zake wakawa wanamshauri aombe msamaha. Lakini yeye aliwajibu; *“Pengine hukumu hii yaweza kuwa hati (passport) ya kunipeleka peponi.”*

Hatimaye Afande Nicholas alikuja akamuomba msamaha Badee-U-Zaman na kumwambia: “Kwa sababu ya ukweli, imani na ujasiri wako adhabu ya kifo imefutwa”. Baada ya miaka miwili na nusu ya ufungwa na utumwa huko Siberia; Badee-U-Zaman

alitoroka na kuingia Istambul kupitia Petersburg, Warsaw na Vienna. Alipoingia Ankara alipata mapokezi makubwa kutoka kwa maulamaa na watu wa kawaida.

Mwaka 1920 Mustafa Kamal Ataturk alimwalika ahudhurie sherehe za siku ya Uhuru huko Ankara. Bade-U-Zaman alikwenda Ankara. Lakini kwa mshangao hakuona alama yoyote ya Uislamu kwa Mustafa Kamal Ataturk. Akaamua aondoke Ankara bila kuhudhuria sherehe hizo huku akiacha ujumbe kwa bunge la Uturuki lililokuwa likiongozwa na Kamal Pasha. Ujumbe wenyewe ulisema:

*Enyi wabunge! Kumbukeni siku ambapo mtahudhuria mbele ya Allah (s.w), Mfalme wa siku ya malipo. Msiharibu mazuri yaliyopatikana kutokana na kuwashinda maadui toka nje kwa ubaya kutokea ndani. Kama mna hiari kuwaiga wazungu na mifumo isiyokuwa ya Kiislamu; Waislamu watatafuta msaada kutoka watu wengine.*

Ujumbe huu ulisomwa Bungeni na Kazim Pasha na kuleta athari ya ajabu. Wabunge waliowengi walichukua ahadi ya kuanza maisha mapya ya Ucha-Mungu ambapo Swala tano zilipewa umuhimu wa kwanza.

Hali hii iliumuiza sana Mustafa Kamal. Alimwita Badee-U-Zaman na kumshutumua kwanini analeta vurugu kwa kuisitiza umuhimu wa swala. Badee-U-Zaman alimjibu kuwa swala ndio jambo nambari moja katika Uislamu. Kama unaipuuza swala, Umemuasi Mwenyezi Mungu na hivyo basi utawala wako hauwezi kukubaliwa na kutiwa.”

Mustafa Kamal alidhani njia nzuri ya kumnyamazisha ni kumpa wadhifa. Akamchagua kuwa Mhubiri Mkuu wa jimbo la Anatolia na Mjumbe wa Baraza la Utendaji la Chuo Kikuu cha Dar-ul-Hikmat. Pamoja na marupurupu mengine alipewa jumba la

fahari la kuishi. Lakini Badee-U-Zaman alikataa fadhila hizo akakimbilia Ankara ambapo aliendelea na kazi yake ya kuwaelimisha watu.

Haukupita muda Serikali ikamkamata na wafuasi wake. Kwa miaka minane Badee-U-Zaman aliwekwa kizuizini katika jela yenye ulinzi mkali sana. Hata hivyo askari jela waligeuka kuwa wafuasi wake kutokana na ujumbe aliowafikishia.

Akiwa kifungoni huko Burla, Badee-U-Zaman alianza kuandika ujumbe aliouita **Risalat-Nuur** uliopenya kuta za gereza na ulinzi mkali wa askari magereza na kuwafikia watu mitaani. Kila aliyepata nakala; aliinakili upya na kuisambaza kwa wengine. Kwa mtindo huo **Risalat-Nuur** iliwafikia maelfu ya wasomaji.

Baada ya kifungo chake Burla, alielekea Isparta ambapo haukupita muda alikamatwa tena na wafuasi wake 120 kwa tuhuma kuwa amekula njama za kutaka kuipindua Serikali na kwamba anafanya shughuli za kuhubiri na kufundisha Qur-an bila ya kibali cha Serikali wakati kuna idara ya kazi hizo.

Kwa shutuma hii ya kufanya kazi bila ya kibali cha Serikali Badee-U-Zaman aliwajibu kuwa hawezi kuomba kibali cha kumuabudu Mwenyezi Mungu. Kisha akawauliza; “Hivi nyinyi mwaweza kuzuia kifo (watu wasiendeleo kufa) kwa kuyafunga maeneo yote ya makaburi?” Maana yake ni kwamba kama hilo hamliwezi vile vile hamuwezi kuzuia dini ya Allah kwa kuwazuia watu wasihubiri ila kwa vibali vyenu.

Baada ya malumbano makali mahakamani, Badee-U-zama aliachwa huru. Hata hivyo miaka michache baadaye alikamatwa tena na kufikishwa katika mahakama kuu ya Afyon kwa shutuma na madai yale yale ya awali.

Badee-U-Zaman alitoa maelezo marefu katika mahakama kuu ya Afyon na akamalizia kwa kusema:

*“Endapo Qur-an haina wafuasi katika ardhi hii nitahisi mateso makubwa hata kama nitawekwa peponi; lakini kama nitaona imani (ya Kiislamu) ya Waturuki ipo katika salama; nitapata furaha kubwa hata kama kiwiliwili changu kitakuwa kinaunguzwa katika moto”.*

Mahakimu na majaji waliokuwa wanaiendesha kesi hii walisita. Wakamuona Badee-U-Zaman hana hatia na wakageuka kuwa wafuasi wake. Lakini hamu ya dikiteta Mustafa Kamal Ataturk ni kuona harakati za Kiislamu haziendelei. Kesi ilihamishiwa mahakama nyingine ambapo ikawa inapigwa tarehe huku Mujaddid Badee-U-Zaman akiozea rumande.

Miezi miwili kabla ya kifo chake alipata ruhusa maalum akatembelea Ankara kisha Istambul ambapo alipata mapokezi makubwa sana. Maadui wakahisi taabu wakamkamata na kumweka ndani. Katikati ya mwezi wa Ramadhan alipata maradhi ya ghafila. Aliwaomba wafuasi wake wamtoroshe kwa siri hadi Urfa ambapo alifariki mnamo 27 Ramadhan, mwaka 1959 akiwa na umri wa miaka 86.

Baada ya harakati za Kiislamu zilizoandamana na vifungo na mateso mbali mbali kwa ajili ya Allah (s.w), maisha ya Badee-U-Zaman, yalifikia ukingoni akiwa ameteteleza wasia wa aya ifuatayo:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَابْتَغُوا إِلَيْهِ الْوَسِيلَةَ وَجَاهِدُوا فِي

سَبِيلِهِ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٣٥﴾

*Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na tafuteni njia ya kumfikilia (kufikilia Pepo yake). Na piganeni kwa ajili ya dini yake ili mpate kufaulu. (5:35).*

## **Mafunzo:**

Kupitia Maisha na harakati za Badee-U-Zaman tunapata mafunzo makuu yafuatayo:

**(1) Ujasiri na uvumilivu.** Maisha ya Badee-U-Zaman ni kielelezo tosha cha kiwango cha ujasiri na uvumilivu anaotakiwa awe nao Muislamu. Mateso na vitimbi vya madhalimu havikumyumbisha wala kumtoa kwenye lengo.

**(2) Subira na kukamatana na lengo.** Pamoja na ujasiri lipo suala la subira na kudumu katika lengo. Pamoja na mateso na wakati mwingine vishawishi vya kupewa maslahi, Badee-U-Zaman hakutoka katika lengo la kuifundisha na kuisimamisha Qur-an.

**(3) Nafasi ya Elimu.** Pengine jambo lililosaidia sana kufanikiwa Badee-U-Zaman ni kuzingatia kwake umuhimu wa elimu. Yeye binafsi alijielimisha na alipoanza harakati, mkazo mkubwa aliuweka katika kuanzisha taasisi za elimu. Kwa njia hiyo watu wengi walielimika na kulijua lengo.

**(4) Mwenendo mzuri.** Badee-U-Zaman na wafuasi wake walikuwa ni watu wa maadili mazuri ya kuigwa katika jamii. Hakuna mmoja wao aliyekamatwa au kushutumiwa kwa makosa ya kipuuzi au uhalifu dhidi ya sheria za nchi. Muda wote Serikali ilikuwa inapata taabu kufikisha mahakamani tuhuma za kutunga ambapo mahakama nazo zilikuwa zikipata taabu kuzikubali. Mtu unapoingia katika harakati za Kiislamu uangalifuzaidi unatakiwa. Usipatikane mwanya wowote wa mtu kushutumiwa kwa dosari zozote ambazo zaweza kutia doa msimamo na juhudi zake katika dini.

## **Ikhwani Muslimiin wa Misr.**

Ikhwani Muslimiin ni kikundi cha harakati za Kiislamu ambacho kimeenea takriban katika nchi zote za Kiarabu. Harakati za Ikhwani toka kuanzishwa kwake zimelenga katika kuusimamisha Uislamu, ambapo sheria za Allah zitatawala katika kila kipengele cha maisha ya Muislamu kijamii na kwa mtu binafsi. Njia inayotumiwa kufikia lengo hilo ni:

- (a) Kujenga imani madhubuti juu ya Uislamu.
- (b) Mafunzo maalum ya harakati.
- (c) Kazi au utendaji wa kudumu.

Historia ya Ikhwani Muslimiin huanzia mwaka 1906 alipozaliwa muasisi wake – Shahiid Hassan Al-Banna. Yeye alizaliwa katika kijiji cha Mahmudiya na kupata elimu yake mjini Cairo ambapo mwaka 1927 alihitimu na kupata stahhada ya ualimu na kupangiwa kusomesha huko Ismailiya.

Katika kipindi hiki cha historia, wimbi la kuingia na kusambaa kwa utamaduni wa kimagharibi liliathiri sana Misri. Nadharia za kutenganisha Dini na Serikali (secularism), wanawake kwenda nusu uchi, kuenea kwa vishawishi vya zinaa, sinema na maovu mengine vilikuwa vikikita mizizi Misri kwa kasi kubwa. Uislamu ulikuwa ni suala la mtu binafsi na hata kwa ngazi hiyo kwa wengi ulibaki wa kuswali na kufunga tu.

Hali hii ilimuathiri sana Hassan Al-Banna. Alijiona anajukumu la kuuelimisha Ummah na kuuhuisha upya Uislamu. Jitihada zake zilianza kwa kuunda kikundi cha wenye kuamrisha mema na kukatiza maovu. Walielimisha watu, wakachapisha mabango yenye maamrishi na makatazo na wakayabandika misikitini na mitaani.

Kadri Hassan Al-Banna aliyoichambua jamii yake aliona inakwenda kasi kuelekea maangamizi yake kwa kuutupa mfumo wa maisha wa Kiislamu. Katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili aligundua kuwa:

- (1) Mahubiri ya Masheikh misikitini pekee hayatoshi.
- (2) Masheikh walio wengi walishindwa kabisa kupambana na wanaojiita “Secularists”(wasiofuata dini katika mambo yao) na “Modernists (wasomi wa kisasa).”Moderatist” (wanao chukua nusu Uislamu na nusu umagharibi)
- (3) Masheikh walio wengi walinunuliwa kirahisi na Serikali. Kwa kuzingatia haya na hali halisi ya jamii, Hassan Al-Banna alianzisha kundi la harakati za Kiislamu mwaka 1928. Kundi hilo aliliita **Ikhwani Muslimiin** na alianza na wafuasi sita.

Kwa muda kama wa miaka minane hivi jitihada zote zilielekezwa katika kuwaelimisha Waislamu juu ya Uislamu wao kwa njia za darasa, mihadhara, mawaidha misikitini na kwa njia ya maandishi ya vitabu, magazeti,vipeperushi, n.k.. Uangalifu mkubwa sana ulichukuliwa katika kupata wanao harakati. Yaliwekwa mafunzo maalum ambayo ilikuwa ni lazima kila mwana harakati ayapitie.

Harakati zilianza kuyavuta macho ya Serikali mwaka 1936 wakati Hassan Al-Banna alipomwandikia Mfalme na Mawaziri wake kuwa waache tamaduni za Ulaya Magharibi na wafuate Uislamu.

Baada ya kupita kipindi cha mafunzo, wanaharakati wa Ikhwani Muslimiin waliingia katika kipindi kigumu ambapo makucha yote ya Serikali yalielekezwa kwao.



Mwaka 1949 Serikali ilipiga marufuku chama cha Ikhwani Muslimiin, wanachama wakawekwa ndani na mali zao kutaifishwa. Tarehe 12/2/1949 Hassan Al-Banna aliuawa kwa kupigwa risasi.

Kuuawa kwa Hassan Al-Banna hakukusimamisha harakati. Hassan Ismail Hidaybi alishika hatamu za uongozi na mapambano dhidi ya viongozi wasiotaka Uislamu kusimama yakaendelea. Yafaa kusesitiza hapa kuwa wanaharakati wa Ikhwani Muslimiin hawakuwa wanaendesha harakati ili wao wachukuwe madaraka ya kuiongoza Serikali, bali lengo lao ni kuona uovu unaondoshwa katika jamii na Uislamu unasimamishwa na Serikali ya kitwaghati. Maneno yafuatayo ya Rais Jamal Abdul Nasser yanathibitisha mahitaji yao:

*“I met the Supreme Guide of the Muslim Brothers who then made demand on me. The first thing he asked was that we should proclaim that women should wear the veil, He then made other demands such as the closing down of the cinemas and theatres – in other words to make life dark and gloomy. It was of course, impossible to do such a thing”.*<sup>47</sup>

Tafsiri:

*“Nimekutana na kiongozi wa ngazi ya juu wa Ikhwani Muslimiin ambaye alileta madai kwangu. Kitu cha kwanza alichokitaka ni kwamba tuwaamrishe wanawake kuvaa Hijabu. Pia ameleta madai mengine kama vile kufunga majumba ya senema na majumba mengine ya starehe, kwa maana nyingine kuyatia maisha gizani na kuyadodesha. Bila shaka haikuwezekana kufanya kitu kama hicho”.*

Jaribio la kutaka kumuua Jamal Abdul Nasser Desemba 1964 lilitoa mwanya kwa Serikali, ikasingizia kuwa ni Ikhwani waliohusika. Wengi wakafungwa na sita wakahukumiwa kifo.

Rais Nasser aliunda kikosi maalum cha kuwashughulikia Ikhwani. Kikosi hicho kilitoa mapendekezo yafuatayo:

- (1) Somo la Uislamu (Islamiat) liondolewe katika mitaala ya masomo mashuleni. Badala yake utengenezwe mtaala wenye kusisitiza maadili ya Ujamaa.
- (2)Ukomunisti upewe fursa uvunjilie mbali imani za dini na harakati za vikundi vyenye mwelekeo wa Kikomunisti ziruhusiwe na vingine vyote vya Kiislamu vipigwe vita.
- (3) Watu wa dini (Uislamu) hata wale wasiotambulika kama memba wa Ikhwani wapigwe vita.
- (4) Vifungo na adhabu kali ziwaandame Ikhwani na wasipewe muda wa kupumua.

Kutokana na mapendekezo haya mateso makali yaliwaandama Ikhwani.Hassan Ismail Hundaybi aliyeshika uongozi baada ya Hassan Al-Banna alichapwa kwa mnyororo mzito mpaka akafa. Tarehe 29 agosti 1966 viongozi watatu walihukumiwa kunyongwa miongoni mwao akiwemo Mwanachuoni na Mwandishi mashuhuri, Sayyid Qutb. Kaka yake, Muhammad Qutb na dada yake, Amina Qutb, nao walitiwa kifungoni miezi michache kabla ya kuuwawa kwake. Dada yao mwingine Hamida Qutb alihukumiwa kifungo cha miaka 10 na kazi ngumu. Bibi Zainabu Al-Ghazal aliyekuwa Amirat wa Umoja wa Wanawake wa Kiislamu chini ya Ikhwani alikamatwa na kuteswa sana – rejea Kitabu chake – “***Siku katika Maisha yangu***”.

“Hawa ni baadhi tu ya wanaharakati wa Ikhwani Muslimiin na mateso waliyoyapata. Hata hivyo mateso hayo hayakusaidia kitu zaidi ya kuwapa mafunzo na kuwanoa zaidi kiimani wana-Ikhwani kwani harakati mpaka hivi leo zinaendelea. Hii ndio kawaida kama anvayo tukumbusha Allah(s.w):

وَلَمَّا رَأَى الْمُؤْمِنُونَ الْأَحْزَابَ قَالُوا هَذَا مَا وَعَدَنَا اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَصَدَقَ

اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَمَا زَادَهُمْ إِلَّا إِيمَانًا وَتَسْلِيمًا ﴿٣٢﴾

*Na Waumini walipoyaona majeshi (ya makafiri yamewashambulia hivyo), walisema: “Haya ndiyo aliyotuahidi Mwenyezi Mungu na Mtume wake “(kuwa tutapata misuko suko kisha tutashinda). Mwenyezi Mungu na Mtume wake wamesema kweli.” Na (jambo hili) halikuwazidishia ila imani na utii”. (33:22)*

## **Muundo**

Wanaharakati waligawanywa katika daraja tatu kutokana na kiwango cha juhudi na ushupavu waliokuwa nao katika kuendesha harakati hizi za Kiislamu. Palikuwa na:

- Kundi la kwanza (1st class)
- Kundi la pili (2nd class)
- Kundi la tatu (3rd class)

Mwana harakati alipanda daraja baada ya kupitia mafunzo maalum na kula kiapo. Ili kuwadhibiti wanaharakati na kurahisisha ufuatiliaji wa majukumu, wanaharakati waligawanyika katika vitengo(idara) mbali mbali yenye majukumu tofauti. Mfano: Idara ya kushughulikia harakati za wanafunzi, kundi la mambo ya siasa, Idara la mambo ya Usalama na ulinzi, Idara ya mambo ya utamaduni; Idara ya huduma za kijamii na misaada; kundi la elimu na mafunzo; Idara ya uchumi, Idara ya habari na utafiti n.k. Kila mwanaharakati alitakiwa aweke kumbukumbu za utekelezaji wa majukumu yake.

## **Matatizo**

- Kupambana na nguvu za Jahiliya.
- Watu wengi kuteswa na kuuawa.

## ***Mafanikio***

Ikhwani Muslimiin walifanikiwa kuweka msingi madhubuti wa harakati za kuung'oa ujahili. Harakati nyingi ambazo leo hii zinaupigania Uislamu, zina athari ya Ikhwani Muslimiin. Mfano mkubwa ni Sudan.

## **Ikhwani Muslimiin wa Sudan.**

Harakati za Ikhwani Muslimiin ziliingia Sudan katika miaka ya 1950 hivi. Harakati zilianzia Chuo Kikuu cha Khartoum, kisha zilienea kwenye vyuo vingine, mashuleni na sehemu za kazi.

Kimuundo na mbinu, harakati zilichukua sura ile ile ya Ikhwani Muslimiin wa Misr. Wakati harakati hizi zinaingia Sudan, hali ya jamii ilikuwa mbaya sana. Kwani Uislamu ulikuwa ni kitu kilichotupwa na badala yake maadili ya Ulaya Magharibi na “*Umaksists*” vikawa vinashindana kushikilia hatamu za uongozi katika jamii.

Kupiga adhana na kuswali katika Chuo Kikuu kulionekana kiroja, mitaani wanawake walishavua Hijab zao, ulevi, kamari na maovu mengine yalishamiri mno katika jamii.

Katika Chuo Kikuu pamoja na jitihada za kuufundisha Uislamu vilivyo, harakati ziliendesha kampeni dhidi ya ukomunisti. Wanafunzi wanaharakati walisoma historia na nadharia ya Ukomusti wakaelewa vyema. Kisha kwa kutumia hoja toka kwenye Qur-an wakaonyesha udhaifu na upotofu wa Ukomunisti.

Kutokanana jitihada kubwa waliyoifanya kidogo kidogo Uislamu ukawa unaibuka chuo Kikuu na ukomunisti hatimaye ukawa ni kitu cha mtu kuona aibu kunasibishwa nacho.

Mwaka 1963 Dr. Hassan Turabi alirudi toka masomoni Ufaransa na kushika hatamu za uongozi wa haraklati za Kiislamu.

Kuelekea miaka ya 1970 hadi 1973 wanaharakati walipambana na mateso makubwa. Wengi walifungwa na kazi ngumu, kufilisiwa mali, kuishi uhamishoni n.k. Kutokana na matatizo haya uongozi uliangalia upya mbinu za utendaji kazi na wakaamua kubadili mbinu. Badala ya kufanya kazi nje ya serikali wakaona waingie ndani ya Serikali,waibane na kushinikiza kusimamisha Dola ya Kiislamu.

Mbinu hii ilifanyiwa kazi na hadi kufikia mwaka 1980 ikawa wanaharakati wengi wameshaingia katika sehemu nyingi nyeti za serikali. Ikawa serikali haipangi jambo la kuwadhuru wanaharakati ila watapata habari.

Wakati harakati zinaendeshwa kuizingira serikali, wanachi kwa ujumla walielimishwa na kuhamasishwa juu ya umuhimu na ulazima wa kusimamisha Sheria za Kiislamu katika jamii.

Kutokana na mbinu hizi serikali ilijikuta imezingirwa katika vyombo vyake vyote muhimu na wakati huo huo ikawa imenyang'anywa imani ya wananchi. Ni katika hali hii aliye kuwa Rais wa nchi hiyo Jaafar Nimeir, ilibidi atangaze Serikali ya Kiislamu. Wanaharakati walijua vyema kuwa tangazo la Nimeiri ni la kinafiki kwani limetoka wakati maji yamemfika shingoni. Lakini waliona ni vyema waliunge mkono tangazo lake ili wapate kutumia fursa ile na kutumia vyombo vya dola kufanikisha harakati zao.

Baada ya Nimeir kupumua kidogo aliandaa mkakati wa kuwakamata wanaharakati,hasa viongozi na kuwaweka ndani. Hata hivyo baada ya kuwakamata haukupita muda mrefu naye akapinduliwa na wanaharakati wakazidi kupata nguvu.

## **Wanaharakati wa Sudan katika Uwanja wa Siasa**

Kutokana na mabadiliko ya kisiasa yaliyoruhusu kuwapo vyama vingi vya siasa, mwaka 1985 wanaharakati walianzisha chama chao ambacho hujulikana kama National Islamic Front

(N.I.F). Chama hiki kimekuwa maarufu na chenye sauti kubwa katika maongozi ya nchi. Hivi leo Sudan hakiwezi kufanikiwa kuchukua uongozi chama chochote bila ya ridhaa ya NIF.

Serikali ya Saddik Al-Mahd ilijaribu kuwaweka Ikhwan nje ya serikali lakini haikuweza kupiga hatua. Na alipowaingiza ndani ya serikali hakuweza kupitisha lake kama hakupata ridhaa ya NIF.

### ***Matatizo:***

Kama ilivyo mahali popote ambapo pana harakati za Kiislamu, wanaharakati wa Sudan walipambana na makucha ya serikali. Kuna waliouawa, wengi wametumikia vifungo virefu, na wengi wameishi uhamishoni muda mrefu, n.k.

### ***Mafanikio***

Kundi limefanikiwa kuweka msingi madhubuti wa harakati za Kiislamu Sudan. Wamefanikiwa kujiimarisha kiuchumi kwa kuanzisha makampuni makubwa ya biashara na uzalishaji mali ndani na nje ya Sudan. Wamefanikiwa kuendesha mabenki ya Kiislamu. Mabenki haya yana matawi mengi ndani na nje ya Sudan pia. Kwa hiyo utaona kuwa zaidi ya kuwa wanapanga mambo yao kulingana na uwezo wao bila kuomba misaada, wanatoa nafasi za ajira kwa wananchi. Yaani wanajijiri kutokana na makampuni yao ya uzalishaji mali.

### **Jama'atil Islamy ya Pakistan.**

Mwanzishi wa Jumuiya ya Jama'atil-Islamy ni Maulana Sayyid Abul Ala Mauduud aliyezaliwa tarehe 25 Septemba, 1903 huko Aurangabad, Pakistan wakati huo Pakistan ikiwa ni sehemu ya India.

Sehemu kubwa ya elimu ya Mauduud aliipata nyumbani katika madrasa na Masheikh. Hii ni kwa sababu baba yake aliogopa kuwa mtoto wake ataharibika katika shule za kawaida zilizofuata mitaala ya kimagharibi.

Wakati akiwa na miaka kumi na sita, baba yake alifariki. Kwa hiyo, mwaka 1920 alianza kujitegemea kwa kufanya kazi ya uadishi wa habari. Aliyafanyia kazi magazeti ya “Taj” na “al-Jamiat”. Mwaka 1932 alikwenda Hyderabad ambapo alianzisha gazeti lake la kila mwezi lililoitwa “Tarjuman ul-Qur-an”.

Januari 1938 aliitwa na Allama Muhammad Iqbal kwenda Punjab kufanya kazi ya kuihuisha sheria ya Kiislamu. Iqbal alikufa mwaka huo huo mwezi April na Mauduud akahamia Lahore ambapo alichaguliwa kuwa Mkuu wa kitivo cha dini bila ya malipo. Mwaka mmoja baadaye, Serikali ilisisitiza apewe mshahara lakini Mauduud, alikataa kwa kuhofia kuwa wakimlipa watamdhiti katika harakati zake. Kwa hiyo aliacha kazi hiyo na mwaka 1941 akaanzisha rasmi kikundi cha harakati za Kiislamu alichokiita **Jama’atil-Islamy**.

Maulana Mauduud alianza kutambulika umaarufu wake mwaka 1926 baada ya kufafanua kwa kina katika jarida lake nadharia ya Jihad na kuitofautisha na vita vya kawaida.

Mwaka 1932 Mauduud aliandika kitabu maarufu kitiwacho Towards Understanding Islam (Katika kuufahamu Uislamu). Lengo la kuandika kitabu hicho lilikuwa kuwasaidia wasomi kuuelewa Uislamu katika usahihi wake. Mwaka huo huo wa 1932 alianza kuchapisha Tarjuman ul-Qur-an.

Maulana Mauduud alieleza kwamba mpango aliokuwa nao mwaka 1932 alipoanza kuandika Tarjuman ul-Qur-an, ulikuwa kuvunja fikra potofu za Kimagharibi ambazo zilishaingizwa katika bongo za wasomi wa Kislamu. Alitaka kuwaonyesha kuwa Uislamu

ni mfumo kamili na sahihi wa maisha usiohitaji kukopa jambo lolote kutoka mfumo wa kikafiri.

Zilipoanza harakati za Pakistan kujitenga kutoka India ya leo, Mauduud aliziunga mkono. Hata hivyo alionyesha wasi wasi wake kuwa yaelekea harakati hizo hazina msingi madhubuti wa kusimamisha Dola ya Kiislamu Pakistan bali Utaifa tu. Ili kuhakikisha kuwa Paksitan inakuwa dola ya Kiislamu na Waislamu watakaobaki India bado wanabaki Waislamu; Maulana Mauduud aliona kuna ulazima wa kuanzishakundi la harakati, Jama'atil-Islamy. Kwa kujua majukumu na lengo la Jama'atil-Islamy Mauduud alikuwa makini katika kupata wanakundi. Hakutaka kuunda jumuiya ambayo itakuwa wazi kwa kila mtu. Alitaka kundi la watu wenye tabia njema wasiotetereka katika maadili. Alitaka watu walio tayari kujitoa muhanga kwa ajili ya Uislamu.

Baada ya Pakistan kujitenga tarehe 14 Agosti, 1947 Mauduud alizipeleka juhudi zake katika kusimamisha mfumo wa Kiislamu Pakistan. Kati ya Januari na Machi, 1948 alitoa mfululizo wa vipindi katika Redio ambapo aliuchambua mfumo wa Uislamu kwa kuangalia falsafa, maisha ya kiroho, maadili, mfumo wa elimu, uchumi na utamaduni. Kwa kuendesha harakati kuwa Pakistan iongozwe Kiislamu, alishutumiwa kuwa ni adui wa Serikali kwa hiyo akatupwa gerezani toka tarehe 4 Oktoba 1948 hadi 28 Mei, 1950.

Hata hivyo juhudi zake hazikupotea bure, kwani hoja na mapendekezo yake yalipitishwa na bunge mnamo 7 machi, 1949

Kati ya mwaka 1952 na 1953 Waislamu wa Pakistan waliitaka Serikali ipitishie sheria ambayo itatamka wazi kuwa Makadiani sio Waislamu. Serikali ilitangaza sheria ya kijeshi kuzima harakati hizo. Mauduud aliandika makala aliyoiita: "Tatizo la Kadiani" (The Qadiani Problem) kuishutumu Serikali kwa msimamo wake na kuwatumia Makadiani kwa lengo la kuvuuruga Uislamu. Kwakuandika makala hiyo iliyobainisha wazi kwa data kuwa



ukadiani si dhehebu la waislamu bali ni dini iliyeundwa na waingereza ili kuwagawanya waislamu ipate kuwatawala vizuri, ilimgharimu Mauduud kufungwa gerezani bila yakufikishwa Mahakamani na hatimaye kuhukumiwa adhabu ya kifo. Hata hivyo Mauduud aliposikia hukumu hiyo alisema:

*“Kama Mungu amependa ninyongwe, nitaipokea hukumu hiyo kwa furaha; lakini kama si mapenzi ya Mungu nife sasa; kwa vyovyote watakavyofanya, hawatanidhuru hata chembe.”*

Alipotakiwa aombe msamaha ili asamehewe Maulana Mauduud alikataa. Hata hivyo ulimwengu wa Kiislamu ulipiga kelele kupinga hukumu hiyo ya kifo. Hali hiyo ilipelekea hukumu ya kifo kubatilishwa na kuwa kifungo cha miaka 14. Lakini alipofikia tarehe 25 Mei, 1955 aliachiwa huru kwa amri ya Mahakama Kuu.

Mwezi machi 1956 katiba ya Serikali ya Kiislamu ya Paksitan ilipitishwa ambapo mapendekezo mengi ya Jama’atil-Islamy yalikuwemo katika katiba hiyo. Hata hivyo ubaya wa bahati, tarehe 7 Oktoba, 1958 Rais Iskander Hirza alipitisha sheria ya kuivunja katiba hiyo na mwezi huo huo tarehe 27, “Field marshal” Muhammad Ayub Khan akapindua Serikali na kutangaza sheria za kijeshi ambapo vyama vyote vya kisiasa vilipigwa marufuku ikiwemo Jama’atul Islamy.

Pamoja na vikwazo hivyo Mauduud hakukata tamaa. Katika hali hiyo ngumu ya sheria za kijeshi, alikusanya nakala na hotuba zake za kati ya 1939 na 1958 akatoa kitabu alichokiita; Sheria ya Kiislamu na Katiba (Islamic Law and Constitution). Ndani ya kitabu hicho alitoa hoja kuonesha usahihi na utekelezaji wa sharia na Katiba ya Kiislamu katika ulimwengu wa leo. Kutokana na hoja zake katika kikao cha Majaji cha mahakama Kuuu ya Pakistan 17 Februari, 1967, Majaji walieleza matakwa yao, kuona sheria ya Kiislamu inatekelezwa.

Mwaka 1961 Serikali ilipitisha sheria ya familia (the Muslim Family Law Ordinance) ambayo iliweka vikwazo vingi katika kanuni na taratibu za Kiislamu za ndoa na talaka. Maulana Mauduud akiongoza kundi la Maulamaa wapatao 209 alipinga sheria hiyo kwa nguvu zote. Serikali ilikuja juu na kuwaweka ndani baadhi ya Maulamaa.

Katika jumla ya kazi muhimu alizoacha Maulana Mauduud ni tafsiri yake ya Qur-an, tafhimul ul-Qur-an (The meaning of the Qur-an). Kazi hii alianza mwaka 1943 na kuikamilisha Juni 1972. Katika kufanya kazi hiyo ilimbidi kusafiri sehemu mbali mbali kuziona sehemu zote za kihistoria zilizotajwa katika Qur-an.

Zaidi ya kupigania haki ya Pakistan kutawaliwa Kiislamu, Mauduud alipigania pia haki ya jimbo la Kashmir kujitawala, haki ya Wapalestina na kupinga udhalimu wa Israel katika ardhi za Waarabu. Aidha katika vikao muhimu vya Jumuiya za Kimataifa za Kiislamu kama Rabita-al-Alam-al-Islamia, Maulana Mauduud alisisitiza haja ya nchi za Kiislamu kujitegemea kiuchumi na kijamii kuliko kuzitegemea nchi za Magharibi.

Harakati za Maulana Mauduud zimekuwa ni kigezo cha kuuhisha Uislamu katika karne ya Ishirini. Pamoja na kupigania kusimama kwa Dola ya Kiislamu Pakistan; Mauduud alikuwa pia mpinzani mkali wa sera za kimataifa zilizokinyume na mafundisho ya Uislamu.

Mwaka 1962 aliandika kitabu juu ya Uislamu na Udhibiti wa Uzazi (Birth Control) akipinga sera za kitaifa na kimataifa za kidhibiti idadi ya watu kwa kuhofia uhaba wa rasilimali. Kitabu hicho kilipigwa marufuku tarehe 9 Agosti, 1966.

## **Muundo na kazi za Jama'atil-Islamy**

Jama'atil-Islamy huongozwa na Amir akiwa msimamizi mkuu wa katiba na program za Jumuiya. Lipo Baraza Kuu (Central council) ambalo humsaidia na kumchunga Amir katika utendaji wake. Baraza hili pia huweka taratibu za mafunzo, upataji wa wanachama wapya; mipango ya uchumi na kutunza fedha.

Katika kila mji mkubwa lipo tawi la jumuiya ambalo huchagua Amir na Baraza la tawi. Aidha huwa na kamati mbali mbali kushughulikia masuala muhimu.

Vipo pia vikundi vidogo vidogo vya Jumuiya katika kila eneo. Vikundi hivi chini ya Amir wao hukutana mara moja kwa wiki ambapo hufanya darsa maalum na kutoa taarifa za kazi kutoka kwa kila mwanachama. Kila mwanachama anawajibika kuwasilisha ripoti ya kazi zake kwa wiki nzima kwa Amir kabla ya kikao.

Kuhusu mafunzo huandaliwa semina, Itqaf na kambi ambapo zaidi ya kutolewa mafunzo ya Uislamu kwa ujumla; mafunzo maalum juu ya harakati hutolewa. Hii ni pamoja na mbinu, mipango (planning) na uongozi.

Jama'atil-Islamy imeanza kwa kuweka mkazo mkubwa sana katika elimu. Imejenga na kuendesha taasisi za elimu katika viwango mbali mbali. Kutokana na kukua na kuimarika kwa mipango yake ya kiuchumi Jam'at-Islamy hujishughulisha pia na kutoa huduma za kijamii. Hii ni pamoja na huduma za afya, kusaidia wenye njaa na waliofikwa na maafa kama mafuriko, n.k.

### ***Mafanikio***

Katika jumla ya mafanikio makubwa iliyopata Jama'atil-Islamy ni kuwa na utaratibu mzuri wa mafunzo, utendaji na ushirikishwaji wa wanajumuiya katika kazi. Hali hiyo iliwezesha harakati za

Jama'atil-Islamy kudumu hata pale viongozi wakuu wanapowekwa ndani au hata kufariki. Kwa hiyo haikuwa ni jumuiya iliyomtegemea mtu moja. Kwa mfano Maulana Mauduud alijiuzulu uongozi 1972 kutokana na hali yake ya afya kulega lega; Mian Tufail Muhammad akawa Amir na harakati zikaendelea kwa nguvu kama kawaida. Maulana Mauduud alifariki mwaka 1979. Jama'atil-Islamy bado inaendelea na harakati zake ikiwa na tawi la wanafunzi Jama'at-Talabal-Islamy.

### **Matatizo:**

**Kwanza**, kuna migawanyiko mikubwa miongoni mwa Waislamu. Hii imepelekea kuwa na vyama vingi vya kisiasa vinavyodai kusimamia Uislamu. Vyama hivi vimekuwa maadui huku wafuasi wa vyama wakihesimiana na kuitana makafiri.

**Pili**, zipo pia taasisi na Jumuiya nyingi sana za Kiislamu na zote hizo hazifahamiani na kusaidiana. Kila jumuiya huhodhi wafuasi bila kuzingatia umuhimu na ulazima wa kushirikiana na kushikamana kidugu.

**Tatu**, tatizo jingine ni kuwepo kwa madrasa nyingi za kizamani ambazo huzalisha Masheikh vilema wa roho na akili. Madrasa hizo huwadumaza wanafunzi kiasi kwamba wanashindwa kuwa na uoni mpana na kujiendeleza kielimu ili kupambana na hali halisi ya maisha ya ulimwengu wa utandawazi.

Kwa ujumla historia ya Pakistan toka ikiwa sehemu ya India imekumbwa na mgawanyiko mkubwa wa Waislamu katika Twarika za kisufi, madh'hab na jumuiya mbali mbali zenye utii na mshikamano na Masheikh wao kuliko hata Qur-an na maelekezo ya Mtume(s.a.w). Hali hiyo imefanya kazi za Jama'atul-Islamy kuwa ngumu. Hata hivyo harakati zinaendelea.

## **Zoezi la 7**

1. Orodhesha mambo aliyofanya mwanaharakati Badee-u-Zaman katika jitihada zake za kutaka wanajamii wapate haki na amani ya kweli kupitia mfumo wa maisha ya kiislamu
2. Bainisha changamoto aliyokutana nayo Badee-u-Zaman katika harakati za kuhuisha Uislamu.
3. Bainisha wasifu na sifa za waliokuwa waasisi na viongozi wa Ikhwanil Muslimina wa Misr na Sudan.
4. Onesha pingamizi na fursa walizokuwanazo katika Da'awah
  - (a) Ikhwanil -Muslimiina wa Misr
  - (b) Ikhwanil-Muslimiina wa Sudan
5. Eleza kwa muhtasari matunda ya harakati za Ikhwanil - Muslimiina wa Misr na Sudan
6. Toa maelezo mafupi juu ya
  - (a) Maulana Sayyid Abul Ala Mauduud
  - (b) Mafunzo tuyapatayo toka maisha ya Abul Ala Mauduud na Jama'atul Islamy.
7. Taja na kufafanua njia na mbinu za kuhuisha Uislamu, zinazojitokeza kwenye harakati za Badee-U-Zamman, Ikhwanil Muslimiina na Jamaatil Islamy.

## *Sura ya Nane*

### **HISTORIA YA KUHUISHA UISLAMU TANZANIA**

Hapana namna ya kuelewa vizuri harakati za kuhuisha Uislamu Tanzania au kuweka mikakati mizuri ya kuhuisha Uislamu na kuusimamisha katika jamii ya Tanzania, bila kwanza kurejea historia ya kuingia Uislamu Pwani ya Afrika ya Mashariki kisha Tanzania na namna ulivyosoteshwa mpaka kufikia hali hii iliyopo. Pia huna namna ya kutenganisha kupatikana uhuru wa Tanganyika kisha Tanzania na harakati za kuhuisha Uislamu Tanzania.

#### **Historia ya Kuingia Uislamu Afrika ya Mashariki**

Kwa karne nyingi yalikuwepo mahusiano baina ya Pwani ya Afrika ya Mashariki na Asia. Wafanya biashara toka Saudi Arabia, India na nchi za Ghuba, walizitumia pepo za misimu (monsoon winds) kutembelea Afrika ya Mashariki kwa shughuli za kibiashara. Kufikia karne ya 9 na 10 A.D. wahamiaji toka Saudi Arabia walifanya makazi ya mwanzo huko Benadir katika pwani ya Somalia. Kisha ikafuatia miji ya Marca, Moghadishu na Barawa. Katika karne ya 12 A.D. wafanya biashara wengi walihama toka pwani ya Somalia wakaelekea kusini hadi Kilwa, Tanzania. Ni katika kipindi hiki vile vile ambapo wageni wengi kutoka Uajemi (Persia) na Oman walifika Kilwa. Katika karne ya 13 A.D. wageni wengine wengi toka Hadharamaut na Yemen walifika Afrika ya Mashariki.

Alama ya kale ya Uislamu kusini mwa Benadir (Somalia) ni Msikiti wa Kizimkazi Dimbani huko mkoa wa kusini Unguja. Katika msikiti huo lipo jiwe lililojengwa Mihrabu lililoandikwa kwa nakshi za

herufi za kufi ambalo linaeleza kuwa msikiti huo ulijengwa mwaka wa 500 A.H. sawa na 1107 A.D. Wakati huo katika kisiwa cha Unguja Kizimkazi ilikuwa ni njia na bandari muhimu ya kuwasiliana na nchi za nje kama Uajemi (Persia), Saud Arabia na nchi nyingine za Ghuba. Hivyo, msikiti wa Kizimkazi ni uthibitisho usio na wasi wasi kuwa katika kipindi cha mwisho wa karne ya 11 A.D. Zanzibar tayari ilikuwa na Waislamu wengi.

Ibn Batuta alipotembelea Afrika ya Mashariki kwa mara ya pili 1332, miji ya pwani hasa Kilwa, ilikaliwa zaidi na Waislamu. Kutokana na mchanganyiko wa wageni na wenyeji, liliibuka kabila la Waswahili na lugha ya Kiswahili ambayo ni mchanganyiko wa lugha ya Kiarabu na Lugha za wenyeji. Miji ya Tanga, Dar-es-Salaam, Mombasa, Lamu, Malindi na Mikindani ikaibuka na kuwa vituo muhimu vya kueneza Uislamu katika miji mbali mbali ya Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Zaire, Msumbiji, Malawi na Burundi.

Tokea Unguja na Miji ya Pwani misafara ya biashara ya Waarabu na Waswahili iliingia miji ya Bara. Na kila walipofanya makao walijenga misikiti na kusilimisha wenyeji. Kutokana na fursa walizopata Waislamu kufanya biashara na wageni, miji mingi ya Afrika ya Mashariki ilikuja kukaliwa zaidi na Waislamu wakimiliki biashara za maduka, mahoteli, usafirishaji, n.k.

Ukizingatia maelezo haya, utagundua kuwa waliotuletea Uislamu Afrika ya Mashariki hawakuwa (missionaries) waliokuja rasmi kwa lengo hilo. Bali wao walikuja kutafuta maisha na kusilimisha na kufundisha kusoma Qur'an na fiqh ya utekelezaji wa Ibada maalumu ilikuwa jambo la ziada. Hali hii iliathiri sana hali ya Uislamu baadae. Tokea awali haikuwepo azma ya kusimamisha Uislamu Afrika Mashariki. Hapakuwa na program madhubuti za kutoa elimu na mafunzo kwa muelekeo wa kusimamisha Uislamu. Toka zama hizo Uislamu umebakia Afrika ya Mashariki kuwa ni jambo la kiroho la mtu binafsi bila kujali nafasi ya Uislamu katika maisha ya jamii.

Pamoja na upungufu huo; wageni kutoka Ulaya ambao pia ni Wakristo hawakuacha kuonyesha wasi wasi wao hata katika huo Uislamu dhaifu. Wajerumani na Waingereza waliweka mikakati ambayo ilihakikisha Uislamu haupati nguvu na Waislamu wanabaki watu dhalili. Kinyume chake walilipa Kanisa fursa mbali mbali za kuliwezesha kustawi na kushamiri Afrika Mashariki. Mikakati hiyo ilikuja kurithiwa na kuendelezwa na viongozi wa Serikali baada ya Uhuru.

## **Upinzani Dhidi ya Uislamu Afrika ya Mashariki.**

Wamishionari na Wakoloni waliona kuwa Uislamu ni kikwazo kwa ukoloni na utamaduni wao. Waliuona Ukristo na utamaduni wa Ulaya Magharibi kuwa ni pande mbili za sarafu moja. Hivyo mkakati ukawekwa wa kuupiga vita Uislamu hapa Afrika na kuunza Ukristo kama kitangulizi cha kuja kwa wakoloni. Vyama vingi vya makanisa viliundwa Ulaya ili vije vifanye kazi hii Afrika. Chama cha White Fathers ambacho kimefanya kazi kubwa sana hapa Afrika ya Mashariki pia kilianzishwa na Kadinal Lavigire kwa lengo maalumu la kuupiga vita Uislamu na kueneza Ukristo<sup>48</sup> Pia kumbu kumbu za chama cha “Church Missionary Society” za mwaka 1880-81 (uk. 2-3) zinasema wazi kuwa lengo lake ni kuukomboa ulimwengu uepukane na Uislamu. Na H.M. Stanley ameandika kuwa alipotembelea Uganda lengo lake lilikuwa kumfanya Mutesa awache Uislamu na ampokee Yesu Mnazareti.<sup>49</sup>

Katika mkutano wa Berlin wa wakoloni katika kugawana Bara la Afrika mwaka 1884, Ukristo ulipewa upendeleo (hadhi) maalumu. Ibara ya 6 ya makubaliano yao iliagiza kuwa dola zote za kikoloni zitoe hifadhi maalumu kwa makanisa ya Kikristo.<sup>50</sup> Na Bwana Roland Oliver ameandika kuwa huko Ulaya Wazungu walihofia kuwa Afrika ya Mashariki ya Kiislamu itakuwa ni Afrika ya Mashariki dhidi ya Wazungu.<sup>51</sup>



Kutokana na mtizamo huu wa wakoloni kufikia mwaka 1900 na kuendelea iliwekwa sera ya kuhakikisha kuwa Wakristo wanashika nafasi za juu katika Serikali na Waislamu wanashika nafasi za chini kabisa. Kamishina wa Uganda kati ya 1899 -1901, Sir Herry Johnston, alitamka sera hii alipomwandikia D.C. wa Busoga kuhusiana na wasi wasi aliouonesha askofu Tucker juu ya kuenea kwa Uislamu. Sir H. Johnston alisema:

*“Haitakuwa kwa maslahi ya Serikali ya Uingereza iwapo Uislamu utapata wafuasi wengi kwani kwa asili yao Waislamu niwagumu kuwatawala na katika nyoyo zao wanapinga utawala wa dola ya Kikristo.”<sup>52</sup>*

Na akawaonya Machifu wafanye kila njia kuupiga vita Uislamu. Kufikia mwaka 1917 Uislamu ulikuwa umedhoofishwa sana Afrika Mashariki. Lakini pamoja na hayo Wakoloni wakaona bado haitoshi. Wakaweka mkakati wa kuzuia Uislamu usienee kusini mwa Sudan ili Uganda isiathiriwe sana na Uislamu. Waislamu wabakie Pwani ya Kenya na Tanganyika tu. Na wakati huo huo kuzidisha kampeni za kueneza Ukristo. Mkakati huu upo katika nyaraka za Serikali zilizopo Entebbe No. A. 23 na katika Uganda Annual Report, 1900-1.

Hatua nyingine kubwa iliyochukuliwa na wakoloni ilikuwa ni kuzibana juhudi za Waislamu za kueneza Uislamu na kuwabana katika fursa za elimu. Serikali ya Kikoloni huko Uganda kwa mfano ilimzuia Mwalimu wa Kiislamu kutoka India aliyeitwa na Waislamu wa huko kuingia Uganda. Mwaka 1944 Waislamu wa Uganda walipewa Pauni 213 tu kwa ajili ya elimu yao. Wakristo walipewa Pauni 134,000!! Ama kubanwa kwa Waislamu wa Tanganyika kielimu tangu zama hizo hadi leo hakuna haja ya kutolewa maelezo zaidi. Itoshe tu kusema kuwa katika utafiti uliofanywa na Dr. Malekela wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1983 umeonyesha kuwa katika kila watoto 100 wanaosoma sekondari 78 ni Wakristo na 22 ni Wapagani na Waislamu.

## **Mbinu za Kuwaghibu na Kuwaritadisha Waislamu Afrika Mashariki**

Tafsiri ya hatua zote hizo hapo juu ni kwamba Uislamu uliokuja Afrika Mashariki miaka elfu moja iliyopita ukawa unadumaa na Ukristo uliokuja Afrika mashariki miaka mia moja tu iliyopita ukawa unazidi kustawi. Utafiti uliofanywa juu ya siri ya mafanikio ya Wakristo dhidi ya Waislamu umegundua mbinu zilizotumika zifuatazo:

Mbinu na siri ya **kwanza** ni kujenga mahusiano ya karibu na waislamu. Mwanzoni kulikuwa na uhasama wa dhahiri kati ya Waislamu na Wakristo hivyo haikuwezekana kabisa kwa Muislamu kuwa Mkristo. Baadaye Wakristo wakabadili mbinu. Wakajifanya ni marafiki wakubwa wa Waislamu na kuishi pamoja nao kindugu. Waislamu wakaamini na hata kuwasaidia sana katika harakati zao. Sultani Seyyid Said wa Unguja aliwakaribisha Wamishionari Unguja na akawapa barua ya kuwatambulisha iliyosema: “Dk. Krapf, Mjerumani, ni mtu mwema anayetaka kuwalingania watu kwa Mungu. Mfanyieni ihsani na msaidieni kila aendako.”<sup>53</sup>

Hata wale watu waliokuwa na chuki sana dhidi ya Uislamu walipata msaada wa Waislamu. Hali hii yaendelea hadi leo. Utafiti uliofanywa na Wakristo juu ya Waislamu wa Tanzania na kuchapishwa katika kitabu kiitwacho Development and Religion in Tanzania uk. 27 unasema kuwa Waislamu wa Tanzania wanajali zaidi utaifa wao kuliko dini yao. Utawajua kuwa ni Waislamu wakiwa msikitini tu na siyo katika maisha ya jamii ya kila siku. Waislamu wanajali sana kuwa na uhusiano mwema na watu wa dini nyingine. Matokeo ya msimamo huu wa Waislamu ni kuwa Wakristo walipata fursa nzuri ya kuwaritadisha. Takwimu za 1965/6 zilizokusanywa na James D. Holway kwa nchi za Afrika Mashariki ni kama ifuatavyo:

## **Wakristo Waliosilimu**

<i>Tanzania</i>	3104
<i>Uganda</i>	5
<i>Kenya</i>	42
<i>Jumla</i>	3151

## **Waislamu walioritadi**

<i>Tanzania</i>	8741
<i>Uganda</i>	-
<i>Kenya</i>	430
<i>Jumla</i>	9171

**Source: James D. Holway; Mimeo 1965.**

Mtu anaweza kuhoji usahihi wa takwimu hizi. Hata hivyo lililo muhimu ni kuwa Wakristo walikuwa wakifanikiwa zaidi kuliko Waislamu katika kulingania dini yao. Na kutokana na mafanikio hayo ndipo Wakristo wakaamua kuanzisha mradi mkubwa sana wa kuwaritadisha Waislamu wa Afrika uitwao ***Islam in Africa Project*** wenye makao yake makuu huko Nairobi Kenya. Ulianzishwa na Rev. James Jitchie aliyekuwa mshauri wa Baraza la Kikristo la Kenya (The National Christian Council of Kenya). Mwaka 1971 na Rev. Tom Beetham akawa ndiye Mkurugenzi wa Mradi huo. Miongoni mwa Programu zinazoratibiwa na ***Islam in Africa Project*** ni pamoja na ile semina iliyofanyika Nairobi, Kenya Septemba 23, 1989 juu ya kukabiliana na Uislamu, kuandaa November Crusades katika nchi mbali mbali za Afrika n.k. Hii ni mbinu yao kubwa ya mwanzo iliyowapa mafanikio dhidi ya Waislamu wa Afrika Mashariki.

Mbinu na Siri ya **pili** ya mafanikio ya Wakristo ni kuwa wamejitahidi sana kuingia vijijini na kujenga makanisa, mashule na hospitali. Waislamu wengi wameishia mijini. Matokeo yake Wakristo wametapakaa Afrika Mashariki mzima hadi vijijini lakini Waislamu wengi wako mijini. Na huu ni udhaifu mkubwa.

Mbinu na Siri kubwa ya **tatu** ya mafanikio ya Wakristo ni Umoja na mipango madhubuti ya muda mfupi na muda mrefu ya kufikia lengo lao. Ikiwa mtu atazingatia programu zinazoendeshwa na Wakristo kwa upande wa elimu tu peke yake na akatazama matunda yake itamdhihirikia ni kwa kiasi gani Waislamu tulivyo nyuma. Waislamu wa Kenya, Uganda na Tanzania hatuonyeshi kuwa tuna mwelekeo wala mpango wowote wa maana wa kuipigania Dini yetu. Mtu akisoma historia ya Waislamu wa Uganda, jinsi walivyopigwa vita na wakoloni na walivyogombanishwa wao kwa wao na Serikali ya Obote, Idi Amin na ya hivi sasa ya Museveni na wanavyoshitakiana kwa Serikali hiyo hiyo na halafu akatazama historia ya Waislamu wa Tanzania na Kenya atastushwa sana na kufanana mno kwa matatizo yetu.<sup>54</sup>

Pengine swali la kujiuliza hivi sasa ni: Je! Kwanini Waislamu wa Afrika Mashariki, pamoja na matatizo yote haya yanayotukabili, hatuoneshi kuwa na mpango wowote wa kukabiliana nayo?

## **Kupigwa Vita Uislamu Tanganyika**

Wafanya biashara wa Kiarabu waliwatangulia watawala wa Kijerumani kuingia Tanganyika. Waarabu hawakuingia Tanganyika kama nchi au Serikali inayokuja kutawala. Ilikuwa ni familia zilizokuja kutafuta biashara. Kwa hiyo Tanganyika haikuwahi kutawaliwa na Serikali au nchi ya Kiarabu. Wafanya biashara hawa wa Kiarabu kila mahali walipoweka makao yao walijenga shule za Qur-an (madrasa). Pia walifundisha ujuzi wa kusoma na kuandika kwa kutumia herufi na nambari za Kiarabu.

Wakoloni wa Kijerumani walipoingia Tanganyika walijiimarisha kwanza katika miji ya Pwani. Waliwakuta wenyeji wa Pwani wengi wao wakijua kusoma na kuandika kwa kutumia herufi za Kiarabu. Hawa wakawatumia katika kazi zao za utawala.

Shule za mwanzo za Serikali ya kikoloni zilianza kujengwa Bagamoyo na Tanga. Kulingana na hali halisi ya maeneo hayo wanafunzi wengi wakawa Waislamu. Wakristo wakaja juu kumshutumu Gavana Von Soden kuwa anaendesha sera za kupendelea Waislamu. (Taz: Hornsby, German Achievement” uk. 84) Kutokea hapo Serikali ya kikoloni kwa kushirikiana na mashirika ya Kikristo toka Ulaya yakawa yanaendesha kampeni na mikakati ya kuwabana Waislamu katika elimu. Kwa hiyo japo Watanganyika wote walilipa kodi ya kichwa lakini ni Wakristo pekee waliokatiwa donge nono la kodi hiyo kujiimarisha kielimu.<sup>55</sup>

Alipoingia Muingereza alifuata sera ile ile ya Mjerumani. Mashirika ya Kikristo toka Ulaya yakapewa fursa zaidi kuimarisha elimu ya Wakristo. Na Serikali yenyewe ikawa inatoa mapesa ya kodi za Watanganyika kuimarisha Ukristo na Wakristo. Dhuluma hii hawakuikubali Waislamu. Bwana J.G. Liebenow katika kitabu chake “The Colonial Rule and Political Development in Tanzania. The case of the Makonde”; anatufahamisha kuwa watu wa mikoa ya Kusini hasa Wayao na Wamakonde waliilalamikia Serikali kuwa kwanini wakati walipa kodi wa eneo hilo wengi ni Waislamu, lakini fedha hupewa Wakristo wajenge na kuendesha shule. Muandishi Muchy Makajenga katika makala yake “Serikali inapendelea Wakristo?” amewaelezea ‘watu wa’ Mikoa ya Kusini kwamba hawajui thamani ya elimu. (Taz: WAKATI NI HUU na 20, Juni 1-7, 1993).

Watu hawa wasingejua thamani ya elimu vipi wangemlalamikia mkoloni? Dosari yoyote itakayoelezwa leo hii juu yao katika suala la elimu ni matokeo ya kudhalilishwa kwao kwa muda mrefu.

Kutokana na malalamiko ya Waislamu Serikali ya kikoloni ilianza kuwapa Waislamu nao fedha kidogo kwa ajili ya elimu. Mwaka 1957 Serikali ilitoa paundi 1,338,925 kwa ajili ya mashirika yanayotoa elimu. Waislamu walipewa paundi 6,848 tu kati ya hizo.

Kwa hiyo utaona katika kipindi hicho nyeti na muhimu sana kwa upanuzi wa elimu kupitia msaada wa Serikali (Aided System of Education), Waislamu walifungiwa milango.

Hali hiyo ndiyo iliyompelekea Sheikh K. S. Kiangi Msuya kutoa maneno yafuatayo kwa uchungu mkubwa sana juu ya udhalili wa elimu kwa Waislamu wa Tanganyika. Maneno yake hayo yalichapishwa katika gazeti la Kiongozi la tarehe 26 Oktoba, 1956 uk. 3 chini ya kichwa cha habari:

“Udhalili wa elimu kwa Waislamu Tanganyika”

*“Inasemekana kuwa hesabu ya watu wa tanganyika ni zaidi ya 8,102,000 na katika hesabu hii Waislamu ni zaidi ya 4,500,000. Sasa nataja schools zote uonekane udhalili ulioko juu ya Waislamu.*

***HESABU YA SCHOOLS ZOTE TANGANYIKA 1955***

1. (a) *Schools za Utawala (Government & Native Authority) Primary School 656.*  
(b) *Schools za wakristo Primary 1692.*  
(c) *Schools za Waislamu Primary 28.*
2. (a) *Schools za Utawala (Government) Rural Middle 104.*  
(b) *Schools za Wakristo Rural Middle 223.*  
(c) *Schools za Waislamu Rural Middle - Hawana.*
3. (a) *Schools za Utawala (Government) Secondary 10*  
(b) *Schools za Wakristo Secondary 16.*  
(c) *Schools za Waislamu Secondary – hawana.*
4. (a) *Schools za Utawala (Government) T.T.C 7.*  
(b) *Schools za Wakristo T.T.C 23*  
(c) *Schools za Waislamu T.T.C. – Hawana.*

5. (a) *Schools za Utawala (Government) Ufundi, Utibabu n.k. 7*

(b) *Schools za Wakristo Ufundi & Utibabu 5.*

(c) *Schools za Waislamu Ufundi, utibabu – Hawana.*

*Schools hizi hapa juu huendeshwa kwa fedha tulipayo kwa kodi na ushuru wa watu wote wa Tanganyika, na Muislamu akihitaji kuingia Secondary ama T.T.C. za Wakristo huambiwa abatizwe awe Mkristo (ndipo ataweza kutumia fedha yake aliyolipa) ndipo atakubaliwa kusoma hapo. Pia schools za Middle 104 za government ambazo Serikali inasema inapokea watu wote; sivyo kabisa, kwani ataingiaje Middle naye hana Primary? Nataja moja kwa mfano Kibohehe, Machame wilaya ya Moshi ni school ya Utawala ina wanafunzi 140 kati yao Waislamu ni 12 tu na 128 ni Wakristo. Je, kuingia Secondary na Teacher Training college(T.T.C) itakuwaje?*

*Wanafunzi wa Tanganyika walioingia Makerere college 1950-1955 ni 500 na Waislamu katika mia ni watano na 95 Wakristo hivyo Waislamu watapataje maendeleo?” (Sheikh K.S. Kiangi Msuya).*

Mwaka 1958 Novemba 20, Waislamu waliitisha mkutano mjini Dar es Salam. Katika mkutano huo ambao uliitwa “Africa Muslim Education conference”, Waislamu waliorodhesha malalamiko yao dhidi ya Serikali ya kikoloni kuhusiana na ubaguzi katika elimu.

Miongoni mwa mambo yaliyolalamikiwa ni kuwa:

1. Mara Waislamu walipoanza kufungua shule Serikali ya kikoloni iliweka mpango wa elimu wa miaka mitano (FYP) kuwa isifunguliwe shule ya msingi tena.
2. Pale ambapo Waislamu wamefungua shule hulazimishwa wafundishe Qur-an tu; vinginevyo wanashitakiwa.

3. Shule za Muslim ambazo zimekubaliwa na Serikali zinanyimwa misaada (Grant in Aid) wakati Waislamu wanalipa kodi Serikalini.

## **Mchango wa Waislamu Katika Kuleta Uhuru Tanganyika**

Kwa upande mmoja wakoloni walijenga mahusiano ya karibu sana na mashirika ya dini ya Kikristo na walisomesha kundi la Wakristo na kuwa karibu nalo ili wawatumie katika kutawala.

Kwa upande mwingine kama tulivyokwishaona Waislamu walitengwa, kubaguliwa na kukandamizwa. Hali ilikuwa ngumu kiasi cha kuwapelekea Waislamu kuwa mstari wa mbele katika kuanzisha harakati za kumng'oa mkoloni. Harakati za mwanzo za kupambana na Serikali ya kikoloni zilianzia katika maeneo ya Waislamu. Katika vita vya maji maji mwaka 1905 Waislamu walipigana huku wakiyachukulia mapambano yale kuwa ni Jihad. Kwa upande wa Wakristo, wao walisimama kuwaunga mkono Wajerumani kupambana na Watanganyika wenzao.

Kati ya mwaka 1939 na 1947 Wafanyakazi bandarini Tanga na Dar es Salaam ambao wengi wao walikuwa Waislamu waliongoza migomo mikubwa kupinga dhuluma za kikoloni na kujenga mazingira ambayo baadaye yaliwaruhusu kuanzisha vyama vya wafanyakazi. Kiongozi wa harakati hizo Kleist Sykes alichaguliwa kuwa Katibu wa kwanza wa Jumuiya ya kwanza ya wafanyakazi Tanganyika. Ama huko nyuma mwaka 1940 Kleist na Waislamu wengine mashuhuri pamoja na Shariff Salim Omari aliyekuwa Liwali wa Dar es Salaam, Maalim Popo Saleh, Ali Kiro na Idi Tosiri walianzisha Al Jamiatul Islamiyya fi Tanganyika. Shariff Salim alichaguliwa kuwa Rais na Kleist Sykes katibu. Shariff Salim alipotoka chamani mnamo mwaka 1936, Mzee bin Sudi alichaguliwa kuwa Rais. Uongozi wa juu wa African Association



iliyoanzishwa mwaka 1929 ulikuwa ndiyo ule ule katika Al Jamiatul Islamiyya fi Tanganyika. Ushawishi wa uongozi huu wa Waislamu katika African Association unaweza kuonekana katika mwaka 1930 wakati chama na siyo Al Jamiatul Islamiyya kilipoandikia Serikali ya kikoloni kikidai kuchaguliwa kwa Mwafrika kama kadhi ili kuongoza kwa “sharia”.

TANU(Tangayika African National Union) asili yake ni TAA.Tanganyika African Association). TAA kulikuwa na kamati ya siasa ambayo ilikuwa na wajumbe Waislamu: Sheikh Hassan bin Amir, Mzee Kleist Sykes, Abdulwaheed Sykes,Hamza Kibwana Mwapachu,Said Chaurembo. Sheikh Hassan bin Amir alikuwa mjumbe wa kamati ya Utendaji ya Da’awat Al-Islamiyy wakati Kleist Sykes alikuwa katibu mkuu wa Jamiatul Islamiyya. Nyerere alikaribishwa na kupewa uongozi katika harakati za kisiasa katika hatua za mwanzo za kuanzishwa kwa TANU. Kuingia kwa Nyerere na wasomi wa Kikristo wengine katika TANU kulibadili sura ya siasa Tanganyika. Japo chama kilikuwa kimepata wasomi lakini muungano baina ya Waislamu na Wakristo nao ulianza. Kwa vile Wakristo hawa ndio wengi waliokuwa wasomi wakawa wanashika nafasi nyeti katika chama. Mwelekeo huu uliwatisha baadhi ya Waislamu. Waliona kuwa kuna uwezekano mkubwa kwa Wakristo hao kutokutenda haki, kinyume chake wakatumia nafasi zao kuendeleza dhulma ile ile ya wakoloni. Sheikh Suleiman Takadiri akiwa mwenyekiti wa Baraza la Wazee la TANU alikuwa wa mwanzo kuonesha wasiwasi wake hadharani. Hata hivyo akapigwa vita kwa kuitwa mdini “anachanganya dini na siasa”. Waislamu wengine walipoona TANU imesahau agenda ya Waislamu wakaanzisha chama cha AMNUT, All Muslim National Union of Tanganyika mwaka 1957. Lengo lilikuwa ni kupigania haki sawa kwa wote. Lakini nacho kikapigwa vita kikatoweka. Kwa hiyo Waislamu wakabakia kuwa mstari wa mbele katika kupigania uhuru lakini katika mtizamo ulioitwa wa kutochanganya dini na siasa (Secularism). Sio wa kusimamisha Haki au “Ukhalifa”. Kwa mtizamo huo wakampamba Mwalimu Nyerere kuwa Mwalimu wao

katika siasa na harakati za kuendesha nchi baada ya uhuru. Lakini wakati Waislamu wanaacha agenda yao ya kusimamisha Ukhalifa, kisirisiri Mwalimu Nyerere alikuwa akipewa maandalizi ili aje kusimika utawala wa Kikatoliki Tanganyika. Mashirika ya Kikristo yalimsomesha na kumuandaa ili aje kutawala kama mkristo mkatoliki. Kufuatia safari yake Umoja wa Mataifa mwaka 1956 ambayo kwa kiwango kikubwa alisaidiwa na shirika la Kikatoliki la Maryknoll Fathers, Serikali ya kikoloni iliilalamikia Vatican. Padri William Collins aliyekuwa Katibu Mkuu wa Shirika la Maryknoll 1957, alitakiwa na Vatican, makao makuu ya Kanisa Katoliki duniani kuandika ripoti maalum. Ripoti hiyo ilitoa majibu kuhusiana na malalamiko ya Serikali ya wakoloni Tanganyika. Sehemu ya ripoti hiyo inasema:

*“Mapadri wa Maryknoll wamekubali kulipia tiketi ya kwenda na kurudi kutoka England kwenda New York. Safari yake kutoka Tanganyika hadi England na kurudi ililipiwa na chama chake. Shirika la Maryknoll limekubali kumlipia kuja hapa kwa vile ni **kiongozi Mkatoliki** kutoka wilaya ya Musoma tumeonelea ni vizuri apate fursa kuona hali ya Ukatoliki huko Amerika na pengine kupata nafasi za masomo zaidi kwa Watanzania.*

*Alifika mjini New York Novemba 13, 1956 na kuondoka Januari 5, kiasi cha majuma saba hivi. Wakati ule huko New York aliishi katika jumba la “Leo House” ambalo lilisimamiwa na Masista wa Mt. Agnes. Kisha alisafiri mpaka Washington ambako aliishi na White Fathers, halafu Chicago na Boston ambako alikaa na Maryknoll Fathers. Huko Washington katika Chuo Kikuu cha John Hopkins alitoa mhadhara, nako Chicago alikutana na viongozi wa vyama vya wafanyakazi na huko Boston alikuwa na mazungumzo katika Chuo Kikuu cha Boston. Akiwa mjini New York alihudhuria mikutano kadhaa ya Umoja wa Mataifa.*

*Maryknoll Fathers wamekubali kulipa tiketi ya kwenda Amerika na kurudi England kwa vile huyu ni kiongozi wa Kikatoliki, mtu kutoka*

*jimbo la Musoma ambaye anaheshimiwa na Mapadri wetu. Kwa vile ni nia ya Serikali ya Waingereza kuwaandaa wenyeji kwa madaraka, Shirika la Maryknoll limeona kuwa msaada wowote linaoweza kuwapatia viongozi wa Kikatoliki utakuwa ni kulisaidia kanisa. Huyu ni Mkatoliki mzuri, mtu mwenye msimamo na busara katika kutaka kuwaelekeza watu wake kwenye uhuru kamili. Hakosi kuwa na habari kwamba kuna wapinzani fulani wenye siasa kali zaidi katika chama chake lakini anajitahidi kukiongoza kwa njia inayokubalika. Chama hiki, kimeandikishwa rasmi Serikalini na wala siyo chama cha siri”.*

Haya yameandikwa na William Collins katika ripoti iliyoitwa; “Report on Julius Nyerere and his relations with the Maryknoll Fathers in Tanganyika; British East Africa”. Feb. 11, 1957. Ilitumwa kwa Fr. Heinzmann Rome, Italy).

Pamoja na kuandaliwa Nyerere, Maryknoll Fathers na White Fathers walikuwa pia wakiwaandaa watu wengine ili kuja kushika nafasi muhimu Serikalini baada ya uhuru. Padri Paul Crane aliyetembelea Tanganyika mwaka 1959 alidhihirisha siri hii pale aliposema:

*“Lazima tujitahidi kadri ya uwezo wetu kupata wasomi Wakatoliki ambao watahika nafasi muhimu kwenye ngazi zote za kijamii. Wakatoliki wajitahidi kushika nafasi hizi. Tutaweza kuwaingiza kwenye nafasi za uongozi kwa njia ya kujenga vikundi vidogo vidogo vya wasomi Wakatoliki”. (Haya yanapatikana katika kitabu cha Paul Crane “Problems of the movement of the Young away from the Church; Rome: CIPA; 1960).*

Kutokana na maandalizi hayo Wakristo walihodhi nafasi zote nyeti za uongozi katika Serikali baada ya uhuru. Hali hiyo anasema Dk. Sivalon kuwa “imefanya matendo, msimamo na uamuzi wa viongozi wa Serikali ufanane mara kwa mara na kwa namna moja au nyingine na mafundisho na mwelekeo wa Kanisa.”<sup>56</sup>

Kwa hiyo kutokana na Nyerere kuwa Mkatoliki na kuwa kiini cha kikundi cha watawala Wakristo alikuja kuwa kiungo muhimu kati ya kanisa na Serikali. Kiungo hiki kililipa kanisa nafasi nzuri ya kuupiga vita Uislamu.

Kwa hiyo wakati Waislamu walikuwa wakipigania uhuru huku wakiitupa agenda ya Uislamu, wenzao walikuwa wakijiandaa kuja kushika Serikali katika mazingira ambayo yatawezesha kupambana na Uislamu. Na kweli walipambana nao mara tu baada ya uhuru.

### **Mkutano wa Kwanza wa Waislamu, 1962.**

Baada ya uhuru kupatikana mwaka 1961 Waislamu waliamini kuwa hali yao ya baadae katika Serikali huru itakuwa nzuri. Mwaka 1962 ukaitishwa mkutano wa Waislamu wa nchi nzima kujadili nafasi ya Uislamu katika Tanganyika huru. Taasisi zifuatazo zilihudhuria mkutano huo: East African Muslim Welfare Society (EAMWS), Da'awat Islamiyya, *Jamiatul Islamiya fi Tanganyika*, na *Muslim Education Union*. Mkutano ule ulikubaliana pamoja na mambo mengine umuhimu kuanzisha idara ya elimu chini ya EAMWS. Waislamu hawakusubiri Serikali itimize ahadi yake ya kurekebisha upogo uliokuwepo wa elimu kati ya Waislamu na Wakristo. Waislamu walianzisha mipango yao wenyewe ili isaidiane na juhudi ya Serikali. Mipango ikatayarishwa ya kujenga shule Tanganyika nzima na mwishowe kujenga Chuo Kikuu cha kwanza kwa Waislamu katika Afrika ya Mashariki. Mkutano ukamchagua Tewa Said Tewa, waziri wa Serikali, mwanasiasa wa TAA na mmoja wa wale wazalendo kumi na saba walioanzisha TANU, kuwa mwenyekiti wa EAMWS kwa upande wa Tanganyika.

Huu ndiyo ukawa mwanzo wa uadui kati ya Waislamu na Serikali ambayo ilikuwa mikononi mwa Wakristo. Uelewano uliodumu wakati wa kudai uhuru ukaanza kutoweka na siasa zikachukua sura mpya ya uhasama, kutoaminiana na kutofautiana

kati ya jamii hizi mbili. Kisa cha hali hii mpya ni Waislamu kutaka kuondoa hali ya kikoloni iliyowakandamiza kwa miaka mingi. Waislamu waliona kuwa hili lilikuwa ni jambo lisilokuwa na pingamizi kufanyika. Uhuru ili uwe na maana ni lazima Waislamu wajitoe ndani ya unyonge waliogubikwa na wakoloni. Kwa upande wa Wakristo hali hii ilisababisha hofu kuu nyoyoni mwao.

### **Pingamizi Katika Kuleta Mabadiliko ya Kunufaisha Waislamu, 1963.**

Uhuru ulipopatikana kulikuwa na makundi makubwa mawili yaliyokuwa yanatawala siasa Tanganyika. Kwanza kulikuwa na Waislamu ambao tegemeo lao kubwa lilikuwa kuona ile hali yao ya unyonge iliyodumu kipindi chote cha ukoloni ikitoweka. Nguvu ya pili ilikuwa vyama vya wafanyakazi. Makundi haya yote yalikuwa na mategemeo makubwa kwa Serikali ya TANU kuwa itawapa haki zao bila ya matatizo yoyote. Pamoja na makundi haya palikuwapo na vyama vya upinzani, AMNUT na Congress ambavyo kwa kweli havikuwa na nguvu yoyote ya kuweza kupambana na TANU. Miezi michache kabla ya uhuru, Nyerere alitoa onyo ambalo dhahiri lilikuwa limeelekezwa kwa makundi haya. Mwezi Mei, 1961 Nyerere alionya kuwa hatosita kuwaweka kizuizini viongozi wa vyama vya wafanyakazi, viongozi wa dini na wengineo endapo watakuwa tishio kwa Serikali yake.<sup>57</sup> Hapa ieleweke wazi kuwa viongozi wa dini aliowakusudia Nyerere kuwaweka kizuizini hawakuwa viongozi wa kanisa, bali Masheikh. Hawakuwa viongozi wa kanisa kwa kuwa mpaka uhuru unapatikana makanisa yalikuwa yamejitenga na siasa kwa ukamilifu. Huenda Nyerere alitoa onyo hilo kutokana na shutuma alizotoa mpinzani wake Rais wa Congress, Zuberi Mtemvu. Akiwahutubia wanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Karl Marx mjini Leipzig, Ujerumani ya Mashariki, Mtemvu alibashiri kuwa kutolewa kwa uhuru wa Tanganyika kwa uongozi wa TANU, hakutabadili chochote kwa kuwa wanaoingia madarakani wameamua kushirikiana na wale wale wanyonyaji wa zamani na hii itavunja nguvu za wazalendo na matumaini yao.<sup>58</sup>

Haiwezekani kuielewa ahadi ya Nyerere katika haki na usawa kwa raia wote kama alivyoahidi wakati wa kudai uhuru, hadi usome hotuba yake aliyoitoa tarehe 10 Desemba, 1962 katika Bunge wakati Tanganyika inakuwa jamuhuri. Hotuba ya Nyerere ilijikita kwenye matatizo ya upogo kati ya Waislamu na Wakristo. Nyerere alifanya hivi labda akijua kuwa ingawa yeye alikuwa Rais Mkatoliki lakini waliomuweka madarakani kuitawala Tanganyika walikuwa Waislamu. Katika hotuba yake Nyerere alisema yafuatayo:

*“Hakuna njia nyepesi ya kuondoa tofauti baina ya raia wetu Waafrika na wasio Waafrika; hakuna njia nyepesi ya kuondoa tofauti za elimu kati ya Wakristo na Waislamu, au baina ya wachache wenye elimu na wengi wa watu wetu wasio kuwa na elimu; hakuna njia nyepesi ambayo Wamasai na Wagogo wanaweza wakalingana na Wahaya, Wachagga na Wanyakyusa.”*<sup>59</sup>

Hii ilikuwa kauli ya Serikali ya kudhihirisha nia yake njema. Kauli hii ilikuwa ya kuwapa matumaini na kuwahakikishia Waislamu na wale wote walioathirika na dhulma ya wakoloni, kuwa Serikali ilikuwa inatambua shida zao na ingechukua hatua zifaazo kurekebisha hali hiyo. Wakati Nyerere anatoa kauli hii ya kutia moyo, Serikali iliyokuwa imejaa viongozi wa Kikristo na taasisi za Kikristo zilikuwa zimejaa hofu zikiogopa harakati za Waislamu za kujiletea maendeleo zilizokuwa zikitapakaa nchi nzima kwa kasi. Walifahamu nguvu na umoja wa Waislamu ukitumiwa vyema hapana shaka Waislamu wangukuja juu. Kwa viongozi wa Kikristo walioshikilia madaraka ya Serikali, kwao ilimaanisha kugawana madaraka sawa na Waislamu. Harakati hizi mpya za waislamu ziliashiria kuanguka kwa himaya yao katika madaraka kama viongozi. Hii ilionekana kama harakati za awamu ya pili za Waislamu, safari hii kuchukua Serikali kutoka kwa Wakristo. Harakati za awamu ya kwanza zilikuwa zile za kumng’oa Mwingereza katika ardhi ya Tanganyika. Bila ya kutegemea,

Serikali ikajikuta inakabiliana ana kwa ana na jumuiya ya Kiislamu iliyokuwa na nguvu ambayo kwa dhahiri yake kila Muislamu alikuwa ni mwanachama, na ndani yake imejumuisha wana-TANU shupavu pamoja na wapinzani wa TANU. Wakati huo huo Baraza la Wazee wa TANU katika nafasi yake ya ushauri likawa linaishinikiza Serikali ifanye mabadiliko haraka kutokomeza mabaki ya ukoloni. Serikali ikaona harakati hizi ni sawasawa na kuendesha nchi katika misingi ya Uislamu. Baraza la Wazee wa TANU lilikuwa sasa limejigeuza kutoka kundi dogo la wazalendo na kuwa kundi lililokuwa likishinikiza Serikali ndani ya TANU. Serikali ilikuwa ama ikubali matakwa ya Waislamu au ikatae na ipambane na upinzani kutoka kwao. Tarehe 11 Machi, 1963, Kamati Kuu ya TANU iliyokutana Dar es Salaam ilipiga kura kuvunja kamati ya wajumbe kumi na moja ya Baraza la Wazee wa TANU chini ya Mwenyekiti wake Idd Tulio. Wazee walikusanyika katika ukumbi wa Arnautoglo na wakasomewa uamuzi wa Kamati Kuu ya kulivunja Baraza la Wazee.

Taarifa ilisema wazee hao ni kero kwa sababu 'dini na siasa vilikuwa vitu viwili tofauti na hawa wazee walikuwa wanachanganya dini na siasa.<sup>60</sup> Hiki kilikuwa chombo cha ushauri ambacho wajumbe wake wote walikuwa Waislamu; chombo kilichokuwa ndani ya TANU ambacho kilimuunga mkono Nyerere na TANU tangu siku za mwanzo kabisa, kwanza chini ya uongozi wa Sheikh Suleiman Takadir na kisha chini ya Idd Tulio baada ya kufukuzwa kwa Sheikh Takadir kutoka TANU. Wakati haya yote yakitendeka Kanisa ambalo wakati wa kudai uhuru lilijiweka mbali na halikutoa msaada wowote sasa likawa linanyemelea kujiingiza katika siasa likiwa na agenda yake: kuwaweka viongozi Wakristo katika nafasi za uongozi na kuwatoa nje ya uongozi Waislamu ambao Kanisa liliwaona hawana elimu.<sup>61</sup>

Jumuiya za Kiislamu kama *Al Jamiatul Islamiyya fi Tanganyika* na *EAMWS* zilikuwa sasa zikipigwa vita na Serikali ya Nyerere kama vyombo ambavyo havikuwa na umuhimu wowote katika

Tanganyika mpya. Katika kumuhakikishia utiifu wao juu yake, Waislamu walijitahidi mwisho wa uwezo wao kuziweka Taasisi zao kando na chuki za kidini dhidi ya Wakristo.<sup>62</sup> Juhudi hizi hazikuthaminiwa. Serikali ilifanya juhudi za siri kuhakikisha kuwa jumuiya zote za Waislamu zinapigwa marufuku.<sup>63</sup>

Huu ndiyo ukawa mwanzo wa kampeni za kufuta historia ya Uislamu katika TANU na mwisho wa Waislamu kuwa na sauti katika siasa baada ya uhuru kupatikana. Baada ya kupatikana kwa uhuru, ile nguvu ya Waislamu iliyotumika kupambana na Waingereza kuleta uhuru, ikaonekana haina maana yoyote na haifai kitu tena. Kuvunjwa kwa Baraza la Wazee ndiyo ilikuwa kishiko cha mwisho cha Waislamu katika TANU. Baada ya hapo Kanisa lililokuwa pembeni wakati wa kudai uhuru sasa likajitokeza waziwazi kuwapiga vita Waislam katika TANU. Katika kitendo ambacho kanisa halikupata kufanya, Kanisa Katoliki Bukoba liliteua wagombea wake wenyewe wapambane na wagombea Waislamu walioteuliwa na TANU kugombea nafasi katika uchaguzi wa Serikali za mitaa. Kanisa lilisema limeweka wagombea wake binafsi kwa kuwa wana elimu kupita wagombea wa TANU Waislamu. Kampeni kama hii ilifanyika vilevile Kigoma. Hakuna ushahidi wowote unaoonyesha kuwa Nyerere, Serikali au TANU yenyewe ilichukua hatua zozote dhidi ya Kanisa kwa kuchanganya “*dini na siasa*”.

### **Mkutano wa Pili wa Waislamu, 1963**

Ulipoitishwa Mkutano wa Pili wa Waislamu Dar es Salaam matatizo haya mazito yaliwekwa kwenye agenda ili yajadiliwe. Mkutano ule ulithibitisha bila wasiwasi wowote kuwa kulikuwapo na njama za sirisiri ndani ya TANU kuhujumu Waislamu na njama hizi zikienda sambamba na kampeni nchi nzima dhidi ya Waislamu na viongozi wa EAMWS.<sup>64</sup> Nyerere alialikwa kufunga mkutano ule na Waislamu wakamueleza masikitiko yao kwa hali ile iliyojitokeza.



Nyerere alizungumza kwa kirefu matatizo ya Waislamu na kwa kiasi aliweza kutuliza mambo. Lakini kulikuwa hapana shaka katika fikra za viongozi wa EAMWS kuwa kulikuwa na njama zilizopangwa na Kanisa mahsusi kwa minajili ya kupiga vita Uislamu na Waislamu. Uongozi wa Wakristo katika TANU, Serikali na Nyerere binafsi alitumika kufanikisha azma hiyo. Uongozi wa Kikristo katika taasisi za umma sasa ukawa unatumia nguvu za dola kulipa Kanisa madaraka ili liweze kudhibiti Serikali na TANU.

Tarehe 20 Januari, 1964 kulitokea maasi katika *jeshi la Tanganyika Rifles*. Nyerere alirudishwa madarakani na jeshi la Waingereza lililoletwa kuzima maasi. Baada ya mambo kutulia Nyerere akachukua nafasi hiyo kuwaweka kizuizini viongozi wa vyama vya wafanyakazi na masheikh maarufu katika Tanganyika. Kesi ya uhaini ya wanajeshi ilipofikishwa Mahakama Kuu hapakuwa na ushahidi wowote ule kuwa Masheikh walihusika kwa njia moja au nyingine katika uasi wa *Tanganyika Rifles*. Uvumi uliokumba mji wa Dar es salaam ni kuwa masheikh hao walikuwa wanapanga njama za kupindua Serikali. Baada ya hapo, mwanazuoni maarufu, Sharif Hussein Badawiy na mdogo wake Mwinyibaba, walipewa notisi ya kuondoka nchini kama wahamiaji wasiotakiwa. Kilichofanya Shariff Badawiy afukuzwe nchini ni kauli aliyotoa Mwinyibaba katika maulid.

Akiwahutubia Waislamu katika maulid yale, Sheikh Abdallah Chaurembo alisema kuwa Waislamu wanapaswa kuishukuru Serikali kwa kutoa ruhusa kwa Waislamu kuondoka kazini mapema siku ya Ijumaa ili wapate fursa ya kuswali swala ya Ijumaa. Baadhi ya Waislamu waliokuwapo pale waliona kama kwamba Sheikh Chaurembo alikuwa akijikomba kwa Serikali ili apate umaarufu wa bure na kwa ajili hiyo afaidike kisiasa. Iliamuliwa kuwa Waislamu lazima wajibu hotuba ya Sheikh Chaurembo usiku ule ule bila ya kungoja. Mwinyibaba alipanda kwenye mimbari ile ile ambayo muda mfupi uliopita Sheikh Chaurembo alihutubu. Mwinyibaba aliwaeleza Waislamu kuwa wao hawahitaji kumshukuru yeyote

kwa ajili ya kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu. Vyovyote iwavyo sala ya Ijumaa ni fardh inayomwajibikia kila Muislamu na hana khiyari ila kutekeleza, Serikali iwe imetoa ruhusa au vinginevyo.

Sheikh Abdallah Chaurembo alikuwa hapo mwanzoni mwanafunzi wa Sheikh Hassan bin Amir na alikuwa chini ya Sheikh Hassan hadi ilipotokea mtafaruku baina yake na mwalimu wake mwaka 1961. Chanzo cha mtafaruku ilikuwa ni kuhusu mambo ya akida katika siasa za TANU. Kwa ajili hii ikabidi Sheikh Chaurembo ajiondoe kwa sheikh na akajihusisha katika siasa hadi akachaguliwa kuwa mjumbe wa Kamati Kuu ya TANU.

Jibu kama lile aliltoa Mwinyibaba likaonekana kama ni kuonyesha fedhuli kwa Serikali na TANU. Siku ya pili yake Serikali ikatoa amri Shariff Hussein afukuzwe nchini pamoja na mdogo wake Mwinyibaba ingawa yeye Shariff Hussein hakuwepo hata kwenye hafla ile ya maulid kwa kuwa alikuwa nje ya Dar es Salaam. Shariff Hussein na Mwinyibaba ikabidi waondoke na kurudi kwao Kenya. Lakini ili ieleweke sababu ya kutiwa kizuizini hawa masheikh inabidi turudi nyuma katika mkutano wa mwaka wa EAMWS uliofanyika mwaka 1963.

Jaribio la mwanzo la Nyerere kutaka kuivunja EAMWS lilikuwa mwaka 1963. Lakini jaribio hilo halikufanikiwa kwa sababu ya mpango uliopangwa na Mufti Sheikh Hassan bin Amir na kutekelezwa na Bilali Rehani Waikela, katibu wa EAMWS Tabora. Mwaka huu wa 1963 EAMWS ilifanya mkutano wake katika ukumbi wa Shule ya wasichana ya Aga Khan (shule ya Jangwani ya leo). Wajumbe wa mkutano huo walipowasili mjini Dar es Salaam walikuta uvumi kuwa wajumbe wa mkutano wa EAMWS watakatwa na kuwekwa kizuizini. Chanzo cha uvumi huu hakikufahamika lakini haikuwa vigumu kukisia. Baada ya kuvunja kwa Baraza la Wazee wa TANU mwaka ule ilikuwa wazi kuwa Nyerere alikuwa amewatupa mkono washirika wake wa zamani na sasa alikuwa akitafuta wapya ili kujenga upya msingi wake wa

siasa. Kutokana na mambo yalivyokuwa yakienda ilikuwa ni dhahiri washirika wake wapya hawatakuwa Waislamu. Katibu wa EAMWS Tabora, Waikela alipowasili Dar es Salaam kuhudhuria mkutano alitwa na Sheikh Hassan bin Amir. Mufti Sheikh Hassan bin Amir mbele ya Mzee Ali Comorian, alimfahamisha Waikela kuwa kulikuwa na njama zilizokuwa zikipikwa na Nyerere kumuangamiza yeye na Tewa Said Tewa ili kuvunja EAMWS ipatikane nafasi ya kuanzishwa jumuiya ya Kiislamu ya Watanganyika itakayokuwa chini ya wanafiki. Sheikh Hassan bin Amir alimwambia Waikela kuwa harakati za uhuru zilikuwa zinatekwa nyara na Wakristo kwa manufaa ya makanisa yao. Sheikh Hassan alimfahamisha Waikela kuwa ni lazima yeye afanye kila linalowezekana ili njama za Nyerere zishindwe. Baada ya maneno hayo Sheikh Hassan bin Amir alinyanyua mikono yake juu na kumuomba dua Waikela. Nyerere alikuwa anamfahamu Waikela kwa kuwa alikuwa muasisi wa TANU na alikuwa ametoa mchango mkubwa katika kupigania uhuru.

Nchi nzima hasa sehemu za Waislamu kulikuwa na mpango wa Serikali wa kuwavunja Waislamu nguvu na kuwakatisha tamaa. Waikela, kama ilivyokuwa kwa viongozi wengine wa EAMWS, alikuwa anasugana na Mkuu wa Mkoa wa Jimbo la Magharibi, Richard Wambura. Kulikuwa na ujeuri kwa upande wa Serikali walipokuwa wanashughulikia matatizo ya Waislamu, mbali na mategemeo ya Waislamu waliyokuwanayo kabla ya uhuru. Subira ya Waikela ilifikia kikomo pale Wambura alipowatukana Waislamu katika mkutano wa hadhara. Baada ya kuhutubia Wambura, Waikela alipanda jukwaani na akaikumbusha Serikali kuwa isiwe mwizi wa fadhila kwa kusahau jinsi Waislamu walivyojitolea muhanga katika kudai uhuru. Serikali ikachukulia hotuba ya Waikela kama usaliti na yenye kuwashawishi Waislamu wasiitii Serikali. Ilikuwa katika hali hii Waikela mwanachama shupavu wa TANU alijitoa kwenye chama na akaamua kutumia nguvu zake kuwatumikia Waislam kupitia EAMWS. Ilikuwa wazi kuwa Nyerere alikuwa na habari za msugano kati ya Serikali na Waislamu kule Tabora na mtu aliyehusika na msugano huo.

Siku kabla ya mkutano wa EAMWS, Nyerere aliwaalika wajumbe wa mkutano *Government House* kwa chakula cha usiku. Hao waalikwa walikuwa wajumbe waliochaguliwa mahsusi. Waikela hakuwa mmoja wa hao waalikwa. Nyerere alichukua nafasi ile kuwashauri wajumbe wale waanzishe jumuiya ya Waislamu wa Tanganyika ichukue nafasi ya EAMWS. Wajumbe hawa walipoleta katika mkutano hoja ya kuanzisha jumuiya ya Waislamu wa Tanganyika, Waikela alisimama na kuipinga hoja ile. Alizungumza vilevile kuhusu uadui wa Serikali kwa Waislamu na Uislamu. Waikela alimaliza hotuba yake kwa kutoa changamoto kwa wajumbe wamuite Nyerere kwenye ufunguzi wa mkutano ili awaeleze wajumbe msimamo wake kuhusu kadhia ile ya chinichini baina ya Serikali na Waislamu.

Baada ya kushindwa kwa hoja ya kuivunja EAMWS wajumbe wa mkutano ikaonekana kuwa ingekuwa vyema Nyerere aitwe kufunga mkutano ule na asomewe makubaliano yaliyofikiwa. Nyerere alifika kufunga ule mkutano na akakutana uso kwa uso na Waikela, ambae alimsomea maazimio ya mkutano. Waikela alimfahamisha Nyerere kuwa umoja kwa Waislamu ni fardh (wajibu wa lazima). Ni kwenda kinyume na maamrishi ya Allah(s.w) kuwagawa watu. Baada ya utangulizi huu Waikela huku akimnyooshea Nyerere kidole alieleza uadui uliooneshwa na Serikali dhidi ya Waislamu. Waikela alimaliza hotuba yake kwa kitisho. Alimwambia Nyerere ikiwa Waislamu watamgeuka kupambana naye hatakuwa na uwezo wa kuwashinda. Nyerere alitulia pembeni mwa Rais wa Baraza la Tanganyika la EAMWS Tewa Said Tewa, akimsikiliza Waikela. Aliposimama kujibu hotuba ya Waikela Nyerere alisisitiza msimamo wa Serikali wa kutoa haki na usawa kwa raia wake wote. Kwa kiasi fulani Nyerere alikuwa amefanikiwa kupunguza joto kati ya Waislamu na Serikali.

Hotuba ya Waikela na ya Nyerere zikapewa umuhimu mkubwa katika radio. Waislamu wengi wakajitokeza stesheni ya gari moshi Tabora kumpokea shujaa Waikela. Alipewa heshima ile

kwa kuwa na ujasiri wa kuweza kusimama kidete dhidi ya wale waliodhani kuwa wanaweza kuwakalia Waislamu vichwani. Nyerere alihisi ameumbuka na hili lilimchoma moyo sana. Kuanzia hapa Nyerere hakumtazama Sheikh Hassan bin Amir kwa jicho jema. Mwaka uliofuata, tarehe 20 Januari, 1964 jeshi liliasi. Nyerere alichukua fursa ile kuwatia kizuizini masheikh walioonekana wanapinga Serikali na viongozi wa vyama vya wafanyakazi. Waikela alikuwa mmoja wa wale waliokamatwa na kuwekwa kizuizini.<sup>65</sup> Nyerere kwa wakati ule hakuwa na nguvu ya kumgusa Mufti Sheikh Hassan bin Amir.

Wakati ule, mwaka wa 1963, shughuli za kuendesha mafundisho ya Uislamu EAMWS ilikuwa ikienda vizuri sana. Da'awah ilikuwa chini ya Sheikh Amir bin Juma kutoka Tanga na Wakristo wengi walikuwa wakirudi katika Uislamu. Tabligh ilikuwa ikiongozwa kutoka kwa masheikh wa mikoa na wilaya. Fedha za kufanyia shughuli hizi zilikuwa zikichangwa na Waislamu wenyewe. Mufti Sheikh Hassan Bin Amir yeye alikuwa akisomesha fikh, mantik, tauhiid, na tafsir ya Qur'an katika misikiti mbalimbali ya Dar es Salaam. Wakati ule Katibu Mkuu wa EAMWS kwa Afrika ya Mashariki alikuwa V.M. Nazarali.

## **Juhudi za Kuanzisha Chuo Kikuu cha Kiislamu Chini ya EAMWS, 1964**

Mwezi Aprili 1964 ujumbe wa hali ya juu wa EAMWS ndani yake wakiwemo Sheikh Hassan bin Amir, Sheikh Said Omari Abdallah, Tewa Said Tewa, Katibu wa EAMWS Abdul-Aziz Khaki na mzee wa TANU, Mzee Mwinjuma Mwinyikambi; Makisi Mbwana, Issa Mtambo, Omari Muhaji na Saleh Masasi waliondoka kwenda ziara ya nchi za Kiislamu kutafuta msaada wa kujenga Chuo Kikuu cha Kiislamu na kuanzisha uhusiano na nchi za Waislamu. Gamal Abdul Nasser alikutana na ujumbe ule akaupatia ofisi, huduma za simu, na makatibu muhtasi ili waweze kutayarisha mipango yao kwa Serikali ya Misr. Halikadhalika alimuagiza makamu wake Sharbasy afanye makubaliano na EAMWS kwa

niaba yake. Serikali ya Misr ilikubali kugharamia ujenzi wa chuo hicho. Mkataba wa makubaliano ukatiwa sahihi mjini Cairo kati ya Tewa Said Tewa kwa niaba ya EAMWS na Makamu wa Rais wa Misr, Sharbasy kwa niaba ya Serikali yake.

Serikali ya Misr iliahidi kujenga Chuo cha Kiislamu ambacho kingemilikiwa na kuendeshwa na EAMWS. Gharama ya mradi mzima ilikuwa pauni milioni hamsini na tano za (£ 55,000,000)Ki-Misri. Baada ya kukamilisha kazi ile ujumbe ule uliondoka Cairo kuelekea Makka kufanya ibada ya Hija. Baada ya kumaliza Hija wajumbe wanne walirudi nyumbani na Tewa, Aziz Khaki, Sayyid Omar Abdallah wakaendelea na safari kwenda Aman, Jordan ambako walifanya mazungumzo na Mufti na Waziri wa Aukaf. Kutokea hapo ujumbe ulikwenda Kuwait ambako walikutana na Sheikh wa Kuwait kisha wakaenda Baghdad, Iraq na kukutana na Rais wake, Abdisalama Arifek. Kutoka hapo ujumbe ulielekea Beirut, Lebanon ambako ulifanya mazungumzo na viongozi wa harakati za Kiislamu. Baada ya kutoka Beirut ujumbe ule ulirudi tena Cairo kwa ajili ya kukamilisha makubaliano ya kujenga Chuo Kikuu. Tarehe 20 Mei, 1964 ujumbe ulirejea Dar es Salaam na kupokelewa na viongozi wa EAMWS na Waislamu kwa ujumla.

Mkutano wa Halmashauri Kuu ya EAMWS ukaitishwa na Tewa Said Tewa akatoa taarifa yake kuhusu ujenzi wa Chuo Cha Kiislam. Siku ya pili Tewa akaitisha mkutano wa waandishi wa habari na kutoa habari za kujengwa kwa Chuo Cha Kiislamu kwa vyombo vya habari na kwa Waislamu kwa ujumla. Kwa mafanikio haya Tewa akawa amejichimbia kaburi. Matokea haya yalijaza hofu kwa viongozi wa Kanisa. Kampeni za chinichini dhidi ya Tewa binafsi na uongozi mzima wa EAMWS zilianza. Mara baada ya ujumbe wa EAMWS kurudi kutoka ziara yake, Nyerere alifanya mabadiliko katika Baraza la Mawaziri na Tewa Said Tewa, Mwenyekiti wa EAMWS upande wa Tanzania akajikuta nje ya Serikali. Nyerere akamteua Tewa Balizi wa Tanzania katika Jamuhuri ya Watu wa China. Mwezi Januari, 1965 Tewa alikwenda

China kuanza kazi yake mpya. Inasemekana uteuzi wa Tewa kwenda China ulisababishwa na juhudi zake za kutaka kuwaunganisha Waislamu kuwa kitu kimoja chini ya jumuiya moja yenye nguvu. Wakati ule ile mipango iliyopitishwa na mkutano wa Waislamu mwaka 1962 ilikuwa ikitekelezwa vyema, shule zilikuwa zimejengwa Ilala, Kigogo na Kurasini, Dar es Salaam; Ruvu na Maneromango. Shule hii ya Maneromango ilikuwa na umuhimu wa pekee kwa sababu hii ndiyo ilikuwa shule ya kwanza ya Waislamu kujengwa Uzaramoni. Shule za sekondari zilikuwa zikijengwa Dar es Salaam, Kinondoni na Moshi, Kibohehe. EAMWS ilikuwa vilevile imetiliana mkataba wa makubaliano na Serikali ya Misr kuipa scholarship thelathini na tano kila mwaka kwa wanafunzi wa Kiislamu kusoma Misri. EAMWS ilikuwa imejenga shule, misikiti, shule za ufundi na hosteli kwa ajili ya wanafunzi katika sehemu nyingi za Afrika ya Mashariki.

	Uganda	Tanzania	Kenya
Shule	77	70	28
Misikiti	67	53	29
Shule za Ufundi	3	-	-
Hosteli	1	-	-

**Chanzo: Utafiti**

Baada ya Tewa kuondoka Bibi Titi Mohamed akachaguliwa kuwa makamu mwenyekiti wa tawi la EAMWS la Tanzania ili kuongeza nguvu makao makuu kwa kuwa mwenyekiti hakuwepo. Kutokuwepo kwa Tewa nchini kulileta pengo ambalo ilibidi lijazwe. Ghafila palizuka uvumi kuwa Sheikh Abdallah Chaurembo alikuwa achukue uongozi wa EAMWS. Inasemekana nia yake ilikuwa ni kupata Urais wa EAMWS na kisha achaguliwe kuwa Mufti wa Tanzania. Uvumi huu ulidumu kwa karibu mwaka mzima hadi pale Tewa aliporudi kutoka Peking baada ya kujiuzulu Ubalozzi kuja kugombea Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1965. Aliporudi Tewa alihojiwa na waandishi wa habari kuhusu uvumi ule na yeye jibu lake lilikuwa: “Muislamu yeyote mwenye sifa ya maadili mema ana haki ya kugombea nafasi yoyote katika uongozi wa EAMWS”.

Neno alilolitumia Tewa katika kumueleza mtu ambaye angeweza kuwaongoza Waislamu lilikuwa “*taq-wa*”, neno la Kiarabu lenye maana ya ucha-mungu.

Nikuanzia katika matukio haya ndipo tunaweza sasa kuanza kuchunguza jinsi Nyerere akiitumia Serikali alivyoanza kuuhujumu umoja wa Waislamu kwa kutumia njama na hujuma za dhahiri na za kificho, propaganda na kueneza uongo dhidi ya uongozi wa EAMWS, ambao ulionekana ni tishio kwa utawala wake. Wakati ule Serikali nzima ilikuwa mikononi mwa Wakristo. Ukiwatoa Wazanzibari waliokuwa katika Serikali ya muungano – A.M. Maalim, Waziri wa Biashara na Viwanda; Aboud Jumbe, Waziri wa Nchi; A.M. Babu, Waziri wa Ardhi, Makazi na Maji; Hasnu Makame, Waziri wa Habari na Utalii; Rashid Kawawa ambae alikuwa mtu wa karibu sana na Nyerere, waziri Muislam katika Baraza la Mawaziri kumi na tano kutoka bara alikuwa Said Ali Maswanya, Waziri wa Mambo ya Ndani.

### **“Mgogoro” wa EAMWS, 1968**

Kutokana na katiba ya mwaka wa 1957 lengo kuu la EAMWS lilikuwa ni “kuutangaza Uislamu katika Afrika ya Mashariki”. EAMWS yenyewe ilikuwa ikijigamba kuwa uti wake wa mgongo ilikuwa ni tabligh, yaani utangazaji wa dini. Jumuiya hii toka ilipoanzishwa 1933 ilikuwa ya Waislamu wa mataifa yote katika uanachama na katika uongozi wake. Katika uhai wake wa miaka thelathini na tano EAMWS ilijiweka mbali sana na siasa. Jumuiya hii ilishughulikia kuutetea na kueneza Uislamu katika Afrika ya Mashariki. Lakini baada ya kutokea maasi ya *Tanganyika Rifles* mwaka 1964 yaliyopelekea viongozi wengi wa Kiislam kuwekwa kizuizini, EAMWS ikawa imepoteza mwelekeo wake na kudhoofika. Baadhi ya matawi yaliyokuwa katika majimbo yakafungwa kwa woga na kukosa viongozi thabiti. Matawi mengine yalifungwa kwa sababu viongozi wake walikuwa wakichimbwa chinichini na Serikali. Waislamu wengi walihisi vitisho vya Serikali



kwa hiyo waliogopa kuchukua uongozi wa EAMWS. Wengi waliogopa kuitumikia EAMWS kwa kuwa walihisi ofisi za jumuiya hiyo zilikuwa zikichukuliwa na Serikali kama vituo vya upinzani dhidi yake. Kwa zaidi ya miaka mitatu toka ule mkutano wa mwaka 1963, EAMWS haikuweza kufanya mkutano wowote.

EAMWS ilipokuja kuitisha mkutano wake wa mwaka mjini Arusha mwaka 1966 kikajitokeza kikundi kutoka upande wa Tanzania kikidai EAMWS ijigawe, kila nchi iwe na mamlaka yake na ijitegemee yenyewe, yaani Tanzania, Kenya na Uganda zote ziwe mbalimbali. Kikundi hiki kilichokuwa kikidai utengano vilevile kikadai kuwa katiba ya EAMWS nayo iwe ya 'kizalendo'<sup>66</sup> Hii ilikuwa na maana kuwa uongozi uifanyie katiba marekebisho ili kuiwezesha Tanzania kuwa huru ndani ya EAMWS. Wajumbe waliokuwa wanaona mbali kutoka Tanzania na wengine kutoka Kenya na Uganda, na kwa hakika mkutano mzima kwa ujumla walipinga kitendo hicho, wakidai kuwa kwa kufanya hivyo Waislamu wa Tanzania watakuwa wamejitenga na wa Uganda na Kenya. Jambo hili likitokea, si tu lingekuwa limewadhoofisha Waislamu wa Tanzania peke yao, bali Waislamu wa Afrika ya Mashariki nzima. Wajumbe wa Kenya na Uganda walikuwa wanatambua kuwa kulikuwa na shinikizo kubwa kutoka Serikali ya Tanzania kwa Watanzania kujitoa kutoka EAMWS.

Halikadhalika ilikuwa inafahamika kuwa wajumbe wa Tanzania walikuwa wakifanya kazi chini ya shinikizo kali kutoka Serikali ya Nyerere. Haikuwa siri sana kuwa baadhi ya viongozi wa EAMWS walikuwa kisirisiri wakiandamwa na Serikali. Lakini mkutano ule haukuzungumzia matatizo haya kwa kuwa hayo yalichukuliwa kama matatizo ya ndani ya nchi. Hata hivyo kwa ule moyo wa Kiislamu wa kuhurumiana, wajumbe wa Kenya na Uganda kwa faragha walionyesha masikitiko yao kwa Tewa kuhusu ile hali iliyokuwa ikiwakabili Waislamu wa Tanzania. Wajumbe walipokuwa wakiondoka kurejea makwao, ilikuwa wazi

kuwa Serikali ya Tanzania ilikuwa ikiingilia kati EAMWS kiasi cha kuifanya jumuiya hiyo ishindwe kufanya kazi yake vyema na kupitisha maamuzi yake. Hali hii ilijidhihirisha wazi pale kwa kipindi kizima cha mkutano, makachero wa Serikali walikuwa wamejitokeza kwa wingi mjini Arusha. Haukupita muda ikadhihirika kuwa Serikali ilikuwa imepania kuivunja EAMWS kwa kuwatumia Waislamu wachache walioteuliwa kwa kazi hiyo. Lengo likiwa ni kuanzisha taasisi mpya ambayo Serikali ingeweza kuiamuru. leleweke hapa kuwa kama tulivyokwisha eleza hapo nyuma, Serikali nzima ya Tanzania ilikuwa mikononi mwa Wakristo na watendaji hawa walikuwa wapo chini ya Kanisa. Hii ilikuwa na maana kuwa kilichotakiwa kuwepo ilikuwa taasisi ya Kiislamu ambayo Kanisa ingeweza kuiamuru.

Hili lilikuwa ni jambo la lazima kufanyika ili kuwadhibiti Waislamu kama nguvu inayoweza kuleta mabadiliko ya siasa. Baada ya kuelewa hali hii ndipo sasa tunaweza kuuangalia kile kilichoitwa '*mgogoro*' wa EAMWS ambao ulidumu kwa miezi mitatu ya mwisho wa mwaka wa 1968.

Ili tuweze kuelewa vyema kisa kizima cha '*mgogoro*' ni muhimu kwanza kuelewa chanzo chake, hadhi za wahusika wakuu na nafasi zao katika '*mgogoro*' ule. Mwisho, ni muhimu kuweka bayana na kuchambua nafasi ya Julius Nyerere, Serikali yake, chama cha TANU na vyombo vya dola katika '*mgogoro*' ule. Hii itasaidia kuelewa kama kweli ulikuwepo '*mgogoro*' katika EAMWS, au '*mgogoro*' ulibambikizwa na watu katika TANU, Serikali na ndani ya Waislamu wenyewe ili kuwadhoofisha Waislam kwa nia ya kuwa usije Uislamu ukawa na nguvu katika Tanzania hivyo kuwawezesha Waislamu kushika madaraka ya nchi. Mwaka wa 1967 Mwalimu Julius Nyerere alitangaza Azimio la Arusha hatua ambayo iliingiza Tanzania katika siasa ya ujamaa.

Adam Nasibu, mwalimu wa shule ya msingi, aliyekuwa katibu wa EAMWS kule Bukoba alijitafutia umaarufu kwa kuongoza

maandamano hadi ofisi ya TANU ya Mkoa kumuunga mkono Mwl. Nyerere na sera yake mpya ya Azimio la Arusha. Inesemekana Adamu Nasibu alisema kuwa ujamaa ni sawa na mafundisho ya Qur'an Tukatifu. Adam Nasibu hakuishia hapo alikwenda mbele zaidi na kutoa 'miongozo kwa viongozi wote wa Kiislamu wa Bukoba akifafanua Azimio la Arusha'.<sup>67</sup> Wasiokuwa Waislamu walimuona Adam Nasibu kama Muislamu mwenye mwamko mzuri wa kimaendeleo, na kwa kuwa yeye alikuwa ni kiongozi wa EAMWS, kuunga kwake mkono Azimio la Arusha kulionekana kama kitendo rasmi cha jumuiya hiyo kuunga mkono sera hiyo.

Katika hali ya kawaida, uongozi wa EAMWS pale makao makuu Dar es Salaam ulikasirishwa kidogo na kitendo cha Adam Nasibu cha ushabiki wa siasa. Lakini uongozi wa EAMWS haukumuonya kiongozi wake wa Bukoba kuhusu jambo lile ambalo dhahiri halikuwa la kupendeza katika jumuiya. Bila shaka uongozi wa EAMWS ulichelea kuwa kwa kufanya hivyo wangelionekana si wazalendo, hasa ukiichukulia jinsi wananchi walivyohamasika na Azimio la Arusha.

Tofauti na mwaka wa 1963 wakati Nyerere alipojaribu kufanya mapinduzi dhidi ya uongozi wa EAMWS, mwaka wa 1967 hali ya mambo ilikuwa imebadilika sana yakimwendea Nyerere vyema. Serikali ilikuwa imedhibiti vyombo vyote vya habari ukiondoa gazeti la The Tanganyika Standard ambalo bado lilikuwa chini ya Lonrho. Nyerere alikuwa amemuweka Martin Kiama kama mkurugenzi wa radio ya taifa, na Benjamin Mkapa<sup>68</sup> kama mhariri wa magazeti mawili ya TANU, The Nationalist na Uhuru. Adam Nasibu aliandikwa katika magazeti na habari zake kutangazwa katika radio kwa ajili ya kitendo chake, hasa kuhusu yale maneno aliyosema kuwa ujamaa ni sawa na mafundisho ya Qur'an.

Katika hali ya mambo kama yalivyokuwa wakati ule hasa jinsi ile hali ya uhasama ilivyokuwapo baina ya Serikali na Waislamu, baadhi ya Waislamu walimuona Adam Nasibu kama kibaraka

anayetafuta umaarufu wa bure kwa kujipendekeza kwa TANU, Nyerere na Serikali yake. Kwa wengine Adam Nasibu alionekana kama mzalendo na Muislamu aliyekuwa na 'uoni wa mbali'. Kwa ajili hii basi Serikali ikamuoana kama kiongozi wa baadaye ambaye ingeweza kumtegemea wakati wa shida. Uongozi wa EAMWS makao makuu ukaonekana haupo pamoja na wananchi, wala haujali shida zao na uko mbali sana na sera za Serikali. Lakini kwa hakika EAMWS kama taasisi ya dini isingeliweza kujitokeza na kuunga mkono Azimio la Arusha kwa kuwa hayo yalikuwa mambo ya siasa. Kwa kufanya hivyo ingelikuwa inakwenda kinyume na msimamo wake wa kutojiingiza katika siasa.

Hata hivyo kuwa nje ya Azimio la Arusha kukaonekana kama kitendo cha kukosa uzalendo na kutoa picha kuwa jumuiya hiyo ilikuwa haijali maendeleo na ustawi wa watu wa Tanzania. Mambo yakawa yamevurugika zaidi kwa kuwa Rais wa EAMWS, Tewa Said na makamo wake Bibi Titi Mohamed waliokuwa katika Baraza la Mawaziri la Nyerere walipoteza nyadhifa zao za ubunge katika uchaguzi mkuu wa mwaka 1965. Kwa ajili hii basi Serikali ikawa inaeneza propaganda kuwa kwa kuwa Tewa na Bibi Titi waliokuwa katika uongozi wa juu wa EAMWS, walikuwa wanatumia nafasi zao kujijengea himaya mpya kutoka kwa Waislamu dhidi ya Nyerere. Viongozi hawa ikawa lazima washughulikiwe na kuangamizwa. Mtu wa kufanya kazi hii hakuwa mwingine ila Adam Nasibu, katibu wa EAMWS Bukoba. Adam Nasibu alikuwa tayari keshafanikiwa kufanya mapinduzi dhidi ya Rais wa EAMWS, Tewa Said Tewa. Kutokana na vitendo vyake alikuwa ameidhihirishia Serikali kuwa yeye angeweza kuwa mtumishi bora kwa dola kuliko ule uongozi wa EAMWS uliokuwa pale makao makuu Dar es Salaam ambao ulikuwa ukionekana umechoka.

Wakazi wa Dar es Salaam kila mwaka walikuwa wakifanya maulidi katika viwanja vya Mnazi Mmoja kuadhimisha kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (s.a.w). Huu ndio toka asili ulikuwa uwanja ambao TANU ilifanya mikutano yake yote wakati wa kupigania

uhuru. Mwezi Juni 1968 maulidi mbili katika usiku mmoja zilisomwa kuadhimisha kuzaliwa kwa Mtume(s.a.w). Maulidi moja ilisomwa Mnazi Mmoja na nyingine Ilala. Chanzo cha haya yote ni kuwepo kwa kutoelewana kati ya viongozi wa Waislamu waliokuwa wanajiona kuwa ni 'wazalendo' wafuasi wa TANU na wale viongozi wa EAMWS ambao kambi nyingine ilikuwa ikiwaona kama wapinzani wa TANU. Yale maulidi yaliyosomwa Ilala yalihudhuriwa na viongozi wa EAMWS na yalipata watu wengi na yakafana sana ukilinganisha na yale maulidi ya Mnazi Mmoja, ya wafuasi wa TANU. Uongozi wa TANU ulitishika na hali hii iliyokuwa ikijitokeza kwa maana ilikuwa inaonyesha kuwa chama kilikuwa kinapoteza wafuasi ambao walikuwa wakijiunga na kambi ya Tewa na Titi iliyokuwa ikisemekana ipo dhidi ya Nyerere.

Tarehe 17 Juni, 1968, Adam Nasibu akatokea tena katika magazeti akifahamika kama katibu wa EAMWS kutoka Bukoba mwenye hamasa za kisiasa ambaye aliunga mkono Azimio la Arusha na kutoa maelekezo kwa viongozi wengine wa Kiislamu akieleza vipengele vya azimio hilo. Adam Nasibu alitangaza kupitia radio ya Serikali na magazeti ya TANU kuwa mkoa wake, Bukoba unajitoka kutoka EAMWS.<sup>69</sup> Ghafila Adam Nasibu akawa mtu mashuhuri wa kufahamika nchi nzima, magazeti ya TANU na radio ya Serikali ikaanza kumjenga haiba yake pamoja na kutangaza kile kilichokuja kujulikana kama 'mgogoro' wa Waislamu. Magazeti ya TANU chini ya Wiliam Benjamin Mkapa yakawa yamepata habari ya kushabikia: Radio ya Serikali na magazeti ya TANU kwa pamoja yakawa yanatoa habari kwa uzito wa hali ya juu kuhusu kujitoka kwa Bukoba katika EAMWS. Magazeti ya TANU yakiwa yamesheheneza vichwa vya habari na maelezo ya mgogoro na picha za Adam Nasibu zikipamba kurasa zake za mbele.<sup>70</sup>

Ilikuwa baada ya magazeti na radio kutangaza na kuandika habari hizo ndipo Waislamu kwa mara ya kwanza wakaja kutanabahi kuwa walikuwa wanakabiliwa na 'mgogoro' mkubwa wa

nchi nzima. Lakini matatizo yalikuwa yameanza hasa toka siku ile watu wa Dar es Salaam waliposoma maulidi mbili mwezi wa Juni, 1968. Siku tano baadae, yaani tarehe 22 Oktoba, 1968 Sheikh Juma Jambia mwanakamati wa halmashauri kuu ya EAMWS kutoka Tanga na yeye akatangaza kuwa Tanga inajitoka katika EAMWS.<sup>71</sup> Mwenyekiti wa EAMWS Tewa Said Tewa akamfahamisha Sheikh Jambia kuwa uamuzi wake ulikuwa ni uamuzi wa mtu mmoja. Jibu la Sheikh Jambia lilikuwa ni kutoa taarifa kwa vyombo vya habari kuvifahamisha uamuzi huo. Sheikh Jambia alitoka taarifa hiyo pamoja na mtu mmoja aliyefahamika kwa jina la Abdi Matunga. Haukupita muda mrefu, Iringa nayo ikatangaza kuwa inajitoka kutoka EAMWS. Uongozi wa EAMWS kwa haraka ukaitisha mkutano kujadili hali ile mpya iliyojitokeza. Vyombo vile vya habari, Uhuru na The Nationalist ambavyo vilikuwa vikiwatumikia wale waliodai kujitenga na EAMWS, sasa vikawa havitaki kutoa au kuandika habari za viongozi wa EAMWS ambao walikuwa wanapigania umoja wa Waislamu. Hapa ikawa ni wazi kuwa Serikali ilikuwa inatumia vyombo vya habari, yaani magazeti yaliyokuwa chini ya TANU na radio ya Serikali kuwahujumu Waislamu na EAMWS. Uongozi wa EAMWS ulipokuja kutanabahi ni nani walikuwa nyuma ya hujuma ile wakawa wamebaini hatari iliyokuwa ikiwakabili, kwa ajili hii basi waliwageukia Waislamu kutaka msaada wao.

Kile kikundi kilichokuwa kikitaka kujitenga kilitoa sababu nyingi za uamuzi wao huo. Lakini katika sababu zao zote kubwa zaidi ilikuwa katiba ya jumuiya ile ilikuwa haipo sawa na uongozi wa nchi. Walidai kuwa katiba iwe ya Kitanzania na Aga Khan asiwe patroni. Vilevile wakadai kuwa Katibu Mkuu wa jumuiya awe Mwafrika Muislamu. Wakati ule katibu alikuwa Abdul Aziz Khaki, Muismailia na Mtanzania wa asili ya Kihindi. Kikundi kile vile vile kilitaka kujua vyanzo vya misaada kwa Waislamu na misaada hiyo ilikuwa ikitumikaje.<sup>72</sup> Dai lingine na hili likawa zito kwa uongozi wa EAMWS lilikuwa kuwa 'viongozi wa EAMWS wawe wale

wanaoamini malengo ya TANU, wale ambao wanapinga TANU hawafai kuwa viongozi wa Waislamu wa Tanzania.<sup>73</sup> Madai haya yalifikishwa makao makuu ya EAMWS na Adam Nasibu, Muhammad Zoharia na Hamisi Kayamba. Tewa Said Tewa akiongoza Kamati Kuu ya EAMWS alijaribu kuzungumza na viongozi wale lakini hawakutaka maelewano ya aina yoyote. Siku ya pili baada ya kutoa madai haya Adam Nasibu aliitisha mkutano wa waandishi wa magazeti na ndipo akaeleza kuwa Bukoba imejitoa EAMWS.

Uislamu una kanuni na sheria zake za msingi ambazo ndizo zingewaongoza Waislamu katika maisha yao ya kila siku. Madai yaliyotolewa na kile kikundi hayakuwa madai yenye uzito mkubwa kiasi cha kusababisha farka kubwa kiasi kile kwa sababu madai yale yote yangeliweza kujibiwa kwa urahisi kabisa. Kulikuwa na baadhi ya madai ambayo yalikuwa hayajadiliki kwa sababu ya mafunzo ya msingi ya Uislamu. Tatizo la katiba lingeliweza kujadiliwa na kumalizwa katika vikao vya kawaida. Lakini kuhoji rangi ya Muislamu hilo halijadiliki kwa kuwa Uislamu haubagui rangi ya mja kwa kuwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume na mafunzo ya Qur'an Tukufu. Ilikuwa wazi kuwa wale waliokuwa wakidai utengano katika EAMWS hawakuwa watu wajinga kiasi cha kukosa kujua kuwa hayo waliyokuwa wakidai yalikuwa kinyume na Uislamu. Kwa kuwa walikuwa wanang'ang'ania kujitoa katika EAMWS, ilikuwa sasa kitu dhahiri kuwa hiki kikundi cha Waislamu waliojawa na 'hamasa za kizalendo' walikuwa na mpango maalum uliokuwa ukisaidiwa na Serikali wa kuvunja umoja wa umma wa Kiislamu ili Waislamu wadhoofike na wawe hawana nguvu tena katika siasa.

Hata hivyo, tarehe 14 Novemba, 1968, Baraza la EAMWS la Tanzania liliitisha mkutano wa wajumbe kutoka mikoa yote ya Tanzania kujadili 'mgogoro'. Pamoja na waliohudhuria ni wajumbe kutoka mikoa ambayo tayari ilikuwa imekwishajitenga na EAMWS.

Mkutano huu ulifanyika katika shule ya Kiislamu ya Kinondoni. Hapajatokea katika historia ya Uislamu Tanzania mkutano kama ule. Uongozi ulikuwa unaingia katika chumba cha mkutano tayari umeshajeruhiwa vibaya sana na propaganda za magazeti ya TANU na radio ya Serikali. Katika moja ya shutuma ambazo zilikuwa zikiuandama uongozi wa EAMWS ilikuwa ni matumizi mabaya ya fedha za jumuiya.

Akifungua mkutano ule Tewa aliwatahadharisha wajumbe kuwa makini katika lolote watakaloamua kwa kuwa endapo wajumbe watashindwa kuafikiana basi matokeo yake ni kuvunjika kwa EAMWS, umoja wa Waislamu na mwisho wa miradi yote ya elimu pamoja na ujenzi wa Chuo Kikuu.<sup>74</sup> Hisia kali zilitawala mkutano huu na baadhi ya wajumbe wanawake walikuwa wakilia hasa pale baadhi ya wajumbe walipokuwa wakitoa michango yao katika mjadala walipokuwa wakisoma aya za Qur'an Tukufu na kueleza fadhila za kupigana jihad dhidi ya madhalimu na wanafiki. Hisia hizi kali zilitokana na ukweli kuwa wajumbe walikuwa wanafahamu kuwa wale wenzao waliokuwa wakidai kujitenga walikuwa wakitumiwa na madhalimu wala hawakuwa wakiyafanya yale kwa ajili ya Allah(s.w) na Mtume wake(s.aw). Mwenyekiti wa mkutano Tewa Said Tewa, aliahirisha mkutano hadi siku ya pili ili wajumbe wapoe na watoe mchango wakiwa katika hali ya utulivu.

Katika wajumbe ambao walisimama kidete kutetea umoja wa Waislamu walikuwa Sheikh Issa Mchowera kutoka Mtwara, Bilali Rehani Waikela, Hassan Johari na Sheikh Abdallah Said kutoka Kigoma.

Mkutano uliamua kuunda Tume ya Uchunguzi ya watu saba, kuchunguza chanzo cha 'mgogoro' na kisha itoe taarifa. Tume ya Uchunguzi ya Waislamu ilikuwa na wajumbe wafuatao: Mussa Kwikima (Dar es Salaam), Rajab Ukwaju (Mara), Dr. Hussein Lweno (Dar es Salaam), Mussa Nabahani (Lindi), Bilali Rehani



Waikela (Tabora), Abdul Karim (Tanga) na Khamis Khalfani (Dodoma).

Mussa Kwikima kijana mwanasheria alichaguliwa kuwa katibu wa tume hiyo ya uchunguzi. Wakati huo mikoa tisa ilikuwa tayari imeshajitenga na EAMWS na magazeti ya TANU yakawa tayari yamejenga 'mgogoro' ule kufikia hali ya kuonekana kuwa ni 'mgogoro' wa taifa zima ambao kila mtu anaweza kuingilia na kusema atakalo. Magazeti ya TANU yakawa yanaandika na kuchapisha mambo ya EAMWS kama yanavyotaka, wakizidi kutia chumvi katika ugomvi ambao tayari ulikuwa umeshaleta hofu na farka kubwa katika jamii. Inasemekana viongozi wengine wa EAMWS walikuwa wakiambiwa wajitoe huku wameshikiwa bunduki.

## **Mvutano wa Nyerere, Tewa na Bibi Titi Kuhusu EAMWS, 1968.**

Ili tume ya uchunguzi ya Waislamu iweze kufanya kazi yake vyema na bila upendeleo, ilikuwa lazima kwanza ile tume iionbe Serikali izuie propaganda iliyokuwa ikiendeshwa na wale waliokuwa wamejitenga na EAMWS, wakitumia jukwaa la radio ya Serikali na magazeti ya TANU. Tume ya Waislamu ilikutana na Waziri wa Habari na Utangazaji, Hasnu Makame, ofisini kwake tarehe 20 Novemba, 1968, kujadili tatizo lile. Hii haikusaidia kitu. Propaganda dhidi ya uongozi wa EAMWS iliendelea kwa nguvu zote. Mashambulizi kutoka pande tatu yaliyopangwa vyema yalikuwa kazini. Benjamini Mkapa akitumia gazeti la Nationalist ataandika habari yoyote ya Adam Nasibu, Martin Kiama alitumia Radio Tanzania kutoa habari ile kama habari muhimu na kuitangaza kutwa nzima huku ofisi ya Rais ikiwa kimya kwa fitna ile. Lile kundi la waliojitenga na umma wa Waislamu, Adam Nasibu akiwa kama msemaji wao mkuu wakati mwingine kwa mastaajabu makubwa wakawa wanakiuka hata misingi ya akida ya Tanzania,

wakitoa madai ya ubaguzi wa rangi, wakikazania lazima EAMWS ivunjwe. Adam Nasibu alinukuliwa na The Nationalist akisema kuwa:

*“Waislamu lazima wafahamishwe kwa nini East African Muslim Welfare Society iwe na katiba isiyoendana na mwelekeo wa nchi. Hatujui nafasi ya Aga Khan katika nchi yetu na ndiyo maana tunamkataa”.*<sup>75</sup>

Lakini cha kushangaza zaidi ilikuwa ule ukimya wa Serikali kuhusu matakwa ya kundi la Adam Nasibu lililokuwa likidai kuwa Waislamu wachanganye dini na siasa katika suala hili, wakati ilikuwa ikijulikana wazi kuwa kufanya hivyo ni mwiko mkubwa katika siasa za Tanzania.

Haya yote mbali, lile la kushangaza hasa na kitu ambacho kilikuwa kigeni katika Tanzania ilikuwa yale madai ya kuingiza ubaguzi wa rangi katika siasa za Tanzania. Ilikuwa inastaajabisha kuona magazeti ya TANU yaliyokuwa na sifa ya kuheshimu haki za binadamu yakichapisha na kuzipa uzito wa hali ya juu habari za kundi dogo la Waislamu waliokuwa wanawalaumu Waislamu wenzao wa Kiismailia kwa kutozaliwa weusi. Miaka kumi iliyopita watu wa Tanganyika, Waislamu wenyewe waliokuwa ndiyo walioanzisha na kujenga TANU, walipambana vikali dhidi ya siasa za kibaguzi za Zuberi Mtemvu na chama chake cha African National Congress. Mtemvu alishindwa na matokeo yake ikawa Tanganyika kuwa na Serikali ya watu wote isiyobagua rangi na ikitawala raia wa rangi zote kwa misingi ya haki. Kwa ajili hii nchi ikawa haina msugvano kwa ajili ya ubaguzi wa rangi.

Haya matokeo mapya yalikuwa hayaendani na misingi ya TANU. Ilipofikia hali hii, Rais wa EAMWS, Tewa Said Tewa na makamo wake Bibi Titi Mohamed, waliamua kulipeleka suala hili kwa Julius Nyerere, Rais wa Tanzania na mwenyekiti wa TANU, chama tawala. Watu hawa walikuwa wakichekeana jino pembe.

Lakini ili tuelewe chanzo cha uadui huu inatulazimu turudi nyuma hadi mwaka 1963, katika siku za mwanzo za uhuru, katika mkutano wa Halmashauri Kuu ya TANU uliofanyika Ukumbi wa Karimjee. Kama ilivyokwishaelezwa hapo mwanzoni kuwa mwaka 1963 ulikuwa mwaka wa mambo mazito. Ilikuwa ndiyo mwaka ambao Kanisa Katoliki liliteua wagombea wake wapambane na wagombea wa TANU waliokuwa Waislamu katika uchaguzi wa Serikali za mitaa kule Kigoma na Bukoba. Ulikuwa ndiyo mwaka ambao Rais wa TANU, Nyerere alipogombana na EAMWS kupitia Bilali Rehani Waikela. Mwaka wa 1963 ndiyo ulikuwa mwaka ambao Halmashauri Kuu ya TANU ilivunja Baraza la Wazee wa TANU lililokuwa limetawaliwa na Waislamu kwa madai kuwa baraza hilo lilikuwa 'likichanganya dini na siasa'. Mwaka 1963 ulikuwa mwaka muhimu kwa Halmashauri Kuu ya TANU kwa sababu ulikuwa mwaka ambao ilifanya maamuzi nyeti ya kidini. Mwaka ule Bibi Titi na Nyerere walishambuliana kwa maneno ndani ya Halmashauri Kuu ya TANU kuhusu jambo jingine tena la dini lililokuwa likihusu EAMWS.

Wanakamati wawili wa Halmashauri Kuu ya TANU, Selemani Kitundu na Rajab Diwani, waliomba Halmashauri Kuu ya TANU imjadili Aga Khan na nafasi yake kama patroni wa EAMWS. Kitundu na Diwani walidai kuwa wana habari Aga Khan anataka kuitawala Tanganyika kupitia Waislamu na EAMWS. Kwa ajili hii basi wakapendekeza EAMWS ifungiwe. Nyerere aliwaunga mkono Selemani Kitundu na Rajab Diwani. Bibi Titi akasimama kishujaa dhidi ya Diwani, Kitundu na Nyerere, akasema hakuna kati yao aliyekuwa na haki ya kuifungia jumuiya yoyote ya Waislamu. Kama walikuwepo watu ndani ya EAMWS ambao walikuwa wanakwenda kinyume na sheria basi watu hao wapelekwe mahakamani na sheria ichukue mkondo wake. Bibi Titi akaendelea kusema kuwa EAMWS imekuwepo kabla ya TANU na siku zote imekuwa ikitoa huduma kwa Uislamu. Inasemekana hasira zilipanda na kukawa na kutoleana maneno kati ya Bibi Titi na Nyerere. Bibi Titi akamwambia Nyerere yeye hamuogopi yeyote ila Allah.

Tuhuma zile dhidi ya Aga Khan na EAMWS hazikuweza kuthibitishwa na Halmashauri Kuu ya TANU ikaliacha jambo lile kwa wakati ule. Lakini Nyerere alikuwa amefedheheka. Kuanzia hapo akajenga chuki dhidi ya Bibi Titi na kumweka Rajab Diwani na Selemani Kitundu karibu yake. Katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1965 Bibi Titi na Tewa wakapoteza viti vyao kwa watu ambao walikuwa hata hawafahamiki – A.M. Mtanga na Ramadhani Dollah. Iliaminika kuwa Nyerere alikuwa anahusika na kuanguka kwa Bibi Titi na Tewa. Kuanzia hapo mambo yakawa dhahiri. Nyerere alikuwa amewatangazia vita wote wawili, Bibi Titi na Tewa. Nyerere alikuwa sasa ana imani kuwa wale maadui zake wawili walikuwa wamekwisha kisiasa. Lakini kilichokuwa kikimuudhi Nyerere zaidi ilikuwa taarifa ambazo alikuwa akizipata kuwa Tewa alikuwa akipewa mapokezi makubwa sana na Waislamu katika ziara zake huko mikoani kama Rais wa EAMWS.<sup>76</sup> Sasa mwaka wa 1968, Bibi Titi na Tewa walipokwenda kumuona Nyerere kuhusu jambo lililokuwa likiwahusu Waislamu, Nyerere alikuwa amejitayarisha vyema.

Viongozi hawa wawili wa Waislamu walimueleza Mwalimu masikitiko yao jinsi radio ya Serikali na magazeti ya TANU yalivyokuwa yakiandika habari kuhusu matatizo yale ya Waislamu. Walidai kuwa TANU ilikuwa ikichanganya dini na siasa. Waliokuwa wakimtahadharisha kuhusu jambo hilo hawakuwa wengine ila marafiki zake wa zamani na wa kutumainiwa, Tewa na Bibi Titi. Marafiki wa kutumainiwa kwa sababu Titi ndiye aliyemuunga mkono Nyerere katika siku za mwanzo za TANU, pale Suleiman Takadir, mmoja wa wazee wa TANU, aliposema kuwa TANU ilikuwa na Ukristo kama Mwalimu na Rupia, Rais na makamo wake walivyokuwa Wakristo. Yeye mwenyewe aliupa mzalendo nafasi ya mbele na Uislamu uwakawa unafuatia nyuma. Nyerere alijibu kwa mkato. ***'Mmeamua kunipiga vita, jiandaeni.'***<sup>77</sup>

Mwalimu Nyerere alikuwa anawaambia Tewa Said Tewa na Bibi Titi Mohamed uso kwa uso wajiandae kwa kile kilichokuwa

dhahiri: vita ya msalaba dhidi ya umoja wa Waislamu. Sheikh Suleiman Takadir aliyaona haya na aliomba TANU toka mwaka wa 1958 pawepo na uhakika kuwa Wakristo ambao walikuwa wanapanda juu ya migongo ya Waislamu na kuchukua uongozi hawatakuja kuwafanyia uadui Waislamu pale Waislamu watakapokuwa sasa wanataka kugawana madaraka ya kuongoza nchi sawa na Wakristo baada ya uhuru. Tewa Said Tewa, muasisi wa TANU, waziri katika Serikali ya kwanza ya uhuru, Balozi katika Jamuhuri ya watu wa China na Rais wa Baraza la Tanzania la EAMWS, pamoja na Bibi Titi, mwanamke aliyewakusanya wanawake wote nyuma ya Mwalimu Nyerere na TANU, walikuwa wakisemwa na Nyerere kama vile watoto wadogo wa shule waliokuwa watukutu kwa sababu tu, walikuja kumfahamisha Rais kuhusu kukiukwa kwa maadili ambayo ilihitaji yeye ashughulikie mara moja na kutoa uamuzi.

Ulipofika mwezi Oktoba, ‘mgogoro’ ukachukua mwelekeo mpya pale Makamo wa Rais wa Tanzania, Abeid Amani Karume, alipoishambulia EAMWS kuwa ni chombo cha unyonyaji.<sup>78</sup> Kutokea hapo Karume akawa anafanya mashambulizi na kutoa shutuma kwa EAMWS, wakati mwingine akijaribu kufafananisha uhusiano wa EAMWS na Waislamu katika mtazamo wa Ki-Marxist, akidai kuwa jumuiya ile kilikuwa ‘chombo cha makabaila wakubwa na kilikuwa chini yao kikiwanyonya watu wa chini’. Mgogoro ulipozidi kukua mashambulizi yakahama sasa kutoka EAMWS na kuhamia kwenye mafunzo ya msingi katika Qur’an Tukufu. Katika mkutano wa hadhara Zanzibar, Karume alitoa changamoto kwa Muislamu yeyote ajitokeze bila ya woga kupinga kauli zake mbili kuwa ‘Hakuna tofauti kati ya Uislamu na Ukristo’, na ‘Kufunga siyo lazima’.

Lakini juu ya mashambulizi dhidi ya uongozi wa Waislamu kutoka Serikalini, Nyerere alikuwa hana uwezo wa kumgusa Mufti Sheikh Hassan bin Amir licha ya kuwa alishaonesha kukosana na

Serikali mara tu baada ya uhuru pale Kanisa Katoliki lilipotoa vitu vya kukumbuka uhuru vilivyokuwa vimenakshiwa picha za Kikristo. Sheikh Hassan bin Amir alikereka na hili na hasa pale George Kahama, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, alipokwenda Italia kuweka uhusiano baina ya Tanganyika na Vatikano. Kuanzia hapo, Sheikh Hassan bin Amir, kupitia *Daawat Islamiyya* na kwa kupitia wanafunzi wake waliokuwa wameenea nchi nzima alianza kuandika khutba za Ijumaa na kuzisambaza katika misikiti ya nchi nzima na khutba hizo zikawa zinasomwa katika sala ya Ijumaa. Ujumbe wake kwa Waislamu ulikuwa Waislamu watumie fursa iliyoletwa na uhuru kwa kujielimisha ili wagawanne madaraka sawa na Wakristo katika kuiendesha nchi. Sheikh Hassan bin Amir akaanzisha mfuko wa elimu ambao Waislamu walitakiwa kuchanga fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule. Kwa ajili ya kuingia kwake kati pale Nyerere alipotaka kuivunja EAMWS, Sheikh Hassan bin Amir akaonekana ni kikwazo kwa Ukristo kuukalia juu Uislam.<sup>79</sup>

Sheikh Hassan bin Amir alikuwa na nguvu sana kiasi cha kwamba si Nyerere au yeyote yule liyeweza kumgusa kwa wakati ule. Sheikh Hassan alikuwa kwenye siasa kabla ya vijana waliokuwa katika TANU na nafasi yake katika umma wa Kiislamu na uzalendo wake ulikuwa hauna shaka. Sheikh Hassan bin Amir aliingizwa TAA kwa mara ya kwanza mwaka 1950 na Abdulwahid Sykes akiwa mwanakamati katika Kamati ndogo ya siasa ya TAA. Kwa ajili hii basi, akawa mmoja wa wale waliotia sahihi ile memorandam iliyotayarishwa na TAA kwenda kwa Gavana wa Tanganyika, Edward Twining, kuhusu mabadiliko ya katiba ya Tanganyika. TANU ilipoasisiwa, Sheikh Hassan bin Amir alikuwa akiwakatia watu kadi za TANU msikitini huku akidarsisha. Baadhi ya wanachama shupavu wa TANU ambao Sheikh Hassan bin Amir aliwaingiza katika TANU ni Sheikh Mussa Rehani ambaye alipewa kadi yake ndani ya msikiti Kigoma. Wakati Nyerere alipokuja Dar es Salaam mwaka 1953, alimkuta Sheikh Hassan bin Amir

mwenyeji katika siasa. Baada ya uhuru Sheikh Hassan bin Amir alijiuzulu siasa, kutokana na kauli yake alisema kuwa, ili awatumikie Waislamu vyema.

Nyerere alifahamu fika kuwa haitakuwa rahisi kwake kumweka Sheikh Hassan bin Amir kizuizini kama alivyofanya kwa Waislamu wengine. Sheikh Hassan bin Amir alikuwa ndiye Mufti wa Tanganyika na Zanzibar na kwa ajili hii alikuwa na hadhi kubwa katika umma wa Waislamu. Halikadhalika haikuwa rahisi kwa yoyote kumkiuka Sheikh Hassan bin Amir na kuchukua uongozi wa Waislamu.

### **Kuasisiwa BAKWATA, 1968**

Hadi kufikia juma la kwanza la mwezi wa Desemba, mikoa mitatu kati ya kumi na saba ilikuwa tayari imeshajitenga kutoka EAMWS. Kile kikundi cha Adam Nasibu kikaunda kamati kwa ushirikiano na Kamati ya Maulidi ya Dar es Salaam Adam Nasib akiwa katibu na Sheikh Abdallah Chaurembo mwenyekiti. Kamati hii ikaitisha mkutano Ukumbi wa Arnatouglo tarehe 3 Desemba, 1968 kujadili '*mgogoro*'. Aliyetumiwa kutoa tangazo lile alikuwa katibu wa Kamati ya Maulidi na Swala ya Iddi, Y. Osman. Kundi la Adam Nasib lilikuwa na mchanganyiko wa watu waliokuwa wanaungwa mkono na Serikali, Adam Nasib akiwa kiongozi Halikadhalika kulikuwa na Waislamu waliokuwa na nafasi katika TANU kama Sheikh Abdallah Chaurembo na Juma Sued kiongozi wa TANU kutoka Bukoba. Ilikuwa wazi kuwa Serikali ilikuwa inamtayarisha Sheikh Abdallah Chaurembo kuchukua nafasi ya mwalimu wake na mtu aliyemfikisha pale alipo, Sheikh Hassan bin Amir. Ikawa sasa lazima Sheikh Hassan bin Amir aondolewe na kupelekwa Zanzibar ili lile kundi la Serikali chini ya Adam Nasibu liweze kuchukua uongozi wa Waislam bila ya kipingamizi chochote.

Wakati vurugu hizi zinaendelea, Kamati Kuu ya TANU ilikuwa ikifanya kikao chake Tanga. Adam Nasibu, Omari Muhaji, Sheikh

Abdallah Chaurembo na Saleh Masasi walipanda ndege hadi Tanga kwenda kushauriana na Kamati Kuu ya TANU jinsi ya kumaliza 'mgogoro' wa Waislamu. Ujumbe huu ulikwenda Tanga kuonana na Nyerere huku ukiwa na orodha ya Waislamu ambao kile kikundi cha Adam Nasibu kilitaka Serikali iwakamate na kuwatia kizuizini ili msugurano upate kumalizika. Dossa Aziz aliona Nyerere akipewa karatasi wakati kikao kikiendelea lakini hakufahamu ujumbe uliokuwamo ndani ya karatasi ile hadi hapo baadae. Alikuwa kutambua habari za karatasi ile baada ya majuma mawili kupita wakati alipofuatwa na jamaa yake mmoja na kumuomba aingilie kati ili rafiki yake aliyetiwa kizuizini na Nyerere aachiwe kutoka Jela ya Ukonga. Nyerere alipofahamishwa habari zile na Dossa, alisema kuwa yeye hakufahamu kuwa rafiki yake Dossa alikuwa katika orodha ile ambayo kwa umuhimu wa jambo lile ilibidi aletewe Tanga wakati wa mkutano wa Kamati Kuu. Kwa kejeli Nyerere akamwambia Dossa kuwa yeye huwa hachukuwi tabu ya kusoma majina ya watu anaowaweka kizuizini kwa kuwa anawaamini wale wanaofanya kazi ya kumletea majina yale.

Inspekta Jenerali wa Polisi, Hamza Aziz, mdogo wake Dossa alipopokea amri kutoka kwa Rais kupitia Waziri wa Mambo ya Ndani kuwa amkamate Sheikh Hassan bin Amir, hakuweza kuamini masikio yake. Alitaka afahamishwe sababu za kutaka kukamatwa Mufti, kiongozi wa juu kabisa katika safu ya uongozi wa Waislamu katika Tanzania. Alipoambiwa kuwa sababu ni kuwa anaijumu Serikali, Hamza Aziz alimwambia Waziri wa Mambo ya Ndani kuwa huenda kuna makosa katika amri ile. Alimfahamisha waziri kuwa yeye binafsi alikuwa anamfahamu mzee yule toka yeye Hamza alipokuwa mtoto mdogo. Akimfahamu Sheikh Hassan bin Amir kama mwalimu na mtu aliyeshiriki katika ukombozi wa Tanganyika. Msimamo wake, heshima na hadhi yake mbele ya Waislamu ipo juu kabisa. Inspekta Jenerali wa Polisi alimwambia waziri kuwa haitawezekana kwake yeye kutii amri ile kwa sababu yeye haamini kuwa tuhuma zile dhidi ya Mufti Sheikh Hassan bin Amir ni za kweli. Nyerere alifahamishwa na Waziri wa Mambo ya



Ndani kuwa Inspekta Generali wa Polisi, Hamza Aziz amekataa kutii amri yake ya kumkamata Mufti. Nyerere alitoa amri kwa watu wa Usalama wa Taifa kumkamata Sheikh Hassan bin Amir. Hii ilikuwa ni kinyume na utaratibu kwa kuwa Usalama wa Taifa hawana mamlaka ya kukamata watu.

Usiku wa manane siku hiyo hiyo Sheikh Hassan bin Amir alikamatwa na makachero wa Usalama wa Taifa akapelekwa uwanja wa ndege na kurudishwa Zanzibar.<sup>80</sup> Inaelekea kulikuwa na mpango uliokuwa umetayarishwa kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kumpokea Sheikh Hassan bin Amir. Inasemekana mara kadhaa Karume alipata kumueleza Sheikh Hassan bin Amir kuwa Nyerere alikuwa hamtaki nchini kwake na akawa anamshauri arudi nyumbani Zanzibar. Sheikh Hassan alikataa ushauri ule hadi alipokamatwa na kurudishwa kwa nguvu. Karume alimpa Sheikh Hassan bin Amir hadhi zote alizostahili kama ulamaa na akamruhusu kuendesha darasa zake. Lakini Zanzibar ilikuwa imebadilika. Mapinduzi ya mwaka 1964 yalikuwa yameingiza katika Zanzibar fikra potofu zilizokuwa zinapinga Uislamu. Karume mwenyewe alikuwa ametoa amri ya kuchoma vitabu vyote vya Uislamu. Nakala za Qur'an Tukufu zilichomwa moto pamoja na taka za mji. Muslim Academy chuo kilichokuwa kikisomesha masomo ya dini kilifungwa. Mashine za kuchapa kwa lugha ya Kiarabu zikatupwa kutoka Government Press.<sup>81</sup> Maulamaa wengi na wanafunzi wa Sheikh Hassan bin Amir walikuwa wamekimbia Zanzibar kwenda kuishi uhamishoni. Zanzibar haikuwa tena kitovu cha elimu na maarifa ya Uislamu. Sheikh Hassan bin Amir akawa sasa mfungwa katika nchi yake mwenyewe kwa kuwa hakuwa na ruhusa ya kuondoka visiwani hapo na kurejea Tanzania bara. Mara baada ya kukamatwa kwa Sheikh Hassan bin Amir, Adam Nasibu akatangaza kufanyika kwa mkutano ambao ulikuja kujulikana kama Mkutano wa Waislamu wa Taifa. Mkutano ambao ilitangazwa utafanyika Iringa kuanzia tarehe 12-15 Desemba, 1968. Agenda kuu ya mkutano ule ilikuwa kujadili katiba kwa ajili ya jumuiya mpya ya Waislamu.

Baada ya kukamatwa kwa Sheikh Hassan Bin Amir, gazeti moja la Kiingereza lilimfuata Tewa Said Tewa ili afanye mazungumzo nalo. Tewa alimfahamisha mwandishi kuwa kulikuwa na hofu juu ya maendeleo yanayofanywa na Waislamu na mikutano mikubwa ya Waislamu iliyokuwa ikifanyika nchi nzima. Waislamu waliokuwa na vyeo katika Serikali walikataa kabisa kuisaidia Tume ya Kwikima kwa njia yeyote wakidai kuwa kufanya hivyo ni sawasawa na kuchanganya dini na siasa. Waislamu hawa walikaa pembeni kama watazamaji huku Nyerere kwa taratibu akivunja uongozi wa EAMWS na kutayarisha watu wake kuwaongoza Waislamu. Kundi la Adam Nasibu lilikataa kukutana na Tume ya Kwikima. Maulamaa hawakuweza kufanya lolote kwa kuwa walikuwa wanajua fika kuwa aliyekuwa akivunja EAMWS hakuwa Adam Nasibu, yeye na wenzake walikuwa wakitumiwa tu. Kundi la Adam Nasibu lilikuwa halitaki chochote ila EAMWS ivunjwe na badala yake iundwe jumuiya itakayokuwa chini ya kivuli cha Serikali. Vilevile kukawa na uvumi kuwa Muislamu yeyote atakayejihusisha na shughuli za EAMWS atawekwa kizuizini na Serikali. Tume ya Kwikima haikuweza kupuuza vitisho hivyo kwa sababu Serikali ilishawahi kuwaweka vizuizini masheikh.

Tume ya Kwikima ilikuwa ikilifamu lile kundi la Adam Nasibu kuwa halikuwa na nguvu wala uwezo wa kuvunja EAMWS. Kufuatia kutangazwa kwa mkutano wa Iringa wa kundi la Adam Nasibu, Tume ya Kwikima ilitoa taarifa yake tarehe 11 Desemba–siku moja kabla ya mkutano wa Iringa kuanza.<sup>82</sup> Taarifa ambayo ilitolewa kwa Waislamu wote, iliitisha mkutano mkuu wa EAMWS ambao ulikuwa ufanyike mwezi Februari mwaka unaofuata kujadili na kutoa uamuzi wa mwisho kuhusu ‘mgogoro’.<sup>83</sup> Tarehe ya mkutano ilibadilishwa hapo baadae na kuwa Januari kutokana na umuhimu wa ‘mgogoro’ uliokuwa ukikabili EAMWS. Mhariri wa Gazeti la TANU baada ya kusoma taarifa ya Kwikima aliamua kutoa maoni yake kuhusu taarifa ile

kwa kusema kuwa haikuwa sawa.<sup>84</sup> Huu ulikuwa mpango uliosukwa mapema kuonyesha kuwa uongozi wa EAMWS ulikuwa na ubadhirifu. Juma lile lile Aga Khan ambae ndiye aliyekuwa akishambuliwa na kundi la Adam Nasibu, baada ya kutambua kuwa EAMWS isingeweza kamwe kuokolewa, akiwa Paris, Ufaransa alijiuzulu nafasi yake kama mlezi(patron) wa EAMWS.<sup>85</sup>

Wakati Tume ya Waislamu inasubiri mawazo ya Waislamu sasa kundi la Adam Nasibu wakijionesha wazi kuwa Serikali na TANU ilikuwa nyuma yao, lilikutana kwa ajili ya kile walichokiita Mkutano wa Waislamu wa Taifa ulioanza tarehe 13 Desemba, 1968. Serikali ikifanya kazi nyuma ya pazia ilijitahidi sana kuhakikisha kuwa mkutano ule unafanikiwa. Serikali ikitumia idara ya usalama ndiyo iliyotoa fedha za kufanyia mkutano ule, ikatoa vyombo vyake vya habari kwa ajili ya kuutangaza vizuri na ukatoa ulinzi kwa wajumbe wote. Operesheni hiyo iliendeshwa na Rashid Kayugwa Afisa wa Usalama Taifa, Dar es Salaam ambaye alipewa kazi ya kudumisha mawasiliano kati ya kundi la Adam Nasibu na Serikali. Kayugwa ndiye aliyekuwa akielekeza kundi la Adam Nasibu mbinu za propaganda na nini kifanyike na kwa wakati gani ili kuvunja umoja wa Waislamu. Kayugwa alikuwa amepata mafunzo yake ya ukachero Israel, Checkoslovakia na Marekani. Katika kuhakikisha mafanikio ya mkutano wa Iringa, Kayugwa ambae ni mzaliwa wa Iringa alipendekeza mkutano wa Waislamu wa Taifa ufanyike Iringa kwa kuhofu vurugu na upinzani kutoka kwa Waislamu wa Dar es Salaam.

Bwana Rashid Kayugwa baada ya kusoma kitabu cha Padri John Sivalon kilichoeleza kuwa Kanisa baada ya uhuru liliendesha hujuma dhidi ya Uislamu na Waislamu kwa kupitia Serikali, ndipo ilipomdhihirikia ukweli; kuwa alipokuwa akitumiwa kuhujumu EAMWS hakuwa akitumikia Serikali kama alivyokuwa anadhani bali alikuwa akilitumikia Kanisa. Kama kuomba maghufira kwa Mwenyezi Mungu, aliamua kueleza mchango wake katika

kuwahujumu Waislamu na Uislamu ili iwe fundisho na onyo kwa Waislamu watakaokuwa katika utumishi wa vyombo kama hivyo siku za usoni. Kabla ya kufa kwake alieleza masikitiko yake kwa kukandamizwa kwa Waislamu na akatoa mfano wake mwenyewe wa kutopandishwa cheo katika Usalama wa Taifa kwa sababu tu yeye alikuwa Muislamu. Wajumbe waliohudhuria mkutano wa Iringa walikuwa kama mia mbili. Mkutano huu ulihudhuriwa na Waislamu waliokuwa na vyeo katika Serikali na TANU, Waislamu waliokuwa wakuu wa wilaya na mikoa na Waislamu wenyeviti wa TANU. Waislamu wote wenye majina walialikwa, pamoja na Waislamu waliokuwa katika halmashauri kuu ya TANU na baadhi ya wajumbe wa mkutano walitoka Zanzibar. Ulikuwa mkutano wa wanasiasa Waislamu ambao ukitoa majina yao walikuwa hawana chochote katika Uislamu. Lakini uzito wa mkutano huu ulitokana hasa na kuwa ulikuwa mkutano ambao ulitawaliwa na Waislamu waliokuwa hawapendezi mbele ya macho ya umma wa Kiislamu. Ni ukweli usioweza kupingika kuwa kama mkutano ule ungelikuwa hasa umetayarishwa kwa ajili ya kumtumikia Allah(s.w) ni wazi ungehudhuriwa na Waislamu wa kweli na wenye historia ya unyenyekevu na mapenzi kwa dini yao. Waislamu wa sifa hizi hawakuwepo katika mkutano ule ukimtoa Sheikh Mohamed Ramia wa Bagamoyo na wengine wachache ambao kwa kutotambua mambo waliitika mwito. Mkutano ulifunguliwa na Makamu wa kwanza wa Rais Abed Aman Karume na kufungwa na Makamu wa pili wa Rais Rashid Mfaume Kawawa. Katika hotuba yake ya ufunguzi Karume alisema maneno haya:

*“Dini haiwezi kuwa nje ya siasa kwa sababu siasa ndiyo damu inayoipa jamii uhai wake. Wakati wa ukoloni wananchi na dini zao zilikuwa chini ya utawala wa wageni. Hivi sasa watu wamevua mabaki ya ukoloni pamoja na kutawaliwa kwa misingi ya dini. Kuanzia sasa uongozi wa dini lazima uwe chini ya wananchi wenyewe bila ya kuongozwa na kiongozi kutoka nje”.*<sup>86</sup>

Mkutano wa Iringa ulipitisha katiba ya jumuiya mpya ya Waislamu, katiba ambayo ilikuwa sawasawa na katiba ya TANU. Hivi ndivyo Baraza Kuu la Waislamu Tanzania, BAKWATA, lilivyoundwa. BAKWATA ikamchagua Saleh Masasi, Muislamu tajiri na ambae alikuwa kama mwenyekiti wa mkutano ule kuwa Mwenyekiti wa Taifa na Adam Nasibu akawa Katibu Msaidizi. Nafasi zote za juu katika BAKWATA kama ilivyotegemewa zilichukuliwa na kundi la Adam Nasibu, kundi ambalo toka mwanzo lilikuwa likidai kuvunjwa kwa EAMWS. Uongozi wa BAKWATA uliomba Serikali itambue jumuiya hiyo mara moja na ipige marufuku EAMWS kama jumuiya isiyo halali na mali zake zizuiwe. BAKWATA ilitoa maazimio kadha lakini azimio namba nne ndilo hasa linafaa kuelezwa. Azimio hilo liliomba Serikali, TANU na ASP kuwatazama na kufanya uchunguzi wa kina kwa viongozi wote wa EAMWS, hasa Rais, Makamo wa Rais, Katibu wao na baadhi ya viongozi wa mikoa na wilaya ambao wana chuki na hii jumuiya mpya.<sup>87</sup> Uongozi wa BAKWATA katika ushindi wao hawakutaka salama na maelewano na Waislamu wenzao katika EAMWS wala kuwaonea huruma kama Uislamu unavyofundisha, bali ulitaka chama na Serikali ya kitwaghuti viwaandame, hasa wale waliokuwa viongozi.

Baada ya kuundwa BAKWATA, ili kuondoa wasiwasi na kuwarudishia imani Waislamu, Katibu wa Tume ya Waislamu, Mussa Kwikima alitoa taarifa iliyosema:

*“Hakuna anaeweza kutishia kuwepo kwa EAMWS isipokuwa wanachama wake, sheria na Serikali, lakini si watu binafsi hata ikiwa mikoa yote kumi na saba ikijitoe haitamaanisha kuwa jumiya imekufa kwa kuwa kuwepo kwake hakutokani na kuwepo kwa mikoa hiyo kama wanachama isipokuwa kuwepo kwa wanachama wake, Waislamu”.*<sup>88</sup>

Wakati ilipotoka taarifa hii BAKWATA ilikuwa bado haijaandikishwa rasmi na Msajili wa Vyama. Kisheria ilikuwa haiwezekani kwa kundi la Adam Nasibu kuunda jumuiya mpya iliyokuwa na malengo sawa na jumuiya ambayo tayari ishaandikishwa. Kwa muda wa siku tatu BAKWATA na EAMWS zikawepo kwa wakati mmoja. Iiionekana kama kwamba EAMWS itashinda vitimbi vya Serikali na vya kundi la Adam Nasibu.

Tarehe 19 Desemba, 1968 Serikali kama vile imegutushwa na taarifa ya Kwikima, iliipa BAKWATA Certificate of Exemption na kuifungia EAMWS.<sup>89</sup> Waziri wa Mambo ya Ndani Said Ali Maswanya kwa niaba ya Serikali alitoa taarifa fupi:

*“Waziri wa Mambo ya Ndani kwa kuamriwa na Rais anatangaza kuwa tawi la Tanzania la East African Muslim Welfare Society na Baraza la Tanzania la East African Muslim Welfare Society ni jumuiya zisizotambulika kisheria chini ya kifungu 6 (i) cha Sheria ya Vyama”.*<sup>90</sup>

Kwa tangazo hilo la Rais wa Tanzania, Julius Nyerere, Waislamu walinyimwa nafasi ya kukutana na kuzungumza kuhusu tatizo ambalo kwa kweli liliwahusu Waislamu peke yao. Kwa ajili hii basi Waislamu walinyimwa nafasi ya kujadili na kulitolea uamuzi tatizo hilo.

Viongozi wa EAMWS waliitwa mbele ya Kabidhi Wasii ambae ndiye alikuwa amekabidhiwa na Serikali jukumu la kusimamia shughuli za kufunga rasmi shughuli za EAMWS. Viongozi walifahamishwa kuwa chini ya sheria ya vyama, mali zote za EAMWS zitauzwa na madeni yatalipwa kutokana na fedha hizo na fedha zitakazobaki watapewa wanachama. Serikali ilikuwa haiwezi kufanya kama sheria ilivyokuwa imeelekeza. Ilikuwa jambo zito sana kwa Serikali ya Nyerere kuonekana anasimamia kuuzwa kwa mali za Waislamu. Viongozi wa EAMWS walipoitwa kwa Kabidhi Wasii mara ya pili walifahamishwa kuwa Serikali

imebadilisha mawazo yake kutekeleza amri kama sheria inavyosema kwa ajili hiyo basi imefanya mabadiliko ya sheria ya vyama ambayo inaiwezesha sasa kutoa mali ya EAMWS na kuikabidhi BAKWATA. Hivi ndivyo mali za EAMWS zilivyochukuliwa na kupewa BAKWATA bila ya ridhaa ya Waislamu wenyewe. Hivi ndivyo shule zote zilizojengwa na EAMWS pamoja na mradi wa Chuo Kikuu cha Kiislamu, ilipoangukia katika mikono ya kundi la Adam Nasibu.

BAKWATA haikuwa na uwezo wa kuendesha mipango yoyote na taratibu za shule na miradi yote ya elimu ikafikia na mwishowe kufa kabisa. Hivi ndivyo halikadhalika moto wa Waislamu uliowashwa kwa kupatikana kwa uhuru walioupigania ulivyozimika. Huu ukawa ndio mwisho wa kile kilichokuwa kikijulikana kama “mgogoro” wa Waislamu. Mgogoro ambao ulianza pale Bwana Adamu Nasibu alipofanya maandamano katika mitaa ya Bukoba akimuunga mkono Julius Nyerere na Azimio lake la Arusha na ukaishia kwa mwalimu huyu akiwa na nafasi ya juu katika jumuiya ya Kiislamu ambayo ilikuwa ikichukiza machoni mwa Waislamu. Adamu Nasibu alianza kazi yake kwa kuwashutumu Waislamu. Katika mkutano na waandishi wa habari, Adam Nasibu aliomba TANU na ASP kujikinga na watu wanaohujumu umoja wa nchi kupitia dini. Akaendelea na kusema kuwa BAKWATA ni sawa na Baraza la Kikristo la Tanzania.<sup>91</sup>

Mjumbe mmoja wa Tume ya Waislamu Mussa Kwikima anastahili kuelezwa habari zake. Mussa Kwikima mwaka 1968 alikuwa ameteuliwa kuwa jaji na Rais Nyerere. Yeye ndiye hasa alikuwa nguvu kuu katika tume ya Waislamu. Wakati alipojitolea kuisaidia tume katika kupambana na kundi la Adam Nasibu, Waikela alimuonya kuhusu hatari ambayo ingemkabili yeye mwenyewe binafsi na kazi yake. Kwikima alijibu kuwa umoja wa Waislamu ni muhimu kuliko maslahi yake binafsi. Ilipoundwa BAKWATA na hapo kuwa ndiyo mwisho wa ‘mgogoro’, Kwikima

aliamishwa kutoka Dar es Salaam na kupelekwa Mwanza kama Hakimu Mkazi na Rais Nyerere akamvua madaraka ya ujaji wake.<sup>92</sup>

Kilichobakia baada ya kuvunjika kwa EAMWS ilikuwa ni kujaribu kuiweka BAKWATA katika mikoa kama jumuiya inayowakilisha Waislamu wote wa Tanzania Bara. Mwaka mzima wa 1969 Adam Nasibu na kamati ya watu wanne walitembea katika mikoa wakiahidi msaada wa fedha kwa katibu yeyote wa zamani wa EAMWS ambae atashirikiana na BAKWATA makao makuu kuisaidia kufungua ofisi katika mkoa wake. Waislamu waliipuuza BAKWATA. Tabora ambayo haikujitoa katika EAMWS, Serikali iliwaruhusu Adam Nasibu na kikundi chake kufanya mkutano wa hadhara. Kabla Adam Nasibu hajahutubia Waislamu, Maulid Kivuruga, mmoja wa wakongwe wa *African Association* na muasisi wa TANU Tabora, alipanda jukwaani kwa niaba ya Waislamu wa Tabora na kuweka sharti kuwa Waislamu wangukuwa tayari kumsikiliza Adam Nasibu endapo Waikela mjumbe wa Tume ya Waislamu iliyokuwa ikitafuta sulhu na yeye angeruhusiwa na Serikali kuwahutubia Waislamu ili aeleze upande wa pili wa kisa kile. Kivuruga alisema kuwa Waislamu wanaomba sharti hili likubaliwe kwa sababu katika Uislamu panapotokea mgogoro basi mpatanishi ni lazima asikilize pande zote mbili. Sharti hili lilikataliwa na BAKWATA na Serikali. Palepale mbele ya waheshimiwa wa Serikali na viongozi wa BAKWATA, Waislamu wakaanza kuzomea huku wakitawanyika wakipiga takbir na wengine wakiitikia Allahu Akbar.

Siku chache baada ya tukio hili Waikela alitwa na Mkurugenzi wa Upelelezi wa Jinai kusailiwa kwa nini anaipinga BAKWATA. Wakiwa ndani ya chumba cha Tabora Hotel, Geoffrey Sawaya, Mkurugenzi wa C.I.D, alimpiga maswali Waikela na kutaka kujua kwa nini yeye hayuko tayari kushirikiana na Serikali kuipa nguvu na kuieneza BAKWATA. Sawaya akatoa hongo ya shilingi elfu



arobaini kwa Waikela ili asaidie kuimarisha BAKWATA. Waikela alikataa kupokea hongo ile. Sawaya akamtisha lakini Waikela hakutishika. Waikela aliwekwa ndani ya chumba kile akiulizwa maswali kwa kiasi cha saa nne na kisha akaamrisha kuweka sahihi yake katika makaratasi fulani. Hili alilifanya. Waikela hakufuatwa tena na Serikali. Ingawa kulikuwepo na juhudi za chinichini za kuipinga BAKWATA, juhudi hizi hazikushinda kwa kuwa BAKWATA iliweza kufungua matawi yake nchi nzima pamoja na Tabora. Wapo baadhi ya viongozi ambao hawakuweza kuhimili vishawishi vya kupokea ile hongo ya Serikali na kwa ajili hii walishirikiana na Serikali hivyo kuwezesha ofisi za BAKWATA kufunguliwa, hata kama zipo pale kwa jina tu. Kuangushwa kwa EAMWS kulisababishwa na watu watatu ambao wao ndiyo walikuwa mstari wa mbele kabisa Adam Nasibu, Sheikh Kassim Juma na Abdallah Chaurembo<sup>93</sup> na njama hii ikaungwa mkono na Rashid Kawawa na Abeid Amani Karume. Mkono wa Julius Nyerere na Kanisa Katoliki katika njama hii haukuonekana kabisa kama ilivyo kawaida katika njama zote za kupiga vita Uislamu na Waislamu Tanzania.

## **Athari ya BAKWATA kwa Waislamu na Uislamu**

Kama ilivyoielezwa EAMWS ilivunjwa 20/12/1968. Siku hiyo Rais wa Jamhuri ya Muugano wa Tanzania, wakati huo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alimwamuru Waziri wa mambo ya Ndani wa wakati huo, Bwana Said Ali Maswanya, kutoa amri ya kulipiga marufuku tawi la Tanzania la EAMWS chini ya kifungu cha 6(1) cha sheria ya kuandikisha vyama.

Kutokana na mazingira ya kuanza kwake BAKWATA imeshindwa kuwa ya manufaa kwa Waislamu katika kipindi chote cha uhai wake. Hii inatokana na sababu kuu zifuatazo:

**Kwanza**, Waislamu waliitambua BAKWATA kama ni chombo cha Serikali cha kuwadhibiti. Hivyo Waislamu walio wengi waliiofota BAKWATA na viongozi wake na kuichukia pia.

**Pili**, Hofu na chuki hiyo ilizidi kupata nguvu kutokana na vitendo vyenyewe vya BAKWATA. Kila Waislamu walipojitutumua kutaka kufanya jambo lolote la maana basi adui yao wa kwanza alikuwa BAKWATA.

**Tatu**, Pale ambapo Waislamu wamedhulumiwa haki zao BAKWATA kwa kawaida imekuwa haizipiganii haki za Waislamu. Kwa mfano Waislamu walipodhalilishwa na sungusungu Mwanza 1984 na kutakiwa kuliabudu jua, kuchapwa viboko na kuchanwa kwa Qur'an, Waislamu nchi nzima walikilaani kitendo hicho. Lakini Bakwata iliyakanusha madai ya watu wa Mwanza. Na katika kuishukuru BAKWATA gazeti la CCM, Uhuru 7/12/1984 liliandika hivi katika maoni yake:

*“Kufuatana na taarifa iliyotolewa na Sheikh Mkuu baada ya uchunguzi huo, ilidhihirika kwamba hakuna vitabu vya Qur'an vilivyochanwa na sungu sungu bali vilikuwepo vitabu vya aina nyingine. Ni vizuri kwamba BAKWATA ilifanya uchunguzi wa jambo hili na kupata uhakika kwa sababu bila ya hivyo, baadhi ya Waislamu wangeweza kuchochewa na maandishi yaliyotawanywa ambayo hayakuwa na ukweli wowote (uk. 4)”.*

Na Sofia Kawawa alipoikashifu Qur'an wale waliondamana Zanzibar walilaaniwa na BAKWATA! Wala BAKWATA haikutoa kauli yoyote ya kuilaani kauli ya Sofia Kawawa.

Serikali ya CCM imekuwa ikiendesha kampeni nyingi za kuangamiza maadili ya Uislamu na jamii kwa ujumla. Kampeni hizo ni kama sera ya idadi ya watu, elimu ya ngono kwa watoto wa skuli, ugawaji wa kondomu kwa watoto wa skuli, na kadhalika.

BAKWATA haijatoa kauli yoyote ya kulaani kampeni hizo. Aidha lipo tatizo la ufugaji na ulaji wa maguruwe kiholela bila ya kujali imani na uhuru wa Waislamu. BAKWATA haijathubutu kulikemea jambo hilo bali kinyume chake imekuwa ikishirikiana na maadui wa Uislamu. Mfano ni jinsi BAKWATA ilivyoshirikiana na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani A. Mrema kuwashambulia Waislamu wakati wa sakata ya uvunjaji wa mabucha ya nguruwe 1993. Jambo jingine ni juu ya mihadhara . Wakristo wakiishinikiza Serikali iwapige marufuku Waislamu wasihubiri hadharani kwa kisingizio kuwa wanakashifu dini nyingine, Mufti wa BAKWATA amekuwa akiungana na Maaskofu kutoa kauli mbalimbali za kuwasakama na kuwashitaki Waislamu Serikalini.

BAKWATA imekuwa ikishiriki waziwazi kuzuia na kuvuruga maendeleo ya Uislamu. Mfano ni kuvunjwa kwa shule za Kiislamu za seminari Kinondoni na Jumua mwaka 1982. Mfano mwingine ilivamia shule ya sekondari ya Bondeni Arusha na kuwafukuza waalimu Waislamu na kuweka Wakatoliki.

BAKWATA ilipoundwa ilirithi shule, miradi kadhaa na Taasisi nyingi za EAMWS. Ilichofanya BAKWATA ni ama kuua au kudumaza maendeleo ya miradi ya Uislamu. Aidha, toka imeundwa BAKWATA, haikuwahi kusajiliwa shule ya Kiislamu mpaka Marehemu Prof. Ali Kigoma Malima alipopata fursa ya kuwa Waziri wa Elimu kwa muda mfupi. Ukitaka kuanzisha shule unaambiwa lazima uwe chini ya BAKWATA. Ni Waziri Malima aliyewafunua macho Waislamu kuwa hapakuwa na sheria kama hiyo. Kila Waislamu walipotaka kufanya jambo lolote la maendeleo waliambiwa walete kibali cha BAKWATA. Wakienda BAKWATA haiwapi kibali hicho. Kwa hiyo kwa mahusiano na mawasiliano kati ya BAKWATA na Serikali miradi ya maendeleo ya Waislamu imedumazwa na kukwamishwa kwa kiwango cha kutisha.

BAKWATA imejishughulisha sana na kusimamia usalama wa nchi, ilhali Serikali inavyo vyombo vyake.

Kutokana na udhaifu huu Waislamu wengi wamejitenga na baraza hilo pandikizi(BAKWATA) na badala yake kumechipuka jumuiya nyingi sana za Kiislamu zilizosajiliwa Serikalini na ambazo hazijasajiliwa. Katika kipindi cha uongozi wa awamu ya pili, baada ya kung'atuka Mwalimu Nyerere.

## **Kuibuka kwa Vikundi Mbali Mbali Badala ya BAKWATA**

Kwa kipindi cha zaidi ya miaka kumi toka iundwe BAKWATA **15 Desemba,1968** hakukuibuka kikundi chochote cha Kiislamu kufanya kazi za Da'awah. Serikali ilifunga milango ya kusajili jumuiya za Kiislamu na kuipa BAKWATA ukiritimba wa kuwa chombo pekee kinachotambulika kuyashughulikia masuala ya Kiislamu.

Lakini BAKWATA kwa upande wake nayo ikawa haifanyi lolote la kuwaletea maendeleo Waislamu. Na kila aliyethubutu kuikosoia BAKWATA na pengine kutaka kufanya jambo lolote la Kiislamu bila ya kibali cha BAKWATA alifanyiwa fitna Serikalini.

Kuelekea mwisho wa miaka ya 1980 kulianza kuibuka jumuiya za Kiislamu ambazo zilifanya kazi bila kujali kuwa zina kibali cha BAKWATA au kusajiliwa na Serikali. Jumuiya hizo zilielekeza nguvu zake katika kuwaelimisha Waislamu na wakati huo huo kuishambulia BAKWATA kila inaponekana kuuhujumu Uislamu.

Jumuiya ambazo zilivuma sana ni Umoja wa Wanafunzi wa Kiislamu wa chuo Kikuu cha Dar es Salaam (MSAUD) na Warsha ya Waandishi wa Kiislamu (Warsha).

MSAUD japo ilikuwa ni jumuiya ya wanafunzi lakini ilifanya kazi kubwa ya kuwaelimisha na kuwaamsha Waislamu kupitia majarida; makala mbali mbali na kuandaa semina. Jumuiya ilikuwa macho kufuatilia matukio mbali mbali ya kisiasa na yale ya kijamii yanayougusa Uislamu. Aidha walikuwa wakifuatilia kauli

mbali mbali za viongozi wa BAKWATA na kuzitolea maelezo pale wanapoona wamekwenda kombo.

Kundi la Warsha lilijishughulisha zaidi na uandishi wa vitabu na makala mbali mbali za Kiislamu. Kama ilivyokuwa MSAUD Warsha nao walifuatilia kwa karibu sana shughuli za BAKWATA na kuwakosoa hadharani pale walipokwenda kombo.

Warsha ilikuwa ni kundi la vijana waliokuwa na ujasiri wa pekee. Walikuwa wa mwanzo kumsema na kumkosoa Nyerere na siasa zake hadharani. Waliandika na kusambaza makaratasi na makabrasha yaliyokuwa yakimshutumu Nyerere jinsi alivyokuwa akiwadhalilisha na kuwakandamiza Waislamu. Aidha walionyesha jinsi nchi hii ilivyokuwa ikiongozwa Kikristo.

Zaidi ya hivyo vijana wa Warsha walifanya kazi kubwa kuuelezea Uislamu kama mfumo sahihi wa maisha uliokamilika; kinyume na ilivyokuwa inafahamika kwa wengi kuwa Uislamu ni kuswali na kufanya Ibada nyingine maalumu tu. Walijaribu kuisafisha sumu iliyoenezwa na Mwalimu Nyerere kuwa Dini haichanganywi na siasa au Serikali haina dini. Katika kulifafanua hilo walitoa tafsiri sahihi ya dini ambapo walisema kuwa hata ujamaa wa Nyerere ni dini pia.

Waliandika vitabu juu ya mtizamo wa Uislamu juu ya Elimu, Mtizamo wa Uislamu juu ya Dini; Uchumi katika Uislamu n.k.

Warsha walifanya kazi kubwa kwani walifanikiwa kuingia ndani ya BAKWATA ambapo walileta mafanikio makubwa. Wakisihirikiana na Uongozi wa Bakwata walizigeuza shule za sekondari za Kinondoni na Jumuiya kuwa za Seminari. Aidha walianzisha gazeti la Muislamu ambalo lilikuwa likitoka kila mwezi.

Pamoja na kazi kubwa iliyokuwa inaonekana ikifanywa na kikundi hicho, hakikuwa na watendaji wengi wenye ujuzi. Utendaji ulikuwa wa hamasa bila ya kujali nguvu zake na zile za mpinzani.

Aidha hapakuwa na utaratibu wa kuwafunza, kuwalea na kuwachuja wanachama wake. Watu wakawa anaingia katika Warsha kiholela jambo ambalo baadaye lilisababisha migogoro ndani ya Warsha na kuathiri sana shughuli zake na hatimaye kuisambaratisha.

## **Sheikh Malik na Warsha**

Haiwezekani ikatajwa warsha bila ya kumtaja Sheikh Mohamad Hussein Malik. Sheikh Malik alifika Tanzania katika miaka ya 1970 akiwa Mwalimu wa shule ya Tambaza; kisha Kinondoni Muslimu. Pamoja na kusomesha shule za Sekondari alikusanya vijana wa Sekondari na Vyuho na kuwasomesha Uislamu katika mtizamo wa kiutekelezaji na usimamishaji Uislamu katika jamii kama mfumo pekee sahihi wa Maisha.

Akiwa mwanafunzi wa Sheikh Abul Ala Mauduud; Sheikh Mohamed Hussein Malik alifundisha Uislamu kwa mtizamo wa Qur-an na Hadith kuwa Uislamu ni utaratibu kamili wa maisha. Aidha kutokana na ufundishaji wake aliwawutia vijana wengi ambao aliwahimiza waandike vitabu na makala mbali mbali juu ya yale anayoyafundisha.

Sheikh Malik binafsi alisimamia kuanzishwa kwa Warsha ya Waandishi wa Vitabu vya Kiislamu katika Ofisi za Bakwata Kinondoni. Yeye binafsi aliandika kitabu cha “Islamiati”. Mwaka 1978 Warsha ilihamishiwa Magomeni na ikawa na malengo na muelekeo tofauti na ule wa awali. Kwanza jina jipya likawa Warsha ya Waandishi wa Kiislamu badala ya Warsha ya Wandishi wa vitabu vya Kiislamu. Kisha ikapewa sura ya kiharakati kuliko kubakia tu kwenye kuandika vitabu. Waanzilishi wa Warsha zote mbili ni wanafunzi wa Sheikh Malik wakiwemo Mtengwa Burhani Mtengwa, Musa Abdul-Rahmaani Mdidi; Mohamed Ramadhan Kassim, Suleiman Swalehe, Ali Kilima, Abubakari Mwarwiro, Mohamed Bakari, Ahmed Mbaraka na wengineo.

Katika ufundishaji wake, Sheikh Malik hakuwa na darasa moja maalum. Bali alikuwa akizunguka Vyuoni na Misikitini kwa siku tofauti tofauti katika wiki. Kwa mtindo huu aliwafikia watu wengi. Wanafunzi wake wa kudumu walikuwa wakimfuata kila penye darasa.

Haukupita muda mrefu maneno “*Uislamu mfumo wa sahihi wa maisha*” *Uchumi katika Uislamu, dini na ujamaa, kusimamisha Uislamu* n.k. yakaanza kusikika na kuwekwa katika maandishi.

Kufikia hapo maadui wa Uislamu ambao siku zote walikuwa wakifuatilia kwa karibu sana darsa za Sheikh Malik hawakuweza kuvumilia tena. Alipewa wiki moja kuondoka nchini na hakuruhusiwa kubadili fedha zake.

Lakusikitisha ni kuwa waliotumiwa kumjengea fitna Sheikh Malik ni Masheikh. Na hili lilidhihirika pale Sheikh Mohammad Ali alipokwenda kwa aliyekuwa Rais wakati huo Mwalimu Nyerere kulalamika kuwa inakuwaje Sheikh Malik afukuzwe bila ya kosa lolote. Nyerere alijitetea kuwa si yeye bali Masheikh ndio hawamtaki. Akamtajia na Orodha ya Masheikh waliohusika na fitina hiyo.

Sheikh Mohammad Hussein Malik aliamia Nairobi ambapo aliendelea kufundisha Uislamu katika Vyuo Vikuu mbali mbali na kuwa Mlezi wa Vijana wa Kiislamu wa Vyuo hivyo. Sheikh Malik ni Sheikh pekee aliyetoa mchango mkubwa sana katika kufundisha na kupandikiza fikra sahihi za kuusimamisha Uislamu nchini Tanzania.

Mchango wake katika kufundisha na kuwalea wanafunzi katika Mashule na vyuo ni mfano bora wa kuigwa. Siku zote alikuwa akiwahimiza wanafunzi wake kuwa watakuwa wanafanya jambo la maana pale watakapo dumu kufundisha Elimu ya Dini ya Kiislamu katika shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu vya serikali na vya Binafsi. Sheikh Malik amefariki dunia April, 2009.

Pamoja na kuibuka na kusajiliwa Taasisi na Jumuiya nyingi za kiislamu katika uongozi wa Rais Al-Hajj Hassan Mwinyi, harakati za kiislamu hazikuonekana kuzaa matunda yaliyotegemewa. Maendeleo ya waislamu yalizidi kudumaa na uislamu uliendelea kufutika katika maisha ya watu na jamii kwa ujumla. Dosari kubwa zilizokabili jumuiya hizo ni pamoja na:

- (i) Kukosa malengo yaliyo wazi na mipango ya uteklezaji ya Taasisi na Jumuiya zilizotawaliwa na hamasa na jaziba.
- (ii) Nyingi ya Taasisi na Jumuiya za waislamu zilianzishwa kama vitega uchumi vya watu binafsi
- (iii) Kukosa nguvu kazi. Hapakuwa na taratibu za kuwafunza, kuwaandaa na kuwalea wanaharakati.
- (iv) Kukosa mtizamo sahihi wa Uislamu na namna ya kuusimamisha
- (v) Kukosekana kwa ushirikiano na mshikamano wa Taasisi na Jumuiya za Kiislamu. Baadhi zilihasimiana na kupigana vita.

## **Juhudi za Kuirekebisha BAKWATA 1979**

Mwaka 1979, kulitokea kutoelewana baina ya Mwenyekiti wa BAKWATA, Al-Haj Salehe Masasi na katibu wake Mkuu, Sheikh Mohamed Ali. Ilionenakana Sheikh Mohamed Ali, hakuridhishwa na uendeshaji wa BAKWATA, ikabidi Salehe Masasi atumike kumuondoa kwa kisingizio kuwa haonekani ofisini na mahali pake kumuweka Juma Mrindoko. Kipindi hicho Sheikh Mohamed Ali alikuwa katika tume ya Rais ya kuchunguza nidhamu ya viongozi, ambayo ilimshughulisha sana.

Sheik Mohamed Ali aliyekuwa mcha-mungu na sheikh msomi mwenye shahada ya sheria ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam, alikuwa nitumaini la vijana wasomi na wanaharakati wa kiislamu kuwa wakimuunga mkono ataweza kuleta mabadiliko ndani ya BAKWATA. Vijana wa warsha na waislamu wengine wenye uoni



mzuri walimuendea Sheikh Mohamed Ali na kumshawishi kuwa asikubali kutoka BAKWATA, bali uitishwe mkutano wa Halimashauri kuu ya BAKAWATA ili uthibitisha uhalali wa kufukuzwa kwake, kwani kikatiba Masasi hakuwa na mamlaka ya kumfukuza. Sheikh Mohamed Ali alikubali na vijana wa Warsha na waislamu wenye kuhitajia maendeleo ya Dini yao walishiriki kikamilifu kuitisha na kuufanikisha mkutano ule wa Halimashauri Kuu ya BAKWATA, uliofanyika katika ukumbi wa Elimu ya Watu Wazaima, mtaa wa Lumumba, Dar es salaam. Mkutano ule uliokuwa halali kwa mujibu wa katiba ya BAKWATA ulipitisha maamuzi yafuatayo:

- (1) Kumfukuza katika uongozi, Salehe Masasi kwa kosa la kukataa kuhudhuria mkutano ule halali.
- (2) Kuteua kamati ya muda, Sheikh Mohamed Ali akiwa mwenyekiti wake iliyokuwa na kazi ya kuendesha shughuli za kila siku za BAKWATA makao makuu na kuandaa rasimu ya katiba mpya ya BAKWATA yenye muelekeo wa kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii. Kazi ya kuanda katiba na kupata uongozi mpya wa BAKWATA iltarajiwa ikamilike katika kipindi cha miaka miwili.

Katika hiki kipindi cha mpito pamoja na kazi ya kuandaa rasimu ya katiba mpya ya BAKWATA lilianzishwa mara moja gazeti la "Muislamu" la kila mwezi lililotoa mchango mkubwa sana katika kuwaelimisha na kuwazindua waislamu. Pia kwa mtindo wa "phasing out" Shule za Kinondoni, Dar es salaam na Jumuiya, Tanga, zilizokabidhiwa BAKWATA kutoka EAMWS, zilifanywa seminari na kuanza kidato cha kwanza 1981 baada ya kuidhinishwa na Halimashauri Kuu ya BAKWATA. Lengo la shule hizi lilikuwa kutoa elimu na malezi sahihi kwa vijana wa Kiislamu ili kuwaandaa kuwa viongozi wa kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii kama seminari za wakatoliki zipatazo 23 wakati huo, zilivyokuwa na lengo la kuandaa vijana wa kikatoliki

watakaochukua nafasi za uongozi wa jamii katika sekta mbalimbali.

Juhudi hizi zilipokelewa kwa furaha na matumaini makubwa na waislamu. Lakini kwa maadui wa uislamu hii ilionekana ni tishio na hatari kwa serikali ya Tanzania iliyo chini ya kanisa Katoliki.

Ndani ya BAKWATA kwenyewe mawakala wa maadui wa Uislamu walianza kuwa na wasiwasi. Walichukulia juhudi hizo za kuleta maendeleo ya Uislamu na Waislamu kuwa ni kulisaliti Baraza la Serikali. Mawakala wa maadui wa Uislamu ndani ya serikali nao wakaindama BAKWATA na kuitaka iwafukuze vijana wa warsha walioingia ndani ya BAKWATA na kutaka kuleta maendeleo ya Waislamu.

Mwalimu Nyerere, aliyeahidi kulipa kanisa katoliki upendeleo pekee, alidhihirisha chuki zake binafsi dhidi ya maendeleo haya ya BAKWATA, na hasa kuanzishwa kwa Seminari ya Kionondoni. Katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Dar es salaam, Novemba, 1981, Mwalimu Nyerere alidhihirisha chuki yake hiyo alipo muagiza makamu wa kwanza wa Rais, Al-Hajj Aboud Jumbe na makamu wake wa pili, Rashidi Mfaume Kawawa, kuwa akirudi kutoka safarini aikute Kinondoni imesharudishwa kuwa shule ya kawaida yenye mchanganyiko wa waislamu na wakristo na sio seminari tena. Viongozi hawa wa serikali walitii agizo la Rais kwa kuwaita viongozi wa BAKWATA ili kuweka mikakati ya utekelezaji wa amri ile. Sheikh Mohamed Ali alikataa kutii amri ile kwa hoja kuwa atawaambia nini waislamu waliopitisha uamuzi ule kwenye Halimshauri kuu, ikizingatiwa kuwa wakati huo wakatoliki walikuwa na Seminari 23 zilizotapakaa kote nchi.

Mwaka 1982 Serikali kupitia kwa mawakala wake ndani ya BAKWATA, iliitisha mkutano wa Halimashauri kuu ya BAKWATA uliofanyika Chuo cha Ardhi, Dar es salaam. Mkutano ulizingirwa na ulinzi mkali na kabla mkutano haujaanza wajumbe wawili,

Mtengwa Burhani Mtengwa na Musa Abdul-Rahmani Mdidi, waliokuwa watendaji na wawakilishi wa vijana wanaharakati walitolewa kwenye ukumbi wa mkutano na polisi na kusindikizwa na ulinzi mkali mpaka majumbani mwao. Sheikh Mohamed Ali alishutumiwa kwa kosa la kuwaingiza vijana wanaharakati ndani ya BAKWATA waliokuwa na lengo la kusimamisha Uislamu katika jamii. Kwa kosa hili na makosa mengine mengi aliyobambikiziwa, Sheikh Mohamed Ali aliwajibika kujiuzulu ukatibu Mkuu wa BAKWATA.

Baada ya kujiuzulu Sheikh Mohamed Ali na kufukuzwa watendaji walionekana wakorofi, gazeti la “*muislamu*” lilianza kuyumba, likabadilishwa jina likaitwa “*sifina*” na hatimaye likafa kabisa. Shule mbili pekee za seminari nazo zikauwawa mara moja.

Kutoka kwa Sheikh Mohamed Ali kulimpa fursa Bwana Adam Nasibu kuchukua nafasi ya Katibu Mkuu wa BAKWATA, makamu mwenyekiti akiwa Mustafa Songambe. Adam Nasibu alitembea nchi nzima kuonesha uhatari wa vijana wa “**Warsha ya Waandishi wa Kiislamu**” na makala na vitabu walivyoandika vyenye lengo la kuhuisha na kusimamisha Dola ya kiislamu nchini.

## **Kuanzishwa kwa Seminari ya Masjid Qubah, 1983**

Vijana wa “Warsha” waliokuwa watendaji wakuu katika BAKWATA ya Sheikh Mohamed Ali wakishirikiana na wazazi waislamu waliokerwa na kuuliwa kwa seminari ya Kinondoni waliamua kuanzisha seminari nyingine chini ya usimamizi wa **kamati teule** ya watu nane akiwemo Musa Abdulrahman Mdidi, Mtengwa Burhan Mtengwa, Mohamed Ramadhani Kassim, Ahmed Mbaraka, Abubakar Marwiro, Waziri Nyelo, Mzee Abdallah Amour Suleiman na Mzee Abbas Shabani Kilima.

Kistratejia, Shule hii haikutakiwa iwe moja kwa moja chini ya “Warsha ya waandishi wa Kiislamu” kwa sababu mbili, **kwanza**

“Warsha” ilikuwa ni kikundi cha uhamasishaji kisichokuwa na tasjila ya kisheria. **Pili** propaganda za uhatari wa “Warsha” zilizofanywa na Adam Nasibu ziliwafanya waislamu waogope kujihusisha au kushirikiana na “Warsha”.

Mwaka 1983, mwaka uliofuatia baada ya kuvunjwa seminari ya Kinondoni, Dar es salaam na Jumuiya, Tanga, ilianzishwa, Seminari ya Masjid Qubah katika madarasa ya msikiti wa “Masjid Al-Amin” ulipo karibu na uwanja wa Taifa ilipo shule ya Kiislamu ya Temeke hivi leo. Palikuwa na madarasa matatu na ofisi yaliyo kodiwa kwa Sh.2,000 kwa mwezi kwa wakati ule. Mwaka 1984, Shule ilihamia Kijitonyama, ilipo Masjid Qubah ya leo, ikiwa na mikondo minne ya kidato cha kwanza na mikondo miwili ya kidatu cha pili.

Wislamu nchi nzima walifarijika na kuhamasika kutoa michango yao ya hali na mali katika kujenga na kuendeleza shule hii pekee ya Sekondari ya Kiislamu iliyoendeshwa kwa lengo la kuandaa nguvu kazi ya kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii.

Nyerere na Serikali yake ya mfumo katoliki, hakuwa radhi kabisa na maendeleo haya ya waislamu. Pamoja na kutekeleza masharti yote ya usajili, Serikali ilikataa kuisajili shule hii kwa shart kwamba lazima iandikishwe chini ya BAKWATA. Sharti hili lilikataliwa kwa hoja kuwa, iweje seminari ya Masjid Qubah isajiliwe chini ya BAKWATA ambayo iliua seminari za waislamu za Kinondoni na Jumuiya. Pamoja na kutosajiliwa waislamu walimiminika Masjid Qubah kuleta watoto wao wapate elimu na maadili ya kiislamu Mwaka 1985, Serikali ilifanikiwa kupenyeza watu wake ndani ya “warsha” na kuzusha fitina iliyopelekea kutolewa kundini watendaji wakuu wa kituo na ikawa ndio mwisho wa “Warsha” na Masjid Qubah ile.

## **Kuibuka kwa Seminari Nyingi za Kiislamu**

Alipoingia madarakani Rais wa awamu ya pili, Al-Hajj Ali Hassan Mwinyi, na kumuweka Kigoma Ali Malima kuwa Waziri wake wa Wizara ya Elimu, iligundulika kuwa hapakuwa na sheria yeyote ya Wizara ya Elimu inayowalazimisha waislamu kusajili shule zao za Kiislamu (seminari) chini ya BAKWATA. Kumbe hayo yalikuwa matashi binafsi ya Mwalimu Nyerere, mkatoliki, ili kudhibiti maendeleo ya waislamu. Kinyume chake, Rais Mwinyi mwenyewe alikuwa akiwahimiza waislamu kuanzisha shule zao na ikawa sababu ya kuanzishwa Al-Haramain Islamic College 1986 chini ya BAKWATA.

Miaka miwili iliyofuatia, 1989 zilianzishwa shule za Ununio Boys Islamic High School na Kunduchi Girls Islamic High School chini ya “Munadhamat-Da’awah”. Mwaka 1992, ilianzishwa Ubungo Islamic High School chini ya Islamic Propagation Centre ikifuatiwa na Mudio Islamic Seminary, Kirinjiko Islamic Secondary School na nyingine nyingi zilizoibuka. Mpaka hivi leo, 2009 tuna shule za Kiislamu za Msingi na Sekondari zinazo karibia hamsini (50). Shule hizi zinajengwa na kuendeshwa na waislamu wenyewe pamoja na uchumi duni na uhaba wa nguvu kazi waliyo nayo.

## **Kuanzishwa Vyuo vya Ualimu na Chuo Kikuu**

Sambamba na ujenzi wa Shule za Kiislamu za Msingi na Sekondari pamekuwa na ujenzi wa Vyuo vya Ualimu vya Kiislamu vyenye lengo la kutoa walimu bora katika ngazi ya cheti na stahhada ambao pamoja na kufundisha elimu ya mazingira watafundisha pia Maarifa ya Uislamu na kuwa walezi bora wa vijana wa Kiislamu. “Al-Haramain Islamic Teacher College ndicho chuo cha kwanza kilichoanzishwa kwa msukumo wa Rais Mwinyi, 1987. Chuo kilichofuatia ni “Ubungo Islamic Teachers’ College”, 1998 kisha kikafuatia Kirinjiko Islamic Teachers’ College, 2004.

Chuo cha Ubungo na Kirinjiko pamoja na kutoa kozi za Cheti na Stashahada vinaendesha pia kozi za muda mfupi (miezi sita/saba) kwa lengo la kuandaa walimu wa kufundisha somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu katika shule za awali, msingi na sekondari.

Mwaka 2005, Waislamu walianzisha Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro katika majengo waliyopewa na Serikali ya Rais Benjamin Mkapa. Majengo haya yalikuwa ya Chuo cha TANESCO. Chuo hiki kinatarajiwa kutoa masomo katika fani mbalimbali za elimu ya mazingira na elimu ya mwongozo kwa lengo la kutoa wataalamu watakao kuwa nguvu kazi tarajiwa ya kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii. Chuo hiki kiko chini ya taasisi ya Muslim Development Foundation(MDF). Iliyoanzishwa na waislamu kwa lengo la kusajili na kuendeleza chuo hiki.

Ili waislamu waweze kuhuisha Uislamu na kutwaa mikonini mwao Uognozi wa jamii hawana budi kuwa na wataalamu na nguvu kazi ya kutosha itakayoweza kuendesha kwa ufanisi kila sekta ya maisha ya binafsi na jamii. Kwa kujua hili, waislamu wanaharakati kote nchini wanafanya jitihada za kuanzisha na kuenSdesha vituo vya elimu kwa njia ya mshikamano.

## **Kuanzishwa BARAZA KUU, 1992**

Katika kipindi chote cha uongozi wa Mwalimu Nyerere na hasa baada ya kuvunjwa kwa E.A.M.W.S na jumuiya nyingine za waislamu, haikuruhusiwa kusajiliwa Jumuiya au Taasisi yoyote ya Kiislamu ila sharti ipate kibali cha BAKWATA, na iwe chini ya BAKWATA. Kwahiyo, BAKWATA, iliyofanya kazi ya kuuhujumu Uislamu zaidi kuliko kuuendeleza, ilikuwa ndiyo Jumuiya pekee ya waislamu kwa kipindi cha miaka kumi na sita(16) kuanzia 15 Desemba,1968 ilipoanzishwa BAKWATA hadi 1985 alipong'atuka Mwalimu Nyerere.

Rais Mwinyi alipiongia madarakani mwishoni mwa mwaka 1985, iligundulika kwa waislamu kuwa hapakuwa na sheria yeyote ya nchi iliyoipa BAKWATA ukiritimba bali ilikuwa ni sera binafsi ya Nyerere na kanisa lake. Baada ya waislamu kugundua hili, kwa hamasa na hamu kubwa walianzisha utitiri wa Jumuiya na Taasisi za kiislamu kwa kiasi kwamba hata misikiti ilisajiliwa kama taasisi ili kujitoa kwenye makucha ya BAKWATA.

BAKWATA iliyolewa ukiritimba uliodumu kwa miongo miwili haikuwa radhi kuona ule mfumuko wa Jumuiya na Taasisi za Kiislamu zilizosajiliwa kihalali na Seriali bila ya kibali chake. Katika Baraza la Idil-Haji mwaka 1991 ambalo mgeni rasmi alikuwa mheshimiwa Rais Ali Hassan Mwinyi; Bwa Suleiman Hega aliyekuwa kaimu Makamu Mwenyekiti wa BAKWATA aliilamu Serikali kwanini imeruhusu kuwepo kwa vikundi vingi vya Kiislamu. Aidha alitaka Serikali ividhibiti vikundi hivyo. Wakati Bwana Hega analilia kubakishwa kwa ukiritimba wa BAKWATA, tayari Serikali ishaingia kwenye sera ya vyama vingi vya siasa.

Mheshimiwa Rais wakati wa kujibu risala hiyo, alikataa suala la kudhibitiwa Taasisi na Jumuiya za Waislamu, kwani mchango wake katika kuleta maendeleo ya waislamu ulikuwa mkubwa kuliko ule wa BAKWATA. Rais aliinasihi BAKWATA ikutanishe vikundi vyote vya waislamu ili tofauti zilizopo zijadiliwe ili hatimaye upatikane umoja na mshikamano wa waislamu unaohitajika na ulioamrisha katika Qur-an (3:103).

BAKWATA hawakutekeleza nasaha hizo. Lakini walitokea wanaharakti wa kiislamu waliotumia fursa ile na kuandaa mkutano ambapo walialikwa wawakilishi toka Jumuiya na Taasisi za Kiislamu nchini kote. Aidha viongozi wa BAKWATA toka ngazi za wilaya hadi makao makuu walialikwa. Lengo la mkutano huo lilikuwa kujadili namna ya kuifanya BAKWATA ifanye kazi kwa maslahi ya Uislamu na waislamu wa nchi hii.

Lakini wakati maandalizi ya mkutano huo yanaendelea BAKWATA ilikuwa ikiendesha kampeni kujaribu kuwazuia Waislamu wasihudhurie mkutano huo. Hata hivyo juhudi zao hizo hazikuzaa matunda kwani maelfu ya Waislamu walikutana Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika Ukumbi wa Nkrumah siku ya Jumapili tarehe 15 Sep, 1991.

Mkutano huo ambao ulifunguliwa na Waziri katika Ofisi ya Rais anayeshughulikia ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa, Mheshimiwa Abdurahman Kinana pamoja na mambo mengine ulipitisha maazimio yafuatayo:

- (1) Kuwaondoa madarakani Kaimu Makamu Mwenyekiti wa Bakwata Bwana Suleiman Hegga na Kaimu Katibu Mkuu Bwana Rajab Kundyia.
- (2) Kuteua kamati ya muda ambayo itasimamia shughuli za kila siku za Bakwata Makao Makuu na kuandaa Rasimu ya marekebisho ya Katiba ya Bakwata.

Kiutekelezaji azimio la kuwaondoa Bwana Hegga na Kundyia lilikwama. Aidha, kwa vile mabwana hao hawakubali kuachia ofisi, kamati ya muda iliyoundwa kusimamia shughuli za kila siku za Baraza makao Makuu haikuweza kufanya kazi.

Hata hivyo kamati iliendelea kuandaa rasimu ya marekebisho ya katiba ya Bakwata. Zoezi hilo lilipokamilika uliitishwa mkutano mkuu ambao ulifanyika katika ukumbi wa Diamond Jubilee mjini Dar es Salaam.

Pamoja na kupitishwa kwa rasimu ya katiba Waislamu waliamua kulitwaa Bakwata kwa nguvu ambapo ofisi za Bakwata makao makuu, ofisi ya mkoa Dar es Salaam na shule ya Al-haramain ilizingirwa na kuzuia watendaji wa ofisi hizo kuingia.



Ofisi hizo zilizingirwa kwa muda wa wiki moja hadi Rais Ali Hassan Mwinyi alipoingilia kati na kuzikutanisha pande mbili, 11, Januari, 1992. Viongozi wa Bakwata na viongozi wa kamati teule iliyowekwa na mkutano wa 15 Septemba, 1991, walikubaliana mbele ya Rais Mwinyi kuwa zichaguliwe kamati za kusimamia uchaguzi toka ngazi ya chini hadi Taifa ambapo BAKWATA watatoa watu watano na “kamati teule” watu watano. Lengo lilikuwa kwamba endapo uchaguzi utasimamiwa vyema watapatikana viongozi waadilifu wanaokubalika watakao simamia maendeleo ya Uislamu na Waislamu. BAKWATA walivunja makubaliano yale kwa madai kuwa, kwa kauli ya aliyekuwa Sheikh Mkuu wa BAKWATA Hemed bin Juma bin Hemed katika Baraza la Idd kule Shinyanga, kuwa Rais Mwinyi ameingilia kati kitu asichokijua asili yake na madhumuni yake. Akaeleza Sheikh Mkuu huyo kuwa BAKWATA iliundwa na Serikali ili kudhibiti na kuzuia uanzishwaji wa vikundi mbalimbali vya Kiislamu vitakavyoweza kufanya harakati za kuleta maendeleo ya Uislamu na Waislamu. Katika Baraza hilo, Sheikh Mkuu alimsikitikia ndugu yake, Sheikh Moahmed Ali, kuwa aliponzwa na vijana wa “Warsha” aliowaingiza ndani ya BAKWATA ambao walikuwa na azma ya kusimamisha Dola ya kiislamu hapa nchini, ikabidi alazimishwe kujiuzulu ukatibu Mkuu wa BAKWATA. Rais Mwinyi baada ya kugundua kuwa BAKWATA ni zimwi la watu alizira na kujitoa katika usimamizi wa suluhu ile.

Kufikia hapo wale waliokuwa katika harakati za kuirekebisha BAKWATA wakaona waiache BAKWATA kama ilivyo na waanzishe Baraza litakalo kuwa mbadala, **Baraza Kuu la Jumuiya na Taasisi za Kiislamu**, kwa ufupi **BARAZA KUU**. Baraza Kuu lilisajiliwa rasmi mwaka huo wa 1992. Pamoja na Baraza Kuu, kupata tasjila, bado palikuwa na utata katika mchakato wa usajili wake. Aliyekuwa akifuatilia usajili ni Bwana mmoja aliyenjeingiza katika ile kamati teule na kupora ukatibu katika hali ya kutatanisha na baadaye ikadhihirika kuwa alikuwa Swahiba yake Mwalimu Nyerere mwenye BAKWATA yake iliyotaka kuuliwa au

kudhoofishwa. Utata huu ulizidi kudhihiri pale tasjila ya **Baraza Kuu** ilipoletwa nyumbani kwa aliyekuwa Mwenyekiti wa kamati, Mzee Salumu Khamis na waziri wa mambo ya ndani mwenyewe, mheshimiwa Augustine Lyatonga Mrema. Halikuwa jambo la kawaida. Baadhi ya waislamu wenye kuona mbali walitilia mashaka tasjila ile na wakathubutu kusema Baraza Kuu lilikufa siku ile lilipopata tasjila yake. Ukweli huu ulidhihiri katika mkutano Mkuu wa kwanza wa Baraza Kuu pale walipozuiliwa kuhudhuria mkutano huo wajumbe halali miongoni mwa waasisi wa Baraza Kuu walioitisha ule mkutano wa 15 Septemba, 1991. Matokeo yake, ule ukawa ni mkutano mkuu wa kwanza na wa mwisho wa Baraza kuu kwa mujibu wa katiba yake.

Waislamu walifarijika sana kwa kusajiliwa Baraza Kuu. Walitegemea kuwa lingeliwaunganisha waislamu na kujenga nguvu ya pamoja itakayopokea kuhuika na kusimama kwa Uislamu katika jamii. Kinyume na matumaini hayo katika siku za mwanzoni. Baraza Kuu lilibakia kushindana na BAKWATA katika kuendesha mabaraza ya Idd na Maulid. Baadaye likabakia na kutoa vyeti vya ndoa na kusuluhisha migogoro baina ya wana ndoa.

Hivyo, mpaka hivi sasa (2009) waislamu hawajawa na umoja wala uongozi unaoheshimika (central Authority) bali wamebakia kuwa na jumuiya na taasisi nyingi zisizoelewana katika mipango na utekelezaji wake. Wakati mwingine inafikia hatua ya jumuiya na taasisi hizi kuhasimiana, kushutumiana na kupigana vita. Tatizo hili la waislamu kukosa uongozi wa pamoja linaambatana na matatizo mengine yafuatayo:

- (i) Hakuna mipango ya kazi kulingana na mahitajio ya umma wa waislamu.
- (ii) Hakuna utaratibu wa kuwafunza na kuwalea watu kuelekea kwenye kusimamisha Uislamu.
- (iii) Kusema na kulalamika kumekuwa kwingi kuliko kupanga na kutenda.

- (iv) Kutokana na kukosekana kwa mafunzo na uongozi wa pamoja, waislamu wamekuwa wakifanya mambo kwa jazba. Hali hii imekuwa ikiwa sababishia waislamu madhara makubwa ikiwa ni pamoja na kadhia ya “mabucha ya nguruwe, 1993” na mauaji ya mwembe chai, 1998”.
- (v) Kutokana na kukosekana kwa malengo na mipango ya pamoja waislamu wa nchi hii wamekuwa hawapigi hatua yoyote ya maendeleo ya pamoja inayolandana na kasi ya adui.
- (vi) Kwa kukosa malengo na mipango ya pamoja waislamu wamekuwa wakiingizwa kwenye agenda za watu wengine na wakamalizia muda na guvu zao humo. Agenda za “**O.I.C**” na “**Kadhi**” zimewashughulisha sana waislamu.

## **Kadhia ya Mabucha ya Nguruwe, 1993**

Katika kuwachokoza na kuwadhalilisha waislamu ilifikia mahali wakristo kuachia huru mifugo yao ya nguruwe kuchafua mazingira ya waislamu hadi kuingia Misikitini Ubungo Darajani na Mabibo karibu na Mabibo Hostel ya Vyuo Vikuu. Pia wakristo walifikia hatua ya kufungua mabucha ya nyama ya nguruwe sambamba na mabucha ya nyama halali kiasi kwamba mtoto akitumwa nyama hawezi kutofautisha nyama ya nguruwe na ya ngombe au mbuzi. Kwa namna hiyo ilitokea kwa mara kadhaa watoto wa kiislamu kununua nyama ya nguruwe kwenye bucha la “Mbokomu Centre” Manzese/Tandale.

Hili suala la ufugaji na uuzaji wa nyama ya nguruwe katikati ya makazi ya waislamu si suala geni hapa Tanzania bali ni sera ya Serikali za mfumo kristo tangu wakati wa mkoloni. Katika kuupiga vita Uislamu ufugaji wa nguruwe ulitumika kama miongoni mwa zana za kudhibiti Uislamu usienee kama tunavyojifunza kutokana na waraka uliotolewa Dar-es-Salaam na Gavana wa Kijeruman, Schnee, 13 Oktoba 1913 kwenda kwa wakuu wa wilaya zote za Tanganyika na wakuu wote wa vituo vya jeshi. Waraka huo uliagiza:

*Mnaombwa mlete taarifa katika kipindi cha miezi mitatu tokea kupokea waraka huu. Taarifa hiyo ieleze mambo gani wanaweza kufanyiwa watumishi wa Serikali na walimu wa serikali ili kuzuia kuenea kwa mafunzo ya Uislamu. Je, mnadhani inawezekana kutunga sheria ya kupiga marufuku Uislamu ? Bila shaka inawezekana kutunga sheria ambayo itawazuia walimu waislamu wasitahiriwe, kuwazuia kuhubiri misikitini, n.k. Watumishi wengine wa serikali itabidi wahusike na sheria hiyo. Wataalamu wameshauri kuwa wenyeji(natives)washauriwe na watiwe hima kufuga nguruwe kwani kwa kufanya hivyo ueneaji wa uislamu utasimamishwa. Wazo hili lifikiriwe pia.<sup>94</sup>*

Waislamu wa Dar es salaam hawakuridhika na uchokozi huu wa ufugaji holela wa nguruwe na ufunguaji holela wa mabucha ya nyama ya nguruwe. Waislamu wa Ubungo Kisiwani walioathiriwa na ufungaji holela wa nguruwe hadi nguruwe kukutwa amefia msikitini mwao,tarehe 2Juni,1987 walipeleka malalamiko yao kwa Rais Mwinyi kwa niaba ya wakazi wote wa Ubungo Kisiwani kama ifuatavyo:

**YAH: UFUGAJI MBAYA WA NGURUWE KATIKA ENEO  
HILI LA UBUNGO KISIWANI**

*Mtukufu Rais,*

*Kichwa cha habari hapo juu cha husika. Tunayo heshima kubwa kutuma barua yetu ya malalamiko ya wanyama hao mbele yako ili utusaidie kutupatia ufumbuzi wa swala hili.*

*Mtukufu Rais, wanyama hao wanafugwa katika sehemu za kuishi. Wafugaji wa wanyama hawa kwa hakika wanatunyanyasa sana tusiowatumia wanyama hao, hususan sisi waislamu.*

*Wanatembea ovyo majumbani mwetu, wanalamba vyombo makaroni mwetu, wanaingia Misikitini na wanafia Misikitini jambo ambalo kwa sisi waislamu ni baya sana tena sana.*

*Mtukufu Rais, tumeshapeleka malalamiko yetu haya kwa Katibu Kata tarehe 22/4/1985 hatimaye tumepeleka barua ya malalamiko kwa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni tarehe 10/2/1986 hata hivyo hakuna hatua zozote zilizochukuliwa.*

*Mtukufu Rais, sisi wenye majina hapa chini tunatuma malalamiko haya ya kuomba waondolewe nguruwe hawa wapelekwe sehemu ambazo hazitaleta maudhi kwa niaba ya wakazi wote wa eneo hili.*

*Mtukufu Rais, tunakuomba utusaidie kututatulia matatizo yetu kikamilifu Waislamu tulio mashakani.*

*Pamoja na bura hii hapa tunaambatanisha nakala za barua za malalamiko yetu kama uthibitisho wa madai haya.*

Hata baada ya kuandika barua hii bado ufumbuzi wa ufugaji holela wa nguruwe haukupatikana. Tumenukuu barua hii hapa ili kuonesha ni kiasi gani waislamu wa nchi hii wamekuwa wakiwavumilia wananchi wenzao wakristo ili tu upatiane ueleweno wa kijamii.

Mashuleni, Vyuu na Jeshini ufugaji wa nguruwe umefamywa mradi mkubwa. Mara nyingi vijana wakiislamu hulazimishwa kushiriki katika mradi huu. Hata wale wanao samehewa kushiriki kwenye mradi huu baada ya kuvutana sana na uongozi baadhi ya shule au vyuo, bado hawajaweza kuepukana na nguruwe, kwani shule nyingi huamua kuwalisha wanafunzi nyama ya nguruwe, na kutumia vyombo vilevile vinavyotumiwa na wanafunzi wote wa

waislamu wakiwemo. Pia pato linalotokana na mradi wa nguruwe huchanganywa katika mfuko wa shule au Chuo ambao hutumika kwa wanafunzi wote.

Kuna kesi nyingi sana za wanafunzi wa Kiislamu kulazimishwa kushiriki katika mradi wa nguruwe na upikwaji wa nyama ya nguruwe shuleni au vyuoni kwa kutumia vyombo vile vile vya wanafunzi wote. Kesi ya shule ya sekondari ya Rungwe ni miongoni mwa kesi hizo kama mwalimu Muislamu wa shule hiyo alivyolalamika katika gazeti la “Daily News” la tarehe 27/7/1988, uk.5:

*Rungwe Secondary School is among the best schools in the United Republic due to its best performance in both academic and development projects. But what has spoiled the school's good image is the Headmaster's dictatorial decision to include pork on the students menu disregarding the fact that the school is composed of both Christians and Moslems. How can pork be cooked in the same utensils used to cook food eaten by non-Christians, namely Muslim students? Doesn't the Headmaster know this is against the teaching of the Holy Qur'an?*

### Tafsiri

*Shule ya Sekondari Rungwe ni miongoni mwa shule bora katika Jamhuri ya Muungano kutokana na kufanya kwake vizuri katika masomo na katika miradi ya maendeleo.*

*Lakini kinacho haribu jina zuri la shule ni maamuzi ya kibinafsi (ya kidikteta) ya Mwalimu Mkuu ya kuingiza nyama ya nguruwe katika chakula cha wanafunzi bila ya kujali kuwa shule ina mchanganyiko wa wanafunzi Wakristo na Waislamu. Nyama ya nguruwe itapikwaje kwa kutumia vyombo vile vile vinavyotumika kupikia chakula kinacholiwa na wanafunzi wote, Waislamu na Wakristo? Je, Mkuu wa Shule hafahamu kuwa hili ni kinyume na mafundisho ya Qur'an?*

Dhidi ya shutuma hizi, Mkuu wa Shule alitoa jibu lifuatalo:

*The decision to allow Christian students to eat pork was made by the teaching staff in a staff meeting held on 14/4/87.*

*The decision was communicated to the students through the school Baraza on the 21/4/87. The Muslim students were involved and they allowed some of the school utensils to be used.*

Tafsiri:

*Uamuzi wa kuwaruhusu wanafunzi wakristo kula nyama ya nguruwe ulitolewa na walimu katika mkutano wao uliofanyika tarehe 14/4/87. Uamuzi huu ulifikishwa kwa wanafunzi kwenye Baraza la Shule lililofanyika 21/4/87. Wanafunzi waislamu walihusishwa na waliruhusu baadhi ya vyombo vya shule vitumiwe.*

Jibu hili la Mkuu wa Shule laonyesha jinsi wanafunzi Waislamu wanavyokandamizwa mashuleni katika suala zima la kufuata dini yao vilivyo. Kuna maswali mengi ya kujiuliza juu ya ufugaji na ulaji nguruwe mashuleni na vyuoni ambapo kuna mchanganyiko wa wanafunzi Waislamu na wasiokuwa waislamu. Kwa nini usichaguliwe mradi usioleta ubaguzi na ukandamizaji wa kundi la Waislamu? Kuna ulazima gani wa kupika nyama ya nguruwe shuleni au chuoni ambako kuna mchanganyiko wa wanafunzi waislamu na wasiokuwa waislamu? Je, uchache wa wanafunzi waislamu humo shuleni na vyuoni ndio unawafanya wastahiki kukosa haki na uhuru wao wa kuabudu? Na kwa nini waislamu wawe wachache humo shuleni na vyuoni na ili hali kundi la waislamu ndilo kubwa katika nchi? Je, tunaweza kusema shuleni hapana ubuguzi wa Dini? Ni nani aliyelea ubaguzi huu: Wanafunzi waislamu wanaokataa kulishwa nguruwe na kushirikishwa kwenye mradi wa nguruwe katika kutetea imani yao, au viongozi wa shule,

vyuo na Wizara zinazohusika kwas ujumla, unaowalazimisha wanafunzi Waislamu kushiriki katika mradi wa nguruwe au kula nguruwe kinyume na imani yao? Je, “udugu wetu” na “umoja wetu” vinapatikana tu wakati waislamu wanapoidharau na kuibeza Dini yao na kuziunga mkono na kuziendeleza dini za wengine kwa njia moja au nyingine, lakini waislamu hao hao wanapotanabahi na kuamu kuifuata dini yao vilivyo, wanashutumiwa kufanya fujo na kuleta ubaguzi wa kidini na Serikali kuchukua hatua kali dhidi yao?

Kuhusu kulishwa nyama ya nguruwe pale “Mbokomu Centre” Manzese Tandale. Waislamu wa mtaa ule walipeleka malalamiko yao kwa uongozi wa serikali ya mtaa hadi kwa Mkuu wa Wilaya ambapo pote walipuuzwa. Baada ya malalamiko yao kupuuzwa na serikali, vijana wanaharakati wa kiislamu wa Mkoa wa Dar es salaam waliamua kuchukua sheria mkononi na kuvunja bucha la nguruwe la “Mbokomu Centre” la pale Manzese Tandele na lingine la Magomeni karibu na kituo cha polisi.

Serikali iliyopuuzwa malalamiko ya waislamu haikuvumilia hatua ile waliyoichukua waislamu, bali kesho yake vyombo vyote vya habari vililaani waislamu kwa kitendo kile. Rais Mwinyi aliyekuwa ziarani Zanzibar, baada ya kupelekewa habari za kadhia ile na viongozi wake wa juu wa chama na serikali akiwemo Waziri Mkuu, Waziri wa Mambo ya Ndani na Katibu Mkuu wa C.C.M. alitoa kauli huko huko kuwa “Rungu la Dola liwaangukie kwa nguvu zote” wote waliohusika na kitendo hicho.

Kilichofuatia sio serikali kuwakamata wale vijana waliohusika na uvunjaji wa mabucha yale ambao walivunja mchana mweupe (saa 11 alasiri), askari polisi na askari kanzu wakiwa wanawashuhudia, bali kuwa kamata na kuwasweka ndani wanaharakati wote wa nchi nzima wakiwemo wahadhiri waislamu waliokuwa wakitumia Biblia, viongozi wa Taasisi za Kiislamu, n.k.

Wanaharakati na viongozi hawa wa waislamu walipofikishwa mahakamani, pamoja na shitaka la kuvunja bucha la nguruwe la



“Mbokomu centre” Manzese na lile la Magomeni, walisomewa *mashitaka mengine ya kutengeneza mabomu kwa lengo la kulipulia mabaa na kiwanda cha pombe cha Tanzania Breweries”,Ilala, Dar es salaam.* Watuhumiwa walinyimwa dhamana na kubakishwa rumande takriban kwa kipindi cha miezi sita. Katika jambo la kushangaza ni kuwa mlalamikaji wa uvunjaji wa mabucha ya nguruwe alikuwa serikali badala ya wenye mabucha yale.

Wahutuhumiwa wakitengeneza mabomu waliachiwa huru kwakukosekana ushahidi lakini wale walioshutumiwa kuvunja mabucha ya nyama ya nguruwe pale manzese na magomeni Dar es salaam, ambao kihalisia hawakuhusika kabisa hata kwenye mchakato wa maandalizi walihukumiwa kifungo cha mwaka mmoja. Baada ya kutumikia kifungo kwa miezi kadhaa waliachiwa huru kwa msamaha wa Rais.

## **Mauaji ya Waislamu Mwembechai,1998**

Rais William Benjamin Mkapa,Mkatoliki, alipoingia madarakani wakristo wakatoliki walitumia serikali yake vizuri kuwadhibiti na kuwakandamiza waislamu. Viongozi wa kanisa katokiki waliichochea na kuishinikiza serikali ya Mkapa idhibiti mihadhara ya Waislamu inayotumia Biblia iliyokuwa kero yao katika kipindi chote cha Rais Mwinyi.

January, 29,1998 waislamu wa Dar es salaam walifanya Baraza la Iddil-Fitr katika Msikiti wa Mwembechai na maudhui makubwa ya Baraza hilo yalikuwa kuitanabahisha serikali juu ya kukiuka kwake katiba ya nchi kwa kuingilia uhuru wa dini. Aliyekuwa makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Omar Juma alitangaza kuwa itakuwa ni marufuku waislamu kuswali Iddil-Fitr kinyume na siku itakayotangazwa na Muft wa BAKWATA, Sheikh Hemed bin Jumaa bin Hemed. Wanaharakati wa kiislamu walipinga amri hiyo ya serikali na wakaswali swala ya Iddil-Fitr

kama kawaida kabla ya siku iliyotangazwa na Muft Hemed. Katika Baraza la Idd waislamu walionyesha hisia zao na msimamo wao kuwa wamechoka kukandamizwa na serekali ya mfumo kristo(katoliki)

Februari 8,1998, wiki moja baada ya Baraza la Idd la mwembechai, Padre Camillius Lwembano wa Parokia ya Mburahati, Dar es salaam, alidai kuwa siku ya Idd alipita msikiti wa Mtambani,Kinondoni na Mwembechai, Magomeni na kusikia Yesu akikashifiwa katika mihadhara ya Waislamu. Madai yake haya aliyoyotoa kwa jazba yalirushwa hewani na Radio Tumaini inayomilikwa na kuendeshwa na Kanisa Katoliki. Madai yake yalikuwa ni ya uwongo uliodhahiri kwani siku ile ya Idd hapakufanyika mihadhara ya Biblia katika misikiti aliyoitaja bali lilifanyika Baraza la Idd tu katika Msikiti wa Mwembachai.

Padre Lwambano aliilaumu Serikali ya Mkaapa kwa kutotekeleza kwake ahadi ya kuwachukulia hatua wahadhiri waislamu wanaotumia Biblia na aliichagiza serikali ichague kati ya mawili: Kupiga marufuku mihadhara ya waislamu inayotumia Biblia na kuwachukulia hatua kali wahadhiri au itangaze kuwa imeshindwa kuzuia kashafa dhidi ya dini ya kikristo katika nchi.

Chagizo hilo lilitolewa Jamapili, 8 Februari,1998. Jumatatu, 9 Februari, 1998, Serikali ilichukua hatua mbili:

**Kwanza**, Wakristo wote nchini walitakwa radhi kwa jinsi walivyoathiriwa na kashafa za waislamu dhidi ya dini yao siku ya Iddil-Fitr na **Pili**, iliahidi kuchukua hatua kali dhidi ya wahadhiri wa kiislamu walioendesha mihadhara ile siku ya Idd. Kauli hii ya Serikali ilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam, Yusufu Makamba.

Siku iliyofuatia,Jumanne, 10 Februari,1998, Mkuu wa Polisi wa Mkoa wa Dar es salaam, Bw. Alfred Gewe, alitoa tamko lingine lililosisitiza lile la Mkuu wa Mkoa kuwa Serikali itachukuwa hatua

kali sana dhidi ya wahadhiri waislamu wanaolinganisha dini kwa kutumia Biblia. Usiku uliofuatia walianza kukamatwa maimamu wa Misikiti ya Mtambani, Kibo na Mwenge kwa kuviziwa majumbani mwao usiku usiku karibu na alfajiri. Tarehe 11, Februari 1998 kikosi cha askari Polisi wenye silasha waliizingira shule ya Kiislamu ya Ubungo, wakidai kuwa wanamtafuta Shaabani Magezi, aliyekuwa miongoni mwa wahadhiri wa ulinganisho wa dini kwa kutumia Biblia na Qur-an. Walijibiwa kuwa Magezi hakuwa mwajiriwa wala mwanafunzi wa Ubungo Islamic High School.

Mnamo Saa 9 mchana siku ya Al-hamis, 12 Februari, 1998 kundi la askari Polisi kumi na mbili wenye silaha walivamia msikiti wa mwembechai na kumteka nyara Bw. Shabani Magezi na kuondoka naye. Hapakuwa na muhadhara siku hiyo. Saa moja hivi baada ya kutekwa nyara Magezi, Msikiti wa Mwembechai ulivamiwa na kuzingira na askari Polisi na Jeshi la kutuliza Fujo (F.F.U). Waislamu waliokutwa msikitini waliamua kutulizana mle ili wasije singiziwa kuwafanyia fujo askari. Ikawa kosa kufanya vile na ilipofika saa 2 usiku askari wengi zaidi wenye silaha waliongezwa na kuzingira eneo lote la Mwembechai na kuwakamata wapita njia.

Ilipofika saa 7 usiku serikali iliagiza shirika la umeme (TANESCO) kukata umeme wa pale msikitini na eneo linalozunguka. Baada ya eneo lote kuwa giza, askari walitupa mabomu ya machozi ndani ya msikiti kisha waliingia ndani na kuwapiga, kuwajeruhi, kuwakamata na kuwasukumiza kwenye makarandinga watu wapatao mia tatu. Walioathirika sana katika uvamizi ule wa polisi walikuwa wazee na wanawake na ndio wengi waliokamatwa. Swali la msingi la kujiuliza likawa, “kwanini serikali iliwaamuru polisi kuvamia msikiti na kuwafanyia waislamu waliokuwa wakiswali fujo zile? Nini hasa lilikuwa kosa la waislamu wale? Ili kuitakasa serikali na ovu hili, asubuhi yake aliyekuwa Waziri wa mambo ya ndani, Bw. Ali Ameir na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Dar es Salaam, Bw. Alfred Gewe walitoa kauli kuwa ilibidi polisi wavamie msikiti ule kwa sababu ulikuwa unatuhumiwa kuficha wahalifu.

Siku ya Ijumaa, 13 Februari, 1998 eneo lote lilizungukwa na askari polisi. Pamoja na hivyo, waislamu wengi walimiminika pale kwa ajili ya swala ya Ijumaa na kupata taarifa juu ya yale yaliyojiri katika usiku uliopita. Baada ya swala ya Ijumaa waislamu walifahamishwa yaliyotokea na ikaamuliwa kuwa waislamu wote wakitoka pale waende kituo cha Polisi kuwatolea dhamana ndugu zao. Waislamu walipotoka nje ili waanze safari ya kwenda kituo cha polisi Magomeni, walivamiwa na askari polisi na wengine zaidi wakakamatwa na kutupiwa kwenye makarandinga. Kitendo hiki kiliwakasirisha sana waislamu na wasiokuwa waislamu ikabidi waanze kupambana na askari polisi kwa mawe. Kikosi cha kutuliza fujo(F.F.U) kiliongezwa na mapambano yakazidi kuwa makali. Hali hi ilifanywa makusudi ili ipatikane fursa ya kuwauwa waislamu. Mwanja huu ulipopatikana makamanda wa polisi waliwaamrisha askari kuwalenga shabaha watu walio wakusidia kwa kauli ya “piga yule”, “piga shaba,” yule piga shaba”, ..... (rejea mkanda wa mauaji ya mwembechai na I.T.V). Waliuliwa waislamu wanne(4) pale pale na maiti zao kuburuzwa na kutupiwa ndani ya gari la polisi kama mzoga. Waislamu na wananchi kwa ujumla walizidi kukasirika na kuamua kuzuia magari ya serikali, mashirika ya uma na yale ya chama tawala(C.C.M) na kuyachoma moto.



Baada tu ya mauaji ya mwembechai, mkutano mkuu wa chama tawala, C.C.M., mwenyekiti wake akiwa mheshimiwa Benjamin Mkapa ambaye pia alikuwa Rais wa nchi, uliipongeza Serikali kwa hatua iliyochukua Mwembechai. Pia kiongozi Mkuu wa kanisa Katoliki, muadhama Plycarp Cardinal Pengo, aliunga mkono mauaji yale ya waislamu akidai kuwa askari wale walikuwa na haki ya kuwapiga risasi za moto kwa kuwa na wao walikuwa wakiwatupia mawe. Akajaribu kuonesha kwa kurejea kisa cha Nabii Daud kuwa jiwe nalo linaua kama Daud(a.s) alivyomuua mfalme Jalut kwa jiwe. Swali aliloulizwa Muadhama Pengo na Annuur ya wiki ile ni kuwa, “katika tukio la Mwembechai nani alikuwa Daud na nani Jalut?

Tukio la Mwembechai liliwakasirisha sana waislamu. Waislamu waliomba serikali ifuate mkondo wa sheria kwa kuunda tume huru ya kuchunguza mauaji ya waislamu Mwembechai. Serikali ilikataa. Mwanasheria mmoja, kwa jina maarufu, Abu Aziz alimwandikia Mwanasheria Mkuu wa Serikali kumwomba aishauri serikali juu ya kuundwa kwa tume huru ya uchunguzi juu ya mauaji ya mwembe chai. Ombi lake pia lilipuuzwa. Baadhi ya Wabunge waliliomba Bunge liunde Tume ya Uchunguzi. Ombi hilo lilikataliwa kwa hoja kuwa hakukuwa na pesa.

Waziri wa Mambo ya Ndani akatoa taarifa za uwongo Bungeni juu ya sababu zilizopelekea polisi kumpiga risasi mwanafunzi Chuki Athumani pale mwembe chai. Bunge liliambiwa kuwa mwanafunzi huyo alikuwa na karatasi za uchochezi. Lakini serikali haikuweza kufafanua iwapo Chuki Athumani alipigwa risasi kabla au baada ya kukutwa na karatasi za uchochezi. Na karatasi hizo hazijaoneshwa mpaka leo hii. Hatimaye Halmashauri Kuu ya Waislamu walimwandikia Mheshimiwa Rais kumwomba, pamoja na mambo mengine, serikali iunde tume huru ya uchunguzi. Katika majibu yake alisema:

*Kuhusu suala la Mwembechai mimi nilifikiri tulishaelewana haitasaidia sana kuunda Tume ya Uchunguzi, maana tunajua kilichotokea. Na tunajua kuwa zile fujo, ambazo hatimaye zilihitaji nguvu kubwa ya dola kuzizima, hazikuwa na uhusiano na mambo ya dini kabisa. Ndio maana miongoni mwa waliokamatwa walikuwapo watu ambao wala si Waislamu. Bado haja na hoja ya kuunda Tume sijaiona (Mkapa, 1999).*

Tukio jingine muhimu katika kipindi cha kati ya Februari na Aprili, 1998 hapa nchini lilihusu ile kesi maarufu ya mbwa aliyeitwa “Imigresheni”. Bwana Anatory Kachele Chizu wa huko Sumbawanga hakupendezwa na utendaji wa kazi wa maafisa wa Uhamiaji wa huko Sumbawanga. Kwa hasira akampa mbwa wake jina la “Imigresheni” na akajenga ada ya kwenda naye kwenye ofisi hizo. Na huko akawa kila mara anamwita mbwa wake kwa sauti ya

juu. Mfanyakazi mmoja wa Uhamiaji, Bwana Stanley Anyitike, alikerwa na kitendo hicho na akamfikisha Bwana Chizu na mbwa wake mahakamani. Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo, Bwana Onesmo Zunda alimtia hatiani Bwana Chizu na akamhukumu kwenda jela miezi sita na mbwa wake kuuliwa. Papo hapo maafisa wa Uhamiaji wakamwua mbwa huyo kwa rungu. Kesi na hukumu hii vilizua mjadala mkubwa ndani na nje ya nchi yetu. Tarehe 28 Aprili, 1998 Jaji Mkuu (wa wakati huo), Mheshimiwa Francis Nyalali alisema kwamba hukumu hiyo ni kiroja, kinyume na sheria na ni kinyume na haki. Pasi na kuombwa, Idara ya Mahakama iliona umuhimu wa kuchunguza kuuliwa kwa mbwa. Lakini pamoja na kuombwa rasmi Idara hiyo hiyo haikuona umuhimu wa kuchunguza kuuliwa kwa Waislamu Mwembechai. Na serikali pia ilikataa kufanya uchunguzi wa Muislamu Mohamed Omari (50) aliyefia mikononi mwa polisi tarehe 18 Mei, 1998.

Mauaji ya waislamu ni miongoni mwa vielelezo vya kuonesha tadhilila ya waislamu hapa nchini. Hali hii ya waislamu itaendelea mpaka lini? Kisasi cha Mwembechai ni haki ya waislamu wa nchi hii lakini si kuua watu wanne kama wale wa Mwembechai au kumpiga risasi kijana wa shule kama alivyofanywa Chuki Athumani bali ni waislamu kujitahidi kuujua Uislamu sahihi na kufanya jitihada za makusudi za kuutawalisha Uislamu katika jamii kwa mali na nafsi zao.

## **Kuanzishwa kwa Kamati za Kuendeleza Uislamu, 2003**

Katika kujaribu kutatua matatizo yalioanishwa hapo juu, pamoja na kutakeleza amri ya Allah(s.w) ya kuunda kundi la Harakati, Qur'an (3:104), Mwaka 2003, waislamu wanaharakati kutoka kote nchini walikutana Kirinjiko, Same na kuasisi kundi la Harakati kwa jina la "Kamati ya Kuendeleza Uislamu Tanzania", kwa ufupi KKUT itakayokuwa na uongozi kuanzia ngazi ya mtaa hadi Taifa. KKUT itakayokuwa na uongozi kuanzia ngazi ya mtaa hadi Taifa. KKUT

katika kila ngazi inawajumuisha waislamu wote wanaofanya jitihada za makusudi za kuhushia na kusimamisha Uislamu katika jamii. Kamati za kuendeleza Uislamu hazina ubaguzi wa kitaasisi au wa aina yoyote. Muislamu yeyote aliyetayari kushiriki kwa mali yake na nafsi yake katika harakati za kuuendeleza Uislamu kwa lengo la kuudhihirisha na kuutawalisha katika jamii anakuwa ni mwanakamati. Ili kupata wanakamati wenye sifa stahiki zinafanyika semina za uamsho kuanzia ngazi ya Taifa hadi Mtaa na kumewekwa mikakati ya kuwa na darasa duara kila mtaa. Kazi kubwa ya kuanza na ya msingi ya kamati za kuendeleza Uislamu ni kutoa elimu sahihi ya Uislamu na kusimamia utekelezaji wake katika kuyaenda maisha ya kila siku ya kibinafsi na kujamii. Ili hili lifanikiwe kamati za kuendeleza Uislamu katika kila ngazi zimeazimia kufanya yafuatayo:

- (i) Kuanzisha na kuendesha vituo vya elimu kuanzia shule za awali hadi vyuo vya ualimu.
- (ii) Kuanzisha na kuendesha Chuo Kikuu cha Kiislamu kitakachotoa elimu ya fani zote za elimu ya mazingira na mwongozo.
- (iii) Kusimamia ufundishaji wa Elimu ya Dini ya Kiislamu katika shule zote za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu kote nchini.
- (iv) Kuwahamasisha na kuwaandaa walimu wote waislamu kufundisha somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu katika shule zao za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu.
- (v) Kufanya jitihada za makusudi za kuandaa nguvu kazi ya kuendesha harakati za kiislamu kutokana na wanafunzi wa sekondari, vyuo vya ualimu na vyuo vikuu nchini na nje ya nchi.
- (vi) Kujiamarisha kiuchumi kwa kuanzisha na kuendesha mifuko na miradi ya kiuchumi.
- (vii) Kuweka mipango ya muda mfupi na mrefu katika kutekeleza majukuu sita yaliyoainisha hapo juu na kufanya tathmini kitaifa kila baada ya miezi sita.



## **Hitimisho**

Historia ya kuhuisha Uislamu hapa nchini Tanzania iliyoelezwa humu inatarajiwa imuwezeshe msomaji:

- (i) Kuelewa Uislamu ulivyoingia nchini na lengo la wale walioungiza na kuufundisha.
- (ii) Kuwajua maadui mbali mbali wa Uislamu tokea kipindi cha mkoloni hadi hivi sasa, 2009 na mbinu walizozitumia.
- (iii) Kutambua harakati mbalimbali zilizofanywa katika kuuhiisha na kuuendeleza Uislamu hapa nchini.
- (iv) Kufahamu matatizo yanayowakabili waislamu wa Tanzania na namna ya kuyakabili.
- (v) Kutathmini utendaji wake katika kuhuisha Uislamu katika jamii
- (vi) Kujiunga na wanaharakati na kushirikiana nao bega kwa bega katika kuuhiisha na kuusimamisha Uislamu katika jamii.

## **Zoezi la 8**

1. Eleza kwa kifupi namna Uislamu Ulivyoingia Afrika mashariki.
2. Bainisha mbinu zilizotumika kuupiga vita Uislamu wakati wa Ukoloni.
3. Onesha sababu zilizopelekea Waislamu kuasisi na kuwa mstari wa mbele katika harakati za kupigania uhuru wa Tanganyika.
4. Chambua mchango wa waislamu katika harakati za kupigania uhuru wa Tanganyika.
5. Uhuru wa wananchi wa Tanzania haujawa uhuru kamili kwa Waislamu na Uislamu wao. Jadili kwa kuonesha mifano halisi.

6. Linganisha na kutafautisha, mchango wa EAMWS kwa Waislamu wa Tanganyika na ule wa BAKWATA.
7. Ni michango ipi iliyotolewa na Masheikh, jumuiya na Taasisi zifuatazo
  - (a) Sheikh Hassan bin Ameir
  - (b) Sheikh Muhammad Hussein Malik
  - (c) MSAUD na Warsha
8. Tunajifunza nini kutokana na Harakati za vikundi vya kuhuisha Uislamu Tanzania?
9. Toa maelezo mafupi juu ya:
  - (a) Kadhia ya uvunjaji wa mabucha ya nguruwe.
  - (b) Kadhia ya mauji ya waislamu mwembechai.
10. Kutokana na kadhia ya mabucha ya nguruwe na mauaji ya mwembechai, waislamu wa Tanzania tunajifunza nini?
11. (a) Toa maoni yako juu ya kamati za kuendeleza Uislamu Tanzania.
  - (b) Ni vipi waislamu wa Tanzania watahuisha na kusima misha Uislamu kama alivyofanya Mtume(s.a.w) na maswahaba wake.

---

.....سُبْحَانَكَ لَا عِلْمَ لَنَا إِلَّا مَا عَلَّمْتَنَا إِنَّكَ أَنْتَ الْعَلِيمُ الْحَكِيمُ ﴿٣٢﴾

“..... Utukufu ni wako! Hatuna ilimu isipokuwa ile uliyotufundisha, bila shaka wewe ndiye mjuzi na ndiye mwenye Hikima” (2:32)

---

## **REJEA ZILIZOTUMIWA**

1. Sayyid Qutb, Islam the Religion of the Future, 1977.
2. Tax, S. Evolution After Derwin, Vol.3 University of Chicago Press, 1960.
3. Vernet M. 'L' Evolution du monde vivant plo, Paris, 1950.
4. A.H. Siddique, The life of Muhammed, u.k. 78
5. Muhammad Ubaidul Akbar, The Orations of Muhammed(s.a.w), Lahore, 1954, uk..22
6. Ibid, uk. 23 - 24.
7. Ibid Hisham, al-Sirat at mabawiyah, kitabu cha 1, uk.266.
8. Ibid
9. Dr. Majid Ali Khan, Muhammed The Final Messenger, Lahore, 1983, uk.81
10. Ibid, uk. 92
11. Ibid, uk. 92
12. Ibid, uk. 92
13. Abdallah Saleh Farsy, Maisha ya Nabii Muhammed(s.a.w) uk.29
14. Ibid, uk. 32
15. Ibid, uk. 32
16. Dr. Majid Ali Khan, Muhammed the Final Messenger, uk.99
17. Abdallah Saleh Farsy, Maisha ya Nabii Muhammed(s.a.w) uk. 35
18. Muhammad Ubaidul Akbar, The Orations of Muhammed(s.a.w) Lahore 1954, uk. 26 - 30
19. Shibli Mu'mani, Siratun-Maby, vol.1 uk 305
20. Ibid
21. Dr. Majid Ali Khan, Muhammad the Final Messenger, uk.250.

22. Khutuba hii imeandikwa kutokana na Hadithi zilizokusanywa na Imamu Muslim na Tirmidh.
23. Dr. Majid Ali Khan, Muhammed the Final messenger, uk.321.
24. Atha Husain, The Glorious Caliphate, uk.54
25. Ibid, uk. 61
26. Ibid, uk. 57
27. Ibid, uk. 58
28. Dr. Majid Ali Khan, The Pious Caliphs, uk. 153
29. Atha Husain, The Glorious Caliphate, uk.32
30. Dr. Majid Ali Khan, The Pious Caliphs, uk. 50
31. S.A. The Husein, The Glorious Caliphate, uk. 32
32. Dr. Majid Ali Khan, The Pious Caliphs, uk. 131
33. A.H. Siddiq, Historical Survey of Islamic State
34. Ibid
35. Atha Husain, The Glorious Caliphate, uk. 23
36. M.M. Qureish, Land Mark of Jihad, uk.50
37. Ather Husein,the Glorious caliphate, uk. 112.
38. Ather Husein,the Glorious caliphate, uk. 119.
39. Ather Husein,the Glorious caliphate, uk. 120.
40. Ather Husein,the Glorious caliphate, uk. 112.
41. Dr.M.A. Khan, The pious caliphs, uk. 153
42. Dr.M.A. Khan, The pious Caliphs, uk. 153
43. Dr. Majid Ali Khan, The Pious Caliphs, uk. 205.
44. Ather Husein,the Glorious Caliphate, uk. 148.
45. Ather Husein,the Glorious Caliphate, uk. 112.
46. Maryam Jameelah, Islam in Theory and Practice

47. Muslim News international, Karachi, February 1966, uk.25
48. G.D. Kitter, The White Fathers, London 1957 uk. 23 -33
49. Roland Oliver, The missionary Factor in East Africa, London 1962, uk 206
50. Hansen H.B Mission, Church and State in colonial Setting Uganda 1890 - 1925, London, 1984 uk. 26.
51. H.M. Stanley, Through the Dark content,Londoa 1978 Vol.II,uk.194
52. Tazama: Barua ya H. Johnston ya 3/12/1900.
53. Roland Oliver na Gervarase mathews, History of East Africa Vol.I Oup, London 1963 uk. 242.
54. Abdu B. Kasozi, The spread of Islam in Uganda,Nairobi, OUP, 1986
55. M. Singleto, Muslims, Missionaries and the Millennium in up country Tanzania
56. Dr. John Sivalon, Kanisa Katoliki na Siasa Tanzania 1953 - 1985
57. Gazeti la Tanganyika Standerd, 2 May,1961
58. Gazeti la Tanganyika Sandard,15 April,1961. Kwa hoja kama hiyo angalia vile vile John Hatch, Two African Statesmen, London 1976, uk. 128.
59. Press Release B/1629/62 10th December,1962.
60. Tanganyika Standard, 12th March 1963
61. K.Mayanja Kiwanuka, Op.Cil, uk.57 -58.
62. Report ya East Africa Muslim welfare Society, January/ February 1961.
63. AngaliaL Kwikima Report, The Standard 12th December 1968 na The Nationalist, 24th October,1968.
64. Mweka 1963, waliokuwa viongozi wa EAMWS ni: Tewa Said Tewa, Aziz Khaki, Bibi Titi Mohamed, Salehe Masasi, Abdallah Jambia, Khamis Kyeyamba na Bilali Rehani Waikela.

65. Tewa Said Tewa Probe.
66. Kiwanuka, Op. Cit uk. 75
67. Ibid.
68. Benjamin Mkapa alikuja kuwa Rais wa Tanzania wa Awamu ya tatu.
69. Taarifa ya kamati ya utendaji EAMWS Mkoa wa Tanga 23 Oktoba, 1968, Ripoti ya Sheik A.J. Jambia
70. Kiwanuka Op. Cit. Uk.2
71. Ripoti ya Kwikima katika the Tanganyika Standard 12 December, 1968
72. Ripoti ya Kwikima
73. Tewa, 'A Pobe.
74. Ujenzi wa Chuo Kikuu ulikuwa umeanza na jiwe la msingi lililowekwa na Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.
75. The Nationalist, Nukuu kutoka kwa Kiwanuka, uk. 81
76. November 1967, Tewa Said Tewa alifanya ziara Mwanza na Bukoba iliyokuwa na mfanikio makubwa sana. Alifanya majadiliano na Sheikh Amin Abdallah wa Mwanza na Sheikh Sued Kagasheki wa Bukoba.
77. Kiwanuka, uk. 2 - 3
78. Ibid.
79. The Standard, 9 November 1968 kutoka kwa kiwanuka uk.81. Vile vile angalia, The Standard, 20 November 1968 Hassan bin Amir alifariki 1993
80. Miaka mingi baadae Rashid Kawawa alisema kuwa anajuta kuunga mkono kukamatwa kwa Mufti was Tanganyika na Zanzibar, Sheikh Hassan bin Amir, akaelekeza lawama kwa wale waliomshauri kufanya vile.

81. Ali Muhsin, Op. Cit. uk 87
82. Pamoja na mambo mengine taarifa ya Tume ya Kwikima ilipendekeza mabadiliko katika katiba ya EAMWS, kuondolewa kwa nafasi ya Patron, kuasisiwa kwa jumuiya mpya ya Kiislamu isiyo na ubaguzi wa rangi na isiyochanganya dini na siasa.
83. Ibid
84. The Nationalist, 15 December, 1968
85. Baraza (Nairobi), 12 December, 1968
86. Tewa, 'A brobe
87. Kiwanuka, uk. 85. Vile vile proceeding of the Iringa conference 12 -15 December, 1968.
88. The Standard, 18 December 1968
89. The Standard, 20 December, 1968
90. Ibid
91. Tewa, Ibid. Vile vile angalia The Standard, 20 December, 1968
92. Kiwanuka, uk. 86
93. Pamoja na watu hawa watu wengine walikuwa waliokuwa katika mpango ule ni: Omari Muhaji, Juma Jambia na Juma Swedi.
94. Gazeti la Serikali, taarifa ya Serikali Na. 40 ya 15 Mei, 1916.